# Holy Bible

## Aionian Edition®

**Wazi Neno Maandiko Matakatifu**

**Swahili Open Bible**

**New Testament**

*Holy Bible Aionian Edition* ®
Wazi Neno Maandiko Matakatifu
Swahili Open Bible
New Testament

Creative Commons Attribution ShareAlike 4.0 International, 2018-2025
Source text: eBible.org
Source version: 5/20/2025
Source copyright: Creative Commons Attribution ShareAlike 4.0
Biblica, Inc., 2018, 2024

Formatted by Speedata Publisher 5.1.9 (Pro) on 6/18/2025
100% Free to Copy and Print
TOR Anonymously
AionianBible.org

Published by Nainoia Inc, https://Nainoia-Inc.signedon.net
All profits are given to https://CoolCup.org

We pray for a modern Creative Commons translation in every language
Translator resources at https://AionianBible.org/Third-Party-Publisher-Resources
Report content and format concerns to Nainoia Inc
Volunteer help is welcome and appreciated!

*Celebrate Jesus Christ's victory of grace!*

# Utangulizi

Kiswahili at AionianBible.org/Preface

The *Holy Bible Aionian Edition* ® is the world's first Bible *un-translation*! What is an *un-translation*? Bibles are translated into each of our languages from the original Hebrew, Aramaic, and Koine Greek. Occasionally, the best word translation cannot be found and these words are transliterated letter by letter. Four well known transliterations are *Christ*, *baptism*, *angel*, and *apostle*. The meaning is then preserved more accurately through context and a dictionary. The Aionian Bible un-translates and instead transliterates eleven additional Aionian Glossary words to help us better understand God's love for individuals and all mankind, and the nature of afterlife destinies.

The first three words are *aiōn*, *aiōnios*, and *aïdios*, typically translated as *eternal* and also *world* or *eon*. The Aionian Bible is named after an alternative spelling of *aiōnios*. Consider that researchers question if *aiōn* and *aiōnios* actually mean *eternal*. Translating *aiōn* as *eternal* in Matthew 28:20 makes no sense, as all agree. The Greek word for *eternal* is *aïdios*, used in Romans 1:20 about God and in Jude 6 about demon imprisonment. Yet what about *aiōnios* in John 3:16? Certainly we do not question whether salvation is eternal! However, *aiōnios* means something much more wonderful than infinite time! Ancient Greeks used *aiōn* to mean *eon* or *age*. They also used the adjective *aiōnios* to mean *entirety*, such as *complete* or even *consummate*, but never infinite time. Read Dr. Heleen Keizer and Ramelli and Konstan for proofs. So *aiōnios* is the perfect description of God's Word which has *everything* we need for life and godliness! And the *aiōnios* life promised in John 3:16 is not simply a ticket to eternal life in the future, but the invitation through faith to the *consummate* life beginning now!

The next seven words are *Sheol*, *Hadēs*, *Geenna*, *Tartaroō*, *Abyssos*, and *Limnē Pyr*. These words are often translated as *Hell*, the place of eternal punishment. However, *Hell* is ill-defined when compared with the Hebrew and Greek. For example, *Sheol* is the abode of deceased believers and unbelievers and should never be translated as *Hell*. *Hadēs* is a temporary place of punishment, Revelation 20:13-14. *Geenna* is the Valley of Hinnom, Jerusalem's refuse dump, a temporal judgment for sin. *Tartaroō* is a prison for demons, mentioned once in 2 Peter 2:4. *Abyssos* is a temporary prison for the Beast and Satan. Translators are also inconsistent because *Hell* is used by the King James Version 54 times, the New International Version 14 times, and the World English Bible zero times. Finally, *Limnē Pyr* is the Lake of Fire, yet Matthew 25:41 explains that these fires are prepared for the Devil and his angels. So there is reason to review our conclusions about the destinies of redeemed mankind and fallen angels.

The eleventh word, *eleēsē*, reveals the grand conclusion of grace in Romans 11:32. Please understand these eleven words. The original translation is unaltered and a highlighted note is added to 64 Old Testament and 200 New Testament verses. To help parallel study and Strong's Concordance use, apocryphal text is removed and most variant verse numbering is mapped to the English standard. We thank our sources at eBible.org, Crosswire.org, unbound.Biola.edu, Bible4u.net, and NHEB.net. The Aionian Bible is copyrighted with creativecommons.org/licenses/by/4.0, allowing 100% freedom to copy and print, if respecting source copyrights. Check the Reader's Guide and read at AionianBible.org, with Android, and with TOR network. Why purple? King Jesus' Word is royal and purple is the color of royalty! All profits are given to CoolCup.org.

# History

Kiswahili at AionianBible.org/History

06/21/75 - Two boys, P. and J., wonder if Jesus saves all and pray.
04/15/85 - Aionian Bible conceived as B. and J. pray.
12/18/13 - Aionian Bible announced as J. and J. pray.
06/21/15 - Aionian Bible birthed as G. and J. pray.
01/11/16 - AionianBible.org domain registered.
06/21/16 - 30 translations available in 12 languages.
12/07/16 - Nainoia Inc established as non-profit corporation.
01/01/17 - Creative Commons Attribution No Derivatives 4.0 license added.
01/16/17 - Aionian Bible Google Play Store App published.
07/01/17 - 'The Purple Bible' nickname begins.
07/30/17 - 42 translations now available in 22 languages.
02/01/18 - Holy Bible Aionian Edition® trademark registered.
03/06/18 - Aionian Bibles available in print at Amazon.com.
09/15/18 - Aionian Bible dedicated as J. and J. pray again.
10/20/18 - 70 translations now available in 33 languages.
11/17/18 - 104 translations now available in 57 languages.
03/24/19 - 135 translations now available in 67 languages.
10/28/19 - Aionian Bible nursed as another J. and J. pray.
10/31/19 - 174 translations now available in 74 languages.
02/22/20 - Aionian Bibles available in print at Lulu.com.
05/25/20 - Illustrations by Gustave Doré, La Grande Bible de Tours, Felix Just.
08/29/20 - Aionian Bibles now available in ePub format.
12/01/20 - Right to left and Hindic languages now available in PDF format.
03/31/21 - 214 translations now available in 99 languages.
11/17/21 - Aionian Bible Branded Leather Bible Covers now available.
12/20/21 - Social media presence on Facebook, Twitter, LinkedIn, YouTube, etc.
01/01/22 - 216 translations now available in 99 languages.
01/09/22 - StudyPack resources for Bible translation study.
01/23/22 - Volunteers celebrate with pie and prayer.
02/14/22 - Strong's Concordance from Open Scriptures and STEPBible.
02/14/23 - Aionian Bible published on the TOR Network.
12/04/23 - Eleēsē added to the Aionian Glossary.
02/04/24 - 352 translations now available in 142 languages.
05/01/24 - 370 translations now available in 164 languages.
08/05/24 - 378 translations now available in 165 languages.
08/18/24 - Creative Commons Attribution 4.0 International, if source allows.
10/20/24 - Gospel Primer handout format.
11/24/24 - Progressive Web Application off-line format.
01/28/25 - All profits are given to CoolCup.org.
03/12/25 - 382 translations now available in 166 languages.
05/04/25 - 393 translations now available in 175 languages.
05/27/25 - 462 translations now available in 229 languages.
06/21/25 - 469 translations now available in 230 languages.

# Yaliyomo

## AGANO JIPYA

Mathayo ........................................... 1
Marko ............................................ 29
Luka ............................................... 47
Yohana .......................................... 78
Matendo ...................................... 101
Warumi ........................................ 131
1 Wakorintho ................................ 144
2 Wakorintho ................................ 156
Wagalatia ..................................... 164
Waefeso ....................................... 169
Wafilipi ......................................... 173
Wakolosai .................................... 176
1 Wathesalonike ........................... 179
2 Wathesalonike ........................... 182
1 Timotheo ................................... 184
2 Timotheo ................................... 188
Tito ............................................. 191
Filemoni ....................................... 193
Wahebrania .................................. 194
Yakobo ........................................ 203
1 Petro ......................................... 206
2 Petro ......................................... 210
1 Yohana ..................................... 212
2 Yohana ..................................... 216
3 Yohana ..................................... 217
Yuda ............................................ 218
Ufunuo ......................................... 219

**KIAMBATISHO**

Mwongozo kwa Msomaji
Kamusi
Ramani
Hatima
Michoro, Doré

# AGANO JIPYA




*Isa akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!"*
*Wakagawana nguo zake kwa kupiga kura.*
Luka 23:34

# Mathayo

1 Habari za ukoo wa Isa Al-Masihi mwana wa Daudi,
mwana wa Ibrahimu: 2 Ibrahimu akamzaa Isaka,
Isaka akamzaa Yakobo, Yakobo akawazaa Yuda
na ndugu zake, 3 Yuda akawazaa Peresi na Zera,
ambao mama yao alikuwa Tamari, Peresi akamzaa
Esromu, Esromu akamzaa Aramu, 4 Aramu akamzaa
Aminadabu, Aminadabu akamzaa Nashoni, Nashoni
akamzaa Salmoni, 5 Salmoni akamzaa Boazi, na
mama yake Boazi alikuwa Rahabu, Boazi akamzaa
Obedi, ambaye mama yake alikuwa Ruthu, Obedi
akamzaa Yese, 6 Yese akamzaa Daudi, aliyekuwa
mfalme. Daudi akamzaa Sulemani, ambaye mama
yake ni yule aliyekuwa mke wa Uria. 7 Sulemani
akamzaa Rehoboamu, Rehoboamu akamzaa Abiya,
Abiya akamzaa Asa, 8 Asa akamzaa Yehoshafati,
Yehoshafati akamzaa Yoramu, Yoramu akamzaa
Uzia, 9 Uzia akamzaa Yothamu, Yothamu akamzaa
Ahazi, Ahazi akamzaa Hezekia, 10 Hezekia akamzaa
Manase, Manase akamzaa Amoni, Amoni akamzaa
Yosia, 11 wakati wa uhamisho wa Babeli, Yosia alimzaa
Yekonia na ndugu zake. 12 Baada ya uhamisho
wa Babeli: Yekonia alimzaa Shealtieli, Shealtieli
akamzaa Zerubabeli, 13 Zerubabeli akamzaa Abihudi,
Abihudi akamzaa Eliakimu, Eliakimu akamzaa Azori,
14 Azori akamzaa Sadoki, Sadoki akamzaa Akimu,
Akimu akamzaa Eliudi, 15 Eliudi akamzaa Eleazari,
Eleazari akamzaa Matani, Matani akamzaa Yakobo,
16 naye Yakobo akamzaa Yusufu, aliyekuwa mumewe
Mariamu, mama yake Isa, aitwaye Al-Masihi. 17
Hivyo, kulikuwa na jumla ya vizazi kumi na vinne
tangu Ibrahimu hadi Daudi, vizazi kumi na vinne
tangu Daudi hadi wakati wa uhamisho wa Babeli,
na vizazi kumi na vinne tangu wakati wa uhamisho
wa Babeli hadi Al-Masihi. 18 Kuzaliwa kwake Isa Al-
Masihi kulikuwa hivi: Mariamu mama yake alikuwa
ameposwa na Yusufu, lakini kabla hawajakutana
kimwili, Mariamu alionekana kuwa na mimba kwa
uweza wa Roho Mtakatifu wa Mungu. 19 Kwa kuwa
Yusufu, mwanaume aliyekuwa amemposa alikuwa
mtu mwadilifu, hakutaka kumwaibisha Mariamu
hadharani, hivyo basi alikusudia kumwacha kwa
siri. 20 Lakini alipokuwa akifikiri kufanya jambo hili,
malaika wa Mwenyezi Mungu akamtokea katika ndoto
na kusema, “Yusufu mwana wa Daudi, usiogope
kumchukua Mariamu awe mke wako, kwa maana
mimba aliyo nayo ni kwa uweza wa Roho wa Mungu.
21 Naye atamzaa mwana, nawe utamwita jina Isa, kwa
maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka
dhambi zao.” 22 Haya yote yalitukia ili litimie lile
Mwenyezi Mungu alilonena kupitia nabii, aliposema:
23 “Tazama, bikira atachukua mimba, naye atamzaa
mwana, nao watamwita jina Imanueli” (maana yake,
“Mungu pamoja nasi”). 24 Yusufu alipoamka kutoka
usingizini, akafanya jinsi alivyoagizwa na malaika wa
Mwenyezi Mungu, akamchukua Mariamu kuwa mke
wake. 25 Lakini hawakukutana kimwili hadi Mariamu
alipojifungua mwanawe; akamwita jina Isa.

2 Baada ya Isa kuzaliwa katika mji wa Bethlehemu
huko Yudea, wakati wa utawala wa Mfalme
Herode, wataalamu wa mambo ya nyota kutoka
mashariki walifika Yerusalemu 2 wakiuliza, “Yuko
wapi huyo aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa
maana tumeona nyota yake ikitokea mashariki,
nasi tumekuja kumwabudu.” 3 Mfalme Herode
aliposikia jambo hili aliingiwa na hofu sana pamoja
na watu wote wa Yerusalemu. 4 Herode akawaita
pamoja viongozi wa makuhani na walimu wa Torati,
akawauliza ni wapi ambapo Al-Masihi angezaliwa. 5
Nao wakamwambia, “Katika Bethlehemu ya Yudea,
kwa maana hivyo ndivyo ilivyoandikwa na nabii: 6
“‘Nawe, Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, wewe
si mdogo miongoni mwa watawala wa Yuda; kwa
maana kutoka kwako atakuja mtawala atakayekuwa
mchungaji wa watu wangu Israeli.’” 7 Ndipo Herode
akawaita wale wataalamu wa nyota kwa siri na kutaka
kujua kutoka kwao uhakika kamili wa wakati ile
nyota ilionekana. 8 Kisha akawatuma Bethlehemu
na kuwaambia, “Nendeni mkamtafute mtoto huyo
kwa makini. Mara tu mtakapompata, nileteeni taarifa
ili nami niende kumwabudu.” 9 Baada ya kumsikia
mfalme, wale wataalamu wa nyota wakaenda zao,
nayo ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia,
nao wakaifuata hadi iliposimama mahali alipokuwa
mtoto. 10 Walipoiona ile nyota wakajawa na furaha
kubwa mno. 11 Walipoingia ndani ya ile nyumba,
wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mama yake,
wakamsujudia na kumwabudu yule mtoto Isa. Ndipo
wakafungua hazina zao, wakamtolea zawadi za
dhahabu, uvumba na manemane. 12 Kwa kuwa
walikuwa wameonywa katika ndoto wasirudi kwa

Herode, wakarudi nchi yao kwa njia nyingine. 13
Walipokwisha kwenda zao, malaika wa Mwenyezi
Mungu akamtokea Yusufu katika ndoto akamwambia,
“Amka, umchukue mtoto na mama yake, mkimbilie
Misri. Kaeni huko hadi nitakapowaambia, kwa maana
Herode anataka kumtafuta huyu mtoto ili amuue.” 14
Kisha Yusufu akaamka, akamchukua mtoto pamoja na
mama yake wakati wa usiku, nao wakaenda Misri, 15
ambako walikaa hadi Herode alipofariki. Hili lilifanyika
ili litimie lile neno Mwenyezi Mungu alilosema kupitia
kwa nabii: “Nilimwita mwanangu kutoka Misri.” 16
Herode alipogundua kwamba alikuwa amedanganywa
na wale wataalamu wa nyota, alikasirika sana, naye
akatoa amri ya kuwaua watoto wote wa kiume wenye
umri wa miaka miwili kurudi chini katika mji wa
Bethlehemu na sehemu zote za jirani, kwa mujibu wa
ule muda alioambiwa na wale wataalamu wa nyota.
17 Ndipo lilipotimia neno lililonenwa na nabii Yeremia,
aliposema: 18 “Sauti ilisikika huko Rama, maombolezo
na kilio kikubwa, Raheli akilia kwa ajili ya wanawe,
akikataa kufarijiwa, kwa sababu hawako tena.” 19
Baada ya Herode kufa, malaika wa Mwenyezi Mungu
akamtokea Yusufu katika ndoto huko Misri 20 na
kusema, “Ondoka, mchukue mtoto na mama yake
mwende, mrudi katika nchi ya Israeli kwa sababu
wale waliokuwa wakijaribu kumuua mtoto wamekufa.”
21 Basi Yusufu, akainuka, akamchukua mtoto na
mama yake wakaenda hadi nchi ya Israeli. 22 Lakini
aliposikia kwamba Arkelao alikuwa anatawala huko
Yudea baada ya Herode baba yake, aliogopa kwenda
huko. Kwa kuwa alikuwa ameonywa katika ndoto,
akaenda zake sehemu za Galilaya, 23 akaenda kuishi
katika mji ulioitwa Nasiri. Hivyo likawa limetimia neno
lililonenwa na manabii waliposema, “Ataitwa Mnasiri.”

**3** Siku hizo Yahya alikuja akihubiri katika nyika
ya Yudea, akisema, 2 “Tubuni, kwa maana
ufalme wa mbinguni umekaribia.” 3 Huyu ndiye yule
aliyenenwa habari zake na nabii Isaya aliposema:
“Sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia
kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, yanyoosheni mapito
yake.’” 4 Basi Yahya alivaa mavazi yaliyotengenezwa
kwa singa za ngamia, akiwa na mkanda wa ngozi
kiunoni mwake. Chakula chake kilikuwa nzige na
asali ya mwitu. 5 Watu walikuwa wakimwendea
kutoka Yerusalemu, Yudea yote na nchi zote za
kandokando ya Mto Yordani. 6 Nao wakaziungama
dhambi zao, akawabatiza katika Mto Yordani. 7 Lakini
alipowaona Mafarisayo na Masadukayo wengi wakija
ili kubatizwa, aliwaambia: “Ninyi watoto wa nyoka!
Ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu inayokuja?
8 Basi zaeni matunda yastahiliyo toba. 9 Wala
msidhani mnaweza kusema mioyoni mwenu kuwa,
‘Sisi tunaye Ibrahimu, baba yetu.’ Nawaambia kuwa
Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto kutoka
kwa mawe haya. 10 Hata sasa shoka limeshawekwa
tayari katika shina la kila mti, basi kila mti usiozaa
matunda mazuri, hukatwa na kutupwa motoni. 11
“Mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba. Lakini
nyuma yangu anakuja yeye aliye na uwezo kuliko
mimi, ambaye sistahili hata kuvichukua viatu vyake.
Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu wa Mungu na
kwa moto. 12 Pepeto lake liko mkononi mwake, naye
atasafisha sakafu yake ya kupuria, na kuikusanya
ngano ghalani na kuyateketeza makapi kwa moto
usiozimika.” 13 Kisha Isa akaja kutoka Galilaya hadi
Mto Yordani ili Yahya ambatize. 14 Lakini Yahya
akajitahidi kumzuia, akimwambia, “Mimi ninahitaji
kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu nikubatize?”
15 Lakini Isa akamjibu, “Kubali hivi sasa, kwa maana
ndivyo itupasavyo kwa njia hii kuitimiza haki yote.”
Hivyo Yahya akakubali. 16 Naye Isa alipokwisha
kubatizwa, mara alipotoka ndani ya maji, ghafula
mbingu zikafunguka, akamwona Roho wa Mungu
akishuka kama hua na kutulia juu yake. 17 Nayo
sauti kutoka mbinguni ikasema, “Huyu ni Mwanangu
mpendwa; ninapendezwa sana naye.”

**4** Kisha Isa akaongozwa na Roho Mtakatifu wa
Mungu hadi nyikani ili ajaribiwe na ibilisi. 2 Baada
ya kufunga siku arobaini usiku na mchana, hatimaye
akaona njaa. 3 Mjaribu akamjia na kumwambia,
“Ikiwa wewe ndiwe Mwana wa Mungu, amuru
mawe haya yawe mikate.” 4 Lakini Isa akajibu,
“Imeandikwa: ‘Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa
kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.’” 5
Ndipo ibilisi akampeleka Isa hadi mji mtakatifu
na kumweka juu ya mnara mrefu wa Hekalu, 6
akamwambia, “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu,
jitupe chini. Kwa kuwa imeandikwa: “‘Atakuagizia
malaika wake, nao watakuchukua mikononi mwao
ili usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.’” 7 Isa
akamjibu, “Pia imeandikwa: ‘Usimjaribu Mwenyezi
Mungu, Mungu wako.’” 8 Kwa mara nyingine, ibilisi

akampeleka Isa hadi kwenye kilele cha mlima mrefu
na kumwonesha falme zote za dunia na fahari zake, 9
kisha akamwambia, “Nitakupa hivi vyote ukinisujudia
na kuniabudu.” 10 Isa akamwambia, “Ondoka mbele
yangu, Shetani! Kwa maana imeandikwa, ‘Mwabudu
Mwenyezi Mungu, Mungu wako, na umtumikie yeye
peke yake.’” 11 Ndipo ibilisi akamwacha, nao malaika
wakaja na kumhudumia. 12 Isa aliposikia kwamba
Yahya alikuwa amefungwa gerezani, alirudi Galilaya.
13 Akaondoka Nasiri akaenda kuishi Kapernaumu,
mji ulio karibu na bahari, katika nchi ya Zabuloni
na Naftali, 14 ili kutimiza neno lililonenwa na nabii
Isaya, aliposema: 15 “Nchi ya Zabuloni na nchi ya
Naftali, kwenye njia ya bahari, ng’ambo ya Yordani,
Galilaya ya Mataifa: 16 watu wale waliokaa gizani
wameona nuru kuu; nao wale walioishi katika nchi
ya uvuli wa mauti, nuru imewazukia.” 17 Tangu
wakati huo, Isa alianza kuhubiri akisema: “Tubuni,
kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.” 18 Isa
alipokuwa akitembea kando ya Bahari ya Galilaya,
aliwaona ndugu wawili, Simoni aitwaye Petro, na
Andrea ndugu yake. Walikuwa wakizitupa nyavu
zao baharini kwa kuwa walikuwa wavuvi. 19 Isa
akawaambia, “Njooni, nifuateni nami nitawafanya
mwe wavuvi wa watu.” 20 Mara wakaziacha nyavu
zao, wakamfuata. 21 Alipoendelea mbele kutoka pale,
akawaona ndugu wengine wawili, Yakobo mwana wa
Zebedayo na Yohana nduguye, wakiwa wamekaa
kwenye mashua pamoja na baba yao Zebedayo,
wakizitengeneza nyavu zao. Isa akawaita. 22 Nao
mara moja wakaiacha mashua yao, pamoja na baba
yao, wakamfuata. 23 Isa akazunguka Galilaya yote,
akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri Habari
Njema za ufalme, na akiponya kila ugonjwa na kila
aina ya maradhi miongoni mwa watu. 24 Kwa hiyo
sifa zake zikaenea sehemu zote za Siria, nao watu
wakamletea wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali
na maumivu, waliopagawa na pepo wachafu, wenye
kifafa na waliopooza, naye akawaponya. 25 Makundi
makubwa ya watu yakawa yanamjia kutoka Galilaya,
Dekapoli, Yerusalemu, Yudea, na kutoka ng’ambo ya
Yordani.

5 Basi Isa alipoona makundi ya watu, alipanda
mlimani akaketi chini, nao wanafunzi wake
wakamjia. 2 Ndipo akaanza kuwafundisha, akisema:
3 “Heri walio maskini wa roho, maana ufalme wa
mbinguni ni wao. 4 Heri wale wanaohuzunika,
maana hao watafarijiwa. 5 Heri walio wapole, maana
hao watairithi nchi. 6 Heri wenye njaa na kiu ya
haki, maana hao watatoshelezwa. 7 Heri wenye
huruma, maana hao watapata rehema. 8 Heri walio
na moyo safi, maana hao watamwona Mungu. 9
Heri walio wapatanishi, maana hao wataitwa wana
wa Mungu. 10 Heri wanaoteswa kwa sababu ya
haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao. 11 “Heri
ninyi watu watakapowashutumu, na kuwatesa na
kunena mabaya ya aina zote dhidi yenu kwa uongo
kwa ajili yangu. 12 Furahini na kushangilia kwa
maana thawabu yenu ni kubwa mbinguni, kwa kuwa
hivyo ndivyo walivyowatesa manabii waliokuwa kabla
yenu. 13 “Ninyi ni chumvi ya ulimwengu. Lakini
chumvi ikipoteza ladha yake, yawezaje kurudishiwa
ladha yake tena? Haifai tena kwa kitu chochote, ila
kutupwa nje ikanyagwe na watu. 14 “Ninyi ni nuru ya
ulimwengu. Mji uliojengwa kilimani hauwezi kufichika.
15 Wala watu hawawashi taa na kuifunika kwa bakuli.
Badala yake, huiweka kwenye kinara chake, nayo
hutoa mwanga kwa kila mtu aliye ndani ya ile nyumba.
16 Vivyo hivyo, nuru yenu iangaze mbele ya watu,
ili wapate kuona matendo yenu mema wamtukuze
Baba yenu aliye mbinguni. 17 “Msidhani kwamba
nimekuja kufuta Torati au Manabii; sikuja kuondoa
bali kutimiza. 18 Kwa maana, amin nawaambia,
hadi mbingu na dunia zitakapopita, hakuna hata
herufi moja ndogo wala nukta itakayopotea kwa
namna yoyote kutoka kwa Torati, hadi kila kitu
kiwe kimetimia. 19 Kwa hiyo, yeyote atakayevunja
mojawapo ya amri ndogo kuliko zote ya amri hizi,
naye akawafundisha wengine kufanya hivyo, ataitwa
mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni, lakini
yeyote azitendaye na kuzifundisha hizi amri ataitwa
mkuu katika ufalme wa mbinguni. 20 Kwa maana
nawaambia, haki yenu isipozidi haki ya Mafarisayo na
walimu wa Torati, kamwe hamtaingia katika ufalme
wa mbinguni. 21 “Mmesikia walivyoambiwa watu wa
zamani kwamba, ‘Usiue. Yeyote atakayeua atapaswa
hukumu.’ 22 Lakini mimi nawaambia kwamba, yeyote
atakayemkasirikia ndugu yake, atapaswa hukumu.
Tena, yeyote atakayemwambia ndugu yake, ‘Raka,’
atapaswa kujibu kwa Baraza la Wayahudi. Lakini
yeyote atakayesema ‘Wewe mpumbavu!’ atapaswa
hukumu ya moto wa Jehanamu. **(Geenna g1067)** 23

“Kwa hiyo, ikiwa unatoa sadaka yako madhabahuni,
ukakumbuka kuwa ndugu yako ana kitu dhidi yako,
**24** iache sadaka yako hapo mbele ya madhabahu.
Nenda kwanza ukapatane na ndugu yako; kisha
urudi na ukatoe sadaka yako. **25** “Patana na mshtaki
wako upesi wakati mpo njiani kwenda mahakamani,
ili mshtaki wako asije akakutia mikononi mwa hakimu,
naye hakimu akakutia mikononi mwa askari, nawe
ukatupwa gerezani. **26** Amin, nakuambia, hutatoka
humo hadi uwe umelipa senti ya mwisho. **27**
“Mmesikia kwamba ilinenwa, ‘Usizini.’ **28** Lakini mimi
nawaambia kwamba, yeyote amtazamaye mwanamke
kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni
mwake. **29** Jicho lako la kuume likikusababisha
kutenda dhambi, ling’oe ulitupe mbali. Ni afadhali
kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako kuliko
mwili wako mzima ukatupwa Jehanamu. **(Geenna g1067)**
**30** Kama mkono wako wa kuume ukikusababisha
kutenda dhambi, ukate, uutupe mbali. Ni afadhali
kwako kupoteza kiungo kimoja cha mwili wako kuliko
mwili wako mzima utupwe Jehanamu. **(Geenna g1067)**
**31** “Pia ilinenwa kwamba, ‘Mtu yeyote amwachaye
mkewe sharti ampe hati ya talaka.’ **32** Lakini mimi
nawaambia, yeyote amwachaye mkewe isipokuwa
kwa kosa la uasherati, amfanya mkewe kuwa mzinzi.
Na yeyote amwoaye yule mwanamke aliyeachwa,
anazini. **33** “Tena mmesikia walivyoambiwa watu wa
zamani kwamba, ‘Usiape kwa uongo, bali timiza kiapo
kile ulichofanya kwa Mwenyezi Mungu.’ **34** Lakini mimi
nawaambia, msiape kabisa: iwe kwa mbingu, kwa
kuwa ni kiti cha enzi cha Mungu; **35** au kwa dunia,
kwa kuwa ndipo mahali pake pa kuwekea miguu;
au kwa Yerusalemu, kwa kuwa ndio mji wa Mfalme
Mkuu. **36** Nanyi msiape kwa vichwa vyenu, kwa
kuwa hamwezi kuufanya hata unywele mmoja kuwa
mweupe au mweusi. **37** ‘Ndiyo’ yenu iwe ‘Ndiyo,’ na
‘Hapana’ yenu iwe ‘Hapana.’ Lolote zaidi ya hili latoka
kwa yule mwovu. **38** “Mmesikia kwamba ilinenwa,
‘Jicho kwa jicho na jino kwa jino.’ **39** Lakini mimi
nawaambia, msishindane na mtu mwovu. Lakini kama
mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na
la pili pia. **40** Mtu akitaka kukushtaki na kuchukua
joho lako, mwachie achukue na koti pia. **41** Mtu
akikulazimisha kwenda maili moja, nenda naye maili
mbili. **42** Mpe yeye akuombaye, wala usimgeuzie
kisogo yeye atakaye kukukopa. **43** “Mmesikia kwamba
ilinenwa, ‘Mpende jirani yako na umchukie adui yako.’
**44** Lakini ninawaambia: Wapendeni adui zenu, na
waombeeni wanaowatesa ninyi, **45** ili mpate kuwa
watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana
yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu
wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na
wasio haki. **46** Mkiwapenda tu wale wanaowapenda,
mtapata thawabu gani? Je, hata watoza ushuru
hawafanyi hivyo? **47** Nanyi mkiwasalimu ndugu zenu
tu, je, mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu
wasiomjua Mungu hawafanyi hivyo? **48** Kwa hiyo
kuweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni
alivyo mkamilifu.

**6** “Angalieni msitende wema wenu mbele ya watu
ili wawaone. Kwa maana mkifanya hivyo, hamna
thawabu kutoka kwa Baba yenu aliye mbinguni. **2**
“Hivyo mnapowapa wahitaji, msitangaze hadharani
kama wafanyavyo wanafiki katika masinagogi na
mitaani, ili wasifiwe na watu. Amin nawaambia wao
wamekwisha kupokea thawabu yao. **3** Lakini ninyi
mtoapo sadaka, fanyeni kwa siri, hata mkono wako wa
kushoto usijue mkono wako wa kuume unachofanya,
**4** ili sadaka yako iwe ni siri. Ndipo Baba yako wa
mbinguni, yeye aonaye sirini atakupa thawabu kwa
wazi. **5** “Nanyi mnaposali, msiwe kama wanafiki,
maana wao hupenda kusali wakiwa wamesimama
katika masinagogi na kando ya barabara ili waonekane
na watu. Amin nawaambia, wao wamekwisha kupokea
thawabu yao. **6** Lakini wewe unaposali, ingia chumbani
mwako, funga mlango na umwombe Baba yako
aliye sirini. Naye Baba yako aonaye sirini atakupa
thawabu yako. **7** Nanyi mnaposali msiseme maneno
kama wafanyavyo watu wasiomjua Mungu. Kwa
maana wao hudhani kwamba watasikiwa kwa sababu
ya wingi wa maneno yao. **8** Msiwe kama wao,
kwa sababu Baba yenu anajua kile mnachohitaji
kabla hamjamwomba. **9** “Hivi ndivyo mnavyopaswa
kuomba: “‘Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako
litukuzwe. **10** Ufalme wako uje. Mapenzi yako
yafanyike hapa duniani kama huko mbinguni. **11**
Utupatie riziki yetu ya kila siku. **12** Utusamehe deni
zetu, kama sisi nasi tulivyokwisha kuwasamehe
wadeni wetu. **13** Usitutie majaribuni, bali utuokoe
kutoka kwa yule mwovu [kwa kuwa ufalme ni wako,
na nguvu, na utukufu, hata milele. Amen].’ **14** Kwa
kuwa mkiwasamehe watu wengine wanapowakosea,

Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi pia.
15 Lakini msipowasamehe watu wengine makosa
yao, naye Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa
yenu. 16 “Mnapofunga, msiwe wenye huzuni kama
wafanyavyo wanafiki. Maana wao hukunja nyuso
zao ili kuwaonesha wengine kwamba wamefunga.
Amin, amin nawaambia wao wamekwisha kupokea
thawabu yao kamilifu. 17 Lakini unapofunga, jipake
mafuta kichwani na kunawa uso wako, 18 ili kufunga
kwako kusionekane na watu wengine ila Baba yako
anayeketi mahali pa siri; naye Baba yako aonaye
sirini atakupa thawabu yako kwa wazi. 19 “Msijiwekee
hazina duniani, ambapo nondo na kutu huharibu,
nao wezi huvunja na kuiba. 20 Lakini jiwekeeni
hazina mbinguni, ambapo nondo na kutu haviharibu,
wala wezi hawavunji na kuiba. 21 Kwa sababu
mahali hazina yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako
utakapokuwa. 22 “Jicho ni taa ya mwili. Kama jicho
lako ni nyofu, mwili wako wote utajaa nuru. 23 Lakini
kama jicho lako ni ovu, mwili wako wote utajawa na
giza. Hivyo basi, ikiwa nuru iliyo ndani yako ni giza,
je, hilo ni giza nene aje! 24 “Hakuna mtu awezaye
kuwatumikia mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia
huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana
sana na huyu na kumdharau yule mwingine. Hamwezi
kumtumikia Mungu pamoja na Mali. 25 “Kwa hiyo
nawaambia, msisumbukie maisha yenu kwamba
mtakula nini au mtakunywa nini; au msumbukie miili
yenu kwamba mtavaa nini. Je, maisha si zaidi ya
chakula, na mwili zaidi ya mavazi? 26 Waangalieni
ndege wa angani; wao hawapandi wala hawavuni
au kuweka ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni
huwalisha. Je, ninyi si wa thamani kuliko hao ndege?
27 Ni nani miongoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha
kwake anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi
katika maisha yake? 28 “Nanyi kwa nini mnajitaabisha
kwa ajili ya mavazi? Fikirini maua ya shambani
yameavyo. Hayafanyi kazi wala hayafumi. 29 Lakini
nawaambia, hata Sulemani katika fahari yake yote
hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya hayo maua. 30
Basi ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya shambani,
ambayo leo yapo na kesho yanatupwa motoni, je,
hatawavika ninyi vizuri zaidi, enyi wa imani haba? 31
Kwa hiyo msiwe na wasiwasi, mkisema, ‘Tutakula
nini?’ au ‘Tutakunywa nini?’ au ‘Tutavaa nini?’ 32 Watu
wasiomjua Mungu ndio wanaoshindania hayo, lakini
Baba yenu wa mbinguni anafahamu kuwa mnahitaji
haya yote. 33 Lakini utafuteni kwanza ufalme wa
Mungu na haki yake, na haya yote atawapa pia. 34
Kwa hiyo msiwe na wasiwasi kuhusu kesho, kwa
sababu kesho itajitaabikia yenyewe. Kila siku ina
masumbufu yake ya kutosha.

7 “Usihukumu ili usije ukahukumiwa. 2 Kwa
maana jinsi unavyowahukumu wengine, ndivyo
utakavyohukumiwa, na kwa kipimo kile upimiacho,
ndicho utakachopimiwa. 3 “Mbona unatazama kibanzi
kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na wala huoni
boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe? 4 Au
unawezaje kumwambia ndugu yako, ‘Acha nitoe
kibanzi kwenye jicho lako,’ wakati kuna boriti kwenye
jicho lako mwenyewe? 5 Ewe mnafiki, ondoa boriti
ndani ya jicho lako kwanza, ndipo utaweza kuona
dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi kilicho ndani ya
jicho la ndugu yako. 6 “Msiwape mbwa vitu vilivyo
vitakatifu; wala msitupie nguruwe lulu zenu. Mkifanya
hivyo, watazikanyagakanyaga na kisha watawageukia
na kuwararua vipande vipande. 7 “Ombeni nanyi
mtapewa; tafuteni nanyi mtapata; bisheni nanyi
mtafunguliwa mlango. 8 Kwa kuwa kila aombaye
hupewa; naye kila atafutaye hupata; na kila abishaye
hufunguliwa mlango. 9 “Au ni nani miongoni mwenu
ambaye mwanawe akimwomba mkate atampa jiwe?
10 Au mwanawe akimwomba samaki atampa nyoka?
11 Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto
wenu vitu vizuri, si zaidi sana Baba yenu aliye
mbinguni atawapa vitu vizuri wale wamwombao? 12
Kwa hiyo chochote mnachotaka mtendewe na watu,
ninyi nanyi watendeeni vivyo hivyo. Kwa kuwa hii
ndiyo Torati na Manabii. 13 “Ingieni kupitia mlango
mwembamba, kwa maana lango ni pana na njia ni
pana ielekeayo upotevuni, nao ni wengi wanaoingia
kupitia lango hilo. 14 Lakini mlango ni mwembamba na
njia ni finyu ielekeayo kwenye uzima, nao ni wachache
tu waionao. 15 “Jihadharini na manabii wa uongo,
wanaowajia wakiwa wamevaa mavazi ya kondoo,
lakini ndani ni mbwa-mwitu wakali. 16 Mtawatambua
kwa matunda yao. Je, watu huchuma zabibu kwenye
miiba, au tini kwenye michongoma? 17 Vivyo hivyo, mti
mwema huzaa matunda mazuri, na mti mbaya huzaa
matunda mabaya. 18 Mti mwema hauwezi kuzaa
matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa
matunda mazuri. 19 Kila mti usiozaa matunda mazuri

hukatwa na kutupwa motoni. 20 Hivyo, mtawatambua kwa matunda yao. 21 “Si kila mtu aniambiaye, ‘Bwana, Bwana,’ atakayeingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. 22 Wengi wataniambia siku ile, ‘Bwana, Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo wachafu na kufanya miujiza mingi?’ 23 Ndipo nitakapowaambia wazi, ‘Sikuwajua kamwe. Ondokeni kwangu, ninyi watenda maovu!’ 24 “Kwa hiyo kila mtu ayasikiaye haya maneno yangu na kuyatenda, ni kama mtu mwenye busara aliyejenga nyumba yake kwenye mwamba. 25 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, na upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba. Lakini haikuanguka; kwa sababu msingi wake ulikuwa kwenye mwamba. 26 Kila anayesikia haya maneno yangu na asiyatende ni kama mtu mjinga aliyejenga nyumba yake kwenye mchanga. 27 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, nao upepo ukavuma ukaipiga hiyo nyumba, nayo ikaanguka kwa kishindo kikubwa.” 28 Isa alipomaliza kusema maneno haya, umati wa watu wakashangazwa sana na mafundisho yake, 29 kwa sababu alifundisha kama yeye aliye na mamlaka, wala si kama walimu wao wa sheria.

**8** Isa aliposhuka kutoka mlimani, makundi ya watu wakamfuata. 2 Mtu mmoja mwenye ukoma akaja na kupiga magoti mbele yake, akasema, “Bwana, ukitaka, unaweza kunitakasa.” 3 Isa akanyoosha mkono wake akamgusa yule mtu, akamwambia, “Nataka. Takasika!” Mara yule mtu akatakasika ukoma wake. 4 Kisha Isa akamwambia, “Hakikisha humwambii mtu yeyote. Lakini nenda ukajioneshe kwa kuhani, na utoe sadaka aliyoamuru Musa, ili kuwa ushuhuda kwao.” 5 Isa alipoingia Kapernaumu, jemadari mmoja alimjia, kumwomba msaada, 6 akisema, “Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani na amepooza, tena ana maumivu makali ya kutisha.” 7 Isa akamwambia, “Nitakuja na kumponya.” 8 Lakini yule jemadari akamwambia, “Bwana, mimi sistahili wewe kuingia ndani ya nyumba yangu. Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona. 9 Kwa kuwa mimi mwenyewe ni mtu niliye chini ya mamlaka, nikiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu, ‘Nenda,’ yeye huenda; na mwingine nikimwambia, ‘Njoo,’ yeye huja. Nikimwambia mtumishi wangu, ‘Fanya hivi,’ yeye hufanya.” 10 Isa aliposikia maneno haya, alishangaa, akawaambia wale waliomfuata, “Amin, nawaambia, hata katika Israeli sijapata kuona yeyote mwenye imani kubwa namna hii. 11 Ninawaambia kwamba wengi watatoka mashariki na magharibi, nao wataketi karamuni pamoja na Ibrahimu, Isaka na Yakobo katika ufalme wa mbinguni. 12 Lakini warithi wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ambako kutakuwa kilio na kusaga meno.” 13 Kisha Isa akamwambia yule jemadari, “Nenda na iwe kwako sawasawa na imani yako.” Naye yule mtumishi akapona wakati ule ule. 14 Isa alipoingia nyumbani mwa Petro, alimkuta mama mkwe wa Petro amelala kitandani, akiwa ana homa. 15 Akamgusa mkono wake na homa ikamwacha, naye akainuka na kuanza kumhudumia. 16 Jioni ile, wakamletea watu wengi waliopagawa na pepo wachafu, naye akawatoa wale pepo wachafu kwa neno lake, na kuwaponya wagonjwa wote. 17 Haya yalifanyika ili litimie neno lililonenwa kwa kinywa cha nabii Isaya, kwamba: “Mwenyewe alitwaa udhaifu wetu na akachukua magonjwa yetu.” 18 Isa alipoona makundi mengi yamemzunguka, aliwaamuru wanafunzi wake wavuke hadi ng’ambo ya ziwa. 19 Kisha mwalimu mmoja wa sheria akamjia Isa na kumwambia, “Mwalimu, nitakufuata popote utakakoenda.” 20 Naye Isa akamjibu, “Mbweha wana mapango, nao ndege wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana mahali pa kulaza kichwa chake.” 21 Mwanafunzi mwingine akamwambia, “Bwana, niruhusu kwanza nikamzike baba yangu.” 22 Lakini Isa akamwambia, “Nifuate, uwaache wafu wawazike wafu wao.” 23 Naye alipoingia kwenye mashua, wanafunzi wake wakamfuata. 24 Ghafula, kukatokea dhoruba kali baharini hata mashua ikaanza kufunikwa na mawimbi, lakini Isa alikuwa amelala usingizi. 25 Wanafunzi wake wakamwendea na kumwamsha, wakisema, “Bwana, tuokoe! Tunazama!” 26 Naye Isa akawaambia, “Kwa nini mnaogopa, enyi wa imani haba?” Kisha akaamka na kukemea dhoruba na mawimbi, nayo bahari ikatulia kabisa. 27 Wale watu wakashangaa, wakisema, “Ni mtu wa namna gani huyu? Hata upepo na mawimbi vinamtii!” 28 Walipofika ng’ambo katika nchi ya Wagerasi, watu wawili waliopagawa na pepo wachafu walitoka makaburini nao wakakutana naye. Watu hawa walikuwa wakali mno kiasi kwamba hakuna mtu aliyeweza kupita njia ile. 29 Wakapaza sauti wakisema,

“Una nini nasi, Mwana wa Mungu? Umekuja hapa
kututesa kabla ya wakati ulioamriwa?” 30 Mbali kidogo
kutoka pale walipokuwa, kulikuwa na kundi kubwa la
nguruwe wakila. 31 Wale pepo wachafu wakamsihi
Isa, “Ukitutoa humu, turuhusu twende kwenye lile
kundi la nguruwe.” 32 Akawaambia, “Nendeni!” Hivyo
wakatoka na kuwaingia wale nguruwe, nalo kundi
lote likateremka gengeni kwa kasi, likaingia katika
ziwa na kufa ndani ya maji. 33 Wale watu waliokuwa
wakiwachunga hao nguruwe wakakimbia wakaingia
mjini, wakaeleza yote yaliyowatokea wale waliokuwa
wamepagawa na pepo wachafu. 34 Kisha watu wote
wa mji huo wakatoka kwenda kukutana na Isa. Nao
walipomwona wakamsihi aondoke kwenye nchi yao.

9 Isa akaingia kwenye chombo, akavuka na kufika
katika mji wa kwao. 2 Wakati huo huo wakamletea
mtu aliyepooza, akiwa amelazwa kwenye mkeka.
Isa alipoiona imani yao, alimwambia yule mtu
aliyepooza, “Mwanangu, jipe moyo mkuu. Dhambi
zako zimesamehewa.” 3 Kwa ajili ya jambo hili,
baadhi ya walimu wa Torati wakasema mioyoni mwao,
“Huyu mtu anakufuru!” 4 Lakini Isa akiyafahamu
mawazo yao, akawaambia, “Kwa nini mnawaza
maovu mioyoni mwenu? 5 Je, ni lipi lililo rahisi zaidi:
kusema, ‘Umesamehewa dhambi zako,’ au kusema,
‘Inuka, uende’? 6 Lakini nataka mpate kujua kwamba
Mwana wa Adamu ana mamlaka duniani kusamehe
dhambi.” Ndipo akamwambia yule aliyepooza, “Inuka,
chukua mkeka wako, uende nyumbani mwako.” 7
Yule mtu akasimama, akaenda nyumbani mwake.
8 Umati wa watu walipoyaona haya, wakajawa na
hofu ya Mungu, wakamtukuza Mungu aliyekuwa
amewakabidhi wanadamu mamlaka kama haya. 9
Isa alipokuwa akienda kutoka huko, alimwona mtu
mmoja jina lake Mathayo akiwa ameketi forodhani
mahali pa kutoza ushuru. Isa akamwambia, “Nifuate.”
Mathayo akasimama, akamfuata. 10 Isa alipokuwa
ameketi akila chakula ndani ya nyumba ya Mathayo,
watoza ushuru wengi na wenye dhambi wakaja,
wakaketi kula pamoja naye na wanafunzi wake. 11
Mafarisayo walipoona mambo haya, wakawauliza
wanafunzi wake, “Kwa nini Mwalimu wenu anakula
na watoza ushuru na wenye dhambi?” 12 Lakini
Isa aliposikia hayo, akawaambia, “Watu wenye
afya hawahitaji tabibu, lakini wale walio wagonjwa
ndio wanaohitaji tabibu. 13 Nendeni mkajifunze
maana ya maneno haya: ‘Nataka rehema, wala si
dhabihu.’ Kwa maana sikuja kuwaita wenye haki, bali
wenye dhambi.” 14 Wanafunzi wa Yahya wakaja na
kumuuliza Isa, “Imekuwaje kwamba sisi na Mafarisayo
tunafunga, lakini wanafunzi wako hawafungi?” 15
Isa akawajibu, “Wageni wa bwana arusi wanawezaje
kuomboleza wakati angali pamoja nao? Wakati utafika
ambapo bwana arusi ataondolewa kwao. Hapo ndipo
watakapofunga. 16 “Hakuna mtu anayeshonea kiraka
kipya kwenye nguo iliyochakaa, kwa maana kile
kiraka kitachanika kutoka kwenye hiyo nguo, nayo
hiyo nguo itachanika zaidi. 17 Wala watu hawaweki
divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Wakifanya hivyo,
viriba vitapasuka nayo divai itamwagika, navyo viriba
vitaharibika. Lakini divai mpya huwekwa kwenye
viriba vipya, na hivyo divai na viriba huwa salama.”
18 Isa alipokuwa akiwaambia mambo haya, kiongozi
wa sinagogi akaingia, akapiga magoti mbele yake,
akamwambia, “Binti yangu amekufa sasa hivi. Lakini
njoo uweke mkono wako juu yake, naye ataishi.”
19 Isa akaondoka akafuatana naye, nao wanafunzi
wake pia wakaandamana naye. 20 Wakati huo
huo, mwanamke mmoja, aliyekuwa na ugonjwa wa
kutokwa damu kwa muda wa miaka kumi na mbili,
akaja nyuma ya Isa, akagusa upindo wa vazi lake,
21 kwa maana alisema moyoni mwake, “Nikigusa
tu vazi lake, nitaponywa.” 22 Isa akageuka, naye
alipomwona akamwambia, “Binti, jipe moyo, imani
yako imekuponya.” Naye yule mwanamke akapona
kuanzia saa hiyo. 23 Isa alipofika nyumbani mwa
yule kiongozi wa sinagogi na kuwaona waombolezaji
wakipiga filimbi za maombolezo na watu wengi
wakipiga kelele, 24 akawaambia, “Ondokeni! Kwa
maana binti huyu hakufa, bali amelala.” Wakamcheka
kwa dhihaka. 25 Lakini watu walipokwisha kutolewa
nje, akaingia mle ndani na kumshika yule binti
mkono, naye akaamka. 26 Habari hizi zikaenea
katika maeneo yale yote. 27 Isa alipokuwa akiondoka
mahali pale, vipofu wawili wakamfuata wakipaza
sauti na kusema, “Mwana wa Daudi, tuhurumie!”
28 Alipoingia mle nyumbani wale vipofu wakamjia.
Naye Isa akawauliza, “Mnaamini kwamba ninaweza
kufanya jambo hili?” Wakamjibu, “Ndiyo, Bwana.”
29 Ndipo Isa akagusa macho yao na kusema,
“Iwe kwenu sawasawa na imani yenu.” 30 Macho
yao yakafunguka. Isa akawaonya vikali, akisema,

“Chungeni mtu yeyote asijue kuhusu jambo hili.”
**31** Lakini wao wakaenda na kueneza habari zake
katika eneo lile lote. **32** Walipokuwa wanatoka, mtu
mmoja aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu na
ambaye hakuweza kuongea aliletwa kwa Isa. **33**
Yule pepo mchafu alipotolewa, yule mtu aliyekuwa
bubu akaongea, na umati wa watu wakastaajabu
na kusema, “Jambo kama hili kamwe halijapata
kuonekana katika Israeli.” **34** Lakini Mafarisayo
wakasema, “Huyo anatoa pepo wachafu kwa uwezo
wa mkuu wa pepo wachafu.” **35** Isa akazunguka katika
miji yote na vijiji vyote, akifundisha katika masinagogi
yao, akihubiri Habari Njema za ufalme, na akiponya
kila ugonjwa na kila aina ya maradhi. **36** Alipoona
umati wa watu, aliwahurumia kwa sababu walikuwa
wanasumbuka bila msaada, kama kondoo wasiokuwa
na mchungaji. **37** Ndipo akawaambia wanafunzi wake,
“Mavuno ni mengi lakini watendakazi ni wachache.
**38** Kwa hiyo mwombeni Bwana wa mavuno, ili atume
watendakazi katika shamba lake la mavuno.”

**10** Ndipo Isa akawaita wanafunzi wake kumi na
wawili, naye akawapa mamlaka juu ya pepo
wachafu, ili waweze kuwatoa na kuponya kila ugonjwa
na maradhi ya kila aina. **2** Haya ndiyo majina ya
hao mitume kumi na wawili: wa kwanza, Simoni
aitwaye Petro, na Andrea nduguye; Yakobo mwana
wa Zebedayo, na Yohana nduguye; **3** Filipo, na
Bartholomayo; Tomaso, na Mathayo mtoza ushuru;
Yakobo mwana wa Alfayo, na Thadayo; **4** Simoni
Mkananayo, na Yuda Iskariote aliyemsaliti Isa. **5** Hawa
kumi na wawili, Isa aliwatuma akawaagiza: “Msiende
miongoni mwa watu wa Mataifa, wala msiingie mji
wowote wa Wasamaria. **6** Lakini afadhali mshike njia
kuwaendea kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea.
**7** Mnapoenda, hubirini ujumbe huu, ‘Ufalme wa
mbinguni umekaribia.’ **8** Ponyeni wagonjwa, fufueni
wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo wachafu.
Mmepata bure, toeni bure. **9** Msichukue dhahabu,
wala fedha, wala shaba kwenye vifuko vyenu. **10**
Msichukue mkoba wa safari, wala kanzu mbili,
wala jozi ya pili ya viatu, wala fimbo, kwa maana
mtendakazi anastahili posho yake. **11** “Mji wowote
au kijiji chochote mtakapoingia, tafuteni humo mtu
anayestahili, nanyi kaeni kwake hadi mtakapoondoka.
**12** Mkiingia kwenye nyumba, itakieni amani. **13** Kama
nyumba hiyo inastahili, amani yenu na iwe juu yake.
La sivyo, amani yenu na iwarudie ninyi. **14** Kama
mtu yeyote hatawakaribisha ninyi, wala kusikiliza
maneno yenu, kung’uteni mavumbi kutoka miguu
yenu mtakapokuwa mnatoka kwenye nyumba hiyo au
mji huo. **15** Amin, nawaambia, itakuwa rahisi zaidi kwa
miji ya Sodoma na Gomora kustahimili katika hukumu
kuliko mji huo. **16** “Tazama ninawatuma kama kondoo
katikati ya mbwa-mwitu. Kwa hiyo mwe werevu
kama nyoka na wapole kama hua. **17** “Jihadharini
na wanadamu; kwa maana watawapeleka katika
mabaraza yao na kuwapiga kwenye masinagogi yao.
**18** Nanyi mtaburutwa mbele ya watawala na wafalme
kwa ajili yangu, ili kuwa ushuhuda kwao na kwa
watu wa Mataifa. **19** Lakini watakapowapeleka humo,
msisumbuke kufikiria mtakalosema, kwa maana
mtapewa la kusema wakati huo. **20** Kwa sababu
si ninyi mtakaokuwa mkinena, bali ni Roho wa
Baba yenu atakayekuwa akinena kupitia kwenu. **21**
“Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe, naye baba
atamsaliti mtoto wake. Watoto nao wataasi dhidi
ya wazazi wao na kusababisha wauawe. **22** Watu
wote watawachukia kwa ajili ya Jina langu. Lakini
yule atakayevumilia hadi mwisho ataokolewa. **23**
Wakiwatesa katika mji mmoja, kimbilieni mji mwingine.
Amin, amin nawaambia, hamtamaliza miji yote ya
Israeli kabla Mwana wa Adamu kuja. **24** “Mwanafunzi
hawezi kumzidi mwalimu wake, wala mtumishi hamzidi
bwana wake. **25** Yatosha mwanafunzi kuwa kama
mwalimu wake, na mtumishi kuwa kama bwana
wake. Ikiwa mkuu wa nyumba ameitwa Beelzebuli,
je, si watawaita zaidi wale wa nyumbani mwake! **26**
“Basi msiwaogope, kwa maana hakuna kilichofichika
ambacho hakitafunuliwa, wala hakuna siri ambayo
haitajulikana. **27** Ninalowaambia gizani, ninyi lisemeni
mchana peupe. Na lile mnalosikia likinong’onwa
masikioni mwenu, lihubirini juu ya nyumba. **28**
Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua
roho. Afadhali mwogopeni yeye awezaye kuiangamiza
roho na mwili katika Jehanamu. **(Geenna g1067)** **29** Je,
shomoro wawili hawauzwi kwa senti moja tu? Lakini
hakuna hata mmoja wao atakayeanguka chini pasipo
Baba yenu kujua. **30** Hata nywele za vichwa vyenu
zote zimehesabiwa. **31** Hivyo msiogope; kwa maana
ninyi ni wa thamani kubwa kuliko shomoro wengi.
**32** “Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, mimi nami
nitamkiri yeye mbele za Baba yangu aliye mbinguni.

33 Lakini yeyote atakayenikana mimi mbele ya watu,
mimi nami nitamkana mbele za Baba yangu aliye
mbinguni. 34 “Msidhani kwamba nimekuja kuleta
amani duniani. Sikuja kuleta amani bali upanga. 35
Kwa maana nimekuja kuleta uadui kati ya “‘mtu na
baba yake, binti na mama yake, mkwe na mama
mkwe wake; 36 nao adui za mtu watakuwa ni wale
watu wa nyumbani mwake.’ 37 “Yeyote ampendaye
baba yake au mama yake kuliko anavyonipenda mimi,
hastahili kuwa wangu. Yeyote ampendaye mwanawe
au binti yake kuliko anavyonipenda mimi, hastahili
kuwa wangu. 38 Tena yeyote asiyeuchukua msalaba
wake na kunifuata, hastahili kuwa wangu. 39 Kwa
maana yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake
atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza maisha
yake kwa ajili yangu atayapata. 40 “Mtu yeyote
atakayewapokea ninyi atakuwa amenipokea mimi, na
yeyote atakayenipokea mimi atakuwa amempokea
yeye aliyenituma. 41 Mtu yeyote anayempokea nabii
kwa kuwa ni nabii atapokea thawabu ya nabii, naye
mtu anayempokea mwenye haki kwa kuwa ni mwenye
haki atapokea thawabu ya mwenye haki. 42 Mtu
yeyote akimpa hata kikombe cha maji baridi mmoja
wa hawa wadogo kwa kuwa ni mwanafunzi wangu,
amin, nawaambia, hataikosa thawabu yake.”

**11** Baada ya Isa kumaliza kutoa maagizo kwa
wanafunzi wake kumi na wawili, aliondoka hapo
akaenda kufundisha na kuhubiri katika miji ya Galilaya.
2 Yahya aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo
Al-Masihi alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi
wake 3 ili wakamuulize, “Wewe ndiwe yule aliyekuwa
aje, au tumngojee mwingine?” 4 Isa akajibu, “Rudini
mkamwambie Yahya yale mnayosikia na kuyaona:
5 Vipofu wanapata kuona, viwete wanatembea,
wenye ukoma wanatakaswa, viziwi wanasikia, wafu
wanafufuliwa, na maskini wanahubiriwa Habari
Njema. 6 Amebarikiwa mtu yule asiyechukizwa na
mimi.” 7 Wale wanafunzi wa Yahya walipokuwa
wanaondoka, Isa akaanza kusema na umati wa watu
kuhusu Yahya. Akawauliza, “Mlipoenda kule nyikani,
mlienda kuona nini? Je, ni unyasi ukipeperushwa
na upepo? 8 Kama sivyo, mlienda kuona nini
basi? Mtu aliyevaa mavazi ya kifahari? La hasha!
Watu wanaovaa mavazi ya kifahari wako katika
majumba ya wafalme. 9 Basi mlienda kuona nini?
Mlienda kumwona nabii? Naam, nawaambia, yeye ni
zaidi ya nabii. 10 Huyu ndiye ambaye habari zake
zimeandikwa: “‘Tazama nitamtuma mjumbe wangu
mbele yako, atakayetengeneza njia mbele yako.’ 11
Amin, nawaambia, miongoni mwa wale waliozaliwa na
wanawake, hajatokea mtu aliye mkuu kuliko Yahya.
Lakini aliye mdogo kabisa katika ufalme wa mbinguni
ni mkuu kuliko Yahya. 12 Tangu siku za Yahya hadi
sasa, ufalme wa mbinguni hunyakuliwa kwa nguvu,
nao wenye nguvu wanauteka. 13 Kwa maana manabii
wote na Torati walitabiri hadi wakati wa Yahya. 14
Ikiwa mko tayari kukubali hilo, yeye ndiye yule Ilya
ambaye manabii walikuwa wamesema angekuja. 15
Yeye aliye na masikio, na asikie. 16 “Lakini kizazi
hiki nikifananishe na nini? Kinafanana na watoto
waliokaa sokoni wakiwaita wenzao na kuwaambia, 17
“‘Tuliwapigia filimbi, lakini hamkucheza; tuliwaimbia
nyimbo za maombolezo, lakini hamkuomboleza.’
18 Kwa maana Yahya alikuja, alikuwa hali wala
hanywi, nao wanasema, ‘Yeye ana pepo mchafu.’
19 Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa, nao
wanasema, ‘Tazameni huyu mlafi na mlevi, rafiki wa
watoza ushuru na “wenye dhambi.”’ Lakini hekima
huthibitishwa kuwa kweli kwa matendo yake.” 20 Ndipo
Isa akaanza kuishutumu miji ambayo alifanya miujiza
yake mingi, kwa maana watu wake hawakutubu.
21 “Ole wako, Korazini! Ole wako Bethsaida! Kwa
maana kama miujiza iliyofanyika kwenu, ingefanyika
Tiro na Sidoni, miji hiyo ingekuwa imetubu zamani
kwa kuvaa magunia na kujipaka majivu. 22 Lakini
nawaambia, itakuwa rahisi zaidi kwa Tiro na Sidoni
kustahimili katika siku ya hukumu, kuliko ninyi. 23
Nawe Kapernaumu, je, utainuliwa hadi mbinguni? La
hasha! Utashushwa hadi Kuzimu. Miujiza iliyofanyika
kwako ingefanyika huko Sodoma, mji huo ungekuwepo
hadi leo. **(Hadēs g86)** 24 Lakini nakuambia kwamba,
itakuwa rahisi zaidi kwa Sodoma kustahimili katika
siku ya hukumu kuliko wewe.” 25 Wakati huo Isa
alisema, “Nakuhimidi Baba, Bwana wa mbingu na
nchi, kwa kuwa umewaficha mambo haya wenye
hekima na wenye elimu, nawe ukawafunulia watoto
wadogo. 26 Naam, Baba, kwa kuwa hivyo ndivyo
ilivyokupendeza. 27 “Nimekabidhiwa vitu vyote na
Baba yangu: Hakuna mtu amjuaye Mwana ila Baba,
wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana na yeyote
ambaye Mwana anapenda kumfunulia. 28 “Njooni
kwangu, ninyi nyote mnaotaabika na kulemewa na

mizigo, nami nitawapumzisha. 29 Jifungeni nira yangu,
mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole
na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha katika
nafsi zenu. 30 Kwa maana nira yangu ni laini na
mzigo wangu ni mwepesi.”

12 Wakati huo Isa alipitia kwenye mashamba
ya nafaka siku ya Sabato. Wanafunzi wake
walikuwa na njaa, nao wakaanza kuvunja masuke
ya nafaka na kuyala. 2 Lakini Mafarisayo walipoona
jambo hili, wakamwambia, “Tazama! Wanafunzi wako
wanafanya jambo lisilo halali kufanywa siku ya
Sabato.” 3 Isa akawajibu, “Je, hamjasoma alichofanya
Daudi na wenzake walipokuwa na njaa? 4 Aliingia
katika nyumba ya Mungu, akala mikate iliyowekwa
wakfu, yeye na wenzake, jambo ambalo halikuwa
halali kwao kufanya, isipokuwa makuhani tu. 5 Au
hamjasoma katika Torati kwamba siku ya Sabato
makuhani huvunja sheria ya Sabato Hekaluni lakini
hawahesabiwi kuwa na hatia? 6 Nawaambia wazi
kwamba, yeye aliye mkuu kuliko Hekalu yupo hapa.
7 Kama mngekuwa mmejua maana ya maneno haya,
‘Nataka rehema, wala si dhabihu,’ msingewalaumu
watu wasio na hatia, 8 kwa maana Mwana wa
Adamu ndiye Bwana wa Sabato.” 9 Isa akaondoka
mahali hapo, akaingia ndani ya sinagogi lao, 10 na
huko alikuwepo mtu aliyepooza mkono. Wakitafuta
sababu ya kumshtaki Isa, wakamuuliza, “Je, ni halali
kuponya siku ya Sabato?” 11 Isa akawaambia, “Ni
nani miongoni mwenu, mwenye kondoo wake ambaye
huyo kondoo akitumbukia shimoni siku ya Sabato
hatamtoa? 12 Mtu ana thamani kubwa kuliko kondoo.
Kwa hiyo ni halali kutenda mema siku ya Sabato.”
13 Ndipo akamwambia yule mtu, “Nyoosha mkono
wako.” Akaunyoosha, nao ukaponywa ukawa mzima
kama ule mwingine. 14 Lakini Mafarisayo wakatoka
nje na kupanga njama ya kumuua Isa. 15 Lakini
Isa alipoyatambua mawazo yao, akaondoka mahali
hapo. Watu wengi walimfuata, naye akawaponya
wote waliokuwa wagonjwa miongoni mwao, 16
akiwakataza wasiseme yeye ni nani, 17 ili neno
lililonenwa na nabii Isaya litimie, aliposema: 18
“Tazama mtumishi wangu niliyemchagua, mpendwa
wangu, ninayependezwa naye. Nitaweka Roho wangu
Mtakatifu juu yake, naye atatangaza haki kwa mataifa.
19 Hatagombana wala kupaza sauti, wala hakuna
atakayesikia sauti yake njiani. 20 Mwanzi uliopondeka
hatauvunja, na utambi unaofuka moshi hatauzima,
hadi atakapoifanya haki ishinde. 21 Katika Jina lake
mataifa wataweka tumaini lao.” 22 Kisha wakamletea
mtu aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu, na
alikuwa kipofu na bubu. Isa akamponya, hata akaweza
kusema na kuona. 23 Watu wote wakashangaa na
kusema, “Je, yawezekana huyu ndiye Mwana wa
Daudi?” 24 Lakini Mafarisayo waliposikia jambo hili
wakasema, “Mtu huyu anatoa pepo wachafu kwa
uwezo wa Beelzebuli, mkuu wa pepo wachafu.” 25
Isa alijua walichokuwa wakiwaza, hivyo akawaambia,
“Kila ufalme ukigawanyika dhidi yake wenyewe
huangamia. Hali kadhalika kila mji au watu wa nyumba
moja waliogawanyika dhidi yao wenyewe hawawezi
kusimama. 26 Shetani akimtoa Shetani, atakuwa
amegawanyika yeye mwenyewe. Basi ufalme wake
utawezaje kusimama? 27 Nami kama natoa pepo
wachafu kwa nguvu za Beelzebuli, watu wenu je, wao
hutoa pepo wachafu kwa uwezo wa nani? Hivyo basi,
wao ndio watakaowahukumu. 28 Lakini kama mimi
ninatoa pepo wachafu kwa Roho wa Mungu, basi
ufalme wa Mungu umekuja juu yenu. 29 “Au tena, mtu
anawezaje kuingia katika nyumba ya mtu mwenye
nguvu na kuteka nyara mali yake asipomfunga
kwanza yule mwenye nguvu? Akishamfunga, ndipo
hakika anaweza kuteka nyara mali yake. 30 “Mtu
asiyekuwa pamoja nami yu kinyume nami, na mtu
ambaye hakusanyi pamoja nami, hutawanya. 31
Kwa hiyo nawaambia, kila dhambi na kufuru watu
watasamehewa, lakini mtu atakayemkufuru Roho
Mtakatifu wa Mungu hatasamehewa. 32 Mtu yeyote
atakayesema neno dhidi ya Mwana wa Adamu
atasamehewa, lakini yeyote anenaye neno dhidi
ya Roho wa Mungu hatasamehewa, iwe katika
ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao. (aiōn g165) 33
“Ufanye mti kuwa mzuri, nayo matunda yake yatakuwa
mazuri. Au ufanye mti kuwa mbaya, na matunda yake
yatakuwa mabaya. Kwa maana mti hutambulika kwa
matunda yake. 34 Enyi uzao wa nyoka! Mnawezaje
kunena mambo mema, wakati ninyi ni waovu? Kwa
maana kinywa cha mtu huyanena yale yaliyoujaza
moyo wake. 35 Mtu mwema hutoa yaliyo mema kutoka
hazina ya mambo mema yaliyohifadhiwa ndani yake,
naye mtu mwovu hutoa yaliyo maovu kutoka hazina ya
mambo maovu yaliyohifadhiwa ndani yake. 36 Lakini
nawaambia, katika siku ya hukumu watu watatoa

maelezo kuhusu kila neno walilonena lisilo la maana.
37 Kwa maana kwa maneno yako utahesabiwa haki,
na kwa maneno yako utahukumiwa.” 38 Kisha baadhi
ya Mafarisayo na walimu wa Torati wakamwambia,
“Mwalimu, tunataka kuona ishara kutoka kwako.” 39
Lakini yeye akawajibu, “Kizazi kiovu na cha uzinzi
kinaomba ishara! Lakini hakitapewa ishara yoyote
isipokuwa ile ishara ya nabii Yona. 40 Kwa maana
kama vile Yona alivyokuwa ndani ya tumbo la samaki
mkubwa sana kwa siku tatu, usiku na mchana, vivyo
hivyo Mwana wa Adamu atakuwa katika moyo wa
nchi siku tatu, usiku na mchana. 41 Siku ya hukumu,
watu wa Ninawi watasimama pamoja na kizazi hiki na
kukihukumu; kwa maana wao walitubu waliposikia
mahubiri ya Yona. Na tazama, hapa yupo yeye aliye
mkuu kuliko Yona. 42 Malkia wa Kusini atasimama
wakati wa hukumu na kukihukumu kizazi hiki. Kwa
kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia ili kuisikiliza
hekima ya Sulemani. Na hapa yupo aliye mkuu
kuliko Sulemani. 43 “Pepo mchafu amtokapo mtu,
hutangatanga katika sehemu zisizo na maji akitafuta
mahali pa kupumzika, lakini hapati. 44 Ndipo husema,
‘Nitarudi kwenye nyumba yangu nilikotoka.’ Naye
anaporudi huikuta ile nyumba ikiwa tupu, imefagiliwa
na kupangwa vizuri. 45 Kisha huenda na kuwaleta
pepo wachafu wengine saba wabaya kuliko yeye
mwenyewe, nao huingia na kukaa humo. Nayo hali
ya mwisho ya yule mtu huwa ni mbaya kuliko ile ya
kwanza. Ndivyo itakavyokuwa kwa kizazi hiki kiovu.”
46 Wakati alikuwa angali anazungumza na umati
wa watu, mama yake na ndugu zake wakasimama
nje wakitaka kuongea naye. 47 Ndipo mtu mmoja
akamwambia, “Tazama, mama yako na ndugu zako
wamesimama nje, wanataka kuongea na wewe.”
48 Lakini yeye akamjibu na kumwambia yule mtu,
“Mama yangu ni nani, nao ndugu zangu ni nani?” 49
Akawanyooshea mkono wanafunzi wake, akasema,
“Hawa hapa ndio mama yangu na ndugu zangu! 50
Kwa maana yeyote afanyaye mapenzi ya Baba yangu
wa mbinguni, huyo ndiye kaka yangu, na dada yangu,
na mama yangu.”

**13** Siku hiyo hiyo Isa akatoka nje ya nyumba,
akaketi kando ya bahari. 2 Umati mkubwa mno
wa watu wakakusanyika kumzunguka, hata ikabidi
aingie katika chombo na kuketi humo, nao watu wote
wakawa wamesimama ukingoni mwa bahari. 3 Ndipo
akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema:
“Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake. 4
Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine zilianguka
kando ya njia, nao ndege wakaja na kuzila. 5 Nyingine
zilianguka kwenye ardhi yenye mwamba isiyo na
udongo wa kutosha. Zikaota haraka, kwa kuwa udongo
ulikuwa haba. 6 Lakini jua lilipozidi, mimea ikanyauka
na kukauka kwa kuwa mizizi yake haikuwa na kina.
7 Mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba, nayo
miiba hiyo ikakua, ikaisonga hiyo mimea. 8 Mbegu
nyingine zilianguka kwenye udongo mzuri ambapo
zilitoa mazao, nyingine mara mia moja, nyingine
mara sitini, na nyingine mara thelathini. 9 Mwenye
masikio ya kusikia, na asikie.” 10 Wanafunzi wake
wakamwendea, wakamuuliza, “Kwa nini unasema na
watu kwa mifano?” 11 Akawajibu, “Ninyi mmepewa
ujuzi wa siri za ufalme wa mbinguni, lakini wao
hawajapewa. 12 Kwa maana yule aliye na kitu
atapewa zaidi, naye atakuwa navyo tele. Lakini yule
asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang’anywa.
13 Hii ndiyo sababu nasema nao kwa mifano: “Ingawa
wanatazama, hawaoni; wanasikiliza, lakini hawasikii,
wala hawaelewi. 14 Kwao unatimia ule unabii wa Isaya
aliposema: “‘Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa;
na pia mtatazama lakini hamtaona. 15 Kwa kuwa
mioyo ya watu hawa imekuwa migumu; hawasikii
kwa masikio yao, na wamefumba macho yao. Wasije
wakaona kwa macho yao, na wakasikiliza kwa
masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, na kugeuka
nami nikawaponya.’ 16 Lakini heri macho yenu kwa
sababu yanaona, na heri masikio yenu kwa sababu
yanasikia. 17 Amin, nawaambia, manabii wengi na
wenye haki walitamani kuona yale mnayoyaona
lakini hawakuyaona, na walitamani kusikia yale
mnayoyasikia lakini hawakuyasikia. 18 “Sikilizeni basi
maana ya ule mfano wa mpanzi: 19 Mtu yeyote
anaposikia neno la ufalme naye asilielewe, yule
mwovu huja na kunyakua kile kilichopandwa moyoni
mwake. Hii ndiyo ile mbegu iliyopandwa kando ya
njia. 20 Ile mbegu iliyopandwa kwenye sehemu yenye
mawe ni mtu yule ambaye hulisikia neno na hulipokea
mara moja kwa furaha. 21 Lakini kwa kuwa hana
mizizi yenye kina ndani yake, lile neno hudumu kwa
muda mfupi tu. Kisha dhiki au mateso yanapoinuka
kwa ajili ya lile neno, yeye anarudi nyuma mara
moja. 22 Ile mbegu iliyopandwa katika miiba ni yule

mtu anayelisikia neno, lakini masumbufu ya maisha
haya na udanganyifu wa mali hulisonga lile neno
na kulifanya lisizae matunda. (aiōn g165) 23 Lakini ile
mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri ni yule mtu
ambaye hulisikia neno na kulielewa. Naye hakika
huzaa matunda, akizaa mara mia, au mara sitini,
au mara thelathini ya mbegu iliyopandwa." 24 Isa
akawaambia mfano mwingine, akasema: "Ufalme wa
mbinguni unaweza kufananishwa na mtu aliyepanda
mbegu nzuri katika shamba lake. 25 Lakini wakati
kila mtu alipokuwa amelala, adui yake akaja na
kupanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.
26 Ngano ilipoota na kutoa masuke, magugu nayo
yakatokea. 27 "Watumishi wa yule mwenye shamba
wakamjia na kumwambia, 'Bwana, si tulipanda mbegu
nzuri shambani mwako? Basi, magugu yametoka
wapi?' 28 "Akawajibu, 'Adui ndiye alifanya jambo
hili.' "Wale watumishi wakamuuliza, 'Je, unataka
twende tukayang'oe?' 29 "Lakini akasema, 'Hapana,
msiyang'oe, kwa maana wakati mking'oa magugu
mnaweza mkang'oa na ngano pamoja nayo. 30
Acheni ngano na magugu vikue vyote pamoja hadi
wakati wa mavuno. Wakati huo nitawaambia wavunaji
wayakusanye magugu kwanza, wayafunge matita
matita ili yachomwe moto; kisha wakusanye ngano
na kuileta ghalani mwangu.'" 31 Akawaambia mfano
mwingine, akasema, "Ufalme wa mbinguni ni kama
punje ya haradali, ambayo mtu aliichukua, akaipanda
shambani mwake. 32 Ingawa mbegu hiyo ni ndogo
kuliko mbegu zote, lakini inapokua ni mmea mkubwa
kuliko yote ya bustanini, nao huwa mti mkubwa,
hadi ndege wa angani wanakuja na kutengeneza
viota katika matawi yake." 33 Akawaambia mfano
mwingine, "Ufalme wa mbinguni unafanana na chachu
ambayo mwanamke aliichukua akaichanganya katika
kiasi kikubwa cha unga hadi wote ukaumuka." 34
Isa alinena mambo haya yote kwa umati wa watu
kwa mifano, wala hakuwaambia lolote pasipo mfano.
35 Hii ilikuwa ili kutimiza neno lililonenwa na nabii,
aliposema: "Nitafungua kinywa changu niseme nao
kwa mifano; nitahubiri mambo yaliyofichika tangu
kuumbwa kwa misingi ya ulimwengu." 36 Kisha
Isa akaagana na ule umati, akaingia nyumbani.
Wanafunzi wake wakamjia wakamwambia, "Tueleze
maana ya ule mfano wa magugu shambani." 37
Akawaambia, "Aliyepanda mbegu nzuri ni Mwana
wa Adamu. 38 Shamba ni ulimwengu na mbegu
nzuri ni wana wa ufalme. Magugu ni wana wa yule
mwovu. 39 Yule adui aliyepanda magugu ni ibilisi.
Mavuno ni mwisho wa dunia, nao wavunaji ni malaika.
(aiōn g165) 40 "Kama vile magugu yang'olewavyo na
kuchomwa motoni, ndivyo itakavyokuwa wakati wa
mwisho wa dunia. (aiōn g165) 41 Mwana wa Adamu
atawatuma malaika wake, nao watakusanya kutoka
ufalme wake kila kitu kinachosababisha dhambi na
watenda maovu wote. 42 Nao watawatupa katika
tanuru la moto ambako kutakuwa na kilio na kusaga
meno. 43 Ndipo wenye haki watang'aa kama jua
katika ufalme wa Baba yao. Yeye aliye na masikio,
na asikie. 44 "Ufalme wa mbinguni unafanana na
hazina iliyofichwa shambani, ambayo mtu mmoja
alipoiona akaificha tena. Kisha katika furaha yake,
akaenda akauza vyote alivyokuwa navyo, akalinunua
lile shamba. 45 "Tena, ufalme wa mbinguni unafanana
na mfanyabiashara aliyekuwa akitafuta lulu safi. 46
Alipoipata lulu moja ya thamani kubwa, alienda akauza
vyote alivyokuwa navyo akainunua. 47 "Tena, ufalme
wa mbinguni ni kama wavu wa kuvua samaki uliotupwa
baharini ukavua samaki wa kila aina. 48 Ulipojaa,
wavuvi wakauvuta ufuoni, wakaketi na kukusanya
samaki wazuri kuwaweka kwenye vyombo safi, lakini
wale samaki wabaya wakawatupa. 49 Hivi ndivyo
itakavyokuwa wakati wa mwisho wa dunia. Malaika
watakuja na kuwatenganisha watu waovu na watu
wenye haki. (aiōn g165) 50 Nao watawatupa hao waovu
katika tanuru la moto ambako kutakuwa na kilio na
kusaga meno." 51 Isa akauliza, "Je, mmeyaelewa haya
yote?" Wakamjibu, "Ndiyo." 52 Akawaambia, "Basi kila
mwalimu wa Torati aliyefundishwa elimu ya ufalme
wa mbinguni ni kama mwenye nyumba anayetoa
kutoka ghala yake mali mpya na mali ya zamani."
53 Isa alipomaliza kutoa mifano hii, akaondoka. 54
Alipofika mji wa kwao, akawafundisha watu katika
sinagogi lao. Nao wakastaajabu, wakauliza, "Mtu huyu
amepata wapi hekima hii na uwezo huu wa kufanya
miujiza? 55 Huyu si yule mwana wa seremala? Mama
yake si yeye aitwaye Mariamu, nao ndugu zake si
Yakobo, Yusufu, Simoni na Yuda? 56 Nao dada zake
wote, hawako hapa pamoja nasi? Mtu huyu amepata
wapi basi mambo haya yote?" 57 Wakachukizwa
naye. Lakini Isa akawaambia, "Nabii hakosi heshima,
isipokuwa katika nchi yake na nyumbani mwake." 58

Naye hakufanya miujiza mingi huko kwa sababu ya
kutokuamini kwao.

14 Wakati huo, Mfalme Herode, mtawala wa
Galilaya, alisikia habari za Isa, 2 akawaambia
watumishi wake, “Huyu ni Yahya; amefufuka kutoka
kwa wafu! Hii ndiyo sababu nguvu za kutenda
miujiza zinafanya kazi ndani yake.” 3 Herode
alikuwa amemkamata Yahya, akamfunga na kumweka
gerezani kwa sababu ya Herodia, mke wa Filipo,
ndugu yake, 4 kwa kuwa Yahya alikuwa amemwambia
Herode: “Si halali kwako kuwa na huyo mwanamke.”
5 Herode alitaka sana kumuua Yahya, lakini akaogopa
watu, kwa maana walimtambua kuwa ni nabii. 6 Katika
siku ya kuadhimisha sikukuu ya kuzaliwa kwa Herode,
binti Herodia alicheza mbele ya watu waliohudhuria.
Alimfurahisha Herode sana, 7 kiasi kwamba aliahidi
kwa kiapo kumpa huyo binti chochote angeomba.
8 Huyo binti, akiwa amechochewa na mama yake,
akasema, “Nipe kichwa cha Yahya kwenye sinia.”
9 Mfalme alisikitika, lakini kwa sababu ya viapo
alivyoapa mbele ya wageni, akaamuru kwamba
apatiwe ombi lake. 10 Hivyo akaagiza Yahya akatwe
kichwa mle gerezani. 11 Kichwa chake kikaletwa
kwenye sinia, akapewa yule binti, naye akampelekea
mama yake. 12 Wanafunzi wa Yahya wakaja na
kuuchukua mwili wake, wakamzika. Kisha wakaenda
wakamwambia Isa. 13 Isa aliposikia yaliyokuwa
yametukia, aliondoka kwa chombo akaenda mahali
pasipo na watu ili awe peke yake. Lakini watu
walipopata habari, wakamfuata kwa miguu kupitia
nchi kavu kutoka miji. 14 Isa alipofika kando ya bahari,
aliona makundi makubwa ya watu, akawahurumia
na akawaponya wagonjwa wao. 15 Ilipofika jioni,
wanafunzi wake walienda kwake, wakamwambia,
“Mahali hapa ni nyikani, na muda sasa umekwisha.
Waage makundi ya watu ili waende zao vijijini
wakajinunulie chakula.” 16 Isa akawaambia, “Hakuna
sababu ya wao kuondoka. Ninyi wapeni chakula.” 17
Wakamjibu, “Tuna mikate mitano na samaki wawili
tu.” 18 Akawaambia, “Nileteeni hivyo vitu hapa.” 19 Isa
akaagiza umati wa watu wakae chini kwenye nyasi.
Akaichukua ile mikate mitano na wale samaki wawili,
akainua macho yake akatazama mbinguni, akavibariki
na kuimega ile mikate. Kisha akawapa wanafunzi, nao
wanafunzi wakawagawia ule umati. 20 Wote wakala,
wakashiba. Nao wanafunzi wakakusanya vipande
vilivyosalia, wakajaza vikapu kumi na viwili. 21 Idadi
ya watu waliokula walikuwa wanaume wapatao elfu
tano, bila kuhesabu wanawake na watoto. 22 Mara Isa
akawaambia wanafunzi wake waingie katika mashua
wamtangulie kwenda ng’ambo ya bahari, wakati yeye
alikuwa akiaga ule umati. 23 Baada ya kuwaaga,
akaenda zake mlimani peke yake kuomba. Jioni
ilipofika, Isa alikuwa huko peke yake. 24 Wakati huo ile
mashua ilikuwa mbali kutoka nchi kavu ikisukwasukwa
na mawimbi, kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho.
25 Wakati wa zamu ya nne ya usiku, Isa akawaendea
wanafunzi wake akiwa anatembea juu ya maji. 26
Wanafunzi wake walipomwona akitembea juu ya
maji, waliingiwa na hofu kuu, wakasema, “Ni mzimu.”
Wakapiga yowe kwa kuogopa. 27 Lakini mara Isa
akasema nao, akawaambia, “Jipeni moyo! Ni mimi.
Msiogope.” 28 Petro akamjibu, “Bwana Isa, ikiwa ni
wewe, niambie nije kwako nikitembea juu ya maji.” 29
Isa akamwambia, “Njoo.” Basi Petro akatoka kwenye
chombo, akatembea juu ya maji kumwelekea Isa. 30
Lakini alipoona upepo mkali aliingiwa na hofu, naye
akaanza kuzama, akapaza sauti na kusema, “Bwana,
niokoe!” 31 Mara Isa akaunyoosha mkono wake
na kumshika, akamwambia, “Wewe mwenye imani
haba, kwa nini uliona shaka?” 32 Nao walipoingia
ndani ya mashua, upepo ukakoma. 33 Ndipo wote
waliokuwa ndani ya ile mashua wakamwabudu Isa,
wakisema, “Hakika, wewe ndiwe Mwana wa Mungu.”
34 Walipokwisha kuvuka, wakafika nchi ya Genesareti.
35 Watu wa eneo lile walipomtambua Isa, walipeleka
habari sehemu zote za jirani. Watu wakamletea
wagonjwa wao wote, 36 wakamsihi awaruhusu
wagonjwa waguse tu pindo la vazi lake, nao wote
waliomgusa, wakaponywa.

15 Ndipo baadhi ya Mafarisayo na walimu wa Torati
wakamjia Isa kutoka Yerusalemu na kumuuliza,
2 “Mbona wanafunzi wako wanakiuka mapokeo ya
wazee? Kwa maana wao hawanawi mikono yao kabla
ya kula!” 3 Isa akawajibu, “Mbona ninyi mnavunja amri
ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu? 4 Kwa maana
Mungu alisema, ‘Waheshimu baba yako na mama
yako,’ na, ‘Yeyote amtukanaye baba yake au mama
yake, na auawe.’ 5 Lakini ninyi mwafundisha kwamba
mtu akimwambia baba yake au mama yake, ‘Kile
ambacho ningeweza kukusaidia kimewekwa wakfu
kwa Mungu,’ 6 basi hana tena sababu ya kumheshimu

baba yake nacho. Basi kwa ajili ya mafundisho yenu
mnavunja amri ya Mungu. 7 Ninyi wanafiki! Isaya
alikuwa sawa alipotabiri juu yenu kwamba: 8 "'Watu
hawa huniheshimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao
iko mbali nami. 9 Huniabudu bure; nayo mafundisho
yao ni maagizo ya wanadamu tu.'" 10 Isa akaita umati
wa watu waliokuwa hapo, akawaambia, "Sikilizeni
na mwelewe: 11 kinachomfanya mtu kuwa najisi
mbele za Mungu si kile kiingiacho kinywani mwake,
bali ni kile kitokacho kinywani mwake." 12 Kisha
wanafunzi wake wakamjia na kumuuliza, "Je, unajua
kwamba Mafarisayo walichukizwa sana waliposikia
yale uliyosema?" 13 Akawajibu, "Kila mmea ambao
Baba yangu wa mbinguni hakuupanda utang'olewa.
14 Waacheni; wao ni viongozi vipofu, wanaoongoza
vipofu. Kama kipofu akimwongoza kipofu mwenzake,
wote wawili watatumbukia shimoni." 15 Petro akasema,
"Tueleze maana ya huu mfano." 16 Isa akawauliza, "Je,
bado ninyi hamfahamu? 17 Je, hamwelewi kwamba
chochote kiingiacho kinywani huenda tumboni, na
hatimaye hutolewa nje kikiwa uchafu? 18 Lakini
kitokacho kinywani hutoka moyoni, na hiki ndicho
kimtiacho mtu unajisi. 19 Kwa maana ndani ya moyo
hutoka mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati,
wizi, ushahidi wa uongo na masingizio. 20 Haya ndio
yamtiayo mtu unajisi; lakini kula bila kunawa mikono
hakumtii mtu unajisi." 21 Isa aliondoka mahali pale,
akaenda sehemu za Tiro na Sidoni. 22 Mwanamke
mmoja Mkanaani aliyeishi sehemu jirani na hizo
akaja kwake akilia, akasema, "Nihurumie, Ee Bwana,
Mwana wa Daudi! Binti yangu amepagawa na pepo
mchafu, na anateseka sana." 23 Lakini Isa hakumjibu
neno. Hivyo wanafunzi wake wakamwendea na
kumsihi sana, wakisema, "Mwambie aende zake,
kwa maana anaendelea kutupigia kelele." 24 Isa
akajibu, "Nimetumwa tu kwa ajili ya kondoo wa Israeli
waliopotea." 25 Lakini yule mwanamke akaja, akapiga
magoti mbele ya Isa, akasema, "Bwana, nisaidie!" 26
Isa akajibu, "Si haki kuchukua chakula cha watoto
na kuwatupia mbwa." 27 Yule mwanamke akajibu,
"Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo
yanayoanguka kutoka kwa meza za bwana zao." 28
Ndipo Isa akamwambia, "Mwanamke, imani yako
ni kubwa! Iwe kwako kama unavyotaka." Naye binti
yake akapona tangu saa ile. 29 Isa akaondoka na
kwenda kando ya Bahari ya Galilaya. Kisha akapanda
mlimani, akaketi huko. 30 Umati mkubwa wa watu
wakamjia, wakiwaleta vilema, vipofu, viwete, bubu na
wengine wengi, wakawaweka miguuni pake; naye
akawaponya. 31 Hao watu wakashangaa walipoona
bubu wakisema, vilema wakipona, viwete wakitembea
na vipofu wakiona, wakamtukuza Mungu wa Israeli.
32 Kisha Isa akawaita wanafunzi wake, akawaambia,
"Ninahurumia umati huu wa watu, kwa sababu
sasa wamekuwa pamoja nami kwa muda wa siku
tatu, na hawana chakula chochote. Nami sipendi
kuwaaga watu wakiwa na njaa, wasije wakazimia
njiani." 33 Wanafunzi wake wakasema, "Tutapata
wapi mikate ya kutosha kulisha umati mkubwa namna
hii, nasi tuko nyikani?" 34 Isa akawauliza, "Mnayo
mikate mingapi?" Wakamjibu, "Tunayo mikate saba
na visamaki vichache." 35 Isa akaagiza watu wote
waketi chini. 36 Kisha akachukua ile mikate saba na
wale samaki, naye akamshukuru Mungu, akavimega
na kuwapa wanafunzi wake, nao wakawapa watu.
37 Wote wakala na kushiba. Baadaye wanafunzi
wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu
saba. 38 Idadi ya watu walikuwa wanaume elfu nne,
bila kuhesabu wanawake na watoto. 39 Baada ya
kuaga umati wa watu, Isa aliingia katika mashua,
akaenda sehemu za Magadani.

16 Mafarisayo na Masadukayo wakamjia Isa na
kumjaribu kwa kumwomba awaoneshe ishara
kutoka mbinguni. 2 Isa akawajibu, "Ifikapo jioni,
mnasema, 'Hali ya hewa itakuwa nzuri, kwa kuwa
anga ni nyekundu.' 3 Nanyi wakati wa asubuhi
mnasema, 'Leo kutakuwa na dhoruba, kwa sababu
anga ni nyekundu na mawingu yametanda.' Mnajua
jinsi ya kupambanua kule kuonekana kwa anga,
lakini hamwezi kupambanua ishara za nyakati. 4
Kizazi kiovu na cha uzinzi kinatafuta ishara, lakini
hakitapewa ishara yoyote isipokuwa ishara ya Yona."
Isa akawaacha, akaenda zake. 5 Wanafunzi wake
walipofika ng'ambo ya bahari, walikuwa wamesahau
kuchukua mikate. 6 Isa akawaambia, "Jihadharini.
Jilindeni na chachu ya Mafarisayo na ya Masadukayo."
7 Wakajadiliana wao kwa wao, wakisema, "Ni
kwa sababu hatukuleta mikate." 8 Isa, akifahamu
majadiliano yao, akauliza, "Enyi wa imani haba! Mbona
mnajadiliana miongoni mwenu kuhusu kutokuwa na
mikate? 9 Je, bado hamwelewi? Je, hamkumbuki
ile mikate mitano kwa watu elfu tano, na idadi ya

vikapu vilivyojaa mabaki mlivyokusanya? **10** Au ile
mikate saba kwa watu elfu nne na idadi ya vikapu
vilivyojaa mabaki mlivyokusanya? **11** Inakuwaje
mnashindwa kuelewa kwamba nilikuwa sisemi nanyi
habari za mikate? Jilindeni na chachu ya Mafarisayo
na Masadukayo." **12** Ndipo wakaelewa kwamba
alikuwa hasemi kuhusu chachu ya kutengeneza
mikate, bali kuhusu mafundisho ya Mafarisayo na
Masadukayo. **13** Basi Isa alipofika katika eneo la
Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake, "Watu
husema kwamba mimi Mwana wa Adamu ni nani?"
**14** Wakamjibu, "Baadhi husema ni Yahya; wengine
husema ni Ilya; na bado wengine husema ni Yeremia
au mmoja wa manabii." **15** Akawauliza, "Je, ninyi
mnasema mimi ni nani?" **16** Simoni Petro akamjibu,
"Wewe ndiwe Al-Masihi, Mwana wa Mungu aliye
hai." **17** Naye Isa akamwambia, "Heri wewe, Simoni
Bar-Yona, kwa maana hili halikufunuliwa kwako na
mwanadamu, bali na Baba yangu aliye mbinguni.
**18** Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro na juu ya
mwamba huu nitajenga jumuiya ya wafuasi wangu,
hata malango ya Kuzimu hayataweza kuwashinda.
**(Hadēs g86)** **19** Nitakupa funguo za ufalme wa mbinguni,
na lolote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa
Mbinguni, nalo lolote utakalofungua duniani litakuwa
limefunguliwa mbinguni." **20** Kisha akawakataza
wanafunzi wake wasimwambie mtu yeyote kwamba
yeye ndiye Al-Masihi. **21** Tangu wakati huo, Isa
alianza kuwaeleza wanafunzi wake kwamba hana
budi kwenda Yerusalemu na kupata mateso mengi
mikononi mwa wazee, viongozi wa makuhani, na
walimu wa Torati, na kwamba itampasa auawe,
lakini siku ya tatu kufufuliwa. **22** Petro akamchukua
kando, akaanza kumkemea, akisema, "Haiwezekani,
Bwana! Jambo hili kamwe halitakupata!" **23** Lakini Isa
akageuka na kumwambia Petro, "Rudi nyuma yangu,
Shetani! Wewe ni kikwazo kwangu. Moyo wako
hauwazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu." **24** Ndipo
Isa akawaambia wanafunzi wake, "Mtu yeyote akitaka
kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe, auchukue
msalaba wake, anifuate. **25** Kwa maana yeyote
anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini
yeyote atakayeyapoteza maisha yake kwa ajili yangu
atayapata. **26** Kwa maana itamfaidi mtu nini kuupata
ulimwengu wote, lakini akayapoteza maisha yake?
Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? **27** Kwa
maana Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa
Baba yake pamoja na malaika wake, naye ndipo
atakapomlipa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.
**28** Nawaambia kweli, baadhi yenu hapa hawataonja
mauti kabla ya kumwona Mwana wa Adamu akija
katika ufalme wake."

**17** Siku sita baada ya jambo hili, Isa akawachukua
Petro, Yakobo na Yohana ndugu yake Yakobo,
akawapeleka juu ya mlima mrefu peke yao. **2** Wakiwa
huko, Isa alibadilika sura mbele yao. Uso wake
ukang'aa kama jua na nguo zake zikawa nyeupe kama
nuru. **3** Ghafula wakawatokea mbele yao Musa na Ilya,
wakizungumza na Isa. **4** Ndipo Petro akamwambia Isa,
"Bwana, ni vyema sisi tukae hapa. Ukitaka, nitafanya
vibanda vitatu: kimoja chako, kingine cha Musa na
kingine cha Ilya." **5** Petro alipokuwa angali ananena,
ghafula wingu lililong'aa likawafunika, na sauti ikatoka
kwenye hilo wingu ikisema, "Huyu ni Mwanangu
mpendwa. Ninapendezwa naye sana. Msikieni
yeye." **6** Wanafunzi waliposikia haya, wakaanguka
kifudifudi, wakajawa na hofu. **7** Lakini Isa akaja na
kuwagusa, akawaambia, "Inukeni na wala msiogope."
**8** Walipoinua macho yao, hawakumwona mtu mwingine
yeyote isipokuwa Isa. **9** Walipokuwa wakishuka kutoka
mlimani, Isa akawaagiza, "Msimwambie mtu yeyote
mambo mliyoyaona hapa, hadi Mwana wa Adamu
atakapofufuliwa kutoka kwa wafu." **10** Wale wanafunzi
wakamuuliza, "Kwa nini basi walimu wa Torati husema
kwamba ni lazima Ilya aje kwanza?" **11** Isa akawajibu,
"Ni kweli, Ilya lazima aje kwanza, naye atatengeneza
mambo yote. **12** Lakini nawaambia, Ilya amekwisha
kuja, nao hawakumtambua, bali walimtendea kila
kitu walichotaka. Vivyo hivyo Mwana wa Adamu pia
atateswa mikononi mwao." **13** Ndipo wale wanafunzi
wakaelewa kuwa alikuwa anazungumza nao habari za
Yahya. **14** Walipofika penye umati wa watu, mtu mmoja
akamjia Isa na kupiga magoti mbele yake, akasema,
**15** "Bwana, mhurumie mwanangu. Yeye ana kifafa na
anateseka sana. Mara kwa mara huanguka kwenye
moto au kwenye maji. **16** Nilimleta kwa wanafunzi
wako, lakini hawakuweza kumponya." **17** Isa akajibu,
"Enyi kizazi kisichoamini na kilichopotoka! Nitakaa
nanyi hadi lini? Nitawavumilia hadi lini? Mleteni
mvulana hapa kwangu." **18** Isa akamkemea yule
pepo mchafu, akamtoka yule kijana, naye akapona
tangu saa hiyo. **19** Kisha wanafunzi wakamwendea

Isa wakiwa peke yao, wakamuuliza, “Kwa nini sisi
hatukuweza kumtoa?” 20 Akawajibu, “Kwa sababu
ya imani yenu ndogo. Ninawaambia kweli, mkiwa
na imani ndogo kama punje ya haradali, mtauambia
mlima huu, ‘Ondoka hapa uende pale,’ nao utaondoka.
Wala hakutakuwa na jambo lisilowezekana kwenu.
[ 21 Lakini hali kama hii haitoki ila kwa kuomba
na kufunga.]” 22 Siku moja walipokuwa pamoja
huko Galilaya, Isa akawaambia, “Mwana wa Adamu
atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu. 23 Nao
watamuua, lakini siku ya tatu atafufuliwa.” Wanafunzi
wakahuzunika sana. 24 Baada ya Isa na wanafunzi
wake kufika Kapernaumu, wakusanya kodi ya Hekalu
wakamjia Petro na kumuuliza, “Je, Mwalimu wenu
halipi kodi ya Hekalu?” 25 Petro akajibu, “Ndiyo,
yeye hulipa.” Petro aliporudi nyumbani, Isa akawa
wa kwanza kulizungumzia, akamuuliza, “Unaonaje
Simoni? Wafalme wa dunia hupokea ushuru na kodi
kutoka kwa nani? Je, ni kutoka kwa watoto wao
au kutoka kwa watu wengine?” 26 Petro akamjibu,
“Kutoka kwa watu wengine.” Isa akamwambia, “Kwa
hiyo watoto wao wamesamehewa. 27 Lakini ili
tusije tukawaudhi, nenda baharini ukatupe ndoana.
Mchukue samaki wa kwanza utakayemvua. Fungua
kinywa chake nawe utakuta humo fedha, ichukue
ukalipe kodi yako na yangu.”

**18** Wakati huo, wanafunzi wakamjia Isa na
kumuuliza, “Je, nani aliye mkuu kuliko wote
katika ufalme wa mbinguni?” 2 Isa akamwita mtoto
mdogo na kumsimamisha katikati yao. 3 Naye
akasema: “Amin, nawaambia, msipoongoka na kuwa
kama watoto wadogo, kamwe hamtaingia katika
ufalme wa mbinguni. 4 Kwa hiyo mtu yeyote
anyenyekeaye kama huyu mtoto, ndiye aliye mkuu
kuliko wote katika ufalme wa mbinguni. 5 “Yeyote
amkaribishaye mtoto mdogo kama huyu kwa Jina
langu, anikaribisha mimi. 6 “Lakini kama mtu
yeyote akimsababisha mmoja wa hawa wadogo
wanaoniamini kutenda dhambi, ingekuwa bora kwake
afungiwe jiwe kubwa la kusagia shingoni mwake,
na kutoswa katika kilindi cha bahari. 7 “Ole kwa
ulimwengu kwa sababu ya mambo yanayosababisha
watu kutenda dhambi! Mambo hayo lazima yawepo,
lakini ole wake mtu yule ambaye huyasababisha. 8
Ikiwa mkono wako au mguu wako unakusababisha
utende dhambi, ukate na uutupe mbali. Ni afadhali
kwako kuingia katika uzima ukiwa huna mkono
mmoja au mguu mmoja, kuliko kuwa na mikono
miwili au miguu miwili, na kutupwa katika moto wa
milele. (aiōnios g166) 9 Nalo jicho lako likikusababisha
kutenda dhambi, ling’oe, ulitupe mbali. Ni afadhali
kwako kuingia katika uzima ukiwa na jicho moja,
kuliko kuwa na macho mawili lakini ukatupwa katika
moto wa Jehanamu. (Geenna g1067) 10 “Chungeni ili
msimdharau mmoja wa hawa wadogo. Kwa maana
nawaambia, malaika wao mbinguni daima wanauona
uso wa Baba yangu aliye mbinguni. [ 11 Kwa maana
Mwana wa Adamu alikuja kuokoa kile kilichopotea.]
12 “Mwaonaje? Ikiwa mtu ana kondoo mia moja, na
mmoja wao akapotea, je, hatawaacha wale tisini
na tisa vilimani na kwenda kumtafuta huyo mmoja
aliyepotea? 13 Naye akishampata, amin, nawaambia,
hufurahi zaidi kwa ajili ya huyo kondoo mmoja
kuliko wale tisini na tisa ambao hawakupotea. 14
Vivyo hivyo, Baba yenu wa mbinguni hapendi hata
mmoja wa hawa wadogo apotee. 15 “Ndugu yako
akikukosea, nenda ukamwoneshe kosa lake, kati
yenu ninyi wawili peke yenu. Akikusikiliza, utakuwa
umempata tena ndugu yako. 16 Lakini asipokusikiliza,
nenda na mtu mwingine mmoja au wawili ili kila neno
‘lithibitishwe kwa ushahidi wa mashahidi wawili au
watatu’. 17 Akikataa kuwasikiliza hao, waambieni
kundi lenu la waumini. Naye akikataa hata kuwasikiliza
kundi la waumini, basi awe kwenu kama mtu
asiyeamini au mtoza ushuru. 18 “Amin, nawaambia,
lolote mtakalolifunga duniani litakuwa limefungwa
mbinguni, na lolote mtakalolifungua duniani litakuwa
limefunguliwa mbinguni. 19 “Tena nawaambia, ikiwa
wawili wenu watakubaliana duniani kuhusu jambo
lolote watakaloomba, watatendewa na Baba yangu
aliye mbinguni. 20 Kwa kuwa wanapokusanyika
pamoja watu wawili au watatu kwa Jina langu,
mimi niko papo hapo pamoja nao.” 21 Kisha Petro
akamwendea Isa na kumuuliza, “Bwana, ni mara
ngapi nimsamehe ndugu yangu akinikosea? Hadi
mara saba?” 22 Isa akamjibu, “Sikuambii hata mara
saba, bali hata saba mara sabini. 23 “Kwa hiyo ufalme
wa mbinguni unaweza kufananishwa na mfalme
aliyetaka kufanya hesabu zake za fedha na watumishi
wake. 24 Alipoanza kufanya hesabu zake, mtu mmoja
aliyekuwa anadaiwa talanta elfu kumi aliletwa kwake.
25 Kwa kuwa alikuwa hawezi kulipa deni hilo, bwana

wake akaamuru kwamba auzwe, yeye, mkewe,
watoto wake na vyote alivyokuwa navyo, ili lile deni
lipate kulipwa. **26** “Yule mtumishi akampigia magoti,
akamsihi yule bwana akisema, ‘Naomba univumilie,
nami nitakulipa deni lako lote.’ **27** Yule bwana wa huyo
mtumishi akamwonea huruma, akafuta deni lake lote,
akamwacha aende zake. **28** “Lakini yule mtumishi
alipokuwa anatoka nje, akakutana na mtumishi
mwenzake aliyekuwa amemkopesha dinari mia moja.
Akamkamata, akamkaba koo akimwambia, ‘Nilipe kile
ninachokudai!’ **29** “Yule mtumishi mwenzake akapiga
magoti akamsihi akisema, ‘Naomba univumilie, nami
nitakulipa deni lako lote.’ **30** “Lakini akakataa.
Badala yake, alienda akamtupa gerezani hata
atakapolipa hilo deni. **31** Watumishi wenzake
walipoona haya yaliyotukia wakaudhika sana, nao
wakaenda na kumwambia bwana wao kila kitu
kilichokuwa kimetukia. **32** “Yule bwana akamwita yule
mtumishi akamwambia, ‘Wewe mtumishi mwovu!
Mimi nilikusamehe deni lako lote uliponisihi. **33** Je,
haikukupasa kumhurumia mtumishi mwenzako kama
mimi nilivyokuhurumia wewe?’ **34** Kwa hasira, yule
bwana wake akamtia yule mtumishi mikononi mwa
askari wa gereza ili ateswe hadi atakapolipa yote
aliyokuwa anadaiwa. **35** “Hivi ndivyo Baba yangu wa
mbinguni atakavyomfanyia kila mmoja wenu ikiwa
hatamsamehe ndugu yake kutoka moyoni mwake.”

**19** Isa alipomaliza kusema maneno haya, aliondoka
Galilaya, akaenda sehemu za Yudea, ng’ambo
ya Yordani. **2** Umati mkubwa wa watu wakamfuata,
naye akawaponya huko. **3** Baadhi ya Mafarisayo
wakamjia ili kumjaribu, wakamuuliza, “Ni halali mtu
kumwacha mke wake kwa sababu yoyote?” **4**
Akawajibu, “Je, hamkusoma kwamba hapo mwanzo
Muumba aliwaumba mwanaume na mwanamke,
**5** naye akasema, ‘Kwa sababu hii mwanaume
atamwacha baba yake na mama yake, naye
ataambatana na mkewe, na hao wawili watakuwa
mwili mmoja’? **6** Hivyo si wawili tena, bali mwili mmoja.
Kwa hiyo alichokiunganisha Mungu, mwanadamu
asikitenganishe.” **7** Wakamuuliza, “Kwa nini basi
Musa aliagiza mtu kumpa mkewe hati ya talaka na
kumwacha?” **8** Isa akawajibu, “Musa aliwaruhusu
kuwaacha wake zenu kwa sababu ya ugumu wa mioyo
yenu. Lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo. **9** Mimi
nawaambia, yeyote amwachaye mkewe isipokuwa
kwa sababu ya uasherati naye akaoa mke mwingine,
anazini. Naye amwoaye yule mwanamke aliyeachwa
pia anazini.” **10** Wanafunzi wake wakamwambia,
“Kama hali ndiyo hii kati ya mume na mke, ni afadhali
mtu asioe!” **11** Isa akawaambia, “Si watu wote
wanaoweza kupokea neno hili, isipokuwa wale tu
waliojaliwa na Mungu. **12** Kwa maana wengine ni
matowashi kwa sababu wamezaliwa hivyo; wengine
wamefanywa matowashi na wanadamu; na wengine
wamejifanya matowashi kwa ajili ya ufalme wa
mbinguni. Yeye awezaye kulipokea neno hili na
alipokee.” **13** Kisha watoto wadogo wakaletwa kwa Isa
ili aweke mikono yake juu yao na awaombee. Lakini
wanafunzi wake wakawakemea wale waliowaleta.
**14** Isa akasema, “Waacheni watoto wadogo waje
kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme wa
mbinguni ni wa wale walio kama hawa.” **15** Naye
akaweka mikono yake juu yao, na akaondoka huko.
**16** Mtu mmoja akamjia Isa na kumuuliza, “Mwalimu
mwema, nifanye jambo gani jema ili nipate uzima
wa milele?” **(aiōnios g166)** **17** Isa akamjibu, “Mbona
unaniuliza habari ya mema? Aliye mwema ni Mmoja
tu. Lakini ukitaka kuingia uzimani, zitii amri.” **18** Yule
mtu akamuuliza, “Amri zipi?” Isa akamjibu, “Usiue,
usizini, usiibe, usishuhudie uongo, **19** waheshimu
baba yako na mama yako, na umpende jirani yako
kama nafsi yako.” **20** Yule kijana akasema, “Hizi zote
nimezishika. Je, bado nimepungukiwa na nini?” **21**
Isa akamwambia, “Ukitaka kuwa mkamilifu, nenda,
ukauze vitu vyote ulivyo navyo, na hizo fedha uwape
maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni. Kisha
njoo, unifuate.” **22** Yule kijana aliposikia hayo, akaenda
zake kwa huzuni, kwa sababu alikuwa na mali nyingi.
**23** Ndipo Isa akawaambia wanafunzi wake, “Amin,
nawaambia, itakuwa vigumu kwa mtu tajiri kuingia
katika ufalme wa mbinguni. **24** Tena nawaambia,
ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu
la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika ufalme
wa Mungu.” **25** Wanafunzi wake waliposikia haya,
walishangaa sana na kuuliza, “Ni nani basi awezaye
kuokoka?” **26** Lakini Isa akawatazama, akawaambia,
“Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini
mambo yote yanawezekana kwa Mungu.” **27** Ndipo
Petro akamjibu, “Tazama, sisi tumeacha kila kitu na
kukufuata! Tutapata nini basi?” **28** Isa akawaambia,
“Amin, nawaambia, wakati wa kufanywa upya vitu

vyote, Mwana wa Adamu atakapoketi kwenye kiti
chake kitukufu cha enzi, ninyi mlionifuata pia mtaketi
katika viti kumi na viwili vya utawala, mkiyahukumu
makabila kumi na mawili ya Israeli. **29** Kila mtu
aliyeacha nyumba, au ndugu zake wa kiume au wa
kike, baba au mama, watoto au mashamba kwa
ajili yangu, atapokea mara mia zaidi ya hayo, na
atarithi uzima wa milele. **(aiōnios g166)** **30** Lakini wengi
walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na walio wa
mwisho watakuwa wa kwanza.

**20** “Kwa maana ufalme wa mbinguni unafanana na
mtu mwenye shamba aliyetoka alfajiri kwenda
kuajiri vibarua kufanya kazi katika shamba lake la
mizabibu. **2** Baada ya kukubaliana na hao vibarua
kuwalipa ujira wa dinari moja kwa siku, akawapeleka
kwenye shamba lake la mizabibu. **3** “Mnamo saa
tatu akatoka tena, akawakuta wengine wamesimama
sokoni bila kazi. **4** Akawaambia, ‘Ninyi nanyi nendeni
mkafanye kazi katika shamba langu la mizabibu, nami
nitawalipa chochote kilicho haki yenu.’ **5** Hivyo basi
wakaenda. “Akatoka tena mnamo saa sita na pia saa
tisa akafanya vivyo hivyo. **6** Mnamo saa kumi na moja
akatoka tena akawakuta wengine bado wamesimama
bila kazi. Akawauliza, ‘Kwa nini mmesimama hapa
kutwa nzima pasipo kufanya kazi?’ **7** “Wakamjibu, ‘Ni
kwa sababu hakuna yeyote aliyetuajiri.’ “Akawaambia,
‘Ninyi nanyi nendeni mkafanye kazi katika shamba
langu la mizabibu.’ **8** “Ilipofika jioni, yule mwenye
shamba la mizabibu akamwambia msimamizi, ‘Waite
hao vibarua na uwalipe ujira wao, ukianzia na wale
walioajiriwa mwisho na kuishia na wale walioajiriwa
kwanza.’ **9** “Wale vibarua walioajiriwa saa kumi na
moja wakaja, na kila mmoja wao akapokea dinari moja.
**10** Hivyo wale walioajiriwa kwanza walipofika, walidhani
watalipwa zaidi. Lakini kila mmoja wao pia alipokea
dinari moja. **11** Walipoipokea, wakaanza kulalamika
dhidi ya yule mwenye shamba, **12** wakisema, ‘Hawa
watu walioajiriwa mwisho wamefanya kazi kwa muda
wa saa moja tu, nawe umewafanya sawa na sisi
ambao tumestahimili taabu na joto lote la mchana
kutwa?’ **13** “Yule mwenye shamba akamjibu mmoja
wao, ‘Rafiki, sijakudhulumu. Je, hukukubaliana nami
kwa ujira wa kawaida wa dinari moja? **14** Chukua
ujira wako na uende. Mimi nimeamua kumlipa huyu
mtu aliyeajiriwa mwisho kama nilivyokupa wewe. **15**
Je, sina haki ya kufanya kile nitakacho na mali yangu
mwenyewe? Au unaona wivu kwa kuwa nimekuwa
mkarimu?’ **16** “Vivyo hivyo, wa mwisho watakuwa wa
kwanza, na wa kwanza watakuwa wa mwisho.” **17** Basi
Isa alipokuwa anapanda kwenda Yerusalemu, aliwaita
kando wale wanafunzi kumi na wawili na kuwaambia,
**18** “Tunapanda kwenda Yerusalemu, na Mwana wa
Adamu atatiwa mikononi mwa viongozi wa makuhani
na walimu wa Torati. Nao watamhukumu kifo **19** na
kumtia mikononi mwa watu wa Mataifa ili wamdhihaki
na kumpiga mijeledi na kumsulubisha msalabani.
Naye atafufuliwa siku ya tatu!” **20** Kisha mama yao
wana wa Zebedayo akamjia Isa pamoja na wanawe,
naye akapiga magoti mbele yake, akamwomba Isa
amfanyie jambo fulani. **21** Isa akamuuliza, “Unataka
nini?” Akajibu, “Tafadhali, wajalie wanangu hawa ili
mmoja aketi upande wako wa kuume, na mwingine
upande wako wa kushoto katika ufalme wako.” **22**
Isa akawaambia, “Ninyi hamjui mnaloliomba. Je,
mnaweza kukinywea kikombe nitakachonywea mimi?”
Wakajibu, “Tunaweza.” **23** Isa akawaambia, “Kwa
kweli kikombe changu mtakinywea, lakini kuketi
upande wangu wa kuume au wa kushoto si langu mimi
kuwapa. Nafasi hizo ni za wale ambao wameandaliwa
na Baba yangu.” **24** Wale wanafunzi wengine kumi
waliposikia haya, waliwakasirikia hao ndugu wawili.
**25** Lakini Isa akawaita wote pamoja na kuwaambia,
“Mnafahamu kuwa watawala wa watu wa Mataifa
huwatawala kwa nguvu, nao wenye vyeo huonesha
mamlaka yao. **26** Isiwe hivyo kwenu. Badala yake,
yeyote anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu
hana budi kuwa mtumishi wenu, **27** naye anayetaka
kuwa wa kwanza miongoni mwenu hana budi kuwa
mtumwa wenu: **28** kama vile Mwana wa Adamu
hakuja kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake
uwe fidia kwa ajili ya wengi.” **29** Isa na wanafunzi
wake walipokuwa wakiondoka Yeriko, umati mkubwa
wa watu wakamfuata. **30** Vipofu wawili walikuwa
wameketi kando ya barabara. Waliposikia kwamba Isa
alikuwa anapita, wakapaza sauti wakisema, “Bwana
Isa, Mwana wa Daudi, tuhurumie!” **31** Umati wa watu
wakawakemea na kuwaambia wanyamaze, lakini
wao wakazidi kupaza sauti wakisema, “Bwana Isa,
Mwana wa Daudi, tuhurumie.” **32** Isa akasimama
na kuwaita, akawauliza, “Mnataka niwafanyie nini?”
**33** Wakamjibu, “Bwana, tunataka kuona.” **34** Isa

akawahurumia na kuwagusa macho yao. Mara macho
yao yakapata kuona, nao wakamfuata.

21 Walipokaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage
katika Mlima wa Mizeituni. Ndipo Isa akawatuma
wanafunzi wake wawili, 2 akawaambia, “Nendeni
katika kijiji kilicho mbele yenu, nanyi mtampata
punda amefungwa hapo, na mwana-punda pamoja
naye. Wafungueni na mniletee. 3 Mtu yeyote
akiwasemesha lolote, mwambieni kwamba Bwana
ana haja nao, naye atawaruhusu mwalete mara
moja.” 4 Haya yalitukia ili litimie neno lililonenwa
na nabii, aliposema: 5 “Mwambieni Binti Sayuni,
‘Tazama, mfalme wako anakuja kwako, ni mpole,
naye amepanda punda, juu ya mwana-punda, mtoto
wa punda.’” 6 Wale wanafunzi wakaenda, wakafanya
kama Isa alivyokuwa amewaagiza. 7 Wakamleta yule
punda na mwana-punda, nao wakatandika mavazi
yao juu ya hao punda, naye Isa akaketi juu yake. 8
Umati mkubwa wa watu wakatandaza mavazi yao
barabarani, na wengine wakakata matawi kwenye
miti, wakayatandaza barabarani. 9 Wale umati wa
watu waliomtangulia na wale waliomfuata wakapaza
sauti na kusema, “Hosana, Mwana wa Daudi!”
“Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la Mwenyezi
Mungu!” “Hosana juu mbinguni!” 10 Isa alipoingia
Yerusalemu, mji wote ukataharuki, watu wakauliza,
“Huyu ni nani?” 11 Wale umati wa watu wakajibu,
“Huyu ni Isa, yule nabii kutoka Nasiri ya Galilaya.” 12
Isa akaingia katika eneo la Hekalu na kuwafukuza
wote waliokuwa wakinunua na kuuza vitu Hekaluni.
Akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadilisha
fedha, na pia viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa.
13 Akawaambia, “Imeandikwa, ‘Nyumba yangu itaitwa
nyumba ya sala,’ lakini ninyi mmeifanya kuwa pango
la wanyang’anyi.” 14 Vipofu na vilema wakamwendea
kule Hekaluni, naye akawaponya. 15 Lakini viongozi
wa makuhani na walimu wa Torati walipoona mambo
ya ajabu aliyofanya, na kuwasikia watoto wakishangilia
katika eneo la Hekalu, wakisema, “Hosana Mwana wa
Daudi,” walikasirika. 16 Wakamuuliza Isa, “Je, unasikia
hayo hawa wanayosema?” Akawajibu, “Naam; kwani
hamkusoma, “‘Midomoni mwa watoto wachanga
na wanaonyonya umeamuru sifa’?” 17 Akawaacha,
akatoka nje ya mji, akaenda hadi Bethania, akalala
huko. 18 Asubuhi na mapema, Isa alipokuwa akirudi
mjini, alikuwa na njaa. 19 Akauona mtini kando
ya barabara, naye akaukaribia, lakini hakupata
tunda lolote ila majani. Ndipo akauambia, “Wewe
usizae matunda tena kamwe!” Papo hapo ule mtini
ukanyauka. (aiōn g165) 20 Wanafunzi wake walipoona
jambo hili, wakashangaa, wakamuuliza, “Imekuwaje
mtini huu kunyauka ghafula?” 21 Isa akawajibu, “Amin,
nawaambia, mkiwa na imani wala msiwe na shaka,
si kwamba mtaweza kufanya tu yale yaliyofanyika
kwa huu mtini, bali hata mkiuambia huu mlima,
‘Ng’oka, ukatupwe baharini,’ litafanyika. 22 Yoyote
mtakayoyaomba mkisali na mkiamini, mtayapokea.”
23 Isa alipoingia Hekaluni, viongozi wa makuhani na
wazee wa watu wakamjia alipokuwa anafundisha,
wakamuuliza, “Unafanya mambo haya kwa mamlaka
gani? Na ni nani aliyekupa mamlaka haya?” 24 Isa
akawajibu, “Nami nitawauliza swali moja. Mkinijibu,
nitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo
haya. 25 Je, ubatizo wa Yahya ulitoka wapi? Ulitoka
mbinguni au kwa wanadamu?” Wakahojiana wao
kwa wao na kusema, “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’
atatuuliza, ‘Mbona basi hamkumwamini?’ 26 Lakini
tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’ tunawaogopa
hawa watu, maana wote wanamtambua Yahya
kuwa ni nabii.” 27 Hivyo basi wakamjibu Isa, “Sisi
hatujui.” Naye akawaambia, “Wala mimi sitawaambia
ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya. 28
“Lakini mwaonaje? Mtu mmoja alikuwa na wana
wawili. Akamwendea yule wa kwanza akamwambia,
‘Mwanangu, nenda ukafanye kazi kwenye shamba
la mizabibu leo.’ 29 “Yule mwanawe akamjibu
‘Mimi sitaenda.’ Baadaye akabadili mawazo yake
akaenda. 30 “Kisha yule baba akamwendea yule
mwanawe mwingine, akamwambia vilevile. Yeye
akajibu, ‘Nitaenda, bwana,’ lakini hakuenda. 31 “Ni
yupi kati yao hao wawili aliyetimiza kile alichotaka
baba yake?” Wakamjibu, “Ni yule wa kwanza.”
Isa akawaambia, “Amin, amin nawaambia, watoza
ushuru na makahaba wanawatangulia kuingia katika
ufalme wa Mungu. 32 Kwa maana Yahya alikuja
kwenu kuwaonesha njia ya haki, lakini hamkumsadiki,
lakini watoza ushuru na makahaba wakamsadiki.
Nanyi hata mlipoona hayo, baadaye hamkutubu na
kumsadiki. 33 “Sikilizeni mfano mwingine: Kulikuwa
na mtu mmoja mwenye shamba ambaye alipanda
shamba la mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka,
akatengeneza shinikizo la kukamulia zabibu ndani

yake, na akajenga mnara wa ulinzi. Kisha akalikodisha
hilo shamba la mizabibu kwa wakulima fulani, naye
akaondoka, akasafiri hadi nchi nyingine. **34** Wakati
wa mavuno ulipokaribia, akawatuma watumishi wake
kwa hao wapangaji ili kukusanya matunda yake. **35**
"Wale wapangaji wakawakamata wale watumishi,
wakampiga mmoja, wakamuua mwingine, na yule
wa tatu wakampiga mawe. **36** Kisha akawatuma
watumishi wengine kwao, wengi kuliko wale wa
kwanza, nao wale wapangaji wakawatendea vilevile.
**37** Mwisho wa yote, akamtuma mwanawe kwao,
akisema, 'Watamheshimu mwanangu.' **38** "Lakini wale
wapangaji walipomwona mwanawe, wakasemezana
wao kwa wao, 'Huyu ndiye mrithi. Njooni tumuue,
ili tuchukue urithi wake.' **39** Hivyo wakamchukua,
wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamuua. **40**
"Basi huyo mwenye shamba la mizabibu atakapokuja,
atawafanyia nini hao wakulima?" **41** Wakamjibu, "Kwa
hasira kuu, atawaangamiza kabisa hao wadhalimu
na kulipangisha shamba lake la mizabibu kwa
wakulima wengine ambao watampatia fungu lake la
matunda wakati wa mavuno." **42** Isa akawaambia,
"Je, hamjasoma katika Maandiko kwamba: "'Jiwe
walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni.
Mwenyezi Mungu ndiye alitenda jambo hili, nalo
ni la kushangaza machoni petu'? **43** "Kwa hiyo
ninawaambia, ufalme wa Mungu utaondolewa kwenu
na kupewa watu wengine wawezao kuzaa matunda
yake. **44** Yeye aangukaye juu ya jiwe hili atavunjika
vipande vipande, lakini yule litakayemwangukia
atasagwa kabisa." **45** Viongozi wa makuhani na
Mafarisayo waliposikia mifano ya Isa, walitambua
kuwa alikuwa akiwasema wao. **46** Wakatafuta njia ya
kumkamata, lakini wakaogopa umati wa watu, kwa
kuwa watu walimwona Isa kuwa ni nabii.

**22** Isa akasema nao tena kwa mifano, akawaambia,
**2** "Ufalme wa mbinguni unaweza kufananishwa
na mfalme mmoja aliyemwandalia mwanawe karamu
ya arusi. **3** Akawatuma watumishi wake kuwaita wale
waliokuwa wamealikwa karamuni, lakini wakakataa
kuja. **4** "Kisha akawatuma watumishi wengine
akisema, 'Waambieni wale walioalikwa kwamba
nimeandaa chakula. Nimekwisha kuchinja mafahali
wangu na vinono, karamu iko tayari. Karibuni kwa
karamu ya arusi.' **5** "Lakini hawakuzingatia, wakaenda
zao: huyu shambani mwake na mwingine kwenye
biashara zake. **6** Wengine wao wakawakamata
wale watumishi wake, wakawatesa na kuwaua. **7**
Yule mfalme akakasirika sana, akapeleka jeshi lake
likawaangamiza wale wauaji na kuuteketeza mji
wao kwa moto. **8** "Kisha akawaambia watumishi
wake, 'Karamu ya arusi imeshakuwa tayari, lakini
wale niliowaalika hawakustahili kuja. **9** Kwa hiyo
nendeni katika njia panda mkamwalike karamuni
yeyote mtakayemwona.' **10** Wale watumishi wakaenda
barabarani, wakawakusanya watu wote waliowaona,
wema na wabaya. Ukumbi wa arusi ukajaa wageni.
**11** "Lakini mfalme alipoingia ndani ili kuwaona wageni,
akamwona mle mtu mmoja ambaye hakuwa amevaa
vazi la arusi. **12** Mfalme akamuuliza, 'Rafiki, uliingiaje
humu bila vazi la arusi?' Yule mtu hakuwa na la
kusema. **13** "Ndipo mfalme akawaambia watumishi
wake, 'Mfungeni mikono na miguu mkamtupe nje,
kwenye giza. Huko kutakuwa na kilio na kusaga
meno.' **14** "Kwa maana walioitwa ni wengi, lakini
walioteuliwa ni wachache." **15** Ndipo Mafarisayo
wakatoka nje wakaandaa mpango wa kumtega
Isa katika maneno yake. **16** Wakatuma wanafunzi
wao pamoja na Maherode kwake. Nao wakasema,
"Mwalimu, tunajua kwamba wewe ni mtu mwadilifu
na unafundisha njia ya Mungu katika kweli bila
kuyumbishwa na mtu wala kuonesha upendeleo. **17**
Tuambie basi, wewe unaonaje? Je, ni halali kulipa
kodi kwa Kaisari, au la?" **18** Lakini Isa alifahamu
kusudi lao mbaya, akawaambia, "Enyi wanafiki, kwa
nini mnajaribu kunitega? **19** Nionesheni hiyo sarafu
inayotumika kwa kulipia kodi." Wakamletea dinari. **20**
Naye akawauliza, "Sura hii ni ya nani? Na maandishi
haya ni ya nani?" **21** Wakamjibu, "Ni vya Kaisari."
Basi Isa akawaambia, "Mpeni Kaisari kilicho cha
Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu." **22**
Waliposikia hili, wakashangaa. Hivyo wakamwacha,
wakaenda zao. **23** Siku hiyo hiyo Masadukayo, wale
wasemao kuwa hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Isa na kumuuliza swali, wakisema, **24** "Mwalimu,
Musa alisema, 'Mtu akifa bila kuwa na watoto,
ndugu yake inampasa amwoe huyo mjane ili ampatie
watoto huyo nduguye aliyekufa.' **25** Basi palikuwa
na ndugu saba miongoni mwetu. Yule wa kwanza
akaoa mke, naye akafa, na kwa kuwa hakuwa na
watoto, akamwachia nduguye yule mjane. **26** Ikatokea
vivyo hivyo kwa yule ndugu wa pili, na wa tatu,

hadi wote saba. 27 Hatimaye, yule mwanamke naye
akafa. 28 Sasa basi, siku ya ufufuo, yeye atakuwa
mke wa nani miongoni mwa wale ndugu saba, kwa
kuwa wote walikuwa wamemwoa huyo mwanamke?”
29 Isa akawajibu, “Mwapotoka kwa sababu hamjui
Maandiko wala uweza wa Mungu. 30 Wakati wa
ufufuo, watu hawataoa wala kuolewa, bali watakuwa
kama malaika wa mbinguni. 31 Lakini kuhusu ufufuo
wa wafu, hamjasoma kile Mungu alichowaambia,
kwamba, 32 ‘Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Mungu
wa Isaka, na Mungu wa Yakobo’? Yeye si Mungu
wa wafu, bali ni Mungu wa walio hai.” 33 Wale
umati wa watu waliposikia hayo, walishangaa sana
kwa mafundisho yake. 34 Mafarisayo waliposikia
kwamba Isa alikuwa amewanyamazisha Masadukayo,
Mafarisayo wakakusanyika pamoja. 35 Mmoja wao,
mtaalamu wa Torati, akamuuliza swali ili kumjaribu,
akisema, 36 “Mwalimu, ni amri ipi katika Torati iliyo kuu
kuliko zote?” 37 Isa akamjibu, “‘Mpende Mwenyezi
Mungu, Mungu wako, kwa moyo wako wote na kwa
roho yako yote na kwa akili zako zote.’ 38 Hii ndiyo
amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. 39 Nayo ya pili ni
kama hiyo, nayo ni hii: ‘Mpende jirani yako kama
nafsi yako.’ 40 Amri hizi mbili ndizo msingi wa Torati
na Manabii.” 41 Mafarisayo wakiwa wamekusanyika
pamoja, Isa akawauliza, 42 “Mnaonaje kuhusu Al-
Masihi? Yeye ni mwana wa nani?” Wakamjibu, “Yeye
ni mwana wa Daudi.” 43 Akawaambia, “Inakuwaje
basi kwamba Daudi, akinena kwa kuongozwa na
Roho wa Mungu, anamwita Al-Masihi ‘Bwana’? Kwa
maana asema, 44 “‘Mwenyezi Mungu alimwambia
Bwana wangu: “Keti mkono wangu wa kuume, hadi
nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.”’ 45
Kama basi Daudi anamwita yeye ‘Bwana,’ awezaje
kuwa mwanawe?” 46 Hakuna mtu aliyeweza kumjibu
Isa neno. Tena tangu siku hiyo hakuna aliyethubutu
kumuuliza tena maswali.

**23** Kisha Isa akaambia wale umati wa watu
na wanafunzi wake: 2 “Walimu wa Torati
na Mafarisayo wameketi kwenye kiti cha Musa,
3 hivyo inawapasa kuwatii na kufanya kila kitu
wanachowaambia. Lakini msifuate yale wanayotenda,
kwa sababu hawatendi yale wanayohubiri. 4 Wao
hufunga mizigo mikubwa na kuiweka mabegani mwa
watu, lakini wao wenyewe hawako radhi hata kuinua
kidole ili kuisogeza. 5 “Wao hutenda mambo yao
yote ili waonekane na watu. Hupanua vikasha vyao
vyenye maandiko ya sheria na kurefusha matamvua
ya mavazi yao. 6 Wanapenda kukalia viti vya heshima
katika karamu, na vile viti maalum sana katika
masinagogi. 7 Hupenda kusalimiwa masokoni na
kutaka watu wawaite ‘Mwalimu.’ 8 “Lakini ninyi
msiitwe ‘Mwalimu,’ kwa sababu mnaye Bwana mmoja
na ninyi nyote ni ndugu. 9 Nanyi msimwite mtu
yeyote ‘Baba,’ hapa duniani, kwa maana mnaye
Baba mmoja, naye yuko mbinguni. 10 Wala msiitwe
‘Mwalimu,’ kwa maana mnaye mwalimu mmoja tu,
ndiye Al-Masihi. 11 Yeye aliye mkuu kuliko ninyi nyote
miongoni mwenu atakuwa mtumishi wenu. 12 Kwa
kuwa yeyote anayejikweza atashushwa, na yeyote
anayejinyenyekeza atakwezwa. 13 “Lakini ole wenu,
walimu wa Torati na Mafarisayo, enyi wanafiki! Kwa
maana mnawafungia watu milango ya ufalme wa
mbinguni. Ninyi wenyewe hamuingii humo, nao wale
wanaotaka kuingia mnawazuia. [ 14 Ole wenu walimu
wa Torati na Mafarisayo, enyi wanafiki! Mnakula
katika nyumba za wajane, nanyi kwa kujifanya kuwa
wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo hukumu yenu
itakuwa kuu zaidi.] 15 “Ole wenu walimu wa Torati na
Mafarisayo, enyi wanafiki! Ninyi mnasafiri baharini na
nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja mwongofu, lakini
baada ya kumpata, mnamfanya mwana wa Jehanamu
mara mbili kuliko ninyi! **(Geenna g1067)** 16 “Ole wenu,
viongozi vipofu! Ninyi mwasema, ‘Mtu akiapa kwa
Hekalu, kiapo hicho si kitu; lakini mtu akiapa kwa
dhahabu ya Hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.’
17 Ninyi vipofu wapumbavu! Ni kipi kilicho kikuu zaidi:
ni ile dhahabu, au ni lile Hekalu linaloifanya hiyo
dhahabu kuwa takatifu? 18 Pia mnasema, ‘Mtu akiapa
kwa madhabahu, si kitu; lakini mtu akiapa kwa sadaka
iliyo juu ya madhabahu, amefungwa kwa kiapo chake’
19 Ninyi vipofu! Ni kipi kikuu zaidi: ni sadaka, au ni
madhabahu yanayoifanya hiyo sadaka kuwa takatifu?
20 Basi, mtu anayeapa kwa madhabahu, anaapa kwa
hayo madhabahu na vitu vyote vilivyo juu yake. 21
Naye mtu anayeapa kwa Hekalu, anaapa kwa hilo
Hekalu na kwa huyo akaaye ndani yake. 22 Naye
anayeapa kwa mbingu, anaapa kwa kiti cha enzi cha
Mungu na kwa yeye anayeketi kwenye kiti hicho.
23 “Ole wenu walimu wa Torati na Mafarisayo, ninyi
wanafiki! Kwa maana mnatoa zaka ya mnanaa, bizari
na jira, lakini mmeacha mambo makuu zaidi ya sheria,

yaani haki, huruma na uaminifu. Iliwapasa kufanya
haya makuu ya sheria bila kupuuza hayo matoleo.
**24** Ninyi viongozi vipofu, mnachuja kiroboto lakini
mnameza ngamia! **25** "Ole wenu, walimu wa Torati na
Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnasafisha
kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa
unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. **26** Ewe Farisayo
kipofu! Safisha ndani ya kikombe na sahani kwanza,
ndipo nje itakuwa safi pia. **27** "Ole wenu, walimu wa
Torati na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnafanana na
makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo yanapendeza
kwa nje, lakini ndani yamejaa mifupa ya wafu na
kila aina ya uchafu. **28** Vivyo hivyo, kwa nje ninyi
mnaonekana kwa watu kuwa wenye haki, lakini kwa
ndani mmejaa unafiki na uovu. **29** "Ole wenu, walimu
wa Torati na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Mnajenga
makaburi ya manabii na kuyapamba makaburi ya
wenye haki. **30** Nanyi mwasema, 'Kama tungeishi
wakati wa baba zetu, hatungeshiriki katika kumwaga
damu ya manabii!' **31** Hivyo mnajishuhudia wenyewe
kwamba ninyi ni wana wa wale waliowaua manabii. **32**
Haya basi, kijazeni kipimo cha dhambi ya baba zenu!
**33** "Ninyi nyoka, ninyi uzao wa nyoka wenye sumu!
Mtaiepukaje hukumu ya Jehanamu? **(Geenna g1067)** **34**
Kwa sababu hii, tazameni, natuma kwenu manabii na
wenye hekima na walimu. Baadhi yao mtawaua na
kuwasulubisha, na wengine wao mtawapiga mijeledi
katika masinagogi yenu na kuwafuatia kutoka mji
mmoja hadi mji mwingine. **35** Hivyo ile damu ya wenye
haki wote iliyomwagwa hapa duniani, tangu damu ya
Habili, aliyekuwa mwenye haki, hadi damu ya Zakaria
mwana wa Barakia, mliyemuua kati ya patakatifu na
madhabahu, itawajia juu yenu. **36** Amin, nawaambia,
haya yote yatakuja kwa kizazi hiki. **37** "Ee Yerusalemu,
Yerusalemu, uwauaye manabii na kuwapiga mawe
wale waliotumwa kwako! Mara ngapi nimetamani
kuwakusanya watoto wako pamoja, kama vile kuku
akusanyavyo vifaranga wake chini ya mabawa yake,
lakini hukutaka! **38** Tazama nyumba yenu imeachwa
ukiwa. **39** Kwa maana nawaambia, hamtaniona tena
tangu sasa hadi mtakaposema, 'Amebarikiwa yeye
ajaye kwa Jina la Mwenyezi Mungu.'"

**24** Isa akatoka Hekaluni na alipokuwa akienda zake,
wanafunzi wake wakamwendea ili kumwonesha
majengo ya Hekalu. **2** Ndipo Isa akawauliza, "Je,
mnayaona haya yote? Amin, nawaambia, hakuna hata
jiwe moja hapa litakalobaki juu ya jingine, bali kila moja
litabomolewa." **3** Isa alipokuwa ameketi kwenye Mlima
wa Mizeituni, wanafunzi wake wakamjia faraghani,
wakamuuliza, "Tuambie, mambo haya yatatukia lini,
nayo dalili ya kuja kwako na ya mwisho wa dunia ni
gani?" **(aiōn g165)** **4** Isa akawajibu, "Jihadharini, mtu
yeyote asiwadanganye. **5** Kwa maana wengi watakuja
kwa Jina langu, wakidai, 'Mimi ndiye Al-Masihi,' nao
watawadanganya wengi. **6** Mtasikia habari za vita
na tetesi za vita. Angalieni msitishike, kwa maana
haya hayana budi kutukia. Lakini ule mwisho bado.
**7** Taifa litainuka dhidi ya taifa, na ufalme dhidi ya
ufalme. Kutakuwa na njaa na mitetemeko ya ardhi
sehemu mbalimbali. **8** Haya yote yatakuwa ndio
mwanzo wa uchungu. **9** "Ndipo mtasalitiwa, ili mteswe
na kuuawa, nanyi mtachukiwa na mataifa yote kwa
ajili yangu. **10** Wakati huo, wengi wataacha imani
yao, nao watasalitiana kila mmoja na mwenzake na
kuchukiana. **11** Watatokea manabii wengi wa uongo,
nao watawadanganya watu wengi. **12** Kwa sababu ya
kuongezeka kwa uovu, upendo wa watu wengi utapoa,
**13** lakini yule atakayevumilia hadi mwisho ataokolewa.
**14** Injili hii ya ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote
kuwa ushuhuda kwa mataifa yote. Ndipo mwisho
utakapokuja. **15** "Hivyo mtakapoona lile 'chukizo la
uharibifu' lililonenwa na nabii Danieli limesimama
mahali patakatifu (asomaye na afahamu), **16** basi
wale walio Yudea wakimbilie milimani. **17** Yeyote
aliye juu ya dari ya nyumba asishuke ili kuchukua
chochote kutoka ndani ya nyumba. **18** Aliye shambani
asirudi nyumbani kuchukua vazi lake. **19** Ole wao
wenye mimba na wale wanaonyonyesha watoto siku
hizo! **20** Ombeni ili kukimbia kwenu kusiwe wakati
wa baridi au siku ya Sabato. **21** Kwa maana wakati
huo kutakuwa na dhiki kuu ambayo haijapata kuwepo
tangu mwanzo wa dunia hadi sasa: wala haitakuwepo
tena kamwe. **22** "Kama siku hizo zisingefupishwa,
hakuna mtu ambaye angeokoka. Lakini kwa ajili
ya wateule, siku hizo zitafupishwa. **23** Wakati huo
mtu yeyote akiwaambia, 'Tazama, Al-Masihi huyu
hapa!' au, 'Al-Masihi yuko kule,' msisadiki. **24** Kwa
maana watatokea masihi wa uongo na manabii wa
uongo, nao watafanya ishara kubwa na maajabu
mengi ili kuwapotosha, ikiwezekana, hata wale
wateule hasa. **25** Tazameni, nimekwisha kuwaambia
mapema. **26** "Basi mtu yeyote akiwaambia, 'Yule kule

nyikani,’ msiende huko. Au akisema, ‘Yuko kwenye
chumba,’ msisadiki. 27 Kwa maana kama vile radi
itokavyo mashariki na kuonekana hata magharibi,
ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu.
28 Kwa maana popote ulipo mzoga, huko ndiko
wakusanyikapo tai. 29 “Mara baada ya dhiki ya siku
zile, “‘jua litatiwa giza, nao mwezi hautatoa nuru yake;
nazo nyota zitaanguka kutoka angani, na nguvu za
anga zitatikisika.’ 30 “Ndipo itakapotokea ishara ya
Mwana wa Adamu angani, na makabila yote ya dunia
yataomboleza. Nao watamwona Mwana wa Adamu
akija juu ya mawingu ya angani, katika uwezo na
utukufu mkuu. 31 Naye atawatuma malaika wake
kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya
wateule wake kutoka pande zote nne za dunia,
kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwisho
mwingine. 32 “Basi jifunzeni somo hili kutokana na
mtini: Matawi yake yanapoanza kuchipua na kutoa
majani, mnatambua kwamba wakati wa kiangazi
umekaribia. 33 Vivyo hivyo, mnapoyaona mambo
haya yote, mtambue kwamba wakati u karibu, hata
malangoni. 34 Amin, nawaambia, kizazi hiki hakitapita
hadi mambo haya yote yawe yametimia. 35 Mbingu
na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita
kamwe. 36 “Kwa habari ya siku ile na saa, hakuna
ajuaye, hata malaika walio mbinguni wala Mwana,
ila Baba peke yake. 37 Kama ilivyokuwa wakati wa
Nuhu, ndivyo itakavyokuwa kuja kwake Mwana wa
Adamu. 38 Kwa maana siku zile kabla ya gharika,
watu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa,
hadi siku ile Nuhu alipoingia katika safina. 39 Nao
hawakujua lolote hadi gharika ilipokuja ikawakumba
wote. Hivyo ndivyo itakavyokuwa atakapokuja Mwana
wa Adamu. 40 Watu wawili watakuwa shambani,
naye mmoja atatwaliwa na mwingine ataachwa. 41
Wanawake wawili watakuwa wanasaga kwa kinu
cha mkono, naye mmoja atatwaliwa na mwingine
ataachwa. 42 “Basi kesheni, kwa sababu hamjui ni siku
gani atakapokuja Bwana wenu. 43 Lakini fahamuni
jambo hili: Kama mwenye nyumba angejua ni wakati
gani wa usiku ambao mwizi atakuja, angekesha
na hangekubali nyumba yake kuvunjwa. 44 Kwa
hiyo ninyi pia hamna budi kuwa tayari, kwa sababu
Mwana wa Adamu atakuja saa msiyotazamia. 45
“Ni nani basi aliye mtumishi mwaminifu na mwenye
busara, ambaye bwana wake amemweka kusimamia
watumishi wengine katika nyumba yake, ili awape
chakula chao kwa wakati unaofaa? 46 Heri mtumishi
yule ambaye bwana wake atakaporudi atamkuta
akifanya hivyo. 47 Amin, nawaambia, atamweka
mtumishi huyo kuwa msimamizi wa mali yake yote. 48
Lakini kama huyo mtumishi ni mwovu, naye akasema
moyoni mwake, ‘Bwana wangu atakawia muda mrefu,’
49 kisha akaanza kuwapiga watumishi wenzake, na
kula na kunywa pamoja na walevi. 50 Basi bwana
wa mtumishi huyo atakuja siku asiyodhani na saa
asiyoijua. 51 Atamkata vipande vipande na kumweka
pamoja na wanafiki, mahali ambako kutakuwa ni kulia
na kusaga meno.

**25** “Wakati huo, ufalme wa mbinguni utakuwa
kama wanawali kumi waliochukua taa zao
na kwenda kumlaki bwana arusi. 2 Watano wao
walikuwa wapumbavu na watano walikuwa wenye
busara. 3 Wale wapumbavu walichukua taa zao
lakini hawakuchukua mafuta ya akiba, 4 lakini wale
wenye busara walichukua taa zao na mafuta ya akiba
kwenye vyombo. 5 Bwana arusi alipokawia kuja wale
wanawali wote wakasinzia na kulala. 6 “Usiku wa
manane pakawa na kelele: ‘Tazameni, huyu hapa
bwana arusi! Tokeni nje mkamlaki!’ 7 “Ndipo wale
wanawali wote wakaamka na kuzitengeneza taa
zao. 8 Wale wapumbavu wakawaambia wale wenye
busara, ‘Tupatieni mafuta yenu kidogo; taa zetu
zinazimika.’ 9 “Lakini wale wenye busara wakawajibu,
‘Sivyo, hayatutoshi sisi na ninyi pia. Afadhali mwende
kwa wauzao mkajinunulie mafuta yenu.’ 10 “Nao
walipokuwa wakienda kununua mafuta, bwana arusi
akafika. Wale wanawali waliokuwa tayari wakaingia
ndani pamoja naye kwenye karamu ya arusi na mlango
ukafungwa. 11 “Baadaye wale wanawali wengine
nao wakaja, wakaita, ‘Bwana! Bwana! Tufungulie
mlango!’ 12 “Lakini yeye bwana arusi akawajibu,
‘Amin, amin nawaambia, siwajui ninyi!’ 13 “Kwa hiyo
kesheni, kwa sababu hamjui siku wala saa. 14 “Tena,
ufalme wa mbinguni ni kama mtu aliyetaka kusafiri,
naye akawaita watumishi wake na kuweka mali yake
kwenye uangalizi wao. 15 Mmoja akampa talanta tano,
mwingine talanta mbili, na mwingine talanta moja.
Kila mmoja alipewa kadiri ya uwezo wake. Kisha yeye
akasafiri. 16 Yule aliyepewa talanta tano akaenda
mara moja akafanya nazo biashara akapata talanta
nyingine tano zaidi. 17 Yule aliyepewa talanta mbili

akafanya vivyo hivyo, akapata nyingine mbili zaidi. **18**
Lakini yule mtumishi aliyekuwa amepokea talanta
moja, alienda akachimba shimo ardhini na kuificha ile
talanta ya bwana wake. **19** “Baada ya muda mrefu,
yule bwana wa wale watumishi akarudi na kufanya
hesabu nao. **20** Yule mtumishi aliyepokea talanta
tano akaja, akaleta nyingine tano zaidi. Akasema,
‘Bwana uliweka kwenye uangalizi wangu talanta
tano. Tazama, nimepata faida ya talanta tano zaidi.’
**21** “Bwana wake akamwambia, ‘Umefanya vizuri
sana, mtumishi mwema na mwaminifu! Umekuwa
mwaminifu kwa vitu vichache; nami nitakuweka kuwa
msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha
ya bwana wako!’ **22** “Yule mwenye talanta mbili naye
akaja. Akasema, ‘Bwana, uliweka kwenye uangalizi
wangu talanta mbili. Tazama nimepata hapa talanta
mbili zaidi.’ **23** “Bwana wake akajibu, ‘Umefanya vizuri
sana, mtumishi mwema na mwaminifu. Umekuwa
mwaminifu kwa vitu vichache; nami nitakuweka kuwa
msimamizi wa vitu vingi. Njoo ushiriki katika furaha
ya bwana wako!’ **24** “Kisha yule mtumishi aliyepokea
talanta moja akaja, akasema, ‘Bwana, nilijua kwamba
wewe ni mtu mgumu, unayevuna mahali usipopanda
na kukusanya mahali usipotawanya mbegu. **25** Kwa
hiyo niliogopa, nikaenda, nikaificha talanta yako
ardhini. Tazama, hii hapa ile iliyo mali yako.’ **26**
“Bwana wake akajibu, ‘Wewe mtumishi mwovu na
mvivu! Ulijua kwamba ninavuna mahali nisipopanda
na kukusanya mahali nisipotawanya mbegu. **27**
Vyema basi, ingekupasa kuweka fedha yangu kwa
watoa riba, ili nirudipo, nichukue ile iliyo yangu na
faida yake. **28** “‘Basi mnyang’anyeni hiyo talanta,
mkampe yule mwenye talanta kumi. **29** Kwa maana
kila mtu aliye na kitu atapewa zaidi, naye atakuwa
navyo tele. Lakini yule asiye na kitu, hata kile alicho
nacho atanyang’anywa. **30** Nanyi mtupeni huyo
mtumishi asiyefaa nje, kwenye giza, mahali ambako
kutakuwa na kilio na kusaga meno.’ **31** “Mwana wa
Adamu atakapokuja katika utukufu wake na malaika
wote watakatifu pamoja naye, ndipo atakapoketi
kwenye kiti cha enzi cha utukufu wake. **32** Mataifa
yote watakusanyika mbele zake, naye atawatenga
kama mchungaji anavyotenga kondoo na mbuzi. **33**
Atawaweka kondoo upande wake wa kuume, na
mbuzi upande wake wa kushoto. **34** “Ndipo Mfalme
atawaambia wale walio upande wake wa kuume,
‘Njooni, ninyi mliobarikiwa na Baba yangu; urithini
ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuumbwa kwa
ulimwengu. **35** Kwa maana nilikuwa na njaa mkanipa
chakula, nilikuwa na kiu mkaninywesha, nilikuwa
mgeni mkanikaribisha, **36** nilikuwa uchi mkanivisha
nguo, nilikuwa mgonjwa mkanitunza, nami nilikuwa
kifungoni mkaja kunitembelea.’ **37** “Ndipo wale wenye
haki watakapomjibu, ‘Bwana, ni lini tulikuona ukiwa
na njaa tukakulisha, au ukiwa na kiu tukakunywesha?
**38** Lini tulikuona ukiwa mgeni tukakukaribisha, au
ukiwa uchi tukakuvisha nguo? **39** Tena ni lini tulikuona
ukiwa mgonjwa tukakutunza, au ukiwa kifungoni
tukakutembelea?’ **40** “Naye Mfalme atawajibu, ‘Amin
nawaambia, kwa jinsi mlivyomtendea mmoja wa
hawa ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.’
**41** “Kisha atawaambia wale walio upande wake
wa kushoto, ‘Ondokeni kwangu, ninyi mliolaaniwa,
nendeni kwenye moto wa milele ulioandaliwa kwa ajili
ya ibilisi na malaika wake. **(aiōnios g166)** **42** Kwa maana
nilikuwa na njaa nanyi hamkunipa chakula, nilikuwa na
kiu nanyi hamkuninywesha, **43** nilikuwa mgeni nanyi
hamkunikaribisha, nilikuwa uchi nanyi hamkunivisha
nguo, nilikuwa mgonjwa nanyi hamkunitunza, na
nilikuwa gerezani nanyi hamkuja kunitembelea.’ **44**
“Ndipo wao pia watajibu, ‘Bwana ni lini tulikuona
ukiwa na njaa au kiu, au ukiwa mgeni au uchi, au
ukiwa mgonjwa na kifungoni na hatukukuhudumia?’
**45** “Naye atawajibu, ‘Amin nawaambia, kwa jinsi
hamkumtendea mmoja wa hawa ndugu zangu walio
wadogo, hamkunitendea mimi.’ **46** “Ndipo hawa
watakapoingia kwenye adhabu ya milele, lakini wale
wenye haki wataingia katika uzima wa milele.” **(aiōnios
g166)**

**26** Isa alipomaliza kusema hayo yote, akawaambia
wanafunzi wake, **2** “Kama mnavyojua, baada
ya siku mbili itakuwa Pasaka, naye Mwana wa
Adamu atasalitiwa ili asulubiwe.” **3** Basi viongozi
wa makuhani na wazee wa watu wakakusanyika
katika jumba la utawala la kuhani mkuu, jina lake
Kayafa. **4** Wakapanga kumkamata Isa kwa siri
na kumuua. **5** Lakini wakasema, “Isiwe wakati wa
Sikukuu, kusitokee ghasia miongoni mwa watu.” **6** Isa
alikuwa Bethania nyumbani mwa Simoni aliyekuwa
na ukoma. **7** Naye mwanamke mmoja akamjia akiwa
na chupa ya marhamu yenye manukato ya thamani
kubwa. Akayamimina kichwani mwa Isa alipokuwa

ameketi mezani kula chakula. 8 Lakini wanafunzi wake
walipoona hayo wakakasirika, wakasema, “Upotevu
huu wote ni wa nini? 9 Manukato haya yangeuzwa kwa
bei kubwa, na fedha hizo wakapewa maskini.” 10 Isa,
akijua jambo hili, akawaambia, “Mbona mnamsumbua
huyu mwanamke? Yeye amenitendea jambo zuri
sana. 11 Maskini mtakuwa nao siku zote, lakini mimi
hamtakuwa nami siku zote. 12 Alipomiminia haya
manukato kwenye mwili wangu, amefanya hivyo
ili kuniandaa kwa ajili ya maziko yangu. 13 Amin,
nawaambia, mahali popote ulimwenguni ambapo hii
Injili itahubiriwa, jambo hili alilolitenda huyu mwanamke
litatajwa pia kwa ukumbusho wake.” 14 Kisha mmoja
wa wale wanafunzi kumi na wawili, aitwaye Yuda
Iskariote, alienda kwa viongozi wa makuhani 15 na
kuuliza, “Mtanipa nini nikimtia Isa mikononi mwenu?”
Wakamlipa vipande thelathini vya fedha. 16 Tangu
wakati huo Yuda akawa anatafuta wakati uliofaa
wa kumsaliti Isa. 17 Siku ya kwanza ya Sikukuu
ya Mikate Isiyotiwa Chachu, wanafunzi walimjia Isa
wakamuuliza, “Unataka twende wapi ili tukuandalie
mahali pa kula Pasaka?” 18 Akajibu, “Nendeni
kwa mtu fulani huko mjini, mkamwambie, ‘Mwalimu
asema hivi: Saa yangu imekaribia. Nitaiadhimisha
Pasaka pamoja na wanafunzi wangu katika nyumba
yako.’” 19 Hivyo wanafunzi wakafanya vile Isa
alivyokuwa amewaelekeza, nao wakaandaa Pasaka.
20 Ilipofika jioni, Isa alikuwa ameketi mezani pamoja
na wale wanafunzi wake kumi na wawili. 21 Nao
walipokuwa wakila, Isa akasema, “Amin, nawaambia,
mmoja wenu atanisaliti.” 22 Wakahuzunika sana,
wakaanza kumuuliza mmoja baada ya mwingine,
“Je, ni mimi Bwana?” 23 Isa akawaambia, “Yule
aliyechovya mkono wake katika bakuli pamoja nami
ndiye atakayenisaliti. 24 Mwana wa Adamu anaenda
zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini ole wake
mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu. Ingekuwa
heri kwake mtu huyo kama hangezaliwa!” 25 Kisha
Yuda, yule mwenye kumsaliti, akasema, “Je, ni mimi
Mwalimu?” Isa akajibu, “Naam, wewe mwenyewe
umesema.” 26 Walipokuwa wanakula, Isa akachukua
mkate, akashukuru, akaumega, na kuwapa wanafunzi
wake, akisema, “Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu.”
27 Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa,
akisema, “Nyweni nyote katika kikombe hiki. 28
Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa
ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. 29 Lakini
ninawaambia, tangu sasa sitakunywa tena katika
uzao huu wa mzabibu, hadi siku ile nitakapounywa
mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.”
30 Walipokwisha kuimba wimbo, wakatoka wakaenda
Mlima wa Mizeituni. 31 Kisha Isa akawaambia,
“Usiku huu, ninyi nyote mtaniacha, kwa maana
imeandikwa: “‘Nitampiga mchungaji, nao kondoo
wa hilo kundi watatawanyika.’ 32 Lakini baada ya
kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya.” 33
Petro akajibu, “Hata kama wote watakuacha, kamwe
mimi sitakuacha.” 34 Isa akamjibu, “Amin, nakuambia,
usiku huu, kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.”
35 Lakini Petro akasisitiza, “Hata kama itabidi kufa
pamoja nawe, sitakukana kamwe.” Nao wanafunzi
wale wengine wote wakasema vivyo hivyo. 36
Kisha Isa akaenda pamoja na wanafunzi wake hadi
kwenye bustani iitwayo Gethsemane, akawaambia,
“Kaeni hapa, nami niende kule nikaombe.” 37
Akamchukua Petro pamoja na wale wana wawili
wa Zebedayo, akaanza kuhuzunika na kufadhaika.
38 Kisha Isa akawaambia, “Moyo wangu umejawa
na huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe
pamoja nami.” 39 Akaenda mbele kidogo, akaanguka
kifudifudi, akaomba akisema, “Baba yangu, kama
inawezekana, kikombe hiki na kiniondokee. Lakini si
kama nipendavyo mimi, bali kama upendavyo wewe.”
40 Kisha akarudi kwa wanafunzi wake, akawakuta
wamelala. Akamuuliza Petro, “Je, ninyi hamkuweza
kukesha pamoja nami hata kwa saa moja? 41 Kesheni
na mwombe, msije mkaingia majaribuni. Roho iko
radhi, lakini mwili ni mdhaifu.” 42 Akaenda tena mara
ya pili na kuomba, “Baba yangu, kama haiwezekani
kikombe hiki kiniepuke nisikinywe, basi mapenzi yako
yafanyike.” 43 Aliporudi, akawakuta tena wamelala
kwa sababu macho yao yalikuwa mazito. 44 Hivyo
akawaacha akaenda zake tena mara ya tatu na
kuomba akisema maneno yale yale. 45 Kisha akarudi
kwa wanafunzi wake, akawaambia, “Bado mmelala na
kupumzika? Tazameni, saa imefika ambapo Mwana
wa Adamu anasalitiwa na kutiwa mikononi mwa wenye
dhambi. 46 Inukeni, twende zetu! Tazameni, msaliti
wangu yuaja!” 47 Alipokuwa bado anazungumza,
Yuda, mmoja wa wale kumi na wawili, akafika.
Alikuwa amefuatana na umati mkubwa wa watu
wenye panga na marungu, waliokuwa wametumwa

na viongozi wa makuhani na wazee wa watu. 48 Basi
msaliti alikuwa amewapa hao watu ishara, kwamba:
“Yule nitakayembusu ndiye. Mkamateni.” 49 Mara
Yuda akamjia Isa na kumsalimu, “Salamu, Mwalimu!”
Akambusu. 50 Isa akamwambia, “Rafiki, fanya kile
ulichokuja kufanya hapa.” Kisha wale watu wakasogea
mbele, wakamkamata Isa. 51 Ghafula mmoja wa wale
waliokuwa na Isa alipoona hivyo, akaushika upanga
wake, akauchomoa na kumpiga mtumishi wa kuhani
mkuu, akamkata sikio. 52 Ndipo Isa akamwambia,
“Rudisha upanga wako alani mwake, kwa maana
wote watumiao upanga watakufa kwa upanga. 53 Je,
unadhani siwezi kumwomba Baba yangu naye mara
moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya
malaika? 54 Lakini je, yale Maandiko yanayotabiri
kwamba ni lazima itendeke hivi yatatimiaje?” 55 Wakati
huo, Isa akaambia wale umati wa watu, “Je, mmekuja
na panga na marungu kunikamata kana kwamba
mimi ni mnyang’anyi? Siku kwa siku niliketi Hekaluni
nikifundisha, mbona hamkunikamata? 56 Lakini haya
yote yametukia ili maandiko ya manabii yapate
kutimia.” Ndipo wanafunzi wake wote wakamwacha
na kukimbia. 57 Wale waliomkamata Isa wakampeleka
kwa Kayafa, kuhani mkuu, mahali ambapo walimu wa
Torati pamoja na wazee walikuwa wamekusanyika.
58 Lakini Petro akamfuata kwa mbali hadi uani kwa
kuhani mkuu. Akaingia ndani, akaketi pamoja na
walinzi ili aone litakalotukia. 59 Viongozi wa makuhani
na Baraza la Wayahudi lote wakatafuta ushahidi
wa uongo dhidi ya Isa ili wapate kumuua. 60 Lakini
hawakupata jambo lolote, ingawa mashahidi wengi wa
uongo walijitokeza. Hatimaye wakajitokeza mashahidi
wawili wa uongo 61 na kusema, “Huyu mtu alisema,
‘Ninaweza kulivunja Hekalu la Mungu na kulijenga
tena kwa siku tatu.’” 62 Kisha kuhani mkuu akasimama
na kumwambia Isa, “Je, wewe hutajibu? Ni ushahidi
gani hawa watu wanauleta dhidi yako?” 63 Lakini
Isa akakaa kimya. Ndipo kuhani mkuu akamwambia,
“Nakuapisha mbele za Mungu aliye hai. Tuambie
kama wewe ndiwe Al-Masihi, Mwana wa Mungu.” 64
Isa akajibu, “Wewe umenena. Lakini ninawaambia
nyote: Siku za baadaye, mtamwona Mwana wa
Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mwenye
Nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni.” 65
Ndipo kuhani mkuu akararua mavazi yake na kusema,
“Amekufuru! Tuna haja gani tena ya mashahidi zaidi?
Tazama, sasa ninyi mmesikia alivyokufuru. 66 Uamuzi
wenu ni gani?” Wakajibu, “Anastahili kufa.” 67 Kisha
wakamtemea mate usoni na wengine wakampiga
ngumi. Wengine wakampiga makofi 68 na kusema,
“Tutabirie, wewe Al-Masihi! Ni nani aliyekupiga?” 69
Wakati huu Petro alikuwa amekaa nje uani. Mjakazi
mmoja akamjia na kumwambia, “Wewe pia ulikuwa
pamoja na Isa wa Galilaya.” 70 Lakini Petro akakana
mbele yao wote akisema, “Sijui hilo usemalo.” 71
Alipotoka nje kufika kwenye lango, mjakazi mwingine
alimwona, akawaambia watu waliokuwako, “Huyu mtu
alikuwa pamoja na Isa Al-Nasiri.” 72 Akakana tena
kwa kiapo akisema, “Mimi simjui huyo!” 73 Baada
ya muda mfupi, wale waliokuwa wamesimama pale
wakamwendea Petro, wakamwambia, “Hakika wewe
ni mmoja wao, kwa maana usemi wako ni kama wao.”
74 Ndipo Petro akaanza kujilaani na kuwaapia, “Mimi
simjui mtu huyo!” Papo hapo jogoo akawika. 75 Ndipo
Petro akakumbuka lile neno Isa alilokuwa amesema:
“Kabla jogoo hajawika, utanikana mara tatu.” Naye
akaenda nje, akalia kwa majonzi.

**27** Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani
wote na wazee wa watu wakafanya shauri
pamoja dhidi ya Isa ili kumuua. 2 Wakamfunga,
wakampeleka na kumkabidhi kwa Pilato, aliyekuwa
mtawala Mrumi. 3 Yuda, aliyemsaliti Isa, alipoona
kuwa Isa amehukumiwa, akajuta na akarudisha vile
vipande thelathini vya fedha alivyopewa na viongozi
wa makuhani na wazee wa watu. 4 Akasema,
“Nimetenda dhambi, kwa maana nimeisaliti damu isiyo
na hatia.” Wakamjibu, “Hilo latuhusu nini sisi? Ni shauri
yako.” 5 Basi Yuda akavitupa vile vipande vya fedha
ndani ya Hekalu akaondoka akaenda kujinyonga.
6 Wale viongozi wa makuhani wakazichukua zile
fedha wakasema, “Si halali kuchanganya fedha
hizi na sadaka kwa sababu hizi ni fedha zenye
damu.” 7 Hivyo basi, baada ya kushauriana, waliamua
kuzitumia kununulia shamba la mfinyanzi, liwe
mahali pa kuzikia wageni. 8 Hii ndiyo sababu lile
shamba likaitwa Shamba la Damu hadi leo. 9 Ndipo
likatimia neno lililonenwa na nabii Yeremia, kwamba,
“Walichukua vile vipande thelathini vya fedha, thamani
aliyowekewa na watu wa Israeli, 10 wakanunulia
shamba la mfinyanzi, kama vile Mwenyezi Mungu
alivyoniagiza.” 11 Wakati huo Isa akiwa amesimama
mbele ya mtawala, mtawala akamuuliza, “Wewe

ndiwe mfalme wa Wayahudi?” Isa akasema, “Wewe
wasema hivyo.” **12** Lakini viongozi wa makuhani
na wazee walipomshtaki, hakujibu neno. **13** Ndipo
Pilato akamuuliza, “Je, husikii ni mambo mangapi
wanayokushtaki nayo?” **14** Lakini Isa hakumjibu hata
kwa shtaka moja, kiasi kwamba mtawala alishangaa
sana. **15** Basi ilikuwa ni desturi ya mtawala kumfungua
mfungwa mmoja aliyechaguliwa na umati wa watu
wakati wa sikukuu. **16** Palikuwa na mfungwa mmoja
mwenye sifa mbaya, aliyeitwa Baraba. **17** Hivyo umati
wa watu walipokusanyika, Pilato akawauliza hao
watu, “Mnataka niwafungulie yupi: Baraba au Isa
aitwaye Al-Masihi?” **18** Kwa kuwa alitambua kwamba
walikuwa wamemkabidhi Isa kwake kwa ajili ya wivu.
**19** Pilato akiwa ameketi kwenye kiti cha hukumu,
mkewe akampelekea ujumbe huu: “Usiwe na jambo
lolote juu ya mtu huyu asiye na hatia, kwa kuwa leo
nimeteseka sana katika ndoto kwa sababu yake.” **20**
Lakini viongozi wa makuhani na wazee wakashawishi
umati wa watu kwamba waombe Baraba afunguliwe,
naye Isa auawe. **21** Mtawala akawauliza tena, “Ni
yupi kati ya hawa wawili mnayetaka niwafungulie?”
Wakajibu, “Baraba.” **22** Pilato akawaambia, “Basi
nifanye nini na huyu Isa aitwaye Al-Masihi?” Wakajibu
wote, “Msulubishe!” **23** Pilato akauliza, “Kwa nini?
Amefanya kosa gani?” Lakini wao wakazidi kupiga
kelele, wakisema, “Msulubishe!” **24** Pilato alipoona
kwamba hawezi kufanya lolote, lakini badala yake
ghasia zilikuwa zinaanza, akachukua maji, akanawa
mikono yake mbele ya umati wa watu, akasema,
“Sina hatia kwa damu ya mtu huyu, hili ni jukumu
lenu!” **25** Watu wote wakajibu, “Damu yake na iwe juu
yetu na juu ya watoto wetu!” **26** Basi akawafungulia
Baraba. Lakini baada ya kuamuru Isa apigwe mijeledi,
akamtoa ili asulubishwe. **27** Kisha askari wa mtawala
wakampeleka Isa kwenye Praitorio, na wakakusanya
kikosi kizima cha askari kumzunguka. **28** Wakamvua
nguo zake na kumvika vazi la rangi nyekundu, kisha
**29** wakasokota taji la miiba, wakaiweka kichwani pake.
Wakamwekea fimbo katika mkono wake wa kuume,
na wakapiga magoti mbele zake na kumdhihaki,
wakisema, “Salamu, mfalme wa Wayahudi!” **30**
Wakamtemea mate, wakachukua ile fimbo wakampiga
kichwani tena na tena. **31** Baada ya kumdhihaki,
wakamvua lile joho, wakamvika tena nguo zake. Kisha
wakampeleka ili wakamsulubishe. **32** Walipokuwa
wakienda, wakakutana na mtu mmoja kutoka Kirene,
jina lake Simoni, nao wakamlazimisha kuubeba ule
msalaba. **33** Wakafika mahali palipoitwa Golgotha
(maana yake ni Mahali pa Fuvu la Kichwa). **34**
Hapo wakampa Isa divai iliyochanganywa na nyongo
ili anywe; lakini alipoionja, akakataa kuinywa. **35**
Walipokwisha kumsulubisha, wakagawana mavazi
yake kwa kuyapigia kura. [Hili lilifanyika ili litimie
neno lililonenwa na nabii, “Waligawa nguo zangu
miongoni mwao na vazi langu wakalipigia kura.”] **36**
Kisha wakaketi, wakamchunga. **37** Juu ya kichwa
chake, kwenye msalaba, wakaandika shtaka lake hivi:
Huyu ni Isa Mfalme wa Wayahudi. **38** Wanyang’anyi
wawili walisulubiwa pamoja naye, mmoja upande
wake wa kuume na mwingine upande wa kushoto.
**39** Watu waliokuwa wakipita njiani wakamtukana
huku wakitikisa vichwa vyao, **40** na kusema, “Wewe
ambaye utalivunja Hekalu na kulijenga kwa siku tatu,
jiokoe mwenyewe basi! Kama wewe ni Mwana wa
Mungu, shuka msalabani.” **41** Vivyo hivyo, viongozi
wa makuhani, walimu wa Torati pamoja na wazee
wakamdhihaki, wakisema, **42** “Aliwaokoa wengine,
lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! Yeye ni mfalme wa
Israeli! Ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini.
**43** Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe
sasa kama anamtaka, kwa maana alisema, ‘Mimi
ni Mwana wa Mungu.’” **44** Hata wale wanyang’anyi
waliosulubiwa pamoja naye wakamtukana vivyo
hivyo. **45** Tangu saa sita hadi saa tisa giza liliifunika
nchi yote. **46** Ilipofika saa tisa, Isa akapaza sauti
akalia, “Eloi, Eloi, lama sabakthani?” (maana yake,
“Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?”)
**47** Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama pale
waliposikia hayo, wakasema, “Anamwita Ilya.” **48**
Ghafula mmoja wao akaenda mbio na kuleta sifongo,
akaichovya kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi
na akampa Isa ili anywe. **49** Wengine wakasema,
“Basi mwacheni. Hebu tuone kama Ilya atakuja
kumwokoa.” **50** Isa alipolia tena kwa sauti kuu,
akaitoa roho yake. **51** Wakati huo huo pazia la
Hekalu likachanika vipande viwili, kuanzia juu hadi
chini. Dunia ikatetemeka na miamba ikapasuka.
**52** Makaburi yakafunguka na miili ya watakatifu
waliokuwa wamekufa ikafufuliwa. **53** Wakatoka
makaburini, na baada ya Isa kufufuka, waliingia
kwenye Mji Mtakatifu na kuwatokea watu wengi. **54**

Basi yule jemadari na wale waliokuwa pamoja naye
wakimlinda Isa walipoona lile tetemeko na yale yote
yaliyokuwa yametukia, waliogopa sana, wakapaza
sauti na kusema, “Hakika huyu alikuwa Mwana
wa Mungu!” **55** Wanawake wengi walikuwa pale
wakitazama kwa mbali. Hawa walikuwa wamemfuata
Isa tangu Galilaya ili kushughulikia mahitaji yake. **56**
Miongoni mwao walikuwemo Mariamu Magdalene, na
Mariamu mama yao Yakobo na Yusufu, na mama yao
wana wa Zebedayo. **57** Ilipofika jioni, alifika mtu mmoja
tajiri kutoka Arimathaya aitwaye Yusufu, ambaye pia
alikuwa mwanafunzi wa Isa. **58** Akamwendea Pilato ili
kumwomba mwili wa Isa. Pilato akaamuru apewe.
**59** Yusufu akauchukua mwili wa Isa, akaufunga kwa
kitambaa cha kitani safi, **60** na kuuweka katika kaburi
lake mwenyewe jipya, alilokuwa amelichonga kwenye
mwamba. Kisha akavingirisha jiwe kubwa katika ingilio
la kaburi, akaenda zake. **61** Mariamu Magdalene
na yule Mariamu mwingine walikuwa mahali pale,
wakiwa wameketi mkabala na kaburi. **62** Kesho yake,
yaani siku iliyofuata ile ya Maandalizi ya Sabato,
viongozi wa makuhani na Mafarisayo wakamwendea
Pilato **63** na kusema, “Bwana, tumekumbuka kwamba
yule mdanganyifu wakati alikuwa bado hai alisema,
‘Baada ya siku tatu nitafufuka.’ **64** Basi uamuru kaburi
lilindwe kwa uthabiti hadi baada ya siku tatu. La sivyo,
wanafunzi wake wanaweza kuja kuuiba mwili wake
na kuwaambia watu kwamba amefufuliwa kutoka kwa
wafu. Udanganyifu huu wa mwisho utakuwa mbaya
kuliko ule wa kwanza.” **65** Pilato akawaambia, “Ninyi
mnao askari walinzi. Nendeni, liwekeeni ulinzi kadiri
mnavyoweza.” **66** Hivyo basi wakaenda na walinzi ili
kulilinda kaburi kwa uthabiti, wakatia muhuri kwenye
lile jiwe na kuweka ulinzi.

**28** Baada ya Sabato, alfajiri mapema siku ya
kwanza ya juma, Mariamu Magdalene na yule
Mariamu mwingine walienda kulitazama kaburi. **2**
Ghafula, pakawa na tetemeko kubwa la ardhi, kwa
sababu malaika wa Mwenyezi Mungu alishuka kutoka
mbinguni, akaenda kwenye kaburi, akalivingirisha
lile jiwe na kulikalia. **3** Sura ya huyo malaika ilikuwa
kama umeme, na mavazi yake yalikuwa meupe kama
theluji. **4** Wale walinzi wa kaburi walimwogopa sana,
wakatetemeka hata wakawa kama wafu. **5** Yule
malaika akawaambia wale wanawake, “Msiogope, kwa
maana ninajua kuwa mnamtafuta Isa aliyesulubiwa. **6**
Hayupo hapa, kwa kuwa amefufuka, kama alivyosema.
Njooni mpatazame mahali alipokuwa amelazwa.
**7** Kisha nendeni upesi mkawaambie wanafunzi
wake kwamba, ‘Amefufuka kutoka kwa wafu,
naye anawatangulia kwenda Galilaya. Mtamwona
huko.’ Sasa nimekwisha kuwaambia.” **8** Hivyo
wale wanawake wakaondoka pale kaburini wakiwa
wamejawa na hofu, lakini wakiwa na furaha
nyingi. Wakaenda mbio kuwaeleza wanafunzi wake
habari hizo. **9** Ghafula, Isa akakutana nao,
akasema, “Salamu!” Wale wanawake wakamkaribia,
wakaishika miguu yake, wakamwabudu. **10** Ndipo
Isa akawaambia, “Msiogope. Nendeni mkawaambie
ndugu zangu waende Galilaya, ndiko watakakoniona.”
**11** Wale wanawake wakiwa njiani wakienda, baadhi
ya wale askari waliokuwa wakilinda kaburi walienda
mjini na kuwaeleza viongozi wa makuhani kila
kitu kilichokuwa kimetukia. **12** Baada ya viongozi
wa makuhani kukutana na wazee na kupanga
njama, waliwapa wale askari kiasi kikubwa cha
fedha, **13** wakawaambia, “Semeni, ‘Wanafunzi wake
walikuja wakati wa usiku na kumwiba sisi tulipokuwa
tumelala.’ **14** Kama habari hizi zikimfikia mtawala,
sisi tutamwondolea mashaka nanyi hamtapata tatizo
lolote.” **15** Hivyo basi, wale askari wakazipokea hizo
fedha nao wakafanya kama walivyoelekezwa. Habari
hii imeenea miongoni mwa Wayahudi hadi leo. **16**
Basi wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda
hadi Galilaya kwenye ule mlima ambao Isa alikuwa
amewaagiza. **17** Walipomwona, wakamwabudu; lakini
baadhi yao wakaona shaka. **18** Isa akawajia na
kusema, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na
duniani. **19** Kwa sababu hii, nendeni mkawafanye
mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina
la Baba na la Mwana na la Roho wa Mungu, **20** nanyi
wafundisheni kuyashika mambo yote niliyowaamuru
ninyi. Hakika mimi niko pamoja nanyi siku zote, hadi
mwisho wa nyakati.” **(aiōn g165)**

# Marko

**1** Mwanzo wa Injili ya Isa Al-Masihi, Mwana wa
Mungu, **2** kama ilivyoandikwa katika kitabu cha
nabii Isaya: “Tazama, nitamtuma mjumbe wangu
mbele yako, atakayetengeneza njia mbele yako”: **3**
“sauti ya mtu aliaye nyikani, ‘Itengenezeni njia ya
Mwenyezi Mungu, yanyoosheni mapito yake.’” **4**
Yahya alikuja akibatiza huko nyikani, akihubiri ubatizo
wa toba kwa ajili ya msamaha wa dhambi. **5** Watu
kutoka Yudea yote na sehemu zote za Yerusalemu
walikuwa wakimwendea. Nao wakaziungama dhambi
zao, akawabatiza katika Mto Yordani. **6** Yahya alivaa
mavazi yaliyotengenezwa kwa singa za ngamia na
mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Alikula nzige na
asali ya mwitu. **7** Naye alihubiri akisema, “Baada
yangu atakuja yeye aliye na uwezo kuliko mimi,
ambaye sistahili hata kuinama na kulegeza kamba za
viatu vyake. **8** Mimi nawabatiza kwa maji, lakini yeye
atawabatiza kwa Roho wa Mungu.” **9** Wakati huo Isa
akaja kutoka Nasiri ya Galilaya, naye akabatizwa na
Yahya katika Mto Yordani. **10** Isa alipokuwa akitoka
ndani ya maji, aliona mbingu zikifunguka na Roho
wa Mungu akishuka juu yake kama hua. **11** Nayo
sauti kutoka mbinguni ikasema, “Wewe ni Mwanangu
mpendwa; nami nimependezwa nawe sana.” **12**
Wakati huo huo, Roho wa Mungu akamwongoza Isa
hadi nyikani, **13** naye Isa akawa huko nyikani kwa
muda wa siku arobaini, akijaribiwa na Shetani. Alikaa
na wanyama pori, nao malaika wakamhudumia.
**14** Baada ya Yahya kutiwa gerezani, Isa alienda
Galilaya, akaanza kuhubiri Injili ya Mungu, **15** akisema,
“Wakati umetimia, ufalme wa Mungu umekaribia.
Tubuni na kuiamini Injili.” **16** Isa alipokuwa akitembea
kando ya Bahari ya Galilaya, aliwaona Simoni na
Andrea nduguye wakizitupa nyavu zao baharini,
kwa kuwa walikuwa wavuvi. **17** Isa akawaambia,
“Njooni, nifuateni nami nitawafanya mwe wavuvi wa
watu.” **18** Mara wakaacha nyavu zao, wakamfuata. **19**
Alipoenda mbele kidogo, akamwona Yakobo mwana
wa Zebedayo na Yohana nduguye, wakiwa kwenye
mashua yao wakizitengeneza nyavu zao. **20** Papo
hapo akawaita, nao wakamwacha Zebedayo baba yao
kwenye mashua pamoja na watumishi wa kuajiriwa,
nao wakamfuata Isa. **21** Wakaenda hadi Kapernaumu.
Mara ilipofika siku ya Sabato, Isa akaingia sinagogi,
akaanza kufundisha. **22** Watu wakashangaa sana kwa
mafundisho yake, kwa maana alikuwa akiwafundisha
kama mtu mwenye mamlaka, wala si kama walimu wa
Torati. **23** Wakati huo huo katika sinagogi lao palikuwa
na mtu aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu, naye
akapaza sauti akisema, **24** “Tuna nini nawe, Isa Al-
Nasiri? Je, umekuja kutuangamiza? Ninakujua wewe
ni nani. Wewe ndiwe Aliye Mtakatifu wa Mungu!” **25**
Lakini Isa akamkemea, akamwamuru, “Nyamaza!
Mtoke mtu huyu!” **26** Yule pepo mchafu akamgaragaza
huyo mtu kwa nguvu, kisha akamtoka akipiga kelele
kwa sauti kubwa. **27** Watu wote wakashangaa,
hata wakaulizana wao kwa wao, “Haya ni mambo
gani? Ni mafundisho mapya, tena yenye mamlaka!
Anaamuru hata pepo wachafu, nao wanamtii!” **28**
Sifa zake zikaanza kuenea haraka katika eneo lote
la karibu na Galilaya. **29** Mara walipotoka katika
sinagogi, walienda pamoja na Yakobo na Yohana
hadi nyumbani mwa Simoni na Andrea. **30** Mama
mkwe wa Simoni alikuwa kitandani, ana homa,
nao wakamweleza Isa habari zake. **31** Hivyo Isa
akamwendea, akamshika mkono na kumwinua. Kisha
homa ikamwacha, naye akaanza kuwahudumia. **32**
Jioni ile baada ya jua kutua, watu wakamletea Isa
wagonjwa wote na waliopagawa na pepo wachafu. **33**
Mji wote ukakusanyika mbele ya nyumba hiyo. **34** Isa
akawaponya watu wengi waliokuwa na magonjwa ya
aina mbalimbali. Akawatoa pepo wachafu wengi, lakini
hakuwaacha hao pepo wachafu waseme, kwa sababu
walimjua yeye ni nani. **35** Alfajiri na mapema sana
kulipokuwa bado kuna giza, Isa akaamka, akaondoka,
akaenda mahali pa faragha ili kuomba. **36** Simoni na
wenzake wakaenda kumtafuta, **37** nao walipomwona,
wakapaza sauti, wakasema, “Kila mtu anakutafuta!”
**38** Isa akawajibu, “Twendeni mahali pengine, kwenye
vijiji jirani, ili niweze kuhubiri huko pia. Maana nilikuja
kwa kusudi hili.” **39** Kwa hiyo akazunguka Galilaya
yote, akihubiri katika masinagogi yao na kutoa pepo
wachafu. **40** Mtu mmoja mwenye ukoma alimjia
Isa, akapiga magoti, akimwomba, “Ukitaka, unaweza
kunitakasa.” **41** Isa, akiwa amejawa na huruma,
akaunyoosha mkono wake akamgusa, akamwambia,
“Nataka. Takasika!” **42** Mara ukoma ukamtoka, naye
akatakasika. **43** Baada ya Isa kumwonya vikali,
akamruhusu aende zake mara moja; **44** akamwambia,
“Hakikisha humwambii mtu yeyote habari hizi, bali

nenda ukajioneshe kwa kuhani, na ukatoe sadaka
alizoagiza Musa kwa utakaso wako, ili kuwa ushuhuda
kwao.” **45** Lakini yule mtu akaenda akaanza kutangaza
habari za kuponywa kwake waziwazi. Kwa hiyo, Isa
hakuweza tena kuingia katika miji waziwazi bali alikaa
sehemu zisizo na watu. Hata hivyo watu wakamfuata
huko kutoka kila upande.

**2** Baada ya siku kadhaa Isa alirudi Kapernaumu, watu
wakasikia kwamba yupo nyumbani. **2** Watu wengi
wakakusanyika, kiasi kwamba hapakubaki nafasi
yoyote hata mlangoni! Naye akawahubiria Neno. **3**
Ndipo baadhi ya watu wakaja wakamletea Isa mtu
aliyepooza, akiwa amebebwa na watu wanne. **4** Kwa
kuwa hawakuweza kumfikisha kwa Isa kwa sababu
ya umati wa watu, walitoboa tundu kwenye paa juu
ya mahali Isa alikuwa, wakamshusha mtu aliyepooza
akiwa amelalia mkeka wake. **5** Isa alipoiona imani
yao, alimwambia yule mtu aliyepooza, “Mwanangu,
dhambi zako zimesamehewa.” **6** Basi baadhi ya
walimu wa Torati waliokuwa wameketi pale wakawaza
mioyoni mwao, **7** “Kwa nini mtu huyu anasema hivi?
Huyu anakufuru! Ni nani awezaye kusamehe dhambi
isipokuwa Mungu peke yake?” **8** Mara moja Isa
akatambua rohoni mwake kile walichokuwa wanawaza
mioyoni mwao, naye akawaambia, “Kwa nini mnawaza
hivyo mioyoni mwenu? **9** Je, ni lipi lililo rahisi zaidi:
kumwambia huyu aliyepooza, ‘Umesamehewa dhambi
zako,’ au kusema, ‘Inuka, uchukue mkeka wako,
uende’? **10** Lakini ili mpate kujua kwamba Mwana
wa Adamu anayo mamlaka duniani ya kusamehe
dhambi”: Isa akamwambia yule aliyepooza, **11**
“Nakuambia, inuka, chukua mkeka wako, uende
nyumbani kwako.” **12** Yule mtu aliyekuwa amepooza
akasimama, akachukua mkeka wake, akatembea
machoni pao wote! Jambo hili likawashangaza wote,
wakamtukuza Mungu, wakisema, “Hatujapata kuona
jambo kama hili kamwe!” **13** Isa akaenda tena
kandokando ya Bahari ya Galilaya. Umati mkubwa
wa watu wakamfuata, naye akaanza kuwafundisha.
**14** Alipokuwa akitembea, akamwona Lawi mwana
wa Alfayo ameketi forodhani mahali pa kutoza
ushuru. Isa akamwambia, “Nifuate.” Naye Lawi
akaondoka, akamfuata Isa. **15** Isa alipokuwa ameketi
akila chakula nyumbani mwa Lawi, watoza ushuru
wengi na wenye dhambi walikuwa wakila pamoja
naye na wanafunzi wake, kwa maana ni watu
wengi waliokuwa wakimfuata. **16** Walimu wa Torati
waliokuwa Mafarisayo walipomwona akila pamoja
na watoza ushuru na wenye dhambi, wakawauliza
wanafunzi wake: “Mbona Isa anakula na watoza
ushuru na wenye dhambi?” **17** Isa aliposikia haya
akawaambia, “Watu wenye afya hawahitaji tabibu,
bali walio wagonjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali
wenye dhambi.” **18** Basi wanafunzi wa Yahya pamoja
na Mafarisayo walikuwa wakifunga. Watu wakamjia
Isa na kumuuliza, “Mbona wanafunzi wa Yahya
na wa Mafarisayo hufunga, lakini wanafunzi wako
hawafungi?” **19** Isa akawajibu, “Wageni wa bwana
arusi wawezaje kufunga wakati angali pamoja nao?
Wakati bwana arusi bado yuko pamoja nao, hawawezi
kufunga. **20** Lakini wakati utafika ambapo bwana arusi
ataondolewa kwao. Siku hiyo ndipo watakapofunga.
**21** “Hakuna mtu ashoneaye kiraka cha nguo mpya
kwenye nguo iliyochakaa. Akifanya hivyo, kile kiraka
kipya kitachanika kutoka ile nguo iliyochakaa, nayo
itachanika zaidi. **22** Wala hakuna mtu awekaye divai
mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo, ile
divai mpya itavipasua hivyo viriba, nayo hiyo divai
itamwagika na viriba vitaharibika. Lakini divai mpya
huwekwa kwenye viriba vipya.” **23** Siku moja ya
Sabato, Isa pamoja na wanafunzi wake walikuwa
wakipita katikati ya mashamba ya nafaka. Walipokuwa
wakitembea, wanafunzi wake wakaanza kuvunja
masuke. **24** Mafarisayo wakamwambia, “Tazama,
mbona wanafanya jambo lisilo halali kufanywa siku
ya Sabato?” **25** Isa akawajibu, “Je, hamjasoma
alivyofanya Daudi yeye na wenzake walipokuwa na
njaa, wakahitaji chakula? **26** Daudi aliingia katika
nyumba ya Mungu, Abiathari alipokuwa kuhani mkuu,
akaila ile mikate iliyowekwa wakfu, ambayo ni halali
kuliwa na makuhani tu. Naye pia akawapa wenzake.”
**27** Kisha Isa akawaambia, “Sabato ilifanyika kwa ajili
ya mwanadamu, lakini si mwanadamu kwa ajili ya
Sabato. **28** Hivyo, Mwana wa Adamu ndiye Bwana
wa Sabato.”

**3** Isa akaingia tena ndani ya sinagogi, na kulikuwa na
mtu aliyepooza mkono. **2** Wakawa wanamwangalia
waone kama atamponya huyo mtu siku ya Sabato, ili
wapate sababu ya kumshtaki. **3** Isa akamwambia yule
mtu mwenye mkono uliopooza, “Njoo hapa mbele ya
watu wote.” **4** Kisha Isa akawauliza, “Je, ni lipi lililo
halali siku ya Sabato: Ni kutenda mema au kutenda

mabaya? Ni kuokoa maisha au kuua?” Lakini wao
wakanyamaza. 5 Isa akawatazama kwa hasira watu
waliomzunguka pande zote, akahuzunika sana kwa
sababu ya ugumu wa mioyo yao. Akamwambia yule
mtu mwenye mkono uliopooza, “Nyoosha mkono
wako.” Akaunyoosha, nao ukawa umeponywa kabisa!
6 Kisha Mafarisayo wakatoka nje, nao wakaanza
kufanya njama ya kumuua Isa wakishirikiana na
Maherode. 7 Isa na wanafunzi wake wakaondoka
huko, wakaenda baharini, nao umati mkubwa wa watu
kutoka Galilaya wakamfuata. 8 Waliposikia mambo
yote aliyokuwa akiyafanya, makundi ya watu wakamjia
kutoka Yudea, Yerusalemu, Idumaya, na ng’ambo
ya Yordani, pamoja na wale wa maeneo ya Tiro na
Sidoni. 9 Kwa sababu ya umati mkubwa wa watu,
aliwaambia wanafunzi wake watayarishe mashua
ndogo kwa ajili yake, ili kuwazuia watu kumsonga. 10
Kwa kuwa alikuwa amewaponya wagonjwa wengi,
wale wenye magonjwa walikuwa wanasukumana
ili wapate kumgusa. 11 Kila mara pepo wachafu
walipomwona, walianguka chini mbele yake na kupiga
kelele wakisema, “Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.”
12 Lakini aliwaonya wasiwaambie wengine kumhusu.
13 Isa akapanda mlimani na kuwaita wale aliowataka,
nao wakamjia. 14 Akawachagua watu kumi na wawili
ambao aliwaita mitume, ili wapate kuwa naye, na
awatume kwenda kuhubiri 15 na kuwa na mamlaka
ya kutoa pepo wachafu. 16 Hawa ndio wale kumi na
wawili aliowachagua: Simoni (ambaye alimwita Petro);
17 Yakobo mwana wa Zebedayo, na Yohana nduguye
(ambao aliwaita Boanerge, maana yake Wana wa
Ngurumo); 18 Andrea, Filipo, Bartholomayo, Mathayo,
Tomaso, Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni
Mkananayo, 19 na Yuda Iskariote aliyemsaliti Isa.
20 Kisha Isa alipoingia ndani ya nyumba, umati wa
watu wakakusanyika tena, kiasi kwamba yeye na
wanafunzi wake hawakuweza kula chakula. 21 Ndugu
zake walipopata habari wakaja ili kumchukua kwa
maana watu walikuwa wakisema, “Amerukwa na
akili.” 22 Walimu wa Torati walioteremka kutoka
Yerusalemu walisema, “Amepagawa na Beelzebuli!
Anatoa pepo wachafu kwa nguvu ya mkuu wa pepo
wachafu!” 23 Basi Isa akawaita na kuzungumza
nao kwa mifano akasema: “Shetani awezaje kumtoa
Shetani? 24 Kama ufalme ukigawanyika dhidi yake
wenyewe, ufalme huo hauwezi kusimama. 25 Nayo
nyumba ikigawanyika dhidi yake yenyewe, nyumba
hiyo haiwezi kusimama. 26 Na kama Shetani akijipinga
mwenyewe na awe amegawanyika, hawezi kusimama,
bali mwisho wake umetimia. 27 Hakuna mtu yeyote
awezaye kuingia kwenye nyumba ya mtu mwenye
nguvu na kuteka nyara mali yake asipomfunga kwanza
yule mwenye nguvu. Ndipo ataweza kuteka nyara
mali yake. 28 Amin, nawaambia, watu wataweza
kusamehewa dhambi na kufuru zao zote; 29 lakini
yeyote anayemkufuru Roho Mtakatifu wa Mungu
hatasamehewa kamwe, atakuwa na hatia ya dhambi
ya milele.” **(aiōn g165, aiōnios g166)** 30 Isa alisema hivi kwa
sababu walikuwa wanasema, “Ana pepo mchafu.” 31
Kisha wakaja ndugu zake Isa pamoja na mama yake.
Wakiwa wamesimama nje, wakamtuma mtu kumwita.
32 Umati wa watu walikuwa wameketi kumzunguka,
nao wakamwambia, “Mama yako na ndugu zako wako
nje, wanakutafuta.” 33 Akawauliza, “Mama yangu na
ndugu zangu ni nani?” 34 Kisha akawatazama wale
watu waliokuwa wameketi kumzunguka pande zote,
akasema, “Hawa ndio mama yangu na ndugu zangu.
35 Mtu yeyote anayetenda mapenzi ya Mungu, huyo
ndiye kaka yangu, na dada yangu, na mama yangu.”

**4** Isa akaanza kufundisha tena kando ya bahari.
Palikuwa na umati mkubwa wa watu waliokuwa
wamekusanyika kumzunguka, hata ikambidi Isa aingie
kwenye mashua iliyokuwa baharini na kuketi humo,
nao watu wote walikuwa ufuoni mwa bahari. 2
Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, naye
katika mafundisho yake akasema: 3 “Sikilizeni!
Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu 4
Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine zilianguka
kando ya njia, nao ndege wakaja na kuzila. 5
Nyingine zilianguka kwenye mwamba usio na udongo
mwingi. Ziliota haraka kwa kuwa udongo ulikuwa
kidogo. 6 Lakini jua lilipozidi, mimea ikanyauka na
kukauka kwa kuwa mizizi yake haikuwa na kina.
7 Mbegu nyingine zilianguka kwenye miiba, nayo
miiba ikakua, ikaisonga hiyo mimea, hivyo haikutoa
mazao. 8 Mbegu nyingine zilianguka kwenye udongo
mzuri, zikaota vizuri na kukua, zikatoa mazao, moja
mara thelathini, nyingine mara sitini, na nyingine
mara mia moja.” 9 Kisha Isa akasema, “Mwenye
masikio ya kusikia, na asikie.” 10 Alipokuwa peke
yake, watu waliokuwa naye pamoja na wanafunzi
wake kumi na wawili wakamuuliza kuhusu mifano

yake. 11 Naye akawaambia, “Ninyi mmepewa siri ya
ufalme wa Mungu. Lakini kwa wale walio nje, kila kitu
husemwa kwa mifano, 12 ili, “‘kuona waone lakini
wasitambue, na kusikia wasikie lakini wasielewe;
wasije wakageuka na kusamehewa!’” 13 Kisha Isa
akawauliza, “Hamwelewi maana ya mfano huu? Basi
mtaelewaje mifano mingine? 14 Yule mpanzi hupanda
neno. 15 Hawa ndio wale walio kando ya njia ambako
neno lilipandwa. Walisikiapo neno, mara Shetani
huja na kulinyakua lile neno lililopandwa ndani yao.
16 Nazo zile mbegu zilizoanguka kwenye udongo
wenye miamba, ni wale wanaolisikia neno, na mara
hulipokea kwa furaha. 17 Lakini kwa kuwa hawana
mizizi, wao hudumu kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki
au mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, mara
wao huiacha imani. 18 Lakini wengine, kama mbegu
iliyopandwa kwenye miiba, hulisikia lile neno; 19 lakini
masumbufu ya maisha haya, na udanganyifu wa mali
na tamaa ya mambo mengine huja na kulisonga lile
neno na kulifanya lisizae. (aiōn g165) 20 Wengine,
kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri,
hulisikia lile neno, wakalipokea na kuzaa mazao. Wao
huzaa mara thelathini, au mara sitini, au mara mia
ya mbegu iliyopandwa.” 21 Akawaambia, “Je, taa
huwashwa na kufunikwa chini ya kikapu au mvunguni
mwa kitanda? Je, haiwashwi na kuwekwa juu ya
kinara chake? 22 Kwa kuwa hakuna kilichofichika
ambacho hakitafunuliwa, wala hakuna jambo lolote la
siri ambalo halitaletwa nuruni. 23 Mwenye masikio ya
kusikia, na asikie.” 24 Naye akawaambia, “Kuweni
waangalifu na yale mnayosikia. Kipimo kile mpimacho,
ndicho mtakachopimiwa ninyi, hata na zaidi. 25 Kwa
maana kila mtu aliye na kitu atapewa zaidi, naye
atakuwa navyo tele. Lakini yule asiye na kitu, hata kile
alicho nacho atanyang’anywa.” 26 Pia akawaambia,
“Ufalme wa Mungu unafanana na mtu apandaye
mbegu shambani. 27 Baada yake kuzipanda, usiku
na mchana, akiwa amelala au ameamka, mbegu
huota na kukua pasipo yeye kujua ikuavyo. 28
Udongo huifanya iote kuwa mche, halafu suke,
kisha nafaka kamili kwenye suke. 29 Mara nafaka
inapokuwa imekomaa, mkulima huenda shambani na
mundu kuvuna, maana mavuno yamekuwa tayari.” 30
Akawaambia tena, “Tuufananishe ufalme wa Mungu
na nini? Au tutumie mfano gani ili kuueleza? 31 Ni
kama punje ya haradali, ambayo ni mbegu ndogo
sana kuliko mbegu zote zinazopandwa ardhini. 32
Lakini ikipandwa, hukua ikawa mmea mkubwa kuliko
yote katika bustani, ikawa na matawi makubwa
hata ndege wa angani wanaweza kujenga viota
kwenye kivuli chake.” 33 Kwa mifano mingine mingi
kama hii Isa alinena nao neno lake, kwa kadiri
walivyoweza kulielewa. 34 Hakusema nao neno lolote
pasipo mfano. Lakini alipokuwa na wanafunzi wake,
aliwafafanulia kila kitu. 35 Ilipokaribia jioni ya siku
hiyo, Isa akawaambia wanafunzi wake, “Tuvukeni
hadi ng’ambo ya ziwa.” 36 Wakaacha umati wa watu,
na wakamchukua vile alivyokuwa kwenye mashua.
Palikuwa pia na mashua zingine nyingi pamoja naye.
37 Kukawa na dhoruba kali, nayo mawimbi yakaipiga
ile mashua hata ikawa karibu kujaa maji. 38 Isa
alikuwa katika shetri, akiwa analala juu ya mto.
Wanafunzi wake wakamwamsha, wakamwambia,
“Mwalimu, hujali kama tunazama?” 39 Akaamka,
akaukemea ule upepo, akayaambia yale mawimbi,
“Uwe kimya! Tulia!” Ule upepo ukatulia, kukawa
shwari kabisa. 40 Isa akawaambia wanafunzi wake,
“Kwa nini mnaogopa hivyo? Je, bado hamna imani?”
41 Nao wakawa wameogopa sana, wakaulizana, “Ni
nani huyu? Hata upepo na mawimbi vinamtii!”

5 Isa na wanafunzi wake wakafika upande wa pili
wa ziwa, wakaingia katika nchi ya Wagerasi. 2 Isa
alipotoka kwenye mashua, mara mtu mmoja mwenye
pepo mchafu akatoka makaburini, akakutana naye. 3
Mtu huyu aliishi makaburini, wala hakuna aliyeweza
kumzuia hata kwa kumfunga minyororo. 4 Kwa
kuwa mara kwa mara alikuwa amefungwa minyororo
mikononi na miguuni, lakini akaikata hiyo minyororo
na kuzivunja zile pingu miguuni mwake. Hapakuwa na
mtu yeyote aliyekuwa na nguvu za kumzuia. 5 Usiku
na mchana alikuwa makaburini na milimani, akipiga
kelele na kujikatakata kwa mawe. 6 Alipomwona Isa
kwa mbali, alimkimbilia, akapiga magoti mbele yake.
7 Akapaza sauti kwa nguvu akisema, “Una nini nami,
Isa, Mwana wa Mungu Aliye Juu Sana? Ninakusihi
kwa jina la Mungu, usinitese!” 8 Kwa kuwa Isa alikuwa
amemwambia, “Mtoke mtu huyu, wewe pepo mchafu!”
9 Isa akamuuliza, “Jina lako ni nani?” Akamjibu, “Jina
langu ni Legioni, kwa kuwa tuko wengi.” 10 Akamsihi
Isa sana asiwapeleke nje ya nchi ile. 11 Palikuwa
na kundi kubwa la nguruwe lililokuwa likilisha karibu
kando ya kilima. 12 Wale pepo wachafu wakamsihi Isa

wakisema, “Tuamuru twende kwenye wale nguruwe.
Turuhusu tuwaingie.” 13 Basi Isa akawaruhusu, nao
wale pepo wachafu wakatoka, wakawaingia hao
nguruwe. Lile kundi lilikuwa na nguruwe wapatao
elfu mbili, nao wote wakateremkia gengeni kwa kasi,
nao wakatumbukia ziwani na kuzama. 14 Wale watu
waliokuwa wakichunga hao nguruwe wakakimbilia
mjini na vijijini kueleza yaliyotukia. Watu wakaenda
kuona hayo yaliyokuwa yametukia. 15 Walipofika kwa
Isa, wakamwona yule mtu aliyekuwa amepagawa
na legioni ya pepo wachafu akiwa ameketi hapo,
amevaa nguo na mwenye akili timamu. Wakaogopa.
16 Wale walioyaona mambo hayo wakawaeleza
watu wengine yaliyomtokea yule mtu aliyekuwa
amepagawa na pepo wachafu, na habari za lile kundi
la nguruwe pia. 17 Basi watu wakaanza kumwomba
Isa aondoke katika nchi yao. 18 Isa alipokuwa anaingia
kwenye mashua, yule mtu aliyekuwa amepagawa na
pepo wachafu akamsihi Isa waende pamoja. 19 Isa
hakumruhusu, bali alimwambia, “Nenda nyumbani kwa
jamaa yako ukawaeleze mambo makuu aliyokutendea
Mwenyezi Mungu, na jinsi alivyokuhurumia.” 20
Yule mtu akaenda zake, akaanza kutangaza katika
Dekapoli mambo makuu Isa aliyomtendea. Nao
watu wote wakastaajabu. 21 Isa alipokwisha kuvuka
tena na kufika ng’ambo, umati mkubwa wa watu
wakamzunguka hapo kando ya bahari. 22 Kisha
mmoja wa viongozi wa sinagogi aliyeitwa Yairo
akafika pale. Naye alipomwona Isa, akapiga magoti
miguuni pake, 23 akamsihi akisema, “Binti yangu
mdogo ni mgonjwa mahututi. Tafadhali nakusihi, njoo
uweke mikono yako juu yake ili apate kupona, naye
ataishi.” 24 Hivyo Isa akaenda pamoja naye. Umati
mkubwa wa watu wakamfuata, nao watu wakawa
wanamsonga. 25 Hapo palikuwa na mwanamke
aliyekuwa amesumbuliwa na tatizo la kutokwa damu
kwa miaka kumi na mbili. 26 Mwanamke huyu alikuwa
ameteseka sana kwa mikono ya matabibu wengi, na
kutumia kila kitu alichokuwa nacho. Lakini badala
ya kupona, hali yake ilizidi kuwa mbaya. 27 Alikuwa
amesikia habari za Isa, naye akaja kwa nyuma yake
kwenye umati wa watu, akaligusa vazi lake, 28
kwa maana alisema moyoni mwake, “Nikiligusa vazi
lake tu, nitaponywa.” 29 Mara kutoka damu kwake
kukakoma, naye akajisikia mwilini mwake amepona
kabisa. 30 Ghafula Isa akatambua kuwa nguvu
zimemtoka. Akageukia umati wa watu na kuuliza, “Ni
nani aliyegusa mavazi yangu?” 31 Wanafunzi wake
wakamjibu, “Unaona jinsi watu wanavyokusonga.
Wawezaje kuuliza, ‘Ni nani aliyenigusa?’” 32 Lakini
Isa akaangalia pande zote ili aone ni nani aliyemgusa.
33 Yule mwanamke, akijua kilichomtokea, akaja,
akaanguka miguuni pake akitetemeka kwa hofu,
akamweleza ukweli wote. 34 Isa akamwambia,
“Binti, imani yako imekuponya. Nenda kwa amani,
upone kabisa ugonjwa wako.” 35 Alipokuwa bado
anaongea, watu wakafika kutoka nyumbani mwa
Yairo. Wakamwambia, “Binti yako amekufa. Kwa
nini kuendelea kumsumbua Mwalimu?” 36 Aliposikia
hayo waliyosema, Isa akamwambia huyo kiongozi
wa sinagogi, “Usiogope. Amini tu.” 37 Hakumruhusu
mtu yeyote amfuate isipokuwa Petro, Yakobo na
Yohana, nduguye Yakobo. 38 Walipofika nyumbani
mwa yule kiongozi wa sinagogi, Isa akaona ghasia,
watu wakilia na kuomboleza kwa sauti kubwa.
39 Alipokwisha kuingia ndani, akawaambia, “Kwa
nini mnafanya ghasia na kulia? Mtoto hajafa, bali
amelala tu.” 40 Wale watu wakamcheka. Baada ya
kuwafukuza wote nje, Isa akaenda na baba na mama
wa yule mtoto, pamoja na wale wanafunzi aliokuwa
nao, wakaingia ndani hadi pale alipokuwa mtoto
yule. 41 Akamshika mtoto mkono, akamwambia,
“Talitha koum!” (maana yake, “Msichana, nakuambia:
amka!”) 42 Mara yule msichana akasimama, akaanza
kutembea (alikuwa na umri wa miaka kumi na
mbili). Walipoona haya, wakastaajabu sana. 43 Isa
akawaagiza kwa ukali wasimweleze mtu yeyote
jambo hilo, naye akawaambia wampe yule msichana
chakula.

**6** Isa akaondoka huko na kwenda mji wa kwao,
akiandamana na wanafunzi wake. 2 Ilipofika siku
ya Sabato, akaanza kufundisha katika sinagogi, na
wengi waliomsikia wakashangaa. Nao wakauliza, “Mtu
huyu ameyapata wapi mambo haya yote? Tazama
ni hekima ya namna gani hii aliyopewa? Tazama
matendo ya miujiza ayafanyayo kwa mikono yake! 3
Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu? Na ndugu
zake si Yakobo, Yose, Yuda na Simoni? Dada zake
wote si tuko nao hapa kwetu?” Nao wakachukizwa
sana kwa ajili yake, wakakataa kumwamini. 4 Isa
akawaambia, “Nabii hakosi heshima isipokuwa katika
mji wake mwenyewe, na miongoni mwa jamaa na

ndugu zake, na nyumbani mwake.” 5 Hakufanya
miujiza yoyote huko isipokuwa kuweka mikono yake
juu ya wagonjwa wachache na kuwaponya. 6
Naye akashangazwa sana kwa kutoamini kwao.
Kisha Isa akawa anaenda kutoka kijiji kimoja hadi
kingine akifundisha. 7 Akawaita wale kumi na wawili,
akawatuma wawili wawili, na kuwapa mamlaka kutoa
pepo wachafu. 8 Akawaagiza akisema, “Msichukue
chochote kwa ajili ya safari isipokuwa fimbo tu.
Msichukue mkate, wala mkoba, wala fedha kwenye
mikanda yenu. 9 Vaeni viatu, lakini msivae nguo ya
ziada. 10 Mkiingia kwenye nyumba yoyote, kaeni
humo hadi mtakapoondoka katika mji huo. 11 Kama
mahali popote hawatawakaribisha wala kuwasikiliza,
mtakapoondoka huko, kung’uteni mavumbi kutoka
miguu yenu ili kuwe ushuhuda dhidi yao.” 12 Kwa hiyo
wakaenenda na kuhubiri kwamba inawapasa watu
kutubu na kuacha dhambi. 13 Wakatoa pepo wachafu
wengi, wakawapaka wagonjwa wengi mafuta na
kuwaponya. 14 Mfalme Herode akasikia habari hizi,
kwa maana jina la Isa lilikuwa limejulikana sana. Watu
wengine walikuwa wakisema, “Yahya amefufuliwa
kutoka kwa wafu, ndiyo sababu nguvu za kutenda
miujiza zinafanya kazi ndani yake.” 15 Wengine
wakasema, “Yeye ni Ilya.” Nao wengine wakasema,
“Yeye ni nabii, kama mmoja wa manabii wa zamani.”
16 Lakini Herode aliposikia habari hizi, akasema,
“Huyo ni Yahya, niliyemkata kichwa, amefufuliwa
kutoka kwa wafu!” 17 Herode mwenyewe alikuwa
ameagiza kwamba Yahya akamatwe, afungwe na
kutiwa gerezani. Alifanya hivi kwa sababu ya Herodia,
mke wa Filipo, ndugu yake, ambaye Herode alikuwa
amemwoa. 18 Yahya alikuwa amemwambia Herode,
“Si halali kwako kuwa na mke wa ndugu yako.” 19 Kwa
hiyo Herodia alikuwa amemwekea Yahya kinyongo,
akataka kumuua. Lakini hakuweza, 20 kwa sababu
Herode alimwogopa Yahya akijua kwamba ni mtu
mwenye haki na mtakatifu, hivyo akamlinda. Herode
alifadhaika sana alipomsikia Yohana, lakini bado
alipenda kumsikiliza. 21 Hatimaye Herodia alipata
wakati mwafaka aliokuwa akiutafuta. Mfalme Herode
alifanya karamu kubwa wakati wa sikukuu ya kuzaliwa
kwake. Akawaalika maafisa wake wakuu, majemadari
wa jeshi na watu mashuhuri wa Galilaya. 22 Binti
Herodia alipoingia na kucheza, akamfurahisha Herode
pamoja na wageni wake walioalikwa chakulani.
Mfalme Herode akamwambia yule binti, “Niombe
kitu chochote utakacho, nami nitakupa.” 23 Tena
akamwahidi kwa kiapo, akamwambia, “Chochote
utakachoomba nitakupa, hata kama ni nusu ya
ufalme wangu.” 24 Yule binti akatoka nje, akaenda
kumuuliza mama yake, “Niombe nini?” Mama yake
akamjibu, “Omba kichwa cha Yahya.” 25 Yule binti
akarudi haraka kwa mfalme, akamwambia, “Nataka
unipe sasa hivi kichwa cha Yahya kwenye sinia.” 26
Mfalme akasikitika sana, lakini kwa sababu alikuwa
ameapa viapo mbele ya wageni wake, hakutaka
kumkatalia. 27 Mara mfalme akatuma askari mmoja
wa walinzi wake kukileta kichwa cha Yahya. Akaenda
na kumkata Yahya kichwa humo gerezani, 28
akakileta kichwa chake kwenye sinia na kumpa yule
msichana, naye yule msichana akampa mama yake.
29 Wanafunzi wa Yahya walipopata habari hizi, wakaja
na kuuchukua mwili wake, wakauzika kaburini. 30
Wale mitume wakakusanyika kwa Isa na kumpa
taarifa ya mambo yote waliyokuwa wamefanya na
kufundisha. 31 Basi kwa kuwa watu wengi mno
walikuwa wakija na kutoka, hata wakawa hawana
nafasi ya kula, Isa akawaambia wanafunzi wake,
“Twendeni peke yetu mahali pa faragha, mpate
kupumzika.” 32 Hivyo wakaondoka kwa mashua peke
yao, wakaenda mahali pasipo na watu. 33 Lakini
watu wengi waliowaona wakiondoka, wakawatambua,
nao wakaenda haraka kwa miguu kutoka miji yote,
nao wakatangulia kufika. 34 Isa alipofika kando ya
bahari, aliona kundi kubwa la watu, akawahurumia
kwa maana walikuwa kama kondoo wasiokuwa na
mchungaji. Kwa hiyo akaanza kuwafundisha mambo
mengi. 35 Mchana ulipokuwa umeendelea sana,
wanafunzi wake walienda kwake, wakamwambia,
“Mahali hapa ni nyikani, nazo saa zimeenda sana.
36 Waage watu ili waende mashambani na vijijini
jirani, wakajinunulie chakula.” 37 Lakini Isa akawajibu,
“Ninyi wapeni chakula.” Wakamwambia, “Je, twende
tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape watu
hawa wale?” 38 Akawauliza, “Kuna mikate mingapi?
Nendeni mkaangalie.” Walipokwisha kujua, wakarudi,
wakamwambia, “Kuna mikate mitano na samaki
wawili.” 39 Kisha Isa akawaamuru wawaketishe watu
makundi makundi kwenye majani, 40 nao wakaketi
kwenye vikundi vya watu mia mia, na wengine hamsini
hamsini. 41 Isa akaichukua ile mikate mitano na

wale samaki wawili, akainua macho yake akatazama
mbinguni, akavibariki na kuimega ile mikate. Kisha
akawapa wanafunzi wake ili wawagawie wale watu
wote. Pia akawagawia wote wale samaki wawili. 42
Watu wote wakala, wakashiba. 43 Nao wanafunzi
wake wakakusanya vipande vilivyosalia vya mikate
na samaki, wakajaza vikapu kumi na viwili. 44 Idadi
ya wanaume waliokula walikuwa elfu tano. 45 Mara
Isa akawaambia wanafunzi wake waingie kwenye
mashua wamtangulie kwenda Bethsaida, wakati yeye
alikuwa akiwaaga wale watu. 46 Baada ya kuwaaga,
akaenda mlimani kuomba. 47 Ilipofika jioni, ile mashua
ilikuwa imefika katikati ya bahari, na Isa alikuwa
peke yake katika nchi kavu. 48 Akawaona wanafunzi
wake wanahangaika na kupiga makasia kwa nguvu,
kwa sababu upepo ulikuwa wa mbisho. Wakati wa
zamu ya nne ya usiku, Isa akawaendea wanafunzi
wake, akiwa anatembea juu ya maji. Alikuwa karibu
kuwapita, 49 lakini walipomwona akitembea juu ya
maji, wakadhani ni mzimu. Wakapiga yowe, 50 kwa
sababu wote walipomwona waliogopa. Mara Isa
akasema nao, akawaambia, “Jipeni moyo! Ni mimi.
Msiogope!” 51 Akapanda ndani ya mashua nao,
na ule upepo ukakoma! Wakashangaa kabisa, 52
kwa kuwa walikuwa hawajaelewa kuhusu ile mikate.
Mioyo yao ilikuwa migumu. 53 Walipokwisha kuvuka,
wakafika nchi ya Genesareti, wakatia nanga. 54 Mara
waliposhuka kutoka mashua yao, watu wakamtambua
Isa. 55 Wakaenda katika vijiji vyote upesi, wakawabeba
wagonjwa kwenye mikeka ili kuwapeleka mahali
popote waliposikia kuwa Isa yupo. 56 Kila mahali Isa
alipoenda, iwe vijijini, mijini au mashambani, watu
waliwaweka wagonjwa wao masokoni. Wakamwomba
awaruhusu hao wagonjwa waguse japo upindo wa
vazi lake. Nao wote waliomgusa waliponywa.

7 Mafarisayo na baadhi ya walimu wa Torati
waliokuwa wametoka Yerusalemu wakakusanyika
mbele ya Isa. 2 Wakawaona baadhi ya wanafunzi
wake wakila chakula kwa mikono iliyo najisi, yaani
bila kunawa kama ilivyotakiwa na Torati ya Wayahudi.
3 (Kwa kuwa Mafarisayo na Wayahudi wote hawali
chakula pasipo kunawa kwa kufuata desturi za wazee
wao. 4 Wanapotoka sokoni hawawezi kula pasipo
kunawa. Pia kuna desturi zingine nyingi wanazofuata
kama vile jinsi ya kuosha vikombe, vyungu na vyombo
vya shaba.) 5 Hivyo, wale Mafarisayo na walimu
wa Torati wakamuuliza Isa, “Mbona wanafunzi wako
hawafuati desturi za wazee, na badala yake wanakula
kwa mikono najisi?” 6 Isa akawajibu, “Nabii Isaya
alisema ukweli alipotabiri juu yenu, ninyi wanafiki.
Kama ilivyoandikwa: “‘Watu hawa huniheshimu kwa
midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami. 7
Huniabudu bure, nayo mafundisho yao ni maagizo ya
wanadamu tu.’ 8 Ninyi mmeziacha amri za Mungu na
kushika desturi za watu.” 9 Naye akawaambia, “Ninyi
mnayo njia nzuri ya kukataa amri za Mungu ili mpate
kuyashika mapokeo yenu! 10 Kwa mfano, Musa
alisema, ‘Waheshimu baba yako na mama yako,’
na, ‘Yeyote amtukanaye baba yake au mama yake,
na auawe.’ 11 Lakini ninyi mwafundisha kwamba
mtu akimwambia baba yake au mama yake, ‘Kile
ambacho ningeweza kukusaidia ni Korbani’ (yaani
kimewekwa wakfu kwa Mungu), 12 basi hawajibiki
tena kumsaidia baba yake au mama yake. 13
Kwa njia hiyo ninyi mnabatilisha neno la Mungu
kwa mapokeo yenu mliyojiwekea. Nanyi mnafanya
mambo mengi ya aina hiyo.” 14 Isa akaita tena umati
ule wa watu, akawaambia, “Nisikilizeni nyote, na
mwelewe jambo hili. 15 Hakuna kitu kinachomwingia
mtu kimtiacho unajisi, lakini kile kimtokacho ndicho
kimtiacho unajisi. [ 16 Kama mtu yeyote ana masikio
ya kusikia na asikie.]” 17 Baada ya Isa kuacha ule
umati wa watu na kuingia ndani, wanafunzi wake
wakamuuliza maana ya mfano ule. 18 Akawajibu, “Je,
hata nanyi hamwelewi? Je, hamfahamu kwamba kitu
kimwingiacho mtu hakimtii unajisi? 19 Mtu akila kitu
hakiingii moyoni mwake bali tumboni, na baadaye
hutolewa nje ya mwili wake.” (Kwa kusema hivi,
Isa alivihalalisha vyakula vyote kuwa ni safi.) 20
Akaendelea kusema, “Kile kimtokacho mtu ndicho
kimtiacho unajisi. 21 Kwa maana kutoka ndani ya
moyo wa mtu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wizi,
uuaji, uzinzi, 22 tamaa mbaya, uovu, udanganyifu,
ufisadi, wivu, matukano, kiburi na upumbavu. 23
Maovu haya yote hutoka ndani ya mtu, nayo ndiyo
yamtiayo mtu unajisi.” 24 Ndipo Isa akaondoka hapo
akaenda sehemu za Tiro. Akaingia katika nyumba
moja, naye hakutaka mtu yeyote ajue kwamba yuko
humo. Lakini hakuweza kujificha. 25 Mara mwanamke
mmoja, ambaye binti yake mdogo alikuwa na pepo
mchafu, akaja na kumpigia magoti miguuni pake. 26
Basi huyo mwanamke alikuwa Myunani, aliyezaliwa

Foinike ya Siria. Akamsihi Isa amtoe binti yake huyo
pepo mchafu. **27** Isa akamwambia, “Waache watoto
washibe kwanza, kwa maana si vyema kuchukua
chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.” **28** Lakini
yule mwanamke akamjibu, “Bwana, hata mbwa walio
chini ya meza hula makombo ya chakula cha watoto.”
**29** Ndipo Isa akamjibu, “Kwa sababu ya jibu lako,
nenda zako nyumbani; yule pepo mchafu amemtoka
binti yako.” **30** Akaenda zake nyumbani akamkuta
binti yake amelala kitandani, yule pepo mchafu
akiwa amemtoka. **31** Kisha Isa akaondoka sehemu
za Tiro, akapita katikati ya Sidoni, hadi Bahari ya
Galilaya na kuingia eneo la Dekapoli. **32** Huko, watu
wakamletea Isa mtu mmoja kiziwi, ambaye pia alikuwa
na kigugumizi, wakamwomba aweke mkono wake juu
ya huyo mtu. **33** Isa akampeleka yule kiziwi kando,
mbali na watu, akatia vidole vyake masikioni mwa yule
mtu. Kisha akatema mate na kuugusa ulimi wa yule
mtu. **34** Ndipo Isa akatazama mbinguni, akashusha
pumzi kwa nguvu, akamwambia, “Efatha!” (yaani,
“Funguka!”) **35** Mara masikio yake yakafunguka na
ulimi wake ukaachiliwa, akaanza kuongea sawasawa.
**36** Isa akawaamuru wasimwambie mtu yeyote habari
hizi. Lakini kadiri alivyowakanya, ndivyo walivyozidi
kutangaza kwa bidii. **37** Walistaajabu mno. Wakasema,
“Amefanya mambo yote vizuri mno! Amewawezesha
viziwi wasikie na bubu waseme!”

**8** Katika siku hizo, umati mkubwa wa watu
walikusanyika tena. Kwa kuwa walikuwa hawana
chakula, Isa akawaita wanafunzi wake akawaambia,
**2** “Ninahurumia umati huu wa watu, kwa sababu sasa
wamekuwa nami kwa muda wa siku tatu na hawana
chakula. **3** Nikiwaaga waende nyumbani bila kula,
watazimia njiani kwa sababu baadhi yao wametoka
mbali.” **4** Wanafunzi wake wakamjibu, “Lakini hapa
nyikani tutapata wapi mikate ya kutosha kuwalisha?”
**5** Isa akawauliza, “Mna mikate mingapi?” Wakajibu,
“Tuna mikate saba.” **6** Akawaambia watu waketi
chini. Akaichukua ile mikate saba na kushukuru,
baadaye akaimega na kuwapa wanafunzi wake ili
wawagawie watu. Wanafunzi wake wakafanya hivyo.
**7** Walikuwa pia na visamaki vichache, Isa akavibariki,
akawaamuru wanafunzi wake wawagawie watu. **8**
Wale watu walikula na kutosheka. Baadaye wanafunzi
wakakusanya vipande vilivyosalia, wakajaza vikapu
saba. **9** Watu waliokula walikuwa wapata elfu nne.
Baada ya kuwaaga, **10** aliingia kwenye mashua
pamoja na wanafunzi wake, akaenda sehemu za
Dalmanutha. **11** Mafarisayo wakaja, wakaanza
kumhoji Isa. Ili kumtega, wakamwomba awaoneshe
ishara kutoka mbinguni. **12** Akahuzunika moyoni,
akawaambia, “Kwa nini kizazi hiki kinataka ishara?
Amin nawaambieni, hakitapewa ishara yoyote.” **13**
Kisha akawaacha, akarudi kwenye mashua, akavuka
hadi ng’ambo. **14** Wanafunzi walikuwa wamesahau
kuchukua mikate ya kutosha. Walikuwa na mkate
mmoja tu kwenye mashua. **15** Isa akawaonya:
“Jihadharini na chachu ya Mafarisayo na ya Herode.”
**16** Wakajadiliana wao kwa wao, na kusema, “Anasema
hivi kwa sababu hatukuleta mikate.” **17** Isa, akifahamu
majadiliano yao, akawauliza: “Mbona mnajadiliana
kuhusu kutokuwa na mikate? Je, bado hamtambui
wala hamwelewi? Je, mbona mioyo yenu ni migumu
kiasi hicho? **18** Je, mna macho lakini mnashindwa
kuona, na mna masikio lakini mnashindwa kusikia?
Je, hamkumbuki? **19** Nilipoimega ile mikate mitano
kwa watu elfu tano, mlikusanya vikapu vingapi
vilivyojaa mabaki?” Wakamjibu, “Kumi na viwili.”
**20** “Je, nilipoimega ile mikate saba kwa watu elfu
nne, mlikusanya vikapu vingapi vilivyojaa mabaki?”
Wakamjibu, “Saba.” **21** Ndipo akawauliza, “Je, bado
hamwelewi?” **22** Wakafika Bethsaida na baadhi
ya watu wakamleta mtu mmoja kipofu wakamsihi
Isa amguse. **23** Isa akamshika mkono huyo kipofu
akampeleka nje ya kijiji. Baada ya kuyatemea mate
macho ya yule kipofu na kumwekea mikono, Isa
akamuuliza, “Unaona chochote?” **24** Yule kipofu
akaangalia, akasema, “Ninaona watu, wanaonekana
kama miti inayotembea.” **25** Isa akamwekea tena
mikono machoni. Kisha macho yake yakafunguka,
kuona kwake kukarejea naye akaona kila kitu dhahiri.
**26** Isa akamtuma nyumbani mwake, akamwambia,
“Hata kijijini usiingie.” **27** Isa na wanafunzi wake
wakaelekea vijiji vya Kaisaria-Filipi. Walipokuwa njiani,
Isa akawauliza, “Watu husema mimi ni nani?” **28**
Wakamjibu, “Baadhi husema wewe ni Yahya, wengine
husema ni Ilya, na bado wengine husema wewe
ni mmoja wa manabii.” **29** Akawauliza, “Je, ninyi
mnasema mimi ni nani?” Petro akajibu, “Wewe ndiwe
Al-Masihi.” **30** Isa akawaonya wasimwambie mtu
yeyote habari zake. **31** Ndipo akaanza kuwafundisha
wanafunzi wake kuwa Mwana wa Adamu lazima

atapata mateso mengi na kukataliwa na wazee,
viongozi wa makuhani, na walimu wa Torati, na
kwamba itampasa auawe lakini baada ya siku tatu
afufuliwe. **32** Aliyasema haya waziwazi. Ndipo Petro
akamchukua kando na akaanza kumkemea. **33** Lakini
Isa akageuka na kuwaangalia wanafunzi wake, na
akamkemea Petro. Akasema, “Rudi nyuma yangu,
Shetani! Moyo wako hauwazi yaliyo ya Mungu,
bali ya wanadamu.” **34** Ndipo akawaita umati ule
wa watu pamoja na wanafunzi wake, akasema,
“Mtu yeyote akitaka kunifuata, ni lazima ajikane
mwenyewe, auchukue msalaba wake, anifuate. **35**
Kwa maana yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake
atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza maisha
yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili atayaokoa. **36**
Je, itamfaidi nini mtu kuupata ulimwengu wote, lakini
akayapoteza maisha yake? **37** Au mtu atatoa nini
badala ya nafsi yake? **38** Mtu yeyote akinionea aibu
mimi na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi
na dhambi, Mwana wa Adamu naye atamwonea aibu
wakati atakapokuja katika utukufu wa Baba yake
pamoja na malaika watakatifu.”

**9** Isa akaendelea kuwaambia, “Amin, nawaambia,
kuna watu waliosimama hapa ambao hawataonja
mauti kabla ya kuuona ufalme wa Mungu ukija kwa
nguvu.” **2** Baada ya siku sita, Isa akawachukua
Petro, Yakobo na Yohana, akawapeleka juu ya
mlima mrefu, mahali walipokuwa faraghani. Huko, Isa
akageuka sura mbele yao. **3** Mavazi yake yakawa
na weupe wa kuzima macho, meupe kuliko vile
mtu yeyote duniani angeweza kuyang’arisha. **4**
Musa na Ilya wakawatokea, wakawa wanazungumza
na Isa. **5** Petro akamwambia Isa, “Mwalimu, ni
vyema sisi tukae hapa. Turuhusu tujenge vibanda
vitatu: kimoja chako, kingine cha Musa na kingine
cha Ilya.” **6** Petro hakujua aseme nini kwa maana
yeye na wenzake walikuwa wameogopa sana. **7**
Ndipo pakatokea wingu, likawafunika, nayo sauti
kutoka lile wingu ikasema, “Huyu ni Mwanangu
mpendwa. Msikieni yeye.” **8** Mara walipotazama
huku na huku, hawakuona tena mtu mwingine yeyote
pamoja nao isipokuwa Isa. **9** Walipokuwa wakishuka
kutoka mlimani, Isa akawakataza wasimwambie
mtu yeyote mambo waliyoyaona, hadi Mwana wa
Adamu atakapokuwa amefufuka kutoka kwa wafu. **10**
Wakalihifadhi jambo hilo wao wenyewe, lakini wakawa
wanajiuliza, “Huku kufufuka kwa wafu maana yake
nini?” **11** Wakamuuliza, “Kwa nini walimu wa Torati
husema kwamba ni lazima Ilya aje kwanza?” **12** Isa
akawajibu, “Ni kweli, Ilya yuaja kwanza ili kutengeneza
mambo yote. Mbona basi imeandikwa kwamba Mwana
wa Adamu ni lazima ateseke sana na kudharauliwa?
**13** Lakini nawaambia, Ilya amekwisha kuja, nao
wakamtendea walivyopenda, kama ilivyoandikwa
kumhusu.” **14** Walipowafikia wale wanafunzi wengine,
wakawakuta wamezungukwa na umati mkubwa wa
watu na baadhi ya walimu wa Torati wakibishana nao.
**15** Mara wale watu walipomwona Isa, wakastaajabu
sana, wakamkimbilia ili kumsalimu. **16** Akawauliza
wanafunzi wake, “Mnabishana nao kuhusu nini?” **17**
Mtu mmoja miongoni mwa umati ule wa watu akajibu,
“Mwalimu, nilimleta kwako mwanangu ambaye ana
pepo mchafu anayemfanya asiweze kuongea. **18** Kila
mara huyo pepo mchafu ampagaapo mwanangu,
humwangusha chini na kumfanya atokwe povu
mdomoni na kusaga meno, kisha mwili wake hukauka.
Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe huyo pepo
mchafu, lakini hawakuweza.” **19** Isa akawaambia,
“Enyi kizazi kisichoamini! Nitakuwa pamoja nanyi
hadi lini? Nitawavumilia hadi lini? Mleteni mvulana
kwangu.” **20** Nao wakamleta yule mvulana. Yule
pepo mchafu alipomwona Isa, mara akamtia yule
mvulana kifafa, akaanguka, akagaagaa chini huku
akitokwa na povu kinywani. **21** Isa akamuuliza
baba yake, “Mwanao amekuwa katika hali hii tangu
lini?” Akamjibu, “Tangu utoto wake. **22** Mara kwa
mara huyo pepo mchafu amekuwa akimwangusha
kwenye moto au kwenye maji ili kumwangamiza.
Lakini kama unaweza kufanya jambo lolote, tafadhali
tuhurumie utusaidie.” **23** Isa akamwambia, “Ati, ‘Kama
unaweza kufanya jambo lolote’? Yote yawezekana
kwake yeye aaminiye.” **24** Mara baba yake yule
mvulana akapaza sauti akisema, “Ninaamini. Nisaidie
kutokuamini kwangu!” **25** Isa alipoona kwamba umati
wa watu wanakusanyika pamoja mbio, akamkemea
yule pepo mchafu, akimwambia, “Wewe pepo bubu
na kiziwi, nakuamuru umtoke, wala usimwingie tena!”
**26** Baada ya yule pepo mchafu kupiga kelele, akamtia
kifafa kwa nguvu, akamtoka. Yule mvulana alikuwa
kama maiti, hivyo watu wengi wakasema, “Amekufa.”
**27** Lakini Isa akamshika mkono, akamwinua, naye
akasimama. **28** Baada ya Isa kuingia ndani ya

nyumba, wanafunzi wake wakamuuliza wakiwa
peke yao, “Mbona sisi hatukuweza kumtoa huyo
pepo mchafu?” 29 Isa akawajibu, “Pepo aina
hii haiwezi kutoka isipokuwa kwa kuomba [na
kufunga].” 30 Wakaondoka huko, wakapitia Galilaya.
Isa hakutaka mtu yeyote afahamu mahali walipo,
31 kwa maana alikuwa anawafundisha wanafunzi
wake. Akawaambia, “Mwana wa Adamu atasalitiwa
na kutiwa mikononi mwa watu. Nao watamuua, lakini
siku tatu baada ya kuuawa atafufuka.” 32 Lakini
wao hawakuelewa kile alimaanisha, nao waliogopa
kumuuliza maana yake. 33 Basi wakafika Kapernaumu
na baada ya kuingia nyumbani akawauliza, “Mlikuwa
mnabishana nini kule njiani?” 34 Lakini hawakumjibu,
kwa sababu njiani walikuwa wakibishana kuhusu nani
miongoni mwao alikuwa mkuu zaidi ya wote. 35 Akaketi
chini, akawaita wote kumi na wawili, akawaambia:
“Kama mtu yeyote akitaka kuwa wa kwanza, hana
budi kuwa wa mwisho na mtumishi wa wote.” 36 Kisha
akamchukua mtoto mdogo, akamsimamisha katikati
yao. Akamkumbatia, akawaambia, 37 “Mtu yeyote
amkaribishaye mmoja wa hawa watoto wadogo kwa
Jina langu, anikaribisha mimi. Naye anikaribishaye
mimi, amkaribisha Baba yangu aliyenituma.” 38
Yohana akamwambia, “Mwalimu, tumemwona mtu
akitoa pepo wachafu kwa jina lako, nasi tukamkataza,
kwa sababu yeye si mmoja wetu.” 39 Isa akasema,
“Msimkataze, kwa kuwa hakuna yeyote atendaye
miujiza kwa Jina langu ambaye baada ya kitambo
kidogo aweza kunena lolote baya dhidi yangu. 40 Kwa
maana yeyote asiye kinyume chetu, yuko upande
wetu. 41 Amin, nawaambia, yeyote awapaye ninyi
kikombe cha maji kwa Jina langu kwa sababu ninyi ni
mali ya Al-Masihi, hakika hataikosa thawabu yake. 42
“Mtu yeyote akimsababisha mmoja wa hawa wadogo
wanaoniamini kutenda dhambi, ingekuwa bora kwake
afungiwe jiwe kubwa la kusagia shingoni mwake, na
kutoswa baharini. 43 Mkono wako ukikusababisha
kutenda dhambi, ukate. Ni afadhali kwako kuingia
katika uzima ukiwa na mkono mmoja, kuliko kuwa
na mikono miwili lakini ukaingia Jehanamu, mahali
ambako moto hauzimiki. [ **(Geenna g1067)** 44 Ni mahali
ambako funza wao hawafi wala moto wao hauzimiki.]
45 Mguu wako ukikusababisha kutenda dhambi, ukate.
Ni afadhali kwako kuingia katika uzima ukiwa kiwete,
kuliko kuwa na miguu miwili lakini ukaingia Jehanamu.
[ **(Geenna g1067)** 46 Ni mahali ambako funza wao
hawafi wala moto wao hauzimiki.] 47 Nalo jicho lako
likikusababisha kutenda dhambi, ling’oe. Ni afadhali
kwako kuingia katika ufalme wa Mungu ukiwa na jicho
moja, kuliko kuwa na macho mawili lakini ukatupwa
Jehanamu. **(Geenna g1067)** 48 Ni mahali ambako funza
wao hawafi, wala moto wao hauzimiki. 49 Kila mmoja
atatiwa chumvi kwa moto. 50 “Chumvi ni nzuri, lakini
ikipoteza ladha yake utaifanyaje ili iweze kukolea
tena? Mwe na chumvi ndani yenu, mkaishi kwa
amani, kila mmoja na mwenzake.”

**10** Isa akaondoka huko, akavuka Mto Yordani,
akaenda sehemu za Yudea. Umati mkubwa wa
watu wakaenda kwake tena, naye akawafundisha,
kama ilivyokuwa desturi yake. 2 Baadhi ya Mafarisayo
wakaja ili kumjaribu kwa kumuuliza, “Je, ni halali
mtu kumwacha mke wake?” 3 Isa akawajibu, “Je,
Musa aliwaamuru nini?” 4 Wakajibu, “Musa aliruhusu
kwamba mume anaweza kumwandikia mkewe hati
ya talaka na kumwacha.” 5 Isa akawaambia, “Musa
aliwaandikia sheria hiyo kwa sababu ya ugumu wa
mioyo yenu. 6 Lakini tangu mwanzo wa uumbaji,
‘Mungu aliwaumba mwanaume na mwanamke’. 7
‘Kwa sababu hii mwanaume atamwacha baba yake na
mama yake na kuambatana na mkewe, 8 na hao wawili
watakuwa mwili mmoja.’ Kwa hiyo hawatakuwa wawili
tena, bali mwili mmoja. 9 Basi, alichokiunganisha
Mungu, mwanadamu asikitenganishe.” 10 Walipokuwa
tena ndani ya nyumba, wanafunzi wake wakamuuliza
kuhusu jambo hili. 11 Akawajibu, “Mtu yeyote
amwachaye mkewe na kuoa mke mwingine, anazini
naye. 12 Naye mwanamke amwachaye mumewe
na kuolewa na mume mwingine, anazini.” 13
Watu walikuwa wakimletea Isa watoto wadogo ili
awaguse, lakini wanafunzi wake wakawakemea.
14 Isa alipoona yaliyokuwa yakitukia, akachukizwa.
Akawaambia wanafunzi wake, “Waacheni watoto
wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana
ufalme wa Mungu ni wa wale walio kama hawa.
15 Amin, nawaambia, mtu yeyote asiyeupokea
ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo, hatauingia
kamwe.” 16 Akawachukua watoto mikononi mwake,
akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao,
akawabariki. 17 Isa alipokuwa anaondoka, mtu
mmoja akamkimbilia, akapiga magoti mbele yake,
akamuuliza, “Mwalimu mwema, nifanye nini ili

niurithi uzima wa milele?” (aiōnios g166) **18** Isa
akamwambia, “Mbona unaniita mwema? Hakuna
yeyote aliye mwema ila Mungu peke yake. **19**
Unazijua amri: ‘Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie
uongo, usidanganye, waheshimu baba yako na
mama yako.’” **20** Akamjibu, “Mwalimu, amri hizi zote
nimezishika tangu nikiwa mtoto.” **21** Isa akamtazama
na kumpenda, akamwambia, “Umepungukiwa na
kitu kimoja. Nenda ukauze kila kitu ulicho nacho
uwape maskini hizo fedha, nawe utakuwa na hazina
mbinguni. Kisha njoo, unifuate.” **22** Yule mtu aliposikia
hayo, akasikitika sana. Akaondoka kwa huzuni kwa
sababu alikuwa na mali nyingi. **23** Isa akatazama
pande zote, akawaambia wanafunzi wake, “Itakuwa
vigumu sana kwa wenye mali kuingia katika ufalme
wa Mungu!” **24** Wanafunzi wake wakashangazwa
sana na maneno hayo. Lakini Isa akawaambia tena,
“Wanangu, tazama jinsi ilivyo vigumu kwa wale
wanaotumainia mali kuingia katika ufalme wa Mungu.
**25** Ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu
la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika ufalme wa
Mungu.” **26** Wanafunzi wake wakashangaa sana.
Wakaulizana wao kwa wao, “Ni nani basi awezaye
kuokoka?” **27** Isa akawatazama, akawaambia, “Kwa
mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa
Mungu sivyo. Mambo yote yanawezekana kwa
Mungu.” **28** Ndipo Petro akamjibu, “Tazama, tumeacha
kila kitu na kukufuata wewe!” **29** Isa akasema,
“Amin, nawaambia, hakuna mtu yeyote aliyeacha
nyumba, ndugu wa kiume au wa kike, au mama au
baba, au watoto au mashamba kwa ajili yangu na
kwa ajili ya Injili, **30** ambaye hatalipwa mara mia
katika ulimwengu huu: nyumba, ndugu wa kiume
na wa kike, mama na baba na watoto, mashamba
pamoja na mateso, kisha uzima wa milele katika
ulimwengu ujao. (aiōn g165, aiōnios g166) **31** Lakini
wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho, na
wa mwisho watakuwa wa kwanza.” **32** Walikuwa
njiani wakipanda kwenda Yerusalemu, na Isa alikuwa
amewatangulia. Wanafunzi wake walishangaa, nao
watu waliowafuata walijawa na hofu. Isa akawachukua
tena wale wanafunzi wake kumi na wawili kando na
kuwaambia yatakayompata. **33** Akasema, “Tunapanda
kwenda Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atasalitiwa
kwa viongozi wa makuhani na walimu wa Torati. Wao
watamhukumu kifo na kumtia mikononi mwa watu
wa Mataifa, **34** ambao watamdhihaki na kumtemea
mate, watampiga na kumuua. Siku tatu baadaye
atafufuka.” **35** Kisha Yakobo na Yohana, wana wa
Zebedayo, wakaja kwake na kumwambia, “Mwalimu,
tunataka utufanyie lolote tutakalokuomba.” **36** Naye
akawaambia, “Je, mwataka niwafanyie jambo gani?”
**37** Wakamwambia, “Tupe kukaa mmoja upande wako
wa kuume na mwingine upande wako wa kushoto
katika utukufu wako.” **38** Lakini Isa akawaambia,
“Ninyi hamjui mnaloliomba. Je, mnaweza kukinywea
kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo
nibatizwao mimi?” **39** Wakajibu, “Tunaweza.” Kisha
Isa akawaambia, “Kikombe nikinyweacho mtakinywea
na ubatizo nibatizwao mtabatizwa, **40** lakini kuketi
mkono wangu wa kuume au wa kushoto si juu
yangu mimi kuwapa. Nafasi hizi ni kwa ajili ya wale
walioandaliwa.” **41** Wale wanafunzi wengine kumi
waliposikia hayo, wakaanza kuwakasirikia Yakobo
na Yohana. **42** Lakini Isa akawaita wote pamoja na
kuwaambia, “Mnafahamu kuwa wale wanaodhaniwa
kuwa watawala wa watu wa Mataifa huwatawala watu
kwa nguvu, nao wenye vyeo huonesha mamlaka yao.
**43** Lakini isiwe hivyo kwenu. Badala yake, yeyote
anayetaka kuwa mkuu miongoni mwenu hana budi
kuwa mtumishi wenu, **44** na yeyote anayetaka kuwa
wa kwanza, hana budi kuwa mtumwa wa wote. **45** Kwa
kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa,
bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili
ya wengi.” **46** Kisha wakafika Yeriko. Isa alipokuwa
akiondoka mjini na wanafunzi wake pamoja na umati
mkubwa wa watu, kipofu mmoja, jina lake Bartimayo
(maana yake “mwana wa Timayo”), alikuwa ameketi
kando ya njia akiomba msaada. **47** Aliposikia kuwa
ni Isa Al-Nasiri aliyekuwa anapita, akaanza kupaza
sauti akisema, “Isa, Mwana wa Daudi, nihurumie!”
**48** Watu wengi wakamkemea, wakamwambia akae
kimya, lakini yeye akazidi kupaza sauti, akisema,
“Mwana wa Daudi, nihurumie!” **49** Isa akasimama na
kusema, “Mwiteni.” Hivyo wakamwita yule mtu kipofu,
wakamwambia, “Jipe moyo! Inuka, anakuita.” **50** Akiwa
analivua lile joho lake, alisimama na kumwendea
Isa. **51** Isa akamuuliza, “Unataka nikufanyie nini?”
Yule kipofu akajibu, “Mwalimu, nataka kuona.” **52** Isa
akamwambia, “Nenda zako, imani yako imekuponya.”
Mara akapata kuona, akamfuata Isa njiani.

**11** Walipokaribia Yerusalemu, wakafika Bethfage
na Bethania katika Mlima wa Mizeituni. Isa
akawatuma wawili wa wanafunzi wake, **2** akawaambia,
“Nendeni katika kijiji kilicho mbele yenu. Na
hapo mtakapoingia kijijini, mtampata mwana-punda
amefungwa hapo, ambaye hajapandwa na mtu
bado. Mfungueni, mkamlete hapa. **3** Mtu yeyote
akiwauliza, ‘Mbona mnamfungua?’ mwambieni,
‘Bwana anamhitaji, na atamrudisha hapa baada ya
muda mfupi.’” **4** Wakaenda, wakampata mwana-punda
amefungwa kando ya barabara, karibu na mlango
wa nyumba. **5** Walipokuwa wanamfungua, watu
waliokuwa wamesimama karibu wakawauliza, “Kwa
nini mnamfungua huyo mwana-punda?” **6** Wakawajibu
kama vile Isa alivyokuwa amewaagiza, nao wale
watu wakawaruhusu. **7** Kisha wakamleta huyo
mwana-punda kwa Isa na kutandika mavazi yao juu
yake, naye akampanda. **8** Watu wengi wakatandaza
mavazi yao barabarani, na wengine wakatandaza
matawi waliyokuwa wamekata mashambani. **9**
Kisha wale waliokuwa wametangulia mbele na
wale waliokuwa wakifuata nyuma wakapaza sauti,
wakisema, “Hosana!” “Amebarikiwa yeye ajaye kwa
Jina la Mwenyezi Mungu!” **10** “Umebarikiwa ufalme
unaokuja wa baba yetu Daudi!” “Hosana kwake yeye
aliye juu!” **11** Isa akaingia Yerusalemu na kwenda
Hekaluni. Akaangalia kila kitu kilichokuwamo, lakini
kwa kuwa ilishakuwa jioni, akaenda zake Bethania
pamoja na wale kumi na wawili. **12** Kesho yake
walipokuwa wakitoka Bethania, Isa alikuwa na njaa. **13**
Akauona mtini kwa mbali, naye akaenda ili aone kama
ulikuwa na matunda. Alipoufikia, akakuta una majani
tu, kwa kuwa hayakuwa majira ya tini. **14** Akauambia
ule mti, “Tangu leo mtu yeyote asile kamwe matunda
kutoka kwako.” Wanafunzi wake walimsikia akisema
hayo. **(aiōn g165)** **15** Walipofika Yerusalemu, Isa akaingia
katika eneo la Hekalu, akaanza kuwafukuza wale
waliokuwa wakinunua na kuuza humo. Akazipindua
meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha, na
pia viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa, **16** wala
hakumruhusu mtu yeyote kuchukua bidhaa kupitia
ukumbi wa Hekalu. **17** Naye alipokuwa akiwafundisha,
akasema, “Je, haikuandikwa kuwa: “‘Nyumba yangu
itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote’? Lakini
ninyi mmeifanya kuwa ‘pango la wanyang’anyi.’” **18**
Viongozi wa makuhani na walimu wa Torati wakapata
habari hizi, nao wakaanza kutafuta njia ya kumuua,
kwa kuwa walikuwa wakimwogopa, kwa sababu umati
wote walishangazwa na mafundisho yake. **19** Ilipofika
jioni, Isa na wanafunzi wake wakatoka nje ya mji. **20**
Kesho yake asubuhi walipokuwa wakipita, wakauona
ule mtini umenyauka kutoka juu hadi kwenye mizizi
yake. **21** Petro akakumbuka na kumwambia Isa,
“Mwalimu, tazama! Ule mtini ulioulaani umenyauka!”
**22** Isa akawajibu, “Mwaminini Mungu. **23** Amin,
nawaambia, mtu yeyote atakayeuambia mlima huu,
‘Ng’oka ukatupwe baharini,’ wala asione shaka moyoni
mwake, bali aamini kwamba hayo asemayo yametukia,
atatimiziwa. **24** Kwa sababu hiyo nawaambia,
yoyote mtakayoyaomba mkisali, aminini kwamba
mmeyapokea, nayo yatakuwa yenu. **25** Nanyi kila
msimamapo kusali, sameheni mkiwa na neno na mtu,
ili naye Baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi
makosa yenu. [ **26** Lakini kama ninyi msiposamehe,
wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi
makosa yenu.]” **27** Wakafika tena Yerusalemu, na
Isa alipokuwa akitembea Hekaluni, viongozi wa
makuhani, walimu wa Torati pamoja na wazee wa
watu wakamjia. **28** Wakamuuliza, “Unafanya mambo
haya kwa mamlaka gani? Na ni nani aliyekupa
mamlaka ya kufanya hayo?” **29** Isa akawajibu,
“Nitawauliza swali moja. Nijibuni, nami nitawaambia
ni kwa mamlaka gani ninafanya mambo haya. **30**
Je, ubatizo wa Yahya ulitoka mbinguni au kwa
wanadamu? Niambieni!” **31** Wakahojiana wao kwa wao
na kusema, “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atatuuliza,
‘Mbona hamkumwamini?’ **32** Lakini tukisema, ‘Ulitoka
kwa wanadamu’” (waliwaogopa watu, kwa sababu
kila mtu aliamini kwamba Yahya alikuwa nabii wa
kweli); **33** kwa hiyo wakamjibu Isa, “Hatujui.” Naye
Isa akawaambia, “Wala mimi sitawaambia ni kwa
mamlaka gani ninatenda mambo haya.”

**12** Isa akaanza kusema nao kwa mifano,
akawaambia: “Mtu mmoja alipanda shamba la
mizabibu. Akajenga ukuta kulizunguka, na ndani yake
akachimba shimo la shinikizo la kukamulia zabibu,
na akajenga mnara wa ulinzi. Kisha akalikodisha
shamba hilo la mizabibu kwa wakulima fulani, kisha
akasafiri hadi nchi nyingine. **2** Wakati wa mavuno
ulipofika, mwenye shamba akamtuma mtumishi wake
kwa hao wapangaji ili kuchukua sehemu yake ya
mavuno ya shamba la mizabibu kutoka kwa hao

wapangaji. **3** Lakini wale wakulima walimkamata yule
mtumishi, wakampiga, wakamfukuza mikono mitupu.
**4** Kisha yule mwenye shamba akamtuma mtumishi
mwingine kwao; nao wale wakulima wakampiga
kichwani na kumfanyia mambo ya aibu. **5** Kisha
akamtuma mtumishi mwingine, naye huyo wakamuua.
Akawatuma wengine wengi; baadhi yao wakawapiga,
na wengine wakawaua. **6** "Mwenye shamba alikuwa
bado na mmoja wa kumtuma, mwanawe aliyempenda.
Hatimaye akamtuma akisema, 'Watamheshimu
mwanangu.' **7** "Lakini wale wapangaji wakasemezana
pamoja, 'Huyu ndiye mrithi. Njooni tumuue, nao urithi
utakuwa wetu.' **8** Hivyo wakamchukua na kumuua,
wakamtupa nje ya lile shamba la mizabibu. **9** "Sasa
basi yule mwenye shamba atafanya nini? Atakuja na
kuwaua hao wapangaji, kisha atawapa wapangaji
wengine hilo shamba la mizabibu. **10** Je, hamjasoma
andiko hili: "'Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe
kuu la pembeni; **11** Mwenyezi Mungu ndiye alitenda
jambo hili, nalo ni la kushangaza machoni petu'?"
**12** Walipotambua kuwa amesema mfano huo kwa
ajili yao, wakataka kumkamata, lakini wakaogopa
umati ule wa watu. Wakamwacha, wakaenda zao.
**13** Baadaye wakawatuma baadhi ya Mafarisayo na
Maherode ili wamtege Isa katika maneno yake.
**14** Wakamjia, wakamwambia, "Mwalimu, tunajua
kwamba wewe ni mtu mwadilifu. Wewe huyumbishwi
na wanadamu, kwa kuwa huna upendeleo. Lakini
wewe huifundisha njia ya Mungu katika kweli. Je,
ni halali kulipa kodi kwa Kaisari, au la? **15** Je,
tulipe kodi au tusilipe?" Lakini Isa alijua unafiki wao.
Akawauliza, "Mbona mnajaribu kunitega? Nileteeni
hiyo dinari niione." **16** Wakamletea hiyo sarafu. Naye
akawauliza, "Sura hii ni ya nani? Na maandishi
haya ni ya nani?" Wakamjibu, "Ni vya Kaisari." **17**
Ndipo Isa akawaambia, "Mpeni Kaisari kilicho cha
Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu." Nao
wakamstaajabia sana. **18** Kisha Masadukayo, wale
wasemao kuwa hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia
Isa, **19** wakasema, "Mwalimu, Musa alituandikia kuwa
kama ndugu wa mtu akifa na kumwacha mkewe bila
mtoto, basi huyo mtu inampasa amwoe huyo mjane
ili amzalie ndugu yake watoto. **20** Basi kulikuwa na
ndugu saba. Yule wa kwanza akaoa mke, naye akafa
bila kuacha mtoto yeyote. **21** Wa pili akamwoa yule
mjane, lakini naye akafa bila kuacha mtoto yeyote.
Ikawa vivyo hivyo kwa yule wa tatu. **22** Hakuna hata
mmoja wa hao ndugu saba aliyeacha mtoto. Hatimaye
yule mwanamke naye akafa. **23** Basi, wakati wa
ufufuo yeye atakuwa mke wa nani, maana aliolewa na
ndugu wote saba?" **24** Isa akawajibu, "Je, hampotei
kwa sababu hamfahamu Maandiko wala uweza wa
Mungu? **25** Wafu watakapofufuka, hawataoa wala
kuolewa, bali watakuwa kama malaika wa mbinguni.
**26** Basi kuhusu wafu kufufuliwa, je hamjasoma katika
Kitabu cha Musa jinsi Mungu alivyosema na Musa
kutoka kile kichaka akisema, 'Mimi ni Mungu wa
Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo'?
**27** Yeye si Mungu wa wafu, bali ni Mungu wa walio
hai. Kwa hiyo mmekosea kabisa." **28** Mwalimu mmoja
wa sheria akaja, akawasikia wakijadiliana. Akiona
kwamba Isa amewajibu vyema, naye akamuuliza,
"Katika amri zote, ni ipi iliyo kuu?" **29** Isa akajibu,
"Amri iliyo kuu ndiyo hii: 'Sikia ee Israeli. Mwenyezi
Mungu, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. **30** Mpende
Mwenyezi Mungu, Mungu wako, kwa moyo wako
wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote, na
kwa nguvu zako zote.' **31** Ya pili ndiyo hii: 'Mpende
jirani yako kama nafsi yako.' Hakuna amri nyingine
iliyo kuu kuliko hizi." **32** Yule mwalimu wa Torati
akamwambia Isa, "Mwalimu, umejibu vyema kwamba
Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye.
**33** Kumpenda Mungu kwa moyo wako wote, na kwa
ufahamu wako wote, na kwa nguvu zako zote, na
kumpenda jirani kama mtu anavyojipenda mwenyewe
ni bora kuliko kutoa sadaka za kuteketezwa na
dhabihu zote." **34** Isa alipoona kwamba amejibu kwa
busara, akamwambia, "Wewe huko mbali na ufalme
wa Mungu." Tangu wakati huo, hakuna mtu yeyote
aliyethubutu kumuuliza maswali tena. **35** Isa alipokuwa
akifundisha Hekaluni, akauliza, "Imekuwaje walimu
wa Torati wanasema kwamba Al-Masihi ni Mwana wa
Daudi? **36** Kwa maana Daudi mwenyewe, akinena
kwa kuongozwa na Roho wa Mungu, alisema: "'Bwana
alimwambia Bwana wangu: "Keti mkono wangu wa
kuume, hadi nitakapowaweka adui zako chini ya
miguu yako."' **37** Kwa hiyo Daudi mwenyewe anamwita
'Bwana.' Awezaje basi yeye kuwa mwanawe?" Umati
ule wote wa watu wakamsikiliza kwa furaha. **38**
Alipokuwa akifundisha, Isa alisema, "Jihadharini na
walimu wa Torati. Wao hupenda kutembea wakiwa
wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa kwa heshima

masokoni. **39** Pia wao hupenda kukaa kwenye viti
vya mbele katika masinagogi, na kupewa nafasi za
heshima katika karamu. **40** Wao hula nyumba za
wajane, na ili waonekane kuwa wema wanasali sala
ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu iliyo kuu
sana." **41** Kisha Isa akaketi mkabala na sehemu
ambapo sadaka zilikuwa zinawekwa na kuangalia
umati wa watu wakiweka fedha zao kwenye sanduku
la hazina ya Hekalu. Matajiri wengi wakaweka kiasi
kikubwa cha fedha. **42** Lakini mjane mmoja maskini
akaja na kuweka sarafu mbili ndogo za shaba zenye
thamani ya senti mbili. **43** Isa akawaita wanafunzi
wake, akawaambia, "Amin, nawaambia, huyu mjane
maskini ameweka katika sanduku la hazina zaidi
ya watu wengine wote. **44** Wengine wote wametoa
kutokana na ziada ya mali yao. Lakini huyu mjane
ametoa kutokana na umaskini wake, akaweka kila
kitu alichokuwa nacho, hata kile alichohitaji ili kuishi."

**13** Isa alipokuwa akitoka Hekaluni, mmoja wa
wanafunzi wake akamwambia, "Mwalimu!
Tazama jinsi mawe haya yalivyo makubwa, na
majengo haya yalivyo mazuri!" **2** Ndipo Isa akajibu
akasema, "Je, unayaona majengo haya yalivyo
makubwa? Hakuna hata jiwe moja litakalobaki
juu ya jingine, bali yote yatabomolewa." **3** Isa
alipokuwa ameketi kwenye Mlima wa Mizeituni
mkabala na Hekalu, Petro, Yakobo, Yohana na
Andrea wakamuuliza faraghani, **4** "Tafadhali tuambie,
mambo haya yatatukia lini? Nayo dalili ya kuwa
hayo yote yanakaribia kutimia itakuwa gani?" **5** Isa
akawaambia: "Jihadharini mtu yeyote asiwadanganye.
**6** Wengi watakuja kwa Jina langu wakidai, 'Mimi
ndiye,' nao watawadanganya wengi. **7** Msikiapo
habari za vita na uvumi wa vita, msiwe na hofu.
Mambo haya hayana budi kutukia, lakini ule mwisho
bado. **8** Taifa litainuka dhidi ya taifa na ufalme
dhidi ya ufalme. Kutakuwa na mitetemeko ya ardhi
sehemu mbalimbali na njaa. Haya yatakuwa ndio
mwanzo wa uchungu. **9** "Lakini ninyi jihadharini.
Kwa maana watawapeleka katika mabaraza yao na
kupigwa mijeledi katika masinagogi. Mtashtakiwa
mbele ya watawala na wafalme kwa ajili yangu, ili
kuwa ushuhuda kwao. **10** Nayo Injili lazima ihubiriwe
kwanza kwa mataifa yote. **11** Mtakapokamatwa na
kushtakiwa, msisumbuke awali kuhusu mtakalosema.
Semeni tu lolote mtakalopewa wakati huo, kwa kuwa
si ninyi mtakaokuwa mkinena, bali ni Roho Mtakatifu
wa Mungu. **12** "Ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe,
naye baba atamsaliti mtoto wake. Watoto nao wataasi
dhidi ya wazazi wao na kusababisha wauawe. **13**
Watu wote watawachukia kwa ajili ya Jina langu.
Lakini yule atakayevumilia hadi mwisho ataokolewa.
**14** "Mtakapoona 'chukizo la uharibifu' limesimama
mahali pasipolipasa (asomaye na afahamu), basi
wale walio Yudea wakimbilie milimani. **15** Yeyote
aliye juu ya dari ya nyumba asishuke au kuingia
ndani ili kuchukua chochote. **16** Aliye shambani
asirudi nyumbani kuchukua vazi lake. **17** Ole wao
wenye mimba na wale wanaonyonyesha watoto siku
hizo! **18** Ombeni mambo haya yasitokee wakati
wa baridi. **19** Kwa maana siku hizo zitakuwa za
dhiki kuu ambayo haijapata kuwa tangu mwanzo,
hapo Mungu alipoumba ulimwengu, hadi leo, na
wala haitakuwa tena kamwe. **20** "Kama Mwenyezi
Mungu hangefupisha siku hizo, kamwe hakuna mtu
yeyote angeokoka. Lakini kwa ajili ya wateule, wale
aliowachagua, amezifupisha siku hizo. **21** Wakati
huo mtu yeyote akiwaambia, 'Tazama, Al-Masihi
huyu hapa!' au, 'Tazama, yuko kule,' msisadiki. **22**
Kwa maana watatokea masihi wa uongo na manabii
wa uongo, nao watafanya ishara na maajabu ili
kuwapotosha, ikiwezekana, hata wale wateule. **23**
Hivyo jihadharini. Nimekwisha kuwaambia mambo
haya yote mapema kabla hayajatukia. **24** "Lakini katika
siku hizo, baada ya hiyo dhiki, "'jua litatiwa giza nao
mwezi hautatoa nuru yake; **25** nazo nyota zitaanguka
kutoka angani, na nguvu za anga zitatikisika.' **26**
"Ndipo watu wote watakapomwona Mwana wa Adamu
akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu. **27** Naye
atawatuma malaika wake wawakusanye wateule
wake kutoka pande zote nne za dunia, kutoka
miisho ya dunia hadi miisho ya mbingu. **28** "Basi
jifunzeni somo hili kutokana na mtini: Matawi yake
yanapoanza kuchipua na kutoa majani, mnatambua
kwamba wakati wa kiangazi umekaribia. **29** Vivyo
hivyo, myaonapo mambo haya yakitukia, mnatambua
kwamba wakati u karibu, hata malangoni. **30** Amin,
nawaambia, kizazi hiki hakitapita hadi mambo haya
yote yawe yametimia. **31** Mbingu na nchi zitapita,
lakini maneno yangu hayatapita kamwe. **32** "Kwa
habari ya siku ile na saa hakuna yeyote ajuaye,
hata malaika walio mbinguni wala Mwana, ila Baba

peke yake. 33 Jihadharini! Kesheni! Kwa maana
hamjui wakati ule utakapowadia. 34 Ni kama mtu
anayesafiri. Anaiacha nyumba yake na kuwaachia
watumishi wake kuiangalia, kila mtu na kazi yake,
kisha akamwamuru yule bawabu aliye mlangoni
akeshe. 35 “Basi kesheni, kwa sababu hamjui ni
lini mwenye nyumba atakaporudi: iwapo ni jioni, au
ni usiku wa manane, au alfajiri awikapo jogoo, au
mapambazuko, 36 akija ghafula asije akawakuta
mmelala. 37 Lile ninalowaambia ninyi, nawaambia
watu wote: ‘Kesheni!’”

**14** Zilikuwa zimebaki siku mbili tu kabla ya Sikukuu
ya Pasaka, na Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa
Chachu. Viongozi wa makuhani na walimu wa Torati
walikuwa wakitafuta njia ya kumkamata Isa kwa
hila na kumuua. 2 Lakini walisema, “Tusilifanye
jambo hili wakati wa Sikukuu, maana watu wanaweza
wakafanya ghasia.” 3 Isa alikuwa Bethania nyumbani
mwa Simoni aliyekuwa na ukoma. Alipokuwa ameketi
mezani akila chakula cha jioni, mwanamke mmoja
aliingia akiwa na chupa ya marhamu yenye manukato
ya nardo safi ya thamani kubwa. Akaivunja hiyo
chupa, akamiminia hayo manukato kichwani mwa
Isa. 4 Baadhi ya watu waliokuwa pale walikasirika na
wakasemezana, “Upotevu huu wote wa manukato
ni wa nini? 5 Manukato haya yangeuzwa kwa
zaidi ya dinari mia tatu, na fedha hizo wakapewa
maskini.” Wakamkemea vikali huyo mwanamke. 6
Lakini Isa akawaambia, “Mbona mnamsumbua huyu
mwanamke? Mwacheni! Yeye amenitendea jambo
zuri sana. 7 Maskini mtakuwa nao siku zote na
mnaweza kuwasaidia wakati wowote mnaotaka. Lakini
mimi hamtakuwa nami siku zote. 8 Huyu mwanamke
amenitendea lile aliloweza. Ameumiminia mwili wangu
manukato ili kuniandaa kwa maziko yangu. 9 Amin,
nawaambia, mahali popote ulimwenguni ambapo Injili
itahubiriwa, jambo hili alilolitenda huyu mwanamke
litatajwa pia kwa ukumbusho wake.” 10 Kisha Yuda
Iskariote, mmoja wa wale wanafunzi kumi na wawili,
akaenda kwa viongozi wa makuhani ili kumsaliti
Isa kwao. 11 Walifurahi sana kusikia jambo hili na
wakaahidi kumpa fedha. Hivyo yeye akawa anatafuta
wakati uliofaa wa kumsaliti. 12 Siku ya kwanza ya
Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, siku ambayo
kwa desturi mwana-kondoo wa Pasaka huchinjwa,
wanafunzi wa Isa wakamuuliza, “Unataka twende
wapi ili tukuandalie mahali pa kula Pasaka?” 13
Basi akawatuma wawili miongoni mwa wanafunzi
wake, akawaambia, “Nendeni mjini. Huko mtakutana
na mwanaume amebeba mtungi wa maji. Mfuateni.
14 Mwambieni mwenye nyumba ile atakayoingia,
‘Mwalimu anauliza: Kiko wapi chumba changu cha
wageni, ambamo mimi na wanafunzi wangu tutakula
Pasaka?’ 15 Atawaonesha chumba kikubwa ghorofani,
kilichopambwa tena kilicho tayari. Tuandalieni humo.”
16 Wale wanafunzi wakaondoka na kwenda mjini,
nao wakakuta kila kitu kama Isa alivyowaambia.
Hivyo wakaiandaa Pasaka. 17 Ilipofika jioni, Isa
akaja pamoja na wale wanafunzi wake kumi na
wawili. 18 Walipoketi mezani wakila, Isa akawaambia,
“Amin, nawaambia, mmoja wenu atanisaliti, mmoja
anayekula pamoja nami.” 19 Wakaanza kuhuzunika
na kumuuliza mmoja baada ya mwingine, “Je, ni
mimi, Bwana?” 20 Akawajibu, “Ni mmoja miongoni
mwenu ninyi kumi na wawili, yule anayechovya
mkate kwenye bakuli pamoja nami. 21 Mwana wa
Adamu anaenda zake kama vile alivyoandikiwa. Lakini
ole wake mtu yule amsalitiye Mwana wa Adamu!
Ingekuwa heri kwake mtu huyo kama hangezaliwa.”
22 Walipokuwa wanakula, Isa akachukua mkate,
akashukuru, akaumega na kuwapa wanafunzi wake,
akisema, “Twaeni mle; huu ndio mwili wangu.” 23
Kisha akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, nao
wote wakanywa kutoka humo. 24 Akawaambia, “Hii
ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya
wengi. 25 Amin, nawaambia, sitakunywa tena katika
uzao wa mzabibu, hadi siku ile nitakapounywa mpya
katika ufalme wa Mungu.” 26 Walipokwisha kuimba
wimbo, wakatoka wakaenda Mlima wa Mizeituni.
27 Isa akawaambia, “Ninyi nyote mtaniacha, kwa
maana imeandikwa: “‘Nitampiga mchungaji, nao
kondoo watatawanyika.’ 28 Lakini baada ya kufufuka
kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya.” 29 Petro
akasema, “Hata kama wengine wote watakuacha,
mimi sitakuacha.” 30 Isa akamwambia, “Amin,
nakuambia; leo, usiku huu, kabla jogoo hajawika mara
mbili, wewe mwenyewe utanikana mara tatu.” 31
Lakini Petro akasisitiza zaidi, “Hata kama itabidi kufa
pamoja nawe, sitakukana kamwe.” Nao wale wengine
wote wakasema vivyo hivyo. 32 Wakaenda mahali
paitwapo Gethsemane. Isa akawaambia wanafunzi
wake, “Kaeni hapa, nami niende nikaombe.” 33

Kisha akawachukua pamoja naye Petro, Yakobo na
Yohana. Akaanza kuhuzunika sana na kutaabika. **34**
Akawaambia, “Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi
cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe.” **35** Akaenda mbele
kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba kwamba kama
ingewezekana saa hiyo ya mateso imwondokee. **36**
Akasema, “Abba, Baba, mambo yote yawezekana
kwako. Niondolee kikombe hiki. Lakini si kama
nipendavyo mimi, bali vile upendavyo wewe.” **37**
Akarudi kwa wanafunzi wake, akawakuta wamelala.
Akamwambia Petro, “Simoni, umelala? Je, hukuweza
kukesha hata kwa saa moja? **38** Kesheni na mwombe,
msije mkaingia majaribuni. Roho iko radhi, lakini
mwili ni mdhaifu.” **39** Akaenda tena kuomba, akisema
maneno yale yale. **40** Aliporudi, akawakuta tena
wamelala kwa sababu macho yao yalikuwa mazito.
Nao hawakujua la kumwambia. **41** Akaja mara ya
tatu, akawaambia, “Bado mmelala na kupumzika?
Imetosha! Saa imewadia. Tazameni, Mwana wa
Adamu anasalitiwa na kutiwa mikononi mwa wenye
dhambi. **42** Inukeni, twende zetu! Tazameni, msaliti
wangu yuaja!” **43** Isa alipokuwa bado anazungumza,
Yuda, mmoja wa wale kumi na wawili, akatokea.
Alikuwa amefuatana na umati wa watu wenye panga
na marungu, waliokuwa wametumwa na viongozi
wa makuhani, walimu wa Torati, na wazee. **44** Basi
msaliti alikuwa amewapa hao watu ishara, kwamba:
“Yule nitakayembusu ndiye. Mkamateni, mkamchukue
chini ya ulinzi.” **45** Mara Yuda akamjia Isa na kusema,
“Mwalimu.” Akambusu. **46** Wale watu wakamkamata
Isa, wakamweka chini ya ulinzi. **47** Ndipo mmoja wa
wale waliokuwa wamesimama karibu aliuchomoa
upanga wake na kumpiga mtumishi wa kuhani mkuu,
akamkata sikio. **48** Kisha Isa akawaambia, “Mmekuja
na panga na marungu kunikamata kana kwamba mimi
ni mnyang’anyi? **49** Siku kwa siku nilikuwa pamoja
nanyi nikifundisha Hekaluni, wala hamkunikamata.
Lakini Maandiko sharti yatimie.” **50** Ndipo wanafunzi
wake wote wakamwacha, wakakimbia. **51** Kijana
mmoja, aliyekuwa amevaa nguo ya kitani pekee,
alikuwa akimfuata Isa. Walipomkamata, **52** alikimbia
uchi, akaliacha vazi lake. **53** Wakampeleka Isa kwa
kuhani mkuu, nao viongozi wa makuhani wote, na
wazee na walimu wa Torati wote wakakusanyika
pamoja. **54** Petro akamfuata kwa mbali, hadi uani
kwa kuhani mkuu. Huko akaketi pamoja na walinzi,
akiota moto. **55** Viongozi wa makuhani na Baraza
la Wayahudi lote wakatafuta ushahidi dhidi ya Isa ili
wapate kumuua. Lakini hawakupata jambo lolote. **56**
Wengi walitoa ushahidi wa uongo dhidi yake, lakini
maelezo yao hayakukubaliana. **57** Ndipo wengine
wakasimama wakatoa ushahidi wa uongo dhidi
yake, wakisema: **58** “Sisi tulimsikia akisema, ‘Mimi
nitalibomoa Hekalu hili lililojengwa na wanadamu, na
katika siku tatu nitajenga jingine ambalo halikujengwa
na wanadamu.’” **59** Lakini hata hivyo, ushahidi wao
haukukubaliana. **60** Basi kuhani mkuu akasimama
mbele yao, akamuuliza Isa, “Je, wewe hutajibu? Ni
ushahidi gani hawa watu wanauleta dhidi yako?”
**61** Lakini Isa akakaa kimya, hakusema neno lolote.
Kuhani mkuu akamuuliza tena, “Je, wewe ndiwe Al-
Masihi, Mwana wa Mungu Aliyebarikiwa?” **62** Isa
akajibu, “Mimi ndimi. Nanyi mtamwona Mwana wa
Adamu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mwenye
Nguvu, na akija juu ya mawingu ya mbinguni.” **63**
Kuhani mkuu akayararua mavazi yake, akasema,
“Tuna haja gani tena ya mashahidi zaidi? **64** Ninyi
mmesikia alivyokufuru. Uamuzi wenu ni gani?”
Wote wakamhukumu kwamba anastahili kifo. **65**
Kisha baadhi ya watu wakaanza kumtemea mate;
wakamfunga kitambaa machoni, wakampiga kwa
ngumi na kumwambia, “Tabiri!” Walinzi wakamchukua
na kumpiga makofi. **66** Petro alipokuwa bado yuko
chini uani, tazama akaja mmoja wa wajakazi wa
kuhani mkuu. **67** Alipomwona Petro akiota moto,
akamtazama sana, akamwambia, “Wewe pia ulikuwa
pamoja na Isa, Mnasiri.” **68** Lakini Petro akakana,
akasema, “Sijui wala sielewi unalosema.” Naye
akaondoka kuelekea kwenye njia ya kuingilia. **69** Yule
mjakazi alipomwona mahali pale, akawaambia tena
wale waliokuwa wamesimama hapo, “Huyu mtu ni
mmoja wao.” **70** Lakini Petro akakana tena. Baada
ya muda kidogo wale waliokuwa wamesimama hapo
karibu na Petro wakamwambia, “Hakika wewe ni
mmoja wao, kwa maana wewe pia ni Mgalilaya!” **71**
Petro akaanza kujilaani na kuwaapia, “Mimi simjui
huyu mtu mnayesema habari zake!” **72** Papo hapo
jogoo akawika mara ya pili. Ndipo Petro akakumbuka
lile neno Isa alikuwa amemwambia: “Kabla jogoo
hajawika mara mbili, utanikana mara tatu.” Akavunjika
moyo, akalia sana.

**15** Asubuhi na mapema, viongozi wa makuhani,
pamoja na wazee, walimu wa Torati na Baraza
la Wayahudi lote, wakafikia uamuzi. Wakamfunga
Isa, wakamchukua na kumkabidhi kwa Pilato. **2**
Pilato akamuuliza, “Je, wewe ndiwe mfalme wa
Wayahudi?” Isa akajibu, “Wewe umesema.” **3** Viongozi
wa makuhani wakamshtaki kwa mambo mengi. **4**
Pilato akamuuliza tena, “Je, huna la kujibu? Tazama
ni mashtaka mangapi wanayaleta juu yako.” **5** Lakini
Isa hakujibu lolote, hivyo Pilato akashangaa. **6** Ilikuwa
desturi wakati wa Sikukuu ya Pasaka kumfungulia
mfungwa yeyote ambaye watu wangemtaka. **7**
Wakati huo, mtu aliyeitwa Baraba alikuwa amefungwa
gerezani pamoja na waasi wengine waliokuwa
wametekeleza uuaji wakati wa maasi. **8** Umati ule wa
watu wakamjia Pilato na kumwomba awafanyie kama
ilivyokuwa desturi yake. **9** Pilato akawauliza, “Mnataka
niwafungulie huyu mfalme wa Wayahudi?” **10** Kwa
maana yeye alitambua kuwa viongozi wa makuhani
walikuwa wamemtia Isa mkononi mwake kwa ajili ya
wivu. **11** Lakini viongozi wa makuhani wakachochea
umati ule wa watu wamwombe awafungulie Baraba
badala yake. **12** Pilato akawauliza tena, “Basi mnataka
nifanye nini na huyu mtu mnayemwita mfalme
wa Wayahudi?” **13** Wakapiga kelele, wakisema,
“Msulubishe!” **14** Pilato akawauliza, “Kwa nini?
Amefanya kosa gani?” Lakini wao wakapiga kelele
zaidi, wakisema, “Msulubishe!” **15** Pilato, akitaka
kuridhisha umati ule wa watu, akawafungulia Baraba.
Naye baada ya kuamuru Isa apigwe mijeledi,
akamtoa ili asulubishwe. **16** Askari wakampeleka
Isa hadi kwenye ukumbi wa ndani wa jumba la
kifalme, ndio Praitorio, wakakusanya kikosi kizima
cha askari. **17** Wakamvalisha Isa joho la zambarau,
wakasokota taji la miiba, wakamvika kichwani. **18**
Wakaanza kumsalimu kwa dhihaka, “Salamu, mfalme
wa Wayahudi!” **19** Wakampiga kwa fimbo ya mwanzi
tena na tena kichwani na kumtemea mate. Wakapiga
magoti mbele yake, wakamsujudia kwa kumdhihaki.
**20** Walipokwisha kumdhihaki, wakamvua lile joho
la zambarau, wakamvika tena nguo zake. Kisha
wakamtoa nje ili wakamsulubishe. **21** Mtu mmoja
kutoka Kirene, jina lake Simoni, baba yao Iskanda na
Rufo, alikuwa anaingia mjini kutoka mashambani,
nao wakamlazimisha kuubeba ule msalaba. **22** Kisha
wakampeleka Isa hadi mahali palipoitwa Golgotha
(maana yake ni Mahali pa Fuvu la Kichwa). **23** Nao
wakampa divai iliyochanganywa na manemane, lakini
hakuinywa. **24** Basi wakamsulubisha, nazo nguo
zake wakagawana miongoni mwao kwa kuzipigia
kura ili kuamua ni gani kila mtu ataichukua. **25**
Ilikuwa saa tatu asubuhi walipomsulubisha. **26**
Tangazo likaandikwa la mashtaka dhidi yake lenye
maneno haya: Mfalme wa Wayahudi. **27** Pamoja naye
walisulubiwa wanyang’anyi wawili, mmoja upande
wake wa kuume na mwingine upande wa kushoto. [
**28** Nalo andiko likatimizwa, lisemalo, “Alihesabiwa
pamoja na watenda dhambi.”] **29** Watu waliokuwa
wakipita njiani wakamtukana huku wakitikisa vichwa
vyao na kusema, “Aha! Wewe ambaye utalivunja
Hekalu na kulijenga kwa siku tatu, **30** basi shuka kutoka
msalabani na ujiokoe mwenyewe!” **31** Vivyo hivyo,
viongozi wa makuhani pamoja na walimu wa Torati
wakamdhihaki miongoni mwao wakisema, “Aliwaokoa
wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe! **32** Basi
huyu Al-Masihi, huyu mfalme wa Israeli, ashuke
sasa msalabani, ili tupate kuona na kuamini.” Wale
waliosulubiwa pamoja naye pia wakamtukana. **33**
Ilipofika saa sita, giza liliifunika nchi yote hadi saa
tisa. **34** Hapo saa tisa, Isa akapaza sauti, akalia,
“Eloi, Eloi, lama sabakthani?” (maana yake, “Mungu
wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?”) **35**
Baadhi ya watu waliokuwa wamesimama karibu
waliposikia hayo, wakasema, “Msikieni, anamwita
Ilya.” **36** Mtu mmoja akaenda mbio, akachovya
sifongo kwenye siki, akaiweka kwenye mwanzi na
akampa Isa ili anywe, akisema, “Basi mwacheni.
Hebu tuone kama Ilya atakuja kumshusha kutoka
hapo msalabani.” **37** Kisha Isa akatoa sauti kuu,
akakata roho. **38** Pazia la Hekalu likachanika vipande
viwili kuanzia juu hadi chini. **39** Basi yule jemadari
aliyekuwa amesimama hapo mbele ya msalaba wa
Isa aliposikia ile sauti yake na kuona jinsi alivyokata
roho, akasema, “Hakika mtu huyu alikuwa Mwana
wa Mungu!” **40** Palikuwa na wanawake waliokuwa
wakiangalia kwa mbali. Miongoni mwao walikuwa
Mariamu Magdalene, na Mariamu mama yao Yakobo
mdogo na Yose, pia na Salome. **41** Hawa walifuatana
na Isa na kushughulikia mahitaji yake alipokuwa
Galilaya. Pia walikuwako wanawake wengine wengi
waliokuwa wamekuja pamoja naye hadi Yerusalemu.
**42** Ilipofika jioni, kwa kuwa ilikuwa Siku ya Maandalizi

(yaani siku moja kabla ya Sabato), 43 Yusufu wa
Arimathaya, mtu aliyeheshimiwa katika Baraza, na
alikuwa anautarajia ufalme wa Mungu, akamwendea
Pilato kwa ujasiri na kumwomba mwili wa Isa. 44
Pilato alikuwa akijiuliza kama Isa alikuwa amekwisha
kufa. Hivyo akamwita yule jemadari, akamuuliza
iwapo Isa alikuwa amekwisha kufa. 45 Baada ya
kupata habari kutoka kwa yule jemadari kwamba
kweli amekwisha kufa, Pilato akampa Yusufu ruhusa
ya kuuchukua huo mwili. 46 Hivyo Yusufu akanunua
kitambaa cha kitani safi, akaushusha mwili kutoka
msalabani, akaufunga katika kile kitambaa cha kitani,
na kuuweka ndani ya kaburi lililochongwa kwenye
mwamba. Kisha akavingirisha jiwe kwenye ingilio la
kaburi. 47 Mariamu Magdalene na Mariamu mamaye
Yose walipaona mahali pale alipolazwa.

**16** Sabato ilipomalizika, Mariamu Magdalene,
Mariamu mama yake Yakobo, na Salome
walinunua manukato ili wakaupake mwili wa Isa.
2 Asubuhi na mapema, siku ya kwanza ya juma,
mara tu baada ya kuchomoza jua, walienda kaburini.
3 Njiani wakawa wanaulizana wao kwa wao, "Ni
nani atakayetuvingirishia lile jiwe kutoka ingilio
la kaburi?" 4 Lakini walipotazama, wakaona lile
jiwe, ambalo lilikuwa kubwa sana, limekwisha
kuvingirishwa kutoka pale penye ingilio la kaburi.
5 Walipokuwa wakiingia mle kaburini, wakamwona
kijana mmoja aliyevaa joho jeupe akiwa ameketi
upande wa kuume, nao wakastaajabu. 6 Yule
malaika akawaambia, "Msistaajabu. Mnamtafuta Isa,
Mnasiri, aliyesulubiwa. Amefufuka! Hayuko hapa.
Tazameni mahali walipomlaza. 7 Lakini nendeni
mkawaambie wanafunzi wake pamoja na Petro,
kwamba, 'Anawatangulia kwenda Galilaya. Mtamwona
huko kama alivyowaambia.'" 8 Hivyo wakatoka,
wakakimbia kutoka mle kaburini wakiwa na hofu kuu
na mshangao. Nao hawakumwambia mtu yeyote neno
lolote, kwa sababu waliogopa. [ 9 **(note: The most reliable
and earliest manuscripts do not include Mark 16:9-20.)** Isa
alipofufuka alfajiri na mapema siku ya kwanza ya juma
alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, aliyekuwa
amemtoa pepo wachafu saba. 10 Mariamu akaenda,
naye akawaambia wale waliokuwa wamefuatana
na Isa, waliokuwa wanaomboleza na kulia. 11
Lakini waliposikia kwamba Isa yu hai na kwamba
Mariamu alikuwa amemwona, hawakusadiki. 12
Baadaye Isa akawatokea wawili miongoni mwa
wanafunzi wake walipokuwa wakienda shambani
akiwa katika sura nyingine. 13 Nao wakarudi na
kuwaambia wenzao. Lakini hawakuwasadiki wao pia.
14 Baadaye Isa akawatokea wale wanafunzi kumi na
mmoja walipokuwa wakila chakula. Akawakemea kwa
kutoamini kwao na kwa ugumu wa mioyo yao kwa
kutosadiki wale waliomwona baada yake kufufuka. 15
Akawaambia, "Nendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri
Injili kwa kila kiumbe. 16 Yeyote aaminiye na kubatizwa
ataokoka. Lakini yeyote asiyeamini atahukumiwa. 17
Nazo ishara hizi zitafuatana na wanaoamini: Kwa Jina
langu watatoa pepo wachafu; watasema kwa lugha
mpya; 18 watashika nyoka kwa mikono yao; na hata
wakinywa kitu chochote cha kuua, hakitawadhuru
kamwe; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao
watapona." 19 Baada ya Bwana Isa kusema nao,
alichukuliwa juu mbinguni na kuketi mkono wa kuume
wa Mungu. 20 Kisha wanafunzi wake wakatoka,
wakahubiri kila mahali, naye Bwana Isa akatenda kazi
pamoja nao na kulithibitisha neno lake kwa ishara
zilizofuatana nalo.]

# Luka

1 Kwa kuwa watu wengi wamekaa ili kuandika
habari za mambo yaliyotimizwa katikati yetu, 2
kama vile yalivyokabidhiwa kwetu na wale waliokuwa
mashahidi walioyaona na watumishi wa lile neno
tokea mwanzo, 3 mimi nami baada ya kuchunguza
kila kitu kwa uangalifu kuanzia mwanzo, niliamua
kukuandikia habari za mambo hayo, ewe mtukufu
Theofilo, 4 ili upate kujua ukweli kuhusu yale
uliyofundishwa. 5 Wakati wa utawala wa Herode
mfalme wa Yudea, palikuwa na kuhani mmoja jina
lake Zakaria, aliyekuwa wa ukoo wa kikuhani wa
Abiya. Elizabeti mkewe alikuwa pia mzao wa Haruni.
6 Zakaria na Elizabeti mkewe wote walikuwa watu
wanyofu mbele za Mungu, wakizishika amri zote za
Mwenyezi Mungu na maagizo yote bila lawama. 7
Lakini walikuwa hawana watoto, kwa sababu Elizabeti
alikuwa tasa; nao wote wawili walikuwa wazee sana.
8 Siku moja ilipokuwa zamu ya kikundi cha Zakaria,
yeye akifanya kazi ya ukuhani Hekaluni mbele za
Mungu, 9 alichaguliwa kwa kura kwa kufuata desturi
za ukuhani, kuingia Hekaluni mwa Mwenyezi Mungu ili
kufukiza uvumba. 10 Nao wakati wa kufukiza uvumba
ulipowadia, wale wote waliokuwa wamekusanyika ili
kuabudu walikuwa nje wakiomba. 11 Ndipo malaika
wa Mwenyezi Mungu, akiwa amesimama upande
wa kuume wa madhabahu ya kufukizia uvumba,
akamtokea Zakaria. 12 Zakaria alipomwona huyo
malaika, akafadhaika sana, akajawa na hofu. 13
Lakini malaika akamwambia, “Usiogope, Zakaria,
kwa maana Mungu amesikia maombi yako. Mkeo
Elizabeti atakuzalia mtoto wa kiume, nawe utamwita
jina Yahya. 14 Yeye atakuwa furaha na shangwe
kwako, nao watu wengi watashangilia kwa sababu ya
kuzaliwa kwake. 15 Kwa kuwa atakuwa mkuu mbele
za Mwenyezi Mungu, kamwe hataonja mvinyo wala
kinywaji chochote cha kulevya, naye atajazwa Roho
Mtakatifu wa Mungu hata kabla ya kuzaliwa kwake.
16 Naye atawageuza wengi wa Waisraeli warudi kwa
Mwenyezi Mungu, Mungu wao. 17 Naye atatangulia
mbele za Mwenyezi Mungu katika roho na nguvu ya
Ilya, ili kuigeuza mioyo ya baba kuwaelekea watoto
wao, na wasiotii warejee katika hekima ya wenye
haki, ili kuwaweka tayari watu walioandaliwa kwa
ajili ya Mwenyezi Mungu.” 18 Zakaria akamuuliza
malaika, “Jambo hilo linawezekanaje? Mimi ni
mzee na mke wangu pia ana umri mkubwa.” 19
Malaika akamjibu, akamwambia, “Mimi ni Jibraili,
nisimamaye mbele za Mungu, nami nimetumwa kwako
ili nikuambie habari hizi njema. 20 Basi sasa kwa
kuwa hujaamini maneno yangu ambayo yatatimizwa
kwa wakati wake, utakuwa bubu hadi siku ile mambo
haya yatakapotukia.” 21 Wakati huo watu walikuwa
wanamngojea Zakaria nje huku wakishangaa kukawia
kwake mle Hekaluni. 22 Alipotoka akawa hawezi
kusema nao, wao wakatambua kuwa ameona maono
ndani ya Hekalu. Lakini kwa kuwa alikuwa bubu,
akawa anawaashiria kwa mikono. 23 Muda wake wa
kuhudumu Hekaluni ulipomalizika, akarudi nyumbani
mwake. 24 Baada ya muda usio mrefu, Elizabeti
mkewe akapata mimba, naye akajitenga kwa miezi
mitano. 25 Elizabeti akasema, “Hili ndilo Mwenyezi
Mungu alilonitendea aliponipa kibali na kuniondolea
aibu yangu mbele ya watu.” 26 Mwezi wa sita baada
ya Elizabeti kupata mimba, Mungu alimtuma malaika
Jibraili aende Galilaya katika mji wa Nasiri, 27 kwa
mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu
mmoja jina lake Yusufu wa nyumba ya Daudi. Jina
la huyu mwanamwali bikira ni Mariamu. 28 Naye
malaika akaja kwake akamwambia: “Salamu, wewe
uliyebarikiwa, Mwenyezi Mungu yu pamoja nawe!”
29 Mariamu akafadhaishwa sana na maneno haya,
akajiuliza moyoni salamu hii ni ya namna gani. 30
Ndipo malaika akamwambia, “Usiogope, Mariamu;
umepata kibali kwa Mungu. 31 Tazama, utachukua
mimba, nawe utamzaa mtoto wa kiume na utamwita
jina Isa. 32 Yeye atakuwa mkuu, naye ataitwa Mwana
wa Aliye Juu Sana. Mwenyezi Mungu atampa kiti
cha utawala cha Daudi baba yake. 33 Ataimiliki
nyumba ya Yakobo milele, na ufalme wake hautakuwa
na mwisho.” **(aiōn g165)** 34 Mariamu akamuuliza
huyo malaika, “Maadamu mimi ni bikira, jambo hili
litawezekanaje?” 35 Malaika akamjibu, “Roho wa
Mungu atakujilia juu yako, nazo nguvu zake Yeye
Aliye Juu Sana zitakufunika kama kivuli. Kwa hiyo
mtoto atakayezaliwa atakuwa mtakatifu, naye ataitwa
Mwana wa Mungu. 36 Tazama, jamaa yako Elizabeti
amechukua mimba katika uzee wake, na huu ni mwezi
wake wa sita, yeye aliyeitwa tasa. 37 Kwa maana
kwa Mungu hakuna lisilowezekana.” 38 Mariamu
akasema, “Tazama, mimi ni mtumishi wa Mwenyezi

Mungu. Na iwe kwangu kama ulivyosema." Kisha
malaika akaondoka, akamwacha. 39 Wakati huo
Mariamu akajiandaa, akaharakisha kwenda katika
mji mmoja kwenye nchi ya vilima ya Yudea. 40
Akaingia nyumbani mwa Zakaria na kumsalimu
Elizabeti. 41 Naye Elizabeti aliposikia salamu ya
Mariamu, mtoto aliyekuwa tumboni mwake akaruka.
Elizabeti akajazwa na Roho wa Mungu, 42 akapaza
sauti kwa nguvu, akasema, "Umebarikiwa wewe
miongoni mwa wanawake, naye mtoto utakayemzaa
amebarikiwa. 43 Lakini ni kwa nini mimi nimepata
kibali kiasi hiki, hata mama wa Bwana wangu afike
kwangu? 44 Mara tu niliposikia sauti ya salamu yako,
mtoto aliye tumboni mwangu aliruka kwa furaha. 45
Amebarikiwa yeye aliyeamini kwamba lile Mwenyezi
Mungu alilomwambia litatimizwa." 46 Naye Mariamu
akasema: "Moyo wangu wamwadhimisha Mwenyezi
Mungu, 47 nayo roho yangu inamfurahia Mungu
Mwokozi wangu, 48 kwa kuwa ameangalia kwa
fadhili unyonge wa mtumishi wake. Hakika tangu
sasa vizazi vyote vitaniita aliyebarikiwa, 49 kwa
maana yeye Mwenye Nguvu amenitendea mambo ya
ajabu: jina lake ni takatifu. 50 Rehema zake hudumu
kizazi hadi kizazi, kwa wale wanaomcha. 51 Kwa
kuwa ametenda mambo ya ajabu kwa mkono wake;
amewatawanya wale wenye kiburi ndani ya mioyo
yao. 52 Amewashusha watawala toka kwenye viti
vyao vya utawala, lakini amewainua wanyenyekevu.
53 Amewashibisha wenye njaa kwa vitu vizuri, bali
matajiri amewafukuza mikono mitupu. 54 Amemsaidia
mtumishi wake Israeli, kwa kukumbuka ahadi yake
ya kumrehemu 55 Ibrahimu na uzao wake milele,
kama alivyowaahidi baba zetu." (aiōn g165) 56 Mariamu
akakaa na Elizabeti karibu miezi mitatu, kisha akarudi
nyumbani mwake. 57 Ulipowadia wakati wa Elizabeti
kujifungua, alizaa mtoto wa kiume. 58 Majirani
zake na jamii zake wakasikia jinsi Mwenyezi Mungu
alivyomfanyia rehema kuu, nao wakafurahi pamoja
naye. 59 Siku ya nane wakaja kumtahiri mtoto,
wakataka yule mtoto aitwe Zakaria, ambalo ndilo
jina la baba yake. 60 Lakini mama yake akakataa
na kusema, "Hapana! Jina lake ataitwa Yahya." 61
Wakamwambia, "Hakuna mtu yeyote katika jamaa
yako mwenye jina kama hilo." 62 Basi wakamfanyia
Zakaria baba yake ishara ili kujua kwamba yeye
angependa kumpa mtoto jina gani. 63 Akaomba
wampe kibao cha kuandikia na kwa mshangao wa
kila mtu akaandika: "Jina lake ni Yahya." 64 Papo
hapo kinywa chake kikafunguliwa na ulimi wake
pia, akaanza kuongea, huku akimsifu Mungu. 65
Majirani wote wakajawa na hofu ya Mungu, na
katika nchi yote ya vilima ya Yudea watu walikuwa
wakinena kuhusu mambo haya yote. 66 Kila aliyesikia
habari hizi alishangaa akauliza, "Je, mtoto huyu
atakuwa mtu wa namna gani?" Maana mkono wa
Mwenyezi Mungu ulikuwa pamoja naye. 67 Zakaria,
baba yake, akajazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu,
naye akatoa unabii, akisema: 68 "Ahimidiwe Bwana,
Mungu wa Israeli, kwa kuwa amewajilia watu wake
na kuwakomboa. 69 Naye ametusimamishia pembe
ya wokovu katika nyumba ya Daudi mtumishi wake,
70 (kama alivyonena kwa vinywa vya manabii wake
watakatifu tangu zamani), (aiōn g165) 71 kwamba
atatuokoa kutoka kwa adui zetu, na kutoka mikononi
mwao wote watuchukiao: 72 ili kuonesha rehema kwa
baba zetu na kukumbuka agano lake takatifu, 73
kiapo alichomwapia baba yetu Ibrahimu: 74 kutuokoa
kutoka mikononi mwa adui zetu, tupate kumtumikia
yeye pasipo hofu 75 katika utakatifu na haki mbele
zake, siku zetu zote. 76 "Nawe mtoto wangu, utaitwa
nabii wa Aliye Juu Sana; kwa kuwa utamtangulia
Mwenyezi Mungu na kuandaa njia kwa ajili yake, 77
kuwajulisha watu wake wokovu utakaopatikana kwa
kusamehewa dhambi zao, 78 kwa ajili ya wingi wa
rehema za Mungu wetu, nuru inayotoka juu itatuzukia
79 ili kuwaangazia wale wanaoishi gizani na katika
uvuli wa mauti, kuiongoza miguu yetu katika njia ya
amani." 80 Yule mtoto akakua na kuongezeka nguvu
katika roho; akaishi nyikani hadi siku ile alipojionesha
hadharani kwa Waisraeli.

2 Siku zile Kaisari Augusto alitoa amri kwamba
watu wote waandikishwe katika ulimwengu wa
Rumi. 2 (Orodha hii ndiyo ya kwanza iliyofanyika
wakati Krenio alikuwa mtawala wa Siria.) 3 Kila mtu
alienda kuandikishwa katika mji wake alikozaliwa. 4
Hivyo Yusufu akapanda kutoka mji wa Nasiri ulioko
Galilaya kwenda Yudea, hadi Bethlehemu, mji wa
Daudi, kwa sababu yeye alikuwa wa ukoo na wa
nyumba ya Daudi. 5 Alienda huko kujiandikisha
pamoja na Mariamu, aliyekuwa amemposa, na alikuwa
mjamzito. 6 Wakiwa Bethlehemu, wakati wa Mariamu
wa kujifungua ukawa umetimia, 7 naye akamzaa

mwanawe, kifungua mimba. Akamfunika nguo za
kitoto na kumlaza katika hori la kulia ng'ombe,
kwa sababu hapakuwa na nafasi katika nyumba ya
wageni. 8 Katika eneo lile walikuwako wachungaji
waliokuwa wakikaa mashambani, wakilinda makundi
yao ya kondoo usiku. 9 Ghafula tazama, malaika
wa Mwenyezi Mungu akawatokea, nao utukufu wa
Mwenyezi Mungu ukawang'aria kotekote, wakaingiwa
na hofu. 10 Lakini malaika akawaambia: "Msiogope.
Kwa maana tazama, nawaletea habari njema ya
furaha itakayokuwa kwa watu wote. 11 Leo katika
mji wa Daudi kwa ajili yenu amezaliwa Mwokozi,
ndiye Al-Masihi, Bwana. 12 Hii ndiyo itakayokuwa
ishara kwenu: Mtamkuta mtoto mchanga amefunikwa
nguo za kitoto na kulazwa katika hori la kulia
ng'ombe." 13 Ghafula pakawa na jeshi kubwa la
mbinguni pamoja na huyo malaika wakimsifu Mungu
wakisema, 14 "Utukufu kwa Mungu juu mbinguni,
na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." 15
Hao malaika walipokwisha kuondoka na kwenda zao
mbinguni, wale wachungaji wakasemezana wao kwa
wao, "Twendeni Bethlehemu tukaone mambo haya
yaliyotukia, ambayo Mwenyezi Mungu ametuambia
habari zake." 16 Hivyo wakaenda haraka Bethlehemu,
wakawakuta Mariamu na Yusufu na yule mtoto
mchanga akiwa amelala katika hori la kulia ng'ombe.
17 Walipomwona yule mtoto, wakawaeleza yale
waliyokuwa wameambiwa kuhusu huyo mtoto. 18
Nao wote waliosikia habari hizi wakastaajabia yale
waliyoambiwa na wale wachungaji wa kondoo. 19
Lakini Mariamu akayaweka mambo haya yote moyoni
mwake na kuyatafakari. 20 Wale wachungaji wakarudi,
huku wakimtukuza Mungu na kumsifu kwa ajili ya
mambo yote waliyokuwa wameambiwa na kuyaona.
21 Hata zilipotimia siku nane, uliokuwa wakati wa
kumtahiri mtoto, akaitwa Isa, jina alilopewa na malaika
kabla hajatungwa mimba. 22 Ulipotimia wakati wa
utakaso wake Mariamu kwa mujibu wa Torati ya
Musa, basi Yusufu na Mariamu walimpeleka mtoto
Yerusalemu, ili kumweka wakfu kwa Mwenyezi Mungu
23 (kama ilivyoandikwa katika Torati ya Mwenyezi
Mungu, kwamba, "Kila mtoto wa kiume kifungua
mimba atawekwa wakfu kwa Mwenyezi Mungu"), 24
na pia kutoa dhabihu kulingana na yale yaliyonenwa
katika Torati ya Mwenyezi Mungu: "Hua wawili au
makinda wawili wa njiwa". 25 Basi huko Yerusalemu
kulikuwa mtu mmoja aliyeitwa Simeoni, aliyekuwa
mwenye haki na mcha Mungu. Alikuwa akitazamia
faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu wa Mungu alikuwa
juu yake. 26 Roho wa Mungu alikuwa amemfunulia
kuwa hatakufa kabla hajamwona Al-Masihi wa Bwana.
27 Simeoni, akiwa ameongozwa na Roho wa Mungu,
alienda Hekaluni. Wazazi walipomleta mtoto Isa ili
kumfanyia kama ilivyokuwa desturi ya Torati, 28
ndipo Simeoni akampokea mtoto mikononi mwake
na kumsifu Mungu, akisema: 29 "Bwana Mungu
Mwenyezi, kama ulivyoahidi, sasa mruhusu mtumishi
wako aende kwa amani. 30 Kwa maana macho yangu
yameuona wokovu wako, 31 ulioweka tayari machoni
pa watu wote, 32 nuru kwa ajili ya ufunuo kwa watu wa
Mataifa na kwa ajili ya utukufu kwa watu wako Israeli."
33 Naye Yusufu na mama yake mtoto wakastaajabu
kwa yale yaliyokuwa yamesemwa kumhusu huyo
mtoto. 34 Kisha Simeoni akawabariki, akamwambia
Mariamu mama yake, "Mtoto huyu amewekwa kwa
makusudi ya kuanguka na kuinuka kwa wengi katika
Israeli. Atakuwa ishara ambayo watu watanena dhidi
yake, 35 ili mawazo ya mioyo mingi yadhihirike. Nao
upanga utauchoma moyo wako." 36 Tena alikuwako
Hekaluni nabii mmoja mwanamke, jina lake Ana
binti Fanueli, wa kabila la Asheri. Alikuwa mzee
sana; naye alikuwa ameolewa na kuishi na mume
kwa miaka saba tu, kisha mumewe akafa. 37 Hivyo
alikuwa mjane na umri wake ulikuwa miaka themanini
na nne. Yeye hakuondoka humo Hekaluni usiku
wala mchana, bali alikuwa akimwabudu Mungu,
akifunga na kuomba. 38 Wakati huo huo, Ana alikuja
akaanza kusifu, akimshukuru Mungu na kusema
habari za huyo mtoto kwa watu wote waliokuwa
wakitarajia ukombozi wa Yerusalemu. 39 Yusufu
na Mariamu walipokuwa wamekamilisha mambo
yote yaliyotakiwa na Torati ya Mwenyezi Mungu,
walirudi mjini kwao Nasiri huko Galilaya. 40 Naye
yule mtoto akakua na kuongezeka nguvu, akijawa
na hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake.
41 Kila mwaka Yusufu na Mariamu mama yake Isa
walikuwa na desturi ya kwenda Yerusalemu kwa ajili
ya Sikukuu ya Pasaka. 42 Isa alipokuwa na umri
wa miaka kumi na mbili, walipanda kwenda kwenye
Sikukuu hiyo kama ilivyokuwa desturi. 43 Baada ya
Sikukuu kumalizika, wakati Yusufu na Mariamu mama
yake walipokuwa wakirudi nyumbani, Isa alibaki

Yerusalemu lakini hawakutambua. 44 Wao wakidhani
kuwa yuko miongoni mwa wasafiri, walienda mwendo
wa kutwa nzima. Ndipo wakaanza kumtafuta miongoni
mwa jamaa na rafiki zao. 45 Walipomkosa walirudi
Yerusalemu ili kumtafuta. 46 Baada ya siku tatu
wakamkuta ndani ya Hekalu, akiwa ameketi katikati ya
walimu wa Torati, akiwasikiliza na kuwauliza maswali.
47 Wote waliomsikia walistaajabishwa na uwezo
wake mkubwa wa kuelewa, na majibu aliyoyatoa.
48 Yusufu na Mariamu mama yake walipomwona
walishangaa. Mama yake akamuuliza, “Mwanangu,
mbona umetufanyia hivi? Tazama, mimi na baba yako
tumekuwa tukikutafuta kwa wasiwasi mkubwa kila
mahali.” 49 Isa akawaambia, “Kwa nini kunitafuta?
Hamkujua kwamba imenipasa kuwa katika nyumba
ya Baba yangu?” 50 Lakini wao hawakuelewa maana
ya lile alilowaambia. 51 Ndipo akashuka pamoja
nao hadi Nasiri, naye alikuwa mtiifu kwao. Lakini
mama yake akayaweka moyoni mwake mambo haya
yote. 52 Naye Isa akakua katika hekima na kimo,
akimpendeza Mungu na wanadamu.

**3** Katika mwaka wa kumi na tano wa utawala wa
Kaisari Tiberio, Pontio Pilato akiwa mtawala wa
Yudea, Herode akiwa mfalme wa Galilaya, Filipo
ndugu yake akiwa mfalme wa Iturea na nchi ya
Trakoniti, na Lisania akiwa mfalme wa Abilene, 2
nao Anasi na Kayafa wakiwa makuhani wakuu, neno
la Mungu likamjia Yahya, mwana wa Zakaria huko
jangwani. 3 Akaenda katika nchi yote kandokando
ya Mto Yordani, akihubiri ubatizo wa toba kwa ajili
ya msamaha wa dhambi. 4 Kama ilivyoandikwa
katika kitabu cha nabii Isaya: “Sauti ya mtu aliaye
nyikani, ‘Itengenezeni njia ya Mwenyezi Mungu,
yanyoosheni mapito yake. 5 Kila bonde litajazwa,
kila mlima na kilima vitashushwa. Njia zilizopinda
zitanyooshwa, na zilizoparuza zitasawazishwa. 6
Nao watu wote watauona wokovu wa Mungu.’”
7 Yahya akaambia umati ule wa watu waliokuwa
wanakuja ili kubatizwa naye, “Ninyi watoto wa nyoka!
Ni nani aliyewaonya kuikimbia ghadhabu inayokuja?
8 Basi zaeni matunda yastahiliyo toba. Wala msianze
kusema mioyoni mwenu kuwa, ‘Sisi tunaye Ibrahimu,
baba yetu.’ Kwa maana nawaambia kuwa Mungu
anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto kutoka mawe
haya. 9 Hata sasa shoka limeshawekwa tayari
kwenye shina la kila mti. Basi kila mti usiozaa
matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni.” 10
Umati ule wa watu wakamuuliza, “Inatupasa tufanyeje
basi?” 11 Yahya akawaambia, “Aliye na kanzu mbili
amgawie asiye nayo, naye aliye na chakula na
afanye vivyo hivyo.” 12 Watoza ushuru nao wakaja ili
wabatizwe, wakamuuliza, “Mwalimu na sisi inatupasa
tufanyeje?” 13 Akawaambia, “Msichukue zaidi ya
kiwango mlichopangiwa.” 14 Askari nao wakamuuliza,
“Je, nasi inatupasa tufanye nini?” Akawaambia,
“Msimdhulumu mtu wala msimshtaki mtu kwa uongo,
bali mridhike na mishahara yenu.” 15 Watu walikuwa
na matazamio makubwa. Wakawa wanajiuliza mioyoni
mwao iwapo Yahya angeweza kuwa ndiye Al-Masihi.
16 Yahya akawajibu akawaambia, “Mimi nawabatiza
kwa maji. Lakini atakuja aliye na nguvu kuliko mimi,
ambaye sistahili hata kufungua kamba za viatu vyake.
Yeye atawabatiza kwa Roho wa Mungu na kwa moto.
17 Pepeto lake liko mkononi, tayari kusafisha sakafu
yake ya kupuria na kuikusanya ngano ghalani, lakini
makapi atayateketeza kwa moto usiozimika.” 18 Basi,
kwa maonyo mengine mengi Yahya aliwasihi na
kuwahubiria watu Habari Njema. 19 Lakini Yahya
alipomkemea Mfalme Herode kuhusu uhusiano wake
na Herodia, mke wa ndugu yake, na maovu mengine
aliyokuwa amefanya, 20 Herode aliongezea jambo hili
kwa hayo mengine yote: alimfunga Yahya gerezani. 21
Baada ya watu wote kubatizwa, Isa naye akabatizwa.
Naye alipokuwa akiomba, mbingu zilifunguka. 22
Roho Mtakatifu wa Mungu akashuka juu yake kwa
umbo kama la hua, nayo sauti kutoka mbinguni
ikasema: “Wewe ni Mwanangu mpendwa; nami
nimependezwa nawe sana.” 23 Isa alikuwa na umri
wa miaka thelathini alipoanza huduma yake. Alikuwa
akidhaniwa kuwa mwana wa Yusufu. Yusufu alikuwa
mwana wa Eli, 24 Eli alikuwa mwana wa Mathati,
Mathati alikuwa mwana wa Lawi, Lawi alikuwa mwana
wa Melki, Melki alikuwa mwana wa Yana, Yana
alikuwa mwana wa Yusufu, 25 Yusufu alikuwa mwana
wa Matathia, Matathia alikuwa mwana wa Amosi,
Amosi alikuwa mwana wa Nahumu, Nahumu alikuwa
mwana wa Esli, Esli alikuwa mwana wa Nagai, 26
Nagai alikuwa mwana wa Maathi, Maathi alikuwa
mwana wa Matathia, Matathia alikuwa mwana wa
Semei, Semei alikuwa mwana wa Yoseki, Yoseki
alikuwa mwana wa Yoda, 27 Yoda alikuwa mwana wa
Yoanani, Yoanani alikuwa mwana wa Resa, Resa

alikuwa mwana wa Zerubabeli, Zerubabeli alikuwa
mwana wa Shealtieli, Shealtieli alikuwa mwana wa
Neri, **28** Neri alikuwa mwana wa Melki, Melki alikuwa
mwana wa Adi, Adi alikuwa mwana wa Kosamu,
Kosamu alikuwa mwana wa Elmadamu, Elmadamu
alikuwa mwana wa Eri, **29** Eri alikuwa mwana wa
Yoshua, Yoshua alikuwa mwana wa Eliezeri, Eliezeri
alikuwa mwana wa Yorimu, Yorimu alikuwa mwana
wa Mathati, Mathati alikuwa mwana wa Lawi, **30**
Lawi alikuwa mwana wa Simeoni, Simeoni alikuwa
mwana wa Yuda, Yuda alikuwa mwana wa Yusufu,
Yusufu alikuwa mwana wa Yonamu, Yonamu alikuwa
mwana wa Eliakimu, Eliakimu alikuwa mwana wa
Melea, **31** Melea alikuwa mwana wa Mena, Mena
alikuwa mwana wa Matatha, Matatha alikuwa mwana
wa Nathani, Nathani alikuwa mwana wa Daudi,
**32** Daudi alikuwa mwana wa Yese, Yese alikuwa
mwana wa Obedi, Obedi alikuwa mwana wa Boazi,
Boazi alikuwa mwana wa Salmoni, Salmoni alikuwa
mwana wa Nashoni, **33** Nashoni alikuwa mwana wa
Aminadabu, Aminadabu alikuwa mwana wa Aramu,
Aramu alikuwa mwana wa Esromu, Esromu alikuwa
mwana wa Peresi, Peresi alikuwa mwana wa Yuda,
**34** Yuda alikuwa mwana wa Yakobo, Yakobo alikuwa
mwana wa Isaka, Isaka alikuwa mwana wa Ibrahimu,
Ibrahimu alikuwa mwana wa Tera, Tera alikuwa
mwana wa Nahori, **35** Nahori alikuwa mwana wa
Serugi, Serugi alikuwa mwana wa Ragau, Ragau
alikuwa mwana wa Pelegi, Pelegi alikuwa mwana
wa Eberi, Eberi alikuwa mwana wa Sala, **36** Sala
alikuwa mwana wa Kenani, Kenani alikuwa mwana
wa Arfaksadi, Arfaksadi alikuwa mwana wa Shemu,
Shemu alikuwa mwana wa Nuhu, Nuhu alikuwa
mwana wa Lameki, **37** Lameki alikuwa mwana wa
Methusela, Methusela alikuwa mwana wa Idrisi, Idrisi
alikuwa mwana wa Yaredi, Yaredi alikuwa mwana wa
Mahalaleli, Mahalaleli alikuwa mwana wa Kenani, **38**
Kenani alikuwa mwana wa Enoshi, Enoshi alikuwa
mwana wa Sethi, Sethi alikuwa mwana wa Adamu,
Adamu alikuwa mwana wa Mungu.

**4** Isa, akiwa amejaa Roho Mtakatifu wa Mungu,
akarudi kutoka Yordani. Akaongozwa na Roho
wa Mungu hadi nyikani, **2** ambako alijaribiwa na
ibilisi kwa siku arobaini. Kwa siku zote hizo hakula
chochote, hivyo baada ya muda huo akaona njaa.
**3** Ibilisi akamwambia, "Ikiwa wewe ni Mwana wa
Mungu, amuru jiwe hili liwe mkate." **4** Isa akamjibu,
"Imeandikwa: 'Mtu haishi kwa mkate tu.'" **5** Ibilisi
akampeleka hadi juu ya mlima mrefu akamwonesha
milki zote za dunia kwa mara moja. **6** Akamwambia,
"Nitakupa mamlaka juu ya milki hizi na fahari
zake zote, kwa maana zimekabidhiwa mkononi
mwangu nami ninaweza kumpa yeyote ninayetaka.
**7** Hivyo ukinisujudia na kuniabudu, vyote vitakuwa
vyako." **8** Isa akamjibu, "Imeandikwa: 'Mwabudu
Mwenyezi Mungu, Mungu wako, na umtumikie
yeye peke yake.'" **9** Kisha ibilisi akampeleka hadi
Yerusalemu, akamweka juu ya mnara mrefu wa
Hekalu, akamwambia, "Kama wewe ndiwe Mwana
wa Mungu, jitupe chini kutoka hapa, **10** kwa maana
imeandikwa: "'Atakuagizia malaika wake ili wakulinde
kwa uangalifu; **11** nao watakuchukua mikononi mwao,
usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.'" **12** Isa
akamjibu, "Imenenwa: 'Usimjaribu Mwenyezi Mungu,
Mungu wako.'" **13** Ibilisi alipomaliza kila jaribu,
akamwacha Isa hadi wakati mwingine ufaao. **14**
Kisha Isa akarudi hadi Galilaya, akiwa amejaa nguvu
za Roho wa Mungu, nazo habari zake zikaenea
katika sehemu zote za nchi za kandokando. **15**
Akaanza kufundisha kwenye masinagogi yao, na kila
mmoja akamsifu. **16** Isa akaenda Nasiri, alipolelewa,
na siku ya Sabato alienda katika sinagogi kama
ilivyokuwa desturi yake. Akasimama ili asome, **17**
naye akapewa kitabu cha nabii Isaya, akakifungua
na kukuta mahali palipoandikwa: **18** "Roho wa
Bwana Mungu Mwenyezi yu juu yangu, kwa sababu
amenipaka mafuta kuwahubiria maskini Habari Njema.
Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa
kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka
huru wanaoteswa, **19** na kutangaza mwaka wa
Mwenyezi Mungu uliokubalika." **20** Kisha akakifunga
kitabu, akamrudishia mtumishi na akaketi. Watu wote
waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho.
**21** Ndipo akaanza kwa kuwaambia, "Leo andiko hili
limetimia mkiwa mnasikia." **22** Watu wote walimsifu
na kuyastaajabia maneno yake yaliyojaa neema,
wakaulizana, "Je, huyu si mwana wa Yusufu?" **23**
Isa akawaambia, "Bila shaka mtatumia mithali hii:
'Tabibu, jiponye mwenyewe! Mambo yale tuliyosikia
kwamba uliyafanya huko Kapernaumu, yafanye na
hapa kwenye mji wako.'" **24** Isa akasema, "Amin,
nawaambia, hakuna nabii anayekubalika katika mji

wake mwenyewe. 25 Lakini ukweli ni kwamba palikuwa
na wajane wengi katika Israeli wakati wa Ilya, mbingu
zilipofungwa kwa miaka mitatu na miezi sita pakawa
na njaa kuu katika nchi nzima. 26 Hata hivyo Ilya
hakutumwa hata kwa mmoja wao, bali kwa mjane
mmoja wa Sarepta katika nchi ya Sidoni. 27 Pia
palikuwa na wengi wenye ukoma katika Israeli katika
siku za nabii Al-Yasa, lakini hakuna hata mmoja wao
aliyetakaswa, isipokuwa Naamani mtu wa Shamu."
28 Watu wote katika sinagogi waliposikia maneno
haya, wakakasirika sana. 29 Wakasimama, wakamtoa
nje ya mji, wakamchukua hadi kwenye kilele cha
mlima ambao mji huo ulikuwa umejengwa juu yake,
ili wamtupe chini kutoka mteremko mkali. 30 Lakini
yeye akapita papo hapo katikati ya umati huo wa
watu akaenda zake. 31 Kisha Isa akashuka kwenda
Kapernaumu, mji wa Galilaya, na katika siku ya
Sabato akawa anafundisha. 32 Wakashangazwa
sana na mafundisho yake, maana maneno yake
yalikuwa na mamlaka. 33 Ndani ya sinagogi palikuwa
na mtu aliyekuwa amepagawa na pepo mchafu. Naye
akapaza sauti kwa nguvu akisema, 34 "Tuache! Tuna
nini nawe, Isa Al-Nasiri? Je, umekuja kutuangamiza?
Ninakujua wewe ni nani. Wewe ndiwe Aliye Mtakatifu
wa Mungu!" 35 Basi Isa akamkemea yule pepo
mchafu, akamwamuru, "Nyamaza! Mtoke mtu huyu!"
Yule pepo mchafu akamwangusha yule mtu chini
mbele yao wote, akatoka pasipo kumdhuru. 36 Watu
wote wakashangaa, wakaambiana, "Mafundisho haya
ni ya namna gani? Anawaamuru pepo wachafu kwa
mamlaka na nguvu, nao wanatoka!" 37 Habari zake
zikaanza kuenea kila mahali katika sehemu ile. 38
Isa akatoka katika sinagogi, akaenda nyumbani mwa
Simoni. Basi huko alimkuta mama mkwe wa Simoni
akiwa ameshikwa na homa kali, nao wakamwomba
Isa amsaidie. 39 Hivyo Isa akamwinamia na kukemea
ile homa, nayo ikamwacha. Akaamka mara moja, naye
akaanza kuwahudumia. 40 Jua lilipokuwa linatua, watu
wakamletea Isa watu wote waliokuwa na maradhi
mbalimbali, naye akaweka mikono yake juu ya kila
mgonjwa, naye akawaponya. 41 Pepo wachafu pia
wakawatoka watu wengi, nao walipokuwa wakitoka
wakapiga kelele, wakisema: "Wewe ni Mwana
wa Mungu!" Lakini Isa akawakemea na kuwazuia
wasiseme, kwa maana walimjua kuwa yeye ndiye Al-
Masihi. 42 Kesho yake, kulipopambazuka, Isa alienda
mahali pa faragha. Watu wengi wakawa wanamtafuta
kila mahali, nao walipomwona wakajaribu kumzuia
asiondoke. 43 Lakini yeye akawaambia, "Imenipasa
kuhubiri Habari Njema ya ufalme wa Mungu katika miji
mingine pia, kwa maana kwa kusudi hili nilitumwa."
44 Naye aliendelea kuhubiri katika masinagogi ya
Yudea.

**5** Siku moja Isa alipokuwa amesimama karibu na
Ziwa la Genesareti, watu wengi walimsonga ili
wapate kusikia neno la Mungu. 2 Akaona mashua mbili
ukingoni mwa ziwa, zikiwa zimeachwa hapo na wavuvi
waliokuwa wanaosha nyavu zao. 3 Akaingia katika
mojawapo ya hizo mashua ambayo ilikuwa ya Simoni,
akamwomba aisogeze ndani ya maji kidogo kutoka
ufuoni. Kisha akaketi na kufundisha watu akiwa mle
ndani ya mashua. 4 Alipomaliza kunena, akamwambia
Simoni, "Sasa peleka mashua hadi kilindini kisha
mshushe nyavu zenu mkavue samaki." 5 Simoni
akamjibu, "Bwana, tumefanya kazi ya kuchosha usiku
kucha na hatukuvua chochote. Lakini, kwa neno
lako nitazishusha nyavu." 6 Nao walipozishusha
nyavu zao, wakavua samaki wengi sana, nyavu
zao zikajaa zikaanza kukatika. 7 Wakawaashiria
wavuvi wenzao kwenye ile mashua nyingine ili waje
kuwasaidia. Wakaja, wakajaza mashua zote mbili
samaki hata zikaanza kuzama. 8 Simoni Petro
alipoona haya yaliyotukia, alianguka miguuni pa Isa
na kumwambia, "Bwana, ondoka kwangu. Mimi ni
mtu mwenye dhambi!" 9 Kwa kuwa yeye na wavuvi
wenzake walikuwa wameshangazwa sana na wingi wa
samaki waliokuwa wamepata. 10 Vivyo hivyo wenzake
Simoni, yaani Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo,
walishangazwa pia. Ndipo Isa akamwambia Simoni,
"Usiogope, tangu sasa utakuwa mvuvi wa watu." 11
Hivyo wakasogeza mashua zao hadi ufuoni mwa
bahari, wakaacha kila kitu na kumfuata. 12 Ikawa
siku moja Isa alipokuwa katika mji fulani, mtu mmoja
mwenye ukoma mwili mzima akamjia. Alipomwona Isa,
alianguka chini hadi uso wake ukagusa ardhi, akamsihi
akisema, "Bwana, ukitaka, unaweza kunitakasa." 13
Isa akanyoosha mkono wake, akamgusa yule mtu,
akamwambia, "Nataka. Takasika!" Na mara ukoma
wake ukatakasika. 14 Isa akamwagiza akisema,
"Usimwambie mtu yeyote, bali nenda ukajioneshe
kwa kuhani na ukatoe sadaka alizoagiza Musa kwa
utakaso wako, ili kuwa ushuhuda kwao." 15 Lakini

habari zake Isa zikazidi sana kuenea kotekote kuliko
wakati mwingine wowote. Makundi makubwa ya watu
walikuwa wakikusanyika ili kumsikiliza na kuponywa
magonjwa yao. 16 Lakini mara kwa mara Isa alijitenga
nao ili kwenda mahali pa faragha kuomba. 17
Siku moja Isa alipokuwa akifundisha, Mafarisayo na
walimu wa Torati, waliokuwa wametoka kila kijiji cha
Galilaya na kutoka Yudea na Yerusalemu, walikuwa
wameketi huko. Nao uweza wa Mwenyezi Mungu
ulikuwa juu yake kuponya wagonjwa. 18 Wakaja watu
wamembeba mgonjwa aliyepooza kwenye mkeka.
Wakajaribu kumwingiza ndani ili wamweke mbele ya
Isa. 19 Walipokuwa hawawezi kufanya hivyo kwa
sababu ya umati wa watu, wakapanda juu ya paa,
wakaondoa baadhi ya matofali, wakamteremsha yule
mgonjwa kwa mkeka wake hadi katikati ya umati
ule pale mbele ya Isa. 20 Isa alipoiona imani yao,
akamwambia yule mgonjwa, “Rafiki, dhambi zako
zimesamehewa.” 21 Mafarisayo na wale walimu
wa Torati wakaanza kuuliza, “Ni nani mtu huyu
anayesema maneno ya kukufuru? Ni nani awezaye
kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?”
22 Isa akijua mawazo yao akawauliza, “Kwa nini
mnawaza hivyo mioyoni mwenu? 23 Je, ni lipi lililo
rahisi zaidi, kumwambia, ‘Umesamehewa dhambi
zako,’ au kusema, ‘Inuka, uende’? 24 Lakini ili
mpate kujua kwamba Mwana wa Adamu anayo
mamlaka duniani kusamehe dhambi.” Akamwambia
yule aliyepooza, “Nakuambia, inuka, chukua mkeka
wako, uende nyumbani mwako.” 25 Mara yule mtu
aliyekuwa amepooza akasimama mbele yao wote,
akachukua mkeka wake, akaenda zake nyumbani,
huku akimtukuza Mungu. 26 Kila mmoja akashangaa
na kumtukuza Mungu. Wakajawa na hofu ya Mungu,
wakasema, “Leo tumeona mambo ya ajabu.” 27 Baada
ya haya, Isa alitoka na kumwona mtoza ushuru mmoja
jina lake Lawi akiwa amekaa forodhani, mahali pake
pa kutoza ushuru. Akamwambia, “Nifuate.” 28 Naye
Lawi akaacha kila kitu, akaondoka, akamfuata. 29
Kisha Lawi akamfanyia Isa karamu kubwa nyumbani
mwake, nao umati mkubwa wa watoza ushuru na
watu wengine walikuwa wakila pamoja nao. 30
Lakini Mafarisayo na walimu wa Torati waliokuwa
wa dhehebu lao wakawalalamikia wanafunzi wa Isa,
wakisema, “Mbona mnakula na kunywa pamoja na
watoza ushuru na wenye dhambi?” 31 Isa akawajibu,
“Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa.
32 Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi
wapate kutubu.” 33 Wakamwambia Isa, “Wanafunzi wa
Yahya na wa Mafarisayo mara kwa mara hufunga na
kuomba, lakini wanafunzi wako wanaendelea kula na
kunywa.” 34 Isa akawajibu, “Je, mnaweza kuwafanya
wageni wa bwana arusi kufunga wakati yuko pamoja
nao? 35 Lakini wakati utafika ambapo bwana arusi
ataondolewa kwao. Hapo ndipo watakapofunga.” 36
Isa akawapa mfano huu, akawaambia: “Hakuna mtu
achanaye kiraka kwenye nguo mpya na kukishonea
kwenye nguo iliyochakaa. Akifanya hivyo, atakuwa
amechana nguo mpya, na kile kiraka hakitalingana
na ile nguo iliyochakaa. 37 Hakuna mtu awekaye
divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Akifanya hivyo,
hiyo divai mpya itavipasua hivyo viriba, nayo yote
itamwagika. 38 Divai mpya lazima iwekwe kwenye
viriba vipya. 39 Wala hakuna mtu anayependelea
divai mpya baada ya kunywa divai ya zamani, bali
husema, ‘Ile ya zamani ni nzuri zaidi.’”

6 Ikawa siku moja ya Sabato Isa alikuwa akipita
katika mashamba ya nafaka, nao wanafunzi wake
wakaanza kuvunja masuke ya nafaka, wakayafikicha
kwa mikono yao na kula punje zake. 2 Baadhi ya
Mafarisayo wakawauliza, “Mbona mnafanya mambo
yasiyo halali kufanywa siku ya Sabato?” 3 Isa
akawajibu, “Je, ninyi hamjasoma alivyofanya Daudi
wakati yeye na wenzake walikuwa na njaa? 4 Aliingia
ndani ya nyumba ya Mungu, akaichukua na kuila ile
mikate iliyowekwa wakfu, ambayo ni halali kuliwa na
makuhani tu. Naye pia akawapa wenzake.” 5 Kisha
Isa akawaambia, “Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa
Sabato.” 6 Ikawa siku nyingine ya Sabato, Isa aliingia
ndani ya sinagogi na akawa anafundisha. Huko
palikuwa na mtu ambaye mkono wake wa kuume
ulikuwa umepooza. 7 Mafarisayo na walimu wa Torati
walikuwa wakitafuta sababu ya kumshtaki Isa. Kwa
hivyo wakawa wanamwangalia sana ili waone kama
ataponya katika siku ya Sabato. 8 Lakini Isa alijua
mawazo yao, hivyo akamwambia yule mtu mwenye
mkono uliopooza, “Inuka usimame mbele ya watu
wote.” Hivyo yule mtu akainuka, akasimama mbele yao
wote. 9 Ndipo Isa akawaambia wale walimu wa Torati
na Mafarisayo, “Nawauliza ninyi, ni lipi lililo halali siku
ya Sabato? Ni kutenda mema au kutenda mabaya? Ni
kuokoa maisha au kuyaangamiza?” 10 Akawatazama

watu wote waliokuwepo, kisha akamwambia yule mtu,
“Nyoosha mkono wako!” Akaunyoosha, na mkono
wake ukawa umeponywa kabisa. **11** Wale wakuu
wakakasirika sana, wakashauriana wao kwa wao ni
nini watakachomtendea Isa. **12** Ikawa katika siku hizo
Isa alienda mlimani kuomba, akakesha usiku kucha
akimwomba Mungu. **13** Kulipopambazuka, akawaita
wanafunzi wake, naye akachagua kumi na wawili,
ambao pia aliwaita mitume: **14** Simoni (aliyemwita
Petro) na Andrea nduguye, Yakobo, Yohana, Filipo,
Bartholomayo, **15** Mathayo, Tomaso, Yakobo mwana
wa Alfayo, Simoni aliyeitwa Zelote, **16** Yuda mwana
wa Yakobo, na Yuda Iskariote, aliyekuwa msaliti. **17**
Akashuka pamoja nao, akasimama mahali penye
uwanja tambarare. Hapo palikuwa na idadi kubwa ya
wanafunzi wake na umati mkubwa wa watu kutoka
sehemu zote za Yudea, kutoka Yerusalemu, na kutoka
pwani ya Tiro na Sidoni. **18** Walikuwa wamekuja
kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. Wale
waliokuwa wakiteswa na pepo wachafu akawaponya.
**19** Watu wote walikuwa wanajitahidi kumgusa kwa
sababu nguvu zilikuwa zikimtoka na kuwaponya
wote. **20** Akawatazama wanafunzi wake, akasema:
“Mmebarikiwa ninyi mlio maskini, kwa sababu ufalme
wa Mungu ni wenu. **21** Mmebarikiwa ninyi mlio na njaa
sasa, kwa sababu mtashibishwa. Mmebarikiwa ninyi
mnaolia sasa, kwa sababu mtacheka. **22** Mmebarikiwa
ninyi, watu watakapowachukia, watakapowatenga
na kuwatukana na kulikataa jina lenu kama neno
ovu, kwa ajili ya Mwana wa Adamu. **23** “Furahini na
kurukaruka kwa shangwe, kwa sababu thawabu yenu
ni kubwa mbinguni, kwa kuwa hivyo ndivyo baba zao
walivyowatenda manabii. **24** “Lakini ole wenu ninyi mlio
matajiri, kwa sababu mmekwisha kupokea faraja yenu.
**25** Ole wenu ninyi mlioshiba sasa, maana mtaona njaa.
Ole wenu ninyi mnaocheka sasa, maana mtaomboleza
na kulia. **26** Ole wenu watu watakapowasifu, kwani
ndivyo baba zao walivyowasifu manabii wa uongo.
**27** “Lakini nawaambia ninyi mnaonisikia: Wapendeni
adui zenu. Watendeeni mema wanaowachukia.
**28** Wabarikini wale wanaowalaani, waombeeni
wale wanaowatendea mabaya. **29** Kama mtu
akikupiga shavu moja, mgeuzie na la pili pia. Mtu
akikunyang’anya koti lako, usimzuie kuchukua joho
pia. **30** Mpe kila akuombaye, na kama mtu akichukua
mali yako usitake akurudishie. **31** Watendeeni wengine
kama ambavyo mngetaka wawatendee ninyi. **32**
“Mkiwapenda tu wale wanaowapenda, mwapata
sifa gani? Hata wenye dhambi huwapenda wale
wanaowapenda. **33** Tena mkiwatendea mema wale
tu wanaowatendea ninyi mema, mwapata sifa gani?
Hata wenye dhambi hufanya vivyo hivyo. **34** Tena
mnapowakopesha wale tu mnaotegemea wawalipe,
mwapata sifa gani? Hata wenye dhambi huwakopesha
wenye dhambi wenzao wakitarajia kulipwa mali yao
yote. **35** Lakini wapendeni adui zenu, watendeeni
mema, wakopesheni bila kutegemea kurudishiwa
mlichokopesha. Ndipo thawabu yenu itakapokuwa
kubwa, nanyi mtakuwa wana wa Aliye Juu Sana, kwa
sababu yeye ni mwema kwa watu wasio na shukrani
na kwa wale waovu. **36** Kuweni na huruma, kama
Baba yenu alivyo na huruma. **37** “Msihukumu, nanyi
hamtahukumiwa. Msilaumu, nanyi hamtalaumiwa.
Sameheni, nanyi mtasamehewa. **38** Wapeni watu vitu,
nanyi mtapewa. Kipimo cha kujaa na kushindiliwa
na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu
watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile
mpimacho, ndicho mtakachopimiwa.” **39** Pia akawapa
mfano akasema, “Je, kipofu aweza kumwongoza
kipofu? Je, wote wawili hawatatumbukia shimoni?
**40** Mwanafunzi hawezi kumzidi mwalimu wake, ila
yule aliyehitimu aweza kuwa kama mwalimu wake.
**41** “Mbona unatazama kibanzi kilicho ndani ya jicho
la ndugu yako, wala huoni boriti iliyo ndani ya jicho
lako mwenyewe? **42** Utawezaje kumwambia ndugu
yako, ‘Ndugu yangu, acha nitoe kibanzi kilicho ndani
ya jicho lako,’ wakati wewe mwenyewe huoni boriti
iliyo ndani ya jicho lako? Ewe mnafiki, ondoa boriti
ndani ya jicho lako kwanza, ndipo utaweza kuona
dhahiri jinsi ya kuondoa kibanzi kilicho ndani ya jicho
la ndugu yako. **43** “Hakuna mti mzuri uzaao matunda
mabaya, wala hakuna mti mbaya uzaao matunda
mazuri. **44** Kila mti hujulikana kwa matunda yake.
Kwa maana watu hawachumi tini kwenye miiba,
wala zabibu kwenye michongoma. **45** Vivyo hivyo
mtu mwema hutoa mambo mema kutoka hazina
ya moyo wake, naye mtu mwovu hutoa mambo
maovu kutoka hazina ya moyo wake. Kwa kuwa mtu
hunena kwa kinywa chake yale yaliyoujaza moyo
wake. **46** “Kwa nini mnaniita, ‘Bwana, Bwana,’ nanyi
hamfanyi ninayowaambia? **47** Nitawaonesha jinsi
alivyo mtu yule anayekuja kwangu na kusikia maneno

yangu na kuyatenda. 48 Yeye ni kama mtu aliyejenga
nyumba, akachimba chini sana, na kuweka msingi
kwenye mwamba. Mafuriko yalipokuja, mkondo wa
maji ukaipiga ile nyumba, lakini haikutikisika, kwa
sababu ilikuwa imejengwa vizuri. 49 Lakini yeye
anayesikia maneno yangu wala asiyatende, ni kama
mtu aliyejenga nyumba juu ya ardhi bila kuweka
msingi. Mafuriko yalipoikumba nyumba ile, ikaanguka
mara na kubomoka kabisa.”

**7** Baada ya Isa kumaliza kusema haya yote kwa watu
waliokuwa wanamsikiliza, akaingia Kapernaumu.
2 Mtumishi wa jemadari mmoja Mrumi, ambaye bwana
wake alimthamini sana, alikuwa mgonjwa sana karibu
na kufa. 3 Jemadari huyo aliposikia habari za Isa,
aliwatuma wazee wa Wayahudi kwake, wakamwomba
aje kumponya mtumishi wa huyo jemadari. 4 Wale
wazee walipofika kwa Isa, wakamsihi sana amsaidie
yule jemadari wakisema, “Mtu huyu anastahili wewe
umfanyie jambo hili, 5 kwa sababu analipenda taifa letu
tena ametujengea sinagogi.” 6 Hivyo Isa akaongozana
nao. Lakini alipokuwa hayuko mbali na nyumbani,
yule jemadari akatuma rafiki zake kumwambia Isa,
“Bwana, usijisumbue, kwani mimi sistahili wewe
kuingia chini ya dari yangu. 7 Ndiyo maana sikujiona
hata ninastahili kuja kwako wewe. Lakini sema neno
tu, naye mtumishi wangu atapona. 8 Kwa kuwa mimi
mwenyewe ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka,
nikiwa na askari chini yangu. Nikimwambia huyu,
‘Nenda,’ yeye huenda; na mwingine nikimwambia,
‘Njoo,’ yeye huja. Nikimwambia mtumishi wangu,
‘Fanya hivi,’ yeye hufanya.” 9 Isa aliposikia maneno
haya, alishangazwa naye sana. Akageukia umati
ule wa watu waliokuwa wanamfuata, akawaambia,
“Sijaona imani kubwa namna hii hata katika Israeli.”
10 Nao wale watu waliokuwa wametumwa kwa
Isa waliporudi nyumbani walimkuta yule mtumishi
amepona. 11 Baadaye kidogo, Isa alienda katika
mji mmoja ulioitwa Naini. Nao wanafunzi wake na
umati mkubwa wa watu walienda pamoja naye. 12
Alipokaribia lango la mji, alikutana na watu waliokuwa
wamebeba maiti wakitoka nje ya mji. Huyu aliyekufa
alikuwa mwana pekee wa mwanamke mjane. Umati
mkubwa wa watu wa mji ule walikuwa pamoja
na huyo mwanamke. 13 Bwana Isa alipomwona
yule mjane, moyo wake ulimhurumia, akamwambia,
“Usilie.” 14 Kisha akalikaribia jeneza, akaligusa. Nao
wale waliokuwa wamelibeba wakasimama. Akasema,
“Kijana, nakuambia, inuka.” 15 Yule aliyekuwa amekufa
akaketi akaanza kuongea, naye Isa akamkabidhi
kwa mama yake. 16 Watu wote wakajawa na hofu
ya Mungu, nao wakamtukuza Mungu wakisema,
“Nabii mkuu ametokea miongoni mwetu. Mungu
amekuja kuwakomboa watu wake.” 17 Habari hizi
za mambo aliyoyafanya Isa zikaenea Yudea yote
na sehemu zote za jirani. 18 Wanafunzi wa Yahya
wakamweleza Yahya mambo haya yote. Hivyo Yahya
akawaita wanafunzi wake wawili 19 na kuwatuma
kwa Bwana Isa ili kumuuliza, “Wewe ndiwe yule
aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?” 20 Wale
watu walipofika kwa Isa wakamwambia, “Yahya
ametutuma tukuulize, ‘Wewe ndiwe yule aliyekuwa
aje, au tumtazamie mwingine?’” 21 Wakati huo
huo, Isa aliwaponya wengi waliokuwa na magonjwa,
maradhi na pepo wachafu, na pia akawafungua vipofu
wengi macho wakapata kuona. 22 Hivyo akawajibu
wale wajumbe, “Rudini mkamwambie Yahya yote
mnayoyaona na kuyasikia: Vipofu wanapata kuona,
viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakaswa,
viziwi wanasikia, wafu wanafufuliwa na maskini
wanahubiriwa Habari Njema. 23 Amebarikiwa mtu
yule asiyechukizwa na mimi.” 24 Wajumbe wa
Yahya walipoondoka, Isa akaanza kusema na umati
wa watu kuhusu Yahya. Akawauliza, “Mlipoenda
kule nyikani, mlienda kuona nini? Je, ni unyasi
ukipeperushwa na upepo? 25 Kama sivyo, mlienda
kuona nini basi? Mtu aliyevaa mavazi ya kifahari? La
hasha! Watu wanaovaa mavazi ya kifahari na kuishi
maisha ya anasa wako katika majumba ya kifalme.
26 Lakini mlienda kuona nini? Mlienda kumwona
nabii? Naam, nawaambia, yeye ni zaidi ya nabii.
27 Huyu ndiye ambaye habari zake zimeandikwa:
“‘Tazama, nitamtuma mjumbe wangu mbele yako,
atakayetengeneza njia mbele yako.’ 28 Nawaambia,
miongoni mwa wale waliozaliwa na wanawake, hakuna
aliye mkuu kuliko Yahya. Lakini yeye aliye mdogo
kabisa katika ufalme wa Mungu ni mkuu kuliko Yahya.”
29 (Watu wote, hata watoza ushuru, waliposikia
maneno ya Isa, walikubali kwamba mpango wa Mungu
ni haki, maana walikuwa wamebatizwa na Yahya. 30
Lakini Mafarisayo na wataalamu wa Torati walikataa
mpango wa Mungu kwao kwa kutokubali kubatizwa
na Yahya.) 31 Isa akawauliza, “Niwafananishe na

nini watu wa kizazi hiki? Wanafanana na nini? 32
Wao ni kama watoto waliokaa sokoni wakiitana
wao kwa wao, wakisema: "'Tuliwapigia filimbi, lakini
hamkucheza; tuliwaimbia nyimbo za maombolezo,
lakini hamkulia.' 33 Kwa maana Yahya alikuja,
alikuwa hali mkate wala hanywi divai, nanyi mkasema,
'Yeye ana pepo mchafu.' 34 Mwana wa Adamu
alikuja akila na kunywa, nanyi mnasema: 'Tazameni
huyu mlafi na mlevi, rafiki wa watoza ushuru na
"wenye dhambi."' 35 Lakini hekima huthibitishwa
kuwa kweli na watoto wake wote." 36 Basi Farisayo
mmoja alimwalika Isa kwake ale chakula. Hivyo Isa
akaenda nyumbani mwa yule Farisayo na kuketi
mezani. 37 Palikuwa na mwanamke mmoja katika
mji ule aliyekuwa mwenye dhambi. Alipopata habari
kwamba Isa alikuwa akila chakula nyumbani mwa
yule Farisayo, akaleta chupa ya marhamu yenye
manukato. 38 Yule mwanamke akasimama nyuma
ya miguu ya Isa akilia. Akailowanisha miguu yake
kwa machozi yake, kisha akaifuta kwa nywele zake,
akaibusu na kuimiminia manukato. 39 Yule Farisayo
aliyemwalika Isa alipoona yanayotendeka, akawaza
moyoni mwake, "Kama huyu mtu angekuwa nabii,
angejua kwamba ni nani anayemgusa, na kwamba
yeye ni mwanamke wa namna gani, na ya kuwa huyu
mwanamke ni mwenye dhambi." 40 Isa akamjibu,
"Simoni, nina jambo la kukuambia." Simoni akajibu,
"Mwalimu, sema." 41 "Palikuwa na mtu mmoja
aliyewakopesha watu wawili fedha: Mmoja alidaiwa
dinari mia tano na mwingine dinari hamsini. 42
Wote wawili walipokuwa hawawezi kulipa, aliyafuta
madeni yao wote wawili. Sasa ni yupi kati yao
atakayempenda zaidi yule aliyewasamehe?" 43
Simoni akajibu, "Nadhani ni yule aliyesamehewa deni
kubwa zaidi." Naye Isa akamwambia, "Umehukumu
kwa usahihi." 44 Kisha akamgeukia yule mwanamke,
akamwambia Simoni, "Je, unamwona mwanamke
huyu? Nilipoingia nyumbani mwako, hukunipa maji
ya kunawa miguu yangu, lakini huyu ameninawisha
miguu kwa machozi yake, na kunifuta kwa nywele
zake. 45 Hukunisalimu kwa busu, lakini huyu
mwanamke hajaacha kuibusu miguu yangu tangu
nilipoingia. 46 Hukunipaka mafuta kichwani mwangu,
lakini yeye ameipaka miguu yangu manukato. 47
Kwa hiyo, nakuambia, dhambi zake zilizokuwa nyingi
zimesamehewa, kwani ameonesha upendo mwingi.
Lakini yule aliyesamehewa kidogo, hupenda kidogo."
48 Kisha akamwambia yule mwanamke, "Dhambi zako
zimesamehewa." 49 Lakini wale waliokuwa wameketi
pamoja naye chakulani wakaanza kusemezana wao
kwa wao, "Huyu ni nani ambaye hata anasamehe
dhambi?" 50 Isa akamwambia yule mwanamke, "Imani
yako imekuokoa; nenda kwa amani."

8 Baada ya haya Isa alienda, akawa anazunguka
katika miji na vijiji akihubiri Injili ya ufalme wa
Mungu. Wale wanafunzi wake kumi na wawili walikuwa
pamoja naye, 2 pia baadhi ya wanawake waliokuwa
wametolewa pepo wachafu na kuponywa magonjwa.
Miongoni mwao alikuwa Mariamu Magdalene,
aliyetolewa pepo wachafu saba; 3 Yoana mkewe
Kuza, msimamizi wa nyumba ya watu wa nyumbani
mwa Herode; Susana; na wengine wengi waliokuwa
wakimhudumia kwa mali yao. 4 Umati mkubwa wa
watu walipokuwa wakikusanyika, nao watu walikuwa
wakimjia Isa kutoka kila mji, akawaambia mfano
huu: 5 "Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake.
Alipokuwa akitawanya mbegu, nyingine zilianguka
kando ya njia; zikakanyagwa, nao ndege wa angani
wakazila. 6 Mbegu nyingine zilianguka penye miamba,
nazo zilipoota, hiyo mimea ikakauka kwa kukosa
unyevu. 7 Nazo mbegu nyingine zilianguka kwenye
miiba, nayo ile miiba ikakua pamoja nazo, na kuisonga
hiyo mimea. 8 Mbegu nyingine zilianguka kwenye
udongo mzuri. Zikaota na kuzaa mara mia moja zaidi
ya mbegu alizopanda." Baada ya kusema haya, Isa
akapaza sauti, akasema, "Mwenye masikio ya kusikia,
na asikie." 9 Wanafunzi wake wakamuuliza maana
ya mfano huo. 10 Naye akasema, "Ninyi mmepewa
ujuzi wa siri za ufalme wa Mungu, lakini kwa wengine
nazungumza kwa mifano, ili, "'ingawa wanatazama,
wasione; ingawa wanasikiliza, wasielewe.' 11 "Maana
ya mfano huu ni hii: Mbegu ni neno la Mungu. 12 Zile
zilizoanguka kando ya njia ni wale ambao husikia
neno, naye ibilisi anakuja na kuliondoa neno kutoka
mioyoni mwao, ili wasije wakaamini na kuokoka. 13
Zile mbegu zilizoanguka kwenye mwamba ni wale
ambao hulipokea neno kwa furaha wanapolisikia,
lakini hawana mizizi. Wanaamini kwa muda mfupi,
lakini wakati wa kujaribiwa huiacha imani. 14 Zile
mbegu zilizoanguka kwenye miiba ni mfano wa wale
wanaosikia, lakini wanapoendelea husongwa na
masumbufu ya maisha haya, utajiri na anasa, nao

hawakui. 15 Lakini zile mbegu zilizoanguka kwenye
udongo mzuri ni mfano wa wale ambao hulisikia
neno la Mungu na kulishika kwa moyo mnyofu wa
utiifu, nao kwa kuvumilia kwingi huzaa matunda. 16
“Hakuna mtu awashaye taa na kuificha ndani ya
gudulia au kuiweka mvunguni mwa kitanda. Badala
yake, huiweka juu ya kinara, ili wale wanaoingia
ndani waone mwanga. 17 Kwa maana hakuna
jambo lolote lililofichika ambalo halitafichuliwa, wala
lolote lililositirika ambalo halitajulikana na kuwekwa
wazi. 18 Kwa hiyo, kuweni waangalifu mnavyosikia.
Kwa maana yeyote aliye na kitu atapewa zaidi.
Lakini yule asiye na kitu, hata kile anachodhani
anacho atanyang’anywa.” 19 Wakati mmoja mama
yake Isa na ndugu zake walikuja kumwona, lakini
hawakuweza kumfikia kwa sababu ya msongamano
wa watu. 20 Mtu mmoja akamwambia, “Mama yako
na ndugu zako wako nje wanataka kukuona.” 21 Isa
akamjibu, “Mama yangu na ndugu zangu ni wale
wote wanaolisikia neno la Mungu na kulifanya.” 22
Siku moja Isa alipanda ndani ya mashua pamoja
na wanafunzi wake, akawaambia, “Tuvukeni hadi
ng’ambo ya ziwa.” Nao wakaondoka. 23 Hivyo
walipokuwa wakienda, akalala usingizi. Dhoruba kali
ikatokea mle ziwani, hata mashua ikawa inajaa maji,
nao walikuwa katika hatari kubwa. 24 Wanafunzi wake
wakamwendea na kumwamsha, wakisema, “Bwana,
Bwana, tunaangamia!” Yeye akaamka, akaukemea
ule upepo na yale mawimbi; dhoruba ikakoma, nako
kukawa shwari. 25 Akawauliza wanafunzi wake,
“Imani yenu iko wapi?” Kwa woga na mshangao
wakaulizana, “Huyu ni nani, ambaye anaamuru hata
upepo na maji, navyo vikamtii?” 26 Basi wakafika
katika nchi ya Wagerasi, iliyo upande wa pili wa
ziwa kutoka Galilaya. 27 Isa aliposhuka kutoka
mashua na kukanyaga ufuoni, alikutana na mtu
mmoja wa mji ule aliyekuwa amepagawa na pepo
mchafu, naye kwa muda mrefu alikuwa havai nguo
wala kuishi nyumbani, bali aliishi makaburini. 28
Alipomwona Isa, alipaza sauti, akajitupa chini mbele
yake na kusema kwa sauti kuu, “Una nini nami,
Isa, Mwana wa Mungu Aliye Juu Sana? Nakuomba,
usinitese!” 29 Wakati huo Isa alikuwa amemwamuru
yule pepo mchafu amtoke huyo mtu. Mara nyingi
huyo pepo mchafu alimpagaa, na hata alipofungwa
kwa minyororo mikono na miguu na kuwekwa chini ya
ulinzi, alikata hiyo minyororo na kupelekwa na huyo
pepo mchafu kwenda nyikani. 30 Isa akamuuliza,
“Jina lako ni nani?” Akamjibu, “Legioni,” kwa kuwa
alikuwa ameingiwa na pepo wachafu wengi mno. 31
Wale pepo wachafu wakamsihi sana asiwaamuru
kwenda katika Shimo. **(Abyssos g12)** 32 Palikuwa na
kundi kubwa la nguruwe hapo likilisha kando ya
kilima. Wale pepo wachafu wakamsihi Isa awaruhusu
wawaingie hao nguruwe, naye akawaruhusu. 33 Wale
pepo wachafu walipomtoka yule mtu, wakawaingia
wale nguruwe, nalo kundi lote likateremkia gengeni
kwa kasi, likatumbukia ziwani na kuzama. 34 Wale
watu waliokuwa wakichunga lile kundi la nguruwe
walipoona yaliyotukia, wakakimbia, wakaeneza habari
hizi mjini na mashambani. 35 Nao watu wakatoka
kwenda kujionea wenyewe yaliyotukia. Walipofika
hapo alipokuwa Isa, wakamkuta yule mtu aliyetokwa
na pepo wachafu amekaa karibu na Isa, akiwa
amevaa nguo na mwenye akili timamu! Wakaogopa.
36 Wale walioyaona mambo hayo wakawaeleza watu
wengine jinsi yule mtu aliyekuwa amepagawa na
pepo wachafu alivyoponywa. 37 Ndipo watu wote
wa nchi ile ya Wagerasi wakamwomba Isa aondoke
kwao, kwa sababu walikuwa wamejawa na hofu.
Basi akaingia katika mashua, akaondoka zake. 38
Yule mtu aliyetokwa na pepo wachafu akamsihi Isa
afuatane naye, lakini Isa akamuaga, akamwambia:
39 “Rudi nyumbani ukawaeleze mambo makuu
Mungu aliyokutendea.” Kwa hiyo yule mtu akaenda,
akatangaza katika mji wote mambo makuu ambayo
Isa alimtendea. 40 Basi Isa aliporudi, umati mkubwa
wa watu wakampokea kwa furaha, kwani walikuwa
wakimngojea. 41 Kisha mtu mmoja, jina lake Yairo,
aliyekuwa kiongozi wa sinagogi, akaja na kuanguka
miguuni mwa Isa, akimwomba afike nyumbani mwake,
42 kwa kuwa binti yake wa pekee, mwenye umri wa
miaka kumi na mbili, alikuwa anakufa. Isa alipokuwa
akienda, umati wa watu wakamsonga sana. 43
Palikuwa na mwanamke mmoja aliyekuwa na tatizo la
kutokwa damu kwa muda wa miaka kumi na mbili, [na
alikuwa amegharimia mali yake yote kwa matibabu]
lakini hakuna yeyote aliyeweza kumponya. 44 Huyo
mwanamke akaja kwa nyuma ya Isa na kugusa
upindo wa vazi lake. Mara kutokwa damu kwake
kukakoma. 45 Isa akauliza, “Ni nani aliyenigusa?”
Watu wote walipokana, Petro akasema, “Bwana,

umati huu wa watu wanakusonga na kukusukuma
kila upande." 46 Lakini Isa akasema, "Kuna mtu
aliyenigusa, kwa maana nimetambua kuwa nguvu
zimenitoka." 47 Yule mwanamke alipofahamu ya
kuwa hawezi kuendelea kujificha, alikuja akitetemeka,
akaanguka miguuni mwa Isa. Akaeleza mbele ya watu
wote kwa nini alimgusa na jinsi alivyoponywa mara
moja. 48 Basi Isa akamwambia, "Binti, imani yako
imekuponya. Nenda kwa amani." 49 Isa alipokuwa
bado anasema, akaja mtumishi kutoka nyumbani
mwa Yairo, yule kiongozi wa sinagogi, kumwambia,
"Binti yako amekwisha kufa. Usiendelee kumsumbua
Mwalimu." 50 Isa aliposikia jambo hili, akamwambia
Yairo, "Usiogope. Amini tu, naye binti yako atapona."
51 Walipofika nyumbani mwa Yairo, hakumruhusu mtu
yeyote aingie ndani naye isipokuwa Petro, Yohana
na Yakobo, pamoja na baba na mama wa yule binti.
52 Wakati ule ule watu wote walikuwa wakilia na
kuomboleza kwa ajili ya huyo binti. Isa akawaambia,
"Acheni kulia. Huyu binti hajafa, ila amelala." 53 Wao
wakamcheka kwa dharau, wakijua kuwa amekwisha
kufa. 54 Isa akamshika yule binti mkono na kuita,
"Binti, amka!" 55 Roho yake ikamrudia, naye akainuka
mara moja. Akaamuru apewe kitu cha kula. 56 Wazazi
wake wakastaajabu sana, lakini Isa akawakataza
wasimwambie mtu yeyote kuhusu yale yaliyotukia.

**9** Isa kisha akawaita wale kumi na wawili pamoja,
akawapa mamlaka na uwezo wa kutoa pepo
wachafu wote na kuponya magonjwa yote, 2 kisha
akawatuma waende wakahubiri ufalme wa Mungu
na kuponya wagonjwa. 3 Akawaagiza akisema,
"Msichukue chochote safarini: sio fimbo, wala mkoba,
wala mkate, wala fedha, hata msichukue kanzu
ya ziada. 4 Katika nyumba yoyote mwingiayo,
kaeni humo hadi mtakapoondoka katika mji huo.
5 Kama watu wasipowakaribisha, mnapoondoka
katika mji wao, kung'uteni mavumbi kutoka miguu
yenu ili kuwa ushuhuda dhidi yao." 6 Hivyo wale
wanafunzi wakaondoka wakaenda kutoka kijiji hadi
kijiji, wakihubiri habari njema na kuponya wagonjwa
kila mahali. 7 Basi Mfalme Herode, mtawala wa
Galilaya, alisikia habari za yote yaliyotendeka.
Naye akafadhaika, kwa kuwa baadhi ya watu
walikuwa wakisema Yahya amefufuliwa kutoka kwa
wafu. 8 Wengine wakasema Ilya amewatokea,
na wengine kwamba mmoja wa manabii wa kale
amefufuka. 9 Herode akasema, "Yahya nilimkata
kichwa. Lakini ni nani huyu ninayesikia mambo kama
haya kumhusu?" Akatamani sana kumwona. 10
Mitume wake waliporudi, wakamweleza Isa yote
waliyofanya. Kisha akaenda nao faraghani hadi
mji uitwao Bethsaida. 11 Lakini umati wa watu
wakafahamu alikoenda, wakamfuata. Akawakaribisha
na kunena nao kuhusu ufalme wa Mungu na
kuwaponya wale wote waliokuwa wanahitaji uponyaji.
12 Ilipokaribia jioni, wale mitume kumi na wawili
wakaenda kwa Isa na kumwambia, "Waage watu
hawa ili waende vijijini jirani na mashambani, ili
wapate chakula na mahali pa kulala, kwa maana
hapa tuko nyikani." 13 Isa akawajibu, "Ninyi wapeni
chakula." Nao wakajibu, "Tuna mikate mitano na
samaki wawili tu. Labda twende tukanunue chakula
cha kuwatosha watu hawa wote." 14 (Walikuwepo
wanaume wapatao elfu tano.) Isa akawaambia
wanafunzi wake, "Waketisheni katika vikundi vya watu
hamsini hamsini." 15 Wanafunzi wakafanya hivyo,
wakawaketisha wote. 16 Isa akaichukua ile mikate
mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni,
akavibariki na kuvimega. Kisha akawapa wanafunzi
ili wawagawie watu. 17 Wote wakala, wakashiba.
Nao wanafunzi wakakusanya vipande vilivyosalia,
wakajaza vikapu kumi na viwili. 18 Siku moja Isa
alipokuwa akiomba faraghani, nao wanafunzi wake
wakiwa pamoja naye, akawauliza, "Watu husema mimi
ni nani?" 19 Wakamjibu, "Baadhi husema wewe ni
Yahya, wengine husema ni Ilya, na wengine husema
kwamba ni mmoja wa manabii wa kale amefufuka." 20
Kisha akawauliza, "Je, ninyi mnasema mimi ni nani?"
Petro akajibu, "Wewe ndiwe Al-Masihi wa Mungu." 21
Isa akawakataza wasimwambie mtu yeyote jambo
hilo. 22 Isa akasema, "Imempasa Mwana wa Adamu
kupata mateso mengi na kukataliwa na wazee,
viongozi wa makuhani, na walimu wa Torati, na
itampasa auawe, lakini siku ya tatu kufufuliwa kutoka
mauti." 23 Kisha akawaambia wote, "Mtu yeyote
akitaka kunifuata, ni lazima ajikane mwenyewe,
auchukue msalaba wake kila siku, anifuate. 24 Kwa
maana yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake
atayapoteza, lakini yeyote atakayeyapoteza maisha
yake kwa ajili yangu atayaokoa. 25 Je, itamfaidi nini
mtu kuupata ulimwengu wote, lakini akapoteza au
kuangamiza nafsi yake? 26 Mtu yeyote akinionea

aibu mimi na maneno yangu, Mwana wa Adamu
naye atamwonea aibu atakapokuja katika utukufu
wake na katika utukufu wa Baba, pamoja na malaika
watakatifu. **27** “Amin, nawaambia, wako baadhi ya
watu waliosimama hapa ambao hawataonja mauti
kabla ya kuuona ufalme wa Mungu.” **28** Yapata
siku nane baada ya Isa kusema hayo, aliwachukua
Petro, Yohana na Yakobo, akaenda nao mlimani
kuomba. **29** Alipokuwa akiomba, sura ya uso wake
ikabadilika, nayo mavazi yake yakametameta kama
miali ya radi. **30** Ghafula wakawaona watu wawili, ndio
Musa na Ilya, wakizungumza naye. **31** Walionekana
katika utukufu wakizungumza na Isa kuhusu kifo
chake ambacho kingetokea huko Yerusalemu. **32**
Petro na wenzake walikuwa wamelala usingizi mzito.
Walipoamka, wakaona utukufu wa Isa na wale watu
wawili waliokuwa wamesimama pamoja naye. **33** Musa
na Ilya walipokuwa wanaondoka, Petro akamwambia
Isa, “Bwana, ni vizuri tukae hapa! Tutajenga vibanda
vitatu: kimoja chako, kingine cha Musa na kingine cha
Ilya.” Lakini Petro hakujua alichosema. **34** Alipokuwa
bado anazungumza, pakatokea wingu, likawafunika,
nao wakaogopa walipoingia mle kwenye wingu.
**35** Sauti ikatoka kwenye lile wingu ikisema, “Huyu
ni Mwanangu mpendwa, niliyemchagua. Msikieni
yeye.” **36** Baada ya sauti hiyo kusema, walimkuta
Isa akiwa peke yake. Wale wanafunzi wakalihifadhi
jambo hili, wala kwa wakati huo hawakumwambia
mtu yeyote yale waliyokuwa wameyaona. **37** Kesho
yake waliposhuka kutoka mlimani, alikutana na umati
mkubwa wa watu. **38** Mtu mmoja katika umati
ule akapaza sauti, akasema, “Mwalimu, naomba
umwangalie mwanangu, kwani ndiye mtoto wangu wa
pekee. **39** Mara kwa mara pepo mchafu humpagaa
na kumfanya apige mayowe, kisha humwangusha na
kumtia kifafa hata akatokwa na povu kinywani. Huyo
pepo mchafu anamtesa sana, na hamwachi ila mara
chache. **40** Niliwaomba wanafunzi wako wamtoe
huyo pepo mchafu, lakini hawakuweza.” **41** Isa
akawajibu, “Enyi kizazi kisichoamini na kilichopotoka!
Nitakaa nanyi na kuwavumilia hadi lini? Mlete mwanao
hapa.” **42** Hata yule mtoto alipokuwa akija, yule pepo
mchafu akamwangusha, akamtia kifafa. Lakini Isa
akamkemea yule pepo mchafu amtoke, akamponya
yule mtoto, na akamrudisha kwa baba yake. **43**
Watu wote wakastaajabia uweza mkuu wa Mungu.
Wakati bado watu walikuwa wanastaajabia hayo
yote aliyokuwa akiyafanya Isa, yeye akawaambia
wanafunzi wake: **44** “Sikilizeni kwa makini haya
nitakayowaambia sasa: Mwana wa Adamu atasalitiwa
na kutiwa mikononi mwa watu.” **45** Lakini wao
hawakuelewa alimaanisha nini. Maana ya maneno
hayo ilifichika kwao, hivyo hawakuyaelewa, nao
wakaogopa kumuuliza maana yake. **46** Kukazuka
mabishano miongoni mwa wanafunzi kuhusu ni
nani miongoni mwao atakayekuwa mkuu kuliko
wote. **47** Lakini Isa akayatambua mawazo yao, naye
akamchukua mtoto mdogo, akamsimamisha kando
yake. **48** Kisha akawaambia, “Yeyote amkaribishaye
mtoto huyu mdogo kwa Jina langu, anikaribisha
mimi, na yeyote atakayenikaribisha mimi, atakuwa
amemkaribisha yeye aliyenituma. Kwa maana yeye
aliye mdogo miongoni mwenu, ndiye aliye mkuu kuliko
wote.” **49** Yohana akasema, “Bwana, tumemwona
mtu akitoa pepo wachafu kwa jina lako, nasi
tukamzuia, kwa sababu yeye si mmoja wetu.” **50** Isa
akasema, “Msimzuie, kwa sababu yeyote ambaye
si kinyume nanyi, yu upande wenu.” **51** Wakati
ulipokaribia wa yeye kuchukuliwa mbinguni, alikaza
uso wake kwenda Yerusalemu. **52** Akatuma watu
wamtangulie, nao wakaenda katika kijiji kimoja cha
Samaria kumwandalia kila kitu; **53** lakini watu wa
kijiji kile hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa
anaenda zake Yerusalemu. **54** Wanafunzi wake, yaani
Yakobo na Yohana, walipoona hayo, wakasema:
“Bwana Isa, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili
uwaangamize?” **55** Isa akageuka na kuwakemea.
**56** Naye Isa na wanafunzi wake wakaenda kijiji
kingine. **57** Walipokuwa njiani wakienda, mtu mmoja
akamwambia Isa, “Nitakufuata popote utakakoenda.”
**58** Isa akamjibu, “Mbweha wana mapango, nao ndege
wa angani wana viota, lakini Mwana wa Adamu hana
mahali pa kulaza kichwa chake.” **59** Isa akamwambia
mtu mwingine, “Nifuate.” Mtu huyo akamjibu, “Bwana,
niruhusu kwanza nikamzike baba yangu.” **60** Isa
akamwambia, “Waache wafu wawazike wafu wao,
bali wewe nenda ukautangaze ufalme wa Mungu.”
**61** Mtu mwingine akamwambia, “Bwana, nitakufuata
lakini naomba kwanza nikawaage jamaa zangu.”
**62** Isa akamwambia, “Mtu yeyote ashikaye jembe
kulima kisha akatazama nyuma hafai kwa ufalme wa
Mungu.”

**10** Baada ya hayo, Bwana Isa akawachagua
wengine sabini na wawili, akawatuma wawili
wawili katika kila mji na kila sehemu aliyokusudia
kwenda baadaye. **2** Akawaambia, “Mavuno ni mengi,
lakini watendakazi ni wachache. Kwa hiyo mwombeni
Bwana wa mavuno, ili apeleke watendakazi katika
shamba lake la mavuno. **3** Nendeni! Tazama
ninawatuma kama wana-kondoo katikati ya mbwa-
mwitu. **4** Msichukue mkoba, wala mfuko, wala viatu,
na msimsalimu mtu yeyote njiani. **5** “Mkiingia katika
nyumba yoyote, kwanza semeni, ‘Amani iwe kwenu.’
**6** Kama kuna mtu wa amani humo, basi amani yenu
itakuwa juu yake. La sivyo, itawarudia. **7** Kaeni katika
nyumba hiyo, mkila na kunywa kile watakachowapa,
kwa sababu kila mtendakazi anastahili malipo yake.
Msihamehame kutoka nyumba hadi nyumba. **8**
“Mkienda katika mji na watu wake wakawakaribisha,
kuleni chochote kiwekwacho mbele yenu, **9** waponyeni
wagonjwa waliomo na waambieni: ‘Ufalme wa Mungu
umewakaribia.’ **10** Lakini mkiingia katika mji, nao
hawakuwakaribisha, tokeni mwende katika barabara
zake mkaseme: **11** ‘Hata mavumbi ya mji wenu
yaliyoshikamana na miguu yetu, tunayakung’uta
dhidi yenu. Lakini mjue kwamba ufalme wa Mungu
umekaribia.’ **12** Ninawaambia, itakuwa rahisi zaidi
kwa Sodoma kustahimili katika siku ile kuliko mji ule.
**13** “Ole wako Korazini! Ole wako Bethsaida! Kwa kuwa
kama miujiza iliyofanyika kwenu ingefanyika Tiro
na Sidoni, miji hiyo ingekuwa imetubu zamani, kwa
kuvaa magunia na kujipaka majivu. **14** Lakini itakuwa
rahisi zaidi kwa Tiro na Sidoni kustahimili katika siku
ya hukumu, kuliko ninyi. **15** Nawe Kapernaumu, je,
utainuliwa hadi mbinguni? La hasha! Utashushwa
hadi Kuzimu. **(Hadēs g86)** **16** “Yeye awasikilizaye ninyi
anisikiliza mimi; naye awakataaye ninyi amenikataa
mimi. Lakini yeye anikataaye mimi amkataa yeye
aliyenituma.” **17** Wale sabini na wawili wakarudi
kwa furaha, na kusema, “Bwana Isa, hata pepo
wachafu wanatutii kwa jina lako.” **18** Isa akawaambia,
“Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama
radi. **19** Tazama nimewapa mamlaka ya kukanyaga
nyoka na nge na juu ya nguvu zote za adui;
wala hakuna kitu chochote kitakachowadhuru. **20**
Basi, msifurahi kwa kuwa pepo wachafu wanawatii,
bali furahini kwa kuwa majina yenu yameandikwa
mbinguni.” **21** Wakati huo Isa akashangilia katika Roho
wa Mungu, akasema, “Nakuhimidi Baba, Bwana wa
mbingu na nchi, kwa kuwa umewaficha mambo haya
wenye hekima na wenye elimu, nawe ukawafunulia
watoto wadogo. Naam, Baba, kwa kuwa hivyo ndivyo
ilivyokupendeza. **22** “Nimekabidhiwa vitu vyote na
Baba yangu. Hakuna mtu amjuaye Mwana ni nani ila
Baba, wala hakuna amjuaye Baba ni nani ila Mwana
na yeyote ambaye Mwana anapenda kumfunulia.” **23**
Basi Isa akawageukia wanafunzi wake akanena nao
faraghani, akawaambia, “Heri macho yanayoona yale
mambo mnayoyaona. **24** Kwa maana nawaambia,
manabii wengi na wafalme walitamani kuona yale
mnayoyaona lakini hawakuyaona, na walitamani
kusikia yale mnayoyasikia lakini hawakuyasikia.” **25**
Wakati huo mtaalamu mmoja wa Torati alisimama
ili kumjaribu Isa, akamuuliza, “Mwalimu, nifanye
nini ili niurithi uzima wa milele?” **(aiōnios g166)** **26**
Isa akamjibu, “Imeandikwaje katika Torati? Kwani
unasoma nini humo?” **27** Akajibu, “‘Mpende Mwenyezi
Mungu, Mungu wako, kwa moyo wako wote, kwa
roho yako yote, kwa nguvu zako zote, na kwa
akili zako zote’; tena, ‘Mpende jirani yako kama
unavyojipenda mwenyewe.’” **28** Isa akamwambia,
“Umejibu vyema. Fanya hivyo nawe utaishi.” **29**
Lakini yule mtaalamu wa Torati, akitaka kujionesha
kuwa mwenye haki, akamuuliza Isa, “Jirani yangu ni
nani?” **30** Isa akamjibu akasema, “Mtu mmoja alikuwa
akiteremka kutoka Yerusalemu kwenda Yeriko, naye
akaangukia mikononi mwa wanyang’anyi. Wakampiga,
wakaondoka, wakamwacha akiwa karibu kufa. **31**
Kuhani mmoja alikuwa akipitia njia ile, alipomwona
huyo mtu, akapita upande mwingine, akamwacha hapo
barabarani. **32** Vivyo hivyo, Mlawi mmoja naye alipofika
mahali pale, alimwona, akapita upande mwingine,
akamwacha hapo barabarani. **33** Lakini Msamaria
mmoja aliyekuwa akisafiri alipomwona, alimhurumia.
**34** Akaenda alipokuwa na akasafisha majeraha yake
kwa divai na mafuta, kisha akayafunga. Ndipo
akampandisha kwenye punda wake, akampeleka
hadi kwenye nyumba ya wageni na kumtunza. **35**
Kesho yake, yule Msamaria akachukua dinari mbili
akampa yule mwenye nyumba ya wageni na kusema,
‘Mtunze, nami nirudipo nitakulipa gharama yoyote
ya ziada uliyotumia kwa ajili yake.’ **36** “Ni yupi
basi miongoni mwa hawa watatu wewe unadhani
ni jirani yake yule mtu aliyeangukia mikononi mwa

wanyang'anyi?" 37 Yule mtaalamu wa Torati akajibu,
"Ni yule aliyemhurumia." Ndipo Isa akamwambia,
"Nenda, ukafanye vivyo hivyo." 38 Ikawa Isa na
wanafunzi wake walipokuwa wakienda Yerusalemu,
akaingia kwenye kijiji kimoja ambapo mwanamke
mmoja aliyeitwa Martha alimkaribisha nyumbani
mwake. 39 Martha alikuwa na dada yake aliyeitwa
Mariamu, ambaye aliketi chini miguuni mwa Bwana
Isa akisikiliza yale alikuwa akisema. 40 Lakini Martha
alikuwa akihangaika na maandalizi yote yaliyokuwa
yafanyike. Martha akaja kwa Isa na kumuuliza,
"Bwana, hujali kwamba dada yangu ameniachia
kazi zote mwenyewe? Basi mwambie anisaidie." 41
Lakini Bwana Isa akamjibu, "Martha, Martha, mbona
unasumbuka na kuhangaika na mengi? 42 Lakini
kunahitajika kitu kimoja tu. Mariamu amechagua kile
kilicho bora, wala hakuna mtu atakayemwondolea."

**11** Siku moja, Isa alikuwa mahali fulani akiomba.
Alipomaliza kuomba, mmoja wa wanafunzi wake
akamwambia, "Bwana Isa, tufundishe kuomba, kama
vile Yahya alivyowafundisha wanafunzi wake." 2
Akawaambia, "Mnapoomba, semeni: "'Baba yetu
[uliye mbinguni], jina lako litukuzwe, ufalme wako uje.
[ Mapenzi yako yafanyike hapa duniani kama huko
mbinguni.] 3 Utupatie kila siku riziki yetu. 4 Utusamehe
dhambi zetu, kwa kuwa na sisi huwasamehe wote
wanaotukosea. Wala usitutie majaribuni [bali utuokoe
kutoka kwa yule mwovu].'" 5 Kisha akawaambia,
"Ni nani miongoni mwenu mwenye rafiki yake, naye
akamwendea usiku wa manane na kumwambia,
'Rafiki, nikopeshe mikate mitatu, 6 kwa sababu
rafiki yangu amekuja kutoka safarini, nami sina kitu
cha kumpa ale.' 7 "Kisha yule aliye ndani amjibu,
'Usinisumbue. Mlango umefungwa, nami na watoto
wangu tumelala. Siwezi kuamka nikupe chochote.' 8
Nawaambia, ingawa huyo mtu hataamka na kumpa
hiyo mikate kwa sababu ni rafiki yake, lakini kwa
sababu ya kuendelea kwake kuomba, ataamka na
kumpa kiasi anachohitaji. 9 "Kwa hiyo nawaambia:
Ombeni nanyi mtapewa; tafuteni nanyi mtapata;
bisheni nanyi mtafunguliwa mlango. 10 Kwa kuwa
kila aombaye hupewa; naye kila atafutaye hupata;
na kila abishaye hufunguliwa mlango. 11 "Je, kuna
baba yeyote miongoni mwenu ambaye mtoto wake
akimwomba samaki, atampa nyoka badala yake?
12 Au mtoto akimwomba yai atampa nge? 13 Basi
ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto
wenu vitu vizuri, si zaidi sana Baba yenu aliye
mbinguni atawapa Roho Mtakatifu wa Mungu wale
wamwombao!" 14 Basi Isa alikuwa anamtoa pepo
mchafu kutoka kwa mtu aliyekuwa bubu. Yule pepo
mchafu alipomtoka yule mtu aliyekuwa bubu, akaanza
kuongea, nao umati wa watu wakashangaa. 15 Lakini
wengine wakasema, "Anatoa pepo wachafu kwa
uwezo wa Beelzebuli, yule mkuu wa pepo wachafu
wote." 16 Wengine ili kumjaribu wakataka awaoneshe
ishara kutoka mbinguni. 17 Isa akajua mawazo
yao, naye akawaambia, "Kila ufalme ukigawanyika
dhidi yake wenyewe huangamia. Nayo nyumba
iliyogawanyika dhidi yake yenyewe itaanguka. 18
Kama Shetani amegawanyika mwenyewe, ufalme
wake utasimamaje? Nawaambia haya kwa sababu
ninyi mnadai ya kuwa mimi ninatoa pepo wachafu
kwa uwezo wa Beelzebuli. 19 Kama mimi natoa pepo
wachafu kwa nguvu za Beelzebuli, wafuasi wenu nao
je, wao hutoa pepo wachafu kwa uwezo wa nani?
Hivyo basi, wao ndio watakaowahukumu. 20 Lakini
kama mimi ninatoa pepo wachafu kwa kidole cha
Mungu, basi ufalme wa Mungu umewajia. 21 "Mtu
mwenye nguvu aliyejifunga silaha anapoilinda nyumba
yake, mali yake iko salama. 22 Lakini mtu mwenye
nguvu kuliko yeye akimshambulia na kumshinda, yeye
humnyang'anya silaha zake zote alizozitegemea, na
kuchukua nyara. 23 "Mtu asiyekuwa pamoja nami yu
kinyume nami, na mtu ambaye hakusanyi pamoja
nami, hutawanya. 24 "Pepo mchafu anapomtoka
mtu, hutangatanga katika sehemu zisizo na maji
akitafuta mahali pa kupumzika, lakini hapati. Ndipo
husema, 'Nitarudi kwenye nyumba yangu nilikotoka.'
25 Naye anaporudi na kuikuta ile nyumba imefagiwa
na kupangwa vizuri, 26 ndipo huenda na kuchukua
pepo wachafu wengine saba wabaya kuliko yeye
mwenyewe, nao huingia na kukaa humo. Nayo
hali ya mwisho ya yule mtu huwa ni mbaya kuliko
ile ya kwanza." 27 Ikawa Isa alipokuwa akisema
hayo, mwanamke mmoja katikati ya umati ule wa
watu akapaza sauti akasema, "Limebarikiwa tumbo
lililokuzaa na matiti uliyonyonya!" 28 Isa akajibu,
"Wamebarikiwa zaidi wale wanaolisikia neno la Mungu
na kulitii." 29 Umati wa watu walipokuwa wanazidi
kuongezeka, Isa akaendelea kusema, "Hiki ni kizazi
kiovu. Kinatafuta ishara, lakini hakitapewa ishara

yoyote isipokuwa ile ya Yona. 30 Kwa maana kama
vile Yona alivyokuwa ishara kwa watu wa Ninawi,
ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa ishara kwa
kizazi hiki. 31 Malkia wa Kusini atasimama wakati
wa hukumu na kuwahukumu watu wa kizazi hiki.
Kwa kuwa yeye alikuja kutoka miisho ya dunia ili
kuisikiliza hekima ya Sulemani. Na hapa yupo aliye
mkuu kuliko Sulemani. 32 Siku ya hukumu, watu
wa Ninawi watasimama pamoja na kizazi hiki na
kukihukumu; kwa maana wao walitubu waliposikia
mahubiri ya Yona. Na tazama, hapa yupo yeye aliye
mkuu kuliko Yona. 33 "Hakuna mtu yeyote awashaye
taa na kuiweka mahali palipofichika au kuifunikia
chini ya bakuli. Badala yake huiweka juu ya kinara
chake, ili watu wote wanaoingia waone nuru. 34
Jicho lako ni taa ya mwili wako. Kama jicho lako
ni zima, mwili wako wote pia umejaa nuru. Lakini
kama jicho ni bovu, mwili wako wote pia umejaa
giza. 35 Kwa hiyo, hakikisha kwamba nuru iliyo
ndani yako isiwe giza. 36 Basi ikiwa mwili wako wote
umejaa nuru, bila sehemu yake yoyote kuwa gizani,
basi utakuwa na nuru kama vile taa ikuangazavyo
kwa nuru yake." 37 Isa alipomaliza kuzungumza,
Farisayo mmoja alimwalika nyumbani mwake kwa
chakula. Isa akaingia na kuketi katika sehemu yake
mezani. 38 Yule Farisayo akashangaa kwamba Isa
hakunawa kwanza kabla ya kula. 39 Ndipo Bwana Isa
akamwambia, "Sasa, enyi Mafarisayo mnasafisha
kikombe na sahani kwa nje, lakini ndani mmejaa
unyang'anyi na uovu. 40 Enyi wapumbavu! Hamjui
kuwa yeye aliyetengeneza nje ndiye alitengeneza
na ndani pia? 41 Basi toeni sadaka ya vile mlivyo
navyo, na tazama, vitu vyote vitakuwa safi kwenu. 42
"Lakini ole wenu, Mafarisayo, kwa maana mnampa
Mungu zaka za mnanaa, mchicha na kila aina ya
mboga, lakini mnapuuza haki na upendo wa Mungu.
Iliwapasa kufanya haya ya pili bila kupuuza hayo ya
kwanza. 43 "Ole wenu Mafarisayo, kwa sababu ninyi
mnapenda kukalia viti vya mbele katika masinagogi,
na kusalimiwa kwa heshima masokoni. 44 "Ole wenu,
kwa sababu ninyi ni kama makaburi yasiyokuwa na
alama, ambayo watu huyakanyaga pasipo kujua."
45 Mtaalamu mmoja wa Torati akamjibu, akasema,
"Mwalimu, unaposema mambo haya, unatutukana na
sisi pia." 46 Isa akamjibu, "Nanyi wataalamu wa Torati,
ole wenu, kwa sababu mnawatwika watu mizigo
mizito ambayo hawawezi kubeba, wala ninyi wenyewe
hamwinui hata kidole kimoja kuwasaidia. 47 "Ole wenu,
kwa sababu ninyi mnajenga makaburi ya manabii
waliouawa na baba zenu. 48 Hivyo ninyi mwashuhudia
na mnathibitisha kile baba zenu walichofanya. Wao
waliwaua manabii, nanyi mnawajengea makaburi.
49 Kwa sababu ya jambo hili, Mungu katika hekima
yake alisema, 'Tazama, nitatuma kwao manabii na
mitume, nao watawaua baadhi yao na wengine
watawatesa.' 50 Kwa hiyo kizazi hiki kitawajibika
kwa ajili ya damu ya manabii iliyomwagwa tangu
kuwekwa misingi ya ulimwengu, 51 tangu damu
ya Habili hadi damu ya Zakaria, aliyeuawa kati ya
madhabahu na mahali patakatifu. Naam, nawaambia,
kizazi hiki kitawajibika kwa haya yote. 52 "Ole wenu
ninyi wataalamu wa Torati, kwa sababu mmeuondoa
ufunguo wa maarifa. Ninyi wenyewe hamkuingia,
na wale waliokuwa wanaingia mkawazuia." 53 Isa
alipoondoka huko, walimu wa Torati na Mafarisayo
wakaanza kumpinga vikali na kumsonga kwa maswali,
54 wakivizia kumkamata kwa kitu atakachosema ili
wamshtaki.

**12** Wakati huo, umati mkubwa wa watu maelfu
walipokuwa wamekusanyika hata wakawa
wanakanyagana, Isa akaanza kuzungumza kwanza
na wanafunzi wake, akawaambia: "Jihadharini na
chachu ya Mafarisayo, yaani unafiki wao. 2 Hakuna
jambo lolote lililositirika ambalo halitafunuliwa, au
lililofichwa ambalo halitajulikana. 3 Kwa hiyo,
lolote mlilosema gizani litasikiwa nuruni. Na kile
mlichonong'ona masikioni mkiwa kwenye vyumba
vya ndani, kitatangazwa juu ya paa. 4 "Nawaambieni
rafiki zangu, msiwaogope wale wauao mwili, lakini
baada ya hilo hawawezi kufanya lolote zaidi. 5 Lakini
nitawaambia nani wa kumwogopa: Mwogopeni yule
ambaye baada ya kuua mwili, ana mamlaka ya
kuwatupa motoni. Naam, nawaambia, mwogopeni
huyo! **(Geenna g1067)** 6 Mnajua kwamba shomoro
watano huuzwa kwa senti mbili? Lakini Mungu
hamsahau hata mmoja wao. 7 Naam, hata nywele za
vichwa vyenu zote zimehesabiwa. Hivyo msiogope,
kwa maana ninyi ni wa thamani kubwa kuliko shomoro
wengi. 8 "Ninawaambia kwamba yeyote atakayenikiri
mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye atamkiri mbele
za malaika wa Mungu. 9 Lakini yeye atakayenikana
mimi mbele ya watu, Mwana wa Adamu naye

atamkana mbele ya malaika wa Mungu. 10 Naye
kila atakayenena neno baya dhidi ya Mwana wa
Adamu atasamehewa, lakini yeyote atakayemkufuru
Roho Mtakatifu wa Mungu hatasamehewa. 11
“Watakapowapeleka katika masinagogi, na mbele ya
watawala na wenye mamlaka, msiwe na wasiwasi
kuhusu namna mtakavyojitetea au mtakavyosema.
12 Kwa maana Roho wa Mungu atawafundisha wakati
huo huo mnachopaswa kusema.” 13 Mtu mmoja
katika umati ule wa watu akamwambia Isa, “Mwalimu,
mwambie ndugu yangu tugawane naye urithi wetu.”
14 Lakini Isa akamwambia, “Rafiki, ni nani aliyeniweka
mimi kuwa hakimu wenu au msuluhishi juu yenu?” 15
Ndipo Isa akawaambia, “Jihadharini! Jilindeni na aina
zote za choyo. Kwa maana maisha ya mtu hayatokani
na wingi wa mali alizo nazo.” 16 Kisha akawaambia
mfano huu: “Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana.
17 Akawaza moyoni mwake, ‘Nifanye nini? Sina mahali
pa kuhifadhi mavuno yangu.’ 18 “Ndipo huyo tajiri
akasema, ‘Nitafanya hivi: Nitabomoa maghala yangu
ya nafaka na kujenga mengine makubwa zaidi na
nihifadhi mavuno yangu yote na vitu vyangu. 19 Nami
nitaiambia nafsi yangu, “Nafsi, unavyo vitu vingi vizuri
ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi. Pumzika; kula,
unywe, ufurahi.”’ 20 “Lakini Mungu akamwambia,
‘Mpumbavu wewe! Usiku huu uhai wako unatakiwa.
Sasa hivyo vitu ulivyojiwekea akiba vitakuwa vya
nani?’ 21 “Hivyo ndivyo ilivyo kwa wale wanaojiwekea
mali lakini hawajitajirishi kwa Mungu.” 22 Kisha Isa
akawaambia wanafunzi wake: “Kwa hiyo nawaambia,
msisumbukie maisha yenu kwamba mtakula nini; au
msumbukie miili yenu kwamba mtavaa nini. 23 Maisha
ni zaidi ya chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi.
24 Fikirini ndege! Wao hawapandi wala hawavuni,
hawana ghala wala popote pa kuhifadhi nafaka; lakini
Mungu huwalisha. Ninyi ni wa thamani kuliko ndege!
25 Ni nani miongoni mwenu ambaye kwa kujitaabisha
kwake anaweza kujiongezea hata saa moja zaidi
katika maisha yake? 26 Kama hamwezi kufanya
jambo dogo kama hilo, kwa nini basi kuyasumbukia
hayo mengine? 27 “Angalieni maua jinsi yameavyo:
Hayafanyi kazi wala hayafumi. Lakini nawaambia,
hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa
vizuri kama mojawapo ya hayo maua. 28 Basi ikiwa
Mungu huyavika hivi majani ya shambani, ambayo leo
yapo, na kesho yanatupwa motoni, si atawavika ninyi
vizuri zaidi, enyi wa imani haba! 29 Wala msisumbuke
mioyoni mwenu mtakula nini au mtakunywa nini.
Msiwe na wasiwasi juu ya haya. 30 Watu wa mataifa
ya duniani husumbuka sana kuhusu vitu hivi vyote,
lakini Baba yenu anafahamu kuwa mnahitaji haya
yote. 31 Bali utafuteni ufalme wa Mungu, na haya
yote atawapa pia. 32 “Msiogope enyi kundi dogo,
kwa maana Baba yenu ameona vyema kuwapa
ninyi ufalme. 33 Uzeni mali yenu mkawape maskini.
Jifanyieni mifuko isiyochakaa, mkajiwekee hazina
mbinguni isiyokwisha, ambapo mwizi hakaribii wala
nondo haharibu. 34 Kwa sababu mahali hazina
yako ilipo, hapo ndipo moyo wako utakapokuwa
pia. 35 “Kuweni tayari mkiwa mmevikwa kwa ajili
ya huduma na taa zenu zikiwa zinawaka, 36 kama
watumishi wanaomngojea bwana wao arudi kutoka
karamu ya arusi, ili ajapo na kubisha mlango waweze
kumfungulia mara moja. 37 Heri wale watumishi
ambao bwana wao atakapokuja atawakuta wakiwa
wanakesha. Amin, nawaambia, atajifunga mkanda
wake na kuwaketisha ili wale, naye atakuja na
kuwahudumia. 38 Itakuwa heri kwa watumwa hao
ikiwa bwana wao atakapokuja atawakuta wamekesha
hata kama atakuja usiku wa manane, au karibu
na mapambazuko. 39 Lakini fahamuni jambo hili:
Kama mwenye nyumba angejua saa mwizi atakuja,
hangeiacha nyumba yake kuvunjwa. 40 Ninyi nanyi
hamna budi kuwa tayari, kwa sababu Mwana wa
Adamu atakuja saa msiyotazamia.” 41 Ndipo Petro
akamuuliza, “Bwana Isa, mfano huu unatuambia sisi
peke yetu au watu wote?” 42 Isa akamjibu, “Ni yupi
basi wakili mwaminifu na mwenye busara, ambaye
bwana wake atamfanya msimamizi juu ya watumishi
wake wote, ili awape watumishi wengine chakula
chao wakati unaofaa? 43 Heri mtumishi yule ambaye
bwana wake atakaporudi atamkuta akifanya hivyo. 44
Amin nawaambia, atamweka mtumishi huyo kuwa
msimamizi wa mali yake yote. 45 Lakini kama yule
mtumishi atasema moyoni mwake, ‘Bwana wangu
anakawia kurudi,’ kisha akaanza kuwapiga wale
watumishi, wa kiume na wa kike, na kula na kunywa
na kulewa. 46 Basi bwana wa mtumishi huyo atakuja
siku asiyodhani na saa asiyoijua. Atamkata vipande
vipande na kumweka katika sehemu moja pamoja na
wale wasioamini. 47 “Yule mtumishi anayefahamu
vyema mapenzi ya bwana wake na asijiandae wala

kufanya kama apendavyo bwana wake, atapigwa
kwa mapigo mengi. 48 Lakini yeyote ambaye hakujua
naye akafanya yale yastahiliyo kupigwa, atapigwa
kidogo. Yeyote aliyepewa vitu vingi, atadaiwa vingi;
na yeyote aliyekabidhiwa vingi, kwake vitatakiwa
vingi. 49 "Nimekuja kuleta moto duniani; laiti kama
ungekuwa tayari umewashwa! 50 Lakini ninao ubatizo
ambao lazima nibatizwe, nayo dhiki yangu ni kuu hadi
ubatizo huo ukamilike! 51 Mnadhani nimekuja kuleta
amani duniani? La, nawaambia sivyo, nimekuja kuleta
mafarakano. 52 Kuanzia sasa, kutakuwa na watu
watano katika nyumba moja, watatu dhidi ya wawili,
na wawili dhidi ya watatu. 53 Watafarakana baba
dhidi ya mwanawe na mwana dhidi ya babaye, mama
dhidi ya bintiye na binti dhidi ya mamaye, naye mama
mkwe dhidi ya mkwewe na mkwe dhidi ya mama
mkwe wake." 54 Pia Isa akaambia umati ule wa watu,
"Mwonapo wingu likitokea magharibi, mara mwasema,
'Mvua itanyesha,' nayo hunyesha. 55 Nanyi mwonapo
upepo wa kusini ukivuma, ninyi husema, 'Kutakuwa na
joto,' na huwa hivyo. 56 Enyi wanafiki! Mnajua jinsi ya
kutambua kuonekana kwa dunia na anga. Inakuwaje
basi kwamba mnashindwa kutambua wakati huu
wa sasa? 57 "Kwa nini hamwamui wenyewe lililo
haki? 58 Ukiwa njiani na mshtaki wako kwenda
kwa hakimu, jitahidi kupatana naye mkiwa njiani.
La sivyo, atakupeleka kwa hakimu, naye hakimu
atakukabidhi kwa afisa, naye afisa atakutupa gerezani.
59 Nakuambia, hutatoka humo hadi uwe umelipa senti
ya mwisho."

**13** Wakati huo huo, kulikuwa na watu
waliomwambia Isa habari za Wagalilaya ambao
Pilato aliwaua, na damu ya hao watu akaichanganya
na dhabihu yao waliyokuwa wanatoa. 2 Isa akawauliza,
"Mnadhani kwamba hawa Wagalilaya ambao walikufa
kifo kama hicho walikuwa na dhambi kuwazidi
Wagalilaya wengine wote? 3 La hasha! Ninyi nanyi
msipotubu, mtaangamia vivyo hivyo. 4 Au wale watu
kumi na wanane waliokufa walipoangukiwa na mnara
huko Siloamu: mnadhani wao walikuwa waovu kuliko
watu wote walioishi Yerusalemu? 5 Nawaambia, la
hasha! Ninyi nanyi msipotubu, wote mtaangamia vivyo
hivyo." 6 Kisha Isa akawaambia mfano huu: "Mtu
mmoja alikuwa na mtini uliopandwa katika shamba
lake la mizabibu, akaja ili kutafuta tini kwenye mti
huo, lakini hakupata hata moja. 7 Hivyo akamwambia
mtunza shamba: 'Tazama, kwa muda wa miaka mitatu
sasa nimekuwa nikija kutafuta matunda kwenye
mtini huu, nami sikupata hata moja. Ukate! Kwa nini
uendelee kuharibu ardhi?' 8 "Yule mtunza shamba
akamjibu, 'Bwana, uuache tena kwa mwaka mmoja
zaidi, nami nitaupalilia na kuuwekea mbolea. 9
Nao ukizaa matunda mwaka ujao, vyema! La sivyo,
uukate.'" 10 Basi Isa alikuwa akifundisha katika
sinagogi mojawapo siku ya Sabato. 11 Wakati huo huo
akaja mwanamke mmoja aliyekuwa na pepo mchafu,
naye alikuwa amepinda mgongo kwa muda wa
miaka kumi na nane, wala alikuwa hawezi kunyooka
wima. 12 Isa alipomwona, akamwita, akamwambia,
"Mwanamke, uwe huru, umepona ugonjwa wako." 13
Isa alipomwekea mikono yake, akasimama wima mara
moja, akaanza kumtukuza Mungu. 14 Lakini kiongozi
wa sinagogi akakasirika kwa sababu Isa alikuwa
ameponya mtu siku ya Sabato. Akaambia umati ule
wa watu, "Kuna siku sita ambazo watu wanapaswa
kufanya kazi. Katika siku hizo, njooni mponywe,
lakini si katika siku ya Sabato." 15 Lakini Bwana
Isa akamjibu, "Enyi wanafiki! Je, kila mmoja wenu
hamfungulii ng'ombe wake au punda wake kutoka
zizini akampeleka kumnywesha maji siku ya Sabato?
16 Je, huyu mwanamke, ambaye ni binti ya Ibrahimu,
aliyeteswa na Shetani akiwa amemfunga kwa miaka
yote hii kumi na nane, hakustahili kufunguliwa kutoka
kifungo hicho siku ya Sabato?" 17 Aliposema haya,
wapinzani wake wakaaibika, lakini watu wakafurahi
kwa ajili ya mambo ya ajabu aliyoyafanya. 18
Kisha Isa akauliza, "Ufalme wa Mungu unafanana
na nini? Nitaufananisha na nini? 19 Umefanana
na punje ya haradali ambayo mtu aliichukua na
kuipanda katika shamba lake. Nayo ikakua, ikawa
mti, nao ndege wa angani wakatengeneza viota
vyao kwenye matawi yake." 20 Isa akauliza tena,
"Nitaufananisha ufalme wa Mungu na nini? 21
Unafanana na chachu ambayo mwanamke aliichukua
akaichanganya katika kiasi kikubwa cha unga hadi
wote ukaumuka." 22 Isa akapita katika miji na vijiji,
akifundisha wakati alisafiri kwenda Yerusalemu. 23
Mtu mmoja akamuuliza, "Bwana Isa, ni watu wachache
tu watakaookolewa?" Isa akawaambia, 24 "Jitahidini
sana kuingia kupitia mlango mwembamba, kwa
maana nawaambia wengi watajaribu kuingia, lakini
hawataweza. 25 Mwenye nyumba atakapoondoka na

kufunga mlango, mtasimama nje mkibisha mlango
na kusema, ‘Bwana! Tufungulie mlango!’ “Lakini
yeye atawajibu, ‘Siwajui ninyi, wala mtokako.’ **26**
“Ndipo mtamjibu, ‘Tulikula na kunywa pamoja nawe,
tena ulifundisha katika mitaa yetu.’ **27** “Lakini yeye
atawajibu, ‘Siwajui ninyi, wala mtokako. Ondokeni
kwangu, ninyi watenda maovu!’ **28** “Ndipo kutakuwako
kilio na kusaga meno, mtakapowaona Ibrahimu,
Isaka, Yakobo na manabii wote wakiwa katika ufalme
wa Mungu, lakini ninyi mkiwa mmetupwa nje. **29**
Watu watatoka mashariki na magharibi, kaskazini na
kusini, nao wataketi kwenye sehemu walizoandaliwa
karamuni katika ufalme wa Mungu. **30** Tazama,
kuna walio wa mwisho watakaokuwa wa kwanza,
nao wa kwanza watakaokuwa wa mwisho.” **31**
Wakati huo huo baadhi ya Mafarisayo wakamwendea
Isa na kumwambia, “Ondoka hapa uende mahali
pengine kwa maana Herode anataka kukuua.” **32**
Isa akawajibu, “Nendeni mkamwambie yule mbweha,
‘Ninafukuza pepo wachafu na kuponya wagonjwa
leo na kesho, nami siku ya tatu nitaikamilisha kazi
yangu.’ **33** Sina budi kuendelea na safari yangu leo,
kesho na kesho kutwa: kwa maana haiwezekani
nabii kufa mahali pengine isipokuwa Yerusalemu.
**34** “Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii
na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwako! Mara
ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako pamoja,
kama vile kuku akusanyavyo vifaranga wake chini ya
mabawa yake, lakini hukutaka! **35** Tazama nyumba
yenu imeachwa ukiwa. Ninawaambia, hamtaniona
tena hadi wakati ule mtakaposema, ‘Amebarikiwa
yeye ajaye kwa jina la Mwenyezi Mungu.’”

**14** Siku moja ya Sabato, Isa alipoenda kula chakula
kwa mmoja wa viongozi wa Mafarisayo, watu
walikuwa wakimchunguza kwa makini. **2** Hapo mbele
yake palikuwa na mtu mmoja mwenye ugonjwa wa
kuvimba mwili. **3** Isa akawauliza wale Mafarisayo
na walimu wa Torati, “Je, ni halali kuponya watu
siku ya Sabato au la?” **4** Wakakaa kimya. Hivyo
Isa akamshika yule mgonjwa mkono na kumponya,
akamruhusu aende zake. **5** Kisha akawauliza, “Kama
mmoja wenu angekuwa na mtoto au ng’ombe wake
aliyetumbukia katika kisima siku ya Sabato, je,
hamtamvuta mara moja na kumtoa?” **6** Nao hawakuwa
na la kusema. **7** Alipoona jinsi wageni walivyokuwa
wanachagua mahali pa heshima wakati wa kula,
akawaambia mfano huu: **8** “Mtu akikualika arusini,
usikae mahali pa mgeni wa heshima kwa kuwa
inawezekana amealikwa mtu mheshimiwa kuliko
wewe. **9** Mkifanya hivyo, yule aliyewaalika ninyi wawili
atakuja na kukuambia, ‘Mpishe huyu mtu kiti chako.’
Ndipo kwa aibu utalazimika kukaa katika nafasi ya
chini kabisa. **10** Badala yake, unapoalikwa, chagua
nafasi ya chini, ili yule aliyekualika atakapokuona,
atakuja na kukuambia, ‘Rafiki yangu, nenda kwenye
nafasi iliyo bora zaidi.’ Kwa jinsi hii utakuwa umepewa
heshima mbele ya wageni wenzako wote. **11**
Kwa maana kila mtu ajikwezaye atashushwa, naye
ajishushaye atakwezwa.” **12** Kisha Isa akamwambia
yule aliyewaalika, “Uandaapo karamu ya chakula cha
mchana au cha jioni, usialike rafiki zako au ndugu
zako au jamaa zako au majirani zako walio matajiri tu.
Ukifanya hivyo, nao wanaweza kukualika kwao, nawe
ukawa umepata malipo. **13** Bali unapoandaa karamu,
waalike maskini, vilema, viwete na vipofu, **14** nawe
utabarikiwa kwa sababu hawa hawana uwezo wa
kukulipa. Mungu atakulipa wakati wa ufufuo wa wenye
haki.” **15** Mmoja wa wale waliokuwa pamoja naye
mezani aliposikia hivi akamwambia Isa, “Amebarikiwa
mtu yule atakayekula katika karamu ya ufalme
wa Mungu!” **16** Isa akamjibu, “Mtu mmoja alikuwa
anaandaa karamu kubwa, akaalika watu wengi. **17**
Wakati wa karamu ulipofika, akamtuma mtumishi
wake akawaambie wale walioalikwa, ‘Karibuni, kila kitu
ki tayari sasa.’ **18** “Lakini wote, kila mmoja, wakaanza
kutoa udhuru: Wa kwanza akasema, ‘Nimenunua
shamba, lazima niende kuliona. Tafadhali niwie radhi.’
**19** “Mwingine akasema, ‘Ndipo tu nimenunua jozi tano
za ng’ombe wa kulimia, nami ninaenda kuwajaribu,
tafadhali niwie radhi.’ **20** “Naye mwingine akasema,
‘Nimeoa mke, kwa hiyo siwezi kuja.’ **21** “Yule mtumishi
akarudi, akampa bwana wake taarifa. Ndipo yule
mwenye nyumba akakasirika, akamwagiza yule
mtumishi wake, akisema, ‘Nenda upesi kwenye mitaa
na vichochoro vya mjini uwalete maskini, vilema,
vipofu na viwete.’ **22** “Yule mtumishi akamwambia,
‘Bwana, yale uliyoniagiza nimefanya, lakini bado ipo
nafasi.’ **23** “Ndipo yule bwana akamwambia mtumishi
wake, ‘Nenda kwenye barabara na vijia vilivyo nje ya
mji na uwalazimishe watu waingie ili nyumba yangu
ijae. **24** Kwa maana nawaambia, hakuna hata mmoja
wa wale walioalikwa atakayeionja karamu yangu.’” **25**

Umati mkubwa wa watu walikuwa wakisafiri pamoja
na Isa, naye akageuka, akawaambia, **26** “Mtu yeyote
anayekuja kwangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu
kama hatanipenda mimi zaidi ya baba yake na mama
yake, mke wake na watoto wake, ndugu zake na
dada zake, naam, hata maisha yake mwenyewe. **27**
Yeyote asiyeuchukua msalaba wake na kunifuata
hawezi kuwa mwanafunzi wangu. **28** “Ni nani miongoni
mwenu ambaye kama anataka kujenga nyumba,
hakai kwanza chini na kufanya makisio ya gharama
aone kama ana fedha za kutosha kukamilisha? **29** La
sivyo, baada ya kuweka msingi, naye akiwa hana
uwezo wa kuikamilisha, wote waionao wataanza
kumdhihaki, **30** wakisema, ‘Mtu huyu alianza kujenga
lakini hakuweza kukamilisha.’ **31** “Au je, mfalme fulani
akienda vita na mfalme mwingine, si yeye huketi chini
kwanza na kufikiri: je, akiwa na jeshi la watu elfu
kumi, ataweza kupigana na yule anayekuja na jeshi la
watu elfu ishirini? **32** Ikiwa hawezi, basi yule mwingine
akiwa bado yuko mbali, yeye hutuma wajumbe na
kuomba masharti ya amani. **33** Vivyo hivyo, yeyote
miongoni mwenu ambaye hawezi kuacha vyote alivyo
navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. **34** “Chumvi
ni nzuri, lakini chumvi ikiwa imepoteza ladha yake,
itafanywaje ili iweze kukolea tena? **35** Haifai ardhi
wala kwa lundo la mbolea, bali hutupwa nje. “Mwenye
masikio ya kusikia, na asikie.”

**15** Basi watoza ushuru na wenye dhambi
wote walikuwa wanakusanyika ili wapate
kumsikiliza Isa. **2** Lakini Mafarisayo na walimu
wa Torati wakanung’unika wakisema, “Huyu mtu
anawakaribisha wenye dhambi na kula nao.” **3**
Ndipo Isa akawaambia mfano huu: **4** “Ikiwa mmoja
wenu ana kondoo mia moja, naye akapoteza mmoja
wao, je, hawaachi wale tisini na tisa nyikani na
kwenda kumtafuta huyo aliyepotea hadi ampate?
**5** Naye akishampata, humbeba mabegani mwake
kwa furaha **6** na kwenda nyumbani. Kisha huwaita
rafiki zake na majirani, na kuwaambia, ‘Furahini
pamoja nami; nimempata kondoo wangu aliyepotea.’
**7** Nawaambieni, vivyo hivyo kutakuwa na furaha zaidi
mbinguni kwa sababu ya mwenye dhambi mmoja
atubuye, kuliko kwa wenye haki tisini na tisa ambao
hawana haja ya kutubu. **8** “Au ikiwa mwanamke
ana sarafu za fedha kumi, naye akapoteza moja,
je, hawashi taa na kufagia nyumba na kuitafuta
kwa bidii hadi aipate? **9** Baada ya kuipata, yeye
huwaita rafiki zake na majirani na kuwaambia,
‘Furahini pamoja nami; nimeipata ile sarafu yangu
ya fedha iliyopotea.’ **10** Vivyo hivyo, nawaambia,
kuna furaha mbele ya malaika wa Mungu juu ya
mwenye dhambi mmoja atubuye.” **11** Isa akaendelea
kusema: “Kulikuwa na mtu mmoja aliyekuwa na wana
wawili. **12** Yule mdogo akamwambia baba yake,
‘Baba, nipe urithi wangu.’ Hivyo akawagawia wanawe
mali yake. **13** “Baada ya muda mfupi, yule mdogo
akakusanya vitu vyote alivyokuwa navyo, akaenda
nchi ya mbali, na huko akaitapanya mali yake kwa
maisha ya anasa. **14** Baada ya kutumia kila kitu
alichokuwa nacho, kukawa na njaa kali katika nchi
ile yote, naye akawa hana chochote. **15** Kwa hiyo
akaenda akaajiriwa na raia mmoja wa nchi ile ambaye
alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. **16**
Akatamani kujishibisha kwa maganda waliyokula
wale nguruwe, wala hakuna mtu aliyempa chochote.
**17** “Lakini alipozingatia moyoni mwake, akasema,
‘Ni watumishi wangapi walioajiriwa na baba yangu
ambao wana chakula cha kuwatosha na kusaza,
bali mimi hapa nakufa kwa njaa! **18** Nitaondoka
na kurudi kwa baba yangu na kumwambia: Baba,
nimetenda dhambi mbele za Mungu na mbele yako.
**19** Sistahili tena kuitwa mwanao; nifanye kama mmoja
wa watumishi wako.’ **20** Basi akaondoka, akaenda
kwa baba yake. “Lakini alipokuwa bado yuko mbali,
baba yake akamwona, moyo wake ukajawa na
huruma. Akamkimbilia mwanawe, akamkumbatia na
kumbusu. **21** “Yule mwana akamwambia baba yake,
‘Baba, nimekosa mbele za Mungu na mbele yako.
Sistahili kuitwa mwanao tena.’ **22** “Lakini baba yake
akawaambia watumishi, ‘Leteni upesi joho lililo bora
sana, tieni pete kidoleni mwake na viatu miguuni
mwake. **23** Leteni ndama aliyenona, mkamchinje ili
tuwe na karamu, tule na kufurahi. **24** Kwa maana
huyu mwanangu alikuwa amekufa na sasa yu hai
tena; alikuwa amepotea na sasa amepatikana!’ Nao
wakaanza kusherehekea. **25** “Wakati huo, yule mwana
mkubwa alikuwa shambani. Alipokaribia nyumbani,
akasikia sauti ya nyimbo na watu wakicheza. **26**
Akamwita mmoja wa watumishi na kumuuliza maana
ya mambo yale. **27** Akamwambia, ‘Ndugu yako
amekuja, naye baba yako amemchinjia ndama
aliyenona kwa sababu mwanawe amerudi nyumbani

akiwa salama na mzima.’ 28 “Yule mwana mkubwa akakasirika, akakataa kuingia ndani. Basi baba yake akatoka nje na kumsihi. 29 Lakini yeye akamjibu baba yake, ‘Tazama! Miaka yote hii nimekutumikia na hata siku moja sijaacha kutii amri zako, lakini hujanipa hata mwana-mbuzi ili nifurahi na rafiki zangu. 30 Lakini huyu mwanao ambaye ametapanya mali yako kwa makahaba aliporudi nyumbani, wewe umemchinjia ndama aliyenona!’ 31 “Baba yake akamjibu, ‘Mwanangu, umekuwa nami siku zote na vyote nilivyo navyo ni vyako. 32 Lakini ilitubidi tufurahi na kushangilia kwa sababu huyu ndugu yako alikuwa amekufa na sasa yu hai; alikuwa amepotea naye amepatikana.’”

**16** Isa akawaambia wanafunzi wake, “Palikuwa na tajiri mmoja na msimamizi wake. Huyo msimamizi alishitakiwa kwake kwamba alikuwa akitapanya mali ya tajiri yake. 2 Hivyo huyo tajiri akamwita na kumuuliza, ‘Ni mambo gani haya ninayoyasikia kukuhusu? Toa taarifa ya usimamizi wako, kwa sababu huwezi kuendelea kuwa msimamizi.’ 3 “Yule msimamizi akawaza moyoni mwake, ‘Nitafanya nini sasa? Bwana wangu ananiondoa katika kazi yangu. Sina nguvu za kulima, nami ninaona aibu kuombaomba. 4 Najua nitakalofanya ili nikiachishwa kazi yangu hapa, watu wanikaribishe nyumbani mwao.’ 5 “Kwa hiyo akawaita wadeni wote wa bwana wake, mmoja mmoja. Akamuuliza wa kwanza, ‘Deni lako kwa bwana wangu ni kiasi gani?’ 6 “Akajibu, ‘Vipimo mia moja vya mafuta ya mizeituni.’ “Msimamizi akamwambia, ‘Chukua hati ya deni lako, ibadilishe upesi, uandike vipimo hamsini.’ 7 “Kisha akamuuliza wa pili, ‘Wewe deni lako ni kiasi gani?’ “Akajibu, ‘Vipimo elfu moja vya ngano.’ “Yule msimamizi akamwambia, ‘Chukua hati yako, uandike vipimo mia nane!’ 8 “Yule bwana akamsifu yule msimamizi dhalimu kwa jinsi alivyotumia ujanja. Kwa maana watu wa dunia hii wana ujanja zaidi wanapojishughulisha na mambo ya dunia kuliko watu wa nuru. **(aiōn g165)** 9 Nawaambia, tumieni mali ya dunia kujipatia rafiki, ili itakapokwisha, mkaribishwe katika makao ya milele. **(aiōnios g166)** 10 “Yeyote aliye mwaminifu katika mambo madogo, pia ni mwaminifu katika mambo makubwa. Na yeyote asiye mwaminifu katika mambo madogo pia si mwaminifu katika mambo makubwa. 11 Ikiwa hamkuwa waaminifu katika mali ya kidunia, ni nani atakayewaaminia mali ya kweli? 12 Nanyi kama hamkuwa waaminifu na mali ya mtu mwingine, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe? 13 “Hakuna mtumishi awezaye kuwatumikia mabwana wawili. Kwa kuwa atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine, au atashikamana sana na huyu na kumdharau yule mwingine. Hamwezi kumtumikia Mungu pamoja na Mali.” 14 Mafarisayo, waliokuwa wapenda fedha, waliyasikia hayo yote na wakamcheka kwa dharau. 15 Isa akawaambia, “Ninyi mnajionesha kuwa wenye haki mbele za wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa maana vile vitu ambavyo wanadamu wanavithamini sana, kwa Mungu ni machukizo. 16 “Torati na Manabii vilihubiriwa hadi kuja kwa Yahya. Tangu wakati huo Injili ya ufalme wa Mungu inahubiriwa, na kila mmoja hujiingiza kwa nguvu. 17 Lakini ni rahisi zaidi mbingu na dunia kupita kuliko hata herufi moja kuondoka katika Torati. 18 “Mtu yeyote amwachaye mkewe na kumwoa mwanamke mwingine anazini, naye mwanaume amwoaye mwanamke aliyetalikiwa anazini. 19 “Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo za rangi ya zambarau na kitani safi, ambaye aliishi kwa anasa kila siku. 20 Hapo penye mlango wake aliishi maskini mmoja, jina lake Lazaro, mwenye vidonda mwili mzima. 21 Huyo Lazaro alitamani kujishibisha kwa makombo yaliyoanguka kutoka mezani kwa yule tajiri. Hata mbwa walikuwa wakija na kuramba vidonda vyake. 22 “Wakati ukafika yule maskini akafa, nao malaika wakamchukua akae pamoja na Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa na akazikwa. 23 Kule Kuzimu alipokuwa akiteseka, alitazama juu, akamwona Ibrahimu kwa mbali, naye Lazaro alikuwa kifuani mwake. **(Hadēs g86)** 24 Hivyo yule tajiri akamwita, ‘Baba Ibrahimu, nihurumie na umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake ndani ya maji aupoze ulimi wangu, kwa sababu nina maumivu makuu kwenye moto huu.’ 25 “Lakini Ibrahimu akamjibu, ‘Mwanangu, kumbuka kwamba wakati wa uhai wako ulipata mambo mazuri, lakini Lazaro alipata mambo mabaya. Lakini sasa anafarijiwa hapa na wewe uko katika maumivu makuu. 26 Zaidi ya hayo, kati yetu na ninyi huko kumewekwa shimo kubwa, ili wale wanaotaka kutoka huku kuja huko wasiweze, wala mtu yeyote asiweze kuvuka kutoka huko kuja kwetu.’ 27 “Akasema,

‘Basi, nakuomba, umtume Lazaro aende nyumbani
mwa baba yangu, 28 maana ninao ndugu watano.
Awaonye, ili wasije nao wakafika mahali hapa pa
mateso.’ 29 “Ibrahimu akamjibu, ‘Ndugu zako wana
Maandiko ya Musa na Manabii, wawasikilize hao.’
30 “Yule tajiri akasema, ‘Hapana, baba Ibrahimu,
lakini mtu kutoka kwa wafu akiwaendea, watatubu.’
31 “Ibrahimu akamwambia, ‘Kama wasipowasikiliza
Musa na Manabii, hawataweza kushawishika hata
kama mtu akifufuka kutoka kwa wafu.’”

**17** Isa akawaambia wanafunzi wake, “Mambo
yanayosababisha watu watende dhambi
hayana budi kutukia. Lakini ole wake mtu yule
anayeyasababisha. 2 Ingekuwa heri kama mtu huyo
angefungiwa jiwe la kusagia shingoni na kutoswa
baharini, kuliko kumsababisha mmoja wa hawa
wadogo kutenda dhambi. 3 Kwa hiyo, jilindeni.
“Ndugu yako akikukosea, mwonye; naye akitubu,
msamehe. 4 Akikukosea mara saba kwa siku moja,
na mara saba kwa siku moja akaja kwako akisema,
‘Ninatubu,’ msamehe.” 5 Mitume wake wakamwambia
Bwana, “Tuongezee imani.” 6 Bwana akawajibu,
“Kama mngekuwa na imani ndogo kama punje ya
haradali, mngeweza kuuambia mti huu wa mkuyu,
‘Ng’oka ukaote baharini,’ nao ungewatii. 7 “Ikiwa
mmoja wenu ana mtumishi anayelima shambani au
anayechunga kondoo, je, mtumishi huyo arudipo
atamwambia, ‘Karibu hapa keti ule chakula’? 8
Je, badala yake, hatamwambia, ‘Niandalie chakula,
nile, jifunge unitumikie ninapokula na kunywa;
baadaye unaweza kula na kunywa’? 9 Je, huyo
mtu atamshukuru mtumishi huyo kwa kutimiza yale
aliyoamriwa? 10 Vivyo hivyo nanyi mkishafanya
mliyoagizwa, semeni, ‘Sisi tu watumishi tusiostahili;
tumefanya tu yale tuliyopaswa kufanya.’” 11 Isa
alipokuwa njiani akienda Yerusalemu, alipitia mpakani
mwa Samaria na Galilaya. 12 Alipokuwa akiingia
kwenye kijiji kimoja, watu kumi waliokuwa na ukoma
wakakutana naye. Wakasimama mbali, 13 wakapaza
sauti, wakasema, “Isa, Bwana, tuhurumie!” 14
Alipowaona akawaambia, “Nendeni mkajioneshe
kwa makuhani.” Nao walipokuwa njiani wakienda,
wakatakasika. 15 Mmoja wao alipoona kwamba
amepona, akarudi kwa Isa, akimsifu Mungu kwa sauti
kuu. 16 Akajitupa miguuni mwa Isa akamshukuru.
Yeye alikuwa Msamaria. 17 Isa akauliza, “Je,
hawakutakaswa wote kumi? Wako wapi wale wengine
tisa? 18 Hakuna hata mmoja aliyeonekana kurudi
ili kumshukuru Mungu isipokuwa huyu mgeni?” 19
Isa akamwambia, “Inuka na uende zako, imani yako
imekuponya.” 20 Isa alipoulizwa na Mafarisayo ufalme
wa Mungu utakuja lini, yeye akawajibu, “Ufalme wa
Mungu hauji kwa kuchunguza kwa bidii, 21 wala
watu hawatasema, ‘Huu hapa,’ au ‘Ule kule,’ kwa
maana ufalme wa Mungu umo ndani yenu.” 22 Kisha
Isa akawaambia wanafunzi wake, “Wakati utafika
ambapo mtatamani kuiona moja ya siku ya Mwana
wa Adamu, lakini hamtaiona. 23 Watu watawaambia,
‘Yule kule!’ au, ‘Huyu hapa!’ Msiwakimbilie. 24 Kwa
maana kama vile radi imulikavyo katika anga kuanzia
mwisho mmoja hadi mwingine, ndivyo atakavyokuwa
Mwana wa Adamu katika siku yake. 25 Lakini
kwanza itampasa kuteseka katika mambo mengi na
kukataliwa na kizazi hiki. 26 “Kama ilivyokuwa siku za
Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika siku za Mwana
wa Adamu. 27 Watu walikuwa wakila na kunywa,
wakioa na kuolewa, hadi siku ile Nuhu alipoingia
katika safina. Ndipo gharika ikaja na kuwaangamiza
wote. 28 “Ndivyo ilivyokuwa katika siku za Lutu:
Watu walikuwa wakila na kunywa, wakinunua na
kuuza, wakilima na kujenga. 29 Lakini siku ile Lutu
alipoondoka Sodoma, ikanyesha mvua ya moto na
kiberiti kutoka mbinguni ukawaangamiza wote. 30
“Hivyo ndivyo itakavyokuwa siku ile Mwana wa Adamu
atakapofunuliwa. 31 Siku hiyo, mtu yeyote aliye juu
ya dari ya nyumba yake, hata vitu vyake vikiwa
ndani ya hiyo nyumba, asishuke kuvichukua. Vivyo
hivyo mtu aliye shambani asirudi nyumbani kuchukua
chochote. 32 Mkumbukeni mke wa Lutu! 33 Mtu yeyote
anayejaribu kuyaokoa maisha yake atayapoteza, na
yeyote atakayeyapoteza maisha yake atayaokoa.
34 Nawaambia, usiku huo watu wawili watakuwa
wamelala kitanda kimoja; naye mmoja atatwaliwa na
mwingine ataachwa. 35 Wanawake wawili watakuwa
wanasaga nafaka pamoja; naye mmoja atatwaliwa
na mwingine ataachwa. [ 36 Wanaume wawili
watakuwa wanafanya kazi pamoja shambani; mmoja
atachukuliwa na mwingine ataachwa.]” 37 Kisha
wakamuuliza, “Haya yatatukia wapi Bwana Isa?”
Akawaambia, “Pale ulipo mzoga, huko ndiko tai
watakapokusanyika.”

**18** Kisha Isa akawapa wanafunzi wake mfano ili
kuwaonesha kuwa yawapasa kuomba pasipo
kukata tamaa. 2 Akawaambia, “Katika mji mmoja
palikuwa hakimu ambaye hakumwogopa Mungu
wala kumjali mtu. 3 Katika mji huo alikuwako
mjane mmoja aliyekuwa akija kwake mara kwa mara
akimwomba, ‘Tafadhali nipatie haki kati yangu na adui
yangu.’ 4 “Kwa muda mrefu yule hakimu alikataa.
Lakini hatimaye akasema moyoni mwake, ‘Ijapokuwa
simwogopi Mungu wala simjali mwanadamu, 5
lakini kwa kuwa huyu mjane ananisumbuasumbua,
nitahakikisha amepata haki yake ili asiendelee
kunichosha kwa kunijia mara kwa mara!’” 6 Bwana
Isa akasema, “Sikilizeni asemavyo huyu hakimu
dhalimu. 7 Je, Mungu hatawatendea haki wateule
wake wanaomlilia usiku na mchana? Je, atakawia
kuwasaidia? 8 Ninawaambia, atawapatia haki upesi.
Lakini je, Mwana wa Adamu atakapokuja ataikuta
imani duniani?” 9 Isa akatoa mfano huu kwa wale
waliojiamini kuwa wao ni wenye haki na kuwadharau
wengine: 10 “Watu wawili walienda Hekaluni kusali,
mmoja wao alikuwa Farisayo na mwingine alikuwa
mtoza ushuru. 11 Yule Farisayo, akasimama,
akasali hivi na kuomba kwake mwenyewe: ‘Mungu,
nakushukuru kwa sababu mimi si kama watu wengine
ambao ni wanyang’anyi, wadhalimu, na wazinzi,
wala kama huyu mtoza ushuru. 12 Mimi nafunga
mara mbili kwa juma, na natoa sehemu ya kumi
ya mapato yangu.’ 13 “Lakini yule mtoza ushuru
akasimama mbali, wala hakuthubutu hata kuinua uso
wake kutazama mbinguni, bali alijipigapiga kifuani na
kusema: ‘Mungu, nihurumie, mimi mwenye dhambi.’
14 “Nawaambia, huyu mtoza ushuru alirudi nyumbani
akiwa amehesabiwa haki mbele za Mungu zaidi
ya yule Farisayo. Kwa maana yeyote ajikwezaye
atashushwa, na yeyote ajishushaye atakwezwa.” 15
Pia, watu walikuwa wakimletea Isa watoto wachanga
ili awaguse. Wanafunzi wake walipoona hivyo,
wakawakemea. 16 Lakini Isa akawaita wale watoto
waje kwake, akasema, “Waacheni watoto wadogo
waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana ufalme
wa Mungu ni wa wale walio kama hawa. 17 Amin,
nawaambia, mtu yeyote asiyeupokea ufalme wa
Mungu kama mtoto mdogo, hatauingia kamwe.” 18
Mtawala mmoja akamuuliza Isa, “Mwalimu mwema,
nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?” **(aiōnios
g166)** 19 Isa akamjibu, “Mbona unaniita mwema?
Hakuna yeyote aliye mwema ila Mungu peke yake.
20 Unazijua amri: ‘Usizini, usiue, usiibe, usishuhudie
uongo, waheshimu baba yako na mama yako.’” 21
Akajibu, “Amri hizi zote nimezishika tangu nikiwa
mtoto.” 22 Isa aliposikia haya, akamwambia, “Bado
kuna jambo moja ulilopungukiwa. Nenda ukauze kila
kitu ulicho nacho, uwape maskini, nawe utakuwa na
hazina mbinguni. Kisha njoo, unifuate.” 23 Aliposikia
jambo hili, alisikitika sana kwa maana alikuwa mtu
mwenye mali nyingi. 24 Isa akamtazama, akasema,
“Tazama jinsi ilivyo vigumu kwa tajiri kuingia katika
ufalme wa Mungu! 25 Hakika ni rahisi zaidi kwa
ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu
tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu.” 26 Wale
waliosikia haya wakauliza, “Ni nani basi awezaye
kuokoka?” 27 Isa akajibu, “Yasiyowezekana kwa
wanadamu yanawezekana kwa Mungu.” 28 Ndipo
Petro akamjibu, “Tazama, tumeacha vyote tulivyokuwa
navyo tukakufuata!” 29 Isa akajibu, “Amin, nawaambia,
hakuna hata mtu aliyeacha nyumba yake, au mke,
au ndugu, au wazazi au watoto kwa ajili ya ufalme
wa Mungu 30 ambaye hatapewa mara nyingi zaidi
ya hivyo katika maisha haya, na hatimaye kupata
uzima wa milele ujao.” **(aiōn g165, aiōnios g166)** 31
Isa akawachukua wale wanafunzi wake kumi na
wawili kando na kuwaambia, “Tunapanda kwenda
Yerusalemu, na kila kitu kilichoandikwa na manabii
kumhusu Mwana wa Adamu kitatimizwa. 32 Kwa
kuwa atatiwa mikononi mwa watu wasiomjua Mungu,
nao watamdhihaki, watamtukana na kumtemea mate,
watampiga mijeledi na kumuua. 33 Naye siku ya tatu
atafufuka.” 34 Wanafunzi wake hawakuelewa mambo
haya, kwa kuwa maana yake ilikuwa imefichika kwao,
nao hawakujua Isa alikuwa anazungumzia nini. 35 Isa
alipokuwa anakaribia Yeriko, kipofu mmoja alikuwa
ameketi kando ya njia akiomba msaada. 36 Kipofu
huyo aliposikia umati wa watu wakipita, akauliza nini
kilikuwa kikitendeka. 37 Wakamwambia, “Isa Al-Nasiri
anapita.” 38 Akapaza sauti, akasema, “Isa, Mwana wa
Daudi, nihurumie!” 39 Wale waliokuwa wametangulia
mbele wakamkemea, wakamwambia akae kimya.
Lakini yeye akapaza sauti zaidi, “Mwana wa Daudi,
nihurumie!” 40 Isa akasimama, akawaamuru wamlete
huyo mtu kwake. Alipokaribia, Isa akamuuliza, 41
“Unataka nikufanyie nini?” Akajibu, “Bwana, nataka

kuona." 42 Isa akamwambia, "Basi upate kuona.
Imani yako imekuponya." 43 Akapata kuona mara
hiyo, akamfuata Isa, huku akimsifu Mungu. Watu wote
walipoona mambo hayo, nao wakamsifu Mungu.

19 Isa akaingia Yeriko, naye alikuwa anapita katikati
ya huo mji. 2 Tazama, palikuwa na mtu mmoja
mkuu wa watoza ushuru naye alikuwa tajiri, jina
lake Zakayo. 3 Yeye alikuwa akijitahidi kumwona
Isa ni mtu wa namna gani. Lakini kutokana na
umati mkubwa wa watu hakuweza, kwa sababu
alikuwa mfupi wa kimo. 4 Kwa hiyo akatangulia mbio
mbele ya umati wa watu akapanda juu ya mkuyu ili
amwone Isa, kwa sababu angeipitia njia ile. 5 Isa
alipofika pale chini ya huo mkuyu, akatazama juu,
akamwambia, "Zakayo, shuka upesi, kwa maana leo
nitakuwa mgeni nyumbani mwako!" 6 Hivyo Zakayo
akashuka upesi, akamkaribisha Isa nyumbani mwake
kwa furaha kubwa. 7 Watu wote walipoona hivyo,
wakaanza kunung'unika wakisema, "Ameenda kuwa
mgeni wa mtu mwenye dhambi." 8 Lakini Zakayo
akasimama na kumwambia Bwana Isa, "Tazama,
Bwana! Sasa hivi nusu ya mali yangu ninawapa
maskini, nami kama nimemdhulumu mtu yeyote
kitu chochote, nitamrudishia mara nne ya hicho
kiwango." 9 Ndipo Isa akamwambia, "Leo, wokovu
umeingia nyumbani humu, kwa sababu huyu naye
ni mwana wa Ibrahimu. 10 Kwa maana Mwana wa
Adamu amekuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea."
11 Walipokuwa wanasikiliza haya, Isa akaendelea
kuwaambia mfano, kwa sababu alikuwa anakaribia
Yerusalemu na watu walikuwa wakidhani ya kuwa
ufalme wa Mungu ulikuwa unakuja saa hiyo. 12 Hivyo
akawaambia: "Mtu mmoja mwenye cheo kikubwa
alisafiri kwenda nchi ya mbali ili akapokee madaraka
ya kuwa mfalme, kisha arudi. 13 Hivyo akawaita
kumi miongoni mwa watumishi wake, na akawapa
kila mmoja fungu la fedha. Akawaambia, 'Fanyeni
biashara na fedha hizi hadi nitakaporudi.' 14 "Lakini
raia wa nchi yake walimchukia wakapeleka ujumbe
na kusema, 'Hatutaki huyu mtu awe mfalme wetu.'
15 "Hata hivyo alirudi akiwa amekwisha kupokea
mamlaka ya ufalme, akawaita wale watumishi wake
aliokuwa amewaachia fedha, ili afahamu ni faida kiasi
gani kila mmoja wao aliyopata kwa kufanya biashara.
16 "Wa kwanza akaja na kusema, 'Bwana, kutokana
na fedha uliyoniachia, nimepata faida mara kumi
zaidi.' 17 "Yule bwana akamjibu, 'Umefanya vizuri
mtumishi mwema! Kwa sababu umekuwa mwaminifu
katika wajibu mdogo sana, nakupa mamlaka juu ya
miji kumi.' 18 "Wa pili naye akaja. Akasema, 'Bwana,
fedha yako imeleta faida mara tano zaidi.' 19 "Bwana
wake akajibu, 'Nakupa mamlaka juu ya miji mitano.'
20 "Kisha akaja yule mtumishi mwingine, akasema,
'Bwana, hii hapa fedha yako. Niliitunza vizuri kwenye
kitambaa. 21 Nilikuogopa, kwa sababu wewe ni mtu
mgumu. Unachukua ambapo hukuweka, na kuvuna
ambapo hukupanda.' 22 "Bwana wake akamjibu,
'Nitakuhukumu kwa maneno yako mwenyewe, wewe
mtumishi mwovu! Kama ulifahamu kwamba mimi ni
mtu mgumu, ninayechukua nisichoweka, na kuvuna
nisichopanda, 23 kwa nini basi hukuweka fedha
zangu kwa watoa riba, ili nitakaporudi nichukue
iliyo yangu na riba yake?' 24 "Ndipo akawaambia
wale waliokuwa wamesimama karibu, 'Mnyang'anyeni
fungu lake la fedha, mkampe yule mwenye kumi.'
25 "Wakamwambia, 'Bwana, mbona; tayari anayo
mafungu kumi!' 26 "Akawajibu, 'Nawaambia kwamba
kila aliye na kitu, ataongezewa. Lakini yule asiye na
kitu, hata alicho nacho atanyang'anywa. 27 Lakini
wale adui zangu ambao hawakutaka mimi niwe
mfalme juu yao. Waleteni hapa mkawaue mbele
yangu.'" 28 Baada ya Isa kusema haya, alitangulia
kupanda kwenda Yerusalemu. 29 Naye alipokaribia
Bethfage na Bethania kwenye mlima ulioitwa Mlima
wa Mizeituni, aliwatuma wanafunzi wake wawili,
akawaambia, 30 "Nendeni katika kijiji kilichoko mbele
yenu. Na mtakapokuwa mnaingia kijijini, mtampata
mwana-punda amefungwa hapo, ambaye hajapandwa
na mtu bado. Mfungueni, mkamlete hapa. 31 Kama
mtu akiwauliza, 'Mbona mnamfungua?' Mwambieni,
'Bwana anamhitaji.'" 32 Wale waliotumwa wakaenda,
wakapata kila kitu kama Isa alivyowaambia. 33
Walipokuwa wanamfungua yule mwana-punda,
wenyewe wakawauliza, "Mbona mnamfungua huyo
mwana-punda?" 34 Wale wanafunzi wakajibu, "Bwana
anamhitaji." 35 Wakamleta kwa Isa, nao baada
ya kutandika mavazi yao juu ya huyo mwana-
punda, wakampandisha Isa juu yake. 36 Alipokuwa
akienda, watu wakatandaza mavazi yao barabarani.
37 Alipokaribia mahali yanapoanzia miteremko ya
Mlima wa Mizeituni, umati wote wa wafuasi wake
wakaanza kumsifu Mungu kwa furaha kwa sauti kuu

kwa ajili ya matendo yote ya miujiza waliyoyaona. Wakasema: 38 “Amebarikiwa mfalme ajaye kwa Jina la Mwenyezi Mungu!” “Amani mbinguni na utukufu huko juu sana.” 39 Baadhi ya Mafarisayo waliokuwamo miongoni mwa umati ule wa watu wakamwambia, “Mwalimu, waamuru wanafunzi wako wanyamaze.” 40 Isa akawajibu, “Nawaambia ninyi, kama hawa watanyamaza, mawe yatapaza sauti.” 41 Alipokaribia Yerusalemu na kuuona mji, aliulilia, 42 akisema, “Laiti ungejua, hata wewe leo, yale yangeleta amani, lakini sasa yamefichika machoni pako. 43 Hakika siku zinakujia, ambazo adui zako watakuzingira, nao watakuzunguka pande zote na kukuzuilia ndani. 44 Watakuponda chini, wewe na watoto walio ndani ya kuta zako. Nao hawataacha hata jiwe moja juu ya jingine, kwa sababu hukutambua wakati wa kujiliwa kwako.” 45 Ndipo akaingia eneo la Hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza vitu humo. 46 Naye akawaambia, “Imeandikwa, ‘Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala,’ lakini ninyi mmeifanya kuwa ‘pango la wanyang’anyi.’” 47 Kila siku alikuwa akifundisha Hekaluni. Lakini viongozi wa makuhani, walimu wa Torati na viongozi wa watu walikuwa wakitafuta njia ili kumuua. 48 Lakini hawakupata nafasi kwa sababu watu wote walimfuata wakiyasikiliza maneno yake kwa usikivu mwingi.

**20** Siku moja, Isa alipokuwa akifundisha watu Hekaluni na kuhubiri Habari Njema, viongozi wa makuhani, walimu wa Torati, pamoja na wazee wa watu wakamjia. 2 Wakamuuliza, “Tuambie, unafanya mambo haya kwa mamlaka gani? Ni nani aliyekupa mamlaka haya?” 3 Akawajibu, “Nami nitawauliza swali. Nijibuni: 4 Je, ubatizo wa Yahya ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?” 5 Wakahojiana wao kwa wao na kusema, “Tukisema, ‘Ulitoka mbinguni,’ atatuuliza, ‘Mbona hamkumwamini?’ 6 Lakini tukisema, ‘Ulitoka kwa wanadamu,’ watu wote watatupiga mawe, kwa sababu wanaamini kwamba Yahya alikuwa nabii.” 7 Basi wakajibu, “Hatujui ulikotoka.” 8 Isa akawaambia, “Wala mimi sitawaambia ni kwa mamlaka gani ninatenda mambo haya.” 9 Akaendelea kuwaambia watu mfano huu: “Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akalikodisha kwa wakulima fulani, kisha akasafiri kwa muda mrefu. 10 Wakati wa mavuno ulipofika, akamtuma mtumishi wake kwa hao wapangaji ili wampe sehemu ya mavuno ya shamba la mizabibu. Lakini wale wakulima wakampiga, wakamfukuza mikono mitupu. 11 Akamtuma mtumishi mwingine, huyo naye wakampiga, wakamfanyia mambo ya aibu na kumfukuza. 12 Bado akamtuma na mwingine wa tatu, huyu pia wakamjeruhi na kumtupa nje ya shamba. 13 “Basi yule mwenye shamba la mizabibu akasema, ‘Nifanye nini? Nitamtuma mwanangu mpendwa, huenda yeye watamheshimu.’ 14 “Lakini wale wapangaji walipomwona, wakasemezana wao kwa wao. Wakasema, ‘Huyu ndiye mrithi. Basi na tumuue ili urithi uwe wetu.’ 15 Kwa hiyo wakamtupa nje ya shamba la mizabibu, wakamuua. “Sasa basi yule mwenye shamba la mizabibu atawafanyia nini wapangaji hawa? 16 Atakuja na kuwaua hao wapangaji, na kuwapa wapangaji wengine hilo shamba la mizabibu.” Watu waliposikia hayo wakasema, “Mungu apishie mbali jambo hili lisitokee!” 17 Lakini Isa akawakazia macho, akasema, “Basi ni nini maana ya yale yaliyoandikwa: “‘Jiwe walilolikataa waashi, limekuwa jiwe kuu la pembeni’? 18 Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika vipande vipande, lakini yule litakayemwangukia atasagwa kabisa.” 19 Walimu wa Torati na viongozi wa makuhani wakatafuta njia ya kumkamata mara moja, kwa sababu walifahamu kwamba amesema mfano huo kwa ajili yao. Lakini waliwaogopa watu. 20 Kwa hiyo wakawa wanamchunguza na kutuma wapelelezi waliojifanya kuwa wenye haki. Walitaka kumtega kwa maneno yake, ili wampeane katika uwezo na mamlaka ya mtawala. 21 Hivyo wale wapelelezi wakamuuliza, “Mwalimu, tunajua unasema na kufundisha yaliyo kweli wala humpendelei mtu, bali wafundisha njia ya Mungu katika kweli. 22 Je, ni halali sisi kulipa kodi kwa Kaisari, au la?” 23 Lakini Isa akatambua hila yao, akawaambia, 24 “Nionesheni dinari. Je, sura hii na maandishi haya yaliyo juu yake ni vya nani?” Wakamjibu, “Ni vya Kaisari.” 25 Akawaambia, “Basi mpeni Kaisari kilicho cha Kaisari, naye Mungu mpeni kilicho cha Mungu.” 26 Wakashindwa kumkamata kwa yale aliyokuwa amesema hadharani. Nao wakashangazwa mno na majibu yake, wakanyamaza. 27 Baadhi ya Masadukayo, wale wasemao kuwa hakuna ufufuo wa wafu, wakamjia Isa na kumuuliza, 28 “Mwalimu, Musa alituandikia kwamba kama ndugu wa mtu akifa na kumwacha mkewe bila mtoto, basi huyo mtu

inampasa amwoe huyo mjane ili amzalie ndugu yake
watoto. 29 Basi kulikuwa na ndugu saba. Yule wa
kwanza akaoa, akafa bila kuzaa mtoto. 30 Kisha yule
wa pili akamwoa huyo mjane, naye akafa bila mtoto,
31 naye wa tatu pia akamwoa. Vivyo hivyo ndugu wote
saba wakawa wamemwoa huyo mwanamke, na wote
wakafa pasipo yeyote kupata mtoto. 32 Mwishowe,
yule mwanamke naye akafa. 33 Sasa basi, siku ya
ufufuo huyo mwanamke atakuwa mke wa nani, maana
aliolewa na ndugu wote saba?" 34 Isa akawajibu,
"Katika maisha haya watu huoa na kuolewa. (aiōn
g165) 35 Lakini wale ambao wamehesabiwa kwamba
wanastahili kupata nafasi katika ulimwengu ule na
katika ufufuo wa wafu, hawaoi wala hawaolewi. (aiōn
g165) 36 Hawa hawawezi kufa tena, kwa maana
wao ni kama malaika. Wao ni watoto wa Mungu,
kwa sababu ni watoto wa ufufuo. 37 Hata Musa
alidhihirisha kuwa wafu wanafufuka, kwa habari ya
kile kichaka kilichokuwa kikiwaka moto bila kuteketea,
alipomwita Mwenyezi Mungu, 'Mungu wa Ibrahimu,
Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo.' 38 Yeye
si Mungu wa wafu, bali wa walio hai, kwa kuwa
kwake wote ni hai." 39 Baadhi ya walimu wa Torati
wakasema, "Mwalimu, umesema sawasawa kabisa!"
40 Baada ya hayo hakuna mtu aliyethubutu kumuuliza
maswali tena. 41 Kisha Isa akawaambia, "Imekuwaje
basi wao husema Al-Masihi ni Mwana wa Daudi?
42 Daudi mwenyewe anasema katika Kitabu cha
Zaburi: "'Bwana alimwambia Bwana wangu: "Keti
mkono wangu wa kuume, 43 hadi nitakapowaweka
adui zako chini ya miguu yako."' 44 Ikiwa Daudi
anamwita yeye 'Bwana,' basi atakuwaje mwanawe?"
45 Wakati watu wote walikuwa wanamsikiliza, Isa
akawaambia wanafunzi wake, 46 "Jihadharini na
walimu wa Torati. Wao hupenda kutembea wakiwa
wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa kwa heshima
masokoni. Hupenda kukaa kwenye viti vya mbele
katika masinagogi, na kukaa kwenye nafasi za
heshima katika karamu. 47 Wao hula nyumba za
wajane, na ili waonekane kuwa wema, wanasali sala
ndefu. Watu kama hawa watapata hukumu iliyo kuu
sana."

21 Isa alipoinua macho yake, aliwaona matajiri
wakiweka sadaka zao kwenye sanduku la
hazina ya Hekalu. 2 Akamwona pia mjane mmoja
maskini akiweka humo sarafu mbili ndogo za shaba. 3
Isa akasema, "Amin, nawaambia, huyu mjane maskini
ameweka humo zaidi ya watu wengine wote. 4 Hawa
watu wengine wote wametoa sadaka kutokana na
wingi wa mali yao. Lakini huyu mjane ametoa kutokana
na umaskini wake vyote alivyokuwa navyo, hata kile
alichohitaji ili kuishi." 5 Baadhi ya wanafunzi wake
wakawa wanamwonesha jinsi Hekalu lilivyopambwa
kwa mawe mazuri na kwa vitu vilivyotolewa kuwa
sadaka kwa Mungu. Lakini Isa akawaambia, 6 "Kuhusu
haya mnayoyaona hapa, wakati utafika ambapo
hakuna jiwe moja litakalobaki juu ya jingine, bali
kila moja litabomolewa." 7 Wakamuuliza, "Mwalimu,
mambo haya yatatukia lini? Ni dalili gani itaonesha
kwamba yanakaribia kutendeka?" 8 Isa akawajibu,
"Jihadharini msije mkadanganywa. Maana wengi
watakuja kwa Jina langu, wakidai, 'Mimi ndiye,' na,
'Wakati umekaribia.' Msiwafuate. 9 Lakini msikiapo
habari za vita na machafuko, msiogope. Kwa maana
hayo ni lazima yatokee kwanza, ila ule mwisho
hautakuja wakati huo." 10 Kisha akawaambia: "Taifa
litainuka dhidi ya taifa jingine, na ufalme mmoja dhidi
ya ufalme mwingine. 11 Kutakuwa na mitetemeko
mikubwa ya ardhi, na njaa kali, na magonjwa ya
kuambukiza katika sehemu mbalimbali. Pia kutakuwa
na matukio ya kutisha na ishara kuu kutoka mbinguni.
12 "Lakini kabla yote hayajatokea, watawakamata
ninyi na kuwatesa. Watawatia mikononi mwa wakuu
wa masinagogi na kuwafunga magerezani. Nanyi
mtapelekwa mbele ya wafalme na watawala kwa ajili
ya Jina langu. 13 Hii itawapa nafasi ya kushuhudia.
14 Lakini kusudieni mioyoni mwenu msisumbuke awali
kuhusu mtakalosema mbele ya mashtaka. 15 Kwa
maana nitawapa maneno na hekima ambayo hakuna
hata adui yenu mmoja atakayeweza kushindana
nayo wala kuipinga. 16 Mtasalitiwa hata na wazazi,
ndugu, jamaa na rafiki zenu, na baadhi yenu
watawaua. 17 Mtachukiwa na watu wote kwa ajili
ya Jina langu. 18 Lakini hapatakuwa na unywele
mmoja wa kichwa chenu utakaoangamia. 19 Kwa
kuvumilia mtaokoa roho zenu. 20 "Mtakapoona mji
wa Yerusalemu umezungukwa na majeshi, basi
fahamuni kwamba kuharibiwa kwake kumekaribia. 21
Wakati huo, wale walio Yudea wakimbilie milimani,
walio mjini Yerusalemu watoke humo, nao wale
walio mashambani wasiingie mjini. 22 Kwa sababu
huu utakuwa ni wakati wa adhabu ili kutimiza yote

yaliyoandikwa. 23 Ole wao wenye mimba na wale
wanaonyonyesha watoto siku hizo! Kutakuwa na
dhiki kuu katika nchi na ghadhabu juu ya hawa
watu. 24 Wataanguka kwa makali ya upanga, na
wengine watachukuliwa kuwa mateka katika mataifa
yote. Nao mji wa Yerusalemu utakanyagwa na watu
wa Mataifa hadi muda wa hao watu wa Mataifa
utimie. 25 "Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi na
nyota. Hapa duniani, mataifa yatakuwa katika dhiki
na fadhaa kutokana na ngurumo na misukosuko ya
bahari. 26 Watu watazimia roho kutokana na hofu
kuu na kuyaona yale mambo yanayotokea duniani,
kwa maana nguvu za angani zitatikisika. 27 Wakati
huo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija
mawinguni pamoja na uweza na utukufu mkuu. 28
Mambo haya yatakapoanza kutendeka, simameni
na mkaviinue vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi
wenu umekaribia." 29 Akawaambia mfano huu:
"Uangalieni mtini na miti mingine yote. 30 Inapochipua
majani, ninyi wenyewe mnaweza kuona na kutambua
wenyewe ya kuwa wakati wa kiangazi umekaribia.
31 Vivyo hivyo, mnapoyaona mambo haya yakitukia,
mtambue kwamba ufalme wa Mungu umekaribia.
32 "Amin, nawaambia, kizazi hiki hakitapita hadi
mambo haya yote yawe yametimia. 33 Mbingu
na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita
kamwe. 34 "Jihadharini mioyo yenu isije ikalemewa
na anasa, ulevi na fadhaa za maisha haya, nayo
siku ile ikawakuta ninyi bila kutazamia kama mtego
unasavyo. 35 Hivyo ndivyo siku hiyo itakavyowapata
wanadamu wote wanaoishi katika uso wa dunia yote.
36 Kesheni daima na mwombe ili mweze kuokoka
na yale yote yatakayotokea na kusimama mbele
ya Mwana wa Adamu." 37 Kila siku Isa alikuwa
akifundisha Hekaluni, na jioni ilipofika, alienda zake
kwenye Mlima wa Mizeituni na kukaa huko usiku
kucha. 38 Nao watu wote walikuja asubuhi na mapema
Hekaluni ili kumsikiliza.

22 Wakati huu Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu,
iitwayo Pasaka, ilikuwa imekaribia. 2 Viongozi
wa makuhani na walimu wa Torati walikuwa wanatafuta
njia ya kumuua Isa, kwa sababu waliwaogopa watu. 3
Shetani akamwingia Yuda, aliyeitwa Iskariote, mmoja
wa wale kumi na wawili. 4 Yuda akaenda kwa
viongozi wa makuhani na kwa maafisa wa walinzi wa
Hekalu, akazungumza nao jinsi angeweza kumsaliti
Isa. 5 Wakafurahi na wakakubaliana kumpa fedha. 6
Naye akakubali, akaanza kutafuta wakati uliofaa wa
kumsaliti Isa kwao, ambapo hakuna umati wa watu. 7
Basi ikawadia siku ya Mikate Isiyotiwa Chachu, siku
ambayo mwana-kondoo wa Pasaka huchinjwa. 8
Hivyo Isa akawatuma Petro na Yohana, akisema,
"Nendeni mkatuandalie chakula cha Pasaka ili tuweze
kuila." 9 Wakamuuliza, "Unataka tukuandalie wapi?"
10 Isa akawaambia, "Tazameni, mtakapokuwa mkiingia
mjini, mtakutana na mwanaume amebeba mtungi wa
maji. Mfuateni hadi kwenye nyumba atakayoingia.
11 Nanyi mwambieni mwenye nyumba, 'Mwalimu
anauliza: Kiko wapi chumba cha wageni, ambamo
mimi na wanafunzi wangu tutakula Pasaka?' 12
Atawaonesha chumba kikubwa ghorofani, kikiwa
kimepambwa vizuri. Andaeni humo." 13 Wakaenda,
nao wakakuta kila kitu kama Isa alivyowaambia.
Hivyo wakaiandaa Pasaka. 14 Wakati ulipowadia,
Isa akaketi mezani pamoja na wale mitume wake.
15 Kisha akawaambia, "Nimetamani sana kuila
Pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu.
16 Kwa maana, nawaambia, sitaila tena Pasaka
hadi itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu."
17 Baada ya kukichukua kikombe, akashukuru,
akasema, "Chukueni hiki mnywe wote. 18 Kwa maana
nawaambia tangu sasa sitakunywa tena katika uzao
wa mzabibu, hadi ufalme wa Mungu utakapokuja." 19
Kisha akachukua mkate, akashukuru, akaumega, na
kuwapa, akisema, "Huu ni mwili wangu unaotolewa
kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu."
20 Vivyo hivyo baada ya kula, akakitwaa kikombe,
akisema, "Kikombe hiki ni agano jipya katika damu
yangu, imwagikayo kwa ajili yenu. 21 Lakini mkono
wake huyo atakayenisaliti uko hapa mezani pamoja
nami. 22 Mwana wa Adamu anaenda zake kama
ilivyokusudiwa. Lakini ole wake mtu huyo amsalitiye!"
23 Wakaanza kuulizana wenyewe ni nani miongoni
mwao angeweza kufanya jambo hilo. 24 Pia yakazuka
mabishano katikati ya wanafunzi kwamba ni nani
aliyeonekana kuwa mkuu kuliko wote miongoni mwao.
25 Isa akawaambia, "Wafalme na watu wa Mataifa
huwatawala watu kwa nguvu. Nao wenye mamlaka
juu yao hujiita 'Wafadhili.' 26 Lakini ninyi msifanane
nao. Bali yeye aliye mkuu kuliko wote miongoni
mwenu, inampasa kuwa kama yeye aliye mdogo
wa wote, naye anayetawala na awe kama yeye

anayehudumu. 27 Kwani ni nani aliye mkuu? Ni yule
anayeketi mezani au ni yule anayehudumu? Si ni yule
aliyeketi mezani? Lakini mimi niko miongoni mwenu
kama yule anayehudumu. 28 Ninyi mmekuwa pamoja
nami katika majaribu yangu. 29 Nami kama Baba
yangu alivyonipa ufalme, nami ninawapa ninyi, 30 ili
mpate kula na kunywa mezani pangu katika karamu
ya ufalme wangu, na kukaa katika viti vya utawala,
mkihukumu makabila kumi na mawili ya Israeli.”
31 Isa akasema, “Simoni, Simoni, sikiliza, Shetani
ameomba kuwapepeta ninyi wote kama ngano. 32
Lakini nimekuombea wewe Simoni ili imani yako
isishindwe, nawe baada ya kunirudia, uwaimarishe
ndugu zako.” 33 Petro akajibu, “Bwana, niko tayari
kwenda pamoja nawe gerezani na hata katika kifo.”
34 Isa akamjibu, “Ninakuambia Petro, kabla jogoo
hajawika usiku wa leo, utakana mara tatu kwamba
unanijua.” 35 Kisha Isa akawauliza, “Nilipowatuma
bila mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa
na kitu chochote?” Wakajibu, “La, hatukupungukiwa
na kitu chochote.” 36 Akawaambia, “Lakini sasa,
aliye na mfuko na auchukue, na aliye na mkoba
vivyo hivyo. Naye asiye na upanga, auze joho lake
anunue mmoja. 37 Kwa sababu, nawaambia, andiko
hili lazima litimizwe kunihusu, kwamba, ‘Alihesabiwa
pamoja na wakosaji’; kwa kweli yaliyoandikwa
kunihusu hayana budi kutimizwa.” 38 Wanafunzi wake
wakamwambia, “Bwana, tazama hapa kuna panga
mbili.” Akawajibu, “Inatosha.” 39 Isa akatoka, akaenda
kwenye Mlima wa Mizeituni kama ilivyokuwa kawaida
yake, nao wanafunzi wake wakamfuata. 40 Walipofika
huko, akawaambia wanafunzi wake, “Ombeni, msije
mkaingia majaribuni.” 41 Akajitenga nao kama umbali
wa kutupa jiwe, akapiga magoti, akaomba 42 akisema,
“Baba, kama ni mapenzi yako, niondolee kikombe
hiki. Lakini si kama nipendavyo, bali mapenzi yako
yatendeke.” 43 Malaika kutoka mbinguni akamtokea,
akamtia nguvu. 44 Naye akiwa katika maumivu
makuu, akaomba kwa bidii, nalo jasho lake likawa
kama matone ya damu yakidondoka ardhini. 45
Baada ya kuomba, akawarudia wanafunzi wake
akawakuta wamelala, wakiwa wamechoka kutokana
na huzuni. 46 Naye akawauliza, “Mbona mmelala?
Amkeni, mwombe ili msije mkaingia majaribuni.” 47
Isa alipokuwa bado anazungumza, umati mkubwa wa
watu wakaja. Waliongozwa na Yuda, aliyekuwa mmoja
wa wale kumi na wawili. Akamkaribia Isa ili ambusu.
48 Lakini Isa akamwambia, “Yuda, je, unamsaliti
Mwana wa Adamu kwa busu?” 49 Wafuasi wa
Isa walipoona yale yaliyokuwa yanakaribia kutokea,
wakasema, “Bwana, tuwakatekate kwa panga zetu?”
50 Mmoja wao akampiga mtumishi wa kuhani mkuu
kwa upanga, akamkata sikio la kuume. 51 Lakini
Isa akasema, “Acheni!” Akaligusa lile sikio la yule
mtu na kumponya. 52 Kisha Isa akawaambia wale
viongozi wa makuhani, maafisa wa walinzi wa Hekalu,
pamoja na wazee waliokuwa wamekuja kumkamata,
“Mmekuja na panga na marungu, kana kwamba mimi
ni mnyang’anyi? 53 Kila siku nilikuwa pamoja nanyi
Hekaluni lakini hamkunikamata. Lakini hii ni saa
yenu, wakati giza linatawala!” 54 Kisha wakamkamata
Isa, wakamchukua, wakaenda naye hadi nyumbani
mwa kuhani mkuu. Lakini Petro akafuata kwa mbali.
55 Walipokwisha kuwasha moto katikati ya ua na
kuketi pamoja, Petro naye akaketi pamoja nao. 56
Mjakazi mmoja akamwona kwa mwanga wa moto
akiwa ameketi pale. Akamtazama sana, akasema,
“Huyu mtu pia alikuwa pamoja na Isa!” 57 Lakini
Petro akakana, akasema, “Ewe mwanamke, hata
simjui!” 58 Baadaye kidogo, mtu mwingine alimwona
Petro akasema, “Wewe pia ni mmoja wao!” Petro
akajibu, “Wewe mtu, mimi sio mmoja wao!” 59 Baada
ya muda wa kama saa moja hivi, mtu mwingine
akazidi kusisitiza, “Kwa hakika huyu mtu naye alikuwa
pamoja na Isa, kwa maana yeye pia ni Mgalilaya.” 60
Petro akajibu, “Wewe mtu, mimi sijui unalosema!”
Wakati huo huo, akiwa bado anazungumza, jogoo
akawika. 61 Naye Bwana Isa akageuka, akamtazama
Petro. Ndipo Petro akakumbuka lile neno ambalo
Bwana alimwambia: “Kabla jogoo hajawika leo,
utanikana mara tatu.” 62 Naye akaenda nje, akalia
kwa majonzi. 63 Watu waliokuwa wanamlinda Isa
wakaanza kumdhihaki na kumpiga. 64 Wakamfunga
kitambaa machoni na kumuuliza, “Tabiri! Tuambie
ni nani aliyekupiga?” 65 Wakaendelea kumtukana
kwa matusi mengi. 66 Kulipopambazuka, Baraza
la Wazee, yaani viongozi wa makuhani na walimu
wa Torati, wakakutana pamoja, naye Isa akaletwa
mbele yao. 67 Wakamwambia, “Kama wewe ndiwe Al-
Masihi, tuambie.” Isa akawajibu, “Hata nikiwaambia,
hamtaamini. 68 Nami nikiwauliza swali, hamtanijibu.
69 Lakini kuanzia sasa, Mwana wa Adamu ataketi

mkono wa kuume wa Mungu Mwenye Nguvu.” 70
Wote wakauliza, “Wewe basi ndiwe Mwana wa
Mungu?” Yeye akawajibu, “Ninyi mwasema kwamba
mimi ndiye.” 71 Kisha wakasema, “Tuna haja gani
tena ya ushahidi zaidi? Tumesikia wenyewe kutoka
kinywani mwake.”

23 Kisha umati wote wa watu wakainuka na
kumpeleka Isa kwa Pilato. 2 Nao wakaanza
kumshtaki wakisema: “Tumemwona huyu mtu
akipotosha taifa letu, akiwazuia watu wasilipe kodi
kwa Kaisari na kujiita ni Al-Masihi, mfalme.” 3 Basi
Pilato akamuuliza Isa, “Wewe ndiwe mfalme wa
Wayahudi?” Isa akajibu, “Wewe wasema.” 4 Pilato
akawaambia viongozi wa makuhani na umati ule
wote, “Sioni msingi wowote wa kumshtaki mtu huyu!”
5 Lakini wao wakakazana kusema, “Anawachochea
watu kwa mafundisho yake katika Yudea yote,
tangu Galilaya alikoanzia, hadi sehemu hii!” 6 Pilato
aliposikia hayo akauliza kama huyo mtu alikuwa
Mgalilaya. 7 Alipofahamu kwamba Isa alikuwa chini
ya mamlaka ya Herode, akampeleka kwa Herode,
ambaye wakati huo alikuwa pia Yerusalemu. 8 Herode
alipomwona Isa alifurahi sana, kwa sababu kwa muda
mrefu alikuwa amesikia mambo mengi kumhusu.
Pia alitarajia kumwona akifanya miujiza kadha wa
kadha. 9 Herode akamuuliza maswali mengi, lakini Isa
hakumjibu lolote. 10 Wakati huo viongozi wa makuhani
na walimu wa Torati walikuwa wakitoa mashtaka
yao kwa nguvu sana. 11 Herode na askari wake
wakamdhihaki Isa na kumfanyia mzaha. Wakamvika
vazi zuri sana, wakamrudisha kwa Pilato. 12 Siku hiyo,
Herode na Pilato wakapata urafiki; kabla ya jambo hili
walikuwa na uadui kati yao. 13 Basi Pilato akawaita
pamoja viongozi wa makuhani, viongozi wengine
na watu, 14 akawaambia, “Ninyi mlimleta huyu mtu
kwangu kana kwamba ni mtu anayewachochea watu
ili waasi. Nimemhoji mbele yenu nami sikupata msingi
wowote wa mashtaka yenu dhidi yake. 15 Wala
Herode hakumpata na kosa lolote, ndiyo sababu
amemrudisha kwetu. Kama mnavyoona, mtu huyu
hakufanya jambo lolote linalostahili kifo. 16 Kwa hiyo
nitaamuru apigwe mijeledi na kumwachilia.” [ 17 Kwa
kuwa ilikuwa lazima kuwafungulia mfungwa mmoja
wakati wa Sikukuu.] 18 Ndipo watu wote wakapiga
kelele kwa pamoja, “Mwondoe mtu huyu! Tufungulie
Baraba!” 19 (Baraba alikuwa amefungwa gerezani
kwa sababu ya maasi yaliyokuwa yametokea mjini, na
kwa ajili ya uuaji.) 20 Pilato, akitaka kumwachia Isa,
akasema nao tena. 21 Lakini wao wakaendelea kupiga
kelele wakisema, “Msulubishe! Msulubishe!” 22 Kwa
mara ya tatu, Pilato akawauliza, “Kwani amefanya
kosa gani huyu mtu? Sikuona kwake sababu yoyote
inayostahili adhabu ya kifo. Kwa hiyo nitaamuru
apigwe mijeledi, na kisha nitamwachia.” 23 Lakini
watu wakazidi kupiga kelele kwa nguvu, wakidai
kwamba Isa asulubiwe. Hivyo, kelele zao zikashinda.
24 Kwa hiyo Pilato akatoa hukumu kwamba madai
yao yatimizwe. 25 Akamfungua yule mtu aliyekuwa
amefungwa gerezani kwa kuhusika katika uasi dhidi ya
serikali na mauaji. Akamkabidhi Isa mikononi mwao,
wamfanyie watakavyo. 26 Walipokuwa wakienda naye,
wakamkamata mtu mmoja aitwaye Simoni Mkirene,
aliyekuwa anapita zake kuingia mjini kutoka shambani.
Wakambebesha msalaba, wakamlazimisha auchukue
nyuma ya Isa. 27 Idadi kubwa ya watu wakamfuata
Isa, wakiwamo wanawake waliokuwa wakimlilia na
kumwombolezea. 28 Isa akawageukia, akawaambia,
“Enyi binti za Yerusalemu, msinililie mimi bali jililieni
ninyi wenyewe na watoto wenu. 29 Kwa maana wakati
utafika mtakaposema, ‘Wamebarikiwa wanawake
tasa, ambao tumbo zao hazikuzaa, wala matiti yao
hayakunyonyesha!’ 30 Ndipo “‘wataiambia milima,
“Tuangukieni!” na vilima, “Tufunikeni!”’ 31 Kwa maana
kama wamefanya hivi kwa mti mbichi, kwa mti mkavu
itakuwaje?” 32 Watu wawili wahalifu walipelekwa
pamoja na Isa ili wakasulubiwe. 33 Walipofika mahali
paitwapo Fuvu la Kichwa, hapo ndipo walimsulubisha
Isa pamoja na hao wahalifu, mmoja upande wake wa
kuume, na mwingine upande wake wa kushoto. 34
Isa akasema, “Baba, wasamehe, kwa maana hawajui
walitendalo!” Wakagawana nguo zake kwa kupiga
kura. 35 Watu wakasimama hapo wakimwangalia,
nao viongozi wa Wayahudi wakamdhihaki wakisema,
“Aliokoa wengine! Ajiokoe mwenyewe basi, kama
yeye ndiye Al-Masihi wa Mungu, Mteule wake.”
36 Askari nao wakaja, wakamdhihaki. Wakamletea
siki ili anywe, 37 na wakamwambia, “Kama wewe
ni mfalme wa Wayahudi, jiokoe mwenyewe.” 38
Kwenye msalaba juu ya kichwa chake, kulikuwa na
maandishi haya: Huyu ndiye Mfalme wa Wayahudi. 39
Mmoja wa wale wahalifu waliosulubiwa pamoja naye
akamtukana, akasema: “Wewe si ndiye Al-Masihi?

Jiokoe mwenyewe na utuokoe na sisi.” **40** Lakini yule
mhalifu mwingine akamkemea mwenzake, akasema,
“Je, wewe humwogopi Mungu, wakati uko kwenye
adhabu hiyo hiyo? **41** Sisi tumehukumiwa kwa haki
kwa kuwa tunapata tunayostahili kwa ajili ya matendo
yetu. Lakini huyu mtu hajafanya kosa lolote.” **42**
Kisha akasema, “Isa, unikumbuke utakapokuja katika
ufalme wako.” **43** Isa akamjibu, “Amin, nakuambia,
leo utakuwa pamoja nami Paradiso.” **44** Ilikuwa
kama saa sita mchana, nalo giza likafunika nchi
yote hadi saa tisa, **45** kwa sababu jua liliacha
kutoa nuru. Pazia la Hekalu likachanika vipande
viwili. **46** Isa akapaza sauti yake akasema, “Baba,
mikononi mwako naikabidhi roho yangu.” Baada
ya kusema haya, akakata roho. **47** Yule jemadari
alipoona yaliyotukia, akamsifu Mungu, akasema,
“Hakika, mtu huyu alikuwa mwenye haki.” **48** Watu
wote waliokuwa wamekusanyika hapo kushuhudia
tukio hili walipoyaona hayo, wakapigapiga vifua vyao
kwa huzuni na kwenda zao. **49** Lakini wale wote
waliomfahamu, pamoja na wale wanawake waliokuwa
wamemfuata kutoka Galilaya, walisimama kwa mbali
wakiyatazama mambo haya. **50** Basi kulikuwa na mtu
mmoja mwema na mwenye haki, jina lake Yusufu.
Yeye alikuwa mjumbe wa Baraza la Wayahudi, **51**
lakini yeye hakuwa amekubaliana na maamuzi na
vitendo vya viongozi wenzake. Huyu alikuwa raia wa
Arimathaya huko Yudea, naye alikuwa anaungojea
ufalme wa Mungu kwa matarajio makubwa. **52** Yusufu
alienda kwa Pilato, akaomba apewe mwili wa Isa.
**53** Akaushusha kutoka msalabani, akaufunga katika
kitambaa cha kitani safi, na kuuweka katika kaburi
lililochongwa kwenye mwamba, ambalo halikuwa
limezikiwa mtu mwingine bado. **54** Ilikuwa Siku ya
Maandalizi, nayo Sabato ilikuwa karibu kuanza. **55**
Wale wanawake waliokuwa wamekuja pamoja na
Isa wakimfuata kutoka Galilaya wakamfuata Yusufu,
wakaliona kaburi na jinsi mwili wa Isa ulivyolazwa. **56**
Kisha wakarudi nyumbani, wakaandaa manukato na
marhamu ya kuupaka huo mwili. Lakini wakapumzika
siku ya Sabato kama ilivyoamriwa.

**24** Siku ya kwanza ya juma, alfajiri na mapema,
wale wanawake walichukua yale manukato
waliyokuwa wameyaandaa, wakaenda kaburini. **2**
Wakakuta lile jiwe limevingirishwa kutoka mdomo wa
kaburi, **3** lakini walipoingia ndani, hawakuuona mwili
wa Bwana Isa. **4** Walipokuwa wanashangaa kuhusu
jambo hili, ghafula watu wawili waliokuwa wamevaa
mavazi yanayong’aa kama umeme wakasimama
karibu nao. **5** Wale wanawake, wakiwa na hofu,
wakainamisha nyuso zao hadi chini. Lakini wale
watu wakawaambia, “Kwa nini mnamtafuta aliye hai
miongoni mwa wafu? **6** Hayuko hapa; amefufuka!
Kumbukeni alivyowaambia alipokuwa bado yuko
pamoja nanyi huko Galilaya kwamba: **7** ‘Ilikuwa
lazima Mwana wa Adamu atiwe mikononi mwa
watu wenye dhambi na waovu ili asulubiwe, na
siku ya tatu afufuke.’” **8** Ndipo wakayakumbuka
maneno ya Isa. **9** Waliporudi kutoka huko kaburini,
wakawaeleza wale wanafunzi kumi na mmoja pamoja
na wengine wote mambo haya yote. **10** Basi
Mariamu Magdalene, Yoana, na Mariamu mama yake
Yakobo, pamoja na wanawake wengine waliofuatana
nao ndio waliwaelezea mitume habari hizi. **11**
Lakini hawakuwasadiki hao wanawake, kwa sababu
maneno yao yalionekana kama upuzi. **12** Hata hivyo,
Petro akainuka na kukimbia kwenda kule kaburini.
Alipoinama kuchungulia, akaona vile vitambaa vya
kitani, ila hakuona kitu kingine. Naye akaenda
zake akijiuliza nini kilichotokea. **13** Ikawa siku
hiyo hiyo, wanafunzi wawili wa Isa walikuwa njiani
wakienda kijiji kilichoitwa Emau, yapata maili saba
kutoka Yerusalemu. **14** Walikuwa wakizungumza
wao kwa wao kuhusu mambo yote yaliyotukia.
**15** Walipokuwa wakizungumza na kujadiliana, Isa
mwenyewe akaja akatembea pamoja nao, **16**
lakini macho yao yakazuiliwa ili wasimtambue. **17**
Akawauliza, “Ni mambo gani haya mnayozungumza
wakati mnatembea?” Wakasimama, nyuso zao
zikionesha huzuni. **18** Mmoja wao, aliyeitwa Kleopa,
akamuuliza, “Je, wewe ndiwe peke yako mgeni huku
Yerusalemu, ambaye hufahamu mambo yaliyotukia
humo siku hizi?” **19** Akawauliza, “Mambo gani?”
Wakamjibu, “Mambo ya Isa Al-Nasiri. Yeye alikuwa
nabii, mwenye uwezo mkuu katika maneno yake
na matendo yake, mbele za Mungu na mbele ya
wanadamu wote. **20** Viongozi wa makuhani na viongozi
wetu walimtoa ahukumiwe kufa, nao wakamsulubisha.
**21** Lakini tulikuwa tumetegemea kwamba yeye ndiye
atakayewakomboa Israeli. Zaidi ya hayo, leo ni siku ya
tatu tangu mambo haya yatendeke. **22** Isitoshe, baadhi
ya wanawake katika kundi letu wametushtusha.

Walienda kaburini leo alfajiri, 23 lakini hawakuukuta
mwili wake. Walirudi wakasema wameona maono
ya malaika ambao waliwaambia kwamba Isa yu
hai. 24 Kisha baadhi ya wenzetu walienda kaburini
wakalikuta kama vile wale wanawake walivyokuwa
wamesema, lakini yeye hawakumwona." 25 Isa
akawaambia, "Ninyi ni wajinga kiasi gani, nanyi
ni wazito mioyoni mwenu kuamini mambo yote
yaliyonenwa na manabii! 26 Je, haikumpasa Al-
Masihi kuteswa kwa njia hiyo na kisha aingie katika
utukufu wake?" 27 Naye akianzia na Torati ya Musa
na Manabii wote, akawafafanulia jinsi Maandiko
yalivyosema kumhusu. 28 Nao walipokaribia kile kijiji
walichokuwa wakienda, Isa akawa kama anaendelea
mbele. 29 Lakini wao wakamsihi sana akae nao,
wakisema, "Kaa hapa nasi, kwa maana sasa ni jioni
na usiku unaingia." Basi akaingia ndani kukaa nao.
30 Alipokuwa mezani pamoja nao, akachukua mkate,
akashukuru, akaumega, akaanza kuwagawia. 31
Ndipo macho yao yakafumbuliwa, nao wakamtambua,
naye akatoweka machoni pao. Hawakumwona tena.
32 Wakaulizana wao kwa wao, "Je, mioyo yetu
haikuwaka ndani yetu alipokuwa anazungumza nasi
njiani na kutufafanulia Maandiko?" 33 Wakaondoka
mara hiyo, wakarudi Yerusalemu. Wakawakuta wale
wanafunzi kumi na mmoja na wale waliokuwa pamoja
nao wamekusanyika, 34 wakasema, "Ni kweli! Bwana
Isa amefufuka, naye amemtokea Simoni." 35 Kisha
wale wanafunzi wawili wakaeleza yaliyotukia njiani
na jinsi walivyomtambua Isa alipoumega mkate.
36 Walipokuwa bado wanazungumza hayo, Isa
mwenyewe akasimama katikati yao, akasema, "Amani
iwe nanyi!" 37 Wakashtuka na kuogopa wakidhani
kwamba wameona mzuka. 38 Lakini Isa akawauliza,
"Kwa nini mnaogopa? Kwa nini mna shaka mioyoni
mwenu? 39 Tazameni mikono yangu na miguu yangu,
mwone kuwa ni mimi mwenyewe. Niguseni mwone;
kwa maana mzuka huna nyama na mifupa, kama
mnavyoniona mimi." 40 Aliposema haya, akawaonesha
mikono na miguu yake. 41 Wakashindwa kuamini
kwa ajili ya furaha na mshangao waliokuwa nao.
Akawauliza, "Mna chakula chochote hapa?" 42
Wakampa kipande cha samaki aliyeokwa, 43 naye
akakichukua na kukila mbele yao. 44 Akawaambia,
"Haya ndio yale niliyowaambia nilipokuwa bado niko
pamoja nanyi, kwamba yote yaliyoandikwa kunihusu
katika Torati ya Musa, Manabii na Zaburi hayana
budi kutimizwa." 45 Ndipo akafungua fahamu zao
ili waweze kuyaelewa Maandiko Matakatifu. 46
Akawaambia, "Haya ndio yaliyoandikwa: Al-Masihi
atateswa na siku ya tatu atafufuka kutoka kwa wafu. 47
Toba na msamaha wa dhambi zitatangaziwa mataifa
yote kupitia jina lake kuanzia Yerusalemu. 48 Ninyi ni
mashahidi wa mambo haya. 49 "Tazama nitawatumia
ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini hadi
mtakapovikwa uwezo kutoka juu." 50 Baada ya
kuwaongoza hadi Bethania, akainua mikono yake juu
na kuwabariki. 51 Alipokuwa anawabariki, akawaacha,
akachukuliwa mbinguni. 52 Kisha wakamwabudu na
kurudi Yerusalemu wakiwa wamejawa na furaha kuu.
53 Nao wakadumu ndani ya Hekalu wakimtukuza
Mungu.

# Yohana

**1** Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye huyo Neno
alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa
Mungu. **2** Tangu mwanzo huyo Neno alikuwa pamoja
na Mungu. **3** Vitu vyote viliumbwa kupitia kwake, na
hakuna chochote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa
pasipo yeye. **4** Ndani yake kulikuwa na uzima, nao
huo uzima ulikuwa nuru ya watu. **5** Nuru hung'aa
gizani nalo giza halikuishinda. **6** Alikuja mtu mmoja
aliyetumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yahya. **7**
Alikuja kama shahidi apate kuishuhudia hiyo nuru, ili
kupitia kwake watu wote waweze kuamini. **8** Yeye
mwenyewe hakuwa ile nuru, bali alikuja kuishuhudia
hiyo nuru. **9** Nuru halisi inayomwangazia kila mtu
ilikuwa inakuja ulimwenguni. **10** Huyo Neno alikuwako
ulimwenguni, na ingawa ulimwengu uliumbwa kupitia
kwake, haukumtambua. **11** Alikuja kwa walio wake,
lakini wao hawakumpokea. **12** Bali wote waliompokea,
yaani wale walioliamini jina lake, aliwapa uwezo wa
kufanyika wana wa Mungu. **13** Hawa hawakuzaliwa
kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili au kwa
mapenzi ya mtu, bali wamezaliwa kwa mapenzi ya
Mungu. **14** Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni
mwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama
wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema
na kweli. **15** Yahya alishuhudia habari zake, akapaza
sauti, akisema, "Huyu ndiye yule niliyewaambia
kwamba, 'Yeye ajaye baada yangu ni mkuu kuliko
mimi, kwa kuwa alikuwa kabla yangu.'" **16** Kutokana
na ukamilifu wake, sisi sote tumepokea neema juu ya
neema. **17** Kwa kuwa sheria ilitolewa kwa mkono wa
Musa, lakini neema na kweli zimekuja kupitia Isa Al-
Masihi. **18** Hakuna mtu yeyote aliyemwona Mungu
wakati wowote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye
kifuani mwa Baba, ndiye ambaye amemdhihirisha. **19**
Huu ndio ushuhuda wa Yahya wakati viongozi wa
Wayahudi waliwatuma makuhani na Walawi kutoka
Yerusalemu kumuuliza, "Wewe ni nani?" **20** Yahya
alikiri waziwazi pasipo kuficha, akasema, "Mimi si Al-
Masihi." **21** Wakamuuliza, "Wewe ni nani, basi? Je,
wewe ni Ilya?" Yeye akajibu, "Hapana, mimi siye."
"Je, wewe ni yule Nabii?" Akajibu, "Hapana." **22**
Ndipo wakasema, "Basi tuambie wewe ni nani ili
tupate jibu la kuwapelekea wale waliotutuma. Wewe
wasemaje juu yako mwenyewe?" **23** Akawajibu kwa
maneno ya nabii Isaya, akisema, "Mimi ni sauti ya
mtu aliaye nyikani, 'Yanyoosheni mapito ya Mwenyezi
Mungu.'" **24** Basi walikuwa wametumwa watu kutoka
kwa Mafarisayo, **25** wakamuuliza, "Kama wewe si Al-
Masihi, wala si Ilya na wala si yule Nabii, kwa nini basi
unabatiza?" **26** Yahya akawajibu, "Mimi ninabatiza
kwa maji, lakini kati yenu yupo mtu msiyemjua.
**27** Yeye anakuja baada yangu, nami sistahili hata
kufungua kamba za viatu vyake." **28** Mambo haya yote
yalitukia huko Bethania, ng'ambo ya Yordani, mahali
Yahya alipokuwa akibatiza. **29** Siku iliyofuata, Yahya
alimwona Isa akimjia, akasema, "Tazama, Mwana-
Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!
**30** Huyu ndiye yule niliyewaambia kwamba, 'Mtu
anakuja baada yangu ambaye ni mkuu kuliko mimi,
kwa kuwa alikuwa kabla yangu.' **31** Mimi mwenyewe
sikumfahamu, lakini sababu ya kuja nikibatiza kwa
maji ni ili yeye apate kufunuliwa kwa Israeli." **32**
Kisha Yahya akatoa ushuhuda huu: "Nilimwona Roho
Mtakatifu wa Mungu akishuka kutoka mbinguni kama
hua, akakaa juu yake. **33** Mimi nisingemtambua,
lakini yeye aliyenituma nibatize kwa maji alikuwa
ameniambia, 'Yule mtu utakayemwona Roho Mtakatifu
wa Mungu akimshukia na kukaa juu yake, huyo
ndiye atakayebatiza kwa Roho wa Mungu.' **34** Mimi
mwenyewe nimeona jambo hili na ninashuhudia kuwa
huyu ndiye Mwana wa Mungu." **35** Siku iliyofuata,
Yahya alikuwa huko tena pamoja na wanafunzi wake
wawili. **36** Alipomwona Isa akipita, akasema, "Tazama,
Mwana-Kondoo wa Mungu!" **37** Wale wanafunzi wawili
walipomsikia Yahya akisema haya, wakamfuata Isa.
**38** Isa akageuka, akawaona wakimfuata, akawauliza,
"Mnataka nini?" Wakamwambia, "Mwalimu, unaishi
wapi?" **39** Isa akawajibu, "Njooni, nanyi mtapaona!"
Hivyo wakaenda na kupaona mahali alipokuwa
anaishi, wakakaa naye siku ile, kwa kuwa ilikuwa
yapata saa kumi. **40** Andrea, nduguye Simoni Petro,
alikuwa mmoja wa wale wawili waliosikia yale Yahya
alisema na kumfuata Isa. **41** Kitu cha kwanza
Andrea alichofanya ni kumtafuta Simoni nduguye
na kumwambia, "Tumemwona Masihi" (yaani Al-
Masihi). **42** Naye akamleta kwa Isa. Isa akamwangalia
na kusema, "Wewe ni Simoni mwana wa Yohana.
Utaitwa Kefa" (ambalo limetafsiriwa Petro). **43** Siku
iliyofuata Isa aliamua kwenda Galilaya. Akamkuta
Filipo, akamwambia, "Nifuate." **44** Filipo alikuwa raia

wa Bethsaida, mji walikotoka Andrea na Petro. **45**
Filipo naye akamkuta Nathanaeli na kumwambia,
“Tumemwona yeye ambaye Musa aliandika habari
zake katika Torati, na ambaye pia manabii waliandika
kumhusu, yaani Isa Al-Nasiri, mwana wa Yusufu.” **46**
Nathanaeli akauliza, “Nasiri! Je, kitu chochote chema
chaweza kutoka Nasiri?” Filipo akamwambia, “Njoo
uone.” **47** Isa alipomwona Nathanaeli anakaribia,
akanena habari zake, akasema, “Tazama huyu
ni Mwisraeli kweli kweli; hana hila ndani yake.”
**48** Nathanaeli akamuuliza, “Umenifahamuje?” Isa
akamjibu, “Nilikuona ulipokuwa bado uko chini ya
mtini, kabla hata Filipo hajakuita.” **49** Nathanaeli
akamwambia, “Mwalimu, wewe ni Mwana wa Mungu!
Wewe ni Mfalme wa Israeli!” **50** Isa akamwambia,
“Unaamini kwa kuwa nilikuambia nilikuona ulipokuwa
bado uko chini ya mtini? Basi utaona mambo makuu
kuliko hilo.” **51** Ndipo akawaambia, “Amin, amin
nawaambia, ninyi mtaona mbingu ikifunguka na
malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu ya
Mwana wa Adamu.”

**2** Siku ya tatu kulikuwa na arusi katika mji
wa Kana ya Galilaya, naye mama yake Isa
alikuwepo. **2** Isa pamoja na wanafunzi wake walikuwa
wamealikwa arusini pia. **3** Divai ilipokwisha, mama
yake Isa akamwambia, “Wameishiwa na divai.” **4** Isa
akamwambia, “Mama, kwa nini unanihusisha? Saa
yangu haijawadia.” **5** Mama yake akawaambia wale
watumishi, “Fanyeni lolote atakalowaambia.” **6** Basi
hapo palikuwa na mitungi sita iliyotengenezwa kwa
mawe; iliwekwa hapo kwa ajili ya desturi ya Kiyahudi
ya kujitakasa; kila mtungi ungeweza kuchukua vipipa
viwili au vitatu. **7** Isa akawaambia wale watumishi,
“Ijazeni hiyo mitungi maji.” Nao wakaijaza ile mitungi
hadi juu. **8** Kisha akawaambia, “Sasa choteni hayo
maji kidogo; mpelekeeni mkuu wa sherehe.” Hivyo
wakachota, wakampelekea. **9** Yule mkuu wa sherehe
akayaonja yale maji ambayo yalikuwa yamebadilishwa
kuwa divai. Hakujua divai hiyo ilikotoka ingawa wale
watumishi waliochota yale maji walifahamu. Basi
akamwita bwana arusi kando, **10** akamwambia, “Watu
wote hutoa divai nzuri kwanza, kisha huleta ile divai
hafifu wageni wakisha kunywa sana; lakini wewe
umeiweka ile nzuri zaidi hadi sasa.” **11** Huu ndio
muujiza wa kwanza wa Isa; aliufanya huko Kana ya
Galilaya. Hivyo Isa alidhihirisha utukufu wake, nao
wanafunzi wake wakamwamini. **12** Baada ya hayo,
Isa pamoja na mama yake, ndugu zake na wanafunzi
wake, walishuka hadi Kapernaumu, wakakaa huko
siku chache. **13** Ilipokaribia wakati wa Pasaka ya
Wayahudi, Isa alipanda kwenda Yerusalemu. **14** Huko
uani la Hekalu aliwakuta watu wakiuza ng’ombe,
kondoo na njiwa, nao wengine walikuwa wameketi
mezani wakibadili fedha. **15** Akatengeneza mjeledi
kutokana na kamba, akawafukuza wote kutoka ua la
Hekalu, pamoja na kondoo na ng’ombe. Akazipindua
meza za wale wabadili fedha na kuzimwaga fedha
zao. **16** Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa,
“Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya nyumba
ya Baba yangu kuwa mahali pa biashara?” **17**
Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa imeandikwa:
“Wivu wa nyumba yako utanila.” **18** Ndipo Wayahudi
wakamuuliza, “Unaweza kutuonesha ishara gani ili
kuthibitisha mamlaka uliyo nayo ya kufanya mambo
haya yote?” **19** Isa akawajibu, “Libomoeni hili Hekalu,
nami nitalijenga tena kwa siku tatu!” **20** Wale Wayahudi
wakamjibu, “Hekalu hili lilijengwa kwa muda wa
miaka arobaini na sita, nawe wasema utalijenga kwa
siku tatu?” **21** Lakini yeye Hekalu alilozungumzia
ni mwili wake. **22** Baada ya kufufuliwa kutoka kwa
wafu, wanafunzi wake wakakumbuka yale aliyokuwa
amesema. Ndipo wakayaamini Maandiko na yale
maneno Isa alikuwa ameyasema. **23** Ikawa Isa
alipokuwa Yerusalemu kwenye Sikukuu ya Pasaka,
watu wengi waliona ishara na miujiza aliyokuwa
akifanya, nao wakaamini katika jina lake. **24** Lakini Isa
hakujiaminisha kwao, kwa sababu aliwajua wanadamu
wote. **25** Hakuhitaji ushuhuda wa mtu yeyote kuhusu
mwanadamu, kwa kuwa alijua yote yaliyokuwa moyoni
mwa kila mtu.

**3** Basi palikuwa na mtu mmoja Farisayo, jina
lake Nikodemo, mmoja wa Baraza la Wayahudi
lililotawala. **2** Huyu alimjia Isa usiku akamwambia,
“Mwalimu, tunajua kuwa wewe ni mwalimu uliyetumwa
na Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kufanya
miujiza hii uifanyayo wewe, kama Mungu hayuko
pamoja naye.” **3** Isa akamjibu, “Amin, amin nakuambia,
hakuna mtu anayeweza kuuona ufalme wa Mungu
kama hajazaliwa mara ya pili.” **4** Nikodemo akauliza,
“Awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Hakika hawezi
kuingia mara ya pili kwenye tumbo la mama yake ili
azaliwe!” **5** Isa akamwambia, “Amin, amin nakuambia,

hakuna mtu yeyote anayeweza kuingia ufalme wa
Mungu kama hajazaliwa kwa maji na kwa Roho. 6
Mwili huzaa mwili, lakini Roho huzaa roho. 7 Kwa hiyo
usishangae ninapokuambia, 'Huna budi kuzaliwa mara
ya pili.' 8 Upepo huvuma kokote unakopenda. Mvumo
wake unausikia lakini huwezi ukafahamu unakotoka
wala unakoenda. Ndivyo ilivyo kwa kila mtu aliyezaliwa
na Roho." 9 Nikodemo akamuuliza, "Mambo haya
yanawezekanaje?" 10 Isa akamwambia, "Wewe ni
mwalimu wa Waisraeli, nawe huelewi mambo haya?
11 Amin, amin ninakuambia, sisi tunazungumza lile
tunalolijua na tunashuhudia lile tulililoliona. Lakini ninyi
watu hamkubali ushuhuda wetu. 12 Nimewaambia
mambo ya duniani, nanyi hamkuniamini, mtaniaminije
basi nitakapowaambia mambo ya mbinguni? 13
Hakuna mtu yeyote aliyeenda mbinguni isipokuwa
yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani Mwana wa
Adamu. 14 Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka
kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana
budi kuinuliwa juu, 15 ili kila mtu amwaminiye awe
na uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 16 "Kwa maana
jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa
Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee,
bali awe na uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 17 Kwa
maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu
ulimwengu, bali kupitia kwake ulimwengu upate
kuokolewa. 18 Yeyote amwaminiye hahukumiwi, lakini
asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu
hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu. 19 Hii
ndiyo hukumu: Kwamba nuru imekuja ulimwenguni,
nao watu wakapenda giza kuliko nuru, kwa sababu
matendo yao ni maovu. 20 Kwa kuwa kila atendaye
maovu huchukia nuru, wala haji kwenye nuru ili
matendo yake maovu yasifichuliwe. 21 Lakini yule
aishiye kwa ukweli huja kwenye nuru, ili ionekane
wazi kwamba matendo yake yametendeka katika
Mungu." 22 Baada ya haya, Isa na wanafunzi wake
walienda katika eneo la Yudea, nao wakakaa huko
kwa muda na kubatiza watu. 23 Yahya naye alikuwa
akibatiza watu huko Ainoni karibu na Salimu, kwa
sababu huko kulikuwa na maji mengi. Watu wakamjia
huko ili kubatizwa. 24 (Hii ilikuwa kabla Yahya
hajafungwa gerezani.) 25 Mashindano yakazuka kati
ya baadhi ya wanafunzi wa Yahya na Myahudi mmoja
kuhusu suala la desturi ya kunawa kwa utakaso. 26
Wakamwendea Yahya wakamwambia, "Mwalimu,
yule mtu aliyekuwa pamoja nawe ng'ambo ya Yordani,
yule uliyeshuhudia habari zake, sasa anabatiza na
kila mtu anamwendea!" 27 Yahya akawajibu, "Hakuna
mtu yeyote awezaye kupata kitu chochote isipokuwa
kile tu alichopewa kutoka mbinguni. 28 Ninyi wenyewe
ni mashahidi wangu kwamba nilisema, 'Mimi si Al-
Masihi, ila nimetumwa nimtangulie.' 29 Bibi arusi
ni wa bwana arusi. Lakini rafiki yake bwana arusi
anayesimama karibu naye na kusikiliza kutoka kwake,
hufurahi sana aisikiapo sauti ya bwana arusi. Kwa
sababu hii furaha yangu imekamilika. 30 Yeye hana
budi kuwa mkuu zaidi na mimi nizidi kupungua. 31
"Yeye ajaye kutoka juu yu juu ya yote, yeye aliye
wa duniani ni wa dunia, naye huzungumza mambo
ya duniani. Yeye aliyekuja kutoka mbinguni, yu juu
ya yote. 32 Yeye hushuhudia yale aliyoyaona na
kuyasikia, lakini hakuna yeyote anayekubali ushuhuda
wake. 33 Lakini yeyote anayekubali huo ushuhuda
anathibitisha kwamba, Mungu ni kweli. 34 Yeye
aliyetumwa na Mungu husema maneno ya Mungu,
kwa kuwa Mungu humpa Roho wake pasipo kipimo.
35 Baba anampenda Mwana, naye ametia vitu vyote
mkononi mwake. 36 Yeyote anayemwamini Mwana
ana uzima wa milele, lakini yeye asiyemwamini
Mwana hatauona uzima, bali ghadhabu ya Mungu
itakuwa juu yake." **(aiōnios g166)**

**4** Isa alipata habari kuwa Mafarisayo walisikia
kwamba yeye alikuwa akipata wanafunzi kuliko
Yahya na kuwabatiza, 2 ingawa kwa kweli si Isa
mwenyewe aliyekuwa akibatiza, ila ni wanafunzi
wake. 3 Bwana Isa alipojua mambo haya, aliondoka
Yudea akarudi tena Galilaya. 4 Wakati huo ilimlazimu
apitie Samaria. 5 Akafika kwenye mji mmoja wa
Samaria uitwao Sikari, karibu na lile shamba ambalo
Yakobo alimpa mwanawe Yusufu. 6 Kisima cha
Yakobo kilikuwa huko. Naye Isa alikuwa amechoka
kwa kuwa alikuwa ametoka safarini. Akaketi karibu
na hicho kisima. Ilikuwa yapata saa sita mchana.
7 Mwanamke mmoja Msamaria alipokuja kuteka
maji, Isa akamwambia, "Naomba maji ninywe." 8
(Wakati huo wanafunzi wake walikuwa wameenda
mjini kununua chakula.) 9 Yule mwanamke Msamaria
akamjibu, "Wewe ni Myahudi na mimi ni Msamaria.
Yawezekanaje uniombe maji ya kunywa?" (Wayahudi
walikuwa hawashirikiani kabisa na Wasamaria.) 10
Isa akamjibu, "Kama ungeijua karama ya Mungu, na

ni nani anakuomba maji ya kunywa, ungemwomba yeye, naye angekupa maji ya uzima." 11 Yule mwanamke akamjibu, "Bwana, wewe huna chombo cha kutekea maji na kisima hiki ni kirefu. Hayo maji ya uzima utayapata wapi? 12 Kwani wewe ni mkuu kuliko baba yetu Yakobo ambaye alitupatia kisima hiki, ambacho yeye pamoja na watoto wake na mifugo yake walikitumia?" 13 Isa akamjibu, "Kila mtu anayekunywa maji ya kisima hiki ataona kiu tena. 14 Lakini yeyote anywaye maji nitakayompa hataona kiu kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujika uzima wa milele." **(aiōn g165, aiōnios g166)** 15 Yule mwanamke akamwambia, "Bwana, tafadhali nipe maji hayo ili nisipate kiu tena, wala nisije tena hapa kuteka maji!" 16 Isa akamjibu, "Nenda ukamwite mumeo, uje naye hapa." 17 Yule mwanamke akajibu, "Sina mume." Isa akamwambia, "Umesema kweli kuwa huna mume. 18 Kwa maana umeshakuwa na wanaume watano, na mwanaume unayeishi naye sasa si mume wako! Umesema ukweli." 19 Yule mwanamke akasema, "Bwana, naona bila shaka wewe ni nabii. 20 Baba zetu waliabudu kwenye mlima huu, lakini ninyi Wayahudi mnasema ni lazima tukaabudu huko Yerusalemu." 21 Isa akamjibu, "Mwanamke, niamini: wakati unakuja ambapo hamtamwabudu Baba katika mlima huu, wala huko Yerusalemu. 22 Ninyi Wasamaria mnaabudu msichokijua. Sisi Wayahudi tunamwabudu Mungu tunayemjua kwa sababu wokovu unatoka kwa Wayahudi. 23 Lakini saa yaja, tena ipo, ambapo wale waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho na kweli. Kwa maana Baba anawatafuta watu wanaomwabudu kwa namna hii. 24 Mungu ni Roho, na wote wanaomwabudu imewapasa kumwabudu katika roho na kweli." 25 Yule mwanamke akamwambia, "Ninafahamu kwamba Al-Masihi" (yaani Aliyetiwa mafuta) "anakuja. Yeye akija, atatueleza mambo yote." 26 Isa akamwambia, "Mimi ninayezungumza nawe, ndiye." 27 Wakati huo wanafunzi wake wakarudi, wakashangaa sana kumwona akizungumza na mwanamke. Lakini hakuna aliyemuuliza, "Unataka nini kwake?" Au, "Kwa nini unazungumza naye?" 28 Yule mwanamke akaacha mtungi wake, akarudi mjini, akawaambia watu, 29 "Njooni mkamwone mtu aliyeniambia kila kitu nilichotenda! Je, yawezekana huyu ndiye Al-Masihi?" 30 Basi wakamiminika watu kutoka mjini, wakamwendea Isa. 31 Wakati huo wanafunzi wake walikuwa wakimsihi, "Mwalimu, kula." 32 Lakini yeye akawajibu, "Mimi ninacho chakula ambacho ninyi hamkifahamu." 33 Basi wanafunzi wakaanza kuulizana, "Kuna mtu ambaye amemletea chakula?" 34 Lakini Isa akawajibu, "Chakula changu ni kufanya mapenzi ya Mungu ambaye amenituma na kuikamilisha kazi yake. 35 Je, ninyi hamsemi, 'Bado miezi minne tuvune'? Inueni macho yenu myaangalie mashamba jinsi mazao yalivyo tayari kuvunwa! 36 Mvunaji tayari anapokea mshahara wake, naye anakusanya mazao kwa ajili ya uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wafurahi pamoja. **(aiōnios g166)** 37 Hivyo ule msemo, 'Mmoja hupanda na mwingine huvuna,' ni kweli kabisa. 38 Niliwatuma mkavune mazao ambayo hamkupanda. Wengine walifanya kazi ngumu, nanyi mmevuna faida ya taabu yao." 39 Wasamaria wengi katika mji ule wakamwamini Isa kwa sababu ya ushuhuda wa yule mwanamke alipowaambia kwamba, "Ameniambia kila kitu nilichotenda." 40 Hivyo wale Wasamaria walipomjia, wakamsihi akae kwao. Naye akakaa huko siku mbili. 41 Kwa sababu ya neno lake, watu wengi wakaamini. 42 Wakamwambia yule mwanamke, "Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu, bali kwa kuwa tumemsikia sisi wenyewe. Tumejua hakika kwamba huyu ndiye Al-Masihi, Mwokozi wa ulimwengu." 43 Baada ya zile siku mbili, Isa aliondoka kwenda Galilaya. 44 (Basi Isa mwenyewe alikuwa amesema kwamba nabii hapati heshima katika nchi yake mwenyewe.) 45 Alipofika Galilaya, Wagalilaya walimkaribisha, kwani walikuwa wameona yale aliyoyatenda huko Yerusalemu wakati wa Sikukuu ya Pasaka. Kwa maana wao pia walikuwa wamehudhuria hiyo Sikukuu. 46 Hivyo Isa akafika tena Kana ya Galilaya, kule alikuwa amebadili maji kuwa divai. Kulikuwa na afisa mmoja wa mfalme, ambaye mwanawe alikuwa mgonjwa huko Kapernaumu. 47 Huyo mtu aliposikia kwamba Isa alikuwa amewasili Galilaya kutoka Yudea, alimwendea na kumsihi aende akamponye mwanawe, aliyekuwa mgonjwa karibu ya kufa. 48 Isa akamwambia, "Ninyi watu msipoona ishara na miujiza kamwe hamtaamini." 49 Yule afisa wa mfalme akamwambia, "Bwana, tafadhali shuka kabla mwanangu hajafa." 50 Isa akamjibu, "Nenda zako, mwanao yu hai." Yule afisa akaamini

yale maneno Isa aliyomwambia, akaenda zake. 51
Alipokuwa bado yuko njiani, akakutana na watumishi
wake, wakamwambia kwamba mwanawe yu mzima.
52 Akawauliza saa ambayo alianza kupata nafuu.
Wakamwambia, “Jana saa saba, ndipo homa iliisha.”
53 Ndipo baba wa huyo mtoto akakumbuka kuwa huo
ndio wakati Isa alikuwa amemwambia, “Mwanao yu
hai.” Kwa hiyo yeye na wote wa nyumbani mwake
wakamwamini Isa. 54 Hii ilikuwa ishara ya pili ambayo
Isa alifanya aliporudi Galilaya kutoka Yudea.

**5** Baada ya haya, kulikuwa na Sikukuu ya Wayahudi,
naye Isa akapanda kwenda Yerusalemu. 2 Huko
Yerusalemu, karibu na mlango uitwao Mlango wa
Kondoo, palikuwa na bwawa moja lililoitwa Bethzatha
kwa Kiebrania, ambalo lilikuwa limezungukwa na
makumbi matano. 3 Hapa palikuwa na idadi kubwa
ya wasiojiweza, yaani vipofu, viwete, na waliopooza
[wakingojea maji yatibuliwe. 4 Kwa maana malaika
alikuwa akishuka wakati fulani, akayatibua maji.
Yule angekuwa wa kwanza kuingia ndani baada ya
maji kutibuliwa alipona ugonjwa wowote aliokuwa
nao]. 5 Mtu mmoja aliyekuwa ameugua kwa miaka
thelathini na nane alikuwa hapo. 6 Isa alipomwona
akiwa amelala hapo, na akijua amekuwa katika hali
hiyo kwa muda mrefu, akamwambia, “Je, wataka
kuponywa?” 7 Yule mgonjwa akamjibu, “Bwana, mimi
sina mtu wa kuniingiza bwawani maji yanapotibuliwa.
Nami ninapotaka kutumbukia bwawani, mtu mwingine
huingia kabla yangu.” 8 Isa akamwambia, “Inuka!
Chukua mkeka wako na uende.” 9 Mara yule
mtu akapona, akachukua mkeka wake, akaanza
kutembea. Basi siku hiyo ilikuwa siku ya Sabato.
10 Kwa hiyo viongozi wa Wayahudi wakamwambia
yule mtu aliyeponywa, “Leo ni Sabato; si halali
wewe kubeba mkeka wako.” 11 Yeye akawajibu,
“Yule mtu aliyeniponya aliniambia, ‘Chukua mkeka
wako na uende.’” 12 Wakamuuliza, “Ni mtu gani
huyo aliyekuambia uchukue mkeka wako uende?”
13 Basi yule mtu aliyeponywa hakufahamu ni nani
aliyemponya, kwa sababu Isa alikuwa amepotea ndani
ya umati ule wa watu waliokuwa hapo. 14 Baadaye Isa
akamkuta yule mtu aliyemponya ndani ya Hekalu na
kumwambia, “Tazama umeponywa. Usitende dhambi
tena, lisije likakupata jambo baya zaidi.” 15 Yule mtu
akaenda, akawaambia wale viongozi wa Wayahudi
kuwa ni Isa aliyemponya. 16 Kwa hiyo viongozi wa
Wayahudi wakaanza kumsumbua Isa, kwa sababu
alikuwa anafanya mambo kama hayo siku ya Sabato.
17 Isa akawajibu, “Baba yangu anafanya kazi yake
daima hata siku hii ya leo, nami pia ninafanya
kazi.” 18 Maneno haya yaliwaudhi sana viongozi
wa Wayahudi. Wakajaribu kila njia wapate jinsi ya
kumuua, kwani si kwamba alivunja Sabato tu, bali
alikuwa akimwita Mungu Baba yake, hivyo kujifanya
sawa na Mungu. 19 Isa akawaambia, “Amin, amin
nawaambia, Mwana hawezi kufanya jambo lolote
peke yake. Yeye aweza tu kufanya lile analomwona
Baba yake akifanya, kwa maana lolote afanyalo Baba,
Mwana pia hufanya vivyo hivyo. 20 Baba ampenda
Mwana na kumwonesha yale ambayo yeye Baba
mwenyewe anayafanya, naye atamwonesha kazi kuu
kuliko hizi ili mpate kushangaa. 21 Hakika kama vile
Baba awafufuavyo wafu na kuwapa uzima, vivyo hivyo
Mwana huwapa uzima wale anaopenda. 22 Wala Baba
hamhukumu mtu yeyote, lakini hukumu yote amempa
Mwana, 23 ili wote wamheshimu Mwana kama vile
wanavyomheshimu Baba. Yeyote asiyemheshimu
Mwana, hamheshimu Baba aliyemtuma. 24 “Amin,
amin nawaambia, yeyote anayesikia maneno yangu
na kumwamini yeye aliyenituma anao uzima wa
milele, naye hatahukumiwa, bali amepita kutoka
mautini na kuingia uzimani. **(aiōnios g166)** 25 Amin,
amin nawaambia, saa yaja, nayo saa ipo, wafu
watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, nao
watakaoisikia watakuwa hai. 26 Kama vile Baba
alivyo na uzima ndani yake, vivyo hivyo amempa
Mwana kuwa na uzima ndani yake. 27 Naye amempa
Mwanawe mamlaka ya kuhukumu kwa kuwa yeye
ni Mwana wa Adamu. 28 “Msishangae kusikia
haya, kwa maana saa inakuja ambapo wale walio
makaburini wataisikia sauti yake, 29 nao watatoka
makaburini. Wale waliotenda mema watafufuka
wapate uzima, nao wale waliotenda maovu watafufuka
ili wahukumiwe. 30 “Mimi siwezi kufanya jambo lolote
peke yangu. Ninavyosikia ndivyo ninavyohukumu,
nayo hukumu yangu ni ya haki kwa kuwa sitafuti
kufanya mapenzi yangu mwenyewe, bali mapenzi
yake yeye aliyenituma. 31 “Kama ningejishuhudia
mimi mwenyewe, ushuhuda wangu si kweli. 32
Lakini yuko mwingine anishuhudiaye, na ninajua
kwamba ushuhuda wake ni wa kweli. 33 “Mlituma
wajumbe kwa Yahya, naye akaishuhudia kweli. 34

Si kwamba naukubali ushuhuda wa mwanadamu;
la, bali ninalitaja hili ili ninyi mpate kuokolewa. 35
Yahya alikuwa taa iliyowaka na kutoa nuru, nanyi
kwa muda mlichagua kuifurahia nuru yake. 36 “Ninao
ushuhuda mkuu kuliko ule wa Yahya. Kazi ambazo
Baba amenituma nizikamilishe, naam, kazi hizi
ninazofanya, zinashuhudia kuwa Baba amenituma.
37 Naye Baba mwenyewe ameshuhudia juu yangu.
Hamjapata kamwe kuisikia sauti yake wala kuona
umbo lake, 38 wala hamna neno lake ndani yenu,
kwa sababu hamkumwamini yeye aliyetumwa naye.
39 Ninyi mnachunguza Maandiko mkidhani ya kuwa
ndani yake mna uzima wa milele. Maandiko haya
ndio yanayonishuhudia mimi. **(aiōnios g166)** 40 Lakini
mnakataa kuja kwangu ili mpate uzima. 41 “Mimi
sikubali kutukuzwa na wanadamu, 42 lakini mimi
ninawafahamu. Ninajua kwamba hamna upendo
wa Mungu mioyoni mwenu. 43 Mimi nimekuja kwa
jina la Baba yangu, nanyi hamnipokei. Lakini mtu
mwingine akija kwa jina lake mwenyewe, mtampokea.
44 Mnawezaje kuamini ikiwa mnapeana utukufu
ninyi kwa ninyi, lakini hamfanyi bidii kupata utukufu
unaotoka kwa Mungu? 45 “Lakini msidhani kuwa
mimi nitawashtaki mbele za Baba. Mshtaki wenu
ni Musa, ambaye mmemwekea tumaini lenu. 46
Kama mngemwamini Musa, mngeniamini na mimi,
kwa maana aliandika habari zangu. 47 Lakini
ikiwa hamwamini aliyoandika Musa, mtaaminije
ninayoyasema?”

**6** Baada ya haya, Isa alienda ng’ambo ya Bahari ya
Galilaya (ambayo pia huitwa Bahari ya Tiberia). 2
Umati mkubwa wa watu waliendelea kumfuata, kwa
sababu waliona ishara nyingi za miujiza alizofanya kwa
wagonjwa. 3 Kisha Isa akapanda mlimani akaketi huko
pamoja na wanafunzi wake. 4 Pasaka ya Wayahudi
ilikuwa imekaribia. 5 Isa alipotazama na kuona umati
ule mkubwa wa watu wakimjia, akamwambia Filipo,
“Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?” 6 Aliuliza
swali hili kumpima, kwa maana alishajua la kufanya.
7 Filipo akamjibu, “Hata fedha kiasi cha dinari mia
mbili hazitoshi kununua mikate ya kuwapa watu hawa
ili kila mtu apate kidogo.” 8 Mmoja wa wanafunzi
wake aitwaye Andrea, ndugu yake Simoni Petro,
akamwambia, 9 “Hapa kuna mvulana mmoja mwenye
mikate mitano ya shayiri na samaki wawili wadogo.
Lakini hivi vitatosha nini kwa watu hawa wote?” 10
Isa akasema, “Waketisheni watu chini.” Palikuwa na
majani mengi katika eneo lile, nao watu wakaketi
(palikuwa na wanaume wapatao elfu tano). 11 Ndipo
Isa akachukua ile mikate, akamshukuru Mungu na
kuwagawia wale watu waliokuwa wameketi. Akafanya
vivyo hivyo na wale samaki. Kila mtu akapata kadiri
alivyotaka. 12 Watu wote walipokwisha kula na
kushiba, akawaambia wanafunzi wake, “Kusanyeni
vipande vilivyobaki vya ile mikate, kisipotee chochote.”
13 Hivyo wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na
viwili kwa vipande vya ile mikate mitano ya shayiri
na samaki wale wawili wadogo vilivyobakishwa na
waliokula. 14 Baada ya watu kuona muujiza ule
Isa aliofanya, walianza kusema, “Hakika huyu ndiye
Nabii ajaye ulimwenguni!” 15 Isa akijua kwamba
walitaka kuja kumfanya awe mfalme wao, kwa nguvu,
akajitenga nao akaenda milimani peke yake. 16
Ilipofika jioni, wanafunzi wake waliteremka kwenda
baharini. 17 Wakaingia kwenye mashua, wakaanza
kuvuka bahari kwenda Kapernaumu. Wakati huu
kulikuwa tayari giza na Isa alikuwa hajajumuika
nao. 18 Bahari ikachafuka kwa sababu upepo
mkali ulikuwa unavuma. 19 Wanafunzi walipokuwa
wameenda mwendo wa maili tatu au nne, walimwona
Isa akitembea juu ya maji akikaribia mashua, nao
wakaogopa sana. 20 Lakini Isa akawaambia, “Ni
mimi. Msiogope.” 21 Ndipo wakamkaribisha kwa
furaha ndani ya mashua, na mara wakafika ufuoni
walikokuwa wakienda. 22 Siku iliyofuata, wale watu
waliokuwa wamebaki ng’ambo waliona kwamba
palikuwa na mashua moja tu, na kwamba Isa hakuwa
ameondoka pamoja na wanafunzi wake, ila walikuwa
wameondoka peke yao. 23 Lakini zikaja mashua
nyingine kutoka Tiberia zikafika karibu na mahali pale
walipokula mikate baada ya Bwana Isa kumshukuru
Mungu. 24 Mara wale watu wakatambua kwamba
Isa hakuwa hapo, wala wanafunzi wake. Wakaingia
kwenye mashua hizo, wakaenda Kapernaumu ili
kumtafuta Isa. 25 Walipomkuta Isa ng’ambo ya
bahari wakamuuliza, “Mwalimu, umefika lini huku?”
26 Isa akawajibu, “Amin, amin nawaambia, ninyi
hamnitafuti kwa kuwa mliona ishara na miujiza,
bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba. 27
Msishughulikie chakula kiharibikacho, bali chakula
kidumucho hata uzima wa milele, ambacho Mwana
wa Adamu atawapa. Yeye ndiye ambaye Mungu

Baba Mwenyezi amemtia muhuri.” (aiōnios g166) 28
Ndipo wakamuuliza, “Tufanye nini ili tupate kuitenda
kazi ya Mungu?” 29 Isa akawajibu, “Kazi ya Mungu
ndiyo hii: Mwaminini yeye aliyetumwa naye.” 30 Hivyo
wakamuuliza, “Utafanya ishara gani ya muujiza, ili
tuione tukuamini? Utafanya jambo gani? 31 Baba zetu
walikula mana jangwani, kama ilivyoandikwa, ‘Aliwapa
mikate kutoka mbinguni ili wale.’” 32 Isa akawaambia,
“Amin, amin nawaambia, si Musa aliyewapa mikate
kutoka mbinguni, bali Baba yangu ndiye anawapa
mkate wa kweli kutoka mbinguni. 33 Kwa maana
mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni
na kuupa ulimwengu uzima.” 34 Wakamwambia,
“Bwana, kuanzia sasa tupatie huo mkate siku zote.”
35 Isa akawaambia, “Mimi ndimi mkate wa uzima.
Yeye ajaye kwangu, hataona njaa kamwe na yeye
aniaminiye, hataona kiu kamwe. 36 Lakini kama
nilivyowaambia, mmeniona lakini bado hamwamini. 37
Wale wote anipao Baba watakuja kwangu na yeyote
ajaye kwangu, sitamfukuza nje kamwe. 38 Kwa kuwa
nimeshuka kutoka mbinguni si ili kufanya mapenzi
yangu, bali mapenzi yake yeye aliyenituma. 39
Haya ndio mapenzi yake yeye aliyenituma, kwamba,
nisimpoteze hata mmoja wa wale alionipa, bali
niwafufue siku ya mwisho. 40 Kwa maana mapenzi
ya Baba yangu ni kwamba kila mmoja amtazamaye,
Mwana na kumwamini awe na uzima wa milele,
nami nitawafufua siku ya mwisho.” (aiōnios g166) 41
Wayahudi wakaanza kunung’unika kwa kuwa alisema,
“Mimi ndimi mkate ulioshuka kutoka mbinguni.” 42
Wakasema, “Huyu si Isa, mwana wa Yusufu, ambaye
baba yake na mama yake tunawajua? Anawezaje
basi sasa kusema, ‘Nimeshuka kutoka mbinguni’?” 43
Hivyo Isa akawaambia, “Acheni kunung’unikiana ninyi
kwa ninyi. 44 Hakuna mtu awezaye kuja kwangu kama
asipovutwa na Baba aliyenituma, nami nitamfufua
siku ya mwisho. 45 Imeandikwa katika Manabii, ‘Wote
watafundishwa na Mungu.’ Yeyote amsikilizaye Baba
na kujifunza kutoka kwake, huyo huja kwangu. 46
Hakuna mtu yeyote aliyemwona Baba isipokuwa
yeye atokaye kwa Mungu, yeye ndiye peke yake
aliyemwona Baba. 47 Amin, amin nawaambia, yeye
anayeamini anao uzima wa milele. (aiōnios g166) 48
Mimi ni mkate wa uzima. 49 Baba zenu walikula mana
jangwani, lakini wakafa. 50 Lakini hapa kuna mkate
kutoka mbinguni, ambao mtu yeyote akiula, hatakufa.
51 Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni.
Mtu yeyote akiula mkate huu, ataishi milele. Mkate
huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya
uzima wa ulimwengu.” (aiōn g165) 52 Ndipo Wayahudi
wakaanza kuhojiana vikali wao kwa wao wakisema,
“Mtu huyu awezaje kutupatia mwili wake tuule?” 53
Hivyo Isa akawaambia, “Amin, amin nawaambia,
msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa
damu yake, hamna uzima ndani yenu. 54 Mtu yeyote
aulaye mwili wangu na kunywa damu yangu, anao
uzima wa milele. Nami nitamfufua siku ya mwisho.
(aiōnios g166) 55 Kwa maana mwili wangu ni chakula
cha kweli na damu yangu ni kinywaji cha kweli. 56
Yeyote alaye mwili wangu na kunywa damu yangu,
atakaa ndani yangu nami nitakaa ndani yake. 57
Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, na
kama nami ninavyoishi kwa sababu ya Baba, hivyo
anilaye mimi ataishi kwa sababu yangu. 58 Huu
ndio mkate ushukao kutoka mbinguni, si kama ule
mkate baba zenu waliokula nao wakafa. Lakini yeye
aulaye mkate huu ataishi milele.” (aiōn g165) 59 Isa
alisema maneno haya alipokuwa akifundisha katika
sinagogi huko Kapernaumu. 60 Wengi wa wafuasi
wake waliposikia jambo hili wakasema, “Mafundisho
haya ni magumu. Ni nani awezaye kuyapokea?” 61
Isa alipojua kwamba wafuasi wake wananung’unika
kuhusu mafundisho yake, akawaambia, “Je, jambo hili
limewaudhi? 62 Ingekuwaje basi kama mngemwona
Mwana wa Adamu akipaa kwenda zake huko
alipokuwa kwanza? 63 Roho ndiye atiaye uzima,
mwili haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni Roho
tena ni uzima. 64 Lakini baadhi yenu hamwamini.”
Kwa maana Isa alifahamu tangu mwanzo wale
ambao hawangemwamini miongoni mwao na yule
ambaye angemsaliti. 65 Akaendelea kusema, “Hii
ndiyo sababu niliwaambia kwamba hakuna mtu
awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba
yangu.” 66 Tangu wakati huo wafuasi wake wengi
wakarejea nyuma wakaacha kumfuata. 67 Hivyo Isa
akawauliza wale wanafunzi wake kumi na wawili,
“Je, ninyi pia mnataka kuondoka?” 68 Simoni Petro
akamjibu, “Bwana, tuondoke twende kwa nani? Wewe
unayo maneno ya uzima wa milele. (aiōnios g166) 69
Tunaamini na kujua kuwa wewe ndiwe Aliye Mtakatifu
wa Mungu.” 70 Ndipo Isa akajibu, “Je, sikuwachagua
ninyi kumi na wawili? Lakini mmoja wenu ni ibilisi.” 71

(Hapa alikuwa anasema kuhusu Yuda, mwana wa
Simoni Iskariote. Ingawa alikuwa mmoja wa wale
kumi na wawili, ndiye ambaye baadaye angemsaliti
Isa.)

**7** Baada ya mambo haya, Isa alienda sehemu
mbalimbali za Galilaya. Hakutaka kwenda Yudea
kwa sababu viongozi wa Wayahudi huko walitaka
kumuua. **2** Sikukuu ya Vibanda ya Wayahudi ilikuwa
imekaribia. **3** Hivyo ndugu zake Isa wakamwambia,
“Ondoka hapa uende Yudea ili wanafunzi Wako
wapate kuona miujiza unayofanya. **4** Mtu anayetaka
kujulikana hafanyi mambo yake kwa siri. Kama
unafanya mambo haya, jioneshe kwa ulimwengu.”
**5** Hata ndugu zake mwenyewe hawakumwamini. **6**
Isa akawaambia, “Wakati wangu bado haujawadia,
lakini wakati wenu upo siku zote. **7** Ulimwengu
hauwezi kuwachukia ninyi, lakini unanichukia mimi
kwa sababu ninawashuhudia kwamba matendo yao ni
maovu. **8** Ninyi nendeni kwenye Sikukuu, lakini mimi
sitahudhuria Sikukuu hii kwa sababu wakati wangu
haujawadia.” **9** Baada ya kusema hayo, akabaki
Galilaya. **10** Lakini ndugu zake walipokwisha kuondoka
kwenda kwenye Sikukuu, yeye pia alienda lakini kwa
siri. **11** Viongozi wa Wayahudi walikuwa wakimtafuta
huko kwenye Sikukuu na kuulizana, “Yuko wapi huyu
mtu?” **12** Kulikuwa na minong’ono iliyoenea kumhusu
Isa katika umati wa watu, wakati wengine wakisema,
“Ni mtu mwema.” Wengine walikuwa wakisema,
“La, yeye anawadanganya watu.” **13** Lakini hakuna
mtu yeyote aliyemsema waziwazi kwa sababu ya
kuwaogopa viongozi wa Wayahudi. **14** Ilipokaribia
katikati ya Sikukuu, Isa alipanda kwenda Hekaluni
na kuanza kufundisha. **15** Wayahudi wakastaajabia
mafundisho yake wakasema, “Mtu huyu amepataje
kujua mambo haya bila kufundishwa?” **16** Ndipo Isa
akawajibu, “Mafundisho yangu si yangu mwenyewe,
bali yanatoka kwake yeye aliyenituma. **17** Mtu yeyote
akipenda kufanya mapenzi ya Mungu, atajua kama
mafundisho yangu yanatoka kwa Mungu au ninasema
kwa ajili yangu mwenyewe. **18** Wale wanenao kwa
ajili yao wenyewe hufanya hivyo kwa kutaka utukufu
wao wenyewe. Lakini yeye atafutaye utukufu wa
yule aliyemtuma ni wa kweli, wala hakuna uongo
ndani yake. **19** Je, Musa hakuwapa ninyi sheria?
Lakini hakuna hata mmoja wenu anayeishika hiyo
sheria. Kwa nini mnataka kuniua?” **20** Ule umati wa
watu wakamjibu, “Wewe una pepo mchafu! Ni nani
anayetaka kukuua?” **21** Isa akawajibu, “Nimefanya
muujiza mmoja na nyote mkastaajabu. **22** Lakini
kwa kuwa Musa aliwaamuru tohara (ingawa kwa
kweli haikutoka kwa Musa bali kwa baba zetu wa
zamani), mnamtahiri mtoto hata siku ya Sabato. **23**
Ikiwa mtoto aweza kutahiriwa siku ya Sabato kusudi
Torati ya Musa isivunjwe, kwa nini mnanikasirikia kwa
kumponya mtu mwili wake wote siku ya Sabato? **24**
Acheni kuhukumu mambo kwa jinsi mnavyoona tu,
bali hukumuni kwa haki.” **25** Ndipo baadhi ya watu wa
Yerusalemu wakawa wanasema, “Tazameni, huyu si
yule mtu wanayetaka kumuua? **26** Mbona yuko hapa
anazungumza hadharani, na wala hawamwambii
neno lolote? Je, inawezekana viongozi wanafahamu
kuwa huyu ndiye Al-Masihi? **27** Tunafahamu huyu
mtu anakotoka, lakini Al-Masihi atakapokuja, hakuna
yeyote atakayejua atokako.” **28** Ndipo Isa, akaendelea
kufundisha Hekaluni, akisema, “Ninyi mnanifahamu na
kujua nitokako. Mimi sikuja kwa ajili yangu mwenyewe,
bali yeye aliyenituma ni wa kweli na ninyi hammjui. **29**
Mimi namjua kwa kuwa nimetoka kwake, naye ndiye
alinituma.” **30** Ndipo wakatafuta kumkamata, lakini
hakuna mtu yeyote aliyethubutu kumshika kwa sababu
saa yake ilikuwa bado haijawadia. **31** Nao watu wengi
wakamwamini, wakasema, “Je, Al-Masihi atakapokuja,
atafanya miujiza mikuu kuliko aliyoifanya mtu huyu?”
**32** Mafarisayo wakasikia watu wakinong’ona mambo
kama hayo kuhusu Isa, ndipo wao pamoja na viongozi
wa makuhani wakatuma walinzi wa Hekalu waende
kumkamata. **33** Isa akasema, “Mimi bado niko pamoja
nanyi kwa kitambo kidogo, kisha nitarudi kwake
yeye aliyenituma. **34** Mtanitafuta lakini hamtaniona,
nami niliko ninyi hamwezi kuja.” **35** Wayahudi
wakaulizana wao kwa wao, “Huyu mtu anataka
kwenda wapi ambako hatuwezi kumfuata? Je, anataka
kwenda kwa Wayunani ambako baadhi ya watu
wetu wametawanyikia, akawafundishe Wayunani?
**36** Yeye ana maana gani anaposema, ‘Mtanitafuta
lakini hamtaniona,’ na, ‘nami niliko ninyi hamwezi
kuja’?” **37** Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu,
wakati Isa akiwa amesimama huko, akapaza sauti
yake akasema, “Kama mtu yeyote anaona kiu na aje
kwangu anywe. **38** Yeyote aniaminiye mimi, kama
Maandiko yanavyosema, vijito vya maji ya uzima
vitatiririka kutoka ndani yake.” **39** Isa aliposema haya,

alimaanisha Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye
wote waliomwamini wangempokea. Kwa maana hadi
wakati huo Roho wa Mungu alikuwa hajatolewa, kwa
kuwa Isa alikuwa bado hajatukuzwa. **40** Waliposikia
maneno hayo, baadhi ya watu miongoni mwa umati
ule wakasema, “Hakika huyu ndiye yule Nabii.” **41**
Wengine wakasema, “Huyu ndiye Al-Masihi!” Lakini
wengine wakauliza, “Je, Al-Masihi kwao ni Galilaya?
**42** Je, Maandiko hayasemi kwamba Al-Masihi atakuja
kutoka jamaa ya Daudi na kutoka Bethlehemu, mji
alioishi Daudi?” **43** Kwa hiyo watu wakagawanyika kwa
ajili ya Isa. **44** Baadhi yao walitaka kumkamata, lakini
hakuna aliyethubutu kumgusa. **45** Hatimaye wale
walinzi wa Hekalu wakarudi kwa viongozi wa makuhani
na Mafarisayo waliokuwa wamewatuma ili kumkamata
Isa, wakaulizwa, “Mbona hamkumkamata?” **46** Wale
walinzi wakajibu, “Kamwe hajanena mtu yeyote kama
yeye anenavyo.” **47** Mafarisayo wakajibu, “Je, nanyi
pia mmedanganyika? **48** Je, kuna kiongozi yeyote
au mmoja wa Mafarisayo ambaye amemwamini? **49**
Lakini umati huu wa watu wasiojua Torati ya Musa,
wamelaaniwa.” **50** Ndipo Nikodemo, yule aliyekuwa
amemwendea Isa siku moja usiku, na alikuwa mmoja
wao, akauliza, **51** “Je, sheria zetu zinaturuhusu
kumhukumu mtu kabla ya kumsikiliza na kufahamu
alilotenda?” **52** Wakamjibu, “Je, wewe pia unatoka
Galilaya? Chunguza nawe utaona kwamba hakuna
nabii atokae Galilaya!” [ **53** Kisha wakaondoka, kila
mtu akarudi nyumbani mwake.

**8** Lakini Isa akaenda katika Mlima wa Mizeituni.
**2** Alfajiri na mapema Isa akaja tena Hekaluni;
watu wote wakakusanyika, naye akaketi, akaanza
kuwafundisha. **3** Walimu wa Torati na Mafarisayo
wakamleta mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini.
Wakamsimamisha katikati ya umati wa watu wote.
**4** Wakamwambia Isa, “Mwalimu, huyu mwanamke
amekutwa akizini. **5** Katika sheria, Musa alituamuru
kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, hadi
wafe. Sasa wewe wasemaje?” **6** Walimuuliza swali hili
kama mtego ili wapate sababu ya kumshtaki. Lakini
Isa akainama akaanza kuandika ardhini kwa kidole
chake. **7** Walipoendelea kumuulizauliza akainuka,
akawaambia, “Kama kuna mtu yeyote miongoni
mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza
kumtupia jiwe.” **8** Akainama tena na kuandika ardhini.
**9** Waliposikia haya, wakaanza kuondoka mmoja
mmoja, wakianzia wazee, hadi Isa akabaki peke yake
na yule mwanamke akiwa amesimama mbele yake. **10**
Isa akainuka na kumwambia, “Mwanamke, wako wapi
wale waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?”
**11** Yule mwanamke akajibu, “Hakuna hata mmoja,
Bwana.” Isa akamwambia, “Hata mimi sikuhukumu.
Nenda zako. Kuanzia sasa usitende dhambi tena.”]
**12** Kisha Isa akasema nao tena, akawaambia, “Mimi ni
nuru ya ulimwengu. Mtu yeyote akinifuata, hatatembea
gizani kamwe, bali atakuwa na nuru ya uzima.”
**13** Mafarisayo wakamwambia, “Ushuhuda wako
haukubaliki, kwa kuwa unajishuhudia mwenyewe.” **14**
Isa akawajibu, “Hata kama najishuhudia mwenyewe,
ushuhuda wangu ni kweli, kwa sababu najua nilikotoka
na ninakoenda. Lakini ninyi hamjui nilikotoka wala
ninakoenda. **15** Ninyi mnahukumu kwa kufuata vipimo
vya kibinadamu; mimi simhukumu mtu yeyote. **16**
Lakini hata nikihukumu, uamuzi wangu ni sahihi
kwa sababu sitoi hukumu yangu peke yangu, bali
niko pamoja na Baba, aliyenituma. **17** Imeandikwa
katika Torati yenu kwamba ushahidi wa watu wawili ni
thabiti. **18** Mimi najishuhudia mwenyewe, naye Baba
aliyenituma hunishuhudia.” **19** Ndipo wakamuuliza,
“Huyo Baba yako yuko wapi?” Isa akawajibu, “Ninyi
hamnifahamu mimi ni nani, wala hammfahamu Baba
yangu. Kama mngenifahamu mimi, mngemfahamu na
Baba yangu.” **20** Isa alisema maneno haya alipokuwa
akifundisha katika chumba cha hazina Hekaluni. Lakini
hakuna mtu aliyemkamata kwa kuwa saa yake ilikuwa
haijawadia. **21** Isa akawaambia tena, “Ninaenda
zangu, nanyi mtanitafuta, lakini mtakufa katika dhambi
zenu. Niendako mimi, ninyi hamwezi kuja.” **22** Ndipo
wale Wayahudi wakasema, “Je, atajiua? Je, hii ndiyo
sababu amesema, ‘Niendako mimi ninyi hamwezi
kuja’?” **23** Akawaambia, “Ninyi mmetoka chini; mimi
nimetoka juu. Ninyi ni wa ulimwengu huu; mimi si
wa ulimwengu huu. **24** Niliwaambia kuwa mtakufa
katika dhambi zenu; kwa maana msipoamini kwamba
‘Mimi Ndiye,’ mtakufa katika dhambi zenu.” **25**
Wakamuuliza, “Wewe ni nani?” Naye Isa akawajibu,
“Mimi ndiye yule ambaye nimekuwa nikiwaambia tangu
mwanzo. **26** Nina mambo mengi ya kusema kuwahusu
ya kuwahukumu. Lakini yeye aliyenituma ni wa
kuaminika, nami nanena na ulimwengu niliyoyasikia
kutoka kwake.” **27** Hawakuelewa kuwa alikuwa
akiwaambia kuhusu Baba yake wa Mbinguni. **28**

Kisha Isa akawaambia, “Mtakapokwisha kumwinua
Mwana wa Adamu juu, ndipo mtajua kuwa mimi
ndiye yule niliyesema, na kwamba mimi sitendi jambo
lolote peke yangu, bali ninasema yale tu Baba yangu
amenifundisha. **29** Yeye aliyenituma yu pamoja nami;
hajaniacha, kwa kuwa siku zote nafanya mapenzi
yake.” **30** Wengi waliomsikia Isa akisema maneno
haya wakamwamini. **31** Kisha Isa akawaambia wale
Wayahudi waliomwamini, “Mkidumu katika maneno
yangu, mtakuwa wanafunzi wangu kweli kweli. **32**
Ndipo mtaijua kweli, nayo kweli itawaweka huru.” **33**
Wao wakamjibu, “Sisi tu wazao wa Ibrahimu, nasi
hatujakuwa watumwa wa mtu yeyote. Wawezaje
kusema kwamba tutawekwa huru?” **34** Isa akajibu,
“Amin, amin nawaambia, kila atendaye dhambi ni
mtumwa wa dhambi. **35** Mtumwa hakai nyumbani
anakotumika siku zote, lakini mwana hukaa nyumbani
daima. **(aiōn g165)** **36** Hivyo Mwana akiwaweka huru
mtakuwa huru kweli kweli. **37** Ninajua ya kuwa ninyi ni
wazao wa Ibrahimu, lakini mnatafuta wasaa wa kuniua
kwa sababu ndani yenu hamna nafasi ya neno langu.
**38** Ninasema yale niliyoyaona nikiwa mbele za Baba
yangu, nanyi mnafanya yale mliyosikia kutoka kwa
baba yenu.” **39** Wakajibu, “Baba yetu ni Ibrahimu.” Isa
akawaambia, “Kama mngekuwa wazao wa Ibrahimu,
mngefanya mambo yale aliyofanya Ibrahimu. **40**
Lakini sasa ninyi mnatafuta kuniua, mtu ambaye
nimewaambia kweli ile niliyosikia kutoka kwa Mungu.
Ibrahimu hakufanya jambo la namna hii. **41** Ninyi
mnafanya mambo afanyayo baba yenu.” Wakamjibu,
“Sisi hatukuzaliwa kwa uzinzi. Tunaye Baba mmoja,
Mungu pekee.” **42** Isa akawaambia, “Kama Mungu
angekuwa Baba yenu, mngenipenda, kwa maana
nilitoka kwa Mungu na sasa niko hapa. Sikuja kwa
ajili yangu mwenyewe, ila yeye alinituma. **43** Kwa
nini hamwelewi ninayowaambia? Ni kwa sababu
hamwezi kusikia nisemacho. **44** Ninyi ni watoto wa
baba yenu, ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa
ya baba yenu. Yeye alikuwa muuaji tangu mwanzo,
wala hakushikana na kweli, maana hamna kweli ndani
yake. Anaposema uongo, yeye husema lugha yake
ya asili kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo
uongo. **45** Lakini kwa sababu nimewaambia kweli,
hamkuniamini! **46** Je, kuna yeyote miongoni mwenu
awezaye kunithibitisha kuwa mwenye dhambi? Kama
nawaambia yaliyo kweli, mbona hamniamini? **47** Yeye
atokaye kwa Mungu husikia kile Mungu asemacho.
Sababu ya ninyi kutosikia ni kwa kuwa hamtokani
na Mungu.” **48** Wayahudi wakamjibu Isa, “Je, hatuko
sahihi tunaposema kwamba wewe ni Msamaria,
na kwamba una pepo mchafu?” **49** Isa akawajibu,
“Mimi sina pepo mchafu, bali ninamheshimu Baba
yangu, nanyi mnanidharau. **50** Lakini mimi sitafuti
utukufu wangu mwenyewe, bali yuko anayetaka
kunitukuza, naye ndiye mwamuzi. **51** Amin, amin
nawaambia, mtu yeyote akilitii neno langu, hataona
mauti milele.” **(aiōn g165)** **52** Ndipo Wayahudi wakapaza
sauti, wakamwambia, “Sasa tumejua kwamba una
pepo mchafu! Ibrahimu alikufa, na manabii vilevile,
nawe unasema kuwa mtu akitii neno lako hatakufa
milele. **(aiōn g165)** **53** Je, wewe ni mkuu kuliko baba
yetu Ibrahimu ambaye alikufa, na manabii ambao pia
walikufa? Unafikiri wewe ni nani?” **54** Isa akawajibu,
“Nikijitukuza mwenyewe, utukufu wangu hauna
maana. Baba yangu, huyo ambaye ninyi mnadai
kuwa ni Mungu wenu, ndiye anitukuzaye mimi. **55**
Ingawa hamkumjua, mimi ninamjua. Kama ningesema
simjui, ningekuwa mwongo kama ninyi, lakini mimi
ninamjua na ninalitii neno lake. **56** Baba yenu Ibrahimu
alishangilia kwamba angeiona siku yangu, naye
akaiona na akafurahi.” **57** Wayahudi wakamwambia,
“Wewe hujatimiza hata miaka hamsini, nawe wasema
umemwona Ibrahimu?” **58** Isa akawaambia, “Amin,
amin nawaambia, kabla Ibrahimu hajakuwa, Mimi
niko.” **59** Ndipo wakaokota mawe ili kumpiga, lakini
Isa akajificha, naye akatoka Hekaluni.

**9** Isa alipokuwa akipita, akamwona mtu aliyekuwa
kipofu tangu kuzaliwa. **2** Wanafunzi wake
wakamuuliza, “Mwalimu, ni nani aliyetenda dhambi; ni
huyu mtu au wazazi wake hata azaliwe kipofu?” **3** Isa
akawajibu, “Huyu mtu wala wazazi wake hawakutenda
dhambi. Alizaliwa kipofu ili kazi za Mungu zidhihirishwe
katika maisha yake. **4** Yanipasa kuzifanya kazi zake
yeye aliyenituma wakati bado ni mchana, kwa kuwa
usiku waja ambapo hakuna mtu awezaye kufanya
kazi. **5** Wakati niko ulimwenguni, mimi ni nuru ya
ulimwengu.” **6** Baada ya kusema haya, akatema mate
ardhini, akatengeneza tope kwa mate na kumpaka
yule kipofu machoni. **7** Kisha akamwambia, “Nenda
ukanawe katika Bwawa la Siloamu” (Siloamu maana
yake ni Kutumwa). Ndipo yule kipofu akaenda,
akanawa, naye akarudi akiwa anaona. **8** Majirani

zake na wale wote waliokuwa wamemwona hapo
awali akiombaomba wakaanza kuuliza, “Je, huyu si
yule aliyekuwa akiketi akiombaomba?” 9 Wengine
wakasema, “Ndiye.” Wengine wakasema, “Siye,
bali anafanana naye.” Lakini yeye akawaambia,
“Mimi ndiye.” 10 Wakamuuliza, “Basi macho yako
yalifumbuliwaje?” 11 Yeye akawajibu, “Yule mtu
aitwaye Isa alitengeneza tope, akanipaka machoni
mwangu, naye akaniambia, ‘Nenda ukanawe katika
Bwawa la Siloamu,’ ndipo nikanawa nami nikapata
kuona!” 12 Wale wakamuuliza, “Yeye huyo mtu yuko
wapi?” Akawajibu, “Sijui.” 13 Wakamleta yule mtu
aliyekuwa kipofu hapo awali kwa Mafarisayo. 14 Basi
siku hiyo Isa alitengeneza tope na kuyafungua macho
ya huyo mtu ilikuwa Sabato. 15 Mafarisayo nao
wakaanza kumuuliza yule mtu alivyopata kuona. Naye
akawaambia, “Alinipaka tope kwenye macho yangu,
nikanawa na sasa ninaona.” 16 Baadhi ya Mafarisayo
wakasema, “Huyu mtu hatoki kwa Mungu, kwa
sababu hashiki Sabato.” Lakini wengine wakasema,
“Awezaje mtu mwenye dhambi kufanya miujiza
kama hii?” Wakagawanyika. 17 Hivyo wakamwambia
tena yule mtu aliyekuwa kipofu, “Wewe ndiwe
uliyefumbuliwa macho. Wasemaje kuhusu mtu huyo?”
Yeye akawajibu, “Yeye ni nabii.” 18 Wale Wayahudi
hawakuamini ya kuwa mtu huyo alikuwa kipofu
akapata kuona, hadi walipowaita wazazi wake. 19
Wakawauliza, “Je, huyu ni mtoto wenu, ambaye
mnasema alizaliwa kipofu? Imekuwaje basi sasa
anaona?” 20 Wazazi wake wakajibu, “Tunajua ya
kuwa huyu ni mtoto wetu na ya kuwa alizaliwa
kipofu. 21 Lakini hatujui jinsi anavyoweza kuona
sasa, wala hatujui ni nani aliyemfungua macho
yake. Muulizeni; yeye ni mtu mzima na anaweza
kujieleza mwenyewe.” 22 Wazazi wake walisema hivi
kwa sababu waliwaogopa viongozi wa Wayahudi,
kwani walikuwa wamekubaliana kuwa mtu yeyote
atakayemkiri Isa kuwa ndiye Al-Masihi atafukuzwa
kutoka sinagogi. 23 Kwa hiyo wazazi wake wakasema,
“Yeye ni mtu mzima. Muulizeni.” 24 Hivyo kwa
mara ya pili wakamwita yule aliyekuwa kipofu, nao
wakamwambia, “Mpe Mungu utukufu! Sisi tunafahamu
kuwa mtu huyu aliyekuponya ni mwenye dhambi.”
25 Akawajibu, “Mimi sijui kama yeye ni mwenye
dhambi. Lakini jambo moja ninalojua, nilikuwa kipofu
na sasa ninaona.” 26 Wakamuuliza, “Alikufanyia nini?
Aliyafumbuaje macho yako?” 27 Akawajibu, “Tayari
nimekwisha kuwaambia, nanyi hamtaki kunisikiliza.
Mbona mnataka kusikia tena? Je, ninyi nanyi mnataka
kuwa wanafunzi wake?” 28 Ndipo wakamtukana na
kusema, “Wewe ndiwe mwanafunzi wake! Sisi ni
wanafunzi wa Musa. 29 Tunajua kwamba Mungu
alisema na Musa, lakini mtu huyu hatujui anakotoka.”
30 Yule mtu akawajibu, “Hili ni jambo la ajabu! Hamjui
anakotoka, naye amenifungua macho yangu! 31
Tunajua ya kuwa Mungu hawasikilizi wenye dhambi,
lakini huwasikiliza wote wanaomcha na kumtii. 32
Tangu zamani hatujasikia kwamba mtu amemponya
yeyote aliyezaliwa kipofu. (aiōn g165) 33 Kama huyu mtu
hakutoka kwa Mungu, asingeweza kufanya lolote.” 34
Wakamjibu, “Wewe ulizaliwa katika dhambi kabisa,
nawe unajaribu kutufundisha?” Wakamfukuza atoke
nje. 35 Isa aliposikia kuwa wamemfukuza atoke nje
yule mtu aliyemfumbua macho, alimkuta, akamuuliza,
“Je, unamwamini Mwana wa Adamu?” 36 Yule mtu
akamjibu, “Yeye ni nani, Bwana? Niambie ili nipate
kumwamini.” 37 Isa akamjibu, “Umekwisha kumwona;
naye anayezungumza nawe, ndiye.” 38 Yule mtu
akasema, “Bwana, naamini.” Naye akamwabudu. 39
Isa akasema, “Nimekuja ulimwenguni humu kwa ajili
ya kuhukumu, ili wale walio vipofu wapate kuona,
nao wale wanaoona wawe vipofu.” 40 Baadhi ya
Mafarisayo waliokuwa karibu naye wakamsikia na
kumwambia, “Je, kweli sisi ni vipofu?” 41 Isa akawajibu,
“Kama mngekuwa vipofu kweli, msingekuwa na hatia
ya dhambi, lakini kwa kuwa mnasema, ‘Tunaona,’
basi mna hatia.

10 “Amin, amin nawaambia, yeye asiyeingia katika
zizi la kondoo kupitia kwenye lango, lakini
akwea kuingia ndani kwa njia nyingine, huyo ni
mwizi na mnyang’anyi. 2 Yeye anayeingia kupitia
kwenye lango ndiye mchungaji wa kondoo. 3 Mlinzi
humfungulia lango, na kondoo huisikia sauti yake.
Yeye huwaita kondoo wake kwa majina yao na
kuwatoa nje ya zizi. 4 Baada ya kuwatoa wote nje,
yeye hutangulia mbele yao na kondoo humfuata,
kwa kuwa wanaijua sauti yake. 5 Lakini kondoo
hawatamfuata mgeni, bali watamkimbia kwa sababu
hawaijui sauti ya mgeni.” 6 Isa alitumia mfano huu,
lakini wao hawakuelewa hayo aliyokuwa akiwaambia.
7 Kwa hiyo Isa akasema nao tena, akawaambia,
“Amin, amin nawaambia, mimi ndimi lango la kondoo.

8 Wote walionitangulia ni wezi na wanyang'anyi, nao
kondoo hawakuwasikia. 9 Mimi ndimi lango. Yeyote
anayeingia zizini kupitia kwangu ataokoka. Ataingia
na kutoka, naye atapata malisho. 10 Mwizi huja ili
aibe, aue na aangamize. Mimi nimekuja ili wapate
uzima, kisha wawe nao tele. 11 "Mimi ndimi mchungaji
mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa
ajili ya kondoo. 12 Mtu wa kuajiriwa sio mchungaji
mwenye kondoo. Anapomwona mbwa-mwitu akija,
yeye hukimbia na kuwaacha kondoo. Naye mbwa-
mwitu hulishambulia kundi na kulitawanya. 13 Yeye
hukimbia kwa sababu ameajiriwa wala hawajali
kondoo. 14 "Mimi ndimi mchungaji mwema. Ninawajua
kondoo wangu, nao kondoo wangu wananijua. 15
Kama vile Baba anavyonijua mimi, nami ninavyomjua
Baba, ndivyo nami ninautoa uhai wangu kwa ajili
ya kondoo. 16 Ninao kondoo wengine ambao si wa
zizi hili. Inanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti
yangu; hivyo patakuwa na kundi moja na mchungaji
mmoja. 17 Baba yangu ananipenda kwa kuwa
ninautoa uhai wangu ili niupate tena. 18 Hakuna
mtu aniondoleaye uhai wangu, bali ninautoa kwa
hiari yangu mwenyewe. Ninao uwezo wa kuutoa
uhai wangu, na pia ninao uwezo wa kuutwaa tena.
Amri hii nimepewa na Baba yangu." 19 Waliposikia
maneno haya, Wayahudi wakagawanyika. 20 Wengi
wao wakasema, "Huyu amepagawa na pepo mchafu,
naye amechanganyikiwa." 21 Wengine wakasema,
"Haya si maneno ya mtu aliyepagawa na pepo
mchafu. Je, pepo mchafu aweza kufungua macho ya
kipofu?" 22 Ikafika Sikukuu ya Kuwekwa wakfu kwa
Hekalu huko Yerusalemu. Ilikuwa majira ya baridi. 23
Naye Isa alikuwa akitembea ndani ya Hekalu katika
Ukumbi wa Sulemani. 24 Wayahudi wakamkusanyikia,
wakamuuliza, "Utatuweka katika hali ya mashaka hadi
lini? Kama wewe ndiwe Al-Masihi, tuambie waziwazi."
25 Isa akawajibu, "Nimewaambia, lakini hamwamini.
Mambo ninayoyatenda kwa jina la Baba yangu
yananishuhudia. 26 Lakini hamwamini, kwa sababu
ninyi si wa kundi la kondoo wangu. 27 Kondoo wangu
huisikia sauti yangu nami nawajua, nao hunifuata.
28 Nami ninawapa uzima wa milele; hawataangamia
kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya kutoka
mikono yangu. **(aiōn g165, aiōnios g166)** 29 Baba yangu
aliyenipa hawa ni mkuu kuliko wote, na hakuna
awezaye kuwapokonya kutoka mikononi mwake.
30 Mimi na Baba yangu tu umoja." 31 Kwa mara
nyingine Wayahudi wakainua mawe ili wampige nayo,
32 lakini Isa akawaambia, "Nimewaonesha miujiza
mingi mikubwa kutoka kwa Baba yangu. Ni kwa
ipi kati ya hiyo miujiza mnataka kunipiga mawe?"
33 Wayahudi wakamjibu, "Hatukupigi mawe kwa
sababu ya mambo mema uliyotenda, bali ni kwa kuwa
umekufuru. Ingawa wewe ni mwanadamu, unajifanya
kuwa Mungu." 34 Isa akawajibu, "Je, haikuandikwa
katika Torati yenu kwamba, 'Nimesema kuwa ninyi ni
"miungu"'? 35 Kama aliwaita 'miungu' wale ambao
neno la Mungu liliwafikia, nayo Maandiko hayawezi
kutanguka, 36 je, mwawezaje kusema kwamba
yule ambaye Baba amemweka wakfu na kumtuma
ulimwenguni anakufuru, kwa sababu nilisema, 'Mimi
ni Mwana wa Mungu'? 37 Ikiwa sifanyi kazi za Baba
yangu, basi msiniamini. 38 Lakini ikiwa nazifanya kazi
za Mungu, hata kama hamniamini mimi ziamininі hizo
kazi, ili mpate kujua na kuelewa kwamba Baba yu
ndani yangu, nami ni ndani yake." 39 Ndipo wakajaribu
kumkamata kwa mara nyingine, lakini akaponyoka
kutoka mikononi mwao. 40 Isa akaenda tena ng'ambo
ya Yordani hadi mahali Yahya alikuwa akibatiza hapo
awali, naye akakaa huko. 41 Watu wengi wakamjia,
nao wakawa wakisema, "Yahya hakufanya muujiza
wowote, lakini kila jambo alilosema kumhusu huyu
mtu ni kweli." 42 Nao watu wengi wakamwamini Isa
huko.

**11** Basi mtu mmoja, jina lake Lazaro, alikuwa
mgonjwa. Yeye alikuwa akiishi Bethania, kijiji
cha Mariamu na Martha dada yake. 2 (Huyu Mariamu,
ambaye Lazaro kaka yake alikuwa mgonjwa, ndiye
alimpaka Bwana Isa mafuta na kuifuta miguu yake
kwa nywele zake.) 3 Hivyo hawa dada wawili
walituma ujumbe kwa Isa kumwambia, "Bwana, yule
umpendaye ni mgonjwa." 4 Lakini Isa aliposikia hayo,
akasema, "Ugonjwa huu hautaleta mauti, bali ni wa
kudhihirisha utukufu wa Mungu, ili Mwana wa Mungu
apate kutukuzwa kutokana na ugonjwa huu." 5 Isa
aliwapenda Martha, Mariamu na Lazaro ndugu yao.
6 Hata hivyo, baada ya kusikia kwamba Lazaro ni
mgonjwa, alikawia huko alikokuwa kwa siku mbili
zaidi. 7 Ndipo akawaambia wanafunzi wake, "Haya,
turudi Yudea." 8 Wanafunzi wake wakamwambia,
"Mwalimu, Wayahudi walikuwa wanataka kukupiga
mawe, nawe unataka kurudi huko?" 9 Isa akawajibu,

“Si kuna saa kumi na mbili za mchana katika siku
moja? Wanaotembea mchana hawawezi kujikwaa,
kwa maana wanaona kwa nuru ya ulimwengu huu. 10
Lakini wale wanaotembea usiku hujikwaa kwa sababu
hawana nuru ndani yao.” 11 Baada ya kusema haya,
Isa akawaambia, “Rafiki yetu Lazaro amelala, lakini
naenda kumwamsha.” 12 Wanafunzi wakamwambia,
“Bwana, kama amelala usingizi ataamka.” 13 Hata
hivyo, Isa alikuwa anazungumzia kuwa Lazaro
amekufa, lakini wanafunzi wake hawakuelewa,
walidhani kwamba anasema Lazaro amelala usingizi
tu. 14 Kwa hiyo Isa akawaambia waziwazi, “Lazaro
amekufa. 15 Hata hivyo nafurahi kwa kuwa sikuwako
huko kabla ya Lazaro kufa, ili mpate kuamini. Lakini
sasa twendeni kwake.” 16 Tomaso (aliyeitwa Pacha)
akawaambia wanafunzi wenzake, “Sisi nasi twendeni
tukafe pamoja naye.” 17 Isa alipowasili huko alikuta
Lazaro amekuwa kaburini siku nne. 18 Basi Bethania
ulikuwa karibu na Yerusalemu, umbali wa yamkini
maili mbili, 19 na Wayahudi wengi walikuwa wamekuja
kuwafariji Martha na Mariamu kwa ajili ya kufiwa
na ndugu yao. 20 Martha aliposikia kwamba Isa
anakuja, alitoka kwenda kumlaki, ila Mariamu alibaki
nyumbani. 21 Martha akamwambia Isa, “Bwana,
kama ungekuwa hapa, ndugu yangu hangekufa. 22
Lakini sasa ninajua kuwa chochote utakachomwomba
Mungu, atakupa.” 23 Isa akamwambia, “Ndugu yako
atafufuka.” 24 Martha akamjibu, “Ninajua ya kuwa
atafufuka wakati wa ufufuo wa wafu siku ya mwisho.”
25 Isa akamwambia, “Mimi ndiye huo ufufuo na uzima.
Yeye aniaminiye mimi, hata akifa atakuwa anaishi;
26 na yeyote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa
hata milele. Je, unasadiki haya?” **(aiōn g165)** 27 Martha
akamwambia, “Ndiyo Bwana, ninaamini ya kuwa
wewe ndiwe Al-Masihi, Mwana wa Mungu, yeye ajaye
ulimwenguni.” 28 Baada ya kusema haya, Martha
alienda akamwita Mariamu dada yake faraghani na
kumwambia, “Mwalimu yuko hapa anakuita.” 29
Mariamu aliposikia hivyo, akaondoka upesi, akaenda
hadi alipokuwa Isa. 30 Isa alikuwa hajaingia kijijini,
bali alikuwa bado yuko mahali pale alipokutana na
Martha. 31 Wale Wayahudi waliokuwa pamoja na
Mariamu nyumbani wakimfariji walipoona ameondoka
haraka na kutoka nje, walimfuata wakidhani kwamba
alikuwa anaenda kule kaburini kulilia huko. 32
Mariamu alipofika mahali pale Isa alipokuwa, alipiga
magoti miguuni pake na kusema, “Bwana, kama
ungekuwa hapa, ndugu yangu hangekufa.” 33
Isa alipomwona Mariamu akilia na wale Wayahudi
waliokuja pamoja naye pia wakilia, Isa alisikia
uchungu moyoni, akafadhaika sana. 34 Akauliza,
“Mmemweka wapi?” Wakamwambia, “Bwana, njoo
upaone.” 35 Isa akalia machozi. 36 Ndipo Wayahudi
wakasema, “Tazama jinsi alivyompenda Lazaro!” 37
Lakini wengine wakasema, “Je, yule aliyefungua
macho ya kipofu, hakuweza kumfanya na huyu
asife?” 38 Isa akafika penye kaburi akiwa amefadhaika
sana kwa mara nyingine. Hilo kaburi lilikuwa pango
ambalo jiwe liliwekwa kwenye ingilio lake. 39 Isa
akasema, “Liondoeni jiwe.” Martha dada yake yule
aliyekuwa amekufa akasema, “Lakini Bwana, wakati
huu atakuwa ananuka kwani amekwisha kuwa kaburini
siku nne.” 40 Isa akamwambia, “Sikukuambia kwamba
ukiamini utauona utukufu wa Mungu?” 41 Kwa hiyo
wakaliondoa lile jiwe kutoka kaburini. Isa akainua
macho yake juu, akasema, “Baba, ninakushukuru kwa
kuwa wanisikia. 42 Ninajua ya kuwa wewe hunisikia
siku zote, lakini nimesema haya kwa ajili ya watu
hawa waliosimama hapa, ili wapate kuamini ya kuwa
wewe umenituma.” 43 Baada ya kusema haya, Isa
akapaza sauti yake, akaita, “Lazaro, njoo huku!” 44
Yule aliyekuwa amekufa akatoka nje, mikono yake na
miguu yake ikiwa imeviringishiwa vitambaa vya kitani
na leso usoni pake. Isa akawaambia, “Mfungueni;
mwacheni aende zake.” 45 Hivyo Wayahudi wengi
waliokuwa wamekuja kumfariji Mariamu walipoona
yale Isa aliyoyatenda, wakamwamini. 46 Lakini
baadhi yao wakaenda kwa Mafarisayo na kuwaambia
mambo Isa aliyoyafanya. 47 Kwa hiyo viongozi wa
makuhani na Mafarisayo wakaita mkutano wa Baraza
la Wayahudi. Wakaulizana, “Tufanyeje? Huyu mtu
anafanya ishara nyingi. 48 Tukimwacha aendelee
hivi, kila mtu atamwamini, nao Warumi watakuja na
kupaharibu mahali petu patakatifu na taifa letu.” 49
Mmoja wao aliyeitwa Kayafa, aliyekuwa kuhani mkuu
mwaka huo, akasema, “Ninyi hamjui kitu chochote!
50 Hamjui kwamba ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili
ya watu, kuliko taifa lote liangamie?” 51 Hakusema
haya kutokana na mawazo yake mwenyewe, bali
kama kuhani mkuu mwaka huo, alitabiri kuwa Isa
angekufa kwa ajili ya taifa la Wayahudi; 52 wala si
kwa ajili ya taifa hilo pekee, bali pia kwa ajili ya watoto

wa Mungu waliotawanyika, ili kuwaleta pamoja na
kuwafanya wawe wamoja. **53** Hivyo tangu siku hiyo
wakawa wanafanya mipango ili wamuue Isa. **54** Kwa
hiyo Isa akawa hatembei tena hadharani miongoni
mwa Wayahudi, bali alijitenga akaenda sehemu iliyo
karibu na jangwa kwenye kijiji kiitwacho Efraimu.
Akakaa huko na wanafunzi wake. **55** Basi Pasaka ya
Wayahudi ilipokuwa imekaribia, watu wengi walitoka
vijijini wakaenda Yerusalemu ili wakajitakase kabla
ya Pasaka. **56** Watu wakawa wanamtafuta Isa, nao
waliposimama kwenye ua la Hekalu, waliulizana,
“Je, mtu huyu hatakuja kamwe kwenye Sikukuu?”
**57** Viongozi wa makuhani na Mafarisayo walikuwa
wametoa amri kuwa yeyote atakayejua mahali Isa
aliko, lazima atoe taarifa ili wapate kumkamata.

**12** Siku sita kabla ya Pasaka, Isa alienda Bethania,
makao ya Lazaro, aliyekuwa amemfufua kutoka
kwa wafu. **2** Wakaandaa karamu kwa heshima ya
Isa. Martha akawahudumia, wakati Lazaro alikuwa
miongoni mwa waliokaa mezani pamoja na Isa. **3**
Kisha Mariamu akachukua chupa ya painti moja
yenye manukato ya nardo safi ya thamani kubwa,
akayamimina miguuni mwa Isa na kuifuta kwa
nywele zake. Nyumba nzima ikajaa harufu nzuri ya
manukato. **4** Ndipo Yuda Iskariote mwana wa Simoni,
mmoja wa wanafunzi wa Isa, ambaye baadaye
angemsaliti Isa, akasema, **5** “Kwa nini manukato
haya hayakuuzwa kwa dinari mia tatu, na fedha
hizo wakapewa maskini?” **6** Yuda hakusema hivi
kwa kuwa aliwajali maskini, bali kwa kuwa alikuwa
mwizi; ndiye alikuwa akitunza mfuko wa fedha, na
akawa akiiba zile fedha. **7** Isa akasema, “Mwacheni.
Aliyanunua manukato hayo ili ayaweke kwa ajili ya
siku ya maziko yangu. **8** Maskini mtakuwa nao siku
zote, lakini mimi hamtakuwa nami siku zote.” **9** Umati
mkubwa wa Wayahudi walipojua kwamba Isa alikuwa
huko Bethania, walikuja si tu kwa ajili ya Isa, lakini pia
kumwona Lazaro ambaye Isa alikuwa amemfufua. **10**
Kwa hiyo viongozi wa makuhani wakapanga njama
ya kumuua Lazaro pia, **11** kwa kuwa kutokana na
habari za kufufuliwa kwake, Wayahudi wengi walikuwa
wanamfuata Isa na kumwamini. **12** Siku iliyofuata
umati mkubwa wa watu waliokuwa wamekuja kwenye
Sikukuu walisikia kwamba Isa angekuja Yerusalemu.
**13** Basi wakachukua matawi ya mitende, wakatoka
kwenda kumlaki, huku wakipaza sauti wakisema,
“Hosana!” “Amebarikiwa yeye ajaye kwa Jina la
Mwenyezi Mungu!” “Amebarikiwa mfalme wa Israeli!”
**14** Isa akamkuta mwana-punda, akampanda, kama
ilivyoandikwa, **15** “Usiogope, ewe Binti Sayuni; tazama,
mfalme wako anakuja, amepanda mwana-punda!” **16**
Wanafunzi wake Isa mwanzoni hawakuelewa mambo
haya. Lakini Isa alipotukuzwa, ndipo walipokumbuka
kuwa mambo haya yalikuwa yameandikwa kwa ajili
yake na alitendewa yeye. **17** Wale waliokuwepo
Isa alipomwita Lazaro kutoka kaburini na kumfufua
kutoka kwa wafu waliendelea kushuhudia. **18** Na
kwa sababu walikuwa wamesikia kwamba alikuwa
ametenda muujiza huu, umati wa watu wakaenda
kumlaki. **19** Hivyo Mafarisayo walipoona hayo,
wakaambiana, “Mnaona, hamwezi kufanya lolote.
Angalieni, ulimwengu wote unamfuata yeye!” **20**
Basi palikuwa Wayunani fulani miongoni mwa wale
waliokuwa wameenda kuabudu wakati wa Sikukuu.
**21** Hawa wakaenda kwa Filipo, aliyekuwa raia
wa Bethsaida huko Galilaya, wakiwa na ombi.
Wakamwambia, “Tungependa kumwona Isa.” **22**
Filipo akaenda akamweleza Andrea, nao wote wawili
wakamwambia Isa. **23** Isa akawajibu, “Saa imewadia
ya Mwana wa Adamu kutukuzwa. **24** Amin, amin
nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na
kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa,
huzaa mbegu nyingi. **25** Mtu yeyote anayependa
maisha yake atayapoteza, naye ayachukiaye maisha
yake katika ulimwengu huu atayaokoa hata kwa uzima
wa milele. **(aiōnios g166)** **26** Mtu yeyote akinitumikia
lazima anifuate, nami mahali nilipo ndipo mtumishi
wangu atakapokuwa. Mtu akinitumikia, Baba yangu
atamheshimu. **27** “Sasa roho yangu imefadhaika
sana. Niseme nini? ‘Baba, niokoe katika saa hii’?
Lakini ni kwa kusudi hili nimeufikia wakati huu. **28**
Baba, litukuze jina lako.” Ndipo ikaja sauti kutoka
mbinguni, ikasema, “Nimelitukuza, nami nitalitukuza
tena.” **29** Umati ule wa watu waliokuwa mahali pale
waliisikia ile sauti, nao wakasema hiyo ilikuwa sauti
ya radi; wengine wakasema malaika ameongea naye.
**30** Isa akawaambia, “Sauti hii imesikika kwa faida
yenu, wala si kwa faida yangu. **31** Sasa ni saa ya
hukumu kwa ajili ya ulimwengu huu, sasa mkuu
wa ulimwengu huu atatupwa nje. **32** Lakini mimi,
nikiinuliwa kutoka nchi, nitawavuta watu wote waje
kwangu.” **33** Isa aliyasema haya akionesha ni kifo

gani atakachokufa. **34** Umati ule wa watu wakapaza
sauti, wakasema, “Tumesikia kutoka Torati kwamba
Al-Masihi adumu milele; hivyo wewe wawezaje
kusema, ‘Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa
juu’? Huyu ‘Mwana wa Adamu’ ni nani?” **(aiōn g165)**
**35** Ndipo Isa akawaambia, “Bado kitambo kidogo
nuru ingali pamoja nanyi. Nendeni maadamu mna
nuru, msije mkakumbwa na giza. Mtu anayetembea
gizani hajui anakoenda. **36** Wekeni tumaini lenu
katika nuru hiyo ili mpate kuwa wana wa nuru.”
Baada ya kusema haya, Isa aliondoka, akajificha
wasimwone. **37** Hata baada ya Isa kufanya miujiza
hii yote mbele yao, bado hawakumwamini. **38** Hili
lilikuwa ili kutimiza lile neno la nabii Isaya lililosema:
“Mwenyezi Mungu, ni nani aliyeamini ujumbe wetu,
na mkono wa Mwenyezi Mungu umefunuliwa kwa
nani?” **39** Kwa hivyo hawakuamini, kwa sababu
Isaya anasema mahali pengine: **40** “Amewafanya
vipofu, na kuifanya mioyo yao kuwa migumu, ili
wasiweze kuona kwa macho yao, wala kuelewa kwa
mioyo yao, wasije wakageuka nami nikawaponya.”
**41** Isaya alisema haya alipoona utukufu wa Isa na
kunena habari zake. **42** Lakini wengi miongoni mwa
viongozi wa Wayahudi walimwamini, lakini kwa sababu
ya Mafarisayo hawakukiri waziwazi kwa maana
waliogopa kufukuzwa katika masinagogi. **43** Wao
walipenda sifa za wanadamu kuliko sifa zinazotoka
kwa Mungu. **44** Isa akapaza sauti akasema, “Yeyote
aniaminiye, haniamini mimi peke yangu, bali pia yeye
aliyenituma. **45** Yeyote anionaye mimi amemwona
yeye aliyenituma. **46** Mimi nimekuja kama nuru
ulimwenguni, ili kila mtu aniaminiye asibaki gizani.
**47** “Mimi simhukumu mtu yeyote anayesikia maneno
yangu na asiyatii, kwa maana sikuja kuuhukumu
ulimwengu, bali kuuokoa. **48** Yuko anayehukumu yule
anayenikataa mimi na kuyakataa maneno yangu; yale
maneno niliyoyasema yenyewe yatamhukumu siku
ya mwisho. **49** Kwa maana sisemi kwa ajili yangu
mwenyewe, bali Baba aliyenituma aliniamuru ni nini
cha kusema na jinsi ya kukisema. **50** Nami ninajua
amri zake huongoza hadi kwenye uzima wa milele.
Hivyo lolote nisemalo, ndilo lile Baba aliloniambia
niseme.” **(aiōnios g166)**

**13** Sikukuu ya Pasaka ilikuwa imekaribia. Isa alijua
kuwa wakati wake wa kuondoka ulimwenguni ili
kurudi kwa Baba umewadia. Alikuwa amewapenda
watu wake waliokuwa ulimwenguni; naam, aliwapenda
hadi mwisho. **2** Isa alipokuwa akila chakula cha
jioni na wanafunzi wake, ibilisi alikuwa amekwisha
kutia wazo la kumsaliti Isa ndani ya moyo wa Yuda
Iskariote, mwana wa Simoni. **3** Isa, akijua kwamba
Baba ameweka vitu vyote chini ya mamlaka yake,
na kwamba yeye alitoka kwa Mungu na alikuwa
anarudi kwa Mungu, **4** aliondoka chakulani, akavua
vazi lake la nje, akajifunga kitambaa kiunoni. **5**
Kisha akamimina maji kwenye sinia na kuanza
kuwanawisha wanafunzi wake miguu na kuikausha
kwa kile kitambaa alichokuwa amejifunga kiunoni.
**6** Alipomfikia Simoni Petro, Petro akamwambia,
“Bwana, je, wewe utaninawisha mimi miguu?” **7** Isa
akamjibu, “Hivi sasa hutambui lile ninalofanya, lakini
baadaye utaelewa.” **8** Petro akamwambia, “La, wewe
hutaninawisha miguu kamwe.” Isa akamjibu, “Kama
nisipokunawisha, wewe huna sehemu nami.” **(aiōn
g165)** **9** Ndipo Simoni Petro akajibu, “Usininawishe
miguu peke yake, Bwana, bali pamoja na mikono
na kichwa pia!” **10** Isa akamjibu, “Mtu aliyekwisha
kuoga anahitaji kunawa miguu tu, kwani mwili wake
wote ni safi. Ninyi ni safi, ingawa si kila mmoja
wenu.” **11** Kwa kuwa yeye alijua ni nani ambaye
angemsaliti, ndiyo sababu akasema si kila mmoja
aliyekuwa safi. **12** Alipomaliza kuwanawisha miguu
yao, alivaa tena mavazi yake, akarudi alikokuwa
ameketi. Akawauliza, “Je, mmeelewa nililowafanyia?
**13** Ninyi mnaniita mimi ‘Mwalimu’ na ‘Bwana’; hii ni
sawa, maana ndivyo nilivyo. **14** Kwa hiyo, ikiwa mimi
niliye Bwana wenu na Mwalimu wenu nimewanawisha
ninyi miguu, pia hamna budi kunawishana miguu ninyi
kwa ninyi. **15** Mimi nimewawekea kielelezo kwamba
imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea ninyi.
**16** Amin, amin nawaambia, mtumishi si mkuu kuliko
bwana wake, wala aliyetumwa si mkuu kuliko yule
aliyemtuma. **17** Sasa kwa kuwa mmejua mambo
haya, heri kwenu mkiyatenda. **18** “Sisemi hivi kuhusu
ninyi nyote. Ninawajua wale niliowachagua. Lakini
ni kutimiza andiko lisemalo, ‘Yeye aliyekula chakula
changu ameinua kisigino chake dhidi yangu.’ **19**
“Ninawaambia mambo haya kabla hayajatukia, ili
yatakapotukia mpate kuamini ya kuwa Mimi ndiye.
**20** Amin, amin nawaambia, yeyote anayempokea
yule niliyemtuma anipokea mimi, naye anipokeaye
mimi ampokea yeye aliyenituma mimi.” **21** Baada

ya kusema haya, Isa alifadhaika sana moyoni,
akasema, “Amin, amin nawaambia, mmoja wenu
atanisaliti.” 22 Wanafunzi wake wakatazamana bila
kujua kuwa alikuwa anamsema nani. 23 Mmoja
wa wanafunzi wake, ambaye Isa alimpenda sana,
alikuwa ameegama kifuani mwa Isa. 24 Simoni Petro
akampungia mkono yule mwanafunzi, akamwambia,
“Muulize anamaanisha nani.” 25 Yule mwanafunzi
akamwegemea Isa, akamuuliza, “Bwana, tuambie,
ni nani?” 26 Isa akajibu, “Ni yule nitakayempa hiki
kipande cha mkate baada ya kukichovya kwenye
bakuli.” Hivyo baada ya kukichovya kile kipande cha
mkate, akampa Yuda Iskariote, mwana wa Simoni. 27
Mara tu baada ya kukipokea kile kipande cha mkate,
Shetani akamwingia. Isa akamwambia Yuda, “Lile
unalotaka kulitenda, litende haraka.” 28 Hakuna hata
mmoja wa wale waliokuwa wameketi naye mezani
aliyeelewa kwa nini Isa alimwambia hivyo. 29 Kwa
kuwa Yuda alikuwa mtunza fedha, wengine walifikiri
Isa alikuwa anamwambia akanunue vitu vilivyohitajika
kwa ajili ya Sikukuu, au kuwapa maskini kitu. 30
Mara tu baada ya kupokea ule mkate, Yuda akatoka
nje. Wakati huo ulikuwa ni usiku. 31 Baada ya Yuda
kutoka nje, Isa akasema, “Sasa Mwana wa Adamu
ametukuzwa, naye Mungu ametukuzwa ndani yake.
32 Ikiwa Mungu ametukuzwa ndani ya Mwana, Mungu
atamtukuza Mwana ndani yake mwenyewe, naye
atamtukuza mara moja. 33 “Watoto wangu, mimi bado
niko pamoja nanyi kwa kitambo kidogo. Mtanitafuta,
na kama vile nilivyowaambia Wayahudi, vivyo hivyo
sasa nawaambia na ninyi: Niendako, ninyi hamwezi
kuja. 34 “Amri mpya nawapa: Mpendane. Kama mimi
nilivyowapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi mpendane.
35 Mkipendana ninyi kwa ninyi kwa njia hii, watu
wote watajua kuwa ninyi ni wanafunzi wangu.” 36
Simoni Petro akamuuliza, “Bwana, unaenda wapi?”
Isa akamjibu, “Ninakoenda huwezi kunifuata sasa,
lakini utanifuata baadaye.” 37 Petro akamuuliza tena,
“Bwana, kwa nini siwezi kukufuata sasa? Mimi niko
tayari kuutoa uhai wangu kwa ajili yako.” 38 Isa
akamjibu, “Je, ni kweli uko tayari kuutoa uhai wako
kwa ajili yangu? Amin, amin nakuambia, kabla jogoo
hajawika, utanikana mara tatu.”

**14** Isa akawaambia, “Msifadhaike mioyoni mwenu.
Mnamwamini Mungu, mniamini pia. 2 Nyumbani
mwa Baba yangu kuna makao mengi. Kama sivyo,
ningewaambia. Naenda kuwaandalia makao. 3 Nami
nikienda na kuwaandalia makao, nitarudi tena na
kuwachukua mkae pamoja nami, ili mahali nilipo
nanyi mpate kuwepo. 4 Ninyi mnajua njia ya kufika
ninakoenda.” 5 Tomaso akamwambia, “Bwana, sisi
hatujui unakoenda, tutaijuaje njia?” 6 Isa akawaambia,
“Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi
kuja kwa Baba isipokuwa kupitia kwangu. 7 Kama
mngenijua mimi, mngemjua na Baba pia. Tangu
sasa mnamjua Baba yangu, tena mmemwona.” 8
Filipo akamwambia, “Bwana, tuoneshe Baba, na
hiyo itatutosha.” 9 Isa akamjibu, “Filipo, nimekaa
nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu yeyote
aliyeniona mimi amemwona Baba. Sasa wawezaje
kusema, ‘Tuoneshe Baba’? 10 Je, huamini ya kuwa
mimi niko ndani ya Baba, naye Baba yuko ndani
yangu? Maneno ninayowaambia siyasemi kwa ajili
yangu mwenyewe, bali Baba akaaye ndani yangu
ndiye atendaye hizi kazi. 11 Nisadiki mimi kwamba
niko ndani ya Baba, na Baba yuko ndani yangu; la
sivyo, niaminini kwa sababu ya zile kazi nizitendazo.
12 Amin, amin nawaambia, yeyote anayeniamini
mimi, kazi ninazozifanya naye atazifanya. Naam, na
atazifanya kazi kubwa kuliko hizi, kwa sababu mimi
ninaenda kwa Baba. 13 Nanyi mkiomba lolote kwa
Jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa
katika Mwana. 14 Mkiniomba lolote kwa Jina langu,
nitalifanya. 15 “Kama mnanipenda, mtazishika amri
zangu. 16 Nami nitamwomba Baba, naye atawapa
Msaidizi mwingine akae nanyi milele. **(aiōn g165)**
17 Huyo ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu
hauwezi kumpokea, kwa sababu haumwoni wala
haumjui. Ninyi mnamjua kwa kuwa yuko pamoja
nanyi, naye anakaa ndani yenu. 18 Sitawaacha ninyi
yatima; nitakuja kwenu. 19 Bado kitambo kidogo
na ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi mtaniona.
Kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai.
20 Wakati huo mtajua ya kuwa mimi niko ndani ya
Baba, na ninyi mko ndani yangu, na mimi niko ndani
yenu. 21 Yeyote mwenye amri zangu na kuzishika
ndiye anipendaye. Naye anipendaye atapendwa
na Baba yangu, nami nitampenda na kujidhihirisha
kwake.” 22 Ndipo Yuda (siyo Iskariote) akamwambia,
“Bwana, itakuwaje kwamba utajidhihirisha kwetu na
si kwa ulimwengu?” 23 Isa akamjibu, “Mtu yeyote
akinipenda atalishika neno langu na Baba yangu

atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao
yetu kwake. 24 Mtu yeyote asiyenipenda hayashiki
maneno yangu, na maneno niliyowapa si yangu
bali ni ya Baba aliyenituma. 25 “Nimewaambia
mambo haya yote wakati bado niko pamoja nanyi. 26
Lakini huyo Msaidizi, yaani huyo Roho Mtakatifu wa
Mungu, ambaye Baba atamtuma kwenu kwa Jina
langu, atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha
yote niliyowaambia. 27 Amani nawaachia; amani
yangu nawapa. Amani hii ninayowapa si kama ile
ulimwengu unatoa. Msifadhaike mioyoni mwenu,
wala msiogope. 28 “Mlisikia nikisema, ‘Ninaenda
zangu, lakini nitarudi tena.’ Kama kweli mngenipenda,
mngefurahi kwa kuwa naenda kwa Baba, kwani Baba
ni mkuu kuliko mimi. 29 Nimewaambia mambo haya
kabla hayajatukia, ili yatakapotukia mpate kuamini.
30 Sitasema nanyi zaidi, kwa sababu yule mkuu wa
ulimwengu huu anakuja, naye hana kitu kwangu,
31 lakini ulimwengu upate kujua kuwa ninampenda
Baba, nami hufanya vile Baba alivyoniamuru. “Haya
inukeni; twendeni zetu.

**15** “Mimi ndimi mzabibu wa kweli, na Baba yangu
ndiye mkulima. 2 Kila tawi ndani yangu lisilozaa
matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila tawi linalozaa,
hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi. 3 Ninyi
mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno
nililonena nanyi. 4 Kaeni ndani yangu, nami nikae
ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda
lisipokaa ndani ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi msipokaa
ndani yangu hamwezi kuzaa matunda. 5 “Mimi ni
mzabibu, ninyi ni matawi. Akaaye ndani yangu, nami
ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi
ninyi hamwezi kufanya jambo lolote. 6 Mtu yeyote
asipokaa ndani yangu, huyo hutupwa nje kama tawi
na kunyauka. Matawi kama hayo hukusanywa na
kutupwa motoni, yakateketea. 7 Mkikaa ndani yangu
na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote
mtakalo, nanyi mtatendewa. 8 Kwa hiyo Baba yangu
hutukuzwa kwa vile mnavyozaa matunda mengi,
nanyi mtajidhihirisha kuwa wanafunzi wangu. 9 “Kama
vile Baba alivyonipenda mimi, hivyo ndivyo mimi
nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni katika pendo langu.
10 Mkizishika amri zangu mtakaa katika pendo langu,
kama mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na
kukaa katika pendo lake. 11 Nimewaambia mambo
haya ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha
yenu iwe kamili. 12 Amri yangu ndiyo hii: Mpendane
kama mimi nilivyowapenda ninyi. 13 Hakuna mtu
mwenye upendo mkuu kuliko huu, mtu kuutoa uhai
wake kwa ajili ya rafiki zake. 14 Ninyi ni rafiki zangu
mkifanya ninayowaamuru. 15 Siwaiti ninyi watumishi
tena, kwa sababu watumishi hawajui bwana wao
analofanya. Bali nimewaita ninyi rafiki, kwa maana
nimewajulisha mambo yote niliyoyasikia kutoka kwa
Baba yangu. 16 Si ninyi mlionichagua, bali mimi
ndiye niliyewachagua ninyi na kuwaweka mwende
mkazae matunda, na matunda yenu yapate kudumu.
Ili nalo lolote mtakalomwomba Baba katika Jina langu,
awape ninyi. 17 Amri yangu ndiyo hii: Mpendane.
18 “Kama ulimwengu ukiwachukia ninyi, kumbukeni
kwamba ulinichukia mimi kabla yenu. 19 Kama
mngekuwa wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda
kama unavyowapenda walio wake. Kwa sababu
ninyi si wa ulimwengu, lakini mimi nimewachagua
kutoka ulimwengu, hii ndiyo sababu ulimwengu
unawachukia. 20 Kumbukeni lile neno nililowaambia,
‘Hakuna mtumishi aliye mkuu kuliko bwana wake.’
Kama wamenitesa mimi, nanyi pia watawatesa. Kama
walishika neno langu, watalishika na neno lenu
pia. 21 Watawatendea ninyi haya yote kwa ajili ya
Jina langu, kwa sababu hawamjui yeye aliyenituma.
22 Kama sikuja na kusema nao, hawangekuwa na
hatia ya dhambi. Lakini sasa hawana udhuru kwa
ajili ya dhambi zao. 23 Yeyote anayenichukia mimi,
anamchukia pia na Baba yangu. 24 Kama sikuwa
nimefanya miujiza ambayo haijapata kufanywa na
mtu mwingine yeyote, hawangekuwa na hatia ya
dhambi. Lakini sasa wameiona miujiza hii, na bado
wakatuchukia mimi na Baba yangu. 25 Lakini hii ni
kutimiza lile neno lililoandikwa kwenye Torati kwamba,
‘Walinichukia pasipo sababu.’ 26 “Lakini atakapokuja
huyo Msaidizi nitakayemtuma kwenu kutoka kwa
Baba, yaani huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba,
yeye atanishuhudia mimi. 27 Ninyi nanyi itawapasa
kushuhudia kwa sababu mmekuwa pamoja nami
tangu mwanzo.

**16** “Nimewaambia mambo haya yote ili msije
mkaiacha imani. 2 Watawatenga na masinagogi.
Naam, saa yaja ambayo mtu yeyote atakayewaua
atadhani kwa kufanya hivyo anamtumikia Mungu.
3 Nao watawatenda haya kwa sababu hawamjui
Baba wala mimi. 4 Lakini nimewaambia ninyi mambo

haya, ili saa hiyo ikiwadia mpate kukumbuka ya kuwa
nilikuwa nimewaambia. Sikuwaambia mambo haya
tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa pamoja nanyi.
**5** “Sasa mimi ninaenda kwake yeye aliyenituma,
lakini hakuna hata aniulizaye, ‘Unaenda wapi?’ **6**
Kwa sababu nimewaambia mambo haya, mioyo
yenu imejawa na huzuni. **7** Lakini nawaambia kweli,
yafaa mimi niondoke, kwa kuwa nisipoondoka, huyo
Msaidizi hatakuja kwenu; lakini nikienda nitamtuma
kwenu. **8** Naye atakapokuja, atauthibitishia ulimwengu
kuhusu dhambi, haki na hukumu. **9** Kwa habari ya
dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; **10** kwa
habari ya haki, kwa sababu ninaenda kwa Baba,
nanyi hamtaniona tena; **11** kwa habari ya hukumu,
kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha
kuhukumiwa. **12** “Bado ninayo mambo mengi ya
kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili sasa. **13**
Atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza
awatie katika kweli yote. Yeye hatanena kwa ajili yake
mwenyewe, bali atanena yale yote atakayosikia, naye
atawaonesha mambo yajayo. **14** Atanitukuza mimi,
kwa maana atayachukua yaliyo yangu na kuwajulisha
ninyi. **15** Vyote alivyo navyo Baba ni vyangu. Ndiyo
maana nimesema Roho atachukua yaliyo yangu
na kuwajulisha ninyi.” **16** Isa akaendelea kusema,
“Bado kitambo kidogo nanyi hamtaniona, na tena
bado kitambo kidogo nanyi mtaniona.” **17** Baadhi ya
wanafunzi wakaulizana, “Ana maana gani asemapo,
‘Bado kitambo kidogo nanyi hamtaniona, na tena bado
kitambo kidogo nanyi mtaniona’? Naye ana maana
gani asemapo, ‘Kwa sababu ninaenda kwa Baba’?” **18**
Wakaendelea kuulizana, “Ana maana gani asemapo,
‘Kitambo kidogo’? Hatuelewi hilo analosema.” **19** Isa
akatambua kuwa walitaka kumuuliza kuhusu hilo,
hivyo akawaambia, “Je, mnaulizana nina maana gani
niliposema, ‘Bado kitambo kidogo nanyi hamtaniona,
na tena bado kitambo kidogo nanyi mtaniona’? **20**
Amin, amin nawaambia, ninyi mtalia na kuomboleza,
lakini ulimwengu utafurahi. Ninyi mtahuzunika, lakini
huzuni yenu itageuka kuwa furaha. **21** Mwanamke
anapokuwa na uchungu wa kuzaa huwa na maumivu
kwa sababu saa yake imewadia. Lakini baada ya
mtoto kuzaliwa, yule mwanamke husahau maumivu
hayo kwa sababu ya furaha yake ya kuzaliwa mtoto
ulimwenguni. **22** Hivyo ninyi mna maumivu sasa, lakini
nitawaona tena, nayo mioyo yenu itafurahi, na furaha
yenu hakuna awaondoleaye. **23** Katika siku hiyo
hamtaniuliza neno lolote. Amin, amin nawaambia,
mkimwomba Baba jambo lolote kwa jina langu, yeye
atawapa. **24** Hadi sasa hamjaomba jambo lolote kwa
Jina langu. Ombeni nanyi mtapewa, ili furaha yenu
ipate kuwa kamili. **25** “Nimewaambia mambo haya
kwa mafumbo. Saa yaja ambapo sitazungumza nanyi
tena kwa mafumbo bali nitawaeleza waziwazi kuhusu
Baba. **26** Siku hiyo mtaomba kwa Jina langu. Wala
sitawaambia kwamba nitamwomba Baba kwa ajili
yenu, **27** kwa maana Baba mwenyewe anawapenda,
kwa sababu mmenipenda mimi na mmeamini kwamba
nimetoka kwa Mungu. **28** Nilitoka kwa Baba na kuja
ulimwenguni; sasa naondoka ulimwenguni na kurudi
kwa Baba.” **29** Ndipo wanafunzi wake wakasema,
“Sasa unazungumza waziwazi, wala si kwa mafumbo.
**30** Sasa tumejua kwamba wewe unajua mambo yote,
wala hakuna haja ya mtu kukuuliza maswali. Kwa
jambo hili tunaamini kwamba ulitoka kwa Mungu.” **31**
Isa akawajibu, “Je, sasa mnaamini? **32** Saa inakuja,
naam, imekwisha kuwadia, mtakapotawanyika kila
mmoja kwenda nyumbani mwake na kuniacha peke
yangu. Lakini mimi siko peke yangu kwa sababu
Baba yu pamoja nami. **33** “Nimewaambia mambo
haya ili mpate kuwa na amani mkiwa ndani yangu.
Ulimwenguni mtapata dhiki. Lakini jipeni moyo, kwa
maana mimi nimeushinda ulimwengu.”

**17** Baada ya Isa kusema haya, alitazama kuelekea
mbinguni akawaombea na kusema: “Baba,
saa imewadia. Mtukuze Mwanao, ili Mwanao apate
kukutukuza wewe. **2** Kwa kuwa umempa mamlaka juu
ya wote wenye mwili ili awape uzima wa milele wale
uliompa. **(aiōnios g166)** **3** Nao uzima wa milele ndio huu:
wakujue wewe uliye Mungu wa pekee wa kweli, na Isa
Al-Masihi uliyemtuma. **(aiōnios g166)** **4** Nimekutukuza
wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye.
**5** Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele zako kwa
ule utukufu niliokuwa nao pamoja na wewe kabla
ulimwengu haujaumbwa. **6** “Nimelidhihirisha jina
lako kwa wale ulionipa kutoka ulimwengu. Walikuwa
wako, nawe ukanipa mimi, nao wamelitii neno
lako. **7** Sasa wamejua ya kuwa vyote ulivyonipa
vimetoka kwako, **8** kwa kuwa maneno yale uliyonipa
nimewapa wao, nao wameyapokea na kujua kwamba
kweli nimetoka kwako, nao wameamini kuwa wewe
ulinituma. **9** Ninawaombea wao. Siuombei ulimwengu,

bali nawaombea wale ulionipa kwa sababu wao
ni wako. **10** Wote walio wangu ni wako, na walio
wako ni wangu, nami nimetukuzwa ndani yao. **11**
Mimi sasa simo tena ulimwenguni, lakini wao bado
wamo ulimwenguni, nami naja kwako. Baba Mtakatifu,
uwalinde kwa uweza wa jina lako ulilonipa, ili wawe
na umoja kama sisi tulivyo wamoja. **12** Nilipokuwa
pamoja nao, niliwalinda, wakawa salama kwa lile jina
ulilonipa. Hakuna hata mmoja aliyepotea, isipokuwa
yule aliyekusudiwa upotevu, ili Maandiko yapate
kutimia. **13** "Lakini sasa naja kwako, nami ninasema
mambo haya wakati bado nikiwa ulimwenguni, ili wawe
na furaha yangu kamili ndani yao. **14** Nimewapa neno
lako, nao ulimwengu umewachukia, kwa kuwa wao
si wa ulimwengu kama mimi nisivyo wa ulimwengu
huu. **15** Siombi kwamba uwaondoe ulimwenguni,
bali uwalinde dhidi ya yule mwovu. **16** Wao si wa
ulimwengu huu, kama vile mimi nisivyo wa ulimwengu.
**17** Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndilo kweli.
**18** Kama vile ulivyonituma mimi ulimwenguni, nami
nawatuma vivyo hivyo. **19** Kwa ajili yao najiweka
wakfu ili wao nao wapate kutakaswa katika ile kweli.
**20** "Siwaombei hawa peke yao, bali nawaombea na
wale wote watakaoniamini kupitia neno lao, **21** ili
wawe na umoja kama vile wewe Baba ulivyo ndani
yangu na mimi nilivyo ndani yako. Wao nao wawe
ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini ya kuwa
wewe ndiwe uliyenituma mimi. **22** Utukufu ule ulionipa
nimewapa wao, ili wawe na umoja kama sisi tulivyo
wamoja. **23** Mimi ndani yao na wewe ndani yangu:
ili wawe wamekamilika katika umoja, na ulimwengu
upate kujua ya kuwa umenituma, nami nimewapenda
wao kama unavyonipenda mimi. **24** "Baba, shauku
yangu ni kwamba wale ulionipa wawe pamoja nami
pale nilipo, ili waweze kuuona utukufu wangu, yaani
utukufu ule ulionipa kwa kuwa ulinipenda hata kabla
ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. **25** "Baba Mwenye
Haki, ingawa ulimwengu haukujui, mimi ninakujua,
nao wanajua ya kuwa umenituma. **26** Nimefanya
jina lako lijulikane kwao, nami nitaendelea kufanya
lijulikane, ili upendo ule unaonipenda mimi uwe ndani
yao, na mimi mwenyewe nipate kuwa ndani yao."

**18** Isa alipomaliza kuomba, akaondoka na
wanafunzi wake, wakavuka Bonde la Kidroni.
Upande wa pili palikuwa na bustani; yeye na
wanafunzi wake wakaingia humo. **2** Basi Yuda,
aliyemsaliti, alipafahamu mahali hapo, kwani Isa
alikuwa akikutana humo na wanafunzi wake mara
kwa mara. **3** Hivyo Yuda akaja kwenye bustani
akiongoza kikosi cha askari Warumi, na baadhi
ya maafisa kutoka kwa viongozi wa makuhani na
Mafarisayo. Nao walikuwa wamechukua taa, mienge
na silaha. **4** Isa, akijua yale yote yatakayompata,
akajitokeza mbele yao, akawauliza, "Mnamtafuta
nani?" **5** Wao wakamjibu, "Isa Al-Nasiri." Isa akawajibu,
"Mimi ndiye." (Yuda, aliyemsaliti, alikuwa amesimama
pamoja nao.) **6** Isa alipowaambia, "Mimi ndiye,"
walirudi nyuma na kuanguka chini! **7** Akawauliza tena,
"Mnamtafuta nani?" Nao wakamjibu, "Isa Al-Nasiri." **8**
Isa akawaambia, "Nimekwisha kuwaambia kuwa mimi
ndiye; kwa hiyo kama mnanitafuta mimi, waacheni
hawa watu waende zao." **9** Hii ilikuwa ili litimie lile
neno alilosema, "Sikumpoteza hata mmoja miongoni
mwa wale ulionipa." **10** Simoni Petro, aliyekuwa na
upanga, akaufuta na kumkata sikio la kuume mtumishi
wa kuhani mkuu. (Mtumishi huyo aliitwa Malko.) **11** Isa
akamwambia Petro, "Rudisha upanga wako kwenye
ala yake. Je, hainipasi kukinywea kikombe alichonipa
Baba?" **12** Hivyo wale askari, wakiwa na jemadari
wao na maafisa wa Wayahudi, wakamkamata Isa
na kumfunga. **13** Kwanza wakampeleka kwa Anasi,
mkwewe Kayafa, aliyekuwa kuhani mkuu mwaka ule.
**14** Kayafa ndiye alikuwa amewashauri viongozi wa
Wayahudi kwamba imempasa mtu mmoja kufa kwa
ajili ya watu. **15** Simoni Petro pamoja na mwanafunzi
mwingine walikuwa wakimfuata Isa. Huyu mwanafunzi
mwingine alikuwa anafahamika kwa kuhani mkuu,
hivyo aliingia uani kwa kuhani mkuu pamoja na
Isa. **16** Lakini Petro alisimama nje karibu na lango.
Ndipo yule mwanafunzi mwingine, aliyejulikana na
kuhani mkuu, akazungumza na msichana aliyekuwa
analinda lango, akamruhusu Petro aingie ndani. **17**
Yule msichana akamuuliza Petro, "Je, wewe pia si
mmoja wa wanafunzi wa mtu huyu?" Petro akajibu,
"Sio mimi." **18** Wale watumishi na askari walikuwa
wamesimama wakiota moto wa makaa kwa sababu
palikuwa na baridi, Petro naye alikuwa amesimama
pamoja nao akiota moto. **19** Wakati huo kuhani
mkuu akawa anamuuliza Isa kuhusu wanafunzi wake
na mafundisho yake. **20** Isa akamjibu, "Nimekuwa
nikizungumza waziwazi mbele ya watu wote. Siku
zote nimefundisha katika masinagogi na Hekaluni,

mahali Wayahudi wote hukusanyika. Sikusema jambo
lolote kwa siri. **21** Mbona unaniuliza mimi maswali?
Waulize wale waliosikia yale niliyowaambia. Wanajua
niliyoyasema.” **22** Alipomaliza kusema hayo, mmoja wa
askari aliyekuwa amesimama karibu naye akampiga
Isa kofi usoni. Kisha akasema, “Je, hivyo ndivyo
unavyomjibu kuhani mkuu?” **23** Isa akamjibu akasema,
“Kama nimesema jambo baya, shuhudia huo ubaya
niliousema. Lakini kama nimesema yaliyo kweli,
mbona umenipiga?” **24** Ndipo Anasi akampeleka Isa
kwa kuhani mkuu Kayafa, akiwa bado amefungwa. **25**
Wakati huo Simoni Petro alikuwa amesimama akiota
moto. Baadhi ya watu waliokuwepo wakamuuliza, “Je,
wewe si mmoja wa wanafunzi wake?” Petro akakana,
akasema, “Sio mimi.” **26** Mmoja wa watumishi wa
kuhani mkuu, ndugu yake yule mtu ambaye Petro
alikuwa amemkata sikio, akamuuliza, “Je, mimi
sikukuona kule bustanini ukiwa na Isa?” **27** Kwa mara
nyingine tena Petro akakana, naye jogoo akawika
wakati huo huo. **28** Ndipo viongozi wa Wayahudi
wakamchukua Isa kutoka kwa Kayafa na kumpeleka
kwenye jumba la kifalme la mtawala Mrumi. Wakati
huo ilikuwa ni alfajiri. Ili kuepuka kuwa najisi kwa
taratibu za ibada, Wayahudi hawakuingia ndani ya
jumba kwa sababu walitaka kushiriki katika Pasaka.
**29** Hivyo Pilato akatoka nje walikokuwa, akawauliza,
“Mmeleta mashtaka gani kumhusu mtu huyu?” **30**
Wao wakamjibu, “Kama huyu mtu hakuwa mhalifu,
tusingemleta kwako.” **31** Pilato akawaambia, “Basi
mchukueni ninyi mkamhukumu kwa kufuata sheria
zenu.” Wayahudi wakamjibu, “Sisi haturuhusiwi kutoa
hukumu ya kifo kwa mtu yeyote.” **32** Walisema
hivyo ili yale maneno aliyosema Isa kuhusu kifo
atakachokufa yapate kutimia. **33** Kwa hiyo Pilato
akaingia ndani ya jumba la kifalme, akamwita Isa,
akamuuliza, “Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?”
**34** Isa akamjibu, “Je, unauliza swali hili kutokana na
mawazo yako mwenyewe, au uliambiwa na watu
kunihusu?” **35** Pilato akamjibu, “Je, mimi ni Myahudi?
Taifa lako mwenyewe na viongozi wa makuhani
wamekukabidhi kwangu. Umefanya kosa gani?” **36** Isa
akajibu, “Ufalme wangu si wa ulimwengu huu. Ufalme
wangu ungekuwa wa ulimwengu huu, wafuasi wangu
wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa viongozi
wa Wayahudi. Lakini kama ilivyo, ufalme wangu
hautoki hapa ulimwenguni.” **37** Pilato akamuuliza,
“Kwa hiyo wewe ni mfalme?” Isa akajibu, “Wewe
wasema kwamba mimi ni mfalme. Kwa kusudi hili
nilizaliwa, na kwa ajili ya hili nilikuja ulimwenguni:
ili niishuhudie kweli. Mtu yeyote aliye wa kweli
husikia sauti yangu.” **38** Pilato akamuuliza Isa, “Kweli
ni nini?” Baada ya kusema haya Pilato akaenda
nje tena, akawaambia wale viongozi wa Wayahudi
waliomshtaki Isa, “Sioni msingi wowote wa kumshtaki
mtu huyu. **39** Lakini ninyi mna desturi yenu kwamba
wakati wa Pasaka nimwachie huru mfungwa mmoja
mnayemtaka. Je, mnataka niwafungulie huyu ‘mfalme
wa Wayahudi’?” **40** Wao wakapiga kelele, wakajibu,
“Si huyu mtu, bali tufungulie Baraba!” Yule Baraba
alikuwa mnyang’anyi.

**19** Ndipo Pilato akamtoa Isa akaamuru apigwe
mijeledi. **2** Askari wakasokota taji la miiba,
wakamvika Isa kichwani. Wakamvalisha joho la
zambarau. **3** Wakawa wanapanda pale alipo tena na
tena, wakisema, “Salamu, mfalme wa Wayahudi!”
Huku wakimpiga makofi usoni. **4** Pilato akatoka tena
nje, akawaambia wale waliokusanyika, “Tazameni,
namkabidhi Isa kwenu kuwajulisha kwamba mimi
sioni msingi wowote wa kumshtaki.” **5** Kwa hiyo
Isa akatoka nje akiwa amevaa lile taji la miiba
na lile vazi la zambarau. Pilato akawaambia,
“Tazameni, mtu ndiye huyu!” **6** Wale viongozi
wa makuhani na maafisa walipomwona, wakapiga
kelele wakisema, “Msulubishe! Msulubishe!” Pilato
akawaambia, “Mchukueni ninyi mkamsulubishe. Lakini
mimi sioni msingi wowote wa kumshtaki.” **7** Viongozi
wa Wayahudi wakamjibu, “Sisi tunayo sheria, na
kutokana na sheria hiyo, hana budi kufa kwa sababu
yeye alijiita Mwana wa Mungu.” **8** Pilato aliposikia
haya, akaogopa zaidi. **9** Akaingia tena ndani ya
jumba la kifalme, akamuuliza Isa, “Wewe umetoka
wapi?” Lakini Isa hakumjibu. **10** Pilato akamwambia,
“Wewe unakataa kuongea na mimi? Hujui ya kuwa
nina mamlaka ya kukuachia huru au kukusulubisha?”
**11** Ndipo Isa akamwambia, “Wewe hungekuwa na
mamlaka yoyote juu yangu kama hungepewa kutoka
juu. Kwa hiyo yeye aliyenitia mikononi mwako ana
hatia ya dhambi iliyo kubwa zaidi.” **12** Tangu wakati
huo, Pilato akajitahidi kutafuta njia ya kumfungua Isa,
lakini viongozi wa Wayahudi wakazidi kupiga kelele
wakisema, “Ukimwachia huyu mtu, wewe si rafiki wa
Kaisari. Mtu yeyote anayedai kuwa mfalme anampinga

Kaisari.” **13** Pilato aliposikia maneno haya, akamtoa
Isa nje tena. Akaketi kwenye kiti chake cha hukumu,
mahali palipoitwa Sakafu ya Jiwe (kwa Kiebrania
ni Gabatha). **14** Basi ilikuwa siku ya Maandalio ya
Pasaka, yapata kama saa sita hivi. Pilato akawaambia
Wayahudi, “Huyu hapa mfalme wenu!” **15** Wao
wakapiga kelele, “Mwondoe! Mwondoe! Msulubishe!”
Pilato akawauliza, “Je, nimsulubishe mfalme wenu?”
Wale viongozi wa makuhani wakamjibu, “Sisi hatuna
mfalme mwingine ila Kaisari.” **16** Ndipo Pilato
akamkabidhi Isa kwao ili wamsulubishe. Kwa hiyo
askari wakamchukua Isa. **17** Isa, akiwa ameubeba
msalaba wake, akatoka kuelekea mahali palipoitwa
Fuvu la Kichwa (kwa Kiebrania ni Golgotha). **18** Hapo
ndipo walipomsulubisha. Pamoja naye walisulubisha
watu wawili, mmoja kila upande wake, naye Isa
katikati. **19** Pilato akaamuru tangazo liandikwe na
liwekwe juu kwenye msalaba wa Isa; likasema: Isa
Al-Nasiri Mfalme wa Wayahudi. **20** Kwa kuwa mahali
hapo Isa aliposulubiwa palikuwa karibu na mjini,
Wayahudi wengi walisoma maandishi haya yaliyokuwa
yameandikwa kwa lugha za Kiebrania, Kiyunani na
Kilatini. **21** Viongozi wa makuhani wa Wayahudi
wakapinga, wakamwambia Pilato, “Usiandike ‘Mfalme
wa Wayahudi,’ bali andika kwamba mtu huyu alisema
yeye ni mfalme wa Wayahudi.” **22** Pilato akawajibu,
“Nilichokwisha kuandika, nimeandika!” **23** Askari
walipokwisha kumsulubisha Isa, walichukua nguo
zake wakazigawa mafungu manne, kila askari fungu
lake. Ila walikubaliana wasilichane lile vazi lake
kwa maana lilikuwa halina mshono, bali limefumwa
tangu juu hadi chini. **24** Wakaambiana, “Tusilichane
ila tulipigie kura ili kuamua ni nani atalichukua.”
Hili lilitukia ili Maandiko yapate kutimizwa yale
yaliyosema, “Wanagawana nguo zangu, na vazi
langu wanalipigia kura.” Hayo ndiyo waliyoyafanya
wale askari. **25** Karibu na msalaba wa Isa walikuwa
wamesimama mama yake, na dada wa mamaye, na
Mariamu mke wa Klopa, na Mariamu Magdalene.
**26** Isa alipomwona mama yake mahali pale, na
yule mwanafunzi aliyempenda akiwa amesimama
karibu, Isa akamwambia mama yake, “Mama, huyu
hapa ndiye mwanao.” **27** Kisha akamwambia yule
mwanafunzi, “Nawe huyu hapa ndiye mama yako.”
Tangu wakati huo yule mwanafunzi akamchukua
mama yake Isa nyumbani mwake. **28** Baada ya
haya, akijua kuwa mambo yote yamemalizika, na
ili kutimiza Maandiko, Isa akasema, “Naona kiu.”
**29** Hapo palikuwa na bakuli lililojaa siki. Kwa hiyo
wakachovya sifongo kwenye hiyo siki, wakaiweka
kwenye ufito wa mti wa hisopo, wakampelekea
mdomoni. **30** Baada ya kuionja hiyo siki, Isa akasema,
“Imekwisha.” Akainamisha kichwa chake, akaitoa
roho yake. **31** Ilikuwa siku ya Maandalio ya Pasaka,
na siku iliyofuata ingekuwa Sabato maalum. Kwa
kuwa viongozi wa Wayahudi hawakutaka miili ibaki
msalabani siku ya Sabato, wakamwomba Pilato
aamuru miguu ya wale waliosulubiwa ivunjwe, na
miili iondolewe kwenye misalaba. **32** Kwa hiyo askari
wakaenda wakavunja miguu ya mtu wa kwanza
aliyesulubiwa pamoja na Isa, na ya yule mwingine
pia. **33** Lakini walipomkaribia Isa, wakaona ya kuwa
amekwisha kufa, hivyo hawakuvunja miguu yake.
**34** Badala yake mmoja wa wale askari akamchoma
mkuki ubavuni, na mara pakatoka damu na maji. **35**
Mtu aliyeona mambo hayo ndiye alitoa ushuhuda,
nao ushuhuda wake ni kweli. Anajua kuwa anasema
kweli, naye anashuhudia ili pia nanyi mpate kuamini.
**36** Kwa maana mambo haya yalitukia ili andiko
litimie, lisemalo, “Hakuna hata mfupa wake mmoja
utakaovunjwa.” **37** Tena andiko lingine lasema,
“Watamtazama yeye waliyemchoma.” **38** Baada ya
mambo haya, Yusufu wa Arimathaya, aliyekuwa
mfuasi wa Isa, ingawa kwa siri kwa sababu ya
kuwaogopa viongozi wa Wayahudi, alimwomba Pilato
ruhusa ili kuuchukua mwili wa Isa. Pilato alimruhusu,
hivyo akaja, akauchukua. **39** Naye Nikodemo, yule
ambaye kwanza alimwendea Isa usiku, akaja, akaleta
mchanganyiko wa manemane na manukato, yenye
uzito wa zaidi ya kilo thelathini. **40** Wakauchukua
mwili wa Isa, wakaufunga katika sanda ya kitani safi
pamoja na yale manukato, kama ilivyokuwa desturi
ya Wayahudi. **41** Basi palikuwa na bustani karibu
na mahali pale aliposulubiwa, na pale ndani ya ile
bustani palikuwa na kaburi jipya, ambalo halikuwa
limezikiwa mtu bado. **42** Kwa hiyo, kwa kuwa ilikuwa
siku ya Wayahudi ya Maandalio, nalo kaburi hilo
lilikuwa karibu, wakamzika Isa humo.

**20** Alfajiri na mapema siku ya kwanza ya juma,
kulipokuwa bado giza, Mariamu Magdalene
alienda kaburini na kukuta lile jiwe limeondolewa
penye ingilio. **2** Hivyo akakimbia kwa Simoni Petro

pamoja na yule mwanafunzi mwingine ambaye Isa
alimpenda, na kusema, “Wamemwondoa Bwana
kaburini, na hatujui walikomweka!” 3 Petro na
yule mwanafunzi mwingine wakaondoka mara
moja kuelekea kaburini. 4 Wote wawili walikuwa
wanakimbia, lakini yule mwanafunzi mwingine
akakimbia mbio kuliko Petro, akatangulia kufika
kaburini. 5 Akainama na kuchungulia mle kaburini,
akaona vile vitambaa vya kitani, lakini hakuingia. 6
Ndipo Simoni Petro akaja akimfuata nyuma, akaingia
ndani ya kaburi. Naye akaona vile vitambaa vya
ile sanda vikiwa pale chini, 7 na kile kitambaa
kilichokuwa kichwani mwa Isa. Kitambaa hicho
kilikuwa kimekunjwa peke yake, mbali na vile vitambaa
vya kitani vya ile sanda. 8 Kisha yule mwanafunzi
aliyetangulia kufika kaburini akaingia ndani, akaona,
na akaamini. 9 (Kwa kuwa hadi wakati huo walikuwa
bado hawajaelewa kutoka Maandiko kwamba ilikuwa
lazima Isa afufuke kutoka kwa wafu.) 10 Kisha
hao wanafunzi wakaondoka, wakarudi nyumbani
mwao. 11 Lakini Mariamu Magdalene akasimama
nje ya kaburi akilia. Alipokuwa akilia, akainama
kuchungulia mle kaburini, 12 naye akaona malaika
wawili wamevaa mavazi meupe, wameketi pale
mwili wa Isa ulipokuwa umelazwa, mmoja upande
wa kichwani na mwingine upande wa miguuni. 13
Wakamuuliza Mariamu, “Mwanamke, mbona unalia?”
Akawaambia, “Nalia kwa kuwa wamemchukua Bwana
wangu, na sijui walikomweka.” 14 Baada ya kusema
hayo, akageuka, akamwona Isa amesimama, lakini
hakumtambua. 15 Isa akamwambia, “Mwanamke,
mbona unalia? Unamtafuta nani?” Mariamu, akidhani
alikuwa anaongea na mtunza bustani, akamwambia,
“Bwana, kama ni wewe umemchukua, tafadhali
nioneshe ulikomweka, nami nitamchukua.” 16 Isa
akamwita, “Mariamu!” Ndipo Mariamu akamgeukia
Isa na kusema naye kwa Kiebrania, “Raboni!” (maana
yake “Mwalimu”). 17 Isa akamwambia, “Usinishike,
kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini nenda
kwa ndugu zangu ukawaambie, ‘Ninapaa kwenda kwa
Baba yangu ambaye ni Baba yenu, kwa Mungu wangu
ambaye ni Mungu wenu.’” 18 Kwa hiyo Mariamu
Magdalene akaenda kuwatangazia wanafunzi wa Isa,
akisema, “Nimemwona Bwana!” Naye akawaambia
kwamba Isa alikuwa amemweleza mambo hayo yote.
19 Ilipokuwa jioni ya siku hiyo hiyo ya kwanza ya juma,
wanafunzi wake walikuwa pamoja, milango ikiwa
imefungwa kwa kuwaogopa viongozi wa Wayahudi.
Naye Isa akawatokea, akasimama katikati yao,
akasema, “Amani iwe nanyi!” 20 Baada ya kusema
haya, akawaonesha mikono yake na ubavu wake.
Wanafunzi wake wakafurahi sana walipomwona
Bwana Isa. 21 Isa akawaambia tena, “Amani iwe
nanyi! Kama vile Baba alivyonituma mimi, nami
nawatuma ninyi.” 22 Alipokwisha kusema haya,
akawavuvia, akawaambia, “Pokeeni Roho Mtakatifu
wa Mungu. 23 Mkimwondolea mtu yeyote dhambi
zake, zitaondolewa; na yeyote msiyemwondolea
dhambi zake, hazitaondolewa.” 24 Lakini Tomaso
(aliyeitwa Didimasi), mmoja wa wale kumi na wawili,
hakuwa pamoja nao Isa alipokuja. 25 Hivyo wale
wanafunzi wengine wakamwambia, “Tumemwona
Bwana Isa.” Lakini yeye akawaambia, “Nisipoona
zile alama za misumari mikononi mwake, na kuweka
kidole changu kwenye hizo alama za misumari, na
mkono wangu ubavuni mwake, sitaamini.” 26 Baada
ya siku nane, wanafunzi wake walikuwa tena pamoja
ndani ya nyumba, naye Tomaso alikuwa pamoja
nao. Ndipo Isa akaja, milango ikiwa imefungwa,
na kusimama katikati yao, akasema, “Amani iwe
nanyi.” 27 Kisha akamwambia Tomaso, “Weka kidole
chako hapa na uone mikono yangu, nyoosha mkono
wako uguse ubavuni mwangu. Usiwe na shaka,
bali uamini tu.” 28 Tomaso akamwambia, “Bwana
wangu na Mungu wangu!” 29 Isa akamwambia,
“Umeamini kwa kuwa umeniona? Wamebarikiwa wale
ambao hawajaona lakini wameamini.” 30 Isa alifanya
miujiza mingine mingi mbele za wanafunzi wake,
ambayo haikuandikwa katika kitabu hiki. 31 Lakini hii
imeandikwa ili mweze kuamini ya kuwa Isa ndiye Al-
Masihi, Mwana wa Mungu, na kwa kumwamini mpate
uzima katika jina lake.

**21** Baada ya haya Isa akawatokea tena wanafunzi
wake kando ya Bahari ya Tiberia. Yeye
alijionesha kwao hivi: 2 Simoni Petro, Tomaso (aitwaye
Didimasi), Nathanaeli wa Kana ya Galilaya, wana wa
Zebedayo, na wanafunzi wengine wawili walikuwa
pamoja. 3 Simoni Petro akawaambia wenzake,
“Mimi naenda kuvua samaki.” Nao wakamwambia,
“Tutaenda pamoja nawe.” Wakatoka, wakaingia ndani
ya mashua, lakini usiku ule hawakupata chochote.
4 Mara baada ya kupambazuka, Isa akasimama

ufuoni, lakini wanafunzi hawakumtambua kwamba
alikuwa Isa. **5** Isa akawaambia, “Wanangu, je, mna
samaki wowote?” Wakamjibu, “La.” **6** Akawaambia,
“Shusheni nyavu upande wa kuume wa mashua
yenu nanyi mtapata samaki.” Wakashusha nyavu,
na tazama, wakapata samaki wengi mno hata
wakashindwa kuvutia zile nyavu zilizojaa samaki ndani
ya mashua. **7** Basi yule mwanafunzi aliyependwa na
Isa akamwambia Petro, “Huyu ni Bwana Isa!” Simoni
Petro aliposikia kwamba ni Bwana Isa, akajifunga
nguo yake (kwa kuwa alikuwa ameitoa), naye akajitosa
baharini. **8** Wale wanafunzi wengine wakaja kwa ile
mashua huku wakikokota ule wavu uliojaa samaki,
maana hawakuwa mbali na nchi kavu, ilikuwa yapata
dhiraa mia mbili. **9** Walipofika ufuoni, wakaona moto
wa makaa na samaki wakiokwa juu yake, na mikate.
**10** Isa akawaambia, “Leteni baadhi ya hao samaki
mliovua sasa hivi.” **11** Simoni Petro akapanda kwenye
mashua na kuukokota ule wavu ufuoni. Ulikuwa
umejaa samaki wakubwa mia moja hamsini na watatu.
Ingawa samaki walikuwa wengi kiasi hicho, ule wavu
haukuchanika. **12** Isa akawaambia, “Njooni mpate
kifungua kinywa.” Hakuna hata mmoja wa wanafunzi
aliyethubutu kumuuliza, “Wewe ni nani?” Walijua kuwa
ni Bwana Isa. **13** Isa akaja, akachukua ule mkate,
akawapa, na vivyo hivyo akawagawia wale samaki.
**14** Hii ilikuwa mara ya tatu Isa kuwatokea wanafunzi
wake baada yake kufufuliwa kutoka kwa wafu. **15**
Walipokwisha kula, Isa akamuuliza Simoni Petro,
“Je, Simoni mwana wa Yohana, unanipenda kweli
kuliko hawa?” Yeye akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe
unajua ya kuwa ninakupenda.” Isa akamwambia,
“Lisha wana-kondoo wangu.” **16** Isa akamuuliza tena,
“Simoni, mwana wa Yohana, wanipenda?” Petro
akamjibu, “Ndiyo Bwana, wewe unajua ya kuwa
ninakupenda.” Isa akamwambia, “Chunga kondoo
wangu.” **17** Kwa mara ya tatu Isa akamuuliza Petro,
“Simoni mwana wa Yohana, unanipenda?” Petro
akahuzunika sana kwa kuwa Isa alimuuliza mara ya
tatu, “Unanipenda?” Akamjibu, “Bwana, wewe unajua
yote, unajua ya kuwa ninakupenda.” Isa akamwambia,
“Lisha kondoo wangu. **18** Amin, amin nakuambia,
ulipokuwa kijana ulivaa na kwenda unakotaka. Lakini
utakapokuwa mzee, utanyoosha mikono yako na
mtu mwingine atakuvika na kukupeleka usipotaka
kwenda.” **19** Isa alisema haya ili kuashiria aina ya kifo
ambacho Petro angemtukuza nacho Mungu. Kisha
Isa akamwambia Petro, “Nifuate!” **20** Petro akageuka,
akamwona yule mwanafunzi aliyependwa na Isa
akiwafuata. (Huyu ndiye yule mwanafunzi aliyeegama
kifuani mwa Isa walipokula naye chakula cha mwisho
na kuuliza, “Bwana, ni nani atakayekusaliti?”) **21**
Petro alipomwona huyo mwanafunzi, akamuuliza
Isa, “Bwana, na huyu je?” **22** Isa akamjibu, “Ikiwa
nataka aishi hadi nitakaporudi, inakuhusu nini? Wewe
inakupasa unifuate!” **23** Kwa sababu ya maneno haya
ya Isa, uvumi ukaenea miongoni mwa ndugu kwamba
huyu mwanafunzi hangekufa. Lakini Isa hakusema
kuwa hangekufa. Yeye alisema tu kwamba, “Ikiwa
nataka aishi hadi nitakaporudi, inakuhusu nini?” **24**
Huyu ndiye yule mwanafunzi anayeshuhudia mambo
haya, na ndiye ameandika habari hizi. Nasi tunajua
ya kuwa ushuhuda wake ni kweli. **25** Lakini kuna
mambo mengine mengi ambayo Isa alifanya. Kama
yote yangeandikwa, nadhani hata ulimwengu wote
haungekuwa na nafasi ya kutosha kuweka vitabu
ambavyo vingeandikwa.

# Matendo

**1** Katika kitabu changu cha kwanza nilikuandikia,
Theofilo, kuhusu mambo yote Isa aliyoyafanya
na kufundisha tangu mwanzo, **2** hadi siku ile
alipochukuliwa kwenda mbinguni, baada ya kuwapa
maagizo kupitia kwa Roho Mtakatifu wa Mungu wale
mitume aliowachagua. **3** Baada ya mateso yake,
alijionesha kwao na kuwathibitishia kwa njia nyingi
kwamba yeye yu hai. Katika muda wa siku arobaini
baada ya kufufuka kwake aliwatokea na kunena
kuhusu ufalme wa Mungu. **4** Wakati mmoja alipokuwa
pamoja nao, aliwapa amri hii, “Msitoke Yerusalemu,
bali ingojeni ahadi ya Baba, ambayo mmenisikia
nikisema habari zake. **5** Yahya aliwabatiza kwa maji,
lakini baada ya siku chache mtabatizwa kwa Roho
wa Mungu.” **6** Mitume walipokuwa wamekusanyika
pamoja, wakamuuliza Isa, “Bwana, je, huu ndio wakati
wa kuwarudishia Israeli ufalme?” **7** Isa akawaambia,
“Sio wajibu wenu kujua nyakati au majira ambayo
Baba ameyaweka kwa mamlaka yake mwenyewe. **8**
Lakini mtapokea nguvu, Roho wa Mungu akiwajilia
juu yenu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika
Yerusalemu, na Yudea yote, na Samaria, na miisho ya
dunia.” **9** Baada ya kusema mambo haya, walipokuwa
wanatazama, akachukuliwa juu mbinguni mbele ya
macho yao na wingu likampokea wasimwone tena. **10**
Walipokuwa bado wakikaza macho yao kuelekea juu
alipokuwa akienda zake mbinguni, ghafula, wanaume
wawili waliovaa mavazi meupe wakasimama karibu
nao. **11** Wakasema, “Enyi watu wa Galilaya, mbona
mnasimama mkitazama juu angani? Huyu Isa
aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda mbinguni,
atarudi tena jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake
mbinguni.” **12** Ndipo waliporudi Yerusalemu kutoka
Mlima wa Mizeituni, uliokuwa karibu na Yerusalemu,
umbali wa mwendo wa Sabato kutoka mjini. **13**
Walipowasili mjini Yerusalemu, walienda ghorofani
kwenye chumba walichokuwa wakiishi. Waliokuwepo
walikuwa: Petro, Yohana, Yakobo na Andrea; Filipo na
Tomaso; Bartholomayo na Mathayo, Yakobo mwana
wa Alfayo, Simoni Zelote na Yuda mwana wa Yakobo.
**14** Hawa wote waliungana pamoja katika maombi. Pia
walikuwepo wanawake kadhaa, na Mariamu mama
yake Isa, na ndugu zake Isa. **15** Katika siku hizo Petro
akasimama katikati ya waumini (jumla yao walikuwa
watu wapatao mia moja na ishirini), akasema, **16**
“Ndugu zangu, ilibidi andiko litimie, ambalo Roho wa
Mungu alitabiri kupitia kwa Daudi kumhusu Yuda,
aliyewaongoza wale waliomkamata Isa. **17** Yuda
alikuwa mmoja wetu, kwa maana na yeye alichaguliwa
ashiriki katika huduma hii.” **18** (Basi Yuda alinunua
shamba kwa zile fedha za uovu alizopata; akiwa huko
shambani akaanguka, akapasuka na matumbo yote
yakatoka nje. **19** Kila mtu Yerusalemu akasikia habari
hizi, kwa hiyo wakapaita mahali hapo kwa lugha yao,
Akeldama, yaani Shamba la Damu.) **20** “Kama vile
ilivyoandikwa katika Kitabu cha Zaburi, “‘Mahali pake
na pawe ukiwa, wala asiwepo yeyote atakayeishi
humo,’ na, “‘Mtu mwingine aichukue nafasi yake
ya uongozi.’ **21** Kwa hiyo inatubidi tumchague mtu
mwingine miongoni mwa wale ambao wamekuwa
pamoja nasi wakati wote Bwana Isa alipokuwa
akiishi kati yetu, **22** kuanzia ubatizo wa Yahya hadi
siku aliyochukuliwa kutoka kwetu kwenda Mbinguni.
Kwa kuwa mmoja wao inabidi awe shahidi pamoja
nasi wa ufufuo wake.” **23** Wakapendekeza majina
ya watu wawili: Yusufu, aitwaye Barsaba (ambaye
pia alijulikana kama Yusto) na Mathiya. **24** Kisha
wakaomba, wakasema, “Mwenyezi Mungu, wewe
waujua moyo wa kila mtu. Tuoneshe ni yupi kati ya
hawa wawili uliyemchagua **25** ili achukue nafasi ya
huduma ya utume, ambayo Yuda aliiacha ili aende
anapostahili.” **26** Kisha wakawapigia kura, nayo kura
ikamwangukia Mathiya, naye akaongezwa kwenye
wale mitume kumi na mmoja.

**2** Siku ya Pentekoste ilipowadia, waumini wote
walikuwa mahali pamoja. **2** Ghafula, sauti kama
mvumo mkubwa wa upepo mkali ikatoka mbinguni,
ikaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. **3**
Zikatokea ndimi kama za moto zilizogawanyika na
kutua juu ya kila mmoja wao. **4** Wote wakajazwa
na Roho Mtakatifu wa Mungu, wakaanza kunena
kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia. **5**
Basi walikuwako Yerusalemu Wayahudi wanaomcha
Mungu kutoka kila taifa chini ya mbingu. **6** Waliposikia
sauti hii, umati wa watu walikusanyika pamoja
wakistaajabu, kwa sababu kila mmoja wao aliwasikia
wakisema kwa lugha yake mwenyewe. **7** Wakiwa
wameshangaa na kustaajabu, wakauliza, “Je, hawa
wote wanaozungumza si Wagalilaya? **8** Imekuwaje
basi kila mmoja wetu anawasikia wakinena kwa lugha

yake ya kuzaliwa? **9** Wapathi, Wamedi, Waelami,
wakazi wa Mesopotamia, Yudea, Kapadokia, Ponto
na jimbo la Asia, **10** Frigia, Pamfilia, Misri na pande
za Libia karibu na Kirene, na wageni kutoka Rumi **11**
(Wayahudi na wale walioongokea dini ya Kiyahudi),
Wakrete na Waarabu: sote tunawasikia watu hawa
wakisema mambo makuu ya ajabu ya Mungu katika
lugha zetu wenyewe." **12** Wakiwa wameshangaa
na kufadhaika wakaulizana, "Ni nini maana ya
mambo haya?" **13** Lakini wengine wakawadhihaki
wakasema, "Hawa wamelewa kwa divai!" **14** Ndipo
Petro akasimama pamoja na wale mitume kumi na
mmoja, akapaza sauti yake na kuhutubia umati ule
wa watu, akasema: "Wayahudi wenzangu na nyote
mnaoishi Yerusalemu, nisikilizeni kwa makini, ili jambo
hili lijulikane kwenu. **15** Hakika watu hawa hawajalewa
kama mnavyodhania, kwa kuwa sasa ni saa tatu
asubuhi! **16** La, hili ni jambo lililotabiriwa na nabii
Yoeli, akisema: **17** "'Katika siku za mwisho, asema
Mungu, nitamimina Roho wangu juu ya wote wenye
mwili. Wana wenu wa kiume na wa kike watatabiri,
vijana wenu wataona maono, na wazee wenu wataota
ndoto. **18** Hata juu ya watumishi wangu, wanaume
kwa wanawake, katika siku zile nitamimina Roho
wangu, nao watatabiri. **19** Nami nitaonesha maajabu
juu mbinguni, na ishara chini duniani: damu, moto, na
mawimbi ya moshi. **20** Jua litakuwa giza na mwezi
utakuwa mwekundu kama damu, kabla ya kuja siku ile
kuu ya Mwenyezi Mungu iliyo tukufu. **21** Na kila mtu
atakayeliitia jina la Mwenyezi Mungu, ataokolewa.' **22**
"Enyi Waisraeli, sikilizeni maneno haya nisemayo:
Isa Al-Nasiri alikuwa mtu aliyethibitishwa kwenu na
Mungu kwa miujiza, maajabu na ishara, ambayo
Mungu alitenda miongoni mwenu kupitia kwake, kama
ninyi wenyewe mjuavyo. **23** Baada ya huyu mtu
kutolewa kwenu kwa mpango wa Mungu uliokusudiwa
kwa kujua kwake Mungu tangu zamani, ninyi mlimuua
kwa kumsulubisha msalabani, kwa mikono ya watu
waovu. **24** Lakini Mungu alimfufua kutoka kwa wafu
akamwondolea uchungu wa mauti, kwa sababu
haikuwezekana yeye kushikiliwa na nguvu za mauti. **25**
Kwa maana Daudi asema hivi kumhusu: "'Nilimwona
Bwana mbele yangu daima. Kwa sababu yuko mkono
wangu wa kuume, sitatikisika. **26** Kwa hiyo moyo
wangu unafurahia, na ulimi wangu unashangilia; mwili
wangu nao utapumzika kwa tumaini. **27** Kwa maana
hutaniacha kaburini, wala hutamwacha Aliye Mtakatifu
wako kuona uharibifu. **(Hadēs g86)** **28** Umenionesha
njia za uzima, utanijaza na furaha mbele zako.' **29**
"Ndugu zangu Waisraeli, nataka niwaambie kwa
uhakika kwamba baba yetu wa zamani Daudi alikufa
na kuzikwa, nalo kaburi lake lipo hapa hadi leo. **30**
Lakini alikuwa nabii na alijua ya kuwa Mungu alikuwa
amemwahidi kwa kiapo, kwamba angemweka mmoja
wa wazao wake penye kiti chake cha utawala. **31**
Daudi, akiona mambo yaliyo mbele, akanena kuhusu
kufufuka kwa Al-Masihi, kwamba hakuachwa kaburini,
wala mwili wake haukuona uharibifu. **(Hadēs g86)** **32**
Mungu alimfufua huyu Isa, na sisi sote ni mashahidi
wa jambo hilo. **33** Basi yeye ametukuzwa hadi mkono
wa kuume wa Mungu, na amepokea kutoka kwa Baba
ahadi ya Roho Mtakatifu wa Mungu, naye amemimina
kile mnachoona sasa na kusikia. **34** Kwa kuwa
Daudi hakupaa kwenda mbinguni, lakini anasema,
"'Bwana alimwambia Bwana wangu: "Keti mkono
wangu wa kuume, **35** hadi nitakapowaweka adui
zako chini ya miguu yako."' **36** "Kwa hiyo Israeli wote
na wajue jambo hili kwa uhakika kwamba: Mungu
amemfanya huyu Isa, ambaye ninyi mlimsulubisha,
kuwa Bwana na Al-Masihi." **37** Watu waliposikia
maneno haya yakawachoma mioyo yao, wakawauliza
Petro na wale mitume wengine, "Ndugu zetu tufanye
nini?" **38** Petro akawajibu, "Tubuni, mkabatizwe kila
mmoja wenu kwa jina la Isa Al-Masihi, ili mpate
kusamehewa dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa
cha Roho wa Mungu. **39** Kwa kuwa ahadi hii ni
kwa ajili yenu na watoto wenu, na kwa wote walio
mbali, na kila mtu ambaye Bwana Mungu wetu
atamwita amjie." **40** Petro akawaonya kwa maneno
mengine mengi na kuwasihi akisema, "Jiepusheni na
kizazi hiki kilichopotoka." **41** Wale wote waliopokea
ujumbe wa Petro kwa furaha wakabatizwa, na siku
ile waliongezeka watu wapatao elfu tatu. **42** Nao
wakadumu katika mafundisho ya mitume, katika
ushirika, katika kumega mkate na katika kusali. **43** Kila
mtu akaingiwa na hofu ya Mungu, nayo miujiza mingi
na ishara zikafanywa na mitume. **44** Waumini wote
walikuwa mahali pamoja, nao wakashirikiana katika
mambo yote. **45** Waliuza mali yao na vitu walivyokuwa
navyo, kila mtu akagawiwa kadiri ya mahitaji yake.
**46** Siku zote kwa moyo mmoja walikutana ndani ya
ukumbi wa Hekalu, wakimega mkate nyumba kwa

nyumba, wakila chakula chao kwa furaha na moyo
mweupe, **47** wakimsifu Mungu na kuwapendeza watu
wote. Kila siku Bwana akaliongeza kundi la waumini
wa Isa wale waliokuwa wakiokolewa.

**3** Siku moja, Petro na Yohana walikuwa wanapanda
kwenda Hekaluni kusali, yapata saa tisa alasiri.
**2** Basi palikuwa na mtu mmoja aliyekuwa kiwete
tangu kuzaliwa. Alichukuliwa na kuwekwa kwenye
lango la Hekalu liitwalo Zuri, kila siku ili aombe
msaada kwa watu wanaoingia Hekaluni. **3** Huyu
mtu alipowaona Petro na Yohana wakikaribia kuingia
Hekaluni, akawaomba wampe sadaka. **4** Wakamkazia
macho, kisha Petro akamwambia, “Tutazame sisi.”
**5** Hivyo yule mtu akawatazama, akitazamia kupata
kitu kutoka kwao. **6** Ndipo Petro akamwambia, “Sina
fedha wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho
nitakachokupa. Kwa jina la Isa Al-Masihi wa Nasiri,
tembea!” **7** Petro akamshika yule mtu kwa mkono
wa kuume akamwinua, mara nyayo zake na vifundo
vya miguu yake vikapata nguvu. **8** Akaruka juu
na kusimama, akaanza kutembea. Kisha akaingia
Hekaluni pamoja na Petro na Yohana, huku akitembea
na kurukaruka na kumsifu Mungu. **9** Watu wote
walipomwona akitembea na kumsifu Mungu, **10**
wakamtambua kuwa ni yule mtu aliyekuwa akiketi nje
ya Hekalu penye lango liitwalo Zuri akiomba msaada,
nao wakajawa na mshangao, wakastaajabu kwa yale
yaliyomtukia. **11** Aliyeponywa alipokuwa akiambatana
na Petro na Yohana, watu wote walishangaa mno,
wakaja wakiwakimbilia pale Ukumbi wa Sulemani. **12**
Petro alipoona watu wamekusanyika akawaambia,
“Enyi Waisraeli, kwa nini mnastaajabu kuhusu jambo
hili? Mbona mnatukazia macho kwa mshangao kana
kwamba ni kwa uwezo wetu au utakatifu wetu
tumemfanya mtu huyu kutembea? **13** Mungu wa
Ibrahimu na Isaka na Yakobo, Mungu wa baba zetu
amemtukuza Mwanawe Isa, ambaye ninyi mlimtoa
ahukumiwe kifo na mkamkana mbele ya Pilato, ingawa
yeye alikuwa ameamua kumwachia aende zake. **14**
Ninyi mlimkataa huyo Mtakatifu na Mwenye Haki,
mkaomba mpewe yule muuaji. **15** Hivyo mkamuua
aliye chanzo cha uzima, lakini Mungu akamfufua
kutoka kwa wafu. Sisi tu mashahidi wa mambo haya.
**16** Kwa imani katika jina la Isa, huyu mtu mnayemwona
na kumfahamu ametiwa nguvu. Ni jina la Isa na imani
kutoka kwake ambayo imemponya kabisa huyu mtu,
kama nyote mnavyoona. **17** “Sasa ndugu zangu, najua
ya kuwa ninyi mlitenda bila kujua, kama walivyofanya
viongozi wenu. **18** Lakini kwa njia hii Mungu alitimiza
kile ambacho alikuwa ametabiri kwa vinywa vya
manabii wake wote, kwamba Al-Masihi atateswa.
**19** Tubuni basi mkamgeukie Mungu, dhambi zenu
zifutwe, ili zipate kuja nyakati za kuburudishwa kutoka
kwake Mwenyezi Mungu, **20** naye apate kumtuma
Al-Masihi, ambaye ameteuliwa kwa ajili yenu, yaani
Isa. **21** Ilimpasa mbingu zimpokee hadi wakati wa
kufanywa upya kila kitu, kama Mungu alivyoahidi
zamani kupitia kwa manabii wake watakatifu. **(aiōn
g165)** **22** Kwa maana Musa alisema, ‘Mwenyezi Mungu,
Mungu wenu, atawainulia nabii kama mimi kutoka
miongoni mwa ndugu zenu. Itawapasa kumtii huyo
kwa kila jambo atakalowaambia. **23** Mtu ambaye
hatamsikiliza huyo nabii, atatupiliwa mbali kabisa na
watu wake.’ **24** “Naam, manabii wote tangu Samweli
na waliokuja baada yake, wote walitabiri kuhusu siku
hizi. **25** Ninyi ndio wana wa manabii na wa agano
ambalo Mungu alifanya na baba zenu, akimwambia
Ibrahimu, ‘Kupitia kwa uzao wako, watu wote wa
ulimwengu watabarikiwa.’ **26** Mungu alipomfufua Isa
Mwanawe, alimtuma kwenu kwanza, ili awabariki kwa
kumgeuza kila mmoja wenu kutoka njia yake mbaya.”

**4** Petro na Yohana walipokuwa wakisema na
watu, makuhani, mkuu wa walinzi wa Hekalu na
Masadukayo wakawajia, **2** huku wakiwa wamekasirika
sana kwa sababu mitume walikuwa wanawafundisha
watu na kuhubiri kwamba kuna ufufuo wa wafu
ndani ya Isa. **3** Wakawakamata Petro na Yohana
na kuwafunga gerezani hadi kesho yake kwa kuwa
ilikuwa jioni. **4** Lakini wengi waliosikia lile neno
waliamini, idadi yao ilikuwa yapata wanaume elfu
tano. **5** Kesho yake, viongozi wa Wayahudi, wazee
na walimu wa Torati walikusanyika Yerusalemu. **6**
Walikuwemo kuhani mkuu Anasi, Kayafa, Yohana,
Iskanda, na wengi wa jamaa ya kuhani mkuu. **7**
Baada ya kuwasimamisha Petro na Yohana katikati
yao, wakawauliza, “Ni kwa uwezo gani au kwa jina la
nani mmefanya jambo hili?” **8** Petro, akiwa amejawa
na Roho Mtakatifu wa Mungu, akajibu, “Enyi watawala
na wazee wa watu, **9** kama leo tukihojiwa kwa
habari ya mambo mema aliyotendewa yule kiwete
na kuulizwa jinsi alivyoponywa, **10** ijulikane kwenu
nyote na kwa watu wote wa Israeli kwamba: Ni

kwa jina la Isa Al-Masihi wa Nasiri, ambaye ninyi
mlimsulubisha lakini Mungu akamfufua kutoka kwa
wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama mbele yenu
akiwa mzima kabisa. 11 Huyu ndiye "'jiwe ambalo
ninyi wajenzi mlilikataa, ambalo limekuwa jiwe kuu la
pembeni.' 12 Wala hakuna wokovu katika mwingine
yeyote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya
mbingu walilopewa wanadamu linalopasa kutuokoa."
13 Viongozi na wazee walipoona ujasiri wa Petro na
Yohana, na kujua ya kuwa walikuwa watu wa kawaida,
wasio na elimu, walishangaa sana, wakatambua
kwamba hawa watu walikuwa na Isa. 14 Lakini kwa
kuwa walikuwa wanamwona yule kiwete aliyeponywa
amesimama pale pamoja nao, hawakuweza kusema
lolote kuwapinga. 15 Wakawaamuru watoke nje
ya Baraza la Wayahudi, ili wasemezane jambo
hilo wao wenyewe. 16 Wakaulizana, "Tuwafanyie
nini watu hawa? Hatuwezi kukanusha muujiza huu
mkubwa walioufanya, ambao ni dhahiri kwa kila mtu
Yerusalemu. 17 Lakini ili kuzuia jambo hili lisiendelee
kuenea zaidi kwa watu, ni lazima tuwaonye watu
hawa ili wasiseme tena na mtu yeyote kwa jina la
Isa." 18 Kisha wakawaita tena ndani na kuwaamuru
wasiseme wala kufundisha kamwe kwa hili jina la
Isa. 19 Lakini Petro na Yohana wakajibu, "Amueni
ninyi wenyewe iwapo ni haki mbele za Mungu kuwatii
ninyi kuliko kumtii Mungu. 20 Lakini sisi hatuwezi
kuacha kusema yale tuliyoyaona na kuyasikia." 21
Baada ya vitisho vingi, wakawaachia waende zao.
Hawakuona njia yoyote ya kuwaadhibu, kwa sababu
ya watu, kwa kuwa watu wote walikuwa wakimsifu
Mungu kwa kile kilichokuwa kimetukia. 22 Kwa kuwa
umri wa yule mtu aliyekuwa ameponywa kwa muujiza
ulikuwa zaidi ya miaka arobaini. 23 Punde Petro na
Yohana walipoachiliwa, walirudi kwa waumini wenzao
wakawaeleza waliyoambiwa na viongozi wa makuhani
na wazee. 24 Watu waliposikia hayo, wakapaza sauti
zao, wakamwomba Mungu kwa pamoja, wakisema,
"Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeziumba mbingu na
nchi na bahari, na vitu vyote vilivyomo. 25 Wewe
ulinena kwa Roho wa Mungu kupitia kwa kinywa cha
baba yetu Daudi, mtumishi wako, ukasema: "'Mbona
mataifa wanaghadhibika, na makabila ya watu kuwaza
ubatili? 26 Wafalme wa dunia wamejipanga, na
watawala wanakusanyika pamoja dhidi ya Mwenyezi
Mungu na dhidi ya Mpakwa Mafuta wake.' 27 Ni
kweli Herode na Pontio Pilato, pamoja na watu
wa Mataifa na Waisraeli, walikusanyika katika mji
huu kupanga njama dhidi ya mwanao mtakatifu Isa,
uliyempaka mafuta. 28 Wakafanya yale uweza wako
na mapenzi yako yalikusudia yatokee tangu zamani.
29 Sasa, Mwenyezi Mungu, angalia vitisho vyao na
utuwezeshe sisi watumishi wako kulinena neno lako
kwa ujasiri mkuu. 30 Nyoosha mkono wako ili kuponya
wagonjwa na kutenda ishara na miujiza kwa jina la
Mwanao mtakatifu Isa." 31 Walipokwisha kuomba,
mahali walipokuwa wamekutanika pakatikiswa, wote
wakajazwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, wakanena
neno la Mungu kwa ujasiri. 32 Waumini wote walikuwa
na moyo mmoja na nia moja. Wala hakuna hata mmoja
aliyesema chochote alichokuwa nacho ni mali yake
mwenyewe, lakini walishirikiana kila kitu walichokuwa
nacho. 33 Mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka
kwa Bwana Isa kwa nguvu nyingi na neema ya Mungu
ilikuwa juu yao wote. 34 Wala hapakuwa mtu yeyote
miongoni mwao aliyekuwa mhitaji, kwa sababu mara
kwa mara wale waliokuwa na mashamba na nyumba
waliviuza, wakaleta thamani ya vitu vilivyouzwa, 35
wakaiweka miguuni pa mitume, kila mtu akagawiwa
kadiri ya mahitaji yake. 36 Yusufu, Mlawi kutoka Kipro,
ambaye mitume walimwita Barnaba (maana yake
Mwana wa Faraja), 37 aliuza shamba alilokuwa nalo,
akaleta hizo fedha alizopata na kuziweka miguuni pa
mitume.

**5** Lakini mtu mmoja jina lake Anania pamoja na
mkewe Safira waliuza kiwanja. 2 Huku mkewe
akijua kikamilifu, Anania alificha sehemu ya fedha
alizopata, akaleta kiasi kilichobaki na kukiweka
miguuni pa mitume. 3 Petro akamuuliza, "Anania,
mbona Shetani ameujaza moyo wako ili kumwambia
uongo Roho wa Mungu, ukaficha sehemu ya fedha
ulizopata kutokana na kiwanja? 4 Je, kabla hujauza
hicho kiwanja, si kilikuwa mali yako? Hata baada
ya kukiuza, je, fedha ulizozipata, si zilikuwa kwenye
uwezo wako? Kwa nini basi umewaza hila hii
moyoni mwako kufanya jambo kama hili? Wewe
hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu."
5 Anania aliposikia maneno haya akaanguka chini
na kufa. Hofu kuu ikawapata wote waliosikia jambo
lililokuwa limetukia. 6 Vijana wakaja, wakaufunga
mwili wake sanda, wakampeleka nje kumzika. 7
Muda wa saa tatu baadaye, mkewe Anania akaingia,

naye hana habari ya mambo yaliyotukia. **8** Petro
akamuuliza, “Niambie, je, mliuza kiwanja kwa thamani
hii?” Akajibu, “Ndiyo, tuliuza kwa thamani hiyo.” **9**
Ndipo Petro akamwambia, “Imekuwaje mkakubaliana
kumjaribu Roho wa Bwana Mungu Mwenyezi?
Tazama! Nyayo za vijana waliomzika mumeo ziko
mlangoni, wewe nawe watakupeleka nje.” **10** Wakati
ule ule, akaanguka chini miguuni mwake na kufa.
Nao wale vijana wakaingia, wakamkuta amekufa,
wakamchukua wakamzika kando ya mumewe. **11** Hofu
kuu ikalipata kundi la waumini wa Isa lote, pamoja na
watu wote waliosikia kuhusu matukio haya. **12** Mitume
walifanya ishara nyingi na miujiza miongoni mwa watu.
Waumini wote walikuwa wakikusanyika katika Ukumbi
wa Sulemani. **13** Hakuna mtu mwingine aliyethubutu
kuambatana nao, ijapokuwa waliheshimiwa sana na
watu. **14** Hata hivyo, waliomwamini Bwana Isa wakazidi
kuongezeka, wanaume na wanawake. **15** Hata
wakawa wanawaleta wagonjwa na kuwalaza kwenye
magodoro na kwenye vitanda barabarani ili yamkini
Petro akipita kivuli chake kiwaguse baadhi yao. **16** Pia
watu wakakusanyika kutoka miji iliyokuwa karibu na
Yerusalemu, wakileta wagonjwa na watu walioteswa
na pepo wachafu. Hao wote wakaponywa. **17** Kisha
kuhani mkuu na wenzake wote waliokuwa pamoja
naye, waliokuwa wa kundi la Masadukayo, wakajawa
na wivu. **18** Wakawakamata mitume na kuwafunga
gerezani. **19** Lakini wakati wa usiku, malaika wa
Mwenyezi Mungu akaja, akafungua milango ya
gereza na akawatoa nje. Akawaambia, **20** “Nendeni,
mkasimame Hekaluni, mkawaambie watu maneno
yote ya maisha haya mapya.” **21** Waliposikia haya
wakaenda Hekaluni alfajiri wakaendelea kufundisha
watu. Kuhani mkuu na wale waliokuwa pamoja nao
walipowasili, alikusanya Baraza la Wayahudi, yaani
wazee wote wa Israeli. Wakatumana wale mitume
waletwe kutoka gerezani. **22** Lakini wale walinzi
wa Hekalu walipoenda gerezani hawakuwakuta
mitume mle. Kwa hiyo wakarudi na kutoa habari. **23**
Wakasema, “Tumekuta milango ya gereza imefungwa
sawasawa na askari wa gereza wamesimama nje
ya mlango, lakini tulipofungua milango hakuwepo
mtu yeyote.” **24** Basi mkuu wa walinzi wa Hekalu na
viongozi wa makuhani waliposikia haya, wakafadhaika
na kushangaa sana kwa ajili yao kwamba jambo hili
litakuwaje. **25** Ndipo mtu mmoja akaja akawaambia,
“Tazameni watu mliowafunga gerezani wako Hekaluni
wakiwafundisha watu.” **26** Ndipo yule mkuu wa
walinzi wa Hekalu wakaenda pamoja na askari
wakawaleta wale mitume, lakini bila ghasia kwa
sababu waliogopa kupigwa mawe na watu. **27**
Waliwaleta mitume, wakawasimamisha mbele ya
Baraza la Wayahudi ili kuhani mkuu awahoji. **28**
“Tuliwaonya kwa nguvu msifundishe kwa jina hili,
lakini ninyi mmeijaza Yerusalemu yote mafundisho
yenu na tena mmekusudia kuleta damu ya mtu huyu
juu yetu.” **29** Petro na wale mitume wengine wakajibu,
“Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu. **30** Mungu
wa baba zetu alimfufua Isa kutoka kwa wafu, ambaye
ninyi mlimuua kwa kumtundika kwenye msalaba.
**31** Mungu alimtukuza, akamweka mkono wake wa
kuume kuwa Kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli
toba na msamaha wa dhambi. **32** Nasi tu mashahidi
wa mambo haya, vivyo hivyo na Roho Mtakatifu wa
Mungu ambaye Mungu amewapa wale wanaomtii.”
**33** Wale wajumbe wa Baraza la Wazee waliposikia
haya, walijawa na ghadhabu, wakataka kuwaua
mitume. **34** Lakini Farisayo mmoja, jina lake Gamalieli,
aliyekuwa mwalimu wa Torati, aliyeheshimiwa na
watu wote, akasimama mbele ya Baraza la Wayahudi,
akaamuru mitume watolewe nje kwa muda. **35** Ndipo
alipowaambia wazee wa Baraza, “Enyi wanaume wa
Israeli, fikirini kwa uangalifu mnayotaka kuwatendea
watu hawa. **36** Kwa maana wakati uliopita, aliinuka
mtu mmoja jina lake Theuda, alijidai kuwa yeye ni
mtu maarufu, akapata wafuasi wapatao mia nne
walioambatana naye. Lakini aliuawa, na wafuasi
wake wote wakatawanyika, wakawa si kitu. **37** Baada
yake, alitokea Yuda Mgalilaya wakati wa kuorodhesha
watu, naye akaongoza kundi la watu kuasi. Yeye pia
aliuawa, nao wafuasi wake wakatawanyika. **38** Kwa
hiyo, kwa habari ya jambo hili nawashauri, jiepusheni
na watu hawa. Waachieni waende zao! Kwa maana
kama kusudi lao na shughuli yao imetokana na
mwanadamu, haitafanikiwa. **39** Lakini ikiwa imetoka
kwa Mungu, hamtaweza kuwazuia watu hawa. Badala
yake mtajikuta mnapigana na Mungu.” **40** Wakapokea
ushauri wa Gamalieli. Wakawaita mitume ndani,
wakaamuru wachapwe mijeledi, kisha wakawaagiza
wasinene tena kwa jina la Isa, wakawaachia waende
zao. **41** Nao mitume wakatoka nje ya Baraza la
Wayahudi, wakiwa wamejaa furaha kwa sababu

wamehesabiwa kustahili kupata aibu kwa ajili ya jina
la Isa. 42 Kila siku, Hekaluni na nyumba kwa nyumba,
hawakuacha kufundisha na kuhubiri Habari Njema
kwamba Isa ndiye Al-Masihi.

6 Basi ikawa katika siku hizo, wakati idadi ya
wanafunzi ilipokuwa ikiongezeka sana, Wayahudi
wa Kiyunani walinung'unika dhidi ya Waebrania kwa
sababu wajane wao walisahaulika katika mgawo wa
chakula wa kila siku. 2 Wale mitume kumi na wawili
wakakusanya wanafunzi wote pamoja wakasema,
"Haitakuwa vyema sisi kuacha huduma ya neno la
Mungu ili kuhudumu mezani. 3 Kwa hiyo ndugu,
chagueni watu saba miongoni mwenu, watu wenye
sifa njema, waliojawa na Roho Mtakatifu wa Mungu
na hekima, ambao tunaweza kuwakabidhi kazi hii, 4
nasi tutatumia muda wetu kuomba na katika huduma
ya neno." 5 Yale waliyosema yakawapendeza watu
wote, nao wakamchagua Stefano (mtu aliyejawa
na imani na Roho wa Mungu) pamoja na Filipo,
Prokoro, Nikanori, Timoni, Parmena na Nikolao
kutoka Antiokia, mtu wa Mataifa aliyeongokea dini
ya Kiyahudi. 6 Wakawaleta watu hawa mbele ya
mitume, nao wakawaombea na kuwawekea mikono.
7 Neno la Mungu likazidi kuenea. Idadi ya wanafunzi
ikazidi kuongezeka sana katika Yerusalemu, hata
makuhani wengi wakaitii ile imani. 8 Stefano, akiwa
amejaa neema na nguvu za Mungu, alifanya ishara
na miujiza mikubwa miongoni mwa watu. 9 Hata
hivyo, ukainuka upinzani wa watu wa Sinagogi la
Watu Huru (kama lilivyokuwa linaitwa) la Wayahudi
wa Kirene na wa Iskanderia, na wengine kutoka Kilikia
na jimbo la Asia. Watu hawa wakaanza kupingana
na Stefano. 10 Lakini hawakuweza kushindana na
ile hekima aliyopewa na Roho wa Mungu alipokuwa
akisema. 11 Ndipo kwa siri wakawashawishi watu
fulani waseme, "Tumemsikia Stefano akisema maneno
ya kufuru dhidi ya Musa na dhidi ya Mungu." 12
Wakawachochea watu, wazee na walimu wa Torati,
nao wakamkamata Stefano wakamfikisha mbele ya
Baraza la Wayahudi. 13 Wakawaleta mashahidi wa
uongo ambao walishuhudia, wakasema, "Mtu huyu
kamwe haachi kusema dhidi ya mahali hapa patakatifu
na dhidi ya Torati. 14 Kwa maana tumemsikia akisema
kwamba Isa Al-Nasiri atapaharibu mahali patakatifu
na kubadili desturi zote tulizopewa na Musa." 15 Watu
wote waliokuwa wameketi katika Baraza la Wayahudi
wakamkazia macho Stefano, wakaona uso wake
unang'aa kama uso wa malaika.

7 Ndipo kuhani mkuu akamuuliza Stefano, "Je,
mashtaka haya ni ya kweli?" 2 Stefano akajibu,
"Ndugu zangu na baba zangu, nisikilizeni! Mungu
wa utukufu alimtokea baba yetu Ibrahimu, alipokuwa
bado yuko Mesopotamia, kabla hajaishi Harani, 3
akamwambia, 'Ondoka katika nchi yako na katika
jamii yako, uende hadi nchi nitakayokuonesha.' 4
"Hivyo aliondoka katika nchi ya Wakaldayo akaenda
kukaa Harani. Baada ya kifo cha baba yake, Mungu
akamtoa huko akamleta katika nchi hii ambayo
mnaishi sasa. 5 Mungu hakumpa urithi wowote katika
nchi hii, hakumpa hata mahali pa kuweka wayo
mmoja. Bali Mungu alimwahidi kuwa yeye na uzao
wake baada yake wangeirithi hii nchi, ingawa wakati
huo Ibrahimu hakuwa na mtoto. 6 Mungu akasema
naye hivi: 'Wazao wako watakuwa wageni kwenye
nchi ambayo si yao, nao watafanywa watumwa na
kuteswa kwa miaka mia nne.' 7 Mungu akasema,
'Lakini mimi nitaliadhibu taifa watakalolitumikia kama
watumwa, na baadaye watatoka katika nchi hiyo na
wataniabudu mahali hapa.' 8 Ndipo akampa Ibrahimu
agano la tohara. Naye Ibrahimu akamzaa Isaka na
kumtahiri siku ya nane. Baadaye Isaka akamzaa
Yakobo, naye Yakobo akawazaa wale baba zetu wa
zamani kumi na wawili. 9 "Kwa sababu hao baba
zetu wa zamani walimwonea wivu Yusufu ndugu
yao, walimuuza kama mtumwa huko Misri. Lakini
Mungu alikuwa pamoja naye. 10 Akamwokoa kutoka
mateso yote yaliyompata. Tena Mungu akampa
Yusufu kibali na hekima aliposimama mbele ya
Farao, mfalme wa Misri. Naye Farao akamweka kuwa
mtawala wa Misri na wa jumba lote la kifalme. 11
"Basi kukawa na njaa katika nchi yote ya Misri na
Kanaani, ikasababisha dhiki kubwa, nao baba zetu
wakawa hawana chakula. 12 Lakini Yakobo aliposikia
kwamba kuna nafaka huko Misri, aliwatuma baba
zetu, wakaenda huko kwa mara yao ya kwanza. 13
Walipoenda mara ya pili, Yusufu alijitambulisha kwa
ndugu zake; naye Farao akapata habari kuhusu ndugu
za Yusufu. 14 Ndipo Yusufu akawatuma kumleta
Yakobo baba yake pamoja na jamaa yake yote; kwa
jumla walikuwa watu sabini na watano. 15 Hivyo
Yakobo akaenda Misri ambako yeye na baba zetu
walifia. 16 Miili yao ilirudishwa Shekemu na kuzikwa

katika kaburi ambalo Ibrahimu alinunua kutoka kwa
wana wa Hamori kwa kiasi fulani cha fedha. **17** "Lakini
wakati ulipokuwa unakaribia wa kutimizwa kwa ile
ahadi ambayo Mungu alikuwa amempa Ibrahimu,
watu wetu walizidi kuongezeka sana huko Misri.
**18** Ndipo 'mfalme mwingine ambaye hakufahamu
habari za Yusufu akatawala Misri'. **19** Huyu mfalme
akawatendea watu wetu hila na kuwatesa baba zetu
kwa kuwalazimisha wawatupe watoto wao wachanga
ili wafe. **20** "Wakati huo Musa alizaliwa, naye hakuwa
mtoto wa kawaida. Akalelewa nyumbani mwa baba
yake kwa muda wa miezi mitatu. **21** Walipomweka
nje mtoni, binti Farao akamchukua akamlea kama
mtoto wake. **22** Musa akafundishwa hekima yote
ya Wamisri, akawa mtu hodari kwa maneno na
matendo. **23** "Musa alipokuwa na umri wa miaka
arobaini aliamua kuwatembelea ndugu zake Waisraeli.
**24** Aliona mmoja wao akidhulumiwa na Mmisri,
akamtetea yule aliyeonewa, akampiga yule Mmisri
akamuua kulipiza kisasi. **25** Musa alidhani kuwa ndugu
zake wangetambua kwamba Mungu anamtumia ili
kuwaokoa, lakini wao hawakuelewa. **26** Siku iliyofuata
Musa aliwakuta Waisraeli wawili wakigombana,
akajaribu kuwapatanisha kwa kuwaambia, 'Enyi watu,
ninyi ni ndugu, mbona mnataka kudhulumiana?' **27**
"Lakini yule mtu aliyekuwa akimdhulumu mwenzake
akamsukuma Musa kando, akamuuliza, 'Ni nani
aliyekufanya mtawala na mwamuzi juu yetu? **28**
Je, unataka kuniua kama ulivyomuua yule Mmisri
jana?' **29** Musa aliposikia maneno haya, alikimbilia
huko Midiani alikokaa kama mgeni, naye akapata
watoto wawili wa kiume. **30** "Baada ya miaka arobaini
kupita, malaika wa Mungu akamtokea Musa jangwani
karibu na Mlima Sinai katika kichaka kilichokuwa
kinawaka moto. **31** Alipoona mambo haya, alishangaa
yale maono. Aliposogea ili aangalie kwa karibu,
akaisikia sauti ya Mwenyezi Mungu, ikisema: **32** 'Mimi
ndimi Mungu wa baba zako, Mungu wa Ibrahimu,
Isaka na Yakobo.' Musa alitetemeka kwa hofu na
hakuthubutu kutazama. **33** "Ndipo Mwenyezi Mungu
akamwambia, 'Vua viatu vyako kwa maana mahali
unaposimama ni patakatifu. **34** Hakika nimeona
mateso ya watu wangu huko Misri. Nimesikia kilio
chao cha uchungu, nami nimeshuka ili niwaokoe.
Basi sasa njoo, nami nitakutuma Misri.' **35** "Huyu
ndiye Musa waliyemkataa waliposema, 'Ni nani
aliyekufanya mtawala na mwamuzi juu yetu?' Alikuwa
ametumwa na Mungu mwenyewe kuwa mtawala na
mkombozi wao, kupitia kwa yule malaika aliyemtokea
katika kile kichaka. **36** Aliwaongoza Waisraeli kutoka
Misri baada ya kufanya ishara na maajabu mengi
huko Misri, katika Bahari ya Shamu, na katika
jangwa kwa muda wa miaka arobaini. **37** "Huyu
ndiye yule Musa aliyewaambia Waisraeli, 'Mungu
atawainulia nabii kama mimi kutoka miongoni mwa
ndugu zenu wenyewe.' **38** Huyu ndiye yule Musa
aliyekuwa katika kusanyiko huko jangwani, ambaye
malaika alisema naye pamoja na baba zetu kwenye
Mlima Sinai, naye akapokea maneno yaliyo hai
ili atupatie. **39** "Lakini baba zetu walikataa kumtii
Musa, badala yake wakamkataa na kuielekeza mioyo
yao Misri tena. **40** Wakamwambia Haruni, 'Tufanyie
miungu itakayotuongoza, kwa maana mtu huyu Musa
aliyetutoa nchi ya Misri, hatujui yaliyompata.' **41** Huu
ni ule wakati walitengeneza sanamu katika umbo la
ndama, wakailetea sadaka kufanya maadhimisho kwa
ajili ya kile kitu walichokitengeneza kwa mikono yao
wenyewe. **42** Ndipo Mungu akageuka, akawaachia
waabudu jeshi lote la mbinguni, kama ilivyoandikwa
katika Kitabu cha Manabii: "'Je, mliniletea dhabihu
na sadaka kwa miaka arobaini kule jangwani, ee
nyumba ya Israeli? **43** La, ninyi mliinua madhabahu
ya Moleki, na nyota ya mungu wenu Refani, vinyago
mlivyotengeneza ili kuviabudu. Kwa hiyo nitawapeleka
mbali' kuliko Babeli. **44** "Baba zetu walikuwa na
lile Hema la Ushuhuda huko jangwani, ambalo
lilitengenezwa kama Mungu alivyomwelekeza Musa,
kulingana na kielelezo alichokiona. **45** Baada ya
kupokea Hema, baba zetu waliingia nalo walipokuja
na Yoshua wakati walimiliki nchi, Mungu alipoyafukuza
mataifa mbele yao. Nalo lilidumu katika nchi hadi
wakati wa Daudi, **46** ambaye alipata kibali kwa
Mungu, naye akaomba kwamba ampatie Mungu
wa Yakobo maskani. **47** Lakini Sulemani ndiye
aliyemjengea Mungu nyumba. **48** "Hata hivyo, Yeye
Aliye Juu Sana hakai kwenye nyumba zilizojengwa
kwa mikono ya wanadamu. Kama nabii alivyosema:
**49** "'Mbingu ni kiti changu cha enzi, nayo dunia
ni mahali pa kuweka miguu yangu. Mtanijengea
nyumba ya namna gani? asema Mwenyezi Mungu.
Au mahali pangu pa kupumzikia patakuwa wapi?
**50** Je, mkono wangu haukuumba vitu hivi vyote?'

51 “Enyi watu wenye shingo ngumu, msiotahiriwa
mioyo wala masikio, daima hamwachi kumpinga Roho
wa Mungu, kama walivyofanya baba zenu. 52 Je,
kuna nabii gani ambaye baba zenu hawakumtesa?
Waliwaua wale waliotabiri habari za kuja kwake yule
Mwenye Haki. Nanyi sasa mmekuwa wasaliti wake
na wauaji. 53 Ninyi ndio mlipokea sheria zilizoletwa
kwenu na malaika, lakini hamkuzitii.” 54 Wazee wa
Baraza la Wayahudi waliposikia haya wakaghadhibika,
wakamsagia meno. 55 Lakini Stefano, akiwa amejawa
na Roho wa Mungu, alikaza macho mbinguni, akaona
utukufu wa Mungu, na Isa akiwa amesimama mkono
wa kuume wa Mungu. 56 Akasema, “Tazameni!
Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu
amesimama upande wa kuume wa Mungu.” 57 Lakini
wao wakapiga kelele kwa sauti kubwa, wakaziba
masikio yao, wakamrukia kwa nia moja. 58 Wakamtoa
nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi
wakaweka mavazi yao miguuni mwa kijana mmoja
aliyeitwa Sauli. 59 Walipokuwa wakimpiga mawe,
Stefano aliomba, “Bwana Isa, pokea roho yangu.”
60 Kisha akapiga magoti, akalia kwa sauti kubwa
akasema, “Bwana, usiwahesabie dhambi hii.” Baada
ya kusema hayo, akalala.

8 Naye Sauli alikua pale, akiridhia kuuawa kwa
Stefano. Siku ile kukatukia mateso makuu dhidi
ya waumini wa Isa huko Yerusalemu, nao waumini
wote isipokuwa mitume wakatawanyika, wakakimbilia
Yudea na Samaria. 2 Watu wacha Mungu wakamzika
Stefano na kumwomboleza sana. 3 Lakini Sauli
alianza kuangamiza kundi la waumini. Aliingia nyumba
kwa nyumba, akiwaburuta wanaume na wanawake, na
kuwafunga gerezani. 4 Kwa hiyo wale waliotawanyika
wakalihubiri neno la Mungu kila mahali walipoenda. 5
Filipo akaenda mji mmoja wa Samaria akawahubiria
habari za Al-Masihi. 6 Watu walipomsikia Filipo na
kuona ishara na miujiza alizofanya, wakasikiliza kwa
makini yale aliyosema. 7 Pepo wachafu wakawa
wakiwatoka watu wengi huku wakipiga kelele, na
wengi waliopooza na viwete wakaponywa. 8 Hivyo
pakawa na furaha kuu katika mji huo. 9 Basi mtu
mmoja jina lake Simoni alikuwa amefanya uchawi kwa
muda mrefu katika mji huo akiwashangaza watu wote
wa Samaria. Alijitapa kwamba yeye ni mtu mkuu, 10
nao watu wote, wakubwa kwa wadogo, wakamsikiliza
na kustaajabu, wakisema, “Mtu huyu ndiye ajulikanaye
kama Uweza Mkuu wa Mungu.” 11 Wakamfuata kwa
sababu kwa muda mrefu alikuwa amewashangaza
kwa uchawi wake. 12 Lakini watu walipomwamini
Filipo akihubiri Injili ya ufalme wa Mungu na jina la
Isa Al-Masihi, wakabatizwa, wanaume na wanawake.
13 Simoni naye akaamini na akabatizwa. Akamfuata
Filipo kila mahali, akistaajabishwa na ishara kuu
na miujiza aliyoiona. 14 Basi mitume waliokuwa
Yerusalemu waliposikia kuwa Samaria wamelipokea
neno la Mungu, wakawatuma Petro na Yohana
waende huko. 15 Nao walipofika wakawaombea ili
wampokee Roho Mtakatifu wa Mungu, 16 kwa sababu
Roho wa Mungu alikuwa bado hajawashukia hata
mmoja ila wamebatizwa tu katika jina la Bwana Isa.
17 Ndipo Petro na Yohana wakaweka mikono yao
juu ya wale waliobatizwa, nao wakapokea Roho wa
Mungu. 18 Simoni alipoona kuwa watu wanapokea
Roho wa Mungu mitume walipoweka mikono juu yao,
akataka kuwapa fedha 19 akisema, “Nipeni na mimi
uwezo huu ili kila mtu nitakayeweka mikono yangu
juu yake apate kupokea Roho wa Mungu.” 20 Petro
akamjibu, “Fedha yako na iangamie pamoja nawe,
kwa sababu ulidhani unaweza kununua karama ya
Mungu kwa fedha! 21 Wewe huna sehemu wala
fungu katika huduma hii kwa kuwa moyo wako si
mnyofu mbele za Mungu. 22 Kwa hiyo tubu kwa uovu
huu wako na umwombe Mwenyezi Mungu. Yamkini
aweza kukusamehe mawazo uliyo nayo moyoni
mwako. 23 Kwa maana ninaona kwamba wewe
umejawa na uchungu na ni mfungwa wa dhambi.”
24 Ndipo Simoni akajibu, “Niombeeni kwa Mwenyezi
Mungu, ili hayo mliyosema lolote lisinitokee.” 25 Nao
walipokwisha kutoa ushuhuda na kuhubiri neno la
Bwana Isa, wakarudi Yerusalemu wakihubiri Injili
katika vijiji vingi vya Samaria. 26 Basi malaika
wa Mwenyezi Mungu akamwambia Filipo, “Nenda
upande wa kusini kwenye ile barabara inayotoka
Yerusalemu kuelekea Gaza ambayo ni jangwa.”
27 Hivyo akaondoka. Akiwa njiani akakutana na
towashi wa Kushi, aliyekuwa afisa mkuu, mwenye
mamlaka juu ya hazina zote za Kandake, Malkia wa
Kushi. Huyu towashi alikuwa ameenda Yerusalemu ili
kuabudu, 28 naye akiwa njiani kurudi nyumbani alikuwa
ameketi kwenye gari lake la vita akisoma kitabu
cha nabii Isaya. 29 Roho wa Mungu akamwambia
Filipo, “Nenda kwenye lile gari ukae karibu nalo.”

30 Ndipo Filipo akakimbilia lile gari na kumsikia
yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo
akamuuliza, “Je, unaelewa hayo unayoyasoma?”
31 Yule towashi akasema, “Nitawezaje kuelewa
mtu asiponifafanulia?” Hivyo akamkaribisha Filipo
ili apande na kuketi pamoja naye. 32 Huyu towashi
alikuwa anasoma fungu hili la Maandiko: “Aliongozwa
kama kondoo aendaye machinjoni, kama mwana-
kondoo anyamazavyo mbele yake yule amkataye
manyoya, hivyo hakufungua kinywa chake. 33 Katika
kufedheheshwa kwake alinyimwa haki yake. Nani
awezaye kueleza kuhusu kizazi chake? Kwa maana
maisha yake yaliondolewa kutoka duniani.” 34 Yule
towashi akamuuliza Filipo, “Tafadhali niambie, nabii
huyu anena habari zake mwenyewe au habari za mtu
mwingine?” 35 Ndipo Filipo akaanza kutumia fungu lile
la Maandiko, akamweleza Injili ya Isa. 36 Walipokuwa
wakiendelea na safari wakafika mahali palipokuwa
na maji, yule towashi akamuuliza Filipo, “Tazama,
hapa kuna maji. Kitu gani kitanizuia nisibatizwe?” [ 37
Filipo akamwambia, “Ukiamini kwa moyo wako wote,
unaweza kubatizwa.” Akajibu, “Naamini kuwa Isa Al-
Masihi ni Mwana wa Mungu.”] 38 Naye akaamuru lile
gari lisimamishwe. Filipo na yule towashi wakateremka
kwenye maji pamoja, naye Filipo akambatiza. 39 Nao
walipotoka kwenye maji, ghafula Roho wa Bwana
Mungu Mwenyezi akamnyakua Filipo, naye towashi
hakumwona tena, lakini akaenda zake akifurahi. 40
Filipo akajikuta Azoto; akasafiri akihubiri Injili katika
miji yote hadi akafika Kaisaria.

9 Wakati ule ule, Sauli alikuwa bado anazidisha
vitisho vya kuua wanafunzi wa Bwana Isa,
akamwendea kuhani mkuu, 2 naye akamwomba
kuhani mkuu ampe barua za kwenda kwenye
masinagogi huko Dameski, ili akimkuta mfuasi yeyote
wa Njia Ile, akiwa mwanaume au mwanamke,
aweze kuwafunga na kuwaleta Yerusalemu. 3 Basi
akiwa katika safari yake, alipokaribia Dameski,
ghafula nuru kutoka mbinguni ikamwangaza pande
zote. 4 Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia,
“Sauli, Sauli, mbona unanitesa?” 5 Sauli akajibu,
“U nani wewe, Bwana?” Ile sauti ikajibu, “Mimi
ni Isa unayemtesa. 6 Sasa inuka uingie mjini,
nawe utaambiwa unachopaswa kufanya.” 7 Watu
waliokuwa wakisafiri pamoja na Sauli wakasimama
bila la kusema, kwa sababu walisikia sauti lakini
hawakumwona aliyekuwa akizungumza. 8 Sauli
akainuka kutoka pale chini na alipojaribu kufungua
macho yake hakuweza kuona kitu chochote. Basi
wakamshika mkono wakamwongoza hadi Dameski. 9
Kwa muda wa siku tatu alikuwa kipofu; naye hakula
wala kunywa chochote. 10 Huko Dameski kulikuwa
na mwanafunzi mmoja jina lake Anania. Bwana Isa
alimwita katika maono, “Anania!” Akajibu, “Mimi hapa
Bwana.” 11 Bwana Isa akamwambia, “Ondoka uende
katika barabara iitwayo Nyofu ukaulize katika nyumba
ya Yuda mtu kutoka Tarso, jina lake Sauli, kwa maana
wakati huu anaomba, 12 katika maono amemwona
mtu aitwaye Anania akija na kuweka mikono juu yake
ili apate kuona tena.” 13 Anania akajibu, “Bwana,
nimesikia kutoka kwa watu wengi habari nyingi kuhusu
mtu huyu na madhara yote aliyowatendea watakatifu
wako huko Yerusalemu. 14 Naye amekuja hapa
Dameski akiwa na mamlaka kutoka kwa viongozi wa
makuhani ili awakamate wote wanaotaja jina lako.”
15 Lakini Bwana Isa akamwambia Anania, “Nenda!
Mtu huyu ni chombo nilichochagua kutangaza jina
langu kwa watu wa Mataifa na wafalme wao na watu
wa Israeli. 16 Nami nitamwonesha jinsi impasavyo
kuteseka kwa ajili ya Jina langu.” 17 Kisha Anania
akaenda kwenye ile nyumba, akaingia ndani. Akaweka
mikono yake juu ya Sauli akasema, “Ndugu Sauli,
Bwana Isa aliyekutokea njiani amenituma kwako
ili upate kuona tena na ujazwe Roho Mtakatifu wa
Mungu.” 18 Ghafula vitu kama magamba vikaanguka
chini, kutoka machoni mwa Sauli, akapata kuona
tena. Akasimama, akabatizwa. 19 Baada ya kula
chakula, akapata nguvu tena. Sauli akakaa siku
kadhaa pamoja na wanafunzi huko Dameski. 20 Papo
hapo akaanza kuhubiri kwenye masinagogi kwamba
Isa Al-Masihi ni Mwana wa Mungu. 21 Watu wote
waliomsikia Sauli walishangaa na kuuliza, “Huyu si
yule mtu aliyesababisha maangamizi makuu huko
Yerusalemu miongoni mwa watu waliolitaja jina hili?
Naye si amekuja hapa kwa kusudi la kuwakamata
na kuwapeleka wakiwa wafungwa mbele ya viongozi
wa makuhani?” 22 Sauli akazidi kuwa hodari na
kuwashangaza Wayahudi walioishi Dameski kwa
kuthibitisha kuwa Isa ndiye Al-Masihi. 23 Baada
ya siku nyingi kupita, Wayahudi wakapanga njama
kumuua Sauli. 24 Lakini Sauli akagundua njama yao.
Wayahudi wakawa wanalinda malango yote ya mji,

usiku na mchana ili wapate kumuua. **25** Lakini wafuasi
wake wakamchukua usiku wakamshusha akiwa ndani
ya kapu kupitia mahali penye nafasi ukutani. **26** Sauli
alipofika Yerusalemu akajaribu kujiunga na wanafunzi
lakini wote walimwogopa, kwa maana hawakuamini
kwamba kweli naye alikuwa mwanafunzi. **27** Lakini
Barnaba akamchukua, akampeleka kwa wale mitume.
Akawaeleza jinsi Sauli akiwa njiani alivyomwona
Bwana Isa, jinsi Bwana alivyosema naye na jinsi
alivyohubiri kwa ujasiri kwa jina la Isa huko Dameski.
**28** Kwa hiyo Sauli akakaa nao akitembea kwa uhuru
kila mahali huko Yerusalemu, akihubiri kwa ujasiri
katika jina la Bwana Isa. **29** Alinena na kuhojiana
na Wayahudi wenye asili ya Kiyunani, lakini wao
walijaribu kumuua. **30** Wale ndugu walipopata habari
wakampeleka hadi Kaisaria, wakamsafirisha kwenda
Tarso. **31** Ndipo waumini katika Yudea yote, Galilaya
na Samaria wakawa na wakati wa amani. Likatiwa
nguvu; na kwa kuwezeshwa na Roho wa Mungu, idadi
yao ikaongezeka, na wakaendelea kudumu katika
kumcha Bwana. **32** Petro alipokuwa akisafiri sehemu
mbalimbali, alienda kuwatembelea watakatifu walioishi
huko Lida. **33** Huko alimkuta mtu mmoja aitwaye Ainea,
aliyekuwa amepooza na kwa muda wa miaka nane
alikuwa hajatoka kitandani. **34** Petro akamwambia,
“Ainea, Isa Al-Masihi anakuponya, inuka utandike
kitanda chako.” Mara Ainea akainuka. **35** Watu wote
wa Lida na Sharoni walipomwona Ainea akitembea
wakamgeukia Bwana Isa. **36** Huko Yafa palikuwa na
mwanafunzi jina lake Tabitha (ambalo kwa Kiyunani ni
Dorkasi). Huyu alikuwa mkarimu sana, akitenda mema
na kuwasaidia maskini. **37** Wakati huo akaugua,
akafa, na wakauosha mwili wake wakauweka katika
chumba cha ghorofani. **38** Kwa kuwa Yafa hapakuwa
mbali sana na Lida, wanafunzi waliposikia kwamba
Petro yuko huko waliwatuma watu wawili kwake ili
kumwomba, “Tafadhali njoo huku pasipo kukawia.” **39**
Kwa hiyo Petro akainuka akaenda nao. Alipowasili,
wakampeleka hadi kwenye chumba cha ghorofani
alipokuwa amelazwa. Wajane wengi walisimama
karibu naye wakilia na kuonesha majoho na nguo
nyingine ambazo Dorkasi alikuwa amewashonea
alipokuwa pamoja nao. **40** Petro akawatoa wote nje
ya kile chumba, kisha akapiga magoti akaomba,
akaugeukia ule mwili akasema, “Tabitha, inuka.”
Akafumbua macho yake na alipomwona Petro,
akaketi. **41** Petro akamshika mkono akamwinua, ndipo
akawaita wale watakatifu na wajane akamkabidhi
kwao akiwa hai. **42** Habari hizi zikajulikana sehemu
zote za Yafa na watu wengi wakamwamini Bwana
Isa. **43** Petro akakaa Yafa kwa siku nyingi akiishi na
Simoni mtengenezaji ngozi.

**10** Katika mji wa Kaisaria palikuwa na mtu
aliyeitwa Kornelio, aliyekuwa jemadari wa kile
kilichojulikana kama kikosi cha Kiitalia. **2** Yeye na
jamaa yake yote walikuwa wacha Mungu; alitoa kwa
ukarimu kwa wale walio na mahitaji na kumwomba
Mungu mara kwa mara. **3** Siku moja alasiri, yapata
saa tisa, aliona maono waziwazi, malaika wa Mungu
akimjia na kumwambia, “Kornelio!” **4** Kornelio
akamkazia macho kwa hofu akasema, “Kuna nini,
Bwana?” Malaika akamwambia, “Sala zako na sadaka
zako kwa maskini zimefika juu na kuwa ukumbusho
mbele za Mungu. **5** Sasa tuma watu waende Yafa
wakamwite mtu mmoja jina lake Simoni aitwaye
Petro. **6** Yeye anaishi na Simoni mtengenezaji ngozi
ambaye nyumba yake iko kando ya bahari.” **7** Yule
malaika aliyekuwa akizungumza naye alipoondoka,
Kornelio akawaita watumishi wake wawili pamoja
na askari mmoja mcha Mungu aliyekuwa miongoni
mwa wale waliomtumikia. **8** Akawaambia mambo
yote yaliyotukia, kisha akawatuma waende Yafa.
**9** Siku iliyofuata, walipokuwa wanaukaribia mji,
yapata saa sita mchana, Petro alipanda juu ya
nyumba kuomba. **10** Alipokuwa akiomba akahisi njaa,
akatamani kupata chakula. Lakini wakati walikuwa
wakiandaa chakula, akalala usingizi mzito sana. **11**
Akaona mbingu zimefunguka na kitu kama kitambaa
kikubwa kikishushwa duniani kwa ncha zake nne.
**12** Ndani yake walikuwepo aina zote za wanyama
wenye miguu minne, nao watambaao nchini, na
ndege wa angani. **13** Ndipo sauti ikamwambia “Petro,
ondoka, uchinje na ule.” **14** Petro akajibu, “La hasha,
Bwana! Sijawahi kamwe kula kitu chochote kilicho
najisi.” **15** Ile sauti ikasema naye mara ya pili,
“Usikiite najisi kitu chochote Mungu alichokitakasa.”
**16** Jambo hili lilitokea mara tatu, na ghafula kile
kitambaa kikarudishwa mbinguni. **17** Petro alipokuwa
akisumbuka kuhusu maana ya maono hayo, wale
watu waliotumwa na Kornelio waliipata nyumba ya
Simoni, wakasimama kwenye lango. **18** Wakabisha
hodi na kuuliza kama Simoni aliyeitwa Petro alikuwa

anaishi hapo. 19 Wakati Petro akiwa anafikiria kuhusu
yale maono, Roho wa Mungu akamwambia, “Simoni,
kuna watu watatu wanaokutafuta. 20 Inuka na ushuke,
usisite kwenda nao kwa kuwa mimi nimewatuma.” 21
Petro akashuka na kuwaambia wale watu waliokuwa
wametumwa kutoka kwa Kornelio, “Mimi ndiye
mnayenitafuta. Mmekuja kwa sababu gani?” 22
Wale watu wakamjibu, “Tumetumwa na Kornelio yule
jemadari. Yeye ni mtu mwema anayemcha Mungu, na
anaheshimiwa na Wayahudi wote. Yeye ameagizwa
na malaika mtakatifu akukaribishe nyumbani mwake,
ili asikilize maneno utakayomwambia.” 23 Basi Petro
akawakaribisha ndani wawe wageni wake. Kesho
yake akaondoka pamoja nao, na baadhi ya ndugu
kutoka Yafa wakafuatana naye. 24 Siku iliyofuata
wakawasili Kaisaria. Kornelio alikuwa akiwangoja
pamoja na jamaa na rafiki zake wa karibu. 25 Petro
alipokuwa akiingia ndani, Kornelio alikuja kumlaki,
akaanguka miguuni mwake kwa heshima. 26 Lakini
Petro akamwinua akamwambia, “Simama, mimi ni
mwanadamu tu.” 27 Petro alipokuwa akizungumza
naye, akaingia ndani na kuwakuta watu wengi
wamekusanyika. 28 Akawaambia, “Mnajua kwamba
ni kinyume cha sheria yetu Myahudi kuchangamana
na mtu wa Mataifa au kumtembelea. Lakini Mungu
amenionesha kwamba nisimwite mtu yeyote kuwa
najisi au asiye safi. 29 Ndiyo sababu ulipotuma
niitwe nilikuja bila kupinga lolote. Basi sasa naomba
unieleze kwa nini umeniita?” 30 Kornelio akajibu,
“Siku nne zilizopita, nilikuwa nyumbani nikisali saa
kama hii, saa tisa alasiri. Ghafula mtu aliyevaa nguo
zilizong’aa akasimama mbele yangu, 31 akasema,
‘Kornelio, maombi yako yamesikiwa na misaada yako
kwa maskini imekumbukwa mbele za Mungu. 32 Basi
tuma watu waende Yafa wakaulize mtu mmoja Simoni
aitwaye Petro, yeye ni mgeni katika nyumba ya Simoni
mtengenezaji ngozi, ambaye nyumba yake iko kando
ya bahari.’ 33 Nilituma watu kwako mara moja, nawe
umefanya vyema kuja. Basi sasa sisi sote tuko hapa
mbele za Mungu kuyasikiliza yote ambayo Bwana
amekuamuru kutuambia.” 34 Ndipo Petro akafungua
kinywa chake akasema, “Mungu hana upendeleo, 35
lakini katika kila taifa, kila mtu amchaye na kutenda
yaliyo haki hukubaliwa naye. 36 Ninyi mnajua ule
ujumbe uliotumwa kwa Israeli, ukitangaza Injili ya
amani kupitia kwa Isa Al-Masihi. Yeye ni Bwana wa
wote. 37 Mnajua yale yaliyotukia katika Yudea yote
kuanzia Galilaya baada ya mahubiri ya Yahya: 38 Jinsi
Mungu alivyompaka mafuta Isa Al-Nasiri katika Roho
wa Mungu, na jinsi alivyoenda kila mahali akitenda
mema na kuponya wote waliokuwa wameonewa
na nguvu za ibilisi, kwa sababu Mungu alikuwa
pamoja naye. 39 “Sisi ni mashahidi wa mambo yote
aliyoyafanya katika Yudea na Yerusalemu. Wakamuua
kwa kumtundika msalabani. 40 Lakini Mungu alimfufua
kutoka kwa wafu siku ya tatu na akamwezesha
kuonekana na watu. 41 Hakuonekana kwa watu
wote, lakini kwetu sisi tuliochaguliwa na Mungu kuwa
mashahidi, ambao tulikula na kunywa naye baada ya
kufufuka kwake kutoka kwa wafu. 42 Naye alituamuru
kuhubiri kwa watu wote na kushuhudia kwamba ndiye
alipakwa mafuta na Mungu kuwa hakimu wa walio
hai na wafu. 43 Manabii wote walishuhudia juu yake
kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa
dhambi katika Jina lake.” 44 Petro alipokuwa akisema
maneno haya, Roho Mtakatifu wa Mungu aliwashukia
wote waliokuwa wakisikiliza ule ujumbe. 45 Wale
waumini waliokuwa wametahiriwa waliokuja na Petro
walishangaa kwa kuona kuwa kipawa cha Roho wa
Mungu kimemwagwa juu ya watu wa Mataifa. 46
Kwa kuwa waliwasikia wakinena kwa lugha mpya
na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akasema,
47 “Je, kuna mtu yeyote anayeweza kuzuia watu
hawa wasibatizwe kwa maji? Wamempokea Roho
Mtakatifu wa Mungu kama sisi tulivyompokea.” 48
Kwa hiyo akaamuru wabatizwe kwa jina la Isa Al-
Masihi. Wakamsihi Petro akae nao kwa siku chache.

11 Mitume na waumini waliokuwa huko Yudea
wakasikia kuwa watu wa Mataifa nao
wamepokea neno la Mungu. 2 Hivyo Petro alipopanda
Yerusalemu, waumini waliotahiriwa wakamshutumu,
3 wakisema, “Ulienda kwa watu wasiotahiriwa na
kula pamoja nao.” 4 Ndipo Petro akaanza kuwaeleza
kuhusu mambo yote yalivyotokea hatua kwa hatua
akisema, 5 “Nilikuwa katika mji wa Yafa nikiomba,
nami nikapitiwa na usingizi wa ghafula, nikaona
maono. Kulikuwa na kitu kama kitambaa kikubwa
kikishuka kutoka mbinguni, kikashushwa kwa ncha
zake nne, nacho kikanikaribia. 6 Nilipoangalia ndani
yake kwa karibu niliona wanyama wenye miguu minne
wa nchini, wanyama mwitu, wanyama watambaao, na
ndege wa angani. 7 Ndipo nikasikia sauti ikiniambia,

‘Petro, ondoka uchinje na ule.’ **8** “Nikajibu, ‘La
hasha, Bwana! Kitu chochote kilicho najisi hakijaingia
kinywani mwangu.’ **9** “Sauti ikasema kutoka mbinguni
mara ya pili, ‘Usikiite najisi kitu chochote Mungu
alichokitakasa.’ **10** Jambo hili lilitokea mara tatu,
ndipo kile kitu kikavutwa tena mbinguni. **11** “Wakati
ule ule watu watatu, waliokuwa wametumwa kutoka
Kaisaria waliwasili katika nyumba niliyokuwa nikikaa.
**12** Roho Mtakatifu wa Mungu akaniambia niende nao
bila kuwa na ubaguzi kati yao na sisi. Hawa ndugu
sita pia walifuatana nami, nasi tukaingia nyumbani
mwa huyo Kornelio. **13** Akatuambia jinsi alivyoona
malaika aliyekuwa amesimama katika nyumba yake
na kusema, ‘Tuma watu waende Yafa wakamlete
Simoni aitwaye Petro. **14** Yeye atakupa ujumbe
ambao kwa huo wewe na wa nyumbani mwako wote
mtaokoka.’ **15** “Nami nilipoanza kusema, Roho wa
Mungu akashuka juu yao kama vile alivyotushukia
sisi hapo mwanzo. **16** Nami nikakumbuka yale Bwana
Isa aliyosema, ‘Yahya alibatiza kwa maji, lakini
ninyi mtabatizwa katika Roho wa Mungu.’ **17** Basi
ikiwa Mungu aliwapa hawa watu kipawa kile kile
alichotupatia sisi tuliomwamini Bwana Isa Al-Masihi,
mimi ni nani hata nifikirie kuwa ningeweza kumpinga
Mungu?” **18** Waliposikia haya hawakuwa na lingine la
kupinga. Nao wakamsifu Mungu, wakisema, “Basi,
Mungu amewapa hata watu wa Mataifa toba iletayo
uzima wa milele.” **19** Basi wale waliotawanyika kwa ajili
ya mateso yaliyotokea Stefano alipouawa walisafiri
hadi Foinike na Kipro na Antiokia. Nao hawakuhubiri
lile Neno kwa mtu yeyote isipokuwa Wayahudi. **20**
Lakini baadhi yao walikuwa watu wa Kipro na Kirene,
ambao walipokuja Antiokia walinena na Wayunani pia
wakiwahubiria Injili kuhusu Bwana Isa. **21** Mkono wa
Mwenyezi Mungu ulikuwa pamoja nao, nayo idadi
kubwa ya watu wakaamini na kumgeukia Bwana Isa.
**22** Habari hizi zilipofika masikioni mwa waumini wa
Isa huko Yerusalemu, wakamtuma Barnaba aende
Antiokia. **23** Alipofika na kuona madhihirisho ya neema
ya Mungu, akafurahi na kuwatia moyo waendelee
kuwa waaminifu kwa Bwana Isa kwa mioyo yao yote.
**24** Barnaba alikuwa mtu mwema, aliyejaa Roho wa
Mungu, mwenye imani, nayo idadi kubwa ya watu
wakaongezeka kwa Bwana Isa. **25** Kisha Barnaba
akaenda Tarso kumtafuta Sauli, **26** naye alipompata
akamleta Antiokia. Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba
na Sauli wakakutana na waumini na kufundisha idadi
kubwa ya watu. Wanafunzi waliitwa wafuasi wa Al-
Masihi mara ya kwanza huko Antiokia. **27** Wakati huo
manabii walishuka toka Yerusalemu hadi Antiokia. **28**
Mmoja wao aliyeitwa Agabo akasimama, akatabiri
kwa uweza wa Roho Mtakatifu wa Mungu kwamba
njaa kubwa ingeenea ulimwengu mzima. (Njaa hiyo
ilitokea wakati wa utawala wa Klaudio.) **29** Mitume
wakaamua kwamba kila mtu, kulingana na uwezo
alio nao, atoe msaada kwa ajili ya ndugu wanaoishi
Yudea. **30** Wakafanya hivyo, misaada yao ikapelekwa
kwa wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli.

**12** Wakati huo huo Mfalme Herode Agripa
aliwakamata baadhi ya waumini wa Isa. **2**
Akaamuru Yakobo, ndugu yake Yohana, auawe
kwa upanga. **3** Alipoona jambo hilo limewapendeza
Wayahudi, akaendelea, akamkamata Petro pia. Hii
ilitokea wakati wa Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu.
**4** Baada ya kumkamata alimfunga gerezani chini ya
ulinzi wa vikundi vinne vya askari, vyenye askari
wanne kila kimoja. Herode alikuwa amekusudia
kumfanyia mashtaka mbele ya watu baada ya Pasaka.
**5** Kwa hiyo Petro akawekwa gerezani, lakini waumini
wa Isa walikuwa wakimwombea kwa Mungu kwa
bidii. **6** Usiku ule kabla ya siku ambayo Herode
Agripa alikuwa amekusudia kumfanyia mashtaka,
Petro alikuwa amelala kati ya askari wawili, akiwa
amefungwa kwa minyororo miwili. Nao walinzi wa
zamu walikuwa wakilinda lango la gereza. **7** Ghafula
malaika wa Mwenyezi Mungu akatokea, na nuru
ikamulika mle ndani ya gereza. Yule malaika akampiga
Petro ubavuni na kumwamsha, akisema, “Ondoka
upesi!” Mara ile minyororo ikaanguka kutoka mikononi
mwa Petro. **8** Yule malaika akamwambia, “Vaa nguo
zako na viatu vyako.” Petro akafanya hivyo. Kisha
akamwambia, “Jifunge vazi lako na unifuate.” **9**
Petro akatoka mle gerezani akiwa amefuatana na
yule malaika. Hakujua wakati huo kuwa yaliyokuwa
yakitukia yalikuwa kweli. Alidhani kuwa anaona
maono. **10** Walipita kundi la kwanza la walinzi na la
pili, wakafika kwenye lango la chuma linaloelekea
mjini. Lango likawafungukia lenyewe, nao wakapita
hapo, wakatoka nje. Baada ya kutembea umbali wa
mtaa mmoja, ghafula yule malaika akamwacha Petro.
**11** Ndipo Petro akarudiwa na fahamu, akasema,
“Sasa ninajua bila shaka yoyote kuwa Mwenyezi

Mungu amemtuma malaika wake na kuniokoa kutoka
makucha ya Herode Agripa na kutoka matazamio
yote ya Wayahudi.” **12** Mara Petro alipotambua hili
aliienda nyumbani mwa Mariamu, mama yake Yohana
aliyeitwa pia Marko, ambako watu wengi walikuwa
wamekutana kwa maombi. **13** Petro alipobisha hodi
kwenye lango la nje, mjakazi aliyeitwa Roda akaja
kumfungulia. **14** Alipoitambua sauti ya Petro, alifurahi
mno akarudi bila kufungua lango, akapaza sauti,
akasema, “Petro yuko langoni!” **15** Wakamwambia yule
mjakazi, “Umerukwa na akili.” Alipozidi kusisitiza kuwa
ni kweli, wakasema, “Lazima awe ni malaika wake.”
**16** Lakini Petro aliendelea kugonga langoni, nao
walipofungua lango na kumwona Petro, walistaajabu
sana. **17** Yeye akawaashiria kwa mkono wake
wanyamaze kimya, akawaeleza jinsi Mwenyezi Mungu
alivyomtoa gerezani. Naye akaongeza kusema,
“Waelezeni Yakobo na ndugu wengine habari hizi.”
Kisha akaondoka akaenda sehemu nyingine. **18**
Kulipokucha kukawa na fadhaa kubwa miongoni mwa
wale askari kuhusu yaliyomtukia Petro. **19** Baada
ya Herode kuamuru atafutwe kila mahali na bila
kumpata, aliwahoji wale askari walinzi kisha akatoa
amri wauawe. Basi Herode Agripa akatoka Yudea
akaenda Kaisaria, akakaa huko kwa muda. **20** Basi
Herode Agripa alikuwa amekasirishwa sana na watu
wa Tiro na Sidoni. Hivyo watu wa miji hiyo miwili
wakaungana pamoja wakataka kukutana naye. Baada
ya kuungwa mkono na Blasto, mtumishi maalum
wa Mfalme Herode Agripa aliyeaminika, wakaomba
mapatano ya amani maana nchi zao ziliitegemea
nchi ya huyo mfalme kwa mahitaji yao ya chakula.
**21** Katika siku iliyochaguliwa Herode Agripa akavaa
mavazi yake ya kifalme, akaketi kwenye kiti chake
cha utawala, akawahutubia watu. **22** Watu waliokuwa
wamekusanyika wakapaza sauti, wakisema, “Hii si
sauti ya mwanadamu, bali ni ya Mungu!” **23** Ghafula,
kwa kuwa Herode hakumpa Mungu utukufu, malaika
wa Mwenyezi Mungu akampiga, naye akaliwa na
chango, akafa. **24** Lakini neno la Mungu likaendelea
mbele na kuenea, nao wengi wakaambatana nalo.
**25** Barnaba na Sauli walipomaliza ile huduma yao
iliyowapeleka, wakarudi Yerusalemu wakiwa pamoja
na Yohana aitwaye Marko.

**13** Katika kundi la waumini wa Isa huko Antiokia
kulikuwa na manabii na walimu: Barnaba,
Simeoni aitwaye Nigeri, Lukio Mkirene, Manaeni
aliyekuwa amelelewa pamoja na Mfalme Herode
Agripa, na Sauli. **2** Walipokuwa wakimwabudu
Mwenyezi Mungu na kufunga, Roho Mtakatifu wa
Mungu akasema, “Nitengeeni Sauli na Barnaba kwa
kazi niliyowaitia.” **3** Ndipo baada ya kufunga na
kuomba, wakawawekea mikono yao na wakawatuma
waende zao. **4** Hivyo, wakiwa wametumwa na Roho
wa Mungu, wakashuka kwenda Seleukia na kutoka
huko wakasafiri baharini hadi kisiwa cha Kipro. **5**
Walipowasili katika mji wa Salami, wakahubiri neno la
Mungu katika sinagogi la Wayahudi. Pia walikuwa na
Yohana Marko kama msaidizi wao. **6** Walipokwisha
kupita katika nchi zote hizo wakafika Pafo, ambapo
walikutana na Myahudi mmoja mchawi aliyekuwa
nabii wa uongo, jina lake Bar-Yesu. **7** Mtu huyu
alikuwa pamoja na Sergio Paulo, mtu mwenye hekima
aliyekuwa msaidizi wa mwakilishi wa mtawala wa
kile kisiwa. Sergio Paulo akawaita Sauli na Barnaba
akitaka kusikia neno la Mungu. **8** Lakini Elima yule
mchawi (hii ndiyo maana ya jina lake), aliwapinga
Barnaba na Sauli na kujaribu kumpotosha yule
mkuu wa kile kisiwa aiache imani. **9** Ndipo Sauli,
ambaye pia aliitwa Paulo, akiwa amejawa na Roho
wa Mungu, akamkazia macho Elima huyo mchawi, **10**
akamwambia, “Ewe mwana wa ibilisi, wewe ni adui wa
kila kilicho haki! Umejaa kila aina ya udanganyifu na
ulaghai. Je, hutaacha kuzipotosha njia za Mwenyezi
Mungu zilizo nyoofu? **11** Nawe sasa sikiliza, mkono
wa Mwenyezi Mungu u dhidi yako. Utakuwa kipofu,
wala hutaona jua kwa muda.” Mara ukungu na
giza vikamfunika, naye akapapasa akitafuta mtu wa
kumshika mkono ili amwoneshe njia. **12** Yule mkuu wa
kile kisiwa alipoona yaliyotukia, akaamini kwa sababu
alistaajabishwa na mafundisho kuhusu Bwana Isa.
**13** Kisha Paulo na wenzake wakasafiri toka Pafo
wakafika Perga huko Pamfilia. Lakini, Yohana Marko
akawaacha huko, akarejea Yerusalemu. **14** Kutoka
Perga wakaendelea hadi Antiokia ya Pisidia. Siku
ya Sabato wakaingia ndani ya sinagogi, wakaketi.
**15** Baada ya Torati ya Musa na Kitabu cha Manabii
kusomwa, viongozi wa sinagogi wakawatumia ujumbe
wakisema, “Ndugu, kama mna neno la kuwafariji
watu hawa, tafadhali lisemeni.” **16** Paulo akasimama,
akawapungia mkono na kusema: “Enyi wanaume
wa Israeli na ninyi nyote mnaomcha Mungu. **17**

Mungu wa watu hawa wa Israeli aliwachagua baba
zetu, akawafanya kustawi walipokuwa huko Misri,
kwa uwezo mwingi akawaongoza na kuwatoa katika
nchi ile. 18 Kwa muda wa miaka arobaini alivumilia
matendo yao walipokuwa jangwani. 19 Naye baada ya
kuyaangamiza mataifa saba yaliyokuwa yakiishi katika
nchi ya Kanaani, akawapa Waisraeli nchi yao iwe
urithi wao. 20 Haya yote yalichukua kama muda wa
miaka mia nne na hamsini. “Baada ya haya, Mungu
akawapa waamuzi hadi wakati wa nabii Samweli.
21 Ndipo watu wakaomba wapewe mfalme, naye
Mungu akawapa Sauli mwana wa Kishi wa kabila la
Benyamini, aliyetawala kwa miaka arobaini. 22 Baada
ya kumwondoa Sauli katika ufalme, akawainulia
Daudi kuwa mfalme wao. Mungu pia alimshuhudia,
akisema, ‘Nimemwona Daudi mwana wa Yese, mtu
anayeupendeza moyo wangu, atakayetimiza mapenzi
yangu yote.’ 23 “Kutoka uzao wa mtu huyu, Mungu
amewaletea Israeli Mwokozi Isa, kama alivyoahidi.
24 Kabla ya kuja kwa Isa, Yahya alihubiri toba na
ubatizo kwa watu wote wa Israeli. 25 Yahya alipokuwa
anakamilisha kazi yake, alisema: ‘Ninyi mnadhani
mimi ni nani? Mimi si yeye. La, lakini yeye yuaja
baada yangu, ambaye mimi sistahili kufungua kamba
za viatu vya miguu yake.’ 26 “Ndugu zangu, wana
wa Ibrahimu, nanyi watu wa Mataifa mnaomcha
Mungu, ujumbe huu wa wokovu umeletwa kwetu. 27
Kwa sababu watu wa Yerusalemu na viongozi wao
hawakumtambua, wala kuelewa maneno ya manabii
yanayosomwa kila Sabato, bali waliyatimiza maneno
hayo kwa kumhukumu yeye. 28 Ijapokuwa hawakupata
sababu yoyote ya kumhukumu kifo, walimwomba
Pilato aamuru auawe. 29 Walipokwisha kufanya yale
yote yaliyoandikwa kumhusu, walimshusha kutoka
msalabani na kumzika kaburini. 30 Lakini Mungu
alimfufua kutoka kwa wafu. 31 Naye kwa siku nyingi
akawatokea wale waliokuwa pamoja naye kuanzia
Galilaya hadi Yerusalemu. Nao sasa wamekuwa
mashahidi wake kwa watu wetu. 32 “Nasi tunawaletea
Habari Njema: kwamba yale Mungu aliyowaahidi baba
zetu 33 sasa ameyatimiza kwetu sisi, watoto wao,
kwa kumfufua Isa, kama ilivyoandikwa katika Zaburi
ya pili: “‘Wewe ni Mwanangu; leo mimi nimekuwa
Baba yako.’ 34 Kwa kuwa Mungu alimfufua kutoka
kwa wafu asioze kamwe, alitamka maneno haya:
“‘Nitakupa wewe baraka takatifu zilizo za hakika
nilizomwahidi Daudi.’ 35 Kama ilivyosemwa mahali
pengine katika Zaburi, “‘Hutamwacha Aliye Mtakatifu
wako kuona uharibifu.’ 36 “Basi Daudi alipokwisha
kulitumikia kusudi la Mungu katika kizazi chake,
alilala; akazikwa na baba zake, na mwili wake
ukaoza. 37 Lakini yule ambaye Mungu alimfufua
kutoka kwa wafu hakuona uharibifu. 38 “Kwa hiyo
ndugu zangu, nataka ninyi mjue kwamba kupitia kwa
huyu Isa msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu.
39 Kupitia yeye, kila mtu amwaminiye anahesabiwa
haki kwa kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa
haki kwa Torati ya Musa. 40 Kwa hiyo jihadharini ili
yale waliyosema manabii yasiwapate: 41 “‘Angalieni,
enyi wenye dhihaka, mkastaajabu, mkaangamie,
kwa maana nitatenda jambo wakati wenu ambalo
hamtasadiki, hata kama mtu akiwaambia.’” 42 Paulo
na Barnaba walipokuwa wakitoka nje ya sinagogi,
watu wakawaomba wazungumze tena mambo hayo
Sabato iliyofuata. 43 Baada ya kusanyiko la Sinagogi
kutawanyika, wengi wa Wayahudi na watu wa Mataifa
walioongokea dini ya Kiyahudi wakawafuata Paulo na
Barnaba, wakazungumza nao na kuwahimiza wadumu
katika neema ya Mungu. 44 Sabato iliyofuata, karibu
watu wote wa mji walikuja kusikiliza neno la Mwenyezi
Mungu. 45 Lakini Wayahudi walipoona umati ule
mkubwa wa watu, walijawa na wivu, wakayakanusha
maneno Paulo aliyokuwa akisema. 46 Ndipo Paulo na
Barnaba wakawajibu kwa ujasiri, wakisema, “Ilitupasa
kunena nanyi neno la Mungu kwanza. Lakini kwa kuwa
mmelikataa, mkajihukumu wenyewe kuwa hamstahili
uzima wa milele, sasa tunawageukia watu wa Mataifa.
(aiōnios g166) 47 Kwa maana hili ndilo Mwenyezi Mungu
alilotuamuru: “‘Nimewafanya ninyi kuwa nuru kwa
watu wa Mataifa, ili mpate kuuleta wokovu hadi miisho
ya dunia.’” 48 Watu wa Mataifa waliposikia haya
wakafurahi na kulitukuza neno la Mwenyezi Mungu;
nao wote waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele
wakaamini. (aiōnios g166) 49 Neno la Bwana likaenea
katika eneo lile lote. 50 Lakini viongozi wa Wayahudi
wakawachochea wanawake wenye kumcha Mungu,
wenye vyeo pamoja na watu maarufu katika mji,
wakachochea mateso dhidi ya Paulo na Barnaba
na kuwafukuza kutoka eneo hilo. 51 Hivyo Paulo
na Barnaba wakakung’uta mavumbi ya miguu yao
ili kuwapinga, nao wakaenda Ikonio. 52 Wanafunzi
wakajawa na furaha na Roho wa Mungu.

14 Huko Ikonio Paulo na Barnaba waliingia pamoja
katika sinagogi la Wayahudi kama ilivyokuwa
desturi yao. Huko wakahubiri kwa uwezo mkubwa
kiasi kwamba Wayahudi pamoja na watu wa Mataifa
wakaamini. 2 Lakini wale Wayahudi waliokataa
kuamini wakawachochea watu wa Mataifa, wakatia
chuki ndani ya mioyo yao dhidi ya waumini. 3 Hivyo
Paulo na Barnaba wakakaa huko kwa muda wa
kutosha wakihubiri kwa ujasiri kuhusu Bwana Isa,
ambaye alithibitisha ujumbe wa neema yake kwa
kuwawezesha kufanya ishara na miujiza. 4 Lakini watu
wa mji ule waligawanyika, wengine wakakubaliana na
Wayahudi na wengine na mitume. 5 Watu wa Mataifa
na Wayahudi wakajiunga na baadhi ya viongozi,
wakafanya mpango wa kuwatendea mitume mabaya
na kuwapiga mawe. 6 Lakini mitume walipopata habari
hizi wakakimbilia Listra na Derbe, miji ya Likaonia
na sehemu zilizopakana nayo. 7 Huko wakaendelea
kuhubiri Injili. 8 Katika mji wa Listra, kulikuwa
na kiwete, aliyekuwa amelemaa tangu kuzaliwa,
na hakuwa ametembea kamwe. 9 Alimsikiliza
Paulo alipokuwa akihubiri. Paulo alipomtazama
akaona ana imani ya kuponywa. 10 Paulo akapaza
sauti, “Simama kwa miguu yako!” Mara yule mtu
akasimama upesi akaanza kutembea! 11 Umati
ule wa watu walipoona yaliyokuwa yamefanywa na
Paulo, wakapaza sauti, wakasema kwa lugha yao
ya Kilikaonia, “Miungu imetushukia katika umbo la
binadamu!” 12 Wakamwita Barnaba Zeu na Paulo
wakamwita Herme kwa kuwa ndiye alikuwa msemaji
mkuu. 13 Kuhani wa Zeu, ambaye hekalu lake lilikuwa
nje kidogo tu ya mji, akaleta mafahali na mashada
ya maua penye lango la mji kwa sababu yeye na
umati ule wa watu walitaka kuwatolea dhabihu.
14 Lakini mitume Paulo na Barnaba waliposikia
haya, wakararua nguo zao, wakawaendea wale watu
kwa haraka, wakawapigia kelele, wakisema, 15
“Enyi watu, kwa nini mnafanya mambo haya? Sisi
ni wanadamu tu kama ninyi! Tunawaletea Habari
Njema, tukiwaambia kwamba mgeuke mtoke katika
mambo haya yasiyofaa, mmwelekee Mungu aliye
hai, aliyeziumba mbingu na nchi na bahari na vitu
vyote vilivyomo. 16 Zamani aliwaachia mataifa waishi
walivyotaka. 17 Lakini hakuacha kuwaonesha watu
uwepo wake: Ameonesha wema kwa kuwanyeshea
mvua toka mbinguni na kuwapa mazao kwa majira
yake, naye amewapa chakula tele na kuijaza mioyo
yenu na furaha.” 18 Hata kwa maneno haya yote,
ilikuwa vigumu kuzuia umati ule wa watu kuwatolea
dhabihu. 19 Ndipo wakaja baadhi ya Wayahudi
kutoka Antiokia na Ikonio wakawashawishi wale watu,
wakampiga Paulo kwa mawe, wakamburuta hadi
nje ya mji, wakidhani amekufa. 20 Lakini baada ya
wanafunzi kukusanyika akainuka na kurudi mjini.
Kesho yake yeye na Barnaba wakaondoka kwenda
Derbe. 21 Wakahubiri Injili katika mji huo na kupata
wanafunzi wengi. Kisha wakarudi Listra, Ikonio na
Antiokia, 22 wakiwaimarisha wanafunzi na kuwatia
moyo waendelee kudumu katika imani. Wakawaonya
wakisema, “Imetupasa kuingia katika ufalme wa
Mungu kupitia katika taabu nyingi.” 23 Nao baada
ya kuwateua wazee katika kila kundi la waumini wa
Isa, kwa kufunga na kuomba wakawakabidhi kwa
Bwana Isa waliyemwamini. 24 Kisha wakapitia Pisidia
wakafika Pamfilia. 25 Baada ya kuhubiri neno la
Mungu huko Perga, wakateremkia Atalia. 26 Kutoka
Atalia wakasafiri baharini wakarudi Antiokia, ambako
walikuwa wamesifiwa kwa ajili ya neema ya Mungu
kutokana na ile huduma waliyokuwa wameikamilisha.
27 Walipowasili Antiokia wakawaita waumini pamoja
na kutoa taarifa ya yale yote Mungu aliyokuwa
ametenda kupitia kwao na jinsi alivyokuwa amefungua
mlango wa imani kwa ajili ya watu wa Mataifa. 28
Nao wakakaa huko pamoja na wanafunzi kwa muda
mrefu.

15 Baadhi ya watu wakashuka Antiokia kutoka
Yudea, nao wakawa wanawafundisha waumini:
“Msipotahiriwa kulingana na desturi aliyofundisha
Musa, hamwezi kuokoka.” 2 Baada ya Paulo na
Barnaba kutokubaliana nao kukawa na mabishano
makali, Paulo na Barnaba na baadhi ya wengine
miongoni mwao wakachaguliwa kwenda Yerusalemu
ili kujadiliana jambo hili na mitume na wazee. 3
Hivyo wakatumwa na waumini. Wakapitia Foinike
na Samaria, wakielezea jinsi watu wa Mataifa
walivyoongoka. Habari hizi zikaleta furaha kubwa kwa
ndugu wote. 4 Walipofika Yerusalemu, walipokelewa
na kundi la waumini na mitume pamoja na wazee.
Ndipo Paulo na Barnaba wakawaarifu kila kitu Mungu
alichokuwa amefanya kupitia kwao. 5 Ndipo baadhi
ya waumini waliokuwa wa dhehebu la Mafarisayo
wakasimama na kusema, “Hao watu wa Mataifa

lazima watahiriwe na waagizwe kutii Torati ya Musa.”
6 Mitume na wazee wakakutana pamoja ili kufikiri
jambo hili. 7 Baada ya majadiliano mengi, Petro
akasimama na kusema, “Ndugu zangu, mnajua
kwamba siku za kwanza Mungu alinichagua ili kwa
midomo yangu watu wa Mataifa wapate kusikia
ujumbe wa Injili na kuamini. 8 Mungu, ajuaye mioyo
ya watu, alionesha kwamba anawakubali kwa kuwapa
Roho Mtakatifu wa Mungu kama vile alivyotupatia
sisi. 9 Mungu hakutofautisha kati yetu na wao,
bali alitakasa mioyo yao kwa imani. 10 Sasa basi,
mbona mnataka kumjaribu Mungu kwa kuweka nira
shingoni mwa wanafunzi ambayo baba zetu wala
sisi hatukuweza kuibeba? 11 Lakini sisi tunaamini
ya kuwa tunaokolewa kwa neema ya Bwana wetu
Isa Al-Masihi, kama wao wanavyookolewa.” 12
Kusanyiko lote wakakaa kimya, wakawasikiliza Paulo
na Barnaba wakieleza jinsi Mungu alivyowatumia
kutenda ishara na maajabu kwa watu wa Mataifa.
13 Walipomaliza kunena, Yakobo akasema, “Ndugu
zangu, nisikilizeni. 14 Simoni amekwisha kutueleza
jinsi Mungu, kwa mara ya kwanza alivyoonesha
kuhusika kwa kujichagulia watu kutoka watu wa
Mataifa kwa ajili ya Jina lake. 15 Maneno ya manabii
yanakubaliana na jambo hili, kama ilivyoandikwa: 16
“‘Baada ya mambo haya nitarudi, nami nitajenga upya
nyumba ya Daudi iliyoanguka. Nitajenga tena magofu
yake na kuisimamisha, 17 ili wanadamu wengine wote
wapate kumtafuta Mwenyezi Mungu, hata wale watu
wa Mataifa wote ambao wanaitwa kwa Jina langu,
asema Mwenyezi Mungu, anayefanya mambo haya,’
18 ambayo yamejulikana tangu zamani. **(aiōn g165)** 19
“Kwa hivyo uamuzi wangu ni kwamba, tusiwataabishe
watu wa Mataifa wanaomgeukia Mungu. 20 Badala
yake, tuwaandikie kwamba wajiepushe na vyakula
vilivyonajisiwa kwa kutolewa sanamu, wajiepushe na
uasherati, au kula mnyama aliyenyongwa, na damu.
21 Kwa maana katika kila mji kwa vizazi vilivyopita,
Musa amekuwa na wale wanaotangaza sheria yake
kwa kuwa imekuwa ikisomwa kwa sauti kubwa katika
masinagogi kila Sabato.” 22 Mitume na wazee, pamoja
na kundi la waumini wote, wakaamua kuwachagua
baadhi ya watu wao na kuwatuma Antiokia pamoja
na Paulo na Barnaba. Wakamchagua Yuda aitwaye
Barsaba, pamoja na Sila, watu wawili waliokuwa
viongozi miongoni mwa ndugu. 23 Wakatumwa na
barua ifuatayo: Sisi mitume na wazee, ndugu zenu.
Kwa waumini wa Mataifa mlio Antiokia, Siria na
Kilikia. Salamu. 24 Tumesikia kwamba kuna baadhi
ya watu waliokuja huko kutoka kwetu bila ruhusa yetu
na kuwasumbua, wakiyataabisha mawazo yenu. 25
Hivyo tumekubaliana wote kuwachagua baadhi ya
watu na kuwatuma kwenu pamoja na wapendwa wetu
Barnaba na Paulo, 26 watu ambao wamehatarisha
maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Isa
Al-Masihi. 27 Kwa hiyo tunawatuma Yuda na Sila,
kuthibitisha kwa maneno ya mdomo mambo haya
tunayowaandikia. 28 Kwa maana imempendeza
Roho wa Mungu na sisi tusiwatwike mzigo wowote
mkubwa zaidi ya mambo haya yafuatayo ambayo
ni ya lazima: 29 Kwamba mjiepushe na vyakula
vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, au
kula nyama ya mnyama aliyenyongwa, na mjiepushe
na uasherati. Mkiyaepuka mambo haya, mtakuwa
mmefanya vyema. Kwaherini. 30 Hivyo wakaagwa,
wakashuka kwenda Antiokia. Baada ya kulikusanya
kundi la waumini pamoja, wakawapa ile barua. 31
Baada ya hao watu kuisoma, wakafurahishwa sana
kwa ujumbe wake wa kutia moyo. 32 Yuda na
Sila, ambao wenyewe walikuwa manabii, wakanena
maneno mengi ya kuwatia moyo na kuwajenga
waumini katika imani. 33 Baada ya kukaa huko Antiokia
kwa muda, wakaagwa kwa amani na wale ndugu ili
waende kwa wale waliowatuma. [ 34 Lakini Sila bado
akaendelea kukaa huko.] 35 Lakini Paulo na Barnaba
walibaki Antiokia ambako wao pamoja na wengine
wengi walifundisha na kuhubiri neno la Bwana Isa. 36
Baada ya muda, Paulo akamwambia Barnaba, “Turudi
tukawatembelee ndugu katika miji yote tuliyohubiri
neno la Bwana Isa tuone jinsi wanavyoendelea.” 37
Barnaba alitaka wamchukue Yohana aitwaye Marko
waende naye. 38 Lakini Paulo aliona si vyema kwa
sababu aliwahi kuwaacha walipokuwa huko Pamfilia,
hakutaka kuendelea kufanya kazi naye. 39 Pakatokea
ubishi mkali kati ya Paulo na Barnaba kuhusu jambo
hili, hivyo wakagawanyika. Barnaba akamchukua
Yohana Marko wakasafiri baharini kwenda Kipro. 40
Lakini Paulo akamchagua Sila na akaondoka baada
ya ndugu kuwatakia neema ya Bwana Isa. 41 Akapitia
Siria na Kilikia, akiimarisha makundi ya waumini ya
huko.

**16** Paulo akafika Derbe na kisha Listra, ambako
kulikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake
Timotheo, ambaye mama yake alikuwa Myahudi
aliyeamini, lakini baba yake alikuwa Myunani. **2**
Alikuwa amesifiwa sana na wale ndugu waliokuwa
wameamini huko Listra na Ikonio **3** Paulo alitaka
Timotheo aandamane naye, hivyo akamtahiri kwa
sababu ya Wayahudi walioishi eneo lile, kwa maana
wote walimjua baba yake ni Myunani. **4** Walipokuwa
wakienda mji kwa mji, wakawa wanawapa maamuzi
yaliyotolewa na mitume na wazee huko Yerusalemu ili
wayafuate. **5** Hivyo makundi ya waumini yakaimarika
katika imani, na wakaongezeka kwa idadi kila siku.
**6** Paulo pamoja na wenzake wakasafiri sehemu
za Frigia na Galatia, kwa kuwa Roho wa Mungu
hakuwaruhusu kulihubiri neno huko jimbo la Asia.
**7** Walipofika mpaka wa Misia, wakajaribu kuingia
Bithinia lakini Roho wa Isa hakuwaruhusu. **8** Kwa hiyo
wakapita Misia, wakafika Troa. **9** Wakati wa usiku
Paulo akaona maono, mtu wa Makedonia amesimama
akimsihi, “Vuka uje huku Makedonia utusaidie.” **10**
Baada ya Paulo kuona maono haya, tulijiandaa
kwa haraka kuondoka kwenda Makedonia tukiwa
tumesadiki kuwa Mungu alikuwa ametuita kuhubiri
Injili huko. **11** Tukasafiri kwa meli kutoka Troa na
kwenda moja kwa moja hadi Samothrake, na kesho
yake tukafika Neapoli. **12** Kutoka huko tukasafiri hadi
Filipi, mji mkuu wa jimbo hilo la Makedonia, uliokuwa
koloni ya Warumi. Nasi tukakaa huko siku kadhaa. **13**
Siku ya Sabato tukaenda nje ya lango la mji kando
ya mto, ambapo tulitarajia kupata mahali pa kufanyia
maombi. Tukaketi, tukaanza kuongea na baadhi
ya wanawake waliokuwa wamekusanyika huko. **14**
Mmoja wa wale wanawake waliotusikiliza aliitwa
Lidia, mfanyabiashara wa nguo za zambarau, raia wa
mji wa Thiatira, aliyekuwa mcha Mungu. Mwenyezi
Mungu akaufungua moyo wake akaupokea ujumbe
wa Paulo. **15** Basi alipokwisha kubatizwa yeye na watu
wa nyumba yake, alitukaribisha nyumbani mwake,
akisema, “Kama mmeona kweli mimi nimemwamini
Bwana Isa, karibuni mkae nyumbani mwangu.” Naye
akatushawishi. **16** Siku moja, tulipokuwa tukienda
mahali pa kusali, tulikutana na mjakazi aliyekuwa na
pepo wa uaguzi. Naye alikuwa amewapa mabwana
zake mapato makubwa ya fedha kwa ubashiri. **17**
Huyu mjakazi alikuwa akimfuata Paulo na sisi akipaza
sauti na kusema, “Watu hawa ni watumishi wa
Mungu Aliye Juu Sana, wao wanawatangazieni njia
ya wokovu.” **18** Akaendelea kufanya hivi kwa siku
nyingi, lakini Paulo akiwa ameudhika sana, akageuka
na kumwambia yule pepo mchafu, “Ninakuamuru
katika jina la Isa Al-Masihi, umtoke!” Yule pepo
mchafu akamtoka mara hiyo. **19** Basi mabwana
wa yule mjakazi walipoona kuwa tumaini lao la
kuendelea kujipatia fedha limetoweka, wakawakamata
Paulo na Sila wakawaburuta hadi sokoni mbele ya
viongozi wa mji. **20** Baada ya kuwafikisha mbele
ya mahakimu wakawashtaki wakisema, “Hawa watu
wanaleta ghasia katika mji wetu, nao ni Wayahudi.
**21** Wanafundisha desturi ambazo sisi raia wa Rumi
hatuwezi kuzikubali au kuzitimiza.” **22** Umati wa
watu wakajiunga kuwashambulia Paulo na Sila, na
wale mahakimu wakaamuru wavuliwe nguo zao na
wapigwe mijeledi. **23** Baada ya kuwapiga sana,
wakawatupa gerezani na kumwagiza mkuu wa gereza
awalinde kikamilifu. **24** Kufuata maelekezo haya,
yule mkuu wa gereza akawaweka katika chumba
cha ndani sana mle gerezani, na akawafunga miguu
yao kwa minyororo. **25** Ilipokaribia usiku wa manane,
Paulo na Sila walikuwa wakiomba na kuimba nyimbo
za kumsifu Mungu, nao wafungwa wengine walikuwa
wakiwasikiliza. **26** Ghafula pakatokea tetemeko kubwa
la ardhi, hata msingi wa gereza ukatikisika. Mara
milango ya gereza ikafunguka na ile minyororo
iliyowafunga kila mmoja ikafunguka. **27** Yule mkuu
wa gereza alipoamka na kuona milango ya gereza
iko wazi, akachomoa upanga wake akataka kujiua,
akidhani ya kuwa wafungwa wote wametoroka. **28**
Lakini Paulo akapaza sauti kwa nguvu, akisema,
“Usijidhuru kwa maana sisi sote tuko hapa!” **29** Yule
askari wa gereza akaagiza taa ziletwe, akaingia
ndani ya kile chumba cha gereza, akapiga magoti
akitetemeka mbele ya Paulo na Sila. **30** Kisha
akawaleta nje akisema, “Bwana zangu, nifanye nini
nipate kuokoka?” **31** Wakamjibu, “Mwamini Bwana
Isa Al-Masihi, nawe utaokoka, pamoja na watu
wa nyumbani mwako.” **32** Wakamwambia neno
la Bwana Isa, yeye pamoja na wote waliokuwa
nyumbani mwake. **33** Wakati ule ule, yule mkuu wa
gereza akawachukua, akawaosha majeraha yao,
kisha akabatizwa yeye pamoja na wote waliokuwa
nyumbani mwake bila kuchelewa. **34** Akawapandisha

nyumbani mwake akawaandalia chakula, yeye pamoja na nyumba yake yote wakafurahi sana kwa kuwa sasa walikuwa wamemwamini Mungu. **35** Kulipopambazuka wale mahakimu wakawatuma maafisa wao kwa mkuu wa gereza wakiwa na agizo linalosema, “Wafungue wale watu, waachie waende zao.” **36** Mkuu wa gereza akamwambia Paulo “Mahakimu wameagiza niwaachie huru, kwa hiyo tokeni na mwende zenu kwa amani.” **37** Lakini Paulo akawaambia wale maafisa, “Wametupiga hadharani bila kutufanyia mashtaka na kutuhoji, nao wakatutupa gerezani, hata ingawa sisi ni raia wa Rumi. Nao sasa wanataka kututoa gerezani kwa siri? Hapana! Wao na waje wenyewe watutoe humu gerezani.” **38** Wale maafisa wakarudi na kuwaambia wale mahakimu maneno haya, wakaogopa sana walipofahamu kuwa Paulo na Sila ni raia wa Rumi. **39** Kwa hiyo wakaja wakawaomba msamaha, wakawatoa gerezani, wakawaomba waondoke katika ule mji. **40** Baada ya Paulo na Sila kutoka gerezani walienda nyumbani mwa Lidia, ambapo walikutana na waumini, wakawatia moyo, ndipo wakaondoka.

# 17

Wakasafiri kupitia Amfipoli na Apolonia wakafika Thesalonike, ambako kulikuwa na sinagogi la Wayahudi. **2** Kama ilivyokuwa desturi yake, Paulo aliingia ndani ya sinagogi, na kwa muda wa Sabato tatu akawa anahojiana nao kutoka kwa Maandiko, **3** akidhihirisha wazi na kuthibitisha kwamba ilikuwa lazima Al-Masihi ateswe na afufuke kutoka kwa wafu. Akasema, “Huyu Isa ninayewaambia habari zake, ndiye Al-Masihi.” **4** Baadhi ya Wayahudi wakasadiki, wakaungana na Paulo na Sila, wakiwepo idadi kubwa ya Wayunani waliomcha Mungu na wanawake wengi mashuhuri. **5** Lakini Wayahudi ambao hawakuwa wameamini wakawa na wivu, wakawakodi watu waovu kutoka sokoni, wakakutanisha umati wa watu, wakaanzisha ghasia mjini. Wakaenda mbio nyumbani mwa Yasoni wakiwatafuta Paulo na Sila ili kuwaleta nje penye umati ule wa watu. **6** Lakini walipowakosa wakamburuta Yasoni na ndugu wengine mbele ya maafisa wa mji, wakipaza sauti na kusema: “Watu hawa walioupindua ulimwengu wamekuja huku, **7** naye Yasoni amewakaribisha nyumbani mwake. Hawa wote wanaasi amri za Kaisari wakisema yuko mfalme mwingine aitwaye Isa.” **8** Waliposikia haya, umati ule wa watu na maafisa wa mji wakaongeza ghasia. **9** Nao baada ya kuchukua dhamana kwa ajili ya Yasoni na wenzake wakawaachia waende zao. **10** Usiku ule ule, wale ndugu wakawapeleka Paulo na Sila waende zao Beroya. Walipowasili huko wakaenda kwenye sinagogi la Wayahudi. **11** Hawa Waberoya walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa waliupokea ule ujumbe kwa shauku kubwa na kuyachunguza Maandiko kila siku ili kuona kama yale Paulo aliyosema yalikuwa kweli. **12** Wayahudi wengi wakaamini pamoja na wanawake na wanaume Wayunani wa tabaka la juu. **13** Lakini wale Wayahudi wa Thesalonike waliposikia kuwa Paulo anahubiri neno la Mungu huko Beroya, wakaenda huko ili kuwashawishi watu na kuwachochea. **14** Mara hiyo, wale ndugu wakamsafirisha Paulo hadi pwani, lakini Sila na Timotheo wakabaki Beroya. **15** Wale waliomsindikiza Paulo wakaenda naye hadi Athene, kisha wakarudi Beroya wakiwa na maagizo kutoka kwa Paulo kuhusu Sila na Timotheo kwamba wamfuate upesi iwezekanavyo. **16** Paulo alipokuwa akiwasubiri huko Athene, alisumbuka sana moyoni mwake kuona vile mji huo ulivyojaa sanamu. **17** Hivyo akahojiana kwenye sinagogi na Wayahudi pamoja na Wayunani waliomcha Mungu, na pia sokoni kila siku na watu aliopatana nao huko. **18** Kundi la wenye falsafa, Waepikureo na Wastoiko, wakajibizana naye. Baadhi yao wakasema, “Je, huyu mpayukaji anajaribu kusema nini?” Wengine wakasema, “Inaonekana anasema habari za miungu ya kigeni.” Walisema haya kwa sababu Paulo alikuwa anahubiri Injili kuhusu Isa na ufufuo wa wafu. **19** Hivyo wakamchukua na kumleta kwenye mkutano wa Areopago, walikomwambia, “Je, tunaweza kujua mafundisho haya mapya unayofundisha ni nini? **20** Wewe unaleta mambo mapya masikioni mwetu, hivyo tungetaka kujua maana yake ni nini.” **21** (Waathene na wageni wote walioishi humo hawakutumia muda wao kufanya chochote kingine isipokuwa kueleza au kusikia mambo mapya.) **22** Ndipo Paulo akasimama katikati ya mkutano wa Areopago, akasema, “Enyi watu wa Athene! Ninaona kwamba katika kila jambo ninyi ni watu wa dini sana. **23** Kwa kuwa nilipokuwa nikitembea mjini na kuangalia kwa makini vitu vyenu vya kuabudiwa, niliona huko madhabahu moja iliyoandikwa: Kwa Mungu Asiyejulikana. Basi sasa kile ambacho mmekuwa mkikiabudu kama kisichojulikana, ndicho ninachowahubiria. **24** “Mungu aliyeumba dunia

na vyote vilivyomo, ndiye Bwana wa mbingu na nchi;
hakai katika mahekalu yaliyojengwa kwa mikono
ya wanadamu. 25 Wala hatumikiwi na mikono ya
wanadamu kana kwamba anahitaji chochote, kwa
sababu yeye mwenyewe ndiye awapaye watu wote
uhai na pumzi na vitu vyote. 26 Kutoka kwa mtu
mmoja, yeye aliumba mataifa yote ya wanadamu ili
waikalie dunia yote, naye akaweka nyakati za kuishi.
27 Mungu alifanya hivyo ili wanadamu wamtafute na
huenda wakamfikia ingawa kwa kupapasapapasa
ijapokuwa kwa kweli hakai mbali na kila mmoja wetu.
28 'Kwa kuwa ndani yake tunaishi, tunatembea na
kuwa na uzima wetu.' Kama baadhi ya watunga
mashairi wenu walivyosema, 'Sisi ni uzao wake.' 29
"Kwa kuwa sisi ni uzao wa Mungu, haitupasi kudhani
kuwa uungu ni kama sanamu ya dhahabu au ya fedha
au ya jiwe, mfano uliotengenezwa kwa ubunifu na
ustadi wa mwanadamu. 30 Zamani wakati wa ujinga,
Mungu alijifanya kama haoni, lakini sasa anawaamuru
watu wote kila mahali watubu. 31 Kwa kuwa ameweka
siku ambayo atauhukumu ulimwengu kwa haki
akimtumia mtu aliyemchagua. Amewahakikishia watu
wote mambo haya kwa kumfufua Al-Masihi kutoka
kwa wafu." 32 Waliposikia habari za ufufuo wa wafu,
baadhi yao wakadhihaki, lakini wengine wakasema,
"Tunataka kukusikia tena ukizungumza juu ya jambo
hili." 33 Kwa hiyo Paulo akaondoka katikati yao. 34
Lakini baadhi yao wakaungana naye wakaamini. Kati
yao walikuwemo Dionisio, mmoja wa mkutano wa
Areopago, na mwanamke mmoja aliyeitwa Damari,
na wengine wengi.

**18** Baada ya haya, Paulo akaondoka Athene
akaenda Korintho. 2 Huko akakutana na
Myahudi mmoja jina lake Akila, mzawa wa Ponto,
aliyekuwa amewasili karibuni kutoka Italia pamoja na
mkewe Prisila, kwa sababu Klaudio alikuwa ameamuru
Wayahudi wote waondoke Rumi. Paulo akaenda
kuwaona, 3 naye kwa kuwa alikuwa mtengeneza
mahema kama wao, akakaa na kufanya kazi pamoja
nao. 4 Kila Sabato Paulo alikuwa akihojiana nao
katika sinagogi, akijitahidi kuwashawishi Wayahudi
na Wayunani. 5 Sila na Timotheo walipowasili
kutoka Makedonia, walimkuta Paulo akiwa amejitolea
muda wake wote katika kuhubiri, akiwashuhudia
Wayahudi kwamba Isa ndiye Al-Masihi. 6 Wayahudi
walipompinga Paulo na kukufuru, yeye aliyakung'uta
mavazi yake, akawaambia, "Damu yenu na iwe juu
ya vichwa vyenu! Mimi sina hatia, nimetimiza wajibu
wangu. Kuanzia sasa nitawaendea watu wa Mataifa."
7 Kisha akaondoka kwenye sinagogi, akaenda
nyumbani mwa Tito Yusto, aliyekuwa mcha Mungu;
nyumba yake ilikuwa karibu na sinagogi. 8 Kiongozi wa
hilo sinagogi, aliyeitwa Krispo, akamwamini Bwana,
yeye pamoja na watu wote wa nyumbani mwake. Nao
Wakorintho wengi waliomsikia Paulo pia wakaamini
na kubatizwa. 9 Usiku mmoja Bwana Isa akamwambia
Paulo katika maono, "Usiogope, lakini endelea kusema
wala usinyamaze, 10 kwa maana mimi niko pamoja
nawe, wala hakuna mtu atakayeweza kukushambulia
ili kukudhuru, kwa kuwa nina watu wengi katika mji
huu." 11 Hivyo Paulo akakaa huko kwa muda wa
mwaka mmoja na nusu, akiwafundisha Maandiko ya
Mungu. 12 Lakini wakati Galio alipokuwa msaidizi
wa mwakilishi wa mtawala huko Akaya, Wayahudi
waliungana kumshambulia Paulo, wakamkamata na
kumpeleka mahakamani. 13 Wakamshtaki wakisema,
"Mtu huyu anawashawishi watu wamwabudu Mungu
kinyume cha sheria." 14 Paulo alipotaka kujitetea,
Galio akawaambia Wayahudi, "Kama ninyi Wayahudi
mlikuwa mkilalamika kuhusu makosa makubwa ya
uhalifu ingekuwa haki kwangu kuwasikiliza. 15 Lakini
kwa kuwa linahusu maneno, majina na sheria yenu,
amueni ninyi wenyewe. Mimi sitakuwa mwamuzi wa
mambo haya." 16 Akawafukuza kutoka mahakamani.
17 Ndipo wote wakamkamata Sosthene kiongozi wa
sinagogi, wakampiga mbele ya mahakama, lakini
Galio hakujali kitendo chao hata kidogo. 18 Baada ya
kukaa Korintho kwa muda, Paulo akaagana na ndugu,
akasafiri kwa meli kwenda Siria akiwa amefuatana na
Prisila na Akila. Walipofika Kenkrea, Paulo alinyoa
nywele zake kwa kuwa alikuwa ameweka nadhiri. 19
Walipofika Efeso, Paulo aliwaacha Prisila na Akila
huko, lakini yeye akaingia kwenye sinagogi akawa
anajadiliana na Wayahudi. 20 Walipomwomba akae
nao kwa muda mrefu zaidi hakukubali. 21 Lakini
alipokuwa akiondoka, akaahidi, "Nitarudi kama Mungu
akipenda." Kisha akasafiri kwa meli kutoka Efeso.
22 Alitia nanga Kaisaria, akaenda Yerusalemu na
kuwasalimu waumini, kisha akaenda Antiokia. 23
Baada ya kukaa huko kwa muda, akaondoka na
kwenda sehemu moja hadi nyingine huko Galatia
na Frigia, akiwaimarisha wanafunzi wote. 24 Basi

akaja Efeso Myahudi aliyeitwa Apolo, mzawa wa
Iskanderia. Alikuwa na elimu kubwa, pia alikuwa na
ujuzi wa Maandiko. 25 Alikuwa amefundishwa katika
njia ya Bwana Isa, naye alikuwa na bidii katika roho,
akafundisha kwa usahihi kuhusu Isa, ingawa alijua
tu ubatizo wa Yahya. 26 Apolo alianza kunena kwa
ujasiri mkubwa katika sinagogi. Lakini Prisila na Akila
walipomsikia, walimwalika kwao na kumweleza njia
ya Mungu kwa ufasaha zaidi. 27 Naye Apolo alipotaka
kwenda Akaya, ndugu wa Efeso walimtia moyo,
wakawaandikia wanafunzi huko ili wamkaribishe.
Alipofika huko, aliwasaidia sana wale ambao, kwa
neema ya Mungu, walikuwa wameamini. 28 Kwa
uwezo mkubwa aliwakanusha hadharani Wayahudi
waliokuwa wakipinga, akithibitisha kwa Maandiko
kwamba Isa ndiye Al-Masihi.

**19** Apolo alipokuwa huko Korintho, Paulo alisafiri
sehemu za bara, akafika Efeso. Huko akawakuta
wanafunzi kadhaa, 2 akawauliza, “Je, mlipokea Roho
wa Mungu mlipoamini?” Wakajibu, “Hapana, hata
hatukusikia kuwa kuna Roho wa Mungu.” 3 Ndipo
Paulo akawauliza, “Je, mlibatizwa kwa ubatizo gani?”
Wakajibu, “Kwa ubatizo wa Yahya.” 4 Paulo akasema,
“Ubatizo wa Yahya ulikuwa wa toba, aliwaambia watu
wamwamini yeye atakayekuja baada yake, yaani Isa.”
5 Waliposikia haya, wakabatizwa katika jina la Bwana
Isa. 6 Paulo alipoweka mikono yake juu yao, Roho
Mtakatifu wa Mungu akawashukia, nao wakanena
kwa lugha mpya na kutabiri. 7 Walikuwa wapatao
wanaume kumi na wawili. 8 Paulo akaingia katika
sinagogi na kunena humo kwa ujasiri kwa muda wa
miezi mitatu, akijadiliana na watu na kuwashawishi
katika mambo ya ufalme wa Mungu. 9 Lakini baadhi
yao wakakaidi; walikataa kuamini, na wakakashifu
Njia Ile hadharani. Basi Paulo aliachana nao. Akaenda
na wanafunzi wale, akahojiana nao kila siku katika
darasa la Tirano. 10 Jambo hili likaendelea kwa
muda wa miaka miwili, kiasi kwamba Wayahudi
na Wayunani wote walioishi huko jimbo la Asia
wakawa wamesikia neno la Bwana Isa. 11 Mungu
akafanya miujiza mingi isiyo ya kawaida kupitia kwa
Paulo, 12 hivi kwamba leso au vitambaa vilivyokuwa
vimegusa mwili wa Paulo viliwekwa juu ya wagonjwa,
nao wakapona magonjwa yao, na pepo wachafu
wakawatoka. 13 Baadhi ya Wayahudi waliotangatanga
wakitoa pepo wachafu wakajaribu kutumia jina la
Bwana Isa kwa wale wenye pepo, wakisema, “Kwa
jina la Isa, yule anayehubiriwa na Paulo, nakuamuru
utoke.” 14 Wana saba wa Skewa, Myahudi aliyekuwa
kiongozi wa makuhani, walikuwa wanafanya hivyo.
15 Siku moja pepo mchafu akawajibu, “Isa namjua
na Paulo pia namjua, lakini ninyi ni nani?” 16 Kisha
yule mtu aliyekuwa na pepo mchafu akawarukia,
akawashambulia vikali, akawashinda nguvu wote,
wakatoka ndani ya ile nyumba wakikimbia wakiwa
uchi na wenye majeraha. 17 Habari hii ikajulikana kwa
Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu
ikawajaa wote, nalo jina la Bwana Isa likaheshimiwa
sana. 18 Wengi wa wale waliokuwa wameamini
wakati huu wakaja na kutubu waziwazi kuhusu
matendo yao maovu. 19 Idadi kubwa ya wale
waliofanya mambo ya uganga wakaleta vitabu vyao
na kuviteketeza kwa moto hadharani. Walipofanya
hesabu ya thamani ya vitabu vilivyoteketezwa ilikuwa
drakma elfu hamsini za fedha. 20 Hivyo neno la
Bwana Isa likaenea sana na kuwa na nguvu. 21
Baada ya mambo haya kutukia, Paulo akakusudia
rohoni kwenda Yerusalemu kupitia Makedonia na
Akaya. Akasema, “Baada ya kufika huko, yanipasa
pia kwenda Rumi.” 22 Hivyo akatuma wasaidizi wake
wawili, Timotheo na Erasto, waende Makedonia,
wakati yeye mwenyewe alibaki kwa muda kidogo
huko jimbo la Asia. 23 Wakati huo huo pakatokea dhiki
kubwa kwa sababu ya Njia Ile. 24 Mtu mmoja jina lake
Demetrio mfua fedha aliyekuwa akitengeneza vinyago
vya fedha vya Artemi na kuwapatia mafundi wake
biashara kubwa, 25 aliwaita pamoja watu wengine
waliofanya kazi ya ufundi kama yake na kusema,
“Enyi watu, mnajua ya kuwa utajiri wetu unatokana na
biashara hii! 26 Mnaona na kusikia jinsi huyu Paulo
amewashawishi na kuwapoteza watu wengi hapa
Efeso na karibu jimbo lote la Asia. Anasema kwamba
miungu iliyofanywa kwa mikono ya wanadamu si
miungu hata kidogo. 27 Kwa hiyo kuna hatari si kwa
kazi yetu kudharauliwa tu, bali pia hata hekalu la
mungu wa kike Artemi aliye mkuu, anayeabudiwa
jimbo lote la Asia na ulimwengu wote, litakuwa
limepokonywa fahari yake ya kiungu.” 28 Waliposikia
maneno haya, wakaghadhibika, wakaanza kupiga
kelele wakisema, “Artemi wa Waefeso ni mkuu!” 29
Mara mji wote ukajaa ghasia. Watu wakawakamata
Gayo na Aristarko, wenyeji wa Makedonia waliokuwa

wakisafiri na Paulo, wakakimbilia nao katika ukumbi wa maonesho. **30** Paulo akataka kuingia katikati ya umati, lakini wanafunzi hawakumruhusu. **31** Hata baadhi ya viongozi wa sehemu ile, waliokuwa rafiki zake Paulo, wakatuma watu wakitamani asiingie katika ule ukumbi wa maonesho. **32** Umati wa watu walikuwa na taharuki. Walikuwa wakipiga kelele, hawa wakisema hili na wengine lile. Idadi kubwa ya watu hawakujua hata ni kwa nini walikuwa wamekusanyika huko. **33** Wayahudi wakamsukumia Iskanda mbele na baadhi ya watu kwenye umati ule wakampa maelekezo. Akawaashiria kwa mkono ili watulie aweze kujitetea mbele ya watu. **34** Lakini walipotambua kwamba alikuwa Myahudi, wote wakapiga kelele kwa sauti moja kwa karibu muda wa saa mbili, wakisema, “Artemi wa Efeso ni mkuu!” **35** Baadaye karani wa mji akanyamazisha umati ule wa watu na kusema, “Enyi watu wa Efeso, je, ulimwengu wote haujui ya kuwa mji wa Efeso ndio unaotunza hekalu la Artemi aliye mkuu na ile sanamu yake iliyoanguka kutoka mbinguni? **36** Kwa hiyo, kwa kuwa mambo haya hayawezi kukanushwa, inawapasa mnyamaze na wala msifanye lolote kwa haraka. **37** Kwa kuwa mmewaleta hawa watu hapa, ingawa hawajaiba hekaluni wala kumkufuru huyu mungu wetu wa kike. **38** Basi, ikiwa Demetrio na mafundi wenzake wana mashtaka dhidi ya mtu yeyote, mahakama ziko wazi na wasaidizi wa mwakilishi wa mtawala. Wanaweza kufungua mashtaka. **39** Lakini kama kuna jambo jingine lolote zaidi mnalotaka kulileta, itabidi lisuluhishwe katika kusanyiko halali. **40** Kama ilivyo sasa, tuko hatarini kushtakiwa kwa kufanya ghasia kwa sababu ya tukio la leo. Kwa kuwa hakuna sababu tutakayoweza kutoa kuhalalisha msukosuko huu.” **41** Baada ya kusema haya akavunja mkutano.

**20** Baada ya zile ghasia kumalizika, Paulo aliwaita wanafunzi pamoja akawatia moyo, akawaaga, akaanza safari kwenda Makedonia. **2** Alipita katika sehemu zile, akinena na watu maneno mengi ya kuwatia moyo. Ndipo hatimaye akawasili Uyunani, **3** ambako alikaa kwa muda wa miezi mitatu. Kwa sababu baadhi ya Wayahudi walikuwa wamepanga njama dhidi yake alipokuwa karibu kusafiri kwa meli kwenda Siria, aliamua kurudi kupitia Makedonia. **4** Paulo aliandamana na Sopatro mwana wa Piro kutoka Beroya, Aristarko na Sekundo kutoka Thesalonike, na Gayo kutoka Derbe, pia Timotheo pamoja na Tikiko na Trofimo kutoka jimbo la Asia. **5** Hawa watu walitutangulia wakaenda kutungojea Troa. **6** Lakini sisi tukasafiri kwa meli kwa siku tano kutoka Filipi baada ya siku za Sikukuu ya Mikate Isiyotiwa Chachu, nasi tukaungana na wengine huko Troa, ambako tulikaa kwa siku saba. **7** Siku ya kwanza ya juma tulikutana pamoja kwa ajili ya kumega mkate. Paulo akaongea na watu, naye kwa kuwa alikuwa amekusudia kuondoka kesho yake, aliendelea kuongea hadi usiku wa manane. **8** Kwenye chumba cha ghorofani walimokuwa wamekutania kulikuwa na taa nyingi. **9** Kijana mmoja jina lake Eutiko, alikuwa amekaa dirishani, wakati Paulo alipokuwa akihubiri kwa muda mrefu, alipatwa na usingizi mzito, akaanguka kutoka ghorofa ya tatu, wakamchukua akiwa amekufa. **10** Paulo akashuka chini, akajitupa juu yake na kumkumbatia, akasema, “Msishtuke, bado yuko hai!” **11** Kisha Paulo akapanda tena ghorofani, akamega mkate na kula. Baada ya kuongea hadi mapambazuko, akaondoka. **12** Watu wakamrudisha yule kijana nyumbani akiwa hai nao wakafarijika sana. **13** Tukatangulia kwenye meli, tukasafiri kwenda Aso ambako tungemchukua Paulo. Alikuwa amefanya utaratibu huu kwa sababu alikuwa akienda huko kwa miguu. **14** Alipotukuta huko Aso, alijiunga nasi kwenye meli, tukasafiri hadi Mitilene. **15** Kutoka huko tuliendelea kwa meli, na kesho yake tukafika mahali panapokabili Kio. Siku iliyofuata tukavuka kwenda Samo, na kesho yake tukawasili Mileto. **16** Paulo alikuwa ameamua tusipitie Efeso ili asitumie muda mwingi huko jimbo la Asia. Alikuwa na haraka ya kufika Yerusalemu kabla ya siku ya Pentekoste kama ingewezekana. **17** Paulo akiwa Mileto, alituma mjumbe kwenda Efeso kuwaita wazee wa kundi la waumini waje wakutane naye. **18** Walipofika akawaambia, “Ninyi wenyewe mnajua jinsi nilivyoishi muda wote nilikuwa nanyi, tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa jimbo la Asia. **19** Nilimtumikia Bwana Isa kwa unyenyekevu wote na kwa machozi nikivumilia taabu na mapingamizi yaliyonipata kutokana na hila za Wayahudi. **20** Mnajua kwamba sikusita kuhubiri jambo lolote ambalo lingekuwa la kuwafaa ninyi, lakini nilifundisha hadharani na nyumba kwa nyumba. **21** Nimewashuhudia Wayahudi na Wayunani kwamba inawapasa kumgeukia Mungu kwa kutubu dhambi

na kumwamini Bwana wetu Isa Al-Masihi. 22 "Nami
sasa nimesukumwa na Roho wa Mungu, ninaenda
Yerusalemu wala sijui ni nini kitakachonipata huko.
23 Ila ninachojua tu ni kwamba Roho Mtakatifu
wa Mungu amenionya kuwa vifungo na mateso
vinaningoja. 24 Lakini siyahesabu maisha yangu kuwa
ya thamani kwangu, kama kuyamaliza mashindano na
kukamilisha ile kazi Bwana Isa aliyonipa, yaani kazi ya
kuishuhudia Injili ya neema ya Mungu. 25 "Nami sasa
najua kuwa hakuna hata mmoja miongoni mwenu
niliowahubiria ufalme wa Mungu atakayeniona tena.
26 Kwa hiyo nawatangazia leo, sina hatia ya damu
ya mtu yeyote. 27 Kwa kuwa sikusita kuwatangazia
mapenzi yote ya Mungu. 28 Jilindeni nafsi zenu
na mlilinde lile kundi lote ambalo Roho wa Mungu
amewaweka ninyi kuwa waangalizi wake. Chungeni
jumuiya ya waumini ya Mungu, aliowanunua kwa
damu yake mwenyewe. 29 Najua kwamba baada
yangu kuondoka, mbwa-mwitu wakali watakuja kati
yenu, ambao hawatalihurumia kundi. 30 Hata kutoka
miongoni mwenu watainuka watu na kuupotosha
ukweli ili wawavute wanafunzi wawafuate. 31 Hivyo
jilindeni! Kumbukeni kwamba kwa miaka mitatu
sikuacha kamwe kuwaonya kila mmoja kwa machozi
usiku na mchana. 32 "Sasa nawakabidhi kwa Mungu
na kwa neno la neema yake, linaloweza kuwajenga
na kuwapa ninyi urithi miongoni mwa wote ambao
wametakaswa. 33 Sikutamani fedha wala dhahabu
wala vazi la mtu yeyote. 34 Ninyi wenyewe mnajua
kwamba mikono yangu hii imetumika kwa mahitaji
yangu na ya wale waliokuwa pamoja nami. 35 Katika
kila jambo nimewaonesha kwamba kwa njia hii ya
kufanya kazi kwa bidii imetupasa kuwasaidia wadhaifu,
mkikumbuka maneno ya Bwana Isa mwenyewe jinsi
alivyosema, 'Ni heri kutoa kuliko kupokea.'" 36 Paulo
alipomaliza kusema haya akapiga magoti pamoja nao
wote akaomba. 37 Wote wakalia, wakamkumbatia
Paulo na kumbusu. 38 Kilichowahuzunisha zaidi ni
kwa sababu ya yale maneno aliyosema kwamba
kamwe hawatauona uso wake tena. Wakaenda naye
hadi kwenye meli.

**21** Tulipokwisha kujitenga nao, tukasafiri kwa meli
moja kwa moja hadi Kosi. Siku ya pili yake
tukafika Rodo, na kutoka huko tukaenda Patara. 2
Hapo tukapata meli iliyokuwa inavuka kwenda Foinike
tukapanda tukasafiri nayo. 3 Tulipokiona kisiwa cha
Kipro, tukakizunguka tukakiacha upande wetu wa
kushoto, tukasafiri hadi Siria. Tukatia nanga katika
bandari ya Tiro, ambapo meli yetu ilikuwa ipakue
shehena yake. 4 Baada ya kuwatafuta wanafunzi wa
huko, tukakaa nao kwa siku saba. Wale wanafunzi
wakiongozwa na Roho wa Mungu wakamwambia
Paulo asiende Yerusalemu. 5 Lakini muda wetu
ulipokwisha, tukaondoka tukaendelea na safari yetu.
Wale wanafunzi pamoja na wake zao na watoto
wakatusindikiza hadi nje ya mji. Wote tukapiga magoti
pale pwani tukaomba. 6 Baada ya kuagana, tukapanda
kwenye meli, nao wakarudi manyumbani mwao. 7
Tukaendelea na safari yetu toka Tiro tukafika Tolemai,
tukawasalimu ndugu wa huko, tukakaa nao kwa siku
moja. 8 Siku iliyofuata tukaondoka, tukafika Kaisaria.
Huko tukaenda nyumbani mwa mwinjilisti mmoja jina
lake Filipo, aliyekuwa mmoja wa wale Saba, tukakaa
kwake. 9 Filipo alikuwa na binti wanne mabikira
waliokuwa wanatoa unabii. 10 Baada ya kukaa
kwa siku kadhaa, nabii aliyeitwa Agabo akateremka
kutoka Yudea. 11 Alipotufikia, akachukua mshipi wa
Paulo, akajifunga, akautumia kufunga mikono na
miguu yake mwenyewe, akasema, "Roho wa Mungu
anasema: 'Hivi ndivyo viongozi wa Wayahudi huko
Yerusalemu watakavyomfunga mwenye mshipi huu
na kumkabidhi kwa watu wa Mataifa.'" 12 Tuliposikia
maneno haya sisi na ndugu wengine tukamsihi Paulo
asiende Yerusalemu. 13 Lakini Paulo akajibu, "Kwa
nini mnalia na kunivunja moyo? Mimi niko tayari
si kufungwa tu, bali hata kufa huko Yerusalemu
kwa ajili ya jina la Bwana Isa." 14 Alipokataa
kushawishika, tukaacha kumsihi, tukasema, "Mapenzi
ya Mwenyezi Mungu na yatendeke." 15 Baada ya
haya, tukajiandaa, tukaondoka kwenda Yerusalemu.
16 Baadhi ya wanafunzi kutoka Kaisaria wakafuatana
nasi na kutupeleka nyumbani mwa Mnasoni, ambaye
tungekaa kwake. Yeye alikuwa mtu wa Kipro, mmoja
wa wanafunzi wa zamani. 17 Tulipofika Yerusalemu,
ndugu wakatukaribisha kwa furaha. 18 Kesho yake
Paulo pamoja na wengine wetu tulienda kumwona
Yakobo, na wazee wote walikuwako. 19 Baada ya
kuwasalimu, Paulo akatoa taarifa kamili ya mambo
yote ambayo Mungu alikuwa amefanya miongoni
mwa watu wa Mataifa kupitia huduma yake. 20 Baada
ya kusikia mambo haya, wakamsifu Mungu. Ndipo
wakamwambia Paulo, "Ndugu, unaona kulivyo na

maelfu ya Wayahudi walioamini, nao wote wana juhudi
kwa ajili ya sheria. **21** Lakini wameambiwa habari
zako kwamba unafundisha Wayahudi wote wanaoishi
miongoni mwa watu wa Mataifa kumkataa Musa, na
kwamba unawaambia wasiwatahiri watoto wao wala
kufuata desturi zetu. **22** Sasa tufanyeje? Bila shaka
watasikia kwamba umekuja Yerusalemu. **23** Kwa hiyo
fanya lile tunalokuambia. Tuna watu wanne hapa
ambao wameweka nadhiri. **24** Jiunge na watu hawa,
mfanye utaratibu wa ibada ya kujitakasa pamoja nao,
na ulipe gharama ili wanyoe nywele zao. Kwa njia
hii kila mtu atafahamu ya kuwa mambo waliyosikia
si ya kweli na kwamba wewe unaishika sheria. **25**
Lakini kuhusu wale watu wa Mataifa walioamini,
tumewaandikia uamuzi wetu: kwamba wajitenge
na vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na
damu, au kula nyama ya mnyama aliyenyongwa, na
wajiepushe na uasherati." **26** Ndipo kesho yake Paulo
akaenda na wale watu, akajitakasa pamoja nao.
Akaingia ndani ya Hekalu ili atoe taarifa ya tarehe
ambayo siku zao za utakaso zingemalizika na sadaka
ingetolewa kwa ajili ya kila mmoja wao. **27** Zile siku
saba zilipokaribia kumalizika, baadhi ya Wayahudi
kutoka jimbo la Asia waliokuwa wamemwona Paulo
ndani ya Hekalu, wakachochea umati wote wa watu,
nao wakamkamata. **28** Wakapiga kelele wakisema,
"Waisraeli wenzetu, tusaidieni! Huyu ndiye yule mtu
anayefundisha kila mtu na kila mahali, kinyume na
watu wetu, sheria zetu na hata Hekalu hili. Zaidi
ya hayo amewaleta Wayunani ndani ya Hekalu na
kupanajisi mahali hapa patakatifu." **29** (Walikuwa
wamemwona Trofimo Mwefeso, akiwa mjini pamoja na
Paulo, wakadhani kuwa Paulo alikuwa amemwingiza
Hekaluni.) **30** Mji wote ukataharuki, watu wakaja
wakikimbia kutoka pande zote wakamkamata Paulo,
wakamburuta kutoka Hekaluni. Milango ya Hekalu
ikafungwa. **31** Walipokuwa wakitaka kumuua, habari
zikamfikia jemadari wa jeshi la askari Warumi kwamba
mji wa Yerusalemu wote ulikuwa katika machafuko.
**32** Mara yule jemadari akachukua maafisa wengine
wa jeshi pamoja na askari, wakakimbia kwenye ule
umati wa watu. Wale watu waliokuwa wakifanya
ghasia walipomwona yule jemadari na askari wakija,
wakaacha kumpiga Paulo. **33** Yule jemadari akaja,
akamkamata Paulo akaamuru afungwe kwa minyororo
miwili. Akauliza yeye ni nani, na alikuwa amefanya
nini. **34** Baadhi ya watu katika umati ule wakapiga
kelele, hawa wakisema hili na wengine lile. Yule
jemadari alipoona kuwa hawezi kupata hakika ya
habari kwa sababu ya taharuki, akaamuru Paulo
apelekwe katika ngome ya jeshi. **35** Paulo alipofika
penye ngazi, ilibidi askari wambebe juu juu kwa
sababu fujo za umati ule wa watu zilikuwa kubwa.
**36** Umati wa watu waliofuata waliendelea kupaza
sauti na kusema, "Mwondoe huyu!" **37** Mara tu
Paulo alipokaribia kuingizwa kwenye ngome ya jeshi,
akamwambia yule jemadari, "Je, naweza kukuambia
jambo moja?" Yule jemadari akamjibu, "Je, unajua
Kiyunani? **38** Je, wewe si yule Mmisri ambaye siku
hizi za karibuni alianzisha uasi akaongoza kundi
la magaidi elfu nne wenye silaha jangwani?" **39**
Paulo akajibu, "Mimi ni Myahudi kutoka Tarso huko
Kilikia, raia wa mji maarufu. Tafadhali niruhusu
nizungumze na hawa watu." **40** Baada ya kupata
ruhusa kwa yule jemadari, Paulo akasimama penye
ngazi, akawapungia watu mkono ili wanyamaze. Wote
waliponyamaza, Paulo akazungumza nao kwa lugha
ya Kiebrania, akasema:

**22** "Ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni utetezi
wangu." **2** Waliposikia akisema kwa lugha
ya Kiebrania, wakanyamaza kabisa. Ndipo Paulo
akasema, **3** "Mimi ni Myahudi, niliyezaliwa Tarso
huko Kilikia, lakini nimelelewa katika mji huu. Miguuni
mwa Gamalieli, nilifundishwa kikamilifu katika sheria
ya baba zetu, na nikawa mwenye juhudi kwa ajili
ya Mungu kama nyote mlivyo leo. **4** Niliwatesa
wafuasi wa Njia hii hadi kufa, nikiwakamata wanaume
na wanawake, na kuwatupa gerezani, **5** kama
kuhani mkuu na baraza zima la wazee wanavyoweza
kushuhudia kunihusu. Hata nilipokea barua kutoka
kwao kwenda kwa ndugu wale wa Dameski, nami
nikaenda huko ili kuwaleta watu hawa Yerusalemu
kama wafungwa ili waadhibiwe. **6** "Nilipokuwa njiani
kuelekea Dameski, yapata saa sita mchana, ghafula
nuru kubwa kutoka mbinguni ikanimulika kotekote. **7**
Nikaanguka chini, nikasikia sauti ikiniambia, 'Sauli!
Sauli! Mbona unanitesa?' **8** "Nikajibu, 'Wewe ni nani,
Bwana?' "Naye akaniambia, 'Mimi ni Isa Al-Nasiri
unayemtesa.' **9** Basi wale watu waliokuwa pamoja
nami waliiona ile nuru, lakini hawakuisikia sauti ya
yule aliyekuwa akisema nami. **10** "Nikauliza, 'Nifanye
nini, Bwana?' "Naye Bwana Isa akaniambia, 'Inuka

uingie Dameski, huko utaambiwa yote unayopaswa
kufanya.' **11** Kwa kuwa nilikuwa siwezi kuona kwa
ajili ya mng'ao wa ile nuru, wenzangu wakanishika
mkono wakaniongoza kuingia Dameski. **12** "Mtu
mmoja mcha Mungu, jina lake Anania, alikuja kuniona.
Alizishika sana sheria zetu, na aliheshimiwa sana na
Wayahudi walioishi huko Dameski. **13** Akasimama
karibu nami, akasema, 'Ndugu Sauli, pata kuona
tena!' Nami mara hiyo nikaweza kumwona. **14**
"Akasema, 'Mungu wa baba zetu amekuchagua wewe
ili ujue mapenzi yake, umwone yeye Aliye Mwenye
Haki na upate kusikia maneno kutoka kinywani
mwake. **15** Kwa kuwa utakuwa shahidi wake kwa
watu kuhusu kile ulichokiona na kukisikia. **16** Sasa
basi, mbona unakawia? Inuka, ukabatizwe na dhambi
zako zikasafishwe, ukiliita Jina lake.' **17** "Baada ya
kurudi Yerusalemu, nilipokuwa ninaomba Hekaluni,
nilipitiwa na usingizi wa ghafula, **18** nikamwona Bwana
Isa akiniambia, 'Harakisha utoke Yerusalemu upesi,
maana hawataukubali ushuhuda wako kunihusu.' **19**
"Nami nikasema, 'Bwana, wao wenyewe wanajua jinsi
nilivyoenda kwenye kila sinagogi ili kuwatupa gerezani
na kuwapiga wale waliokuamini. **20** Damu ya shahidi
wako Stefano ilipomwagwa, mimi mwenyewe nilikuwa
nimesimama kando, nikikubaliana na kitendo hicho na
kutunza mavazi ya wale waliomuua.' **21** "Ndipo Bwana
Isa akaniambia, 'Nenda, kwa maana nitakutuma
mbali, kwa watu wa Mataifa.'" **22** Umati ule wa watu
wakamsikiliza Paulo hadi aliposema neno hilo, ndipo
wakapaza sauti zao na kupiga kelele wakisema,
"Mwondoeni duniani, hafai kuishi!" **23** Walipokuwa
wakipiga kelele na kutoa mavazi yao huku wakirusha
mavumbi juu hewani, **24** yule jemadari akaamuru
Paulo aingizwe kwenye ngome. Akaelekeza kwamba
apigwe mijeledi na ahojiwe ili kujua kwa nini watu
walikuwa wanampigia kelele namna hiyo. **25** Lakini
walipokwisha kumfunga kwa kamba za ngozi ili
wampige mijeledi, Paulo akamwambia kiongozi wa
askari aliyekuwa amesimama pale karibu naye, "Je,
ni halali kwenu kwa mujibu wa sheria kumpiga mtu
ambaye ni raia wa Rumi hata kabla hajapatikana
na hatia?" **26** Yule kiongozi aliposikia maneno haya,
alimwendea yule jemadari na kumwambia, "Unataka
kufanya nini? Kwa maana huyu mtu ni raia wa Rumi."
**27** Yule jemadari akaja akamuuliza Paulo, "Niambie,
wewe ni raia wa Rumi?" Paulo akajibu, "Naam,
hakika." **28** Ndipo yule jemadari akasema, "Mimi
ilinigharimu kiasi kikubwa cha fedha kupata uraia
wangu." Paulo akasema "Lakini mimi ni raia wa Rumi
kwa kuzaliwa." **29** Mara wale waliokuwa wanataka
kumhoji wakajiondoa haraka, naye yule jemadari
akaingiwa na hofu alipotambua ya kuwa amemfunga
Paulo, ambaye ni raia wa Rumi, kwa minyororo. **30**
Kesho yake, kwa kuwa yule jemadari alitaka kujua
hakika kwa nini Paulo alikuwa anashutumiwa na
Wayahudi, alimfungua, na akawaagiza viongozi wa
makuhani na Baraza la Wayahudi lote likutane. Kisha
akamleta Paulo, akamsimamisha mbele yao.

**23** Paulo akawakazia macho wale wajumbe wa
Baraza la Wayahudi, akasema, "Ndugu zangu,
nimetimiza wajibu wangu kwa Mungu kwa dhamiri
safi kabisa hadi leo." **2** Kwa ajili ya jambo hili
kuhani mkuu Anania akaamuru wale waliokuwa
karibu na Paulo wampige kofi kinywani. **3** Ndipo
Paulo akamwambia, "Mungu atakupiga wewe, ewe
ukuta uliopakwa chokaa! Wewe umeketi hapo ili
kunihukumu kwa mujibu wa sheria, lakini wewe
mwenyewe unakiuka sheria kwa kuamuru kwamba
nipigwe kinyume cha sheria!" **4** Wale watu waliokuwa
wamesimama karibu na Paulo wakamwambia, "Je,
wewe wathubutu kumtukana kuhani mkuu wa Mungu?"
**5** Paulo akajibu, "Ndugu zangu, sikujua kwamba
yeye alikuwa kuhani mkuu. Kwa maana imeandikwa,
'Usimnenee mabaya kiongozi wa watu wako.'" **6**
Paulo alipotambua ya kuwa baadhi yao walikuwa
Masadukayo na wengine ni Mafarisayo, akapaza
sauti kwenye Baraza la Wayahudi, akasema, "Ndugu
zangu, mimi ni Farisayo, mwana Farisayo. Hapa
nimeshtakiwa kuhusu tumaini langu katika ufufuo
wa wafu." **7** Aliposema haya, kukazuka mabishano
kati ya Mafarisayo na Masadukayo, na baraza lote
likagawanyika. **8** (Kwa maana Masadukayo wanasema
kwamba hakuna ufufuo, wala hakuna malaika au
roho, lakini Mafarisayo wanaamini haya yote.) **9**
Kukawa na ghasia kubwa, nao baadhi ya walimu wa
Torati ambao ni Mafarisayo, wakasimama wakapinga
kwa nguvu wakisema, "Hatuoni kosa lolote la mtu
huyu! Huenda ikawa roho au malaika amezungumza
naye" **10** Ugomvi ukawa mkubwa kiasi kwamba yule
jemadari akahofu kuwa wangemrarua Paulo vipande
vipande, akaamuru vikosi vya askari vishuke na
kumwondoa Paulo katikati yao kwa nguvu na kumleta

ndani ya ngome ya jeshi. 11 Usiku uliofuata, Bwana
Isa akasimama karibu naye akamwambia, “Jipe
moyo! Kama vile ulivyonishuhudia hapa Yerusalemu,
hivyo imekupasa kunishuhudia huko Rumi pia.”
12 Kulipopambazuka Wayahudi wakapanga njama
pamoja na kujifunga kwa kiapo kwamba hawatakula
wala kunywa hadi wawe wamemuua Paulo. 13
Waliofanya mpango huo walikuwa zaidi ya watu
arobaini. 14 Wakaenda kwa viongozi wa makuhani na
wazee na kusema, “Tumeapa kwamba hatutakula
chochote hadi tuwe tumemuua Paulo. 15 Sasa basi,
wewe pamoja na Baraza la Wayahudi mwombeni
jemadari amlete Paulo mbele yenu kwa kisingizio
cha kutaka taarifa sahihi zaidi kuhusu kesi yake.
Nasi tuko tayari kumuua kabla hajafika hapa.” 16
Lakini mtoto wa dada yake Paulo aliposikia kuhusu
njama hiyo, alienda kule kwenye ngome ya askari na
kumweleza Paulo. 17 Ndipo Paulo akamwita mmoja
wa viongozi wa askari, akamwambia, “Mpeleke huyu
kijana kwa jemadari, ana jambo la kumweleza.” 18
Hivyo yule kiongozi wa askari akampeleka yule kijana
kwa jemadari, akamwambia, “Paulo yule mfungwa
aliniita na kuniomba nimlete huyu kijana kwako, kwa
sababu ana neno la kukueleza.” 19 Yule jemadari
akamshika yule kijana mkono, akampeleka kando na
kumuuliza, “Unataka kuniambia nini?” 20 Yule kijana
akasema, “Wayahudi wamekubaliana wakuombe
umpeleke Paulo kwenye Baraza la Wayahudi kesho
kwa kisingizio kwamba wanataka kufanya uchunguzi
wa kina kumhusu. 21 Lakini usishawishiwe nao kwa
maana zaidi ya watu arobaini wanamvizia. Wameapa
kwamba hawatakula wala kunywa hadi wamuue
Paulo. Sasa wako tayari, wanangoja idhini yako kwa
ombi lao.” 22 Yule jemadari akamruhusu yule kijana
aende na akamwonya, akisema, “Usimwambie mtu
yeyote kwamba umenieleza habari hizi.” 23 Kisha
yule jemadari akawaita viongozi wake wawili wa
askari akawaambia, “Jiandaeni kuondoka saa tatu
usiku huu kuelekea Kaisaria pamoja na askari mia
mbili, wapanda farasi sabini, na watu mia mbili wenye
mikuki. 24 Pia tayarisheni na farasi watakaotumiwa na
Paulo, mkampeleke salama kwa mtawala Feliksi.” 25
Kisha akaandika barua kwa Feliksi kama ifuatavyo: 26
Klaudio Lisia. Kwa Mtawala, Mtukufu Feliksi. Salamu.
27 Mtu huyu alikamatwa na Wayahudi wakakaribia
kumuua, lakini nikaja na vikosi vyangu vya askari
nikamwokoa, kwa kuwa nilipata habari kwamba
yeye ni raia wa Rumi. 28 Nilitaka kujua kwa nini
walikuwa wanamshutumu, hivyo nikamleta mbele
ya Baraza la Wayahudi. 29 Ndipo nikaona kuwa
alikuwa anashutumiwa kwa mambo yanayohusu
sheria yao, lakini hakuwa ameshtakiwa kwa jambo
lolote linalostahili kifo au kifungo. 30 Nilipoarifiwa
kuwa kulikuwa na njama dhidi ya mtu huyu, nilimtuma
kwako mara moja. Niliwaagiza washtaki wake pia
waeleze mashtaka yao dhidi yake mbele yako. 31
Hivyo askari, kwa kufuata maelekezo waliyopewa,
wakamchukua Paulo wakati wa usiku na kumleta
hadi Antipatri. 32 Kesho yake wakawaacha wale
wapanda farasi waendelee na safari wakiwa na Paulo,
wao wakarudi kwenye ngome ya askari. 33 Askari
walipofika Kaisaria, walimpa mtawala ile barua, na
kumkabidhi Paulo kwake. 34 Mtawala alipokwisha
kuisoma ile barua alimuuliza Paulo alikuwa mtu wa
jimbo gani. Alipojua kuwa anatoka Kilikia, 35 alisema,
“Nitasikiliza kesi yako washtaki wako watakapofika
hapa.” Kisha akaamuru Paulo awekwe chini ya ulinzi
kwenye jumba la kifalme la Herode.

**24** Baada ya siku tano, kuhani mkuu Anania
akateremka hadi Kaisaria pamoja na baadhi ya
wazee na mwanasheria aitwaye Tertulo, wakaleta
mashtaka yao dhidi ya Paulo mbele ya mtawala. 2
Paulo alipoitwa aingie ndani, Tertulo akaanza kutoa
mashtaka akisema, “Mtukufu Feliksi, kwa muda
mrefu tumefurahia amani na mabadiliko mengi mazuri
yamefanywa kwa ajili ya watu hawa kwa sababu ya
upeo wako wa kuona mambo ya mbele. 3 Wakati wote
na kila mahali, kwa namna yoyote, mtukufu Feliksi,
tumeyapokea mambo haya yote kwa shukrani nyingi.
4 Lakini nisije nikakuchosha zaidi, ningekuomba kwa
hisani yako utusikilize kwa kifupi. 5 “Tumemwona
mtu huyu kuwa ni msumbufu, anayechochea ghasia
miongoni mwa Wayahudi duniani pote. Yeye ndiye
kiongozi wa dhehebu la Wanasiri, 6 na hata amejaribu
kulinajisi Hekalu, hivyo tukamkamata. [Tukataka
kumhukumu kufuatana na sheria zetu. 7 Lakini
jemadari Lisia alitujia na nguvu nyingi, akamwondoa
mikononi mwetu, 8 akiwaamuru washtaki wake waje
mbele yako.] Kwa kumchunguza mwenyewe utaweza
kujua ukweli kuhusu mashtaka haya yote tunayoleta
dhidi yake.” 9 Pia wale Wayahudi wakaunga mkono
wakithibitisha kuwa mashtaka haya yote ni kweli. 10

Mtawala Feliksi alipompungia Paulo mkono ili ajitetee,
yeye akajibu, “Najua kwamba wewe umekuwa hakimu
katika taifa hili kwa miaka mingi, hivyo natoa utetezi
wangu kwa furaha. **11** Unaweza kuhakikisha kwa
urahisi kuwa hazijapita zaidi ya siku kumi na mbili
tangu nilipopanda kwenda Yerusalemu kuabudu.
**12** Hawa wanaonishtaki hawakunikuta nikibishana
na mtu yeyote Hekaluni au kuchochea umati wa
watu katika sinagogi au mahali pengine popote mjini.
**13** Wala hawawezi kabisa kukuthibitishia mashtaka
haya wanayoleta dhidi yangu. **14** Lakini ninakubali
kwamba mimi namwabudu Mungu wa baba zetu
kama mfuasi wa Njia Ile, ambayo wao wanaiita
dhehebu. Ninaamini kila kitu kinachokubaliana na
Torati na kile kilichoandikwa katika Manabii, **15**
nami ninalo tumaini kwa Mungu, ambalo hata wao
wenyewe wanalikubali kwamba kutakuwa na ufufuo
wa wafu, kwa wenye haki na wasio na haki. **16**
Kwa hiyo ninajitahidi siku zote kuwa na dhamiri
safi mbele za Mungu na mbele za wanadamu. **17**
“Basi, baada ya miaka mingi nilikuja Yerusalemu ili
kuwaletea watu wangu msaada kwa ajili ya maskini na
kutoa dhabihu. **18** Nilikuwa nimetakaswa waliponikuta
Hekaluni nikifanya mambo haya. Hapakuwa na umati
wa watu pamoja nami, wala sikuhusika katika ghasia
yoyote. **19** Lakini kuna Wayahudi fulani kutoka jimbo
la Asia ambao walipaswa kuwa hapa mbele yako
na kunishtaki kama wana jambo lolote dhidi yangu.
**20** Au, watu hawa walio hapa waseme ni kosa gani
walilonipata nalo waliponisimamisha mbele ya Baraza
la Wayahudi, **21** isipokuwa ni kuhusu jambo hili
moja nililopaza sauti mbele yao na kusema, ‘Mimi
nashtakiwa mbele yenu leo kwa sababu ya ufufuo
wa wafu.’” **22** Basi Feliksi, ambaye alifahamu vizuri
habari za Njia Ile, akaahirisha kesi ile, akasema,
“Jemadari Lisia atakapoteremka huku, nitaamua kesi
yenu.” **23** Ndipo akaamuru kiongozi wa askari amweke
chini ya ulinzi lakini ampe uhuru na kuwaruhusu
rafiki zake wamhudumie. **24** Baada ya siku kadhaa,
Feliksi alikuja pamoja na Drusila mkewe, aliyekuwa
Myahudi. Alituma aitiwe Paulo, naye akamsikiliza
alipokuwa akinena kuhusu imani katika Al-Masihi Isa.
**25** Naye Paulo alipokuwa akinena kuhusu haki, kuwa
na kiasi na kuhusu hukumu ijayo, Feliksi aliingiwa
na hofu, akasema, “Hiyo yatosha sasa! Unaweza
kuondoka. Nitakapokuwa na muda, nitakuita.” **26**
Wakati huo Feliksi alitazamia kwamba Paulo angempa
rushwa. Hivyo akawa anamwita mara kwa mara na
kuzungumza naye. **27** Baada ya miaka miwili kupita,
Porkio Festo akaingia kwenye utawala mahali pa
Feliksi, lakini kwa kuwa Feliksi alitaka kuwapendeza
Wayahudi, akamwacha Paulo gerezani.

**25** Siku tatu baada ya Festo kuwasili Kaisaria
kuchukua wajibu wake mpya, alipanda kwenda
Yerusalemu, **2** ambako viongozi wa makuhani na
viongozi wa Wayahudi walikuja mbele yake na kuleta
mashtaka yao dhidi ya Paulo. **3** Wakamsihi sana Festo,
kama upendeleo kwao, aamuru Paulo ahamishiwe
Yerusalemu, kwa kuwa walikuwa wanaandaa kumvizia
ili wamuue akiwa njiani. **4** Festo akawajibu, “Paulo
amezuiliwa huko Kaisaria, nami mwenyewe ninaenda
huko hivi karibuni. **5** Baadhi ya viongozi wenu
wafuatane nami na kutoa mashtaka dhidi ya mtu
huyo huko, kama amekosa jambo lolote.” **6** Baada
ya Festo kukaa miongoni mwao kwa karibu siku
nane au kumi, akashuka kwenda Kaisaria na siku
iliyofuata akaitisha mahakama, akaketi penye kiti
chake cha hukumu, akaamuru Paulo aletwe mbele
yake. **7** Paulo alipotokea, wale Wayahudi waliokuwa
wameteremka toka Yerusalemu wakasimama wakiwa
wamemzunguka, wakileta mashtaka mengi mazito
dhidi yake ambayo hawakuweza kuyathibitisha. **8**
Ndipo Paulo akajitetea, akasema, “Mimi sikufanya
jambo lolote kinyume cha sheria ya Wayahudi au dhidi
ya Hekalu au kinyume cha Kaisari.” **9** Festo, akitaka
kuwapendeza Wayahudi, akamuuliza Paulo, “Je,
ungependa kwenda Yerusalemu na kukabili mashtaka
mbele yangu huko?” **10** Paulo akasema, “Mimi
sasa nimesimama mbele ya mahakama ya Kaisari,
ambako ninastahili kushtakiwa. Kama vile wewe
mwenyewe unavyojua vyema kabisa sijawatendea
Wayahudi kosa lolote. **11** Basi kama mimi nina hatia
ya kutenda kosa lolote linalostahili kifo, sikatai kufa.
Lakini kama mashtaka yaliyoletwa dhidi yangu na
hawa Wayahudi si kweli, hakuna yeyote aliye na haki
ya kunikabidhi mikononi mwao. Naomba rufaa kwa
Kaisari!” **12** Baada ya Festo kufanya shauri pamoja na
baraza lake, akatangaza, “Wewe umeomba rufaa kwa
Kaisari, nako kwa Kaisari utaenda!” **13** Baada ya siku
kadhaa Mfalme Agripa na Bernike wakapanda kuja
Kaisaria kumsalimu Festo. **14** Kwa kuwa walikuwa
wakae huko Kaisaria kwa siku nyingi, Festo alijadili

kesi ya Paulo na mfalme, akisema, “Kuna mtu
mmoja hapa ambaye Feliksi alimwacha gerezani. 15
Nilipokuwa huko Yerusalemu, viongozi wa makuhani
na wazee wa Wayahudi walinijulisha habari zake
na wakaomba hukumu dhidi yake. 16 “Lakini mimi
nikawaambia kwamba si desturi ya Kirumi kumtoa
mtu yeyote auawe kabla mshtakiwa kuonana uso kwa
uso na washtaki wake, naye awe amepewa nafasi
ya kujitetea kuhusu mashtaka anayoshutumiwa. 17
Hivyo walipokutana hapa, sikukawia, kesho yake
niliitisha baraza, nikaketi kwenye kiti changu cha
hukumu, nikaagiza huyo mtu aletwe. 18 Washtaki
wake walipoinuka kuzungumza, hawakumshtaki kwa
uhalifu wowote kama nilivyotarajia. 19 Badala yake
walikuwa na vipengele fulani vya kutokukubaliana
naye kuhusu dini yao na kuhusu mtu aitwaye Isa
aliyekufa, lakini Paulo alidai kwamba yu hai. 20
Kwa kuwa sikujua jinsi ya kupeleleza jambo hili,
nilimuuliza kama angependa kwenda Yerusalemu
na kuhojiwa huko kuhusu mashtaka haya. 21
Lakini Paulo alipoomba afadhiliwe ili rufaa yake
isikilizwe na Mfalme Agusto, nilimwamuru alindwe
hadi nitakapoweza kumpeleka kwa Kaisari.” 22 Ndipo
Agripa akamwambia Festo, “Ningependa kumsikiliza
mtu huyo mimi mwenyewe.” Yeye akajibu, “Kesho
utamsikia.” 23 Siku iliyofuata Agripa na Bernike
walifika kwa fahari kubwa wakaingia katika ukumbi wa
mahakama, pamoja na majemadari wa jeshi na watu
mashuhuri wa mji. Ndipo Paulo akaletwa ndani kwa
amri ya Festo. 24 Festo akasema, “Mfalme Agripa,
nanyi nyote mlio hapa pamoja nasi, mnamwona mtu
huyu! Jumuiya yote ya Kiyahudi wamenilalamikia
kuhusu mtu huyu huko Yerusalemu na hapa Kaisaria,
wakipiga kelele kwamba hapaswi kuendelea kuishi. 25
Sikuona kwamba ametenda jambo lolote linalostahili
kifo, ila kwa kuwa alikuwa ameomba rufaa yake
kwa mfalme, niliamua kumpeleka Rumi. 26 Lakini
mimi sina kitu maalum cha kumwandikia Bwana
Mtukufu kumhusu mtu huyu. Hivyo basi, nimemleta
mbele yenu ninyi nyote, hasa mbele yako, Mfalme
Agripa, ili kutokana na matokeo ya uchunguzi huu,
niweze kupata kitu cha kuandika. 27 Kwa kuwa naona
hakuna sababu ya kumpeleka mfungwa bila kuainisha
mashtaka dhidi yake.”

**26** Ndipo Agripa akamwambia Paulo, “Una ruhusa
kujitetea.” Hivyo Paulo akawaashiria kwa mkono
wake, akaanza kujitetea, akasema: 2 “Mfalme Agripa,
najiona kuwa na heri kusimama mbele yako leo
ninapojitetea kuhusu mashtaka yote ya Wayahudi,
3 hasa kwa sababu unajua vyema desturi zote za
Kiyahudi na ya kuwa wewe unajua kwa undani
mila na masuala ya mabishano. Kwa hiyo, nakusihi
unisikilize kwa uvumilivu. 4 “Wayahudi wote wanajua
jinsi nilivyoishi tangu nilipokuwa mtoto, kuanzia
mwanzo wa maisha yangu katika nchi yangu na
pia huko Yerusalemu. 5 Wao wamenifahamu kwa
muda mrefu, na wanaweza kushuhudia wakipenda
kushuhudia, kwamba kutokana na misimamo mikali
sana ya dhehebu letu kwenye dini yetu, niliishi nikiwa
Farisayo. 6 Nami sasa ni kwa sababu ya tumaini
langu katika kile ambacho Mungu aliwaahidi baba
zetu, ninashtakiwa leo. 7 Hii ndiyo ahadi ambayo
makabila yetu kumi na mawili yanatarajia kuiona
ikitimizwa wanapomtumikia Mungu kwa bidii usiku na
mchana. Ee mfalme, ninashtakiwa na Wayahudi kwa
ajili ya tumaini hili. 8 Kwa nini yeyote miongoni mwenu
afikiri kwamba ni jambo lisilosadikika Mungu kufufua
wafu? 9 “Mimi pia nilikuwa nimeshawishika kwamba
imenipasa kufanya yote yale yaliyowezekana kupinga
Jina la Isa Al-Nasiri. 10 Nami hayo ndiyo niliyoyafanya
huko Yerusalemu. Kwa mamlaka ya viongozi wa
makuhani, niliwafunga watakatifu wengi gerezani, na
walipokuwa wakiuawa nilipiga kura yangu kuunga
mkono. 11 Mara nyingi nilienda kutoka sinagogi moja
hadi lingine nikiamuru waadhibiwe, nami nilijaribu
kuwalazimisha wakufuru. Katika shauku yangu dhidi
yao, hata nilienda miji ya kigeni ili kuwatesa. 12
“Siku moja nilipokuwa katika mojawapo ya safari
hizi nikiwa ninaenda Dameski, nilikuwa na mamlaka
na agizo kutoka kwa kiongozi wa makuhani. 13
Ilikuwa yapata adhuhuri, ee mfalme, nilipokuwa njiani,
niliona nuru kutoka mbinguni iliyong’aa kuliko jua,
ikatuangaza pande zote, mimi na wale niliokuwa
pamoja nao. 14 Wote tulianguka chini, nami nikasikia
sauti ikisema nami kwa lugha ya Kiebrania, ‘Sauli,
Sauli, mbona unanitesa? Ni vigumu kwako kuupiga
teke mchokoo.’ 15 “Nikauliza, ‘Ni nani wewe, Bwana?’
“Naye Bwana akajibu, ‘Ni mimi Isa unayemtesa. 16
Sasa inuka usimame kwa miguu yako. Nimekutokea
ili nikuteue uwe mtumishi na shahidi wa mambo
ambayo umeyaona, na yale nitakayokuonesha. 17
Nitakuokoa kutoka kwa watu wako na watu wa Mataifa

ambao ninakutuma kwao, 18 uyafumbue macho yao
ili wageuke kutoka gizani waingie nuruni, na kutoka
kwa nguvu za Shetani wamgeukie Mungu, ili wapate
msamaha wa dhambi na sehemu miongoni mwa
wale waliotakaswa kwa kuniamini mimi.’ 19 “Hivyo
basi, Mfalme Agripa, sikuacha kuyatii yale maono
yaliyotoka mbinguni, 20 bali niliyatangaza kwanza
kwa wale wa Dameski, kisha Yerusalemu na katika
vijiji vyote vya Yudea na pia kwa watu wa Mataifa,
kwamba inawapasa kutubu na kumgeukia Mungu
na kuthibitisha toba yao kwa matendo yao. 21 Ni
kwa sababu hii Wayahudi walinikamata nilipokuwa
Hekaluni, wakataka kuniua. 22 Hadi leo nimepata
msaada kutoka kwa Mungu, na hivyo nasimama
hapa nikishuhudia kwa wakubwa na wadogo. Sisemi
chochote zaidi ya yale ambayo manabii na Musa
walisema yatatukia: 23 kwamba Al-Masihi atateswa,
na kwamba yeye atakuwa wa kwanza kufufuka kutoka
kwa wafu, na atatangaza nuru kwa watu wake na kwa
watu wa Mataifa.” 24 Paulo alipokuwa akifanya utetezi
huu, Festo akasema kwa sauti kubwa, “Paulo, wewe
umerukwa na akili! Kusoma kwingi kunakufanya uwe
kichaa!” 25 Lakini Paulo akajibu, “Mimi sijarukwa na
akili, mtukufu sana Festo, bali nanena kweli nikiwa na
akili zangu timamu. 26 Naam, mfalme anajua kuhusu
mambo haya yote, nami nasema naye kwa uhuru. Kwa
sababu nina hakika kwamba hakuna hata mojawapo
ya mambo haya asilolijua, kwa kuwa hayakufanyika
mafichoni. 27 Mfalme Agripa, je, unaamini manabii?
Najua kuwa unaamini.” 28 Agripa akamwambia Paulo,
“Je, unanishawishi kwa haraka namna hii niwe mfuasi
wa Al-Masihi?” 29 Paulo akasema, “Ikiwa ni kwa
haraka au la, namwomba Mungu, si wewe peke yako
bali pia wale wote wanaonisikiliza leo, wawe kama
mimi nilivyo, kasoro minyororo hii.” 30 Baada ya
kusema hayo, mfalme akainuka pamoja na mtawala
na Bernike na wale waliokuwa wameketi pamoja nao.
31 Walipokuwa wakiondoka, wakaambiana, “Mtu huyu
hafanyi jambo lolote linalostahili kifo au kifungo.” 32
Agripa akamwambia Festo, “Mtu huyu angeachwa
huru kama hangekuwa amekata rufaa kwa Kaisari.”

**27** Ilipoamuliwa kwamba tungesafiri kwa meli
kwenda Italia, Paulo na wafungwa wengine
wakakabidhiwa kwa kiongozi mmoja wa askari
aliyeitwa Juliasi, aliyekuwa wa Kikosi cha Walinzi
wa Kaisari. 2 Tulipanda meli iliyotoka Adramitio,
iliyokuwa inakaribia kusafiri kwenda kwenye bandari
zilizopo pwani ya jimbo la Asia, tukaanza safari yetu
tukiwa pamoja na Aristarko, Mmakedonia kutoka
Thesalonike. 3 Kesho yake tukatia nanga Sidoni, naye
Juliasi akamfanyia wema Paulo, akamruhusu aende
kwa rafiki zake ili wamtimizie mahitaji yake. 4 Kutoka
huko tukaingia baharini tena na tukapita upande
wa chini wa kisiwa cha Kipro kwa sababu upepo
ulikuwa wa mbisho. 5 Baada ya sisi kuvuka bahari
iliyo upande wa Kilikia na Pamfilia, tukafika Mira huko
Likia. 6 Huko yule kiongozi wa askari akapata meli ya
Iskanderia ikielekea Italia, akatupandisha humo. 7
Tukasafiri polepole kwa siku nyingi na kwa shida,
hatimaye tukafika karibu na Nido. Kwa kuwa upepo
wa mbisho ulituzuia tusiweze kushika mwelekeo
tuliokusudia, tukapita chini ya Krete mkabala na
Salmone. 8 Tukaambaa na pwani kwa shida, tukafika
sehemu iitwayo Bandari Nzuri, karibu na mji wa
Lasea. 9 Muda mwingi ulikuwa umepotea, na kusafiri
baharini kulikuwa hatari, kwa sababu wakati huu
ulikuwa baada ya Siku ya Kufunga. Hivyo Paulo
akawaonya akasema, 10 “Mabwana, naona kuwa hii
safari ni yenye maafa na ya kuleta hasara kubwa
kwa meli na shehena, pia kwa maisha yetu.” 11
Lakini badala ya yule kiongozi wa askari kusikiliza
yale Paulo aliyosema, akafuata zaidi ushauri wa
nahodha na mwenye meli. 12 Kwa kuwa ile bandari
ilikuwa haifai kukaa wakati wa majira ya baridi, wengi
wakashauri kwamba tuendelee na safari wakitarajia
kufika Foinike na kukaa huko kwa majira ya baridi. Hii
ilikuwa bandari iliyo katika kisiwa cha Krete ikikabili
upande wa kusini-magharibi na kaskazini-magharibi.
13 Upepo mtulivu ulipoanza kuvuma toka kusini,
wakadhani kuwa wangeweza kufikia lengo lao, hivyo
wakang’oa nanga na kusafiri wakipita kandokando ya
pwani ya kisiwa cha Krete. 14 Lakini baada ya muda
mfupi, ikavuma tufani kubwa iitwayo Eurakilo kutoka
kisiwa cha Krete. 15 Meli ikapigwa na dhoruba na
haikuweza kushindana na ule upepo, tukarudishwa
baharini upepo ulikokuwa unaelekea. 16 Hatimaye
tukisafiri kupita chini ya kisiwa kidogo kiitwacho Kauda,
ambapo kwa kuwa tulikuwa tumekingiwa upepo na
hicho kisiwa, tuliweza kwa shida kuifunga mashua ya
kuokolea watu. 17 Watu walipokwisha kuivuta mashua
hiyo na kuiingiza katika meli, waliifunga kwa kamba
chini ya meli yenyewe ili kuzishikanisha pamoja.

Wakiogopa kupelekwa kwenye mchanga karibu na
pwani ya Sirti, wakashusha matanga wakaiacha meli
isukumwe na huo upepo. **18** Tulikuwa tunapigwa
na dhoruba kwa nguvu, kiasi kwamba kesho yake
walianza kutupa shehena toka kwenye meli. **19** Siku
ya tatu, wakatupa vyombo vya meli baharini kwa
mikono yao wenyewe. **20** Wakati jua wala nyota
hazikuonekana kwa siku nyingi, na dhoruba iliendelea
kuvuma, hatimaye tulikata tamaa ya kuokolewa. **21**
Baada ya watu kukaa siku nyingi bila kula chakula,
Paulo akasimama mbele yao na kusema: “Enyi watu,
kama mngekubali ushauri wangu wa kutosafiri kwa
meli kutoka Krete, basi mngejiepusha na uharibifu
na hasara hii. **22** Sasa ninawasihi sana, jipeni moyo
kwa kuwa hakuna hata mmoja wenu atakayepoteza
maisha yake, ila meli itaangamia. **23** Jana usiku,
malaika wa Mungu yule ambaye mimi ni wake
na ninayemwabudu alisimama karibu nami, **24**
akaniambia, ‘Paulo usiogope, kwa kuwa ni lazima
usimame mbele ya Kaisari, naye Mungu amekupa kwa
neema uhai wa wote wanaosafiri pamoja nawe.’ **25**
Hivyo jipeni moyo, enyi watu, kwa kuwa ninamwamini
Mungu kwamba yatakuwa kama vile alivyoniambia.
**26** Lakini hata hivyo meli yetu itakwama kwenye kisiwa
fulani.” **27** Usiku wa kumi na nne ulipofika, tulikuwa
bado tunasukumwa na upepo katika Bahari ya
Adria. Ilipokuwa yapata usiku wa manane, mabaharia
wakahisi kwamba walikuwa wanakaribia nchi kavu. **28**
Kwa hiyo wakapima kina cha maji na kukuta kilikuwa
pima ishirini; baada ya kuendelea mbele kidogo,
wakapima tena wakapata kina cha pima kumi na tano.
**29** Wakiogopa kwamba meli yetu ingegonga kwenye
miamba, wakashusha nanga nne za nyuma ya meli,
wakawa wanaomba kupambazuke. **30** Katika jaribio
la kutoroka kutoka kwa meli, mabaharia wakashusha
mashua ya kuokolea watu baharini, wakijifanya
kwamba wanaenda kushusha nanga za omo. **31** Ndipo
Paulo akamwambia yule jemadari na askari, “Hawa
watu wasipobaki katika meli, hamtaweza kuokoka.” **32**
Hivyo basi wale askari wakakata kamba zilizoshikilia
ile mashua ya kuokolea watu kwenye meli, wakaiacha
ianguke humo baharini. **33** Kabla ya mapambazuko,
Paulo akawasihi watu wote wale chakula akisema,
“Leo ni siku ya kumi na nne mmekuwa katika wasiwasi
mkiwa mmefunga na bila kula chochote. **34** Kwa
hiyo nawasihi mle chakula, kwa maana itawasaidia
ili mweze kuishi. Kwa kuwa hakuna hata mmoja
wenu atakayepoteza unywele hata mmoja kutoka
kichwani mwake.” **35** Baada ya kusema maneno
haya, Paulo akachukua mkate, akamshukuru Mungu
mbele yao wote, akaumega akaanza kula. **36** Ndipo
wote wakatiwa moyo, wakaanza kula chakula. **37**
Ndani ya meli tulikuwa jumla ya watu mia mbili
na sabini na sita. **38** Baada ya watu wote kula
chakula cha kutosha, wakapunguza uzito wa meli
kwa kutupa ngano baharini. **39** Kulipopambazuka,
mabaharia hawakuitambua ile nchi, lakini waliona
ghuba yenye ufuko wa mchanga, ambako waliamua
kuipweleza meli kama ingewezekana. **40** Kwa hiyo
wakatupa nanga zote na kuziacha baharini, na wakati
huo huo wakalegeza kamba zilizokuwa zikishikilia
usukani wa meli. Kisha wakatweka tanga la mbele
lishike upepo na kuisukuma meli kuelekea pwani.
**41** Lakini wakafika mahali bahari mbili zinakutana,
wakaipweleza meli ufuoni; omo ikakwama sana,
ikawa haiwezi kuondolewa; lakini sehemu ya shetri
ikavunjika vipande vipande kutokana na kupigwa kwa
mawimbi yenye nguvu. **42** Wale askari wakapanga
kuwaua wale wafungwa ili kuzuia hata mmoja wao
asiogelee na kutoroka. **43** Lakini yule jemadari
alitaka kuokoa maisha ya Paulo, basi akawazuia
askari wasitekeleze mpango wao. Akaamuru wale
wanaoweza kuogelea wajitupe baharini kwanza,
waogelee hadi nchi kavu. **44** Waliosalia wangefika
nchi kavu kwa kutumia mbao au vipande vya meli
iliyovunjika, hivyo wote wakafika nchi kavu salama.

**28** Baada ya kufika nchi kavu salama, ndipo
tukafahamu kwamba jina la kile kisiwa ni Malta.
**2** Wenyeji wa kile kisiwa walituonesha ukarimu usio
wa kawaida. Waliwasha moto na kutukaribisha sisi
sote kwa sababu mvua ilikuwa inanyesha na kulikuwa
na baridi. **3** Paulo alikusanya mzigo wa kuni, na
alipokuwa anaweka kuni kwenye moto, nyoka mwenye
sumu akatoka humo kwa ajili ya joto na kujisokotea
mkononi mwake. **4** Wale wenyeji wa kile kisiwa
walipomwona yule nyoka akining’inia mkononi mwa
Paulo, wakaambiana, “Huyu mtu lazima awe ni muuaji,
ingawa ameokoka kutoka baharini, haki haijamwacha
aishi.” **5** Lakini Paulo akamkung’utia yule nyoka ndani
ya moto wala yeye hakupata madhara yoyote. **6** Watu
walikuwa wanangoja avimbe au aanguke ghafula
na kufa. Lakini baada ya kungoja kwa muda mrefu

na kuona kwamba hakuna chochote kisicho cha
kawaida kilichomtokea, wakabadili mawazo yao na
kuanza kusema kwamba yeye ni mungu. 7 Basi
karibu na sehemu ile, palikuwa na shamba kubwa
la kiongozi mkuu wa kile kisiwa, aliyeitwa Publio.
Alitupokea kwake, na akatuhudumia kwa ukarimu
mkubwa kwa muda wa siku tatu. 8 Baba yake Publio
alikuwa mgonjwa kitandani, akiwa anaugua homa
na kuhara damu. Paulo akaingia ndani ili kumwona
na baada ya maombi, akaweka mikono juu yake
na kumponya. 9 Jambo hili lilipotukia, watu wote
wa kisiwa kile waliokuwa wagonjwa wakaja, nao
wakaponywa. 10 Wakatupatia heshima nyingi, nasi
tulipokuwa tayari kusafiri kwa meli, wakatupakilia
vitu vyote tulivyokuwa tunavihitaji. 11 Miezi mitatu
baadaye tukaanza safari kwa meli iliyokuwa imetia
nanga kwenye kisiwa hicho kwa ajili ya majira ya
baridi. Hii ilikuwa meli ya Iskanderia yenye alama ya
miungu pacha waitwao Kasta na Poluksi. 12 Kituo
chetu cha kwanza kilikuwa Sirakusa na tukakaa huko
siku tatu. 13 Kisha tukang'oa nanga, tukafika Regio.
Siku iliyofuata, upepo mkali wa kusi ukavuma, na
siku ya pili yake tukafika Puteoli. 14 Huko tukawakuta
ndugu, nasi tukakaribishwa tukae nao kwa siku
saba. Hivyo tukaendelea na safari hadi Rumi. 15
Ndugu wa huko Rumi waliposikia habari zetu, walikuja
hadi Soko la Apio na mahali paitwapo Mikahawa
Mitatu kutulaki. Paulo alipowaona, alimshukuru Mungu
akatiwa moyo. 16 Tulipofika Rumi, Paulo aliruhusiwa
kuishi peke yake akiwa na askari wa kumlinda. 17 Siku
tatu baadaye Paulo akawaita pamoja viongozi wa
Wayahudi. Walipokwisha kukusanyika akawaambia,
"Ndugu zangu, ingawa sikufanya jambo lolote dhidi
ya watu wetu au dhidi ya desturi za baba zetu, lakini
nilikamatwa huko Yerusalemu nikakabidhiwa kwa
Warumi. 18 Wao walipokwisha kunihoji, wakataka
kuniachia huru kwa sababu hawakuona kosa lolote
nililolifanya linalostahili adhabu ya kifo. 19 Lakini
Wayahudi walipopinga uamuzi huo, nililazimika
kukata rufaa kwa Kaisari, ingawa sikuwa na lalamiko
lolote juu ya taifa langu. 20 Basi hii ndiyo sababu
nimewatumania, ili niseme nanyi. Kwa kuwa ni kwa ajili
ya tumaini la Israeli nimefungwa kwa minyororo." 21
Wakamjibu, "Hatujapokea barua zozote kutoka Yudea
zinazokuhusu, wala hapana ndugu yeyote aliyekuja
hapa ambaye ametoa taarifa au kuzungumza jambo
lolote baya juu yako. 22 Lakini tungependa kusikia
kutoka kwako unalofikiri kwa sababu tunajua kwamba
kila mahali watu wanazungumza mabaya kuhusu
jamii hii." 23 Baada ya kupanga siku ya kuonana
naye, watu wengi wakaja kuanzia asubuhi hadi jioni
akawaeleza na kutangaza kuhusu ufalme wa Mungu
akijaribu kuwahadithia juu ya Isa kutoka Torati ya
Musa na kutoka Manabii. 24 Baadhi wakasadiki yale
aliyosema, lakini wengine hawakuamini. 25 Hivyo
hawakukubaliana, nao walipokuwa wanaondoka,
Paulo akatoa kauli moja zaidi: "Roho wa Mungu
alinena kweli na baba zenu aliposema mambo
yale yaliyomhusu Bwana Isa kwa kinywa cha nabii
Isaya kwamba: 26 "'Nenda kwa watu hawa na
useme, "Hakika mtasikiliza lakini hamtaelewa; na
pia mtatazama, lakini hamtaona." 27 Kwa kuwa
mioyo ya watu hawa imekuwa migumu; hawasikii
kwa masikio yao, na wamefumba macho yao. Wasije
wakaona kwa macho yao, na wakasikiliza kwa
masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, na kugeuka
nami nikawaponya.' 28 "Basi na ijulikane kwenu
kwamba, huu wokovu wa Mungu umepelekwa kwa
watu wa Mataifa, nao watasikiliza." [ 29 Baada
yake kusema maneno haya, Wayahudi wakaondoka
wakiwa na hoja nyingi miongoni mwao.] 30 Kwa
miaka miwili mizima Paulo alikaa huko kwa nyumba
aliyokuwa amepanga. Akawakaribisha wote walioenda
kumwona. 31 Akahubiri ufalme wa Mungu na
kufundisha mambo yale yaliyomhusu Bwana Isa Al-
Masihi, kwa ujasiri wote na bila kizuizi chochote.

# Warumi

**1** Paulo, mtumishi wa Al-Masihi Isa, aliyeitwa kuwa
mtume na kutengwa kwa ajili ya Injili ya Mungu, **2**
Injili ambayo Mungu alitangulia kuiahidi kwa vinywa
vya manabii wake katika Maandiko Matakatifu, **3**
yaani Injili inayomhusu Mwanawe, yeye ambaye kwa
uzao wa mwili alikuwa mzao wa Daudi, **4** na ambaye
kwa uwezo wa Roho wa utakatifu alidhihirishwa kuwa
Mwana wa Mungu kwa ufufuo wake kutoka kwa wafu,
yaani Isa Al-Masihi, Bwana wetu. **5** Kupitia kwake
tumepokea neema na utume ili kuwaita watu wote
wa mataifa waje kwenye utii utokanao na imani kwa
ajili ya jina lake. **6** Ninyi nyote pia mko miongoni
mwa watu walioitwa ili wapate kuwa mali ya Isa
Al-Masihi. **7** Kwa wote walio Rumi wanaopendwa
na Mungu na kuitwa kuwa watakatifu. **8** Kwanza
kabisa, namshukuru Mungu wangu kupitia kwa Isa
Al-Masihi kwa ajili yenu nyote, kwa sababu imani
yenu inatangazwa duniani kote. **9** Kwa maana
Mungu ninayemtumikia kwa moyo wangu wote katika
kuhubiri Injili ya Mwanawe, ni shahidi wangu jinsi
ninavyowakumbuka daima **10** katika maombi yangu
siku zote. Nami ninaomba kwamba hatimaye sasa
kwa mapenzi ya Mungu, njia ipate kufunguliwa kwa
ajili yangu ili nije kwenu. **11** Ninatamani sana kuwaona
ili nipate kuwapa karama za rohoni ili mwe imara,
**12** au zaidi, ninyi pamoja nami tuweze kutiana moyo
katika imani sisi kwa sisi. **13** Ndugu zangu, napenda
mfahamu kwamba mara nyingi nimekusudia kuja
kwenu (ingawa hadi sasa nimezuiliwa), ili nipate
kuvuna mavuno miongoni mwenu kama nilivyovuna
miongoni mwa watu wa Mataifa wengine. **14** Mimi ni
mdeni kwa Wayunani na kwa wasio Wayunani, kwa
wenye hekima na kwa wasio na hekima. **15** Ndiyo
sababu ninatamani sana kuihubiri Injili kwenu pia ninyi
mlioko Rumi. **16** Mimi siionei haya Injili, kwa maana ni
uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye,
kwanza kwa Myahudi na kwa Myunani pia. **17** Kwa
maana katika Injili haki ya Mungu imedhihirishwa,
haki ile iliyo ya imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa:
“Mwenye haki ataishi kwa imani.” **18** Ghadhabu ya
Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi
wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli
kwa uovu wao. **19** Kwa maana yote yanayoweza
kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa
sababu Mungu mwenyewe ameyadhihirisha kwao. **20**
Kwa maana tangu kuumbwa kwa ulimwengu, asili
ya Mungu asiyeonekana kwa macho, yaani uweza
wake wa milele na asili yake ya uungu, imeonekana
waziwazi, ikitambuliwa kutokana na yale aliyoyafanya
ili wanadamu wasiwe na udhuru. **(aïdios g126)** **21** Kwa
maana ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza
yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru, bali
fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga
ikatiwa giza. **22** Ingawa walijidai kuwa wenye hekima,
wakawa wajinga, **23** na kubadili utukufu wa Mungu
aishiye milele kwa sanamu zilizotengenezwa zifanane
na mwanadamu ambaye hufa, na mfano wa ndege,
wanyama na viumbe vinavyotambaa. **24** Kwa hiyo,
Mungu akawaacha wazifuate tamaa mbaya za mioyo
yao katika uasherati, hata wakaivunjia heshima miili
yao wao kwa wao. **25** Waliibadili kweli ya Mungu
kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe badala
ya Muumba, ahimidiwaye milele! Amen. **(aiōn g165)** **26**
Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha wazifuate tamaa
za aibu. Hata wanawake wao wakabadili mahusiano
ya kimwili ya asili kwa mahusiano yasiyokusudiwa.
**27** Vivyo hivyo wanaume pia wakaacha mahusiano
ya kimwili ya asili na wanawake, wakawakiana kwa
tamaa mbaya wao kwa wao. Wanaume wakafanya
matendo ya aibu na wanaume wengine, nao wakapata
adhabu waliyostahili kwa ajili ya upotovu wao. **28**
Nao kwa kuwa hawakuona umuhimu wa kudumisha
ufahamu wa Mungu, yeye akawaachilia wafuate
akili za upotovu, watende mambo yale yasiyostahili
kutendwa. **29** Wamejawa na udhalimu wa kila namna,
uasherati, uovu, tamaa mbaya na hila. Wamejawa
na husuda, uuaji, ugomvi, udanganyifu, hadaa na
nia mbaya. Wao pia ni wasengenyaji, **30** wasingiziaji,
wanaomchukia Mungu, wajeuri, wenye kiburi na
majivuno, wenye hila, wasiotii wazazi wao, **31** wajinga,
wasioamini, wasio na huruma na wakatili. **32** Ingawa
wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu
wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti,
si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia
wanakubaliana na wale wanaoyatenda.

**2** Kwa hiyo huna udhuru wowote, wewe utoaye
hukumu kwa mwingine, kwa maana katika
jambo lolote unalowahukumu wengine, unajihukumu
wewe mwenyewe kwa sababu wewe unayehukumu
unafanya mambo hayo hayo. **2** Basi tunajua kwamba

hukumu ya Mungu dhidi ya wale wafanyao mambo
kama hayo ni ya kweli. 3 Hivyo wewe mwanadamu,
unapotoa hukumu juu yao na bado unafanya mambo
yale yale, unadhani utaepuka hukumu ya Mungu?
4 Au waudharau wingi wa wema, ustahimili na
uvumilivu wake, bila kujua kuwa wema wa Mungu
wakuelekeza kwenye toba? 5 Lakini kwa sababu
ya ukaidi wenu na mioyo yenu isiyotaka kutubu,
mnajiwekea akiba ya ghadhabu dhidi yenu wenyewe
kwa siku ile ya ghadhabu ya Mungu, wakati hukumu
yake ya haki itakapodhihirishwa. 6 Kwa maana Mungu
atamlipa kila mtu kulingana na matendo yake. 7 Wale
ambao kwa kuvumilia katika kutenda mema hutafuta
utukufu, heshima na maisha yasiyoharibika, Mungu
atawapa uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 8 Lakini kwa
wale wanaotafuta mambo yao wenyewe na wale
wanaokataa kweli na kuzifuata njia mbaya, kutakuwa
na ghadhabu na hasira ya Mungu. 9 Kutakuwa na
taabu na dhiki kwa kila mmoja atendaye maovu,
Myahudi kwanza na mtu wa Mataifa pia, 10 bali
utukufu, heshima na amani kwa ajili ya kila mmoja
atendaye mema, kwa Myahudi kwanza, kisha kwa mtu
wa Mataifa. 11 Kwa maana Mungu hana upendeleo.
12 Watu wote waliotenda dhambi pasipo sheria
wataangamia pasipo sheria, nao wote waliotenda
dhambi chini ya sheria watahukumiwa kwa sheria.
13 Kwa maana si wale wanaoisikia sheria ambao ni
wenye haki mbele za Mungu, bali ni wale wanaoitii
sheria ndio watakaohesabiwa haki. 14 (Naam,
wakati wa watu wa Mataifa, ambao hawana sheria,
wanapofanya kwa asili mambo yatakiwayo na sheria,
wao ni sheria kwa nafsi zao wenyewe, hata ingawa
hawana sheria. 15 Wao wanaonesha kwamba lile
linalotakiwa na sheria limeandikwa kwenye mioyo yao,
ambayo pia dhamiri zao zikiwashuhudia, nayo mawazo
yao yenye kupingana yatawashtaki au kuwatetea.)
16 Hili litatukia siku hiyo Mungu atakapozihukumu
siri za wanadamu kupitia kwa Isa Al-Masihi, kama
isemavyo Injili yangu. 17 Tazama, wewe ukiwa unajiita
Myahudi na kuitegemea Torati na kujisifia uhusiano
wako na Mungu, 18 kama unajua mapenzi ya Mungu
na kukubali lililo bora kwa sababu umefundishwa
na hiyo Torati, 19 kama unatambua kuwa wewe
ni kiongozi wa vipofu, na mwanga kwa wale walio
gizani, 20 mkufunzi wa wajinga na mwalimu wa watoto
wachanga, kwa kuwa una maarifa ya kweli katika
hiyo Torati, 21 basi wewe, uwafundishaye wengine,
mbona hujifunzi mwenyewe? Wewe uhubiriye kwamba
mtu asiibe, wewe mwenyewe waiba? 22 Wewe
usemaye mtu asizini, wewe mwenyewe wazini? Wewe
uchukiaye miungu ya sanamu, wafanya jambo la
kumchukiza katika mahekalu? 23 Wewe ujivuniaye
Torati, wamwaibisha Mungu kwa kuvunja Torati? 24
Kama ilivyoandikwa, “Kwa ajili yenu ninyi, Jina la
Mungu linatukanwa miongoni mwa watu wa Mataifa.”
25 Kutahiriwa kuna thamani ikiwa unatii Torati, lakini
kama unavunja Torati, kutahiriwa kwako kumekuwa
kutokutahiriwa. 26 Hivyo, ikiwa wale wasiotahiriwa
wanatimiza mambo ambayo Torati inataka, je,
kutokutahiriwa kwao hakutahesabiwa kuwa sawa na
kutahiriwa? 27 Ndipo wale ambao hawakutahiriwa
kimwili lakini wanaitii Torati watawahukumu ninyi,
ambao ingawa mmetahiriwa na kuijua sana Torati ya
Mungu iliyoandikwa, lakini mwaivunja. 28 Kwa maana
mtu si Myahudi kwa vile alivyo kwa nje, wala tohara
ya kweli si kitu cha nje au cha kimwili. 29 Lakini mtu ni
Myahudi alivyo ndani, nayo tohara ya kweli ni jambo
la moyoni, ni la Roho wa Mungu, wala si la sheria
iliyoandikwa. Mtu kama huyo hapokei sifa kutoka kwa
wanadamu bali kwa Mungu.

**3** Basi kuna faida gani kuwa Myahudi? Au kuna
thamani gani katika tohara? 2 Kuna faida
kubwa kwa kila namna! Kwanza kabisa, Wayahudi
wamekabidhiwa maneno halisi ya Mungu. 3
Ingekuwaje kama wengine hawakuwa na imani?
Je, kutokuamini kwao kungebatilisha uaminifu wa
Mungu? 4 La hasha! Mungu na aonekane mwenye
haki, na kila mwanadamu kuwa mwongo, kama
ilivyoandikwa: “Ili uthibitike kuwa wa kweli unaponena,
na ukashinde unapotoa hukumu.” 5 Lakini ikiwa
uovu wetu unathibitisha haki ya Mungu waziwazi,
tuseme nini basi? Je, Mungu kuileta ghadhabu
yake juu yetu ni kwamba yeye si mwenye haki?
(Nanena kibinadamu.) 6 La hasha! Kama hivyo ndivyo
ilivyo, Mungu angewezaje kuhukumu ulimwengu? 7
Mtu aweza kuuliza, “Kama uongo wangu unasaidia
kuonesha kweli ya Mungu na kuzidisha utukufu
wake, kwa nini basi mimi nahukumiwa kuwa mwenye
dhambi?” 8 Nasi kwa nini tusiseme, kama wengine
wanavyotusingizia kuwa tunasema, “Tutende maovu ili
mema yapate kuja”? Wao wanastahili hukumu yao. 9
Tusemeje basi? Je, sisi ni bora kuliko wao? La hasha!

Kwa maana tumekwisha kuhakikisha kwa vyovyote
kwamba Wayahudi na watu wa Mataifa wote wako
chini ya nguvu ya dhambi. 10 Kama ilivyoandikwa:
“Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja. 11
Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata
mmoja amtafutaye Mungu. 12 Wote wamepotoka, wote
wameoza pamoja; hakuna atendaye mema, naam,
hakuna hata mmoja.” 13 “Makoo yao ni makaburi wazi;
kwa ndimi zao wao hufanya udanganyifu.” “Sumu
ya nyoka iko midomoni mwao.” 14 “Vinywa vyao
vimejaa laana na uchungu.” 15 “Miguu yao ina haraka
kumwaga damu; 16 maangamizi na taabu viko katika
njia zao, 17 wala njia ya amani hawaijui.” 18 “Hakuna
hofu ya Mungu machoni pao.” 19 Basi tunajua kwamba
chochote sheria inachosema, inawaambia wale walio
chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na
ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu. 20 Kwa hiyo
hakuna binadamu hata mmoja atakayehesabiwa
haki mbele za Mungu kwa matendo ya sheria, kwa
maana sheria hutufanya tuitambue dhambi. 21 Lakini
sasa, haki ya Mungu imedhihirishwa pasipo sheria,
ambayo Torati na Manabii wanaishuhudia. 22 Haki hii
inayotoka kwa Mungu hupatikana kwa Isa Al-Masihi
kwa wote wanaomwamini. Kwa maana hapo hakuna
tofauti, 23 kwa kuwa wote wametenda dhambi na
kupungukiwa na utukufu wa Mungu, 24 wanahesabiwa
haki bure kwa neema yake kupitia kwa ukombozi ulio
katika Al-Masihi Isa. 25 Mungu alimtoa awe dhabihu
ya upatanisho kupitia kwa imani katika damu yake.
Alifanya hivi ili kuonesha haki yake, kwa sababu kwa
ustahimili wake, Mungu aliziachilia bila adhabu zile
dhambi zilizotangulia kufanywa. 26 Alifanya hivyo ili
kuonesha haki yake wakati huu, ili yeye awe mwenye
haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini
Isa. 27 Basi, kujivuna kuko wapi? Kumewekwa mbali.
Kwa sheria gani? Je, ni kwa ile ya matendo? La,
bali kwa ile sheria ya imani. 28 Kwa maana twaona
kwamba mwanadamu huhesabiwa haki kupitia kwa
imani wala si kwa matendo ya sheria. 29 Je, Mungu
ni Mungu wa Wayahudi peke yao? Je, yeye si Mungu
wa watu wa Mataifa pia? Naam, yeye ni Mungu wa
watu wa Mataifa pia. 30 Basi kwa kuwa kuna Mungu
mmoja tu, atawahesabia haki wale waliotahiriwa kwa
imani na wale wasiotahiriwa kwa imani hiyo hiyo. 31
Je, basi ni kwamba tunaibatilisha sheria kwa imani
hii? La, hasha! Badala yake tunaithibitisha sheria.

**4** Tuseme nini basi, kuhusu Ibrahimu baba yetu kwa
jinsi ya mwili: yeye alipataje kujua jambo hili? 2
Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki kwa
matendo, basi, anacho kitu cha kujivunia, lakini si
mbele za Mungu. 3 Kwa maana Maandiko yasemaje?
“Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake
kuwa haki.” 4 Basi mtu afanyapo kazi, mshahara
wake hauhesabiwi kwake kuwa ni zawadi, bali ni
haki yake anayostahili. 5 Lakini kwa mtu ambaye
hafanyi kazi na anamtumaini Mungu, yeye ambaye
huwahesabia waovu haki, imani yake inahesabiwa
kuwa haki. 6 Daudi pia alisema vivyo hivyo aliponena
kuhusu baraka za mtu ambaye Mungu humhesabia
haki pasipo matendo: 7 “Wamebarikiwa wale ambao
wamesamehewa makosa yao, ambao dhambi zao
zimefunikwa. 8 Heri mtu yule Mwenyezi Mungu
hamhesabii dhambi zake.” 9 Je, huku kubarikiwa
ni kwa wale waliotahiriwa peke yao, au pia na kwa
wale wasiotahiriwa? Tumesema imani ya Ibrahimu
ilihesabiwa kwake kuwa haki. 10 Je, ilihesabiwaje
kwake kuwa haki? Ni kabla ya kutahiriwa, au baada
yake kutahiriwa? Haikuwa baada yake kutahiriwa,
bali kabla hajatahiriwa! 11 Alipewa ishara ya tohara
kuwa muhuri wa haki aliyokuwa nayo kwa imani
hata alipokuwa bado hajatahiriwa. Kusudi lilikuwa
kumfanya baba wa wote waaminio pasipo kutahiriwa,
ili wahesabiwe kuwa wenye haki. 12 Vivyo hivyo
awe baba wa wale waliotahiriwa ambao si kwamba
wametahiriwa tu, bali pia wanafuata mfano wa imani
ambayo baba yetu Ibrahimu alikuwa nayo kabla
ya kutahiriwa. 13 Kwa maana ile ahadi kwamba
angeurithi ulimwengu haikuja kwa Ibrahimu au kwa
wazao wake kupitia kwa sheria bali kupitia kwa
haki ipatikanayo kwa imani. 14 Kwa maana ikiwa
wale wanaoishi kwa sheria ndio warithi, imani haina
thamani na ahadi haifai kitu, 15 kwa sababu sheria
huleta ghadhabu. Mahali ambapo hakuna sheria,
hakuna makosa. 16 Kwa hiyo, ahadi huja kupitia
kwa imani, ili iwe ni kwa neema, na ihakikishiwe
wazao wote wa Ibrahimu, si kwa wale walio wa
sheria peke yao, bali pia kwa wale walio wa imani ya
Ibrahimu. Yeye ndiye baba yetu sisi sote. 17 Kama
ilivyoandikwa: “Nimekufanya wewe kuwa baba wa
mataifa mengi.” Yeye ni baba yetu mbele za Mungu,
ambaye yeye alimwamini, yule Mungu anayefufua
waliokufa, na kuvitaja vitu ambavyo haviko kana

kwamba viko. 18 Akitarajia yasiyoweza kutarajiwa, Ibrahimu akaamini, akawa baba wa mataifa mengi, kama alivyoahidiwa kwamba, “Hivyo ndivyo uzao wako utakavyokuwa.” 19 Ibrahimu hakuwa dhaifu katika imani hata alipofikiri hali ya mwili wake, ambao ulikuwa kama uliokufa, kwani umri wake ulikuwa unakaribia miaka mia moja, au alipofikiri hali ya kufa ya tumbo la Sara. 20 Lakini Ibrahimu hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu katika imani yake na kumpa Mungu utukufu, 21 akiwa na hakika kabisa kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kutimiza lile aliloahidi. 22 Hii ndio sababu, “ilihesabiwa kwake kuwa haki.” 23 Maneno haya “ilihesabiwa kwake kuwa haki,” hayakuandikwa kwa ajili yake peke yake, 24 bali kwa ajili yetu sisi pia ambao Mungu atatupatia haki, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Isa Bwana wetu kutoka kwa wafu. 25 Alitolewa afe kwa ajili ya dhambi zetu, naye alifufuliwa kutoka mauti ili tuhesabiwe haki.

**5** Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kupitia kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi, 2 ambaye kupitia kwake tumepata kuifikia neema hii kupitia kwa imani, neema ambayo tunasimama ndani yake sasa. Nasi twafurahia katika tumaini letu la kushiriki utukufu wa Mungu. 3 Si hivyo tu, bali twafurahi pia katika mateso, kwa sababu tunajua kuwa mateso huleta saburi, 4 nayo saburi huleta uthabiti wa moyo, na uthabiti wa moyo huleta tumaini, 5 wala tumaini halitukatishi tamaa, kwa sababu Mungu amekwisha kumimina pendo lake mioyoni mwetu kupitia kwa Roho wa Mungu ambaye ametupatia. 6 Kwa maana hata tulipokuwa dhaifu, wakati ulipowadia, Al-Masihi alikufa kwa ajili yetu sisi wenye dhambi. 7 Hakika, ni vigumu mtu yeyote kufa kwa ajili ya mwenye haki, ingawa inawezekana mtu akathubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. 8 Lakini Mungu anaudhihirisha upendo wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, Al-Masihi alikufa kwa ajili yetu. 9 Basi, kwa kuwa sasa tumehesabiwa haki kwa damu yake, si zaidi sana tutaokolewa kutoka ghadhabu ya Mungu kupitia kwake! 10 Kwa kuwa kama tulipokuwa adui wa Mungu tulipatanishwa naye kupitia kwa kifo cha Mwanawe, si zaidi sana baada ya kupatanishwa, tutaokolewa kwa uzima wake. 11 Lakini zaidi ya hayo, pia tunafurahi katika Mungu kupitia kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi, ambaye kupitia kwake tumepata upatanisho. 12 Kwa hiyo kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kupitia kwa mtu mmoja, na kupitia dhambi hii mauti ikawafikia watu wote, kwa sababu wote wamefanya dhambi: 13 kwa maana kabla sheria haijatolewa, dhambi ilikuwemo ulimwenguni. Lakini dhambi haihesabiwi wakati hakuna sheria. 14 Hata hivyo, tangu wakati wa Adamu hadi wakati wa Musa, mauti ilitawala watu wote, hata wale ambao hawakutenda dhambi kwa kuvunja amri, kama alivyofanya Adamu, aliye mfano wa yule atakayekuja. 15 Lakini ile karama iliyotolewa haikuwa kama lile kosa. Kwa maana ikiwa watu wengi walikufa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja, basi neema ya Mungu na ile karama iliyokuja kwa neema ya mtu mmoja, yaani Isa Al-Masihi, imezidi kuwa nyingi kwa ajili ya wengi. 16 Tena ile karama ya Mungu haiwezi kulinganishwa na matokeo ya ile dhambi ya mtu mmoja. Kwani hukumu ilikuja kupitia kwa dhambi ya mtu mmoja, ikaleta adhabu; lakini ile karama ilikuja baada ya makosa mengi, ikaleta kuhesabiwa haki. 17 Kwa maana ikiwa kutokana na kosa la mtu mmoja, mauti ilitawala kupitia huyo mtu mmoja, zaidi sana wale wanaopokea wingi wa neema ya Mungu na karama yake ya kuhesabiwa haki, watatawala katika uzima kupitia kwa huyo mtu mmoja, yaani Isa Al-Masihi. 18 Kwa hiyo, kama vile kosa la mtu mmoja lilivyoleta adhabu kwa watu wote, vivyo hivyo pia kwa tendo la haki la mtu mmoja lilileta kuhesabiwa haki ambako huleta uzima kwa wote. 19 Kwa maana kama vile kupitia kutokutii kwa yule mtu mmoja wengi walifanywa wenye dhambi, vivyo hivyo kupitia kutii kwa mtu mmoja wengi watafanywa wenye haki. 20 Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi, 21 ili kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, vivyo hivyo neema iweze kutawala kupitia kwa haki hata kuleta uzima wa milele katika Isa Al-Masihi Bwana wetu. **(aiōnios g166)**

**6** Tuseme nini basi? Je, tuendelee kutenda dhambi ili neema ipate kuongezeka? 2 La hasha! Sisi tulioifia dhambi, tutawezaje kuendelea kuishi tena katika dhambi? 3 Au hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Al-Masihi Isa tulibatizwa katika mauti yake? 4 Kwa hiyo tulizikwa pamoja naye kupitia kwa ubatizo katika mauti, ili kama vile Al-Masihi alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, nasi pia

tupate kuishi maisha mapya. 5 Kwa maana ikiwa
tumeungana naye katika mauti yake, bila shaka
tutaungana naye katika ufufuo wake. 6 Kwa maana
twajua kwamba utu wetu wa kale ulisulubiwa pamoja
naye ili ule mwili wa dhambi upate kuangamizwa,
nasi tusiendelee kuwa tena watumwa wa dhambi. 7
Kwa maana mtu yeyote aliyekufa amehesabiwa haki
mbali na dhambi. 8 Basi ikiwa tulikufa pamoja na Al-
Masihi, tunaamini kwamba pia tutaishi pamoja naye.
9 Kwa maana tunajua kwamba Al-Masihi, kwa sababu
alifufuliwa kutoka kwa wafu, hawezi kufa tena; mauti
haina tena mamlaka juu yake. 10 Kifo alichokufa,
aliifia dhambi mara moja tu; lakini uzima alio nao
anamwishia Mungu. 11 Vivyo hivyo, jihesabuni wafu
katika dhambi lakini mlio hai kwa Mungu katika Al-
Masihi Isa. 12 Kwa hiyo, msiruhusu dhambi itawale
ndani ya miili yenu, ipatikanayo na kufa, ili kuwafanya
mzitii tamaa mbaya. 13 Wala msivitoe viungo vya
miili yenu vitumike kama vyombo vya uovu vya
kutenda dhambi, bali jitoeni kwa Mungu, kama watu
waliotolewa kutoka mautini kuingia uzimani. Nanyi
vitoeni viungo vya miili yenu kwake kama vyombo vya
haki. 14 Kwa maana dhambi haitakuwa na mamlaka
juu yenu, kwa sababu hampo chini ya sheria, bali
chini ya neema. 15 Ni nini basi? Je, tutende dhambi
kwa kuwa hatuko chini ya sheria bali chini ya neema?
La, hasha! 16 Je, hamjui kwamba mnapojitoa kwa
mtu yeyote kama watumwa watiifu, ninyi ni watumwa
wa yule mnayemtii? Iwe ni watumwa wa dhambi
ambayo matokeo yake ni mauti, au watumwa wa utii
ambao matokeo yake ni haki? 17 Lakini Mungu apewe
shukrani kwa kuwa ninyi ambao kwanza mlikuwa
watumwa wa dhambi, mmekuwa watii kutoka moyoni
kwa mafundisho mliyopewa. 18 Nanyi baada ya
kuwekwa huru mbali na dhambi, mmekuwa watumwa
wa haki. 19 Ninasema kwa namna ya kibinadamu
kwa sababu ya udhaifu wenu wa hali ya asili. Kama
vile mlivyokuwa mkivitoa viungo vya miili yenu kama
watumwa wa mambo machafu na uovu uliokuwa
ukiongezeka zaidi, hivyo sasa vitoeni viungo vyenu
kama watumwa wa haki inayowaelekeza mpate
kutakaswa. 20 Mlipokuwa watumwa wa dhambi,
mlikuwa hamtawaliwi na haki. 21 Lakini mlipata faida
gani kwa mambo hayo ambayo sasa mnayaonea
aibu? Mwisho wa mambo hayo ni mauti. 22 Lakini
sasa kwa kuwa mmewekwa huru mbali na dhambi na
mmekuwa watumwa wa Mungu, faida mnayopata ni
utakatifu, ambao mwisho wake ni uzima wa milele.
**(aiōnios g166)** 23 Kwa maana mshahara wa dhambi
ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele
katika Al-Masihi Isa Bwana wetu. **(aiōnios g166)**

**7** Ndugu zangu, sasa ninasema na wale wanaoijua
Torati: Je, hamjui kwamba Torati ina mamlaka
juu ya mtu wakati akiwa hai tu? 2 Kwa mfano,
mwanamke aliyeolewa amefungwa kwa mumewe
wakati akiwa hai, lakini yule mume akifa, yule
mwanamke amefunguliwa kutoka sheria ya ndoa.
3 Hivyo basi, kama huyo mwanamke ataolewa na
mwanaume mwingine wakati mumewe akiwa bado
yuko hai, ataitwa mzinzi. Lakini kama mumewe akifa,
mwanamke huyo hafungwi tena na sheria ya ndoa,
naye akiolewa na mtu mwingine haitwi mzinzi. 4
Vivyo hivyo, ndugu zangu, ninyi mmeifia Torati kupitia
kwa mwili wa Al-Masihi, ili mweze kuwa mali ya
mwingine, yeye ambaye alifufuliwa kutoka kwa wafu,
ili tupate kuzaa matunda kwa Mungu. 5 Kwa maana
tulipokuwa tunatawaliwa na asili ya dhambi, tamaa za
dhambi zilizochochewa na Torati zilikuwa zikitenda
kazi katika miili yetu, hivyo tulizaa matunda ya mauti.
6 Lakini sasa, kwa kufia kile kilichokuwa kimetufunga
kwanza, tumewekwa huru kutokana na Torati ili
tutumike katika njia mpya ya Roho wa Mungu, wala
si katika njia ya zamani ya Torati iliyoandikwa. 7
Tuseme nini basi? Kwamba Torati ni dhambi? La,
hasha! Lakini singejua dhambi isipokuwa kwa sababu
ya Torati. Singejua kutamani ni nini kama Torati
haikusema, “Usitamani.” 8 Lakini dhambi ilipata nafasi
katika amri, nayo ikazaa kila aina ya tamaa ndani
yangu. Kwa maana pasipo sheria, dhambi imekufa.
9 Mwanzoni nilikuwa hai pasipo sheria; lakini amri
ilipokuja, dhambi ikawa hai, nami nikafa. 10 Nikaona
kwamba ile amri iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta
mauti. 11 Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi
katika amri, ilinidanganya, na kupitia katika hiyo amri,
ikaniua. 12 Hivyo basi, Torati yenyewe ni takatifu, na
amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema. 13 Je, kile
kilicho chema basi kilikuwa mauti kwangu? La, hasha!
Lakini ili dhambi itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta
mauti ndani yangu kupitia kile kilichokuwa chema,
ili kupitia kwa amri dhambi izidi kuwa mbaya kupita
kiasi. 14 Kwa maana tunajua kwamba Torati ni ya
kiroho, lakini mimi ni wa kimwili nikiwa nimeuzwa

kwenye utumwa wa dhambi. **15** Sielewi nitendalo, kwa maana lile ninalotaka kulitenda, silitendi, lakini ninatenda lile ninalolichukia. **16** Basi kama ninatenda lile nisilotaka kutenda, ni kwamba ninakubali kuwa Torati ni njema. **17** Lakini, kwa kweli si mimi tena nitendaye lile nisilotaka bali ni ile dhambi inayokaa ndani yangu. **18** Kwa maana ninafahamu kwamba hakuna jema lolote linalokaa ndani yangu, yaani katika asili yangu ya dhambi. Kwa kuwa nina shauku ya kutenda lililo jema, lakini siwezi kulitenda. **19** Sitendi lile jema nitakalo kutenda, bali lile baya nisilolitaka, ndilo nitendalo. **20** Basi kama ninatenda lile nisilotaka kutenda, si mimi tena nifanyaye hivyo, bali ni ile dhambi inayokaa ndani yangu. **21** Hivyo naiona Torati ikitenda kazi. Ninapotaka kutenda jema, jambo baya liko papo hapo. **22** Kwa maana katika utu wangu wa ndani naifurahia Torati ya Mungu. **23** Lakini ninaona kuna sheria nyingine inayotenda kazi katika viungo vya mwili wangu inayopigana vita dhidi ya ile sheria ya akili yangu. Sheria hii inanifanya mateka wa ile sheria ya dhambi inayofanya kazi katika viungo vya mwili wangu. **24** Ole wangu, mimi maskini! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? **25** Namshukuru Mungu anayeniokoa kupitia kwa Isa Al-Masihi Bwana wetu! Hivyo basi, mimi mwenyewe kwa akili zangu ni mtumwa wa Torati ya Mungu, lakini katika asili ya dhambi ni mtumwa wa sheria ya dhambi.

**8** Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Al-Masihi Isa. **2** Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima katika Al-Masihi Isa imeniweka huru mbali na sheria ya dhambi na mauti. **3** Kwa maana kile ambacho Torati haikuwa na uwezo wa kufanya, kwa vile ilivyokuwa dhaifu katika mwili, Mungu kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe kwa mfano wa mwanadamu mwenye mwili ulio wa dhambi na kwa ajili ya dhambi, yeye aliihukumu dhambi katika mwili, **4** ili haki ipatikanayo kwa Torati itimizwe ndani yetu sisi, ambao hatuenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho wa Mungu. **5** Kwa maana wale wanaoishi kwa kuufuata mwili huziweka nia zao katika vitu vya mwili, lakini wale wanaoishi kwa kufuata Roho wa Mungu, huziweka nia zao katika mambo ya huyo Roho. **6** Kwa maana kuwa na nia ya mwili ni mauti, bali kuwa na nia inayoongozwa na Roho wa Mungu ni uzima na amani. **7** Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii Torati ya Mungu, wala haiwezi kuitii. **8** Wale wanaotawaliwa na mwili, hawawezi kumpendeza Mungu. **9** Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Mtu ambaye hana Roho wa Al-Masihi, huyo si wa Al-Masihi. **10** Lakini kama Al-Masihi anakaa ndani yenu, miili yenu imekufa kwa sababu ya dhambi, lakini roho zenu zi hai kwa sababu ya haki. **11** Nanyi ikiwa Roho wa Mungu aliyemfufua Isa kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Al-Masihi Isa kutoka kwa wafu ataihuisha pia miili yenu ambayo hufa, kupitia kwa Roho wake Mtakatifu akaaye ndani yenu. **12** Kwa hiyo ndugu zangu, sisi tu wadeni, si wa mwili, ili tuishi kwa kuufuata mwili, **13** kwa maana mkiishi kwa kuufuata mwili, mtakufa, lakini mkiyaua matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi. **14** Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio watoto wa Mungu. **15** Kwa maana hamkupokea roho ya utumwa iletayo hofu tena, bali mlipokea Roho wa kufanywa wana, ambaye kwa yeye twalia, “Abba, Baba.” **16** Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu kwamba sisi tu watoto wa Mungu. **17** Hivyo, ikiwa sisi ni watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja na Al-Masihi, naam, tukiteswa pamoja naye tupate pia kutukuzwa pamoja naye. **18** Nayahesabu mateso yetu ya wakati huu kuwa si kitu kulinganisha na utukufu utakaodhihirishwa kwetu. **19** Kwa maana viumbe vyote vinangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa watoto wa Mungu. **20** Kwa kuwa viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali kwa mapenzi yake yeye aliyevitiisha katika tumaini, **21** ili viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka kwa utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. **22** Kwa maana twajua ya kuwa hata sasa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa maumivu kama uchungu wa mwanamke wakati wa kuzaa. **23** Wala si hivyo viumbe peke yao, bali hata sisi ambao ndio matunda ya kwanza ya Roho wa Mungu, kwa ndani tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa wana wa Mungu, yaani ukombozi wa miili yetu. **24** Kwa kuwa tuliokolewa kwa tumaini hili. Lakini kama kinachotumainiwa kikionekana, basi hakiwi tumaini tena. Je, kuna mtu anayetumaini kupata kitu alicho nacho tayari? **25** Lakini tunapotumaini kupata kitu ambacho hatuna, basi twakingojea kwa saburi.

26 Vivyo hivyo, Roho wa Mungu hutusaidia katika
udhaifu wetu, kwa sababu hatujui kuomba ipasavyo.
Lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa uchungu
usioweza kutamkwa. 27 Naye Mungu aichunguzaye
mioyo, anaijua nia ya Roho, kwa sababu Roho huyo
huwaombea watakatifu sawasawa na mapenzi ya
Mungu. 28 Nasi tunajua ya kuwa katika mambo yote
Mungu hutenda kazi pamoja na wote wanaompenda,
yaani wale walioitwa kwa kusudi lake, ili kuwaletea
mema. 29 Maana wale Mungu aliowajua tangu
mwanzo, pia aliwachagua tangu mwanzo, wapate
kufanana na mfano wa Mwanawe, ili yeye awe
mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi. 30
Nao wale Mungu aliotangulia kuwachagua, akawaita,
wale aliowaita pia akawahesabia haki, nao wale
aliowahesabia haki, pia akawatukuza. 31 Tuseme nini
basi kuhusu haya? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni
nani awezaye kuwa kinyume chetu? 32 Ikiwa Mungu
hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu
sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu
pamoja naye? 33 Ni nani atakayewashtaki wale ambao
Mungu amewateua? Mungu ndiye anayewahesabia
haki. 34 Ni nani basi atakayewahukumia adhabu?
Hakuna! Al-Masihi Isa aliyekufa, naam, na zaidi ya
hayo, akafufuliwa kutoka kwa wafu, yuko mkono
wa kuume wa Mungu, naye pia anatuombea. 35 Ni
nani atakayetutenga na upendo wa Al-Masihi? Je,
ni shida au taabu au mateso au njaa au uchi au
hatari au upanga? 36 Kama ilivyoandikwa: "Kwa ajili
yako tunauawa mchana kutwa; tumehesabiwa kama
kondoo wa kuchinjwa." 37 Lakini katika mambo haya
yote tu zaidi ya washindi kwa yeye aliyetupenda. 38
Kwa maana nimekwisha kujua kwa hakika ya kuwa
sio mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye
mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuja, wala
wenye uwezo, 39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini,
wala kiumbe kingine chochote zitaweza kututenga na
upendo wa Mungu ulio katika Al-Masihi Isa, Bwana
wetu.

**9** Ninasema kweli katika Al-Masihi, wala sisemi
uongo, dhamiri yangu inanishuhudia katika Roho
wa Mungu. 2 Nina huzuni kuu na uchungu usiokoma
moyoni mwangu. 3 Kwa maana ningetamani hata
mimi nilaaniwe na kutengwa na Al-Masihi kwa ajili
ya ndugu zangu hasa, wale walio wa kabila langu
kwa jinsi ya mwili, 4 yaani watu wa Israeli. Hao ndio
wenye kule kufanywa wana, ule utukufu wa Mungu,
yale maagano, kule kupokea Torati, ibada ya kwenye
Hekalu na zile ahadi. 5 Wao ni wa uzao wa baba zetu
wa zamani, ambao kutoka kwao Al-Masihi alikuja
kwa jinsi ya mwili kama mwanadamu, yeye ambaye
ni Mungu aliye juu ya vyote, mwenye kuhimidiwa
milele! Amen. (aiōn g165) 6 Si kwamba neno la Mungu
limeshindwa. Kwa maana si kila Mwisraeli ambaye ni
wa uzao utokanao na Israeli ni Mwisraeli halisi. 7 Wala
hawawi wazao wa Ibrahimu kwa sababu wao ni watoto
wake, lakini: "Uzao wako utahesabiwa kupitia kwake
Isaka." 8 Hii ina maana kwamba, si watoto waliozaliwa
kimwili walio watoto wa Mungu, bali ni watoto wa
ahadi wanaohesabiwa kuwa uzao wa Ibrahimu. 9
Kwa maana ahadi yenyewe ilisema, "Nitakurudia
tena wakati kama huu, naye Sara atapata mtoto wa
kiume." 10 Wala si hivyo tu, bali pia watoto aliowazaa
Rebeka walikuwa na baba huyo huyo mmoja, yaani
baba yetu Isaka. 11 Lakini, hata kabla hao mapacha
hawajazaliwa au kufanya jambo lolote jema au baya,
ili kusudi la Mungu la kuchagua lipate kusimama, 12
si kwa matendo, bali kwa yeye mwenye kuita, Rebeka
aliambiwa, "Yule mkubwa atamtumikia yule mdogo."
13 Kama vile ilivyoandikwa, "Nimempenda Yakobo,
lakini nimemchukia Esau." 14 Tuseme nini basi? Je,
Mungu ni dhalimu? La, hasha! 15 Kwa maana Mungu
alimwambia Musa, "Nitamrehemu yeye nimrehemuye,
na pia nitamhurumia yeye nimhurumiaye." 16 Kwa
hiyo haitegemei kutaka kwa mwanadamu au jitihada,
bali hutegemea huruma ya Mungu. 17 Kwa maana
Maandiko yamwambia Farao, "Nilikuinua kwa kusudi
hili hasa, ili nipate kuonesha uweza wangu juu yako,
na ili Jina langu lipate kutangazwa duniani kote." 18
Kwa hiyo basi, Mungu humhurumia yeye atakaye
kumhurumia na humfanya mgumu yeye atakaye
kumfanya mgumu. 19 Basi mtaniambia, "Kama ni
hivyo, kwa nini basi bado Mungu anatulaumu? Kwa
maana ni nani awezaye kupinga mapenzi yake?" 20
Lakini, ewe mwanadamu, u nani wewe ushindane
na Mungu? "Je, kilichoumbwa chaweza kumwambia
yeye aliyekiumba, 'Kwa nini umeniumba hivi?'" 21
Je, mfinyanzi hana haki ya kufinyanga kutoka bonge
moja vyombo vya udongo, vingine kwa matumizi
ya heshima na vingine kwa matumizi ya kawaida?
22 Iweje basi, kama Mungu kwa kutaka kuonesha
ghadhabu yake na kufanya uweza wake ujulikane,

amevumilia kwa uvumilivu mwingi vile vyombo vya
ghadhabu vilivyoandaliwa kwa uharibifu? **23** Iweje
basi, kama yeye alitenda hivi ili kufanya wingi wa
utukufu wake ujulikane kwa vyombo vya rehema yake,
alivyotangulia kuvitengeneza kwa ajili ya utukufu
wake? **24** Hivi vyombo ni sisi, ambao pia alituita,
sio kutoka kwa Wayahudi peke yao, bali pia kutoka
kwa watu wa Mataifa. **25** Kama alivyosema Mungu
katika Hosea: “Nitawaita ‘watu wangu’ wale ambao si
watu wangu; nami nitamwita ‘mpendwa wangu’ yeye
ambaye si mpendwa wangu,” **26** tena, “Itakuwa hasa
mahali pale walipoambiwa, ‘Ninyi si watu wangu,’
wao wataitwa ‘wana wa Mungu aliye hai.’” **27** Isaya
anapaza sauti na kusema kuhusu Israeli kwamba:
“Ingawa idadi ya Waisraeli ni wengi kama mchanga
wa pwani, ni mabaki yao tu watakaookolewa. **28** Kwa
kuwa Mwenyezi Mungu ataitekeleza hukumu yake
duniani kwa haraka na kwa ukamilifu.” **29** Ni kama vile
alivyotabiri Isaya, akisema: “Kama Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni, hakutuachia uzao,
tungekuwa kama Sodoma, tungefanana na Gomora.”
**30** Kwa hiyo tuseme nini? Kwamba watu wa Mataifa
ambao hawakutafuta haki, wamepata haki ile iliyo
kupitia kwa imani. **31** Lakini Israeli, ambao walijitahidi
kupata haki kupitia kwa sheria, hawakuipata. **32** Kwa
nini? Kwa sababu hawakuitafuta kupitia kwa imani bali
kupitia kwa matendo. Wakajikwaa kwenye lile “jiwe la
kukwaza”. **33** Kama ilivyoandikwa: “Tazama naweka
katika Sayuni jiwe la kukwaza watu na mwamba wa
kuwaangusha. Yeyote atakayemwamini hataaibika
kamwe.”

**10** Ndugu zangu, shauku ya moyo wangu na
maombi yangu kwa Mungu ni kwa ajili ya
Waisraeli, kwamba waokolewe. **2** Kwa maana
ninaweza nikashuhudia wazi kwamba wao wana
juhudi kubwa kwa ajili ya Mungu, lakini juhudi yao
haina maarifa. **3** Kwa kuwa hawakuijua haki ya Mungu,
wakatafuta kuweka haki yao wenyewe, hawakujitia
chini ya haki ya Mungu. **4** Kwa maana Al-Masihi ni
ukomo wa sheria ili kila mtu aaminiye ahesabiwe haki.
**5** Musa anaandika kuhusu haki ile itokanayo na sheria,
kwamba, “Mtu atendaye matendo hayo ataishi kwa
hayo.” **6** Lakini ile haki itokanayo na imani husema
hivi: “Usiseme moyoni mwako, ‘Ni nani atakayepanda
mbinguni?’” (yaani ili kumleta Al-Masihi chini) **7** “au ‘Ni
nani atashuka kwenda Kuzimu?’” (yaani ili kumleta Al-
Masihi kutoka kwa wafu). **(Abyssos g12)** **8** Lakini andiko
lasemaje? “Lile neno liko karibu nawe, liko kinywani
mwako na moyoni mwako,” yaani lile neno la imani
tunalolihubiri. **9** Kwa sababu, ukikiri kwa kinywa chako
kwamba “Isa ni Bwana,” na kuamini moyoni mwako
kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, utaokoka.
**10** Kwa maana kwa moyo mtu huamini na hivyo
kuhesabiwa haki, tena kwa kinywa mtu hukiri na hivyo
kupata wokovu. **11** Kama Maandiko yanavyosema,
“Yeyote amwaminiye hataaibika kamwe.” **12** Kwa
maana hakuna tofauti kati ya Myahudi na mtu wa
Mataifa, yeye ni Bwana wa wote, mwenye utajiri kwa
wote wamwitao. **13** Kwa maana, “Kila mtu atakayeliitia
Jina la Mwenyezi Mungu, ataokolewa.” **14** Lakini
watamwitaje yeye ambaye hawajamwamini? Nao
watawezaje kumwamini yeye ambaye hawajamsikia?
Tena watamsikiaje bila mtu kuwahubiria? **15** Nao
watahubirije wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa,
“Tazama jinsi ilivyo mizuri miguu yao wale wanaohubiri
Habari Njema!” **16** Lakini si wote waliotii Injili. Kwa
maana Isaya asema, “Mwenyezi Mungu, ni nani
aliyeamini ujumbe wetu?” **17** Basi, imani chanzo
chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la Al-
Masihi. **18** Lakini nauliza: Je, wao hawakusikia?
Naam, wamesikia, kwa maana: “Sauti yao imeenea
duniani pote, nayo maneno yao yameenea hadi
miisho ya ulimwengu.” **19** Nami nauliza tena: Je,
Waisraeli hawakuelewa? Kwanza, Musa asema,
“Nitawafanya mwe na wivu kwa watu wale ambao
si taifa. Nitawakasirisha kwa taifa lile lisilo na
ufahamu.” **20** Naye Isaya kwa ujasiri mwingi anasema,
“Nimeonekana na watu wale ambao hawakunitafuta.
Nilijifunua kwa watu wale ambao hawakunitafuta.”
**21** Lakini kuhusu Israeli anasema, “Mchana kutwa
nimewanyooshea watu wakaidi na wasiotii mikono
yangu.”

**11** Basi nauliza: Je, Mungu amewakataa watu
wake? La, hasha! Mimi mwenyewe ni Mwisraeli,
tena uzao wa Ibrahimu kutoka kabila la Benyamini. **2**
Mungu hajawakataa watu wake, ambao yeye aliwajua
tangu mwanzo. Je, hamjui yale Maandiko yasemayo
kuhusu Ilya, jinsi alivyomlalamikia Mungu kuhusu
Israeli? **3** Alisema, “Mwenyezi Mungu, wamewaua
manabii wako na kuzibomoa madhabahu zako,
nimebaki mimi peke yangu, nao wanataka kuniua?” **4**
Je, Mungu alimjibuje? “Nimejibakizia watu elfu saba

ambao hawajapiga magoti kumwabudu Baali.” 5
Vivyo hivyo pia, sasa wapo mabaki waliochaguliwa
kwa neema ya Mungu. 6 Lakini ikiwa wamechaguliwa
kwa neema, si tena kwa msingi wa matendo. Kama
ingekuwa kwa matendo, neema isingekuwa neema
tena. 7 Tuseme nini basi? Kile kitu ambacho Israeli
alikitafuta kwa bidii hakukipata. Lakini waliochaguliwa
walikipata. Waliobaki walifanywa wagumu, 8 kama
ilivyoandikwa: “Mungu aliwapa bumbuazi la mioyo,
macho ili wasiweze kuona, na masikio ili wasiweze
kusikia, hadi leo.” 9 Naye Daudi anasema: “Karamu
zao na ziwe tanzi na mtego wa kuwanasa, kitu cha
kuwakwaza waanguke, na adhabu kwao. 10 Macho
yao yatiwe giza ili wasiweze kuona, nayo migongo
yao iinamishwe daima.” 11 Hivyo nauliza tena: Je,
Waisraeli walijikwaa ili waanguke na kuangamia
kabisa? La, hasha! Lakini kwa sababu ya makosa yao,
wokovu umewafikia watu wa Mataifa, ili kuwafanya
Waisraeli waone wivu. 12 Basi ikiwa kukosa kwao
kumekuwa utajiri mkubwa kwa ulimwengu, tena
kama kuangamia kwao kumeleta utajiri kwa watu
wa Mataifa, kurudishwa kwao kutaleta utajiri mkuu
zaidi. 13 Sasa ninasema nanyi watu wa Mataifa.
Maadamu mimi ni mtume kwa watu wa Mataifa,
naitukuza huduma yangu 14 ili kuwafanya watu
wangu waone wivu na hivyo kuwaokoa baadhi yao.
15 Kwa kuwa ikiwa kukataliwa kwao ni kupatanishwa
kwa ulimwengu, kukubaliwa kwao si kutakuwa ni
uhai baada ya kufa? 16 Kama sehemu ya donge la
unga uliotolewa kuwa limbuko ni mtakatifu, basi unga
wote ni mtakatifu, nalo shina kama ni takatifu, vivyo
hivyo na matawi nayo. 17 Lakini kama baadhi ya
matawi yalikatwa, nawe chipukizi la mzeituni mwitu
ukapandikizwa mahali pao ili kushiriki unono pamoja
na matawi mengine kutoka shina la mzeituni, 18
basi usijivune juu ya hayo matawi. Lakini ukijivuna,
kumbuka jambo hili: Si wewe unayelishikilia shina,
bali ni shina linalokushikilia wewe. 19 Basi utasema,
“Matawi yale yalikatwa ili nipate kupandikizwa katika
hilo shina.” 20 Hii ni kweli. Matawi hayo yalikatwa
kwa sababu ya kutokuamini kwake, lakini wewe
umesimama tu kwa sababu ya imani. Kwa hiyo
usijivune, bali simama kwa kuogopa. 21 Kwa maana
kama Mungu hakuyahurumia matawi ya asili, wala
hatakuhurumia wewe. 22 Angalia basi wema na
ukali wa Mungu: Ukali kwa wale walioanguka, bali
wema wa Mungu kwako wewe, kama utadumu katika
wema wake. La sivyo, nawe utakatiliwa mbali. 23
Wao nao wasipodumu katika kutokuamini kwao,
watapandikizwa tena kwenye shina, kwa maana
Mungu anao uwezo wa kuwapandikiza tena kwenye
hilo shina. 24 Ikiwa wewe ulikatwa kutoka kile
ambacho kwa asili ni mzeituni mwitu, na kupandikizwa
kinyume cha asili kwenye mzeituni uliopandwa, si
rahisi zaidi matawi haya ya asili kupandikizwa tena
kwenye shina lake la mzeituni wao mwenyewe!
25 Ndugu zangu, ili msije mkajidai kuwa wenye
hekima kuliko mlivyo, nataka mfahamu siri hii: Ugumu
umewapata Israeli kwa sehemu hadi idadi ya watu
wa Mataifa watakaoingia itimie. 26 Hivyo Israeli wote
wataokolewa. Kama ilivyoandikwa: “Mkombozi atakuja
kutoka Sayuni; ataondoa kutokumcha Mungu katika
Yakobo. 27 Hili ndilo agano langu nao nitakapoziondoa
dhambi zao.” 28 Kwa habari ya Injili, wao ni adui wa
Mungu kwa ajili yenu, lakini kuhusu kule kuteuliwa
kwao ni wapendwa, kwa ajili ya baba zao wa zamani;
29 kwa maana akishawapa watu karama, Mungu
haziondoi, wala wito wake. 30 Kama vile ninyi wakati
fulani mlivyokuwa waasi kwa Mungu lakini sasa
mmepata rehema kwa sababu ya kutokutii kwao, 31
hivyo nao Waisraeli wamekuwa waasi ili wao nao
sasa waweze kupata rehema kwa ajili ya rehema za
Mungu kwenu. 32 Kwa maana Mungu amewafunga
wanadamu wote kwenye kuasi ili apate kuwarehemu
wote. **(eleēsē g1653)** 33 Tazama jinsi kilivyo kina cha
utajiri wa hekima na maarifa ya Mungu! Tazama jinsi
hukumu zake hazichunguziki, na ambavyo njia zake
hazitafutiki! 34 “Ni nani aliyeyafahamu mawazo ya
Mwenyezi Mungu? Au ni nani ambaye amekuwa
mshauri wake?” 35 “Au ni nani aliyempa chochote
ili arudishiwe?” 36 Kwa maana vitu vyote vyatoka
kwake, viko kwake na kwa ajili yake. Utukufu ni wake
milele! Amen. **(aiōn g165)**

**12** Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema
zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo
hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo
ibada yenu yenye maana. 2 Msifuatishe tena mfano
wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa
upya nia zenu. Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha
mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza
na kamilifu machoni pake. **(aiōn g165)** 3 Kwa ajili ya
neema niliyopewa nawaambia kila mmoja miongoni

mwenu, asijidhanie kuwa bora kuliko impasavyo, bali
afikiri kwa busara kwa kulingana na kipimo cha imani
Mungu aliyompa. 4 Kama vile katika mwili mmoja
tulivyo na viungo vingi, navyo viungo vyote havina
kazi moja, 5 vivyo hivyo na sisi tulio wengi, tu mwili
mmoja katika Al-Masihi, nasi kila mmoja ni kiungo
cha mwenzake. 6 Tuna karama zilizotofautiana kila
mmoja kutokana na neema tuliyopewa. Kama ni
unabii na tutoe unabii kwa kadiri ya imani. 7 Kama
ni kuhudumu na tuhudumu, mwenye kufundisha na
afundishe, 8 kama ni kutia moyo na atie moyo, kama
ni kuchangia kwa ajili ya mahitaji ya wengine na
atoe kwa ukarimu, kama ni uongozi na aongoze
kwa bidii, kama ni kuhurumia wengine na afanye
hivyo kwa furaha. 9 Upendo lazima usiwe na unafiki.
Chukieni lililo ovu, shikamaneni na lililo jema. 10
Pendaneni ninyi kwa ninyi kwa upendo wa ndugu.
Waheshimuni na kuwatanguliza wengine. 11 Msiwe
wavivu, bali mwe na bidii katika roho mkimtumikia
Bwana Isa. 12 Kuweni na furaha katika tumaini, katika
dhiki kuweni na saburi, dumuni katika maombi. 13
Changieni katika mahitaji ya watakatifu, wakaribisheni
wageni. 14 Wabarikini wale wanaowatesa, barikini
wala msilaani. 15 Furahini pamoja na wenye kufurahi,
lieni pamoja na wale waliao. 16 Kaeni kwa amani ninyi
kwa ninyi. Msijivune, bali mwe tayari kushirikiana na
wanyonge. Wala msiwe watu wenye kujivuna kwamba
mnajua kila kitu. 17 Msimlipe mtu yeyote ovu kwa
ovu. Jitahidini ili mtende yaliyo mema machoni pa
watu wote. 18 Ikiwezekana, kwa upande wenu kaeni
kwa amani na watu wote. 19 Wapendwa, msilipize
kisasi, bali ipisheni ghadhabu ya Mungu, maana
imeandikwa: “Ni juu yangu kulipiza kisasi, nitalipiza,”
asema Mwenyezi Mungu. 20 Badala yake: “Kama
adui yako ana njaa, mlishe; kama ana kiu, mpe
kinywaji. Kwa kufanya hivyo, unaweka makaa ya
moto yanayowaka kichwani pake.” 21 Usishindwe na
ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema.

**13** Kila mtu na atii mamlaka inayotawala, kwa
maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu,
nazo mamlaka zilizopo zimewekwa na Mungu. 2 Kwa
hiyo yeye anayeasi dhidi ya mamlaka inayotawala
anaasi dhidi ya kile kilichowekwa na Mungu, nao
wale wafanyao hivyo watajiletea hukumu juu yao
wenyewe. 3 Kwa kuwa watawala hawawatishi watu
wale wanaotenda mema bali wale wanaotenda
mabaya. Je, wataka usimwogope mwenye mamlaka?
Basi tenda lile lililo jema naye atakusifu. 4 Kwa
maana mwenye mamlaka ni mtumishi wa Mungu
kwa ajili ya mema yako. Lakini ukitenda mabaya,
basi ogopa, kwa kuwa hauinui upanga bila sababu.
Yeye ni mtumishi wa Mungu, mjumbe wa Mungu wa
kutekeleza adhabu juu ya watenda mabaya. 5 Kwa
hiyo ni lazima kutii wenye mamlaka, si kwa sababu
ya kuogopa adhabu iwezayo kutolewa, bali pia kwa
ajili ya dhamiri. 6 Kwa sababu hii mnalipa kodi, kwa
maana watawala ni watumishi wa Mungu, ambao
hutumia muda wao wote kutawala. 7 Mlipeni kila mtu
kile mnachodaiwa. Kama mnadaiwa kodi lipeni kodi,
kama ni ushuru, lipeni ushuru, astahiliye hofu, mhofu,
astahiliye heshima, mheshimu. 8 Msidaiwe kitu na
mtu yeyote, isipokuwa kupendana, kwa maana yeye
ampendaye mwenzake, ameitimiza sheria. 9 Kwa
kuwa amri hizi zisemazo, “Usizini,” “Usiue,” “Usiibe,”
“Usitamani,” na amri nyingine zote, zinajumlishwa
katika amri hii moja: “Mpende jirani yako kama nafsi
yako.” 10 Upendo haumfanyii jirani jambo baya. Kwa
hiyo upendo ndio utimilifu wa sheria. 11 Nanyi fanyeni
hivi, mkiutambua wakati tulio nao. Saa ya kuamka
kutoka usingizini imewadia, kwa maana sasa wokovu
wetu umekaribia kuliko hapo kwanza tulipoamini. 12
Usiku umeendelea sana, mapambazuko yamekaribia.
Kwa hiyo tuyaweke kando matendo ya giza na tuvae
silaha za nuru. 13 Basi na tuenende kwa adabu
kama inavyopasa wakati wa mchana, si kwa kufanya
karamu za ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati,
si kwa ugomvi na wivu. 14 Bali jivikeni Bwana Isa Al-
Masihi, wala msifikiri jinsi mtakavyotimiza tamaa za
miili yenu yenye asili ya dhambi.

**14** Mkaribisheni yeye ambaye imani yake ni dhaifu,
lakini si kwa kugombana na kubishana juu ya
mawazo yake. 2 Mtu mmoja imani yake inamruhusu
kula kila kitu, lakini mwingine ambaye imani yake
ni dhaifu, hula mboga tu. 3 Yeye alaye kila kitu
asimdharau yeye asiyekula. Wala yeye asiyekula kila
kitu asimhukumu yule alaye kila kitu, kwa maana
Mungu amemkubali. 4 Wewe ni nani hata umhukumu
mtumishi wa mtu mwingine? Kwa bwana wake tu
anasimama au kuanguka. Naye atasimama kwa
sababu Bwana anaweza kumsimamisha. 5 Mtu mmoja
anaitukuza siku fulani kuwa ni bora kuliko nyingine,
na mwingine anaona kuwa siku zote ni sawa. Basi

kila mmoja awe na hakika na yale anayoamini. 6 Yeye
anayehesabu siku moja kuwa takatifu kuliko nyingine,
hufanya hivyo kwa kumheshimu Mwenyezi Mungu.
Naye alaye nyama hula kwa Mwenyezi Mungu, kwa
maana humshukuru Mungu, naye akataaye kula
nyama hufanya hivyo kwa Mwenyezi Mungu na
humshukuru Mungu. 7 Kwa kuwa hakuna hata mmoja
wetu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe, wala hakuna
hata mmoja wetu afaye kwa ajili yake mwenyewe. 8
Kama tunaishi, tunaishi kwa Mwenyezi Mungu, nasi
pia tukifa tunakufa kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo
basi, kama tukiishi au kama tukifa, sisi ni mali ya
Mwenyezi Mungu. 9 Kwani kwa sababu hii hasa, Al-
Masihi alikufa na akawa hai tena kusudi apate kuwa
Bwana wa wote, yaani waliokufa na walio hai. 10 Basi
kwa nini wewe wamhukumu ndugu yako? Au kwa
nini wewe unamdharau ndugu yako? Kwa kuwa sote
tutasimama mbele ya kiti cha Mungu cha hukumu.
11 Kwa kuwa imeandikwa: "'Kama vile niishivyo,'
asema Mwenyezi Mungu, 'kila goti litapigwa mbele
zangu, na kila ulimi utakiri kwa Mungu.'" 12 Hivyo
basi kila mmoja wetu atatoa habari zake mwenyewe
kwa Mungu. 13 Kwa hiyo tusiendelee kuhukumiana.
Badala yake mtu aamue kutoweka kamwe kikwazo
au kizuizi katika njia ya ndugu mwingine. 14 Ninajua
tena nimehakikishiwa sana katika Bwana Isa kwamba
hakuna kitu chochote ambacho ni najisi kwa asili
yake. Lakini kama mtu anakiona kitu kuwa ni najisi,
basi kwake huyo kitu hicho ni najisi. 15 Kama ndugu
yako anahuzunishwa kwa sababu ya kile unachokula,
basi huenendi tena katika upendo. Usiruhusu kile
unachokula kiwe sababu ya kumwangamiza ndugu
yako ambaye Al-Masihi alikufa kwa ajili yake. 16
Usiruhusu kile ambacho unakiona kuwa chema
kisemwe kuwa ni kiovu. 17 Kwa maana ufalme wa
Mungu si kula na kunywa, bali ni haki, amani na furaha
katika Roho wa Mungu. 18 Kwa sababu mtu yeyote
anayemtumikia Al-Masihi kwa jinsi hii, anampendeza
Mungu na kukubaliwa na wanadamu. 19 Kwa hiyo
na tufanye bidii kutafuta yale yaletayo amani na
kujengana sisi kwa sisi. 20 Usiiharibu kazi ya Mungu
kwa ajili ya chakula. Hakika vyakula vyote ni safi,
lakini ni kosa kula kitu chochote kinachomsababisha
ndugu yako ajikwae. 21 Ni afadhali kutokula nyama
wala kunywa divai au kufanya jambo lingine lolote
litakalomsababisha ndugu yako ajikwae. 22 Je, wewe
unayo imani? Ile imani uliyo nayo, uwe nayo nafsini
mwako mbele za Mungu. Heri mtu yule asiye na
sababu ya kujihukumu nafsi yake kwa ajili ya kile
anachokifanya. 23 Lakini kama mtu ana shaka kuhusu
kile anachokula, amehukumiwa, kwa sababu hakula
kwa imani. Kwa kuwa chochote kinachofanywa pasipo
imani ni dhambi.

**15** Sisi tulio na nguvu, hatuna budi kuchukuliana
na kushindwa kwa wale walio dhaifu wala si
kujipendeza nafsi zetu wenyewe. 2 Kila mmoja
wetu inampasa kumpendeza jirani yake kwa mambo
mema, ili kumjenga katika imani. 3 Kwa maana
hata Al-Masihi hakujipendeza mwenyewe, bali kama
ilivyoandikwa: "Matukano yao wale wanaokutukana
wewe yalinipata mimi." 4 Kwa maana kila kitu
kilichoandikwa zamani, kiliandikwa kutufundisha, ili
kwa saburi na faraja tunayopata katika Maandiko
tuwe na tumaini. 5 Mungu atoaye saburi na faraja
awajalie ninyi roho ya umoja miongoni mwenu
mnapomfuata Al-Masihi Isa, 6 ili kwa moyo mmoja
mpate kumtukuza Mungu aliye Baba wa Bwana
wetu Isa Al-Masihi. 7 Karibishaneni ninyi kwa ninyi
kama Al-Masihi alivyowakaribisha ninyi ili kumletea
Mungu utukufu. 8 Kwa maana nawaambia kwamba
Al-Masihi amekuwa mtumishi kwa wale waliotahiriwa
ili kuonesha kweli ya Mungu, na kuthibitisha zile
ahadi walizopewa baba zetu wa zamani, 9 na pia
ili watu wa Mataifa wamtukuze Mungu kwa rehema
zake. Kama ilivyoandikwa: "Kwa hiyo nitakutukuza
kati ya watu wa Mataifa; nitaliimbia sifa jina lako." 10
Tena yasema, "Enyi watu wa Mataifa, furahini pamoja
na watu wa Mungu." 11 Tena, "Msifuni Mwenyezi
Mungu, ninyi watu wa Mataifa wote, na kumwimbia
sifa, enyi watu wote." 12 Tena Isaya anasema, "Shina
la Yese litachipuka, yeye atakayeinuka ili kuyatawala
mataifa. Watu wa Mataifa watamtumaini." 13 Mungu
wa tumaini awajaze ninyi furaha yote na amani katika
kumwamini, ili mpate kujawa na tumaini tele kwa
nguvu ya Roho Mtakatifu wa Mungu. 14 Ndugu zangu,
mimi mwenyewe ninasadiki kwamba mmejaa wema,
mkijazwa ufahamu wote na mnaweza kufundishana
ninyi kwa ninyi. 15 Hata hivyo, nimewaandikia kwa
ujasiri vipengele kadha wa kadha katika waraka huu
ili kuwakumbusha tena kuvihusu, kutokana na ile
neema Mungu aliyonipa 16 niwe mhudumu wa Al-
Masihi Isa kwa watu wa Mataifa. Alinipa huduma

ya kikuhani ya kutangaza Injili ya Mungu, ili watu
wa Mataifa wapate kuwa dhabihu inayokubalika na
Mungu, kwa kutakaswa na Roho wa Mungu. 17 Kwa
hiyo ninajisifu katika Al-Masihi Isa, kwenye utumishi
wangu kwa Mungu. 18 Kwa maana sitathubutu
kusema kitu chochote zaidi ya kile ambacho Al-Masihi
amefanya kwa kunitumia mimi katika kuwaongoza
watu wa Mataifa wamtii Mungu kwa yale niliyosema
na kufanya, 19 kwa nguvu za ishara na miujiza,
kwa uweza wa Roho wa Mungu, hivyo kuanzia
Yerusalemu hadi maeneo yote ya kandokando yake
hadi Iliriko, nimekwisha kuihubiri Injili ya Al-Masihi
kwa ukamilifu. 20 Hivyo imekuwa nia yangu kuhubiri
Injili pale ambapo Al-Masihi hajajulikana, ili nisije
nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine. 21 Lakini
kama ilivyoandikwa: "Wale ambao hawajahubiriwa
habari zake wataona, nao wale ambao hawajazisikia
watafahamu." 22 Hii ndiyo sababu nimezuiliwa mara
nyingi nisiweze kuja kwenu. 23 Lakini sasa kwa kuwa
hakuna nafasi zaidi kwa ajili yangu katika sehemu hii,
ninatamani kuja kwenu kama ambavyo nimekuwa na
shauku kwa miaka mingi. 24 Nimekusudia kufanya
hivyo nitakapokuwa njiani kwenda Hispania. Natarajia
kuwaona katika safari yangu na kusafirishwa nanyi
hadi huko, baada ya kufurahia ushirika wenu kwa
kitambo kidogo. 25 Ila sasa niko njiani kuelekea
Yerusalemu kwa ajili ya kuwahudumia watakatifu huko.
26 Kwa kuwa imewapendeza watu wa Makedonia
na Akaya kufanya changizo kwa ajili ya maskini
walio miongoni mwa watakatifu huko Yerusalemu. 27
Imewapendeza kufanya hivyo, naam, kwani ni wadeni
wao. Kwa maana ikiwa watu wa Mataifa wameshiriki
baraka za rohoni za Wayahudi, wao ni wadeni wa
Wayahudi, ili Wayahudi nao washiriki baraka zao za
mambo ya mwilini. 28 Kwa hiyo baada ya kukamilisha
kazi hii na kuhakikisha kuwa wamepokea kila kitu
kilichokusanywa, nitapitia kwenu nikiwa njiani kwenda
Hispania. 29 Ninajua kwamba nitakapokuja kwenu,
nitakuja na wingi wa baraka za Al-Masihi. 30 Basi,
ndugu zangu, nawasihi kwa Jina la Bwana wetu
Isa Al-Masihi na kwa upendo wa Roho wa Mungu,
kujiunga nami katika taabu zangu mkiniombea kwa
Mungu. 31 Ombeni ili nipate kuokolewa mikononi mwa
wale wasioamini walio Yudea, na kwamba utumishi
wangu upate kukubaliwa na watakatifu wa huko
Yerusalemu, 32 ili kwa mapenzi ya Mungu niweze
kuja kwenu kwa furaha, nami niburudishwe pamoja
nanyi. 33 Mungu wa amani na awe pamoja nanyi
nyote. Amen.

16 Napenda kumtambulisha kwenu dada yetu
Foibe, mhudumu katika kundi la waumini la
Kenkrea. 2 Naomba mpokeeni katika Bwana Isa
ipasavyo watakatifu na kumpa msaada wowote
atakaohitaji kutoka kwenu, kwa maana yeye amekuwa
msaada kwa watu wengi, mimi nikiwa miongoni mwao.
3 Wasalimuni Prisila na Akila, watumishi wenzangu
katika Al-Masihi Isa. 4 Wao walihatarisha maisha yao
kwa ajili yangu; wala si mimi tu ninayewashukuru
bali pia makundi yote ya waumini walio watu wa
Mataifa. 5 Salimuni pia kundi la waumini wanaokutana
nyumbani mwao. Msalimuni rafiki yangu mpendwa
Epaineto, aliyekuwa mtu wa kwanza kumwamini Al-
Masihi huko jimbo la Asia. 6 Msalimuni Mariamu,
aliyefanya kazi kwa bidii kwa ajili yenu. 7 Wasalimuni
Androniko na Yunia, jamaa zangu ambao wamekuwa
gerezani pamoja nami. Wao ni maarufu miongoni mwa
mitume, nao walikuwa katika Al-Masihi kabla yangu.
8 Msalimuni Ampliato, yeye nimpendaye katika Bwana
Isa. 9 Msalimuni Urbano, mtendakazi mwenzetu katika
Al-Masihi, pamoja na rafiki yangu mpendwa Stakisi.
10 Msalimuni Apele aliyejaribiwa na akaithibitisha
imani yake katika Al-Masihi. Wasalimuni wote walio
nyumbani mwa Aristobulo. 11 Msalimuni ndugu yangu
Herodioni. Wasalimuni wote walio nyumbani mwa
Narkiso walio katika Bwana Isa. 12 Wasalimuni
Trifaina na Trifosa, wale wanawake wanaofanya kazi
kwa bidii katika Bwana Isa. Msalimuni rafiki yangu
mpendwa Persisi, mwanamke mwingine aliyefanya
kazi kwa bidii katika Bwana Isa. 13 Msalimuni Rufo,
mteule katika Bwana Isa, pamoja na mama yake,
ambaye amekuwa mama kwangu pia. 14 Wasalimuni
Asinkrito, Flegoni, Herme, Patroba, Herma na ndugu
wote walio pamoja nao. 15 Wasalimuni Filologo, Yulia,
Nerea na dada yake, na Olimpa na watakatifu wote
walio pamoja nao. 16 Salimianeni kwa busu takatifu.
Makundi yote ya waumini ya Al-Masihi wanawasalimu.
17 Ndugu zangu, nawasihi mjihadhari na kujiepusha
na wale watu waletao matengano na kuweka vikwazo
mbele yenu dhidi ya mafundisho mliyojifunza. 18 Kwa
maana watu kama hao hawamtumikii Bwana wetu Al-
Masihi, bali wanatumikia tamaa zao wenyewe. Kwa
kutumia maneno laini na ya kubembeleza, hupotosha

mioyo ya watu wajinga. 19 Kila mtu amesikia kuhusu
utii wenu, nami nimejawa na furaha tele kwa ajili
yenu. Lakini nataka mwe na hekima katika mambo
mema na bila hatia katika mambo maovu. 20 Mungu
wa amani atamponda Shetani chini ya miguu yenu
upesi. Neema ya Bwana wetu Isa iwe nanyi. Amen.
21 Timotheo, mtendakazi mwenzangu anawasalimu.
Vivyo hivyo Lukio, Yasoni, na Sosipatro, ndugu zangu.
22 Mimi, Tertio, niliye mwandishi wa waraka huu,
nawasalimu katika Bwana Isa. 23 Gayo, ambaye
ni mwenyeji wangu na wa kundi lote la waumini,
anawasalimu. Erasto, mweka hazina wa mji huu,
pamoja na Kwarto ndugu yetu, pia wanawasalimu. [
24 Neema ya Bwana wetu Isa Al-Masihi iwe pamoja
nanyi nyote. Amen.] 25 Sasa atukuzwe yeye awezaye
kuwafanya imara kwa Injili yangu na kuhubiriwa kwa
Isa Al-Masihi, kutokana na kufunuliwa siri zilizofichika
tangu zamani za kale. **(aiōnios g166)** 26 Lakini sasa
siri hiyo imefunuliwa na kujulikana kupitia maandiko
ya kinabii kutokana na amri ya Mungu wa milele, ili
mataifa yote yaweze kumwamini na kumtii: **(aiōnios
g166)** 27 ndiye Mungu, aliye pekee mwenye hekima,
ambaye kupitia kwa Isa Al-Masihi utukufu ni wake
milele na milele! Amen. **(aiōn g165)**

# 1 Wakorintho

**1** Paulo, niliyeitwa kwa mapenzi ya Mungu kuwa
mtume wa Al-Masihi Isa, na Sosthene ndugu
yetu. 2 Kwa kundi la waumini wa Mungu walioko
Korintho, kwa wale waliotakaswa katika Al-Masihi
Isa na walioitwa kuwa watakatifu, pamoja na wale
wote ambao kila mahali wanaliitia Jina la Al-Masihi
Isa Bwana wetu, aliye Bwana wao na wetu pia. 3
Neema na amani zinazotoka kwa Mungu, Baba yetu,
na kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi ziwe nanyi. 4
Ninamshukuru Mungu siku zote kwa ajili yenu kwa
sababu ya neema yake mliyopewa katika Al-Masihi
Isa. 5 Kwa kuwa katika Al-Masihi mmetajirishwa kwa
kila hali, katika kusema kwenu na katika maarifa
yenu yote, 6 kwa sababu ushuhuda wetu kumhusu
Al-Masihi ulithibitishwa ndani yenu. 7 Kwa hiyo
hamkupungukiwa na karama yoyote ya kiroho wakati
mnangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa Bwana
wetu Isa Al-Masihi. 8 Atawafanya imara hadi mwisho,
ili msiwe na hatia siku ile ya Bwana wetu Isa Al-
Masihi. 9 Mungu ambaye mmeitwa naye ili mwe na
ushirika na Mwanawe Isa Al-Masihi, Bwana wetu ni
mwaminifu. 10 Nawasihi ndugu zangu, katika Jina
la Bwana wetu Isa Al-Masihi, kwamba mpatane nia
zenu ninyi kwa ninyi, ili pasiwepo na matengano kati
yenu, na kwamba mwe na umoja kikamilifu katika
nia na katika kusudi. 11 Ndugu zangu, nimepata
habari kutoka kwa baadhi ya watu wa nyumbani mwa
Kloe kwamba kuna magomvi kati yenu. 12 Maana
yangu ni kwamba: Mmoja wenu husema, “Mimi ni
wa Paulo”; mwingine, “Mimi ni wa Apolo”; mwingine,
“Mimi ni wa Kefa”; na mwingine, “Mimi ni wa Al-
Masihi.” 13 Je, Al-Masihi amegawanyika? Je, Paulo
ndiye alisulubishwa kwa ajili yenu? Je, mlibatizwa kwa
jina la Paulo? 14 Nashukuru kwamba sikumbatiza
mtu yeyote isipokuwa Krispo na Gayo. 15 Kwa hiyo
hakuna mtu yeyote anayeweza kusema kwamba
alibatizwa kwa jina langu. 16 (Naam, niliwabatiza
pia watu wa nyumbani mwa Stefana; lakini zaidi ya
hao sijui kama nilimbatiza mtu mwingine yeyote.)
17 Kwa maana Al-Masihi hakunituma ili kubatiza
bali kuhubiri Injili; sio kwa maneno ya hekima ya
kibinadamu, ili msalaba wa Al-Masihi usije ukakosa
nguvu yake. 18 Kwa maana ujumbe wa msalaba
kwa wale wanaopotea ni upuzi, lakini kwetu sisi
tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. 19 Kwa maana
imeandikwa: “Nitaiharibu hekima ya wenye hekima, na
kubatilisha akili ya wenye akili.” 20 Yuko wapi mwenye
hekima? Yuko wapi msomi? Yuko wapi mwanafalsafa
wa nyakati hizi? Je, Mungu hakufanya hekima ya
ulimwengu huu kuwa upumbavu? **(aiōn g165)** 21 Kwa
kuwa katika hekima ya Mungu ulimwengu kwa hekima
yake haukumjua yeye, ilimpendeza Mungu kuwaokoa
walioamini kwa upuzi wa lile neno lililohubiriwa. 22
Wayahudi wanadai ishara za miujiza na Wayunani
wanatafuta hekima. 23 Lakini sisi tunamhubiri Al-
Masihi aliyesulubiwa: yeye kwa Wayahudi ni kikwazo
na kwa Wayunani ni upuzi. 24 Lakini kwa wale ambao
Mungu amewaita, Wayahudi na pia Wayunani, Al-
Masihi ndiye nguvu ya Mungu na pia hekima ya
Mungu. 25 Kwa maana upumbavu wa Mungu una
hekima zaidi ya hekima ya wanadamu, nao udhaifu
wa Mungu una nguvu kuliko nguvu ya wanadamu. 26
Ndugu zangu, kumbukeni mlivyokuwa mlipoitwa. Kwa
kipimo cha kibinadamu, si wengi wenu mliokuwa na
hekima. Si wengi mliokuwa na ushawishi, si wengi
mliozaliwa katika vyeo. 27 Lakini Mungu alivichagua
vitu vipumbavu vya ulimwengu ili awaaibishe wenye
hekima; Mungu alivichagua vitu dhaifu vya ulimwengu
ili awaaibishe wenye nguvu. 28 Alivichagua vitu vya
chini na vinavyodharauliwa vya dunia hii, vitu ambavyo
haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko, 29 ili mtu yeyote
asijisifu mbele zake. 30 Bali kwa yeye ninyi mmepata
kuwa katika Al-Masihi Isa, aliyefanyika kwetu hekima
inayotoka kwa Mungu, yaani haki yetu, na utakatifu
na ukombozi. 31 Hivyo, kama ilivyoandikwa: “Yeye
ajisifuye na ajisifu katika Mwenyezi Mungu.”

**2** Ndugu zangu nilipokuja kwenu, sikuja na maneno
ya ushawishi wala hekima ya hali ya juu
nilipowahubiria siri ya Mungu. 2 Kwa kuwa niliamua
kutokujua kitu chochote nilipokuwa nanyi, isipokuwa
Isa Al-Masihi aliyesulubiwa. 3 Mimi nilikuja kwenu
nikiwa dhaifu na mwenye hofu na kwa kutetemeka
sana. 4 Kuhubiri kwangu na ujumbe wangu haukuwa
kwa hekima na maneno ya ushawishi, bali kwa
madhihirisho ya nguvu za Roho wa Mungu, 5 ili imani
yenu isiwe imejengwa katika hekima ya wanadamu
bali katika nguvu za Mungu. 6 Lakini miongoni mwa
watu waliokomaa twanena hekima, wala si hekima
ya ulimwengu huu au ya watawala wa dunia hii
wanaobatilika. **(aiōn g165)** 7 Sisi tunanena hekima

ya Mungu ambayo ni siri, tena iliyofichika, ambayo
Mungu aliikusudia kabla ya ulimwengu kuumbwa,
kwa ajili ya utukufu wetu. (aiōn g165) 8 Hakuna hata
mtawala mmoja wa nyakati hizi aliyeelewa jambo hili.
Kwa maana kama wangeelewa, hawangemsulubisha
Bwana wa utukufu. (aiōn g165) 9 Lakini ni kama
ilivyoandikwa: “Hakuna jicho limepata kuona, wala
sikio limepata kusikia, wala hayakuingia moyoni
mwa mwanadamu yeyote, mambo ambayo Mungu
amewaandalia wale wanaompenda”: 10 Lakini mambo
haya Mungu ametufunulia kwa Roho wake. Roho
huchunguza kila kitu, hata mambo ya ndani sana ya
Mungu. 11 Kwa maana ni nani anayejua mawazo ya
mtu isipokuwa roho iliyo ndani ya huyo mtu? Vivyo
hivyo hakuna mtu ajuaye mawazo ya Mungu isipokuwa
Roho Mtakatifu wa Mungu. 12 Basi hatukupokea roho
ya dunia bali Roho atokaye kwa Mungu, ili tuweze
kuelewa kile kipawa ambacho Mungu ametupatia
bure. 13 Haya ndio tusemayo, si kwa maneno
tuliyofundishwa kwa hekima ya wanadamu bali kwa
maneno tuliyofundishwa na Roho, tukifafanua kweli za
kiroho kwa maneno ya kiroho. 14 Mtu ambaye hana
Roho hawezi kupokea mambo yanayotoka kwa Roho
wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi
kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa
upambanuzi wa rohoni. 15 Mtu wa kiroho hubainisha
mambo yote, lakini yeye mwenyewe habainishwi na
mtu yeyote. 16 “Kwa maana ni nani aliyefahamu
mawazo ya Mwenyezi Mungu ili apate kumfundisha?”
Lakini sisi tunayo mawazo ya Al-Masihi.

**3** Ndugu zangu, mimi sikuweza kusema nanyi kama
watu wa kiroho, bali kama watu wa mwilini, kama
watoto wachanga katika Al-Masihi. 2 Niliwanywesha
maziwa, wala si chakula kigumu, kwa kuwa hamkuwa
tayari kwa hicho chakula. Naam, hata sasa hamko
tayari. 3 Ninyi bado ni watu wa mwilini. Kwa kuwa
bado kuna wivu na magombano miongoni mwenu, je,
ninyi si watu wa mwilini? Je, si mwaendelea kama
watu wa kawaida? 4 Kwa maana mmoja anaposema,
“Mimi ni wa Paulo,” na mwingine, “Mimi ni wa Apolo,”
je, ninyi si wanadamu wa kawaida? 5 Kwani, Apolo ni
nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi tu ambao
kupitia wao mliamini, kama vile Bwana Isa alivyompa
kila mtu huduma yake. 6 Mimi nilipanda mbegu,
Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliikuza. 7
Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si
kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue. 8
Apandaye mbegu ana lengo sawa na yule atiaye maji
na kila mmoja atalipwa kulingana na kazi yake. 9
Kwa kuwa sisi tu watendakazi pamoja na Mungu.
Ninyi ni shamba la Mungu, jengo la Mungu. 10 Kwa
neema Mungu aliyonipa, niliweka msingi kama mjenzi
stadi na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila
mmoja inampasa awe mwangalifu jinsi anavyojenga.
11 Kwa maana hakuna mtu yeyote awezaye kuweka
msingi mwingine wowote isipokuwa ule uliokwisha
kuwekwa, ambao ni Isa Al-Masihi. 12 Kama mtu
yeyote akijenga juu ya msingi huu kwa kutumia
dhahabu, fedha, vito vya thamani, miti, majani au
nyasi, 13 kazi yake itaonekana ilivyo, kwa kuwa Siku
ile itaidhihirisha. Itadhihirishwa kwa moto, nao moto
utapima ubora wa kazi ya kila mtu. 14 Kama kile
alichojenga kitabaki, atapokea thawabu yake. 15
Kama kitateketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe
ataokolewa, lakini tu kama mtu aliyenusurika kwenye
moto. 16 Je, hamjui kwamba ninyi wenyewe ni hekalu
la Mungu na kwamba Roho wa Mungu anakaa ndani
yenu? 17 Kama mtu yeyote akiliharibu hekalu la
Mungu, Mungu atamwangamiza; kwa maana hekalu
la Mungu ni takatifu, na ninyi ndio hilo hekalu. 18
Msijidanganye. Kama mtu yeyote miongoni mwenu
akidhani kuwa ana hekima kwa viwango vya dunia
hii, inampasa awe mjinga ili apate kuwa na hekima.
(aiōn g165) 19 Kwa maana hekima ya ulimwengu huu ni
upuzi mbele za Mungu. Kama ilivyoandikwa: “Mungu
huwanasa wenye hekima katika hila yao,” 20 tena,
“Mwenyezi Mungu anajua kwamba mawazo ya wenye
hekima ni ubatili.” 21 Hivyo basi, mtu asijivune kuhusu
wanadamu! Vitu vyote ni vyenu, 22 iwe ni Paulo au
Apolo au Kefa, au dunia au uzima au mauti, au wakati
uliopo au ujao: haya yote ni yenu, 23 na ninyi ni wa
Al-Masihi, naye Al-Masihi ni wa Mungu.

**4** Basi, watu na watuhesabu sisi kuwa tu watumishi
wa Al-Masihi na mawakili wa siri za Mungu.
2 Tena, litakiwalo ni mawakili waonekane kuwa
waaminifu. 3 Lakini kwangu mimi ni jambo dogo
sana kwamba nihukumiwe na ninyi au na mahakama
yoyote ya kibinadamu. Naam, hata mimi mwenyewe
sijihukumu. 4 Dhamiri yangu ni safi, lakini hilo
halinihesabii kuwa asiye na hatia. Bwana Isa ndiye
anihukumuye. 5 Kwa hiyo msihukumu jambo lolote
kabla ya wakati wake. Ngojeni hadi Bwana Isa

atakapokuja. Yeye atayaleta nuruni mambo yale
yaliyofichwa gizani, na kuweka wazi nia za mioyo
ya wanadamu. Wakati huo kila mmoja atapokea
sifa anayostahili kutoka kwa Mungu. 6 Basi ndugu
zangu, mambo haya nimeyafanya kwangu binafsi
na Apolo kwa faida yenu, ili mweze kujifunza kutoka
kwetu maana ya ule usemi usemao, “Msivuke zaidi
ya yale yaliyoandikwa.” Hivyo hamtajivunia mtu fulani
na kumdharau mwingine. 7 Kwa maana ni nani
aliyewafanya kuwa tofauti na wengine? Ni nini mlicho
nacho ambacho hamkupokea? Nanyi kama mlipokea,
kwa nini mnajivuna kama vile hamkupokea? 8 Sasa
tayari mnayo yale yote mnayohitaji! Tayari mmekwisha
kuwa matajiri! Mmekuwa wafalme, tena bila sisi!
Laiti mngekuwa wafalme kweli ili na sisi tupate
kuwa wafalme pamoja nanyi! 9 Kwa maana ninaona
kwamba Mungu ametuweka sisi mitume katika nafasi
ya mwisho kabisa, kama watu waliohukumiwa kufa
kwenye uwanja wa tamasha, kwa sababu tumefanywa
kuwa maonesho kwa ulimwengu wote, kwa malaika
na kwa wanadamu pia. 10 Kwa ajili ya Al-Masihi
sisi ni wajinga, lakini ninyi mna hekima sana ndani
ya Al-Masihi. Sisi tu dhaifu, lakini ninyi mna nguvu.
Tunadharauliwa, lakini ninyi mnaheshimiwa. 11 Hadi
saa hii tuna njaa na kiu, tu uchi, tumepigwa na hatuna
makao. 12 Tunafanya kazi kwa bidii kwa mikono yetu
wenyewe. Tunapolaaniwa, tunabariki; tunapoteswa,
tunastahimili; 13 tunaposingiziwa, tunajibu kwa upole.
Hadi sasa tumekuwa kama takataka ya dunia na
uchafu wa ulimwengu. 14 Siwaandikii mambo haya
ili kuwaaibisha, bali ili kuwaonya, kama wanangu
wapendwa. 15 Hata kama mnao walimu elfu kumi
katika Al-Masihi, lakini hamna baba wengi. Mimi
nilikuwa baba yenu katika Al-Masihi Isa kwa kuwaletea
Injili. 16 Basi nawasihi igeni mfano wangu. 17
Kwa sababu hii ninamtuma Timotheo, mwanangu
mpendwa na mwaminifu katika Bwana Isa. Yeye
atawakumbusha kuhusu njia za maisha yangu katika
Al-Masihi Isa, ambayo yanakubaliana na mafundisho
yangu ninayofundisha katika kila kundi la waumini.
18 Baadhi yenu mmekuwa na jeuri mkidhani kuwa
sitafika kwenu. 19 Lakini kama Bwana Isa akipenda,
nitafika kwenu hivi karibuni, nami nitajua, si tu kile
wanachosema hawa watu jeuri, bali pia nguvu yao.
20 Kwa kuwa ufalme wa Mungu si maneno matupu
tu bali ni nguvu. 21 Ninyi amueni. Je, nije kwenu na
fimbo, au nije kwa upendo na kwa roho ya upole?

5 Yamkini habari imeenea ya kuwa miongoni mwenu
kuna uzinzi ambao haujafanyika hata miongoni
mwa watu wasiomjua Mungu: Kwamba mtu anaishi
na mke wa baba yake. 2 Nanyi mwajivuna! Je,
haiwapasi kuhuzunika na kumtenga na ushirika wenu
mtu huyo aliyefanya mambo hayo? 3 Hata kama siko
pamoja nanyi katika mwili, niko nanyi katika roho.
Nami nimekwisha kumhukumu mtu huyo aliyetenda
jambo hili, kama vile ningekuwepo. 4 Mnapokutana
katika Jina la Bwana wetu Isa nami nikiwepo pamoja
nanyi katika roho, na uweza wa Bwana Isa ukiwepo,
5 mkabidhini mtu huyu kwa Shetani, ili mwili wake
uharibiwe, lakini roho yake iokolewe katika siku ya
Mwenyezi Mungu. 6 Majivuno yenu si mazuri. Je,
hamjui kwamba chachu kidogo huchachusha donge
zima la unga? 7 Ondoeni chachu ya kale ili mpate
kuwa donge jipya lisilotiwa chachu, kama vile mlivyo.
Kwa maana Al-Masihi, Mwana-Kondoo wetu wa
Pasaka amekwisha tolewa kuwa dhabihu. 8 Kwa hiyo,
tusiiadhimishe sikukuu hii kwa chachu ya zamani,
chachu ya nia mbaya na uovu, bali kwa mkate
usiotiwa chachu, ndio weupe wa moyo na kweli. 9
Niliwaandikia katika waraka wangu kuwa msishirikiane
na wazinzi. 10 Sina maana kwamba msishirikiane na
wazinzi wa ulimwengu huu, au wenye tamaa mbaya,
wanyang’anyi au waabudu sanamu. Kwa kufanya
hivyo ingewalazimu mtoke ulimwenguni humu. 11
Lakini sasa nawaandikia kwamba msishirikiane na
mtu yeyote anayejiita ndugu, hali akiwa ni mzinzi,
au mwenye tamaa mbaya, mwabudu sanamu au
msingiziaji, mlevi au mdhalimu. Mtu kama huyo
hata msile naye. 12 Yanihusu nini kuwahukumu
wale watu walio nje ya kundi la waumini? Je, si
mnapaswa kuwahukumu hao walio ndani? 13 Mungu
atawahukumu hao walio nje. “Ninyi mwondoeni huyo
mtu mwovu miongoni mwenu.”

6 Kama mtu yeyote wa kwenu ana ugomvi
na mwenzake, anathubutuje kuupeleka kwa
wasiomcha Mungu ili kuamuliwa badala ya kuupeleka
kwa watakatifu? 2 Je, hamjui kwamba watakatifu
watauhukumu ulimwengu? Nanyi kama mtauhukumu
ulimwengu, je, hamwezi kuamua mambo madogo
madogo? 3 Hamjui kwamba tutawahukumu malaika?

Je, si zaidi mambo ya maisha haya? 4 Kwa hiyo kama
kuna ugomvi miongoni mwenu kuhusu mambo kama
haya, je, mnachagua watu ambao wanaonekana
hata sio wa heshima katika kundi la waumini kuwa
waamuzi kati yenu? 5 Nasema hivi ili mwone aibu.
Je, inawezekana kuwa miongoni mwenu hakuna
mtu mwenye hekima ya kutosha kuamua ugomvi
kati ya waumini? 6 Badala yake ndugu mmoja
anampeleka mwenzake mahakamani, tena mbele ya
watu wasioamini! 7 Huko kuwa na mashtaka miongoni
mwenu ina maana kwamba tayari ni kushindwa
kabisa. Kwa nini msikubali kutendewa mabaya?
Kwa nini msikubali kunyang'anywa? 8 Badala yake,
ninyi wenyewe mwadanganya na kutenda mabaya,
tena mwawatendea ndugu zenu. 9 Je, hamjui
kwamba wasio haki hawataurithi ufalme wa Mungu?
Msidanganyike: Waasherati, wala waabudu sanamu,
wala wazinzi, wala wahanithi, wala walawiti, 10 wala
wezi, wala wenye tamaa mbaya, wala walevi, wala
wanaodhihaki, wala wanyang'anyi hawataurithi ufalme
wa Mungu. 11 Baadhi yenu mlikuwa kama hao. Lakini
mlioshwa, mlitakaswa, mlihesabiwa haki kwa jina
la Bwana Isa Al-Masihi na katika Roho wa Mungu
wetu. 12 "Vitu vyote ni halali kwangu": lakini si vitu
vyote vyenye faida. "Vitu vyote ni halali kwangu":
lakini sitatawaliwa na kitu chochote. 13 "Chakula ni
cha tumbo, na tumbo ni la chakula": lakini Mungu
ataviangamiza vyote viwili. Mwili sio kwa ajili ya zinaa,
bali kwa ajili ya Bwana Isa, na Bwana Isa kwa ajili ya
mwili. 14 Naye Mungu aliyemfufua Bwana Isa kutoka
kwa wafu atatufufua sisi pia kwa uweza wake. 15 Je,
hamjui kwamba miili yenu ni viungo vya Al-Masihi
mwenyewe? Je, nichukue viungo vya mwili wa Al-
Masihi na kuviunganisha na mwili wa kahaba? La
hasha! 16 Hamjui kwamba aliyeungwa na kahaba
anakuwa mwili mmoja naye? Kwa kuwa imenenwa,
"Hao wawili watakuwa mwili mmoja." 17 Lakini mtu
aliyeungwa na Bwana Isa anakuwa roho moja naye.
18 Ikimbieni zinaa. Dhambi zingine zote atendazo mtu
ziko nje ya mwili wake, lakini yeye aziniye hutenda
dhambi ndani ya mwili wake mwenyewe. 19 Je,
hamjui kwamba miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu
wa Mungu akaaye ndani yenu, ambaye mmepewa na
Mungu? Ninyi si mali yenu wenyewe, 20 kwa maana
mmenunuliwa kwa gharama. Kwa hiyo mtukuzeni
Mungu katika miili yenu.

7 Basi kuhusu mambo yale mliyoyaandika: "Ni
vyema mwanaume asimguse mwanamke." 2
Lakini ili kuepuka zinaa, kila mwanaume na awe na
mke wake mwenyewe na kila mwanamke awe na
mume wake mwenyewe. 3 Mume atimize wajibu
wake wa ndoa kwa mkewe, naye vivyo hivyo mke kwa
mumewe. 4 Mwanamke hana mamlaka juu ya mwili
wake bali mumewe, wala mume hana mamlaka juu
ya mwili wake bali mkewe. 5 Msinyimane, isipokuwa
mmekubaliana kufanya hivyo kwa muda, ili mweze
kujitoa kwa maombi. Kisha mrudiane tena, ili Shetani
asije akapata nafasi ya kuwajaribu kwa sababu ya
kutokuwa na kiasi. 6 Nasema haya kama ushauri
na si amri. 7 Laiti watu wangekuwa kama mimi
nilivyo. Lakini kila mtu amepewa kipawa chake kutoka
kwa Mungu, mmoja ana kipawa cha namna hii na
mwingine ana cha namna ile. 8 Kwa wale wasiooa na
kwa wajane, nasema hivi, ingekuwa vizuri wasioe.
9 Lakini kama hawawezi kujizuia, basi waoe na
kuolewa, kwa maana ni afadhali kuoa au kuolewa
kuliko kuwaka tamaa. 10 Kwa wale waliooana nawapa
amri (si mimi, ila ni Bwana Isa): Mke asitengane na
mumewe. 11 Lakini akitengana, ni lazima akae bila
kuolewa, ama sivyo apatane tena na mumewe. Wala
mume asimpe mkewe talaka. 12 Lakini kwa wengine
nasema (si Bwana Isa, ila ni mimi): Kama ndugu ana
mke asiyeamini, naye huyo mke anakubali kuishi
pamoja naye, basi asimwache. 13 Naye mwanamke
aaminiye kama ameolewa na mwanaume asiyeamini
na huyo mume anakubali kuishi naye, basi huyo
mwanamke asimwache. 14 Kwa maana huyo mume
asiyeamini anatakaswa kupitia mkewe, naye mke
asiyeamini anatakaswa kupitia mumewe anayeamini.
Kama haingekuwa hivyo watoto wenu wangakuwa si
safi; lakini ilivyo sasa, wao ni watakatifu. 15 Lakini
kama yule asiyeamini akijitenga, basi afanye hivyo.
Katika hali kama hiyo mwanamke au mwanaume
aaminiye hafungwi, kwa sababu Mungu ametuita
tuishi kwa amani. 16 Wewe mke, unajuaje kama
utamwokoa mumeo? Au wewe mume, unajuaje kama
utamwokoa mkeo? 17 Lakini kila mtu na aishi maisha
aliyopangiwa na Bwana Isa, yale Mungu aliyomwitia.
Hii ni sheria ninayoiweka kwa makundi yote ya
waumini. 18 Je, mtu alikuwa tayari ametahiriwa
alipoitwa? Asijifanye asiyetahiriwa. Je, mtu alikuwa
hajatahiriwa alipoitwa? Asitahiriwe. 19 Kutahiriwa

si kitu, na kutokutahiriwa si kitu. Lakini kuzitii amri
za Mungu ndilo jambo muhimu. 20 Basi kila mtu
na abaki katika hali aliyoitwa nayo. 21 Je, wewe
ulipoitwa ulikuwa mtumwa? Jambo hilo lisikusumbue.
Ingawaje unaweza kupata uhuru, tumia nafasi uliyo
nayo sasa kuliko wakati mwingine wowote. 22 Kwa
maana yeyote aliyeitwa katika Bwana Isa akiwa
mtumwa yeye ni mtu huru kwa Bwana Isa, kama
vile yeyote aliyekuwa huru alipoitwa yeye ni mtumwa
wa Al-Masihi. 23 Mlinunuliwa kwa gharama; msiwe
watumwa wa wanadamu. 24 Ndugu zangu, kama
kila mtu alivyoitwa, akae katika wito wake alioitiwa
na Mungu. 25 Basi, kuhusu wale walio bikira, mimi
sina amri kutoka kwa Bwana Isa, lakini mimi natoa
shauri kama mtu ambaye ni mwaminifu kwa rehema
za Bwana Isa. 26 Kwa sababu ya shida iliyopo
sasa, naona ni vyema mkibaki kama mlivyo. 27 Je,
umeolewa? Basi usitake talaka. Je, hujaoa? Usitafute
mke. 28 Lakini kama ukioa, hujatenda dhambi; na
kama bikira akiolewa, hajatenda dhambi. Lakini wale
wanaooa watakabiliana na matatizo mengi katika
maisha haya, nami nataka kuwazuilia hayo. 29 Lakini
ndugu zangu, nina maana kwamba muda uliobaki ni
mfupi. Tangu sasa wale waliooa waishi kama wasio
na wake; 30 nao wanaoomboleza, kama ambao
hawaombolezi; wenye furaha kama wasiokuwa nayo;
wale wanaonunua, kama vile vitu walivyonunua si
mali yao; 31 nao wale wanaoshughulika na vitu
vya dunia hii, kama ambao hawahusiki navyo. Kwa
maana dunia hii kama tunavyoiona sasa inapita.
32 Ningetaka msiwe na masumbufu. Mwanaume
ambaye hajaoa anajishughulisha na mambo ya
Bwana Isa, jinsi ya kumpendeza Bwana Isa. 33
Lakini mwanaume aliyeoa anajishughulisha na
mambo ya dunia, jinsi ya kumfurahisha mkewe,
34 na mawazo yake yamegawanyika. Mwanamke
asiyeolewa hujishughulisha na mambo ya Bwana:
lengo lake ni awe mtakatifu kimwili na kiroho.
Lakini yule aliyeolewa hujishughulisha na mambo ya
dunia, jinsi atakavyoweza kumfurahisha mumewe.
35 Ninasema haya kwa faida yenu wenyewe, sio
ili kuwawekea vizuizi bali mpate kuishi kwa jinsi
ilivyo vyema bila kuvutwa pengine katika kujitoa
kwenu kwa Bwana Isa. 36 Kama mtu yeyote
anadhani kwamba hamtendei ilivyo sawa mwanamwali
ambaye amemposa, naye akiwa umri wake unazidi
kuendelea na mtu huyo anajisikia kwamba inampasa
kuoa, afanye kama atakavyo. Yeye hatendi dhambi.
Yawapasa waoane. 37 Lakini mwanaume ambaye
ameamua moyoni mwake kutooa bila kulazimishwa
na mtu yeyote, bali anaweza kuzitawala tamaa
zake kutomwoa huyo mwanamwali, basi anafanya
ipasavyo. 38 Hivyo basi, mwanaume amwoaye
mwanamwali afanya vyema, lakini yeye asiyemwoa
afanya vyema zaidi. 39 Mwanamke aliyeolewa
amefungwa na sheria maadamu mumewe yu hai.
Lakini mumewe akifa, basi mwanamke huyo yuko
huru kuolewa na mume mwingine ampendaye, lakini
lazima awe katika Bwana Isa. 40 Lakini kwa maoni
yangu, angekuwa na furaha zaidi akibaki alivyo. Nami
nadhani pia nina Roho wa Mungu.

8 Sasa kuhusu chakula kilichotolewa sadaka kwa
sanamu, tunajua kwamba “sisi sote tuna ujuzi.”
Lakini ujuzi hujivuna, bali upendo hujenga. 2 Mtu
yeyote anayedhani kwamba anajua kitu, bado hajui
kama impasavyo kujua. 3 Lakini mtu ampendaye
Mungu, hujulikana naye Mungu. 4 Hivyo basi, kuhusu
kula chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu:
Tunajua kwamba “Sanamu si kitu chochote kabisa
duniani,” na kwamba “Kuna Mungu mmoja tu.” 5
Kwa kuwa hata kama wapo hao wanaoitwa miungu,
wakiwa mbinguni au duniani (kama ilivyo kweli wapo
“miungu” wengi na “mabwana” wengi), 6 kwetu sisi
yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote
vyatoka kwake na kwa ajili yake sisi twaishi; na kuna
Bwana mmoja tu, Isa Al-Masihi, ambaye kwa yeye vitu
vyote vilitoka na kwa yeye tunaishi. 7 Lakini si wote
wanaojua jambo hili. Baadhi ya watu bado wamezoea
sanamu kuwa halisi hivi kwamba wanapokula chakula
kama hicho wanadhani kimetolewa sadaka kwa
sanamu na kwa kuwa dhamiri zao ni dhaifu, dhamiri
yao inanajisika. 8 Lakini chakula hakituleti karibu
na Mungu, wala hatupotezi chochote tusipokula,
wala hatuongezi chochote tukila. 9 Lakini angalieni
jinsi mnavyotumia uhuru wenu usije ukawa kikwazo
kwao walio dhaifu. 10 Kwa maana kama mtu yeyote
mwenye dhamiri dhaifu akiwaona ninyi wenye ujuzi
huu mkila katika hekalu la sanamu, je, si atatiwa moyo
kula chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu? 11
Kwa njia hiyo, huyo ndugu mwenye dhamiri dhaifu,
ambaye Al-Masihi alikufa kwa ajili yake, ataangamia
kwa sababu ya ujuzi wenu. 12 Mnapotenda dhambi

dhidi ya ndugu zenu kwa njia hii na kujeruhi dhamiri zao zilizo dhaifu, mnamkosea Al-Masihi. 13 Kwa hiyo, kama kile ninachokula kitamfanya ndugu yangu aanguke katika dhambi, sitakula nyama kamwe, nisije nikamfanya ndugu yangu aanguke. **(aiōn g165)**

**9** Je, mimi si huru? Je, mimi si mtume? Je, mimi sikumwona Isa, Bwana wetu? Je, ninyi si matunda ya kazi yangu katika Bwana? 2 Hata kama mimi si mtume kwa wengine, hakika mimi ni mtume kwenu, kwa maana ninyi ni muhuri wa utume wangu katika Bwana Isa. 3 Huu ndio utetezi wangu kwa hao wanaokaa kunihukumu. 4 Je, hatuna haki ya kula na kunywa? 5 Je, hatuna haki ya kusafiri na mke anayeamini, kama wanavyofanya mitume wengine na ndugu zake Bwana Isa na Kefa? 6 Au ni mimi na Barnaba tu inatubidi kufanya kazi ili tuweze kupata mahitaji yetu? 7 Ni askari yupi aendaye vitani kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye shamba la mizabibu na asile matunda yake? Ni nani achungaye kundi na asipate maziwa yake. 8 Je, nasema mambo haya katika mtazamo wa kibinadamu tu? Je, Torati haisemi vivyo hivyo? 9 Kwa maana imeandikwa katika Torati ya Musa: "Usimfunge maksai kinywa apurapo nafaka." Je, Mungu hapa anahusika na ng'ombe? 10 Je, Mungu hasemi haya hasa kwa ajili yetu? Hakika yameandikwa kwa ajili yetu, kwa sababu mtu anapolima na mpuraji akapura nafaka, wote wanapaswa kufanya hivyo wakiwa na tumaini la kushiriki mavuno. 11 Je, ikiwa sisi tulipanda mbegu ya kiroho miongoni mwenu, itakuwa ni jambo kubwa iwapo tutavuna vitu vya mwili kutoka kwenu? 12 Kama wengine wana haki ya kupata msaada kutoka kwenu, isingepasa tuwe na haki hiyo hata zaidi? Lakini sisi hatukutumia haki hii. Kinyume chake, tunavumilia kila kitu ili tusije tukazuia Injili ya Al-Masihi. 13 Je, hamjui kwamba, watu wafanyao kazi hekaluni hupata chakula chao kutoka hekaluni, nao wale wahudumiao madhabahuni hushiriki kile kitolewacho madhabahuni? 14 Vivyo hivyo, Bwana Isa ameamuru kwamba wale wanaohubiri Injili wapate riziki yao kutokana na Injili. 15 Lakini sijatumia hata mojawapo ya haki hizi. Nami siandiki haya nikitumaini kwamba mtanifanyia mambo hayo. Heri nife kuliko mtu yeyote kuninyima huku kujisifu kwangu. 16 Lakini ninapohubiri Injili siwezi kujisifu maana ninalazimika kuhubiri. Ole wangu nisipoihubiri Injili! 17 Nikihubiri kwa hiari, ninayo thawabu. Lakini kama si kwa hiari, basi ninachofanya ni kutekeleza tu uwakili niliowekewa. 18 Basi je, thawabu yangu ni nini? Thawabu yangu ni hii: Ya kwamba katika kuhubiri Injili niitoe bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika Injili. 19 Ingawa mimi ni huru, wala si mtumwa wa mtu yeyote, nimejifanya mtumwa wa kila mtu, ili niweze kuwavuta wengi kadiri iwezekanavyo. 20 Kwa Wayahudi, nilikuwa kama Myahudi, ili niwapate Wayahudi. Kwa watu wale walio chini ya Torati, nilikuwa kama aliye chini ya Torati (ingawa mimi siko chini ya Torati), ili niweze kuwapata wale walio chini ya Torati. 21 Kwa watu wasio na Torati nilikuwa kama asiye na Torati (ingawa siko huru mbali na Torati ya Mungu, bali niko chini ya sheria ya Al-Masihi), ili niweze kuwapata wale wasio na sheria. 22 Kwa walio dhaifu nilikuwa dhaifu, ili niweze kuwapata walio dhaifu. Nimekuwa mtu wa hali zote kwa watu wote ili kwa njia yoyote niweze kuwaokoa baadhi yao. 23 Nafanya haya yote kwa ajili ya Injili, ili nipate kushiriki baraka zake. 24 Je, hamjui kwamba katika mashindano ya mbio wote wanaoshindana hukimbia, lakini ni mmoja wao tu apewaye tuzo? Kwa hiyo kimbieni katika mashindano ili mkapata tuzo. 25 Kila mmoja anayeshiriki katika mashindano hufanya mazoezi makali. Wao hufanya hivyo ili wapokee taji lisilodumu, lakini sisi tunafanya hivyo ili kupata taji linalodumu milele. 26 Kwa hiyo mimi sikimbii kama mtu akimbiaye bila lengo, sipigani kama mtu anayepiga hewa. 27 La, bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha, ili nikiisha kuwahubiria wengine, nisije nikakataliwa.

**10** Ndugu zangu, sitaki mkose kufahamu ukweli huu kwamba baba zetu walikuwa wote chini ya wingu na kwamba wote walipita katikati ya bahari. 2 Wote wakabatizwa kuwa wa Musa ndani ya lile wingu na ndani ya ile bahari. 3 Wote walikula chakula kile kile cha roho, 4 na wote wakanywa kile kile kinywaji cha roho, kwa maana walikunywa kutoka ule mwamba wa roho uliofuatana nao, nao ule mwamba ulikuwa Al-Masihi. 5 Lakini Mungu hakupendezwa na wengi wao, kwa hiyo miili yao ilitapakaa jangwani. 6 Basi mambo haya yalifanyika kama mifano ili kutuzuia tusiweke mioyo yetu katika mambo maovu kama wao walivyofanya. 7 Msiwe waabudu sanamu, kama baadhi yao walivyokuwa,

kama ilivyoandikwa, “Watu waliketi chini kula na
kunywa, kisha wakainuka kucheza na kufanya sherehe
za kipagani.” 8 Wala tusifanye uzinzi kama baadhi yao
walivyofanya, wakafa watu elfu ishirini na tatu kwa
siku moja. 9 Wala tusimjaribu Al-Masihi, kama baadhi
yao walivyofanya, wakafa kwa kuumwa na nyoka.
10 Msinung’unike kama baadhi yao walivyofanya,
wakaangamizwa na malaika mharibifu. 11 Mambo
haya yote yaliwapata wao ili yawe mifano kwa
wengine, nayo yaliandikwa ili yatuonye sisi ambao
mwisho wa nyakati umetufikia. **(aiōn g165)** 12 Hivyo,
yeye ajidhaniaye amesimama, aangalie asianguke.
13 Hakuna jaribu lolote lililowapata ambalo si la
kawaida kwa wanadamu. Naye Mungu ni mwaminifu;
hataruhusu mjaribiwe kupita mnavyoweza. Lakini
mnapojaribiwa atawapa njia ya kushinda ili mweze
kustahimili. 14 Kwa hiyo wapendwa wangu, zikimbieni
ibada za sanamu. 15 Nasema watu wenye ufahamu,
amueni wenyewe kuhusu haya niyasemayo. 16 Je,
kikombe cha baraka ambacho tunakibariki, si ushirika
katika damu ya Al-Masihi? Mkate tunaoumega, si
ushirika wa mwili wa Al-Masihi? 17 Kwa kuwa mkate
ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja, kwa kuwa
wote twashiriki mkate mmoja. 18 Waangalieni watu
wa Israeli: Je, wale wote walao dhabihu si ni wale
watendao kazi madhabahuni? 19 Je, nina maana
kwamba sadaka iliyotolewa kwa sanamu ni kitu
chenye maana yoyote? Au kwamba sanamu ni kitu
chenye maana yoyote? 20 La hasha! Lakini sadaka
za watu wasiomjua Mungu hutolewa kwa mashetani,
wala si kwa Mungu. Nami sitaki ninyi mwe na ushirika
na mashetani. 21 Hamwezi kunywa katika kikombe
cha Bwana Isa na cha mashetani pia. Hamwezi kuwa
na sehemu katika Chakula cha Bwana Isa na katika
chakula cha mashetani pia. 22 Je, tunataka kuamsha
wivu wa Mwenyezi Mungu? Je, sisi tuna nguvu kuliko
yeye? 23 “Vitu vyote ni halali,” lakini si vitu vyote
vilivyo na faida. “Vitu vyote ni halali,” lakini si vyote
vinavyojenga. 24 Mtu yeyote asitafute yaliyo yake
mwenyewe, bali kila mtu atafute yale yanayowafaa
wengine. 25 Kuleni chochote kinachouzwa sokoni,
bila kuuliza swali lolote kwa ajili ya dhamiri. 26
Kwa maana, “Dunia na vyote vilivyomo ni mali ya
Mwenyezi Mungu.” 27 Ukikaribishwa chakula na mtu
asiyeamini nawe ukikubali kwenda, kula kila kitu
kitakachowekwa mbele yako bila kuuliza maswali
kwa ajili ya dhamiri. 28 Lakini kama mtu yeyote
akikuambia, “Hiki kimetolewa sadaka kwa sanamu,”
basi usikile kwa ajili ya huyo aliyekuambia na kwa
ajili ya dhamiri. 29 Nina maana dhamiri ya huyo
aliyekuambia, wala si kwa ajili ya dhamiri yako. Lakini
kwa nini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya
mtu mwingine? 30 Nikila kwa shukrani, kwa nini
nashutumiwa kwa ajili ya kile ambacho ninamshukuria
Mungu? 31 Basi, lolote mfanyalo, kama ni kula au
kunywa, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu. 32
Msiwe kikwazo kwa mtu yeyote, wawe Wayahudi au
Wayunani, au kwa kundi la waumini la Mungu, 33
kama hata mimi ninavyojaribu kumpendeza kila mtu
kwa kila namna. Kwa maana sitafuti mema kwa ajili
yangu mwenyewe bali kwa ajili ya wengi, ili waweze
kuokolewa.

**11** Igeni mfano wangu, kama ninavyouiga mfano
wa Al-Masihi. 2 Ninawasifu kwa kunikumbuka
katika kila jambo na kwa kushika mapokeo kama
nilivyowapatia. 3 Napenda mfahamu kwamba kichwa
cha kila mwanaume ni Al-Masihi, na kichwa cha
mwanamke ni mwanaume, nacho kichwa cha Al-
Masihi ni Mungu. 4 Kila mwanaume anayeomba
au kutoa unabii akiwa amefunika kichwa chake,
anakiaibisha kichwa chake. 5 Naye kila mwanamke
anayeomba au kutoa unabii pasipo kufunika kichwa
chake, anakiaibisha kichwa chake, kwani ni sawa
na yeye aliyenyoa nywele. 6 Kama mwanamke
hatajifunika kichwa chake, basi inampasa kunyoa
nywele zake. Lakini kama ni aibu kwa mwanamke
kukata au kunyoa nywele zake, basi afunike kichwa
chake. 7 Haimpasi mwanaume kufunika kichwa chake
kwa kuwa yeye ni mfano wa Mungu na utukufu wa
Mungu; lakini mwanamke ni utukufu wa mwanaume.
8 Kwa maana mwanaume hakutoka kwa mwanamke,
bali mwanamke alitoka kwa mwanaume. 9 Wala
mwanaume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke,
bali mwanamke kwa ajili ya mwanaume. 10 Kwa
sababu hii na kwa sababu ya malaika, inampasa
mwanamke awe na ishara ya mamlaka juu yake.
11 Lakini katika Bwana Isa, mwanamke hajitegemei
pasipo mwanaume na mwanaume hajitegemei pasipo
mwanamke. 12 Kama vile mwanamke alivyoumbwa
kutoka kwa mwanaume, vivyo hivyo mwanaume
huzaliwa na mwanamke. Lakini vitu vyote vyatoka kwa
Mungu. 13 Hukumuni ninyi wenyewe: Je, inafaa kwa

mwanamke kumwomba Mungu bila kufunika kichwa
chake? 14 Je, maumbile ya asili hayatufundishi kuwa ni
aibu kwa mwanaume kuwa na nywele ndefu? 15 Lakini
mwanamke akiwa na nywele ndefu ni utukufu kwake?
Kwa maana mwanamke amepewa nywele ndefu ili
kumfunika. 16 Kama mtu anataka kubishana kuhusu
jambo hili, sisi wala makundi ya waumini ya Mungu
hatutambui desturi nyingine. 17 Basi katika maagizo
yafuatayo, siwezi kuwasifu, kwa sababu mkutanikapo
si kwa ajili ya faida bali kwa hasara. 18 Kwanza,
mnapokutana kama kundi la waumini, nasikia kwamba
kuna mgawanyiko miongoni mwenu, nami kwa kiasi
fulani nasadiki kuwa ndivyo ilivyo. 19 Bila shaka
lazima pawe na tofauti miongoni mwenu ili kuonesha
ni nani anayekubaliwa na Mungu. 20 Mkutanikapo
pamoja si Chakula cha Bwana Isa mnachokula, 21
kwa kuwa mnapokula, kila mmoja wenu anakula bila
kuwangoja wengine. Mmoja hukaa njaa na mwingine
analewa. 22 Je, hamna nyumbani kwenu ambako
mnaweza kula na kunywa? Au mnalidharau kundi la
waumini la Mungu na kuwadhalilisha wale wasio na
kitu? Niwaambie nini? Je, niwasifu kuhusu jambo hili?
La, hasha! 23 Kwa maana mimi nilipokea kutoka kwa
Bwana Isa yale niliyowapa ninyi, kwamba Bwana Isa,
usiku ule aliposalitiwa, alitwaa mkate, 24 naye baada
ya kushukuru, akaumega, akasema, “Huu ndio mwili
wangu, uliotolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa
ukumbusho wangu.” 25 Vivyo hivyo baada ya kula,
akakitwaa kikombe, akisema, “Kikombe hiki ni agano
jipya katika damu yangu. Fanyeni hivi kila mnywapo,
kwa ukumbusho wangu.” 26 Maana kila mlapo mkate
huu na kunywea kikombe hiki, mnatangaza mauti
ya Bwana Isa hadi ajapo. 27 Kwa hiyo, mtu yeyote
alaye mkate huo au kukinywea kikombe hicho cha
Bwana Isa isivyostahili, atakuwa na hatia ya dhambi
juu ya mwili na damu ya Bwana Isa. 28 Inampasa
mtu ajichunguze mwenyewe, kabla ya kula mkate na
kukinywea kikombe. 29 Kwa maana mtu yeyote alaye
na kunywa pasipo kuutambua mwili wa Bwana Isa,
hula na kunywa hukumu juu yake mwenyewe. 30 Hii
ndiyo sababu wengi miongoni mwenu ni wagonjwa
na dhaifu na wengine wenu hata wamekufa. 31 Lakini
kama tungejichunguza wenyewe tusingehukumiwa.
32 Tunapohukumiwa na Bwana Isa, tunaadibishwa
ili tusije tukahukumiwa pamoja na ulimwengu. 33
Kwa hiyo, ndugu zangu, mkutanikapo pamoja ili kula,
mngojane. 34 Kama mtu akiwa na njaa, ale nyumbani
mwake ili mkutanapo pamoja msije mkahukumiwa.
Nami nitakapokuja nitawapa maelekezo zaidi.

**12** Basi ndugu zangu, kuhusu karama za rohoni,
sitaki mkose kufahamu. 2 Mnajua kwamba
mlipokuwa watu wasiomjua Mungu, kwa njia moja au
nyingine mlishawishika na kupotoshwa mkielekezwa
kwa sanamu zisizonena. 3 Kwa hiyo nawaambieni ya
kuwa hakuna mtu anayeongozwa na Roho Mtakatifu
wa Mungu anayeweza kusema, “Isa na alaaniwe.”
Pia hakuna mtu awezaye kusema, “Isa ni Bwana,”
isipokuwa ameongozwa na Roho wa Mungu. 4 Kuna
aina mbalimbali za karama, lakini Roho ni yule yule. 5
Kuna huduma za aina mbalimbali, lakini Bwana Isa ni
yule yule. 6 Kisha kuna tofauti za kutenda kazi, lakini
ni Mungu yule yule atendaye kazi zote kwa watu wote.
7 Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho wa Mungu
kwa faida ya wote. 8 Maana mtu mmoja kwa Roho
hupewa neno la hekima na mwingine neno la maarifa
kwa Roho huyo huyo. 9 Mtu mwingine imani kwa huyo
Roho na mwingine karama za kuponya kwa huyo
Roho mmoja. 10 Kwa mwingine matendo ya miujiza,
kwa mwingine unabii, kwa mwingine kupambanua
roho, kwa mwingine kunena aina mbalimbali za lugha,
na kwa mwingine bado, tafsiri za lugha. 11 Haya
yote hufanywa na huyo huyo Roho mmoja, Roho
naye humgawia kila mtu, kama apendavyo. 12 Kama
vile mwili ulivyo mmoja nao una viungo vingi; navyo
viungo vyote vya mwili ingawa ni vingi, ni mwili
mmoja; vivyo hivyo na Al-Masihi. 13 Kwa maana
katika Roho mmoja wa Mungu wote tulibatizwa katika
mwili mmoja, kama ni Wayahudi au Wayunani, kama
ni watumwa au watu huru, nasi sote tulinyweshwa
Roho mmoja. 14 Basi mwili si kiungo kimoja, bali
ni viungo vingi. 15 Kama mguu ungesema, “Kwa
kuwa mimi si mkono basi mimi si wa mwili,” hiyo
isingefanya huo mguu usiwe sehemu ya mwili. 16 Na
kama sikio lingesema, “Kwa kuwa mimi si jicho, basi
mimi si wa mwili,” hiyo isingefanya hilo sikio lisiwe
sehemu ya mwili. 17 Kama mwili wote ungakuwa
jicho tu, kusikia kungekuwa wapi? Au kama mwili
wote ungekuwa sikio, kunusa kungekuwa wapi? 18
Lakini kama ilivyo, Mungu ameweka viungo katika
mwili, kila kimoja kama alivyoopenda. 19 Kama vyote
vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? 20
Kama ulivyo, una viungo vingi, lakini mwili ni mmoja.

21 Jicho haliwezi kuuambia mkono, “Sina haja nawe!”
Wala kichwa hakiwezi kuiambia miguu, “Sina haja na
ninyi!” 22 Lakini badala yake, vile viungo vya mwili
vinavyoonekana kuwa dhaifu, ndivyo ambavyo ni vya
muhimu sana. 23 Navyo vile viungo tunavyoviona
havina heshima, ndivyo tunavipa heshima maalum.
Vile viungo vya mwili ambavyo havina uzuri, tunavipa
heshima ya pekee; 24 wakati vile viungo vyenye uzuri
havihitaji utunzaji wa pekee. Lakini Mungu ameviweka
pamoja viungo vya mwili na akavipa heshima zaidi
vile vilivyopungukiwa, 25 ili pasiwe na mafarakano
katika mwili, bali viungo vyote vihudumiane kwa
usawa kila kimoja na mwenzake. 26 Kama kiungo
kimoja kikiumia, viungo vyote huumia pamoja nacho;
kama kiungo kimoja kikipewa heshima, viungo vyote
hufurahi pamoja nacho. 27 Sasa ninyi ni mwili wa
Al-Masihi na kila mmoja wenu ni sehemu ya huo
mwili. 28 Mungu ameweka katika jumuiya ya waumini
kwanza mitume, pili manabii, tatu walimu, kisha
watenda miujiza, pia karama za kuponya, karama za
kusaidiana, karama za uongozi, na aina mbalimbali
za lugha. 29 Je, wote ni mitume? Je, wote ni manabii?
Je, wote ni walimu? Je, wote wanatenda miujiza? 30
Je, wote wana karama ya kuponya? Je, wote hunena
kwa lugha mpya? Je, wote wanatafsiri? 31 Basi
tamanini sana karama zilizo kuu. Nami nitawaonesha
njia iliyo bora zaidi.

13 Hata kama nikisema kwa lugha za wanadamu
na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa
kengele inayolia au toazi linalovuma. 2 Ningekuwa na
karama ya unabii na kujua siri zote na maarifa yote,
hata kama nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha
milima, kama sina upendo, mimi si kitu. 3 Nikitoa
mali yote niliyo nayo, na nikijitolea mwili wangu
uchomwe moto, kama sina upendo, hainifaidi kitu. 4
Upendo huvumilia, upendo hufadhili, upendo hauoni
wivu, hauna majivuno, hauna kiburi. 5 Haukosi
kuwa na adabu, hautafuti mambo yake, haukasiriki
upesi, hauweki kumbukumbu ya mabaya. 6 Upendo
haufurahii mabaya bali hufurahi pamoja na kweli.
7 Upendo huvumilia yote, huamini yote, hutumaini
yote, hustahimili yote. 8 Upendo haushindwi kamwe.
Lakini ukiwepo unabii, utakoma; zikiwepo lugha,
zitakoma; yakiwepo maarifa, yatapita. 9 Kwa maana
tunafahamu kwa sehemu na tunatoa unabii kwa
sehemu. 10 Lakini ukamilifu ukija, yale yasiyo kamili
hutoweka. 11 Nilipokuwa mtoto, nilisema kama mtoto,
niliwaza kama mtoto, nilifikiri kama mtoto. Nilipokuwa
mtu mzima niliacha mambo ya kitoto. 12 Kwa maana
sasa tunaona taswira kama kwa kioo, lakini wakati
huo tutaona wazi. Sasa nafahamu kwa sehemu,
wakati huo nitafahamu kikamilifu, kama vile mimi
ninavyofahamika kikamilifu. 13 Basi sasa, yanadumu
mambo haya matatu: Imani, tumaini na upendo. Lakini
lililo kuu miongoni mwa haya matatu ni upendo.

14 Fuateni upendo na kutaka sana karama za
roho, hasa karama ya unabii. 2 Kwa maana mtu
yeyote anayesema kwa lugha, hasemi na wanadamu
bali anasema na Mungu. Kwa kuwa hakuna mtu
yeyote anayemwelewa, kwani anasema mambo ya siri
kwa roho. 3 Lakini anayetoa unabii anasema na watu
akiwajenga, kuwatia moyo na kuwafariji. 4 Anenaye
kwa lugha hujijenga mwenyewe, bali atoaye unabii
huwajenga waumini. 5 Ningependa kila mmoja wenu
anene kwa lugha, lakini ningependa zaidi nyote mtoe
unabii. Kwa kuwa yeye atoaye unabii ni mkuu kuliko
anenaye kwa lugha, isipokuwa atafsiri, ili waumini
wote wapate kujengwa. 6 Sasa ndugu zangu, nikija
kwenu nikasema kwa lugha mpya, nitawafaidia nini
kama sikuwaletea ufunuo au neno la maarifa au unabii
au mafundisho? 7 Hata vitu visivyo na uhai vitoapo
sauti, kama vile filimbi au kinubi, mtu atajuaje ni wimbo
gani unaoimbwa kusipokuwa na tofauti ya upigaji?
8 Tena kama tarumbeta haitoi sauti inayoeleweka,
ni nani atakayejiandaa kwa ajili ya vita? 9 Vivyo
hivyo na ninyi, mkinena maneno yasiyoeleweka katika
akili, mtu atajuaje mnalosema? Kwa maana mtakuwa
mnasema hewani tu. 10 Bila shaka ziko sauti nyingi
ulimwenguni, wala hakuna isiyo na maana. 11 Basi
kama sielewi maana ya hiyo sauti, nitakuwa mgeni
kwa yule msemaji, naye atakuwa mgeni kwangu. 12
Vivyo hivyo na ninyi. Kwa kuwa mnatamani kuwa na
karama za rohoni, jitahidini kuzidi sana katika karama
kwa ajili ya kuwajenga waumini. 13 Kwa sababu hii,
yeye anenaye kwa lugha na aombe kwamba apate
kutafsiri kile anachonena. 14 Kwa maana nikiomba
kwa lugha, roho yangu inaomba, lakini akili yangu
haina matunda. 15 Nifanyeje basi? Nitaomba kwa
roho, na pia nitaomba kwa akili yangu. Nitaimba
kwa roho na nitaimba kwa akili yangu pia. 16 Ikiwa
unabariki kwa roho, mtu mwingine atakayejikuta
miongoni mwa hao wasiojua, atawezaje kusema

“Amen” katika kushukuru kwako, wakati haelewi
unachosema? 17 Mnaweza kuwa mnatoa shukrani
kweli, sawa, lakini huyo mtu mwingine hajengeki. 18
Namshukuru Mungu kwamba mimi nanena kwa lugha
kuliko ninyi nyote. 19 Lakini katika kundi la waumini
ni afadhali niseme maneno matano ya kueleweka ili
niwafundishe wengine kuliko kusema maneno elfu
kumi kwa lugha. 20 Ndugu zangu, msiwe kama watoto
katika kufikiri kwenu, afadhali kuhusu uovu mwe
kama watoto wachanga, lakini katika kufikiri kwenu,
mwe watu wazima. 21 Katika Torati imeandikwa
kwamba: “Kupitia kwa watu wenye lugha ng’eni na
kupitia midomo ya wageni, nitasema na watu hawa,
lakini hata hivyo hawatanisikiliza, asema Mwenyezi
Mungu.” 22 Basi kunena kwa lugha ni ishara, si kwa
waaminio, bali kwa wasioamini, wakati unabii si kwa
ajili ya wasioamini, bali kwa ajili ya waaminio. 23
Kwa hiyo kama kundi la waumini wote wakikutana
na kila mmoja akanena kwa lugha, kisha wakaingia
wageni wasioelewa au wasioamini, je, hawatasema
kwamba wote mna wazimu? 24 Lakini kama mtu
asiyeamini au asiyeelewa akiingia wakati kila mtu
anatoa unabii, ataaminishwa na watu wote kuwa
yeye ni mwenye dhambi na kuhukumiwa na wote, 25
nazo siri za moyo wake zitawekwa wazi. Kwa hiyo
ataanguka chini na kumwabudu Mungu akikiri, “Kweli
Mungu yuko kati yenu!” 26 Basi tuseme nini ndugu
zangu? Mnapokutana pamoja, kila mmoja ana wimbo,
au neno la mafundisho, au ufunuo, lugha mpya au
atatafsiri. Mambo yote yatendeke kwa ajili ya kulijenga
kundi la waumini. 27 Kama mtu yeyote akinena kwa
lugha, basi waseme watu wawili au watatu, si zaidi,
mmoja baada ya mwingine, na lazima awepo mtu wa
kutafsiri. 28 Lakini kama hakuna mtu wa kutafsiri, hao
watu na wanyamaze kimya katika kundi la waumini,
na wanene na nafsi zao wenyewe na Mungu. 29
Manabii wawili au watatu wanene, na wengine wapime
kwa makini yale yasemwayo. 30 Kama mtu yeyote
aliyeketi karibu, akipata ufunuo, basi yule wa kwanza
na anyamaze. 31 Kwa maana wote mnaweza kutoa
unabii, mmoja baada ya mwingine, ili kila mtu apate
kufundishwa na kutiwa moyo. 32 Roho za manabii
huwatii manabii. 33 Kwa maana Mungu si Mungu
wa machafuko bali ni Mungu wa amani. Kama ilivyo
katika makusanyiko yote ya watakatifu, 34 wanawake
wanapaswa kuwa kimya katika kundi la waumini.
Hawaruhusiwi kusema, bali wanyenyekee kama Torati
isemavyo. 35 Wakitaka kuuliza kuhusu jambo lolote,
wawaulize waume zao nyumbani. Kwa maana ni
aibu kwa mwanamke kuzungumza katika kundi la
waumini. 36 Je, neno la Mungu lilianzia kwenu? Au
ni ninyi tu ambao neno la Mungu limewafikia? 37
Kama mtu yeyote akidhani kwamba yeye ni nabii, au
ana karama za rohoni, basi na akubali kwamba haya
ninayoandika ni maagizo kutoka kwa Bwana Isa.
38 Kama mtu akipuuza jambo hili yeye mwenyewe
atapuuzwa. 39 Kwa hiyo ndugu zangu, takeni sana
kutoa unabii na msikataze watu kusema kwa lugha.
40 Lakini kila kitu kitendeke kwa ufasaha na kwa
utaratibu.

**15** Basi ndugu zangu nataka niwakumbushe kuhusu
Injili niliyowahubiria, mkaipokea na ambayo
katika hiyo mmesimama. 2 Kwa Injili hii mnaokolewa
mkishikilia kwa uthabiti neno nililowahubiria ninyi.
La sivyo, mmeamini katika ubatili. 3 Kwa maana
yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye
umuhimu wa kwanza: Kwamba Al-Masihi alikufa kwa
ajili ya dhambi zetu, kama Maandiko yanavyosema,
4 ya kuwa alizikwa na alifufuliwa siku ya tatu, kama
Maandiko yanavyosema, 5 na kwamba alimtokea
Kefa, kisha akawatokea wale kumi na wawili. 6
Baadaye akawatokea wale ndugu waumini zaidi ya
mia tano kwa pamoja, ambao wengi wao bado wako
hai, ingawa wengine wamelala. 7 Ndipo akamtokea
Yakobo na kisha mitume wote. 8 Mwisho wa wote,
akanitokea mimi pia, ambaye ni kama aliyezaliwa si
kwa wakati wake. 9 Kwa maana mimi ndiye mdogo
kuliko mitume wote, nisiyestahili kuitwa mtume, kwa
sababu niliwatesa waumini wa Mungu. 10 Lakini
kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo, na
neema yake kwangu haikuwa kitu bure. Bali nilizidi
sana kufanya kazi kuliko mitume wote, lakini haikuwa
mimi, bali ni ile neema ya Mungu iliyokuwa pamoja
nami. 11 Hivyo basi, kama ilikuwa mimi au wao, hili
ndilo tunalohubiri, na hili ndilo mliloamini. 12 Basi
kama tumehubiri kwamba Al-Masihi alifufuliwa kutoka
kwa wafu, mbona baadhi yenu mnasema hakuna
ufufuo wa wafu? 13 Lakini kama hakuna ufufuo wa
wafu, basi hata Al-Masihi hakufufuliwa. 14 Tena ikiwa
Al-Masihi hakufufuliwa kutoka kwa wafu, kuhubiri
kwetu kumekuwa ni bure na imani yenu ni batili.
15 Zaidi ya hayo, twaonekana kuwa mashahidi wa

uongo kuhusu Mungu, kwa sababu tumeshuhudia
kumhusu Mungu kwamba alimfufua Al-Masihi kutoka
kwa wafu, lakini hilo haliwezi kuwa kweli kama wafu
hawafufuliwi. **16** Kwa kuwa kama wafu hawafufuliwi,
basi hata Al-Masihi hajafufuka. **17** Tena kama Al-
Masihi hajafufuliwa, imani yenu ni batili; nanyi bado
mko katika dhambi zenu. **18** Hivyo basi, wote waliolala
katika Al-Masihi wamepotea. **19** Ikiwa tumaini letu
ndani ya Al-Masihi ni kwa ajili ya maisha haya tu, sisi
tunastahili kuhurumiwa kuliko watu wote. **20** Lakini
kweli Al-Masihi amefufuliwa kutoka kwa wafu, tunda
la kwanza la wale wote waliolala. **21** Kwa maana
kama vile mauti ilivyokuja kupitia kwa mtu mmoja,
vivyo hivyo, ufufuo wa wafu umekuja kupitia kwa mtu
mmoja. **22** Kwa maana kama vile katika Adamu watu
wote wanakufa, vivyo hivyo katika Al-Masihi wote
watafanywa hai. **23** Lakini kila mmoja kwa wakati
wake: Al-Masihi, tunda la kwanza kisha, wale walio
wake, wakati atakapokuja. **24** Ndipo mwisho utafika,
atakapomkabidhi Mungu Baba Mwenyezi ufalme,
baada ya kuangamiza kila utawala na kila mamlaka
na nguvu. **25** Kwa maana lazima Al-Masihi atawale
hadi awe amewaweka adui zake wote chini ya miguu
yake. **26** Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni
mauti. **27** Kwa maana Mungu “ameweka vitu vyote
chini ya miguu yake”. Lakini isemapo kwamba “vitu
vyote” vimewekwa chini yake, ni wazi kwamba Mungu
aliyetiisha vitu vyote chini ya Al-Masihi hayumo
miongoni mwa hivyo vilivyotiishwa. **28** Atakapokuwa
amekwisha kuyafanya haya, ndipo Mwana mwenyewe
atatiishwa chini yake yeye aliyetiisha vitu vyote, ili
Mungu awe yote katika yote. **29** Basi kama hakuna
ufufuo, watafanyaje wale wabatizwao kwa ajili ya
wafu? Kama wafu hawafufuliwi kamwe, mbona watu
wanabatizwa kwa ajili yao? **30** Nasi kwa upande wetu
kwa nini tunajihatarisha kila saa? **31** Kama majivuno
yangu kwa ajili yenu katika Al-Masihi Isa Bwana wetu
ni kweli, ndugu zangu, ninakufa kila siku. **32** Kama
kwa sababu za kibinadamu tu nilipigana na wanyama
wakali huko Efeso, ningekuwa nimepata faida gani?
Kama wafu hawafufuliwi, “Tuleni na kunywa, kwa
kuwa kesho tutakufa.” **33** Msidanganyike: “Ushirika
na watu wabaya huharibu tabia njema.” **34** Zindukeni
mwe na akili kama iwapasavyo, wala msitende dhambi
tena; kwa maana watu wengine hawamjui Mungu.
Nasema mambo haya ili mwone aibu. **35** Lakini mtu
anaweza kuuliza, “Wafu wafufuliwaje? Watakuwa
na mwili wa namna gani?” **36** Ninyi wapumbavu
kiasi gani? Mpandacho hakiwi hai kama hakikufa.
**37** Mpandapo, hampandi mwili ule utakao kuwa, bali
mwapanda mbegu tu, pengine ya ngano au ya kitu
kingine. **38** Lakini Mungu huipa mbegu umbo kama
alivyokusudia mwenyewe na kila aina ya mbegu huipa
umbo lake. **39** Kwa maana nyama zote si za aina
moja. Binadamu wana nyama ya aina moja, wanyama
wana aina nyingine, kadhalika ndege na samaki wana
nyama tofauti. **40** Pia kuna miili ya mbinguni na miili
ya duniani, lakini fahari ya ile miili ya mbinguni ni ya
aina moja, na fahari ya ile miili ya duniani ni ya aina
nyingine. **41** Jua lina fahari ya aina moja, mwezi nao
una fahari yake na nyota pia, nazo nyota hutofautiana
katika fahari. **42** Hivyo ndivyo itakavyokuwa wakati wa
ufufuo wa wafu. Ule mwili wa kuharibika uliopandwa,
utafufuliwa usioharibika; **43** unapandwa katika aibu,
unafufuliwa katika utukufu, unapandwa katika udhaifu,
unafufuliwa katika nguvu, **44** unapandwa mwili wa
asili, unafufuliwa mwili wa kiroho. Kama kuna mwili
wa asili, basi kuna mwili wa kiroho pia. **45** Kwa
hiyo imeandikwa, “Mtu wa kwanza Adamu alifanyika
kiumbe hai”; Adamu wa mwisho, yeye ni roho iletayo
uzima. **46** Lakini si ule wa kiroho uliotangulia, bali ni
ule wa asili, kisha ule wa kiroho. **47** Mtu wa kwanza
aliumbwa kwa mavumbi ya ardhini, mtu wa pili alitoka
mbinguni. **48** Kama vile alivyokuwa yule wa ardhini,
ndivyo walivyo wale walio wa ardhini; na kwa vile
alivyo mtu yule aliyetoka mbinguni, ndivyo walivyo
wale walio wa mbinguni. **49** Kama vile tulivyochukua
mfano wa mtu wa ardhini, ndivyo tutakavyochukua
mfano wa yule mtu aliyetoka mbinguni. **50** Ndugu
zangu nisemalo ni hili: mwili na damu haviwezi
kuurithi ufalme wa Mungu, wala kuharibika kurithi
kutokuharibika. **51** Sikilizeni, nawaambia siri: Sote
hatutalala, lakini sote tutabadilishwa: **52** ghafula,
kufumba na kufumbua, parapanda ya mwisho
itakapolia. Kwa kuwa parapanda italia, nao wafu
watafufuliwa na miili isiyoharibika, nasi tutabadilishwa.
**53** Kwa maana mwili huu wa kuharibika lazima uvae
kutokuharibika, nao huu wa kufa lazima uvae kutokufa.
**54** Kwa hiyo, mwili huu wa kuharibika utakapovaa
kutokuharibika, nao huu mwili wa kufa utakapovaa
kutokufa, ndipo lile neno lililoandikwa litakapotimia:
“Mauti imemezwa kwa kushinda.” **55** “Kuko wapi,

ee mauti, kushinda kwako? Uko wapi, ee mauti, uchungu wako?” (Hadēs g86) 56 Uchungu wa mauti ni dhambi na nguvu ya dhambi ni sheria. 57 Lakini Mungu apewe shukrani, yeye atupaye ushindi kupitia kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi. 58 Kwa hiyo, ndugu zangu wapendwa, simameni imara. Msitikisike. Mzidi sana katika kuitenda kazi ya Bwana Isa, kwa maana mnajua ya kuwa, kazi yenu katika Bwana Isa si bure.

16 Basi kuhusu changizo kwa ajili ya watakatifu: Kama nilivyoyaagiza makundi ya waumini ya Galatia, fanyeni vivyo hivyo. 2 Siku ya kwanza ya kila juma, kila mmoja wenu atenge kiasi cha fedha, kulingana na mapato yake, na fedha hizo aziweke akiba, ili nitakapokuja pasiwe na lazima ya kufanya mchango. 3 Kwa hiyo nitakapowasili, nitawapa wale mtakaowachagua barua za kuwatambulisha, ili kuwatuma wapeleke zawadi zenu huko Yerusalemu. 4 Ikionekana ni vyema na mimi niende, basi hao watu watafuatana nami. 5 Baada ya kupitia Makedonia nitakuja kwenu, maana ninakusudia kupitia Makedonia. 6 Huenda nitakaa nanyi kwa muda, au hata kukaa nanyi kipindi chote cha baridi, ili mweze kunisaidia katika safari yangu, popote niendapo. 7 Kwa maana sitaki niwaone sasa na kupita tu; natarajia kuwa nanyi kwa muda wa kutosha, kama Bwana Isa akipenda. 8 Lakini nitakaa Efeso hadi wakati wa Pentekoste, 9 kwa maana mlango mkubwa umefunguliwa kwangu kufanya kazi yenye matunda, nako huko kuna adui wengi wanaonipinga. 10 Ikiwa Timotheo atakuja kwenu, hakikisheni kwamba hana hofu yoyote akiwa nanyi, kwa sababu anafanya kazi ya Bwana Isa, kama mimi nifanyavyo. 11 Basi asiwepo mtu atakayekataa kumpokea. Msafirisheni kwa amani ili aweze kunijia tena. Namtarajia pamoja na ndugu. 12 Basi kwa habari za ndugu yetu Apolo, nimemsihi kwa bidii aje kwenu pamoja na hao ndugu. Ingawa alikuwa hapendi kabisa kuja sasa, lakini atakuja apatapo nafasi. 13 Kesheni; simameni imara katika imani; kuweni mashujaa na hodari. 14 Fanyeni kila kitu katika upendo. 15 Ninyi mnajua kwamba watu wa nyumbani mwa Stefana ndio walikuwa wa kwanza kuamini katika Akaya, nao wamejitoa kwa ajili ya kuwahudumia watakatifu. Ndugu nawasihi, 16 mjitie katika kuwahudumia watu kama hawa na kila mmoja aingiaye kwenye kazi na kuifanya kwa bidii. 17 Nilifurahi Stefana, Fortunato na Akaiko walipofika, kwa sababu wamenipatia yale niliyopungukiwa kutoka kwenu. 18 Kwa kuwa waliiburudisha roho yangu na zenu pia. Watu kama hawa wanastahili kutambuliwa. 19 Makundi ya waumini wa jimbo la Asia wanawasalimu. Akila na Prisila pamoja na kundi la waumini walioko nyumbani mwao wanawasalimu sana katika Bwana Isa. 20 Ndugu wote walio hapa wanawasalimu. Salimianeni kwa busu takatifu. 21 Mimi, Paulo, naandika salamu hizi kwa mkono wangu mwenyewe. 22 Kama mtu yeyote hampendi Bwana Isa Al-Masihi, na alaaniwe. Bwana wetu Isa, njoo. 23 Neema ya Bwana Isa iwe nanyi. 24 Upendo wangu uwe nanyi nyote katika Al-Masihi Isa. Amen.

# 2 Wakorintho

**1** Barua hii ni kutoka kwangu mimi Paulo, mtume
wa Al-Masihi Isa kwa mapenzi ya Mungu, na
Timotheo ndugu yetu. **2** Neema na amani zinazotoka
kwa Mungu, Baba yetu, na kwa Bwana wetu Isa
Al-Masihi ziwe nanyi. **3** Ahimidiwe Mungu na Baba
wa Bwana wetu Isa Al-Masihi, Baba wa huruma
na Mungu wa faraja yote. **4** Yeye hutufariji katika
taabu zetu, ili tuweze kuwafariji walio katika taabu
yoyote kwa faraja ambayo sisi wenyewe tumepokea
kutoka kwa Mungu. **5** Kama vile mateso ya Al-
Masihi yanavyozidi maishani mwetu, hivyo ndivyo
faraja yetu inavyofurika kupitia kwa Al-Masihi. **6** Ikiwa
tunataabika, ni kwa ajili ya faraja na wokovu wenu;
tukifarijiwa, ni kwa ajili ya faraja yenu, iwaleteayo
saburi ya mateso yale yale yanayotupata. **7** Nalo
tumaini letu kwenu ni thabiti, kwa sababu tunajua
kwamba kama vile mnavyoshiriki mateso yetu, ndivyo
pia mnavyoshiriki faraja yetu. **8** Ndugu wapendwa,
hatutaki mkose kujua kuhusu zile taabu tulizopata
huko jimbo la Asia. Kwa maana tulilemewa na mizigo
sana, kiasi cha kushindwa kuvumilia, hata tulikata
tamaa ya kuishi. **9** Kwa kweli, mioyoni mwetu tulihisi
tumekabiliwa na hukumu ya kifo, ili tusijitegemee sisi
wenyewe bali tumtegemee Mungu afufuaye wafu.
**10** Yeye ametuokoa kwenye hatari kubwa ya kifo,
na atatuokoa tena. Kwake yeye tumeweka tumaini
letu kwamba ataendelea kutuokoa, **11** kama vile
mnavyoungana kusaidiana nasi katika maombi. Hivyo
wengi watatoa shukrani kwa niaba yetu kwa ajili ya
baraka za neema tulizopata kwa majibu ya maombi ya
wengi. **12** Basi haya ndio majivuno yetu: Dhamiri yetu
inatushuhudia kwamba tumeishi katika ulimwengu
kwa utakatifu na uaminifu unaotoka kwa Mungu, na
hasa katika uhusiano wetu na ninyi. Hatukufanya
hivyo kwa hekima ya kidunia bali kwa neema ya
Mungu. **13** Kwa maana hatuwaandikii mambo ambayo
hamwezi kusoma au kuyaelewa. Natumaini kwamba,
**14** kama vile mlivyotuelewa kwa sehemu, mtakuja
kuelewa kwa ukamilifu ili mweze kujivuna kwa ajili
yetu, kama na sisi tutakavyojivuna kwa ajili yenu
katika siku ya Bwana Isa. **15** Kwa kuwa nilikuwa na
uhakika wa mambo haya, nilitaka nije kwenu kwanza,
ili mpate faida mara mbili. **16** Nilipanga kuwatembelea
nikiwa safarini kwenda Makedonia, na kurudi tena
kwenu nikitoka Makedonia, ili mnisafirishe katika
safari yangu ya kwenda Yudea. **17** Nilipopanga jambo
hili, je, nilikuwa kigeugeu? Au ninafanya mipango
yangu kwa hali ya mwili, ili niseme, “Ndiyo, ndiyo” na
“Siyo, siyo” wakati huo huo? **18** Hakika kama Mungu
alivyo mwaminifu, maneno yetu kwenu hayajakuwa
“Ndiyo” na “Siyo”. **19** Kwa kuwa Isa Al-Masihi, Mwana
wa Mungu, ambaye mimi, Silvano, na Timotheo
tulimhubiri kwenu, hakuwa “Ndiyo” na “Siyo”, bali
kwake yeye siku zote ni “Ndiyo”. **20** Kwa maana ahadi
zote za Mungu zilizo katika Al-Masihi ni “Ndiyo”. Kwa
sababu hii, ni kwake yeye tunasema “Amen” kwa
utukufu wa Mungu. **21** Basi ni Mungu atufanyaye
sisi pamoja nanyi kusimama imara katika Al-Masihi.
Alitupaka mafuta **22** kwa kututia muhuri wake na
kutupatia Roho wake Mtakatifu mioyoni mwetu kuwa
rehani kwa ajili ya kututhibitishia yote aliyotuahidi.
**23** Namwita Mungu awe shahidi wangu kwamba
sikurudi Korintho kwa sababu niliwahurumia ninyi. **24**
Si kwamba tunatawala imani yenu, bali twatenda kazi
pamoja nanyi ili mfurahi, kwa sababu ni kwa imani
mwasimama imara.

**2** Hivyo nilikusudia moyoni mwangu nisifanye
ziara nyingine yenye kuwaumiza ninyi. **2**
Kwa kuwa nikiwahuzunisha ninyi, ni nani
aliyebaki wa kunifurahisha isipokuwa ninyi ambao
nimewahuzunisha? **3** Niliwaandikia hivyo ili nikija
nisihuzunishwe na wale watu ambao walipaswa
kunifurahisha. Nilikuwa na uhakika na ninyi nyote,
kwamba wote mngeshiriki furaha yangu. **4** Kwa
maana niliwaandikia kutokana na dhiki kubwa na
kutaabika sana moyoni mwangu, tena kwa machozi
mengi; shabaha yangu haikuwa niwahuzunishe,
bali niwaoneshe kina cha upendo wangu kwenu.
**5** Lakini ikiwa mtu yeyote amesababisha huzuni,
kwa kiasi fulani hakunihuzunisha mimi kama vile
alivyowahuzunisha ninyi nyote. Nasema hivi ili nisiwe
mkali kupita kiasi. **6** Adhabu hii aliyopewa na wengi
inamtosha. **7** Basi sasa badala yake, inawapasa
kumsamehe na kumfariji, ili asigubikwe na huzuni
kupita kiasi. **8** Kwa hiyo, nawasihi mpate kuuthibitisha
tena upendo wenu kwake. **9** Sababu ya kuwaandikia
ni kuona kama mngeweza kushinda hilo jaribio na
kutii katika kila jambo. **10** Mkimsamehe mtu yeyote,
mimi pia nimemsamehe. Kile nilichosamehe, kama
kulikuwa na kitu chochote cha kusamehe, nimekwisha

kusamehe mbele ya Al-Masihi kwa ajili yenu, **11** ili
Shetani asitushinde. Kwa maana hatujakosa kuzijua
hila zake. **12** Basi nilipofika Troa kuhubiri Injili ya Al-
Masihi na kukuta kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa
amenifungulia mlango, **13** bado nilikuwa sina amani
kwa sababu sikumkuta ndugu yangu Tito huko. Hivyo
niliagana nao, nikaenda Makedonia. **14** Lakini Mungu
apewe shukrani, yeye ambaye siku zote hutufanya
tuandamane kwa ushindi tukiwa ndani ya Al-Masihi.
Naye kupitia kwetu hueneza kila mahali harufu nzuri
ya kumjua yeye. **15** Kwa maana sisi kwa Mungu ni
harufu nzuri ya manukato ya Al-Masihi miongoni mwa
wale wanaookolewa na kwa wale wanaopotea. **16**
Kwa wale wanaopotea, sisi ni harufu ya mauti iletayo
mauti; lakini kwa wale wanaookolewa, sisi ni harufu
nzuri iletayo uzima. Ni nani awezaye mambo hayo? **17**
Tofauti na watu wengine wengi, sisi hatufanyi biashara
na neno la Mungu ili tujifaidishe. Bali tunalinena neno
lake kwa unyofu katika Al-Masihi tukiwa mbele za
Mungu, kama watu waliotumwa na Mungu.

**3** Je, tunaanza tena kujisifu wenyewe? Au tunahitaji
kupata barua za utambulisho kwenu au kutoka
kwenu, kama watu wengine? **2** Ninyi wenyewe
ndio barua yetu iliyoandikwa katika mioyo yetu,
inayojulikana na kusomwa na kila mtu. **3** Nanyi
mwadhihirisha wazi kwamba ninyi ni barua inayotoka
kwa Al-Masihi, matokeo ya huduma yetu, ambayo
haikuandikwa kwa wino bali kwa Roho wa Mungu
aliye hai, si katika vibao vya mawe, bali katika
vibao ambavyo ni mioyo ya wanadamu. **4** Hili ndilo
tumaini tulilo nalo mbele za Mungu kupitia kwa Al-
Masihi. **5** Si kwamba sisi tunafikiri kuwa tunaweza
kufanya jambo lolote wenyewe, lakini utoshelevu
wetu unatoka kwa Mungu. **6** Ndiye alitutosheleza
kuwa wahudumu wa agano jipya: si wa andiko, bali
wa Roho wa Mungu; kwa kuwa andiko huua, bali
Roho hutia uzima. **7** Basi ikiwa ile huduma iliyoleta
mauti, iliyoandikwa kwa herufi juu ya jiwe, ilikuja kwa
utukufu hata Waisraeli wakawa hawawezi kuutazama
uso wa Musa kwa sababu ya ule utukufu wake,
ingawa ulikuwa wa kufifia, **8** je, huduma ya Roho wa
Mungu haitakuwa na utukufu zaidi? **9** Ikiwa huduma
ile inayowahukumu wanadamu ina utukufu, je, ile
huduma iletayo haki haitakuwa ya utukufu zaidi? **10**
Kwa maana kile kilichokuwa na utukufu sasa hakina
utukufu, kikilinganishwa na huu utukufu unaozidi. **11**
Ikiwa kile kilichokuwa kinafifia kilikuja kwa utukufu,
je, si zaidi utukufu wa kile kinachodumu! **12** Kwa
hiyo, kwa kuwa tunalo tumaini hili, tuna ujasiri sana.
**13** Sisi si kama Musa, ambaye ilimpasa kuweka
utaji wa kufunika uso wake ili Waisraeli wasiuone
ule mng’ao uliokuwa juu yake hadi ulipofifia na
hatimaye kutoweka. **14** Lakini akili zao zilipumbazwa,
kwa maana hadi leo utaji ule ule hufunika Torati
inaposomwa. Huo utaji haujaondolewa, kwa maana ni
katika Al-Masihi peke yake unaondolewa. **15** Hata leo
Torati ya Musa inaposomwa, utaji hufunika mioyo yao.
**16** Lakini wakati wowote mtu anapomgeukia Bwana
Mungu Mwenyezi, utaji unaondolewa. **17** Basi Bwana
Isa ndiye Roho. Mahali alipo Roho wa Bwana Mungu
Mwenyezi, hapo pana uhuru. **18** Nasi sote, tukiwa
na nyuso zisizotiwa utaji, tunadhihirisha utukufu wa
Bwana Isa kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili
tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi,
unaotoka kwa Bwana Isa, aliye Roho.

**4** Kwa hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii kwa
rehema za Mungu, hatukati tamaa. **2** Lakini
tumekataa mambo ya siri na ya aibu; hatufuati njia
za udanganyifu, wala kulichanganya neno la Mungu
na uongo. Kinyume cha hayo, tunadhihirisha kweli
waziwazi na kujitambulisha wenyewe kwenye dhamiri
ya kila mtu mbele za Mungu. **3** Hata nayo Injili yetu
kama imetiwa utaji, ni kwa wale tu wanaopotea. **4**
Kwa habari yao, mungu wa dunia hii amepofusha akili
za wasioamini, ili wasione nuru ya Injili ya utukufu
wa Al-Masihi, aliye sura ya Mungu. **(aiōn g165)** **5** Kwa
maana hatujihubiri sisi wenyewe, ila tunamhubiri Isa
Al-Masihi kuwa ni Bwana, na sisi ni watumishi wenu
kwa ajili ya Isa. **6** Kwa kuwa Mungu, yeye aliyesema,
“Nuru na ing’ae gizani,” ameifanya nuru yake ing’ae
mioyoni mwetu ili kutupatia nuru ya maarifa ya utukufu
wa Mungu katika uso wa Al-Masihi. **7** Lakini tunayo
hazina hii katika vyombo vya udongo, ili ijulikane
wazi kwamba uwezo huu wa ajabu unatoka kwa
Mungu, wala si kwetu. **8** Twataabika kila upande
lakini hatuangamizwi; twaona wasiwasi lakini hatukati
tamaa; **9** twateswa lakini hatuachwi; twatupwa chini
lakini hatupondwi. **10** Siku zote twachukua katika mwili
kufa kwake Isa ili uzima wa Isa uweze kudhihirishwa
katika miili yetu. **11** Kwa maana sisi tulio hai siku zote
tumetolewa tufe kwa ajili ya Isa, ili uzima wake upate
kudhihirishwa katika mwili wetu upatikanao na mauti.

12 Hivyo basi, mauti inatenda kazi ndani yetu, bali
uzima unatenda kazi ndani yenu. 13 Imeandikwa,
“Niliamini, kwa hiyo nimesema.” Kwa roho yule yule
wa imani pia tuliamini na hivyo tunasema, 14 kwa
sababu tunajua kwamba yeye aliyemfufua Bwana Isa
kutoka kwa wafu atatufufua sisi pia pamoja na Isa na
kutuleta sisi pamoja nanyi mbele zake. 15 Haya yote
ni kwa faida yenu, ili neema ile inavyowafikia watu
wengi zaidi na zaidi ipate kusababisha shukrani nyingi
kwa utukufu wa Mungu. 16 Kwa hiyo, hatukati tamaa.
Ingawa utu wetu wa nje unachakaa, utu wetu wa
ndani unafanywa upya siku kwa siku. 17 Kwa maana
dhiki yetu nyepesi iliyo ya kitambo inatutayarisha
kwa ajili ya utukufu wa milele unaozidi kuwa mwingi
kupita kiasi. **(aiōnios g166)** 18 Kwa hivyo hatuangalii
yale yanayoonekana, bali yale yasiyoonekana. Kwa
maana yale yanayoonekana ni ya kitambo tu, bali
yale yasiyoonekana ni ya milele. **(aiōnios g166)**

**5** Kwa maana twajua kama hema letu la dunia
tunayoishi likiharibiwa, tunalo jengo kutoka kwa
Mungu, nyumba iliyo ya milele kule mbinguni,
isiyojengwa kwa mikono ya wanadamu. **(aiōnios g166)**
2 Katika hema hili twalia kwa uchungu, tukitamani
kuvikwa makao yetu ya mbinguni, 3 kwa kuwa
tukishavikwa hatutaonekana tena kuwa uchi. 4 Kwa
kuwa tukiwa bado katika hema hili twalia kwa uchungu
na kulemewa, kwa sababu hatutaki kuvuliwa bali
kuvikwa makao yetu ya mbinguni ili kile kipatikanacho
na mauti kimezwe na uzima. 5 Basi Mungu ndiye
alitufanya kwa ajili ya jambo lilo hilo, naye ametupatia
Roho wa Mungu kuwa amana, akituhakikishia ahadi
ya kile kijacho. 6 Kwa hiyo siku zote tuna ujasiri,
hata ingawa tunajua kwamba tukiwa katika mwili huu,
tuko mbali na Bwana Isa. 7 Kwa maana twaenenda
kwa imani wala si kwa kuona. 8 Naam, tuna ujasiri,
na tunaona ingekuwa bora zaidi kuuacha mwili
huu na kwenda kukaa na Bwana Isa. 9 Kwa hiyo,
tukiwa katika mwili huu au tukiwa mbali nao, lengo
letu ni kumpendeza Bwana Isa. 10 Kwa kuwa sisi
sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Al-
Masihi, ili kila mmoja apate kulipwa kwa ajili ya
yale ambayo yametendwa katika mwili wake, yakiwa
mema au mabaya. 11 Basi, kwa kuwa tunajua kumcha
Mwenyezi Mungu, tunajitahidi kuwavuta wengine.
Lakini Mungu anatufahamu dhahiri, nami natumaini
kwamba tu dhahiri katika dhamiri zenu pia. 12 Sio
kwamba tunajaribu kujistahilisha kwenu tena, lakini
tunataka kuwapa nafasi ili mwone fahari juu yetu,
mweze kuwajibu hao wanaoona fahari kuhusu mambo
yanayoonekana badala ya mambo yaliyo moyoni. 13
Kama tumerukwa na akili, ni kwa ajili ya Mungu; kama
tuna akili timamu, ni kwa ajili yenu. 14 Kwa kuwa
upendo wa Al-Masihi unatutia nguvu, kwa sababu
tunasadiki kuwa mmoja alikufa kwa ajili ya wote,
kwa hiyo wote walikufa. 15 Naye alikufa kwa ajili
ya watu wote, ili wote wanaoishi wasiishi tena kwa
ajili ya nafsi zao wenyewe, bali kwa ajili yake yeye
aliyekufa na kufufuliwa tena kwa ajili yao. 16 Hivyo
tangu sasa hatumwangalii mtu yeyote kwa mtazamo
wa kibinadamu. Ingawa wakati fulani tulimwangalia
Al-Masihi kwa namna ya kibinadamu, hatumwangalii
tena hivyo. 17 Kwa hiyo mtu akiwa ndani ya Al-
Masihi, amekuwa kiumbe kipya: ya kale yamepita;
tazama, yamekuwa mapya. 18 Haya yote yanatokana
na Mungu, ambaye ametupatanisha sisi na nafsi yake
kupitia kwa Isa Al-Masihi, na kutupatia sisi huduma
ya upatanisho: 19 kwamba Mungu alikuwa ndani ya
Al-Masihi akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake
mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao.
Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho.
20 Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Al-Masihi, kana
kwamba Mungu anawasihi kupitia kwa vinywa vyetu.
Nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya Al-Masihi:
mpatanishwe na Mungu. 21 Kwa maana Mungu
alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi
kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu
kupitia kwake Al-Masihi.

**6** Kama watendakazi pamoja na Mungu, tunawasihi
msipokee neema ya Mungu bure. 2 Kwa maana
asema: “Wakati wangu uliokubalika nilikusikia, siku
ya wokovu nilikusaidia.” Tazama, wakati uliokubalika
ndio huu, siku ya wokovu ndiyo hii. 3 Hatuweki
kikwazo katika njia ya mtu yeyote, ili huduma yetu
isionekane kuwa na lawama. 4 Bali tunajidhihirisha
kuwa watumishi wa Mungu kwa kila njia: katika saburi
nyingi; katika dhiki, katika misiba, na katika shida; 5
katika kupigwa, katika kufungwa gerezani na katika
ghasia; katika kazi ngumu, katika kukesha na katika
kufunga; 6 katika utakatifu, katika ufahamu, katika
uvumilivu, na katika utu wema; katika Roho wa Mungu
na upendo wa kweli; 7 katika maneno ya kweli na
katika nguvu za Mungu; kwa silaha za haki mkononi

wa kuume na mkononi wa kushoto; **8** katika utukufu
na katika kudharauliwa, katika sifa mbaya na katika
sifa nzuri; tukionekana kama wadanganyaji, lakini
tukiwa wakweli; **9** tukiwa maarufu, lakini tukihesabiwa
kama tusiojulikana; tukiwa kama wanaokufa, lakini
tunaishi; tukipigwa, lakini hatuuawi; **10** tukiwa kama
wenye huzuni, lakini siku zote tukifurahi; tukionekana
maskini, lakini tukitajirisha wengi; tukiwa kama wasio
na kitu, lakini tuna vitu vyote. **11** Tumesema nanyi
wazi, enyi Wakorintho na kuwafungulieni mioyo yetu
wazi kabisa. **12** Sisi hatujizuii kuwapenda, bali ninyi
mmeuzuia upendo wenu kwetu. **13** Sasa nasema
kama na watoto wangu: Ninyi pia ifungueni mioyo
yenu kabisa. **14** Msifungiwe nira pamoja na watu
wasioamini. Kwa maana pana uhusiano gani kati
ya haki na uovu? Au kuna ushirika gani kati ya
nuru na giza? **15** Kuna mapatano gani kati ya Al-
Masihi na Beliari? Yeye aaminiye ana sehemu gani
na yeye asiyeamini? **16** Kuna mapatano gani kati
ya Hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa sisi tu
Hekalu la Mungu aliye hai. Kama Mungu alivyosema:
“Nitakaa pamoja nao na kutembea katikati yao, nami
nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu.”
**17** Kwa hiyo, “Tokeni miongoni mwao, mkatengwe
nao, asema Mwenyezi Mungu. Msiguse kitu chochote
kilicho najisi, nami nitawakaribisha.” **18** Na, “Mimi
nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wanangu wa
kiume na wa kike, asema Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni.”

**7** Wapendwa, kwa kuwa tunazo ahadi hizi, basi
na tujitakase nafsi zetu kutokana na kila kitu
kitiacho mwili na roho unajisi, tukitimiza utakatifu kwa
kumcha Mungu. **2** Tupatieni nafasi mioyoni mwenu.
Hatujamkosea mtu yeyote, wala hatujampotosha
mtu yeyote, wala hatujamdhulumu mtu yeyote. **3**
Sisemi haya ili kuwahukumu, kwa kuwa nilisema
mwanzo kwamba ninyi mko mioyoni mwetu hata kwa
kufa pamoja au kuishi pamoja. **4** Nina ujasiri mwingi
kwa ajili yenu; naona fahari juu yenu. Nimejawa na
faraja. Nina furaha kupita kiasi katika mateso yetu
yote. **5** Kwa maana hata tulipoingia Makedonia, miili
yetu haikuwa na amani. Tulisumbuliwa kila upande;
kwa nje kulikuwa na mapigano, na mioyoni mwetu
tulikuwa na hofu. **6** Bali Mungu, yeye awafarijie wenye
huzuni, alitufariji kwa Tito kufika kwetu. **7** Lakini si
kule kuja kwa Tito tu, bali pia kwa faraja mliyompa.
Alitueleza jinsi mlivyonionea shauku, huzuni yenu
kubwa na juhudi yenu kwa ajili yangu, ili furaha
yangu ipate kuwa kubwa kuliko wakati wowote.
**8** Hata kama niliwahuzunisha kwa barua yangu,
sijutii. Ingawa nilijuta kwa muda mfupi, kwa kuwa
najua kwamba barua yangu iliwaumiza, lakini ni
kwa kitambo tu. **9** Lakini sasa nina furaha, si kwa
sababu mlihuzunika, bali kwa kuwa huzuni hiyo
iliwafanya mtubu. Kwa maana mlihuzunishwa kama
Mungu alivyokusudia watu wahuzunike, na hivyo
sisi hatukuwadhuru kwa njia yoyote. **10** Kwa maana
huzuni ya kiungu huleta toba iletayo wokovu, wala
haina majuto. Lakini huzuni ya kidunia husababisha
mauti. **11** Tazameni jinsi huzuni hii ya kiungu ilivyoleta
faida ndani yenu: bidii mliyo nayo, juhudi mliyofanya
kujitetea, uchungu wenu, hofu yenu, upendo wenu,
shauku yenu na jinsi mlivyokuwa tayari kutoa adhabu
inayostahili. Kwa kila njia mmejithibitisha kuwa safi
katika jambo hilo. **12** Hivyo, ingawa niliwaandikia,
haikuwa kwa sababu ya huyo aliyekosa au huyo
aliyekosewa. Lakini nilitaka ninyi wenyewe mwone
mbele za Mungu jinsi mlivyojitoa kwa ajili yetu. **13**
Kwa ajili ya haya yote tumefarijika. Zaidi ya kule sisi
kutiwa moyo, tulifurahi sana kumwona Tito alivyo
na furaha, kwa sababu roho yake imeburudishwa
na ninyi nyote. **14** Nilikuwa nimewasifu ninyi kwake,
nanyi hamkuniaibisha. Lakini kama vile yale yote
tuliyowaambia yalikuwa kweli, hivyo kule kujisifu
kwetu kwa Tito kuwahusu ninyi kumethibitishwa kuwa
kweli pia. **15** Upendo wake kwenu unaongezeka sana
anapokumbuka jinsi mlivyokuwa watiifu, mkampokea
kwa hofu na kutetemeka. **16** Nafurahi kwamba
ninaweza kuwatumaini ninyi kabisa.

**8** Basi sasa ndugu, nataka ninyi mjue kuhusu ile
neema ambayo Mungu amewapa waumini wa
Makedonia. **2** Ingawa walikuwa na majaribu makali,
furaha yao kubwa na umaskini wao mkuu zilifurika
kwa ukarimu mwingi. **3** Kwa maana nashuhudia
kwamba wao walitoa kwa kadiri walivyoweza, hata
na zaidi ya uwezo wao, kwa hiari yao, **4** wakitusihi
kwa bidii wapewe fursa ya kushiriki katika huduma
hii ya kuwasaidia watakatifu. **5** Wala hawakufanya
tulivyotazamia, bali walijitoa wao wenyewe kwa
Bwana Isa kwanza, na ndipo wakajitoa kwa ajili
yetu kufuatana na mapenzi ya Mungu. **6** Kwa hiyo
tulimsihi Tito, kwa kuwa ndiye alianzisha jambo hili,

akamilishe tendo hili la neema kwa upande wenu.
7 Lakini kama vile mlivyo mbele sana katika yote,
iwe ni katika imani, katika usemi, katika maarifa,
katika uaminifu wote na katika upendo wenu kwetu
sisi, vivyo hivyo tunataka pia mzidi katika neema
hii ya kutoa. 8 Siwaamrishi, lakini nataka kujaribu
unyofu wa upendo wenu kwa kuulinganisha na bidii
ya wengine. 9 Kwa maana mnajua neema ya Bwana
wetu Isa Al-Masihi, kwamba ingawa alikuwa tajiri,
kwa ajili yenu alikubali kuwa maskini, ili kwa umaskini
wake ninyi mpate kuwa matajiri. 10 Ushauri wangu
kuhusu lile lililo bora kwenu katika jambo hili ni huu:
Mwaka uliopita ninyi mlikuwa wa kwanza si tu kutoa
lakini pia mlikuwa na shauku ya kufanya hivyo. 11
Sasa ikamilisheni kazi hii, ili shauku yenu ya kuitenda
iandamane na kuimaliza, mkijitolea kulingana na
uwezo wenu. 12 Kwa kuwa kama nia ya kutoa ipo,
kitolewacho kinakubalika kulingana na kile mtu alicho
nacho, wala si kwa kile ambacho hana. 13 Nia yetu si
kwamba wengine wasaidike wakati ninyi mnateseka,
bali pawe na uwiano. 14 Kwa wakati huu, wingi wa
vitu mlivyo navyo utasaidia kutosheleza mahitaji yao,
ili wakati wao watakapokuwa na wingi wa vitu, nao
wapate kutosheleza mahitaji yenu. 15 Ndipo patakuwa
na usawa, kama ilivyoandikwa: “Aliyekusanya
zaidi hakuwa na ziada, wala aliyekusanya kidogo
hakupungukiwa.” 16 Ninamshukuru Mungu ambaye
amemtia Tito moyo wa kuwajali ninyi kama mimi
ninavyowajali. 17 Si kwamba Tito amekubali tu ombi
letu, bali anakuja kwenu akiwa na shauku kuliko
wakati mwingine, tena kwa hiari yake mwenyewe.
18 Nasi tunamtuma pamoja naye ndugu ambaye
anasifiwa na makundi yote ya waumini kwa huduma
yake ya kuhubiri Injili. 19 Zaidi ya hayo, alichaguliwa na
makundi ya waumini ili asafiri pamoja nasi tulipokuwa
tunapeleka matoleo ya ukarimu, kwa ajili ya utukufu
wa Bwana Isa mwenyewe, na ili kuonesha hisani
yetu kuwasaidia. 20 Tunataka kuepuka lawama
yoyote kuhusu jinsi tunavyosimamia matoleo haya
ya ukarimu. 21 Kwa kuwa tunakusudia kufanya kile
kilicho haki, si machoni mwa Bwana Isa peke yake,
bali pia machoni mwa wanadamu. 22 Pamoja nao,
tunamtuma ndugu yetu ambaye mara kwa mara
ametuthibitishia kwa njia nyingi kwamba ana shauku,
naam, zaidi sana sasa kwa sababu analo tumaini kuu
kwenu. 23 Kwa habari ya Tito, yeye ni mwenzangu
na mtendakazi pamoja nami miongoni mwenu. Kwa
habari za ndugu zetu, wao ni wawakilishi wa makundi
ya waumini, na utukufu kwa Al-Masihi. 24 Kwa hiyo
waonesheni wazi hawa ndugu uthibitisho wa upendo
wenu, na sababu inayotufanya tujivune kwa ajili yenu,
ili makundi ya waumini yapate kuona upendo wenu.

9 Hakuna haja ya kuwaandikia kuhusu huduma hii
kwa watakatifu. 2 Kwa kuwa ninajua mlivyo na
shauku ya kusaidia, nami nimekuwa nikijivuna kwa
ajili ya jambo hilo kwa Wamakedonia, nikiwaambia
kwamba ninyi watu wa Akaya mmekuwa tayari kutoa
tangu mwaka jana. Na shauku yenu imewachochea
wengi wao katika kutoa. 3 Lakini sasa nawatuma
hawa ndugu ili kujivuna kwetu kuhusu mchango wenu
kusiwe maneno matupu, bali mpate kuwa tayari kama
nilivyosema mngekuwa tayari. 4 Kwa maana nikija
na Mmakedonia yeyote na kuwakuta hamko tayari,
sisi, na hata ninyi pia, tungeona haya kwa kuwa
na ujasiri hivi katika ninyi. 5 Kwa hivyo niliona ni
muhimu niwahimize hawa ndugu watangulie kuja
huko kwenu kabla yangu, wafanye mipango ya hayo
matoleo ya ukarimu mliyokuwa mmeahidi, ili yawe
tayari kama matoleo ya hiari wala si kama ya kutozwa
kwa nguvu. 6 Kumbukeni kwamba: Yeyote apandaye
haba pia atavuna haba, naye apandaye kwa ukarimu
pia atavuna kwa ukarimu. 7 Kila mtu atoe kama
anavyokusudia moyoni mwake, si kwa uchoyo au
kwa kulazimishwa, kwa maana Mungu humpenda
yeye atoaye kwa moyo mkunjufu. 8 Naye Mungu
aweza kuwapa kila baraka kwa wingi, ili katika mambo
yote kila wakati mwe na kila kitu mnachohitaji, ili
mweze kushiriki kwa wingi katika kila kazi njema.
9 Kama ilivyoandikwa: “Ametawanya vipawa vyake
kwa ukarimu akawapa maskini; haki yake hudumu
milele.” **(aiōn g165)** 10 Yeye ampaye mpanzi mbegu
ya kupanda, na mkate uwe chakula, atawapa na
kuzizidisha mbegu zenu za kupanda na kuongeza
mavuno ya haki yenu. 11 Mtatajirishwa kwa kila
namna ili mpate kuwa wakarimu kila wakati, na kupitia
kwetu ukarimu wenu utamletea Mungu shukrani. 12
Huduma hii mnayofanya si tu ya kukidhi mahitaji
ya watakatifu, bali huzidi sana kwa shukrani nyingi
kwake Mungu. 13 Kwa sababu ya huduma ambayo
mmejithibitisha wenyewe, watu watamtukuza Mungu
kwa ajili ya utiifu ufuatanao na ukiri wenu wa Injili ya
Al-Masihi, na kwa ukarimu wenu wa kuwashirikisha

wao na watu wengine wote. 14 Nayo mioyo yao
itawaonea shauku wanapowaombea, kwa sababu ya
neema ipitayo kiasi mliyopewa na Mungu. 15 Mungu
apewe shukrani kwa karama yake isiyoelezeka!

**10** Basi, mimi Paulo ninawasihi kwa unyenyekevu
na upole wa Al-Masihi, mimi niliye “mwoga”
ninapokuwa pamoja nanyi ana kwa ana, lakini mwenye
ujasiri nikiwa mbali nanyi! 2 Nawaomba nitakapokuja
kwenu nisipaswe kuwa na ujasiri dhidi ya watu
fulani kama ninavyotazamia kwa wale wanaodhani
kwamba tunaishi kwa kufuata mtazamo wa ulimwengu
huu. 3 Ingawa tunaishi duniani, hatupigani vita
kama ulimwengu ufanyavyo. 4 Silaha za vita vyetu
si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata
kuangusha ngome. 5 Tunaangusha mawazo na
kila kitu kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na
kuteka nyara kila fikira ipate kumtii Al-Masihi. 6 Tena
tunakuwa tayari kuadhibu kila tendo la kutotii, hapo
kutii kwenu kutakapokamilika. 7 Mnayaangalia yaliyo
mbele ya macho yenu tu. Kama mtu yeyote anaamini
kuwa yeye ni mali ya Al-Masihi, basi kumbuka kuwa
kama ulivyo wa Al-Masihi, vivyo hivyo na sisi ndivyo
tulivyo. 8 Basi hata nikijisifu zaidi kidogo kuhusu
mamlaka tuliyo nayo, ambayo Bwana Isa alitupatia ili
kuwajenga wala si kuwabomoa, mimi sitaionea haya.
9 Sitaki nionekane kama ninayejaribu kuwatisha kwa
nyaraka zangu. 10 Kwa maana wanasema, “Nyaraka
zake ni nzito na zenye nguvu, lakini ana kwa ana ni
mdhaifu, na kuzungumza kwake ni kwa kudharauliwa.”
11 Watu kama hao wajue ya kuwa yale tusemayo kwa
barua tukiwa hatupo pamoja nanyi ndivyo tulivyo,
na ndivyo tutakavyofanya tutakapokuwa pamoja
nanyi. 12 Hatuthubutu kujiweka kwenye kundi moja
au kujilinganisha na hao wanaojitukuza wenyewe
kuwa wao ni wa maana sana. Wanapojipima na
kujilinganisha wenyewe kwa wenyewe, wanaonesha
ya kuwa hawana busara. 13 Lakini sisi hatujajivuna
kupita kiasi, bali majivuno yetu yatakuwa katika mipaka
ya huduma ile Mungu aliyotuwekea, mipaka ambayo
inawafikia hata ninyi. 14 Kwa maana hatukuwa
tunavuka mipaka katika kujisifu kwetu, kama ambavyo
ingekuwa tusingekuja kwenu. Kwa maana sisi ndio
tuliokuwa wa kwanza kuja kwenu na Injili ya Al-Masihi.
15 Wala hatuvuki mipaka kwa kujisifu kwetu kwa ajili
ya kazi iliyofanywa na watu wengine. Tumaini letu ni
kwamba imani yenu inavyozidi kukua, ndivyo eneo
letu la utendaji miongoni mwenu litapanuka zaidi, 16 ili
tuweze kuhubiri Injili sehemu zilizo mbali na maeneo
yenu. Kwa maana hatutaki kujisifu kwa ajili ya kazi
ambayo imekwisha kufanyika tayari katika eneo la
mtu mwingine. 17 Lakini, “Yeye ajisifuye na ajisifu
katika Mwenyezi Mungu.” 18 Kwa maana si yeye
ajisifuye mwenyewe akubaliwaye, bali yeye ambaye
Mwenyezi Mungu humsifu.

**11** Laiti mngenivumilia kidogo katika upumbavu
wangu! Naam, nivumilieni kidogo. 2 Ninawaonea
wivu, wivu wa kiungu, kwa kuwa mimi niliwaposea
mume mmoja, ili niwalete kwa Al-Masihi kama
mabikira safi. 3 Lakini nina hofu kuwa, kama vile Hawa
alivyodanganywa kwa ujanja wa yule nyoka, mawazo
yenu yasije yakapotoshwa, mkauacha unyofu na usafi
wa upendo wenu kwa Al-Masihi. 4 Kwa sababu mtu
akija na kuwahubiria Isa mwingine ambaye si yule
tuliyemhubiri, au mkipokea roho mwingine ambaye si
yule mliyempokea, au Injili tofauti na ile mliyoikubali,
ninyi mnaitii kwa urahisi. 5 Lakini sidhani ya kuwa
mimi ni dhalili sana kuliko hao “mitume wakuu”. 6
Inawezekana mimi si mnenaji hodari, lakini ni hodari
katika elimu. Jambo hili tumelifanya liwe dhahiri kwenu
kwa njia zote. 7 Je, nilitenda dhambi kwa kujishusha ili
kuwainua ninyi kwa kuwahubiria Injili ya Mungu pasipo
malipo? 8 Niliyanyang’anya makundi mengine ya
waumini kwa kupokea misaada kutoka kwao ili niweze
kuwahudumia ninyi. 9 Nami nilipokuwa pamoja nanyi,
nilipopungukiwa na chochote, sikuwa mzigo kwa
mtu yeyote, kwa maana ndugu waliotoka Makedonia
walitimiza mahitaji yangu. Kwa hiyo nilijizuia kuwa
mzigo kwenu kwa njia yoyote, nami nitaendelea
kujizuia. 10 Kwa hakika kama vile kweli ya Al-Masihi
ilivyo ndani yangu, hakuna mtu yeyote katika Akaya
nzima atakayenizuia kujivunia jambo hili. 11 Kwa
nini? Je, ni kwa sababu siwapendi? Mungu anajua
ya kuwa nawapenda! 12 Nami nitaendelea kufanya
lile ninalofanya sasa ili nisiwape nafasi wale ambao
wanatafuta nafasi ya kuhesabiwa kuwa sawa na sisi
katika mambo wanayojisifia. 13 Watu kama hao ni
mitume wa uongo, ni wafanyakazi wadanganyifu,
wanaojigeuza waonekane kama mitume wa Al-
Masihi. 14 Wala hii si ajabu, kwa kuwa hata Shetani
mwenyewe hujigeuza aonekane kama malaika wa
nuru. 15 Kwa hiyo basi si ajabu kama watumishi wa
Shetani nao hujigeuza ili waonekane kama watumishi

wa haki. Mwisho wao utakuwa sawa na matendo yao
yanavyostahili. 16 Nasema tena: mtu yeyote asidhani
kwamba mimi ni mjinga. Lakini hata mkinidhania
hivyo, basi nipokeeni kama mjinga ili nipate kujisifu
kidogo. 17 Ninayosema kuhusiana na huku kujisifu
kwa kujiamini, sisemi vile Bwana Isa angesema, bali
kama mjinga. 18 Kwa kuwa wengi wanajisifu kama vile
ulimwengu ufanyavyo, mimi nami nitajisifu. 19 Ninyi
mwachukuliana na wajinga kwa sababu mna hekima
sana! 20 Kweli ni kwamba mnachukuliana na mtu
akiwatia utumwani au akiwatumia kwa ajili ya kupata
faida, au akiwanyang'anya, au akijitukuza mwenyewe,
au akiwadanganya. 21 Kwa aibu inanipasa niseme
kwamba sisi tulikuwa dhaifu sana kwa jambo hilo!
Lakini jambo lolote ambalo mtu mwingine angethubutu
kujisifia, ninene kama mjinga, nami nathubutu kujisifu
kuhusu hilo. 22 Je, wao ni Waebrania? Mimi pia
ni Mwebrania. Je, wao ni Waisraeli? Mimi pia ni
Mwisraeli. Je, wao ni wazao wa Ibrahimu? Mimi pia
ni mzao wa Ibrahimu. 23 Je, wao ni watumishi wa
Al-Masihi? (Nanena kiwazimu.) Mimi ni zaidi yao.
Nimefanya kazi kwa bidii zaidi yao, nimefungwa
gerezani mara kwa mara, nimepigwa mijeledi sana,
na nimekabiliwa na mauti mara nyingi. 24 Mara tano
nimepigwa na Wayahudi mijeledi arobaini kasoro moja.
25 Mara tatu nilipigwa mijeledi, mara moja nilipigwa
kwa mawe, mara tatu nilivunjikiwa na meli, nilikaa
kilindini usiku kucha na mchana kutwa; 26 nimekuwa
katika safari za mara kwa mara. Nimekabiliwa na
hatari za kwenye mito, hatari za wanyang'anyi, hatari
kutoka kwa Wayahudi wenzangu, hatari kutoka kwa
watu wa Mataifa; hatari mijini, hatari nyikani, hatari
baharini; na hatari kutoka kwa ndugu wa uongo. 27
Nimekuwa katika kazi ngumu na taabu, katika kukesha
mara nyingi; nimejua kukaa njaa na kuona kiu;
nimefunga kula chakula mara nyingi; nimehisi baridi
na kuwa uchi. 28 Zaidi ya hayo yote, nakabiliwa kila
siku na mzigo wa wajibu wangu kwa makundi yote ya
waumini. 29 Je, ni nani aliye mdhaifu, nami nisijisikie
mdhaifu? Je, nani aliyekwazwa, nami nisiudhike? 30
Kama ni lazima nijisifu, basi nitajisifia yale mambo
yanayoonesha udhaifu wangu. 31 Mungu na Baba wa
Bwana wetu Isa, yeye ambaye anahimidiwa milele,
anajua ya kuwa mimi sisemi uongo. **(aiōn g165)** 32
Huko Dameski, mtawala aliyekuwa chini ya Mfalme
Areta aliulinda mji wa Dameski ili kunikamata. 33
Lakini niliteremshwa kwa kapu kubwa kupitia dirisha
ukutani, nikaokolewa kutoka mkononi mwake.

**12** Yanipasa nijisifu. Ingawa haifaidi kitu, nitanena
kuhusu maono na mafunuo kutoka kwa Bwana
Isa. 2 Namjua mtu mmoja katika Al-Masihi ambaye
miaka kumi na nne iliyopita alichukuliwa juu hadi
mbingu ya tatu. Kama ni katika mwili au nje ya mwili,
sijui, Mungu ajua. 3 Nami najua kwamba mtu huyu, iwe
ni katika mwili au nje ya mwili mimi sijui, lakini Mungu
ajua, 4 alinyakuliwa hadi Paradiso. Huko alisikia
mambo yasiyoelezeka, mambo ambayo binadamu
hana ruhusa ya kuyasimulia. 5 Nitajisifu kwa ajili ya mtu
kama huyo, lakini sitajisifu mwenyewe, ila nitajisifia
udhaifu wangu. 6 Hata kama ningependa kujisifu,
sitakuwa mjinga, kwa maana nitakuwa nasema kweli.
Lakini najizuia, ili mtu yeyote asije akaniona mimi kuwa
bora kuliko ninavyoonekana katika yale ninayotenda
na kusema, 7 au kwa sababu ya mafunuo haya
makuu. Ili kunizuia nisijivune, nilipewa mwiba katika
mwili wangu, mjumbe wa Shetani, ili anitese. 8 Kwa
habari ya jambo hili, nilimsihi Mwenyezi Mungu mara
tatu aniondolee mwiba huu. 9 Lakini aliniambia,
“Neema yangu inakutosha, kwa kuwa uweza wangu
hukamilika katika udhaifu.” Kwa hiyo nitajisifu kwa
furaha zaidi kuhusu udhaifu wangu, ili uweza wa Al-
Masihi ukae juu yangu. 10 Hii ndiyo sababu nafurahia
katika udhaifu, katika kutukanwa, katika taabu, katika
mateso na katika shida kwa ajili ya Al-Masihi. Kwa
maana ninapokuwa dhaifu, ndipo nina nguvu. 11
Nimejifanya mjinga, lakini mmenilazimisha niwe hivyo.
Kwa kuwa ilinipasa kusifiwa na ninyi, kwa sababu
mimi si dhalili kuliko wale “mitume walio bora”, ingawa
mimi si kitu. 12 Mambo yanayomtambulisha mtume
wa kweli, yaani ishara, miujiza na maajabu, yalifanywa
miongoni mwenu kwa saburi nyingi. 13 Je, ninyi ni kitu
gani mlichopungukiwa kuliko makundi mengine ya
waumini, ila tu kwamba mimi sikuwa mzigo kwenu?
Nisameheni kwa kosa hili! 14 Sasa niko tayari kuja
kwenu kwa mara ya tatu. Nami sitawalemea, kwa
sababu sihitaji chochote chenu, ila ninawahitaji ninyi.
Kwa kuwa watoto hawaweki akiba kwa ajili ya wazazi
wao, bali wazazi huweka akiba kwa ajili ya watoto
wao. 15 Hivyo nitafurahi kutumia kila kitu nilicho
nacho kwa ajili yenu, hata mwili wangu pia. Je,
ninavyozidi kuwapenda, ndivyo upendo wenu kwangu
unavyopungua? 16 Iwe iwavyo, kwa vyovyote vile,

mimi sikuwalemea. Lakini wengine wanadhani mimi
ni mjanja, nami niliwapata kwa hila! 17 Je, nilijipatia
faida kwa kumtumia mtu yeyote niliyemtuma kwenu?
18 Nilimshawishi Tito aje kwenu, nami nilimtuma
pamoja na ndugu yetu. Je, Tito aliwatumia ninyi ili
kujipatia faida? Je, hatukuenenda kwa roho moja,
na kwa hatua zile zile? 19 Je, mmekuwa mkifikiri
kwamba sisi tunajaribu kujitetea mbele yenu? Sisi
tumekuwa tukinena mbele za Mungu kama wale
walio katika Al-Masihi. Na chochote tufanyacho,
ndugu wapendwa, ni kwa ajili ya kuwatia nguvu. 20
Kwa kuwa nina hofu kwamba nitakapokuja naweza
kuwakuta nisivyotaka, nanyi mkanikuta msivyotaka.
Nina hofu kwamba panaweza kuwa na ugomvi,
wivu, ghadhabu, fitina, masingizio, masengenyo,
majivuno na machafuko. 21 Nina hofu kwamba
nitakapokuja tena kwenu, Mungu wangu atanidhili
mbele yenu, nami nitasikitishwa na wengi waliotenda
dhambi mbeleni, na wala hawajatubu kwa uchafu
wao, uasherati, na ufisadi walioushiriki.

13 Hii itakuwa mara ya tatu mimi kuja kwenu.
"Shtaka lolote lazima lithibitishwe na mashahidi
wawili au watatu." 2 Niliwaonya nilipokuwa pamoja
nanyi mara ya pili. Sasa narudia wakati sipo, kwamba
nikija tena sitawahurumia wale waliokuwa wametenda
dhambi hapo awali au wengine wote, 3 kwa kuwa
mnadai uthibitisho kwamba Al-Masihi anazungumza
kwa kunitumia mimi. Yeye si dhaifu katika kushughulika
nanyi, bali ana nguvu kati yenu. 4 Kwa kuwa
alisulubiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za
Mungu. Vivyo hivyo, sisi tu dhaifu kupitia kwake, lakini
katika kuwashughulikia ninyi tutaishi pamoja naye kwa
nguvu za Mungu. 5 Jichunguzeni wenyewe mwone
kama mnaishi katika imani. Jipimeni wenyewe. Je,
hamtambui ya kuwa Isa Al-Masihi yu ndani yenu?
Kama sivyo, basi, mmeshindwa kufikia kipimo hicho!
6 Natumaini mtaona kuwa sisi hatukushindwa. 7 Lakini
tunamwomba Mungu msije mkatenda kosa lolote, si
ili sisi tuonekane kuwa tumeshinda hilo jaribio, bali
ili ninyi mtende lililo haki, hata kama tutaonekana
kuwa tumeshindwa. 8 Kwa maana hatuwezi kufanya
lolote kinyume na kweli, bali kuithibitisha kweli tu.
9 Tunafurahi wakati wowote tunapokuwa dhaifu,
lakini ninyi mkawa na nguvu. Nayo maombi yetu
ni kwamba mpate kuwa wakamilifu. 10 Hii ndiyo
sababu nawaandikia mambo haya wakati sipo, ili
nikija nisiwe mkali katika kutumia mamlaka yangu,
mamlaka Bwana Isa aliyonipa ya kuwajenga ninyi
wala si ya kuwabomoa. 11 Hatimaye, ndugu zangu,
kwaherini. Kuweni wakamilifu, farijianeni, kuweni
na nia moja, na mkae kwa amani. Naye Mungu
wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. 12
Salimianeni kwa busu takatifu. 13 Watakatifu wote
wanawasalimu. 14 Neema ya Bwana Isa Al-Masihi, na
upendo wa Mungu, na ushirika wa Roho wa Mungu
ukae nanyi nyote.

# Wagalatia

1 Paulo mtume, si mtume wa wanadamu wala
aliyetumwa na mwanadamu, bali na Isa Al-Masihi
na Mungu Baba Mwenyezi aliyemfufua Isa kutoka
kwa wafu, 2 na ndugu wote walio pamoja nami. 3
Neema na amani zitokazo kwa Mungu, Baba yetu,
na kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi ziwe nanyi, 4
yeye aliyejitoa kwa ajili ya dhambi zetu ili apate
kutuokoa katika ulimwengu huu wa sasa ulio mbaya,
sawasawa na mapenzi yake yeye aliye Mungu na
Baba yetu. **(aiōn g165)** 5 Utukufu una yeye milele
na milele. Amen. **(aiōn g165)** 6 Nashangaa kwamba
mnamwacha upesi hivyo yeye aliyewaita kwa neema
ya Al-Masihi na kuifuata Injili nyingine, 7 ambayo
kwa kweli si Injili kamwe, ila kwa dhahiri kuna watu
wanaowachanganya na wanaotaka kuipotosha Injili
ya Al-Masihi. 8 Lakini hata ikiwa sisi au malaika
atokaye mbinguni akihubiri Injili nyingine tofauti na ile
tuliyowahubiria sisi, basi mtu huyo alaaniwe milele! 9
Kama vile tulivyokwisha kusema kabla, sasa nasema
tena, ikiwa mtu yeyote atawahubiria Injili kinyume na
ile mliyoipokea na alaaniwe milele! 10 Je, sasa mimi
ninatafuta kukubaliwa na wanadamu au kukubaliwa na
Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama
ningekuwa bado najaribu kuwapendeza wanadamu,
nisingekuwa mtumishi wa Al-Masihi. 11 Ndugu zangu,
nataka mjue kwamba Injili niliyowahubiria haikutokana
na wanadamu. 12 Kwa maana mimi sikuipokea hiyo
Injili kutoka kwa mwanadamu, wala sikufundishwa
na mtu, bali niliipata kwa ufunuo kutoka kwa Isa Al-
Masihi. 13 Ninyi mmekwisha kusikia kuhusu maisha
yangu ya zamani nilipokuwa katika dini ya Kiyahudi,
jinsi nilivyotesa makundi ya waumini wa Mungu kwa
nguvu na kujaribu kuwaangamiza. 14 Nami niliendelea
sana katika dini ya Kiyahudi kuliko Wayahudi wengi
wa rika langu, maana nilijitahidi sana katika desturi
za baba zangu. 15 Lakini ilipompendeza Mungu,
aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu na
kuniita kwa neema yake, 16 alimdhihirisha Mwanawe
kwangu, ili nipate kumhubiri miongoni mwa watu wa
Mataifa. Mimi sikushauriana na mwanadamu yeyote,
17 wala sikupanda kwenda Yerusalemu kuwaona hao
waliokuwa mitume kabla yangu, bali nilienda mara
moja Arabuni na kisha nikarudi Dameski. 18 Kisha
baada ya miaka mitatu nilipanda kwenda Yerusalemu
kuonana na Kefa na nilikaa naye siku kumi na tano. 19
Lakini sikumwona mtume mwingine yeyote isipokuwa
Yakobo, ndugu yake Bwana Isa. 20 Nawahakikishia
mbele za Mungu kuwa ninayowaandikia si uongo.
21 Baadaye nilienda sehemu za Siria na Kilikia. 22
Lakini mimi binafsi sikujulikana kwa makundi ya
waumini huko Yudea yaliyo katika Al-Masihi. 23
Wao walisikia habari tu kwamba, “Mtu yule ambaye
hapo awali alikuwa akitutesa sasa anahubiri imani
ile ile aliyokuwa akijaribu kuiangamiza.” 24 Nao
wakamtukuza Mungu kwa sababu yangu.

2 Kisha, baada ya miaka kumi na nne, nilipanda
tena kwenda Yerusalemu, wakati huu pamoja
na Barnaba, na nikamchukua Tito pia. 2 Nilienda
kwa sababu nilikuwa nimefunuliwa na Mungu, ili
nikawaeleze kwa faragha wale walioonekana kuwa
viongozi, ile Injili ninayoihubiri kwa watu wa Mataifa.
Nilifanya hivyo kwa kuhofia kwamba nisije nikawa
nilikuwa ninakimbia au nilikimbia bure. 3 Lakini
hata Tito aliyekuwa nami, na alikuwa Myunani,
hakulazimika kutahiriwa. 4 Lakini kwa sababu ya
ndugu wa uongo ambao walijiingiza kwa siri katikati
yetu ili kupeleleza uhuru tulio nao katika Al-Masihi
Isa, wapate kututia utumwani, 5 hatukukubaliana nao
hata dakika moja, ili ukweli wa Injili ubaki nanyi. 6
Kwa habari ya wale waliokuwa wakubaliwe kuwa
viongozi (kwangu mimi sikujali vyeo vyao, maana
Mungu hana upendeleo), wale watu hawakuniongezea
chochote. 7 Badala yake walitambua kwamba
nilikuwa nimekabidhiwa kazi ya kuhubiri Injili kwa
watu wa Mataifa, kama vile Petro alivyokabidhiwa
kuhubiri Injili kwa Wayahudi. 8 Kwa maana, Mungu
aliyekuwa akitenda kazi katika huduma ya Petro
kama mtume kwa Wayahudi, ndiye pia aliyekuwa
anatenda kazi katika huduma yangu kama mtume
kwa watu wa Mataifa. 9 Basi Yakobo, Kefa na Yohana,
walioonekana kama nguzo za jumuiya ya waumini,
walitupatia mkono wa shirika, mimi na Barnaba,
walipotambua ile neema niliyopewa. Wakakubali
kwamba sisi twende kwa watu wa Mataifa, na wao
waende kwa Wayahudi. 10 Walichotuomba ni kwamba
tuendelee kuwakumbuka maskini, jambo ambalo ndilo
nililokuwa na shauku ya kulifanya. 11 Lakini Petro
alipofika Antiokia, mimi nilimpinga ana kwa ana kwa
sababu alikuwa amekosea kwa wazi. 12 Kabla baadhi
ya watu waliotoka kwa Yakobo hawajafika, alikuwa

akila pamoja na watu wa Mataifa. Lakini hao watu
walipofika alianza kujiondoa na kujitenga na watu wa
Mataifa kwa sababu aliwaogopa wale wa kundi la
tohara. 13 Pia Wayahudi wengine waliungana naye
katika unafiki huu, hata Barnaba naye akapotoshwa
na unafiki wao. 14 Nilipoona kwamba hawatendi
sawasawa na kweli ya Injili, nilimwambia Petro mbele
ya wote, "Wewe ni Myahudi, nawe unaishi kama mtu
wa Mataifa na wala si kama Myahudi. Imekuwaje basi,
mnawalazimisha watu wa Mataifa kufuata desturi
za Kiyahudi? 15 "Sisi wenyewe ni Wayahudi kwa
kuzaliwa na si watu wenye dhambi kama watu wa
Mataifa, 16 bado tunajua kwamba mtu hahesabiwi
haki kwa matendo ya sheria bali kupitia kwa imani
katika Isa Al-Masihi. Hivyo sisi pia, tumemwamini Al-
Masihi Isa ili tupate kuhesabiwa haki kupitia kwa imani
katika Al-Masihi, wala si kwa matendo ya sheria,
kwa sababu kwa kushika sheria hakuna hata mtu
mmoja atakayehesabiwa haki. 17 "Lakini tukitafuta
kuhesabiwa haki katika Al-Masihi, inakuwa dhahiri
kwamba sisi ni wenye dhambi. Je, ina maana kwamba
Al-Masihi amekuwa mtumishi wa dhambi? La hasha!
18 Lakini ikiwa mimi ninajenga tena kile ambacho
nimekwisha kukibomoa, basi ninaonesha kwamba
mimi ni mkosaji. 19 Kwa maana mimi kupitia kwa
sheria, nimeifia sheria ili nipate kuishi kwa ajili ya
Mungu. 20 Nimesulubiwa pamoja na Al-Masihi, wala
si mimi tena ninayeishi, bali Al-Masihi ndiye aishiye
ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi
kwa imani katika Mwana wa Mungu, aliyenipenda
na kujitoa kwa ajili yangu. 21 Siibatilishi neema ya
Mungu, kwa maana kama haki ingeweza kupatikana
kupitia kwa Torati, basi Al-Masihi alikufa bure!"

**3** Ninyi Wagalatia wajinga! Ni nani aliyewaroga?
Isa Al-Masihi aliwekwa wazi mbele yenu kwamba
amesulubiwa. 2 Nataka nijifunze neno moja kutoka
kwenu: Je, mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika
Torati, au kwa kuyaamini yale mliyosikia? 3 Je,
ninyi ni wajinga kiasi hicho? Baada ya kuanza kwa
Roho, je, sasa mwataka kumalizia katika mwili?
4 Je, mlipata mateso kiasi hicho bure? Ni kama
kweli yalikuwa bure! 5 Je, Mungu huwapa Roho
wake Mtakatifu na kufanya miujiza kati yenu kwa
sababu mnatii Torati, au kwa sababu mnaamini kile
mlichosikia? 6 Kama vile "Ibrahimu alimwamini Mungu
na ikahesabiwa kwake kuwa haki." 7 Fahamuni basi
kwamba wale walio na imani, hao ndio watoto wa
Ibrahimu. 8 Andiko liliona tangu awali kwamba Mungu
angewahesabia haki watu wa Mataifa kwa imani,
hivyo likatangulia kumtangazia Ibrahimu Injili, likisema
kwamba, "Kupitia kwako mataifa yote yatabarikiwa." 9
Kwa sababu hii, wale wote wanaoamini wanabarikiwa
pamoja na Ibrahimu, mtu wa imani. 10 Kwa maana
wote wanaotumainia matendo ya Torati wako chini
ya laana, kwa kuwa imeandikwa, "Alaaniwe kila
mtu asiyeshikilia kutii mambo yote yaliyoandikwa
katika Kitabu cha Torati." 11 Basi ni dhahiri kwamba
hakuna mtu anayehesabiwa haki mbele za Mungu
kwa kushikilia Torati, kwa maana, "Mwenye haki
ataishi kwa imani." 12 Lakini Torati haitegemei imani.
Kinyume chake, "Mtu atendaye matendo hayo ataishi
kwa hayo." 13 Al-Masihi alitukomboa kutoka laana ya
Torati kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana
imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya
mti." 14 Alitukomboa ili baraka aliyopewa Ibrahimu
ipate kuwafikia watu wa Mataifa kupitia kwa Al-Masihi
Isa, ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Roho
wa Mungu. 15 Ndugu zangu, nataka nitoe mfano
kutoka maisha ya kila siku. Kama vile hakuna mtu
awezaye kutangua au kuongeza kitu katika agano
la mtu ambalo limekwisha kuthibitishwa, vivyo hivyo
kwa hali kama hii. 16 Ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu
na kwa mzao wake. Maandiko hayasemi "kwa uzao",
yakimaanisha watu wengi, bali "kwa mzao wako",
yaani mtu mmoja, ndiye Al-Masihi. 17 Ninachotaka
kusema ni kwamba, Torati, ambayo ilitolewa miaka
mia nne na thelathini baadaye, haitangui agano
lililothibitishwa na Mungu ili kuibatilisha ahadi ile. 18
Kwa maana kama urithi hupatikana kwa Torati, basi
hautegemei tena ahadi, lakini Mungu kwa neema
yake alimpa Ibrahimu urithi kupitia kwa ahadi. 19 Kwa
nini basi iwepo Torati? Torati iliwekwa kwa sababu ya
makosa hadi atakapokuja yule Mzao wa Ibrahimu,
ambaye alitajwa katika ile ahadi. Torati iliamriwa
na malaika kwa mkono wa mpatanishi. 20 Basi
mpatanishi huhusisha zaidi ya upande mmoja, lakini
Mungu ni mmoja. 21 Je basi, Torati inapingana na
ahadi za Mungu? La hasha! Kwa maana kama Torati
iliyotolewa ingeweza kuwapa watu uzima, basi haki
ingepatikana kupitia kwa Torati. 22 Lakini Maandiko
yamefanya vitu vyote vifungwe chini ya nguvu ya
dhambi, ili yale yaliyoahidiwa kupitia kwa imani katika

Isa Al-Masihi yapate kupewa wale wanaoamini. 23
Kabla imani hii haijaja tulikuwa tumewekwa chini ya
Torati, tumefungwa hadi ile imani ifunuliwe. 24 Hivyo,
Torati ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Al-Masihi, ili
tupate kuhesabiwa haki kwa imani. 25 Lakini sasa
kwa kuwa ile imani imekuja, hatusimamiwi tena na
Torati. 26 Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto
wa Mungu katika Al-Masihi Isa kupitia kwa imani. 27
Kwa maana wote mliobatizwa ndani ya Al-Masihi,
mmemvaa Al-Masihi. 28 Wala hakuna tena Myahudi
au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala
mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani
ya Al-Masihi Isa. 29 Nanyi mkiwa ni mali ya Al-
Masihi, basi ninyi ni wa uzao wa Ibrahimu na warithi
sawasawa na ile ahadi.

**4** Lile nisemalo ni kwamba wakati wote mrithi bado
ni mtoto, hana tofauti na mtumwa, ingawa ndiye
mmiliki wa mali yote. 2 Yeye huwa chini ya uangalizi
wa walezi na wadhamini hadi ufike wakati uliowekwa
na baba yake. 3 Vivyo hivyo na sisi, tulipokuwa bado
watoto wadogo, tulikuwa utumwani chini ya taratibu
za kawaida za ulimwengu. 4 Lakini wakati uliopangwa
ulipotimia, Mungu alimtuma Mwanawe, ambaye
alizaliwa na mwanamke, akazaliwa chini ya sheria, 5
ili awakomboe wale waliokuwa chini ya sheria, nasi
tupate kupokea zile haki kamili za kufanywa wana.
6 Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu
amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu,
anayelia, “Abba, Baba.” 7 Kwa hiyo, wewe si mtumwa
tena, bali ni mwana. Na kwa kuwa wewe ni mwana,
Mungu amekufanya wewe pia kuwa mrithi kupitia kwa
Al-Masihi. 8 Zamani, mlipokuwa hammjui Mungu,
mlikuwa watumwa wa viumbe ambavyo kwa asili si
Mungu. 9 Lakini sasa kwa kuwa mmemjua Mungu,
au zaidi mmejulikana na Mungu, inakuwaje mnarejea
tena katika zile kanuni za kwanza zenye udhaifu
na upungufu? Mnataka ziwafanye tena watumwa?
10 Mnaadhimisha siku maalum, miezi, nyakati na
miaka! 11 Nina hofu juu yenu, kwamba kazi niliyofanya
kwa ajili yenu inaweza kuwa nimejitaabisha bure.
12 Ndugu zangu, nawasihi mwe kama mimi, kwa
sababu mimi nimekuwa kama ninyi. Hamkunitendea
jambo lolote baya. 13 Ninyi mwajua kwamba ni kwa
ajili ya udhaifu wangu niliwahubiria Injili. 14 Ingawa
hali yangu iliwatia majaribuni, hamkunidharau wala
kunidhihaki, bali mlinikaribisha kama malaika wa
Mungu, kama vile Al-Masihi Isa. 15 Ile hali ya furaha
mliyokuwa nayo imeenda wapi? Naweza kushuhudia
kwamba, kama ingewezekana mngeng’oa macho
yenu na kunipa mimi. 16 Je, sasa nimekuwa adui
yenu kwa kuwaambia ukweli? 17 Hao wana shauku
ya kuwapata lakini si kwa kusudi zuri. Wanachotaka
ni kuwatenga mbali nasi, ili ninyi mpate kuwaonea
wao shauku. 18 Ni vizuri wakati wote kuwa na shauku
kwa ajili ya kusudi zuri, si wakati nikiwa pamoja nanyi
tu. 19 Watoto wangu wapendwa, ambao kwa mara
nyingine ninawaonea uchungu, ninatamani kwamba
Al-Masihi aumbike ndani yenu. 20 Natamani kama
ningekuwa pamoja nanyi sasa, pengine ningebadilisha
sauti yangu. Kwa maana nina wasiwasi kwa ajili
yenu. 21 Niambieni, ninyi mnaotaka kuwa chini ya
sheria, je, hamjui sheria inavyosema? 22 Kwa maana
imeandikwa kwamba Ibrahimu alikuwa na wana
wawili, mmoja wa mwanamke mtumwa na wa pili wa
mwanamke huru. 23 Lakini, mtoto wa mwanamke
mtumwa alizaliwa kwa mapenzi ya mwili, na yule
mwingine wa mwanamke huru alizaliwa kutokana
na ahadi ya Mungu. 24 Mambo haya yanaweza
kuchukuliwa kama mfano. Kwa maana hao wanawake
wawili ni mfano wa maagano mawili: Agano la kwanza
ni lile lililofanyika katika Mlima Sinai, linalozaa watoto
wa utumwa. Hili ndilo huyo Hajiri. 25 Basi Hajiri
anawakilisha Mlima Sinai ulio Arabuni, na unafanana
na Yerusalemu ya sasa ambayo iko utumwani pamoja
na watoto wake. 26 Lakini Yerusalemu wa juu
ni huru, nayo ndiye mama yetu. 27 Kwa maana
imeandikwa: “Furahi, ewe mwanamke tasa, wewe
usiyezaa; paza sauti, na kuimba kwa furaha, wewe
usiyepatwa na uchungu wa kuzaa; kwa maana watoto
wa mwanamke aliyeachwa ukiwa ni wengi kuliko
wa mwanamke mwenye mume.” 28 Basi, sisi ndugu
zangu, ni kama Isaka, tu watoto wa ahadi. 29 Lakini,
kama vile ilivyokuwa siku zile yule aliyezaliwa kwa
mwili alivyomchokoza yule aliyezaliwa kwa uweza
wa Roho wa Mungu, ndivyo ilivyo hata sasa. 30
Lakini Maandiko yasemaje? “Mwondoe mwanamke
mtumwa pamoja na mwanawe, kwa sababu mwana
wa mwanamke mtumwa kamwe hatarithi pamoja na
mwana wa aliye huru.” 31 Kwa hiyo ndugu zangu, sisi
si watoto wa mwanamke mtumwa, bali wa yule aliye
huru.

**5** Al-Masihi alitupatia uhuru, akataka tubaki huru.
Hivyo simameni imara wala msikubali tena
kulemewa na nira ya utumwa. **2** Sikilizeni! Mimi,
Paulo, nawaambieni kwamba mkikubali kutahiriwa,
basi Al-Masihi hatakuwa na thamani kwenu hata
kidogo. **3** Namshuhudia tena kila mtu anayekubali
kutahiriwa kwamba inampasa kushika Torati yote. **4**
Ninyi mnaotafuta kuhesabiwa haki kupitia kwa Torati
mmetengwa na Al-Masihi, mko mbali na neema ya
Mungu. **5** Kwa maana, kupitia Roho wa Mungu
tunangojea kwa shauku tumaini la haki kwa imani. **6**
Kwa maana ndani ya Al-Masihi Isa, kutahiriwa au
kutokutahiriwa hakuleti tofauti, bali lililo muhimu ni
imani itendayo kazi kupitia kwa upendo. **7** Mlikuwa
mkipiga mbio vizuri. Ni nani aliyewazuia msiitii kweli? **8**
Ushawishi kama huo haukutoka kwa yule anayewaita.
**9** “Chachu kidogo huchachua donge zima.” **10**
Nina hakika katika Bwana Isa kwamba hamtakuwa
na msimamo mwingine. Mtu anayewachanganya
anastahili adhabu, hata awe nani. **11** Lakini ndugu
zangu, kama mimi bado ninahubiri kuhusu kutahiriwa,
kwa nini bado ninateswa? Katika hiyo hali basi, kwazo
la msalaba limeondolewa. **12** Laiti hao wanaowavuruga
wangejihasi wao wenyewe! **13** Ndugu zangu, ninyi
mliitwa ili mwe huru, hivyo msitumie uhuru wenu kama
fursa ya kufuata tamaa za mwili, bali tumikianeni
ninyi kwa ninyi kwa upendo. **14** Kwa maana Torati
yote hukamilika katika amri moja: “Mpende jirani
yako kama nafsi yako.” **15** Lakini mkiumana na
kutafunana, angalieni msije mkaangamizana. **16**
Kwa hiyo nasema, nendeni kwa Roho wa Mungu,
wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. **17**
Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume na
Roho, naye Roho hutamani yale yaliyo kinyume na
mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu hiyo
hamwezi kufanya mnayotaka. **18** Lakini mkiongozwa
na Roho wa Mungu, hamko chini ya Torati. **19** Basi
matendo ya mwili ni dhahiri, nayo ni haya: Uasherati,
uchafu, ufisadi, **20** kuabudu sanamu, uchawi, uadui,
ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, **21** husuda,
ulevi, ulafi na mambo mengine yanayofanana na
hayo. Nawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya
kabla, kwamba watu watendao mambo kama hayo,
hawataurithi ufalme wa Mungu. **22** Lakini tunda la
Roho wa Mungu ni upendo, furaha, amani, uvumilivu,
utu wema, fadhili, uaminifu, **23** upole na kiasi. Katika
mambo kama haya hakuna sheria. **24** Wote walio
wa Al-Masihi Isa wameusulubisha mwili na shauku
zake pamoja na tamaa zake. **25** Kwa kuwa tunaishi
kwa Roho wa Mungu, basi, tuenende kwa Roho. **26**
Tusijisifu bure, tukichokozana na kuoneana wivu.

**6** Ndugu zangu, ikiwa mtu amepatikana akitenda
dhambi, basi ninyi mnaoishi kwa Roho wa Mungu
mnapaswa kumrejesha mtu huyo kwa upole. Lakini
jihadharini, ili ninyi wenyewe msije mkajaribiwa. **2**
Chukulianeni mizigo ninyi kwa ninyi, nanyi kwa njia
hii mtatimiza sheria ya Al-Masihi. **3** Mtu yeyote
akijiona kuwa yeye ni bora na kumbe sivyo, basi
mtu huyo anajidanganya mwenyewe. **4** Lakini kila
mtu na aipime kazi yake mwenyewe, ndipo aweze
kujisifu, bila kujilinganisha na mtu mwingine. **5**
Kwa maana, kila mtu atauchukua mzigo wake
mwenyewe. **6** Basi, yeye afundishwaye katika neno
na amshirikishe mwalimu wake mema yote. **7**
Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile
apandacho mtu ndicho atakachovuna. **8** Apandaye
kwa mwili, katika mwili wake atavuna uharibifu,
lakini yeye apandaye katika Roho wa Mungu, katika
Roho atavuna uzima wa milele. **(aiōnios g166)** **9**
Hivyo, tusichoke katika kutenda mema, kwa kuwa
tutavuna kwa wakati wake tusipokata tamaa. **10** Kwa
hiyo, kadiri tupatavyo nafasi na tuwatendee watu
wote mema, hasa wale wa jamaa ya waumini. **11**
Angalieni herufi kubwa ninazotumia nikiwaandikia
kwa mkono wangu mwenyewe! **12** Wale wanaotaka
kuonekana wazuri kwa mambo ya mwili wanataka
wawalazimishe kutahiriwa. Sababu pekee ya kufanya
hivyo ni kuepuka kuteswa kwa ajili ya msalaba wa Al-
Masihi. **13** Hata wale waliotahiriwa wenyewe hawaitii
sheria, lakini wanataka ninyi mtahiriwe ili wapate
kujivuna kwa habari ya miili yenu. **14** Lakini mimi
naomba nisije nikajivunia kitu chochote isipokuwa
msalaba wa Bwana wetu Isa Al-Masihi, ambaye kwake
ulimwengu umesulubiwa kwangu, nami nimesulubiwa
kwa ulimwengu. **15** Kwa maana katika Al-Masihi
Isa, kutahiriwa au kutokutahiriwa si kitu, bali kule
kuwa kiumbe kipya ni kila kitu! **16** Amani na rehema
viwe na wote wanaofuata kanuni hii, hata kwa Israeli
wa Mungu. **17** Hatimaye, tangu sasa mtu yeyote
asinitaabishe, kwa maana nachukua katika mwili
wangu chapa zake Isa. **18** Ndugu zangu, neema ya

Bwana wetu Isa Al-Masihi iwe pamoja na roho zenu.
Amen.

# Waefeso

1 Paulo, mtume wa Al-Masihi Isa, kwa mapenzi
ya Mungu. 2 Neema na amani zinazotoka kwa
Mungu, Baba yetu, na kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi
ziwe nanyi. 3 Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana
wetu Isa Al-Masihi, aliyetubariki sisi kwa baraka zote
za rohoni, katika ulimwengu wa roho ndani ya Al-
Masihi. 4 Kwa maana alituchagua katika yeye kabla
ya kuumbwa kwa ulimwengu ili tuwe watakatifu na
bila lawama mbele zake. Kwa upendo 5 alitangulia
kutuchagua tuwe wanawe kupitia kwa Isa Al-Masihi
kwa furaha na mapenzi yake. 6 Kwa hiyo tunamsifu
Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia sisi
katika Mwanawe Mpendwa. 7 Ndani yake tunao
ukombozi kupitia kwa damu yake, yaani msamaha
wa dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake
8 aliyotumiminia kwa wingi, kwa hekima yote na
maarifa yote. 9 Naye alitujulisha siri ya mapenzi
yake sawasawa na uradhi wa mapenzi yake, ambayo
alikusudia katika Al-Masihi, 10 ili yapate kutimizwa
wakati mkamilifu utakapowadia, yaani kuvitia vitu
vyote vya mbinguni na vya duniani pamoja, chini
ya kiongozi mmoja, ndiye Al-Masihi. 11 Katika Al-
Masihi sisi nasi tumepata urithi, tukisha kuchaguliwa
tangu awali sawasawa na kusudi la Mungu, yeye
ambaye hufanya mambo yote kulingana na kusudi
la mapenzi yake, 12 ili, sisi tuliokuwa wa kwanza
kuweka tumaini katika Al-Masihi, tupate kuishi kwa
sifa ya utukufu wake. 13 Ninyi pia mliingia ndani ya Al-
Masihi mliposikia neno la kweli, Injili ya wokovu wenu.
Baada ya kuamini, mlitiwa muhuri ndani yake, huyo
Roho Mtakatifu wa Mungu mliyeahidiwa, 14 yeye
ambaye ni amana yetu ya kutuhakikishia urithi wetu
hadi ukombozi wa wale walio milki ya Mungu, kwa sifa
ya utukufu wake. 15 Kwa sababu hii, tangu niliposikia
kuhusu imani yenu katika Bwana Isa na upendo wenu
kwa watakatifu wote, 16 sijaacha kumshukuru Mungu
kwa ajili yenu, nikiwakumbuka katika maombi yangu.
17 Nazidi kumwomba Mungu wa Bwana wetu Isa
Al-Masihi, Baba wa utukufu, awajalieni ninyi roho
ya hekima na ya ufunuo, ili mpate kumjua zaidi. 18
Ninaomba pia kwamba macho ya mioyo yenu yatiwe
nuru ili mpate kujua tumaini mliloitiwa, utajiri wa urithi
wa utukufu wake kwa watakatifu 19 na uweza wake
mkuu usiolinganishwa kwa ajili yetu sisi tuaminio.
Uweza huo unaofanya kazi ndani yetu, ni sawa na
ile nguvu kuu mno 20 aliyoitumia katika Al-Masihi
alipomfufua kutoka kwa wafu, na kumketisha mkono
wake wa kuume katika ulimwengu wa roho, 21 juu
sana kuliko falme zote na mamlaka, enzi na milki, na
juu ya kila jina litajwalo, si katika ulimwengu huu tu,
bali katika ule ujao pia. **(aiōn g165)** 22 Naye Mungu
ameweka vitu vyote viwe chini ya miguu yake, na
amemfanya yeye awe kichwa cha vitu vyote kwa ajili
ya jumuiya ya waumini, 23 ambayo ni mwili wake,
ukamilifu wake yeye aliye yote katika yote.

2 Ninyi mlikuwa wafu katika makosa na dhambi zenu,
2 ambazo mlizitenda mlipofuata njia za ulimwengu
huu na za yule mtawala wa ufalme wa anga, yule
roho atendaye kazi sasa ndani ya wale wasiotii. **(aiōn
g165)** 3 Sisi sote pia tuliishi katikati yao hapo zamani,
tukitimiza tamaa za asili yetu ya dhambi na kufuata
tamaa zake na mawazo yake. Nasi kwa asili tulistahili
ghadhabu, kama watu wengine wote. 4 Lakini Mungu
kwa upendo wake mwingi kwetu sisi, ambaye ni
mwingi wa rehema, 5 hata tulipokuwa wafu kwa ajili
ya makosa yetu, alitufanya tuwe hai pamoja na Al-
Masihi Isa, yaani mmeokolewa kwa neema. 6 Mungu
alitufufua pamoja na Al-Masihi na kutuketisha pamoja
naye katika ulimwengu wa roho katika Al-Masihi Isa,
7 ili katika ulimwengu ujao apate kuonesha wingi wa
neema yake isiyolinganishwa, iliyodhihirishwa kwetu
kwa wema wake ndani ya Al-Masihi Isa. **(aiōn g165)** 8
Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kupitia kwa
imani, nayo haikutokana na ninyi wenyewe. Hii ni
zawadi kutoka kwa Mungu, 9 si kwa matendo, ili mtu
yeyote asije akajisifu. 10 Kwa maana sisi ni kazi ya
mikono ya Mungu, tulioumbwa katika Al-Masihi Isa,
ili tupate kutenda matendo mema, ambayo Mungu
alitangulia kuyaandaa tupate kuishi katika hayo.
11 Kwa hiyo kumbukeni kwamba hapo awali ninyi
ambao ni watu wa Mataifa kwa kuzaliwa na kuitwa
“wasiotahiriwa” na wale wanaojiita “waliotahiriwa”
(yaani tohara ifanyikayo katika mwili kwa mikono
ya wanadamu), 12 kumbukeni kwamba wakati ule
mlikuwa mbali na Al-Masihi, mkiwa mmetengwa
kutoka jumuiya ya Israeli, na mkiwa wageni katika yale
maagano ya ahadi, nanyi hamkuwa na tumaini wala
Mungu duniani. 13 Lakini sasa katika Al-Masihi Isa,
ninyi ambao hapo kwanza mlikuwa mbali na Mungu,
sasa mmeletwa karibu kupitia kwa damu ya Al-Masihi.

14 Kwa maana yeye mwenyewe ndiye amani yetu,
aliyetufanya sisi tuliokuwa vikundi viwili tuwe kikundi
kimoja kwa kuvunja kizuizi na kubomoa ule ukuta wa
uadui uliokuwa kati yetu, 15 kwa kuibatilisha ile sheria
pamoja na amri zake na maagizo yake alipoutoa
mwili wake, ili apate kufanya ndani yake mtu mmoja
mpya badala ya hao wawili, hivyo akifanya amani,
16 naye katika mwili huu mmoja awapatanishe wote
wawili na Mungu kupitia msalaba, ili kwa huo msalaba
akaangamiza uadui wao. 17 Alikuja na kuhubiri
amani kwenu ninyi mliokuwa mbali, na pia akahubiri
amani kwao waliokuwa karibu. 18 Kwa maana kupitia
kwake sisi sote tunaweza kumkaribia Baba katika
Roho mmoja. 19 Hivyo basi, ninyi sasa si wageni
tena na wapitaji, bali mmekuwa wenyeji pamoja na
watakatifu na pia jamaa wa nyumbani mwake Mungu.
20 Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii,
naye Al-Masihi Isa ndiye jiwe kuu la pembeni. 21
Ndani yake jengo lote limeshikamanishwa pamoja na
kuinuliwa ili kuwa Hekalu takatifu katika Mwenyezi
Mungu. 22 Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja
ili mpate kuwa makao ambayo Mungu anaishi ndani
yake kupitia kwa Roho wake Mtakatifu.

3 Kwa sababu hii, mimi Paulo, ni mfungwa wa Al-
Masihi Isa kwa ajili yenu ninyi watu wa Mataifa. 2
Kwa hakika mmekwisha kusikia kuhusu ile huduma
ya neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu, 3
yaani ile siri iliodhihirishwa kwangu kupitia ufunuo,
kama nilivyotangulia kuandika kwa kifupi. 4 Kwa
kusoma haya, basi mtaweza kuelewa ufahamu wangu
katika siri ya Al-Masihi. 5 Siri hii haikudhihirishwa
kwa wanadamu katika vizazi vingine kama vile sasa
ilivyodhihirishwa na Roho wa Mungu kwa mitume na
manabii watakatifu wa Mungu. 6 Siri hii ni kwamba,
kupitia kwa Injili, watu wa Mataifa ni warithi pamoja
na Israeli, viungo vya mwili mmoja na washiriki
pamoja wa ahadi katika Al-Masihi Isa. 7 Nimekuwa
mtumishi wa Injili hii kwa kipawa cha neema ya
Mungu niliyopewa kwa nguvu yake itendayo kazi.
8 Ingawa mimi ni mdogo kuliko aliye mdogo kabisa
miongoni mwa watakatifu wote, nilipewa neema hii: ili
niwahubirie watu wa Mataifa kuhusu utajiri usiopimika
ulio ndani ya Al-Masihi, 9 na kuweka wazi kwa
kila mtu siri hii iliyokuwa imefichwa tangu zamani
katika Mungu, aliyeumba vitu vyote. **(aiōn g165)** 10
Ili sasa kupitia kwa jumuiya ya waumini, hekima
ya Mungu iliyo ya namna nyingi ipate kujulikana
kwa watawala na wenye mamlaka katika ulimwengu
wa roho, 11 sawasawa na kusudi lake la milele
alilolitimiza katika Al-Masihi Isa Bwana wetu. **(aiōn
g165)** 12 Ndani yake na kupitia kwa imani katika yeye
twaweza kumkaribia Mungu kwa uhuru na kwa ujasiri.
13 Kwa hiyo, nawaomba msikate tamaa kwa sababu
ya mateso yangu kwa ajili yenu, hayo ni utukufu
wenu. 14 Kwa sababu hii nampigia Baba magoti, 15
ambaye ubaba wote wa kila jamaa za mbinguni na
za duniani unatokana naye. 16 Namwomba Mungu
awaimarishe kwa kuwatia nguvu mioyo yenu kupitia
kwa Roho wake Mtakatifu kwa kadiri ya utajiri wa
utukufu wake, 17 ili Al-Masihi apate kukaa mioyoni
mwenu kupitia kwa imani. Nami ninaomba kwamba
mkiwa wenye mizizi tena imara katika msingi wa
upendo, 18 mwe na uwezo wa kufahamu pamoja
na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, urefu, kimo
na kina upendo wa Al-Masihi, 19 na kujua upendo
huu unaopita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia
kipimo cha ukamilifu wote wa Mungu. 20 Basi kwa
yeye awezaye kutenda mambo ya ajabu yasiyopimika
kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya
uweza wake ule utendao kazi ndani yetu, 21 yeye
atukuzwe katika jumuiya ya waumini, na katika Al-
Masihi Isa kwa vizazi vyote, milele na milele. Amen.
**(aiōn g165)**

4 Basi, mimi niliye mfungwa wa Bwana Isa, nawasihi
mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitiwa.
2 Kwa unyenyekevu wote na upole, mkiwa wavumilivu,
mkichukuliana kwa upendo. 3 Jitahidini kudumisha
umoja wa Roho wa Mungu katika kifungo cha
amani. 4 Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama
vile mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.
5 Tena kuna Bwana mmoja, imani moja, ubatizo
mmoja, 6 Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote,
aliye juu ya yote, katika yote na ndani ya yote.
7 Lakini kila mmoja wetu amepewa neema kwa
kadiri ya kipimo cha kipawa cha Al-Masihi. 8 Kwa
hiyo husema: “Alipopaa juu zaidi, aliteka mateka,
akawapa wanadamu vipawa.” 9 (Asemapo “alipaa
juu,” maana yake nini isipokuwa ni kusema kwamba
Al-Masihi pia alishuka pande za chini sana za dunia?
10 Yeye aliyeshuka ndiye aliyepaa juu zaidi kupita
mbingu zote, ili apate kuujaza ulimwengu wote.)
11 Ndiye aliweka wengine kuwa mitume, wengine

kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine
kuwa wachungaji na walimu, 12 kwa kusudi la
kuwakamilisha watakatifu kwa ajili ya kazi za huduma,
ili mwili wa Al-Masihi upate kujengwa 13 hadi sote
tutakapoufikia umoja katika imani na katika kumjua
Mwana wa Mungu na kuwa watu wazima, kwa kufikia
kimo cha ukamilifu wa Al-Masihi. 14 Basi hatutakuwa
tena watoto wachanga, tukiyumbishwa na mawimbi,
na tukipeperushwa hapa na pale na kila upepo wa
mafundisho, na kwa ujanja na hila za watu katika
njama zao. 15 Badala yake, tukiambiana kweli kwa
upendo, katika mambo yote tukue, hata tumfikie yeye
aliye kichwa, yaani Al-Masihi. 16 Kutoka kwake, mwili
wote ukiwa umeungamanishwa na kushikanishwa
pamoja kwa msaada wa kila kiungo, hukua na
kujijenga wenyewe katika upendo, huku kila kiungo
kikifanya kazi yake. 17 Hivyo nawaambia hivi, nami
nasisitiza katika Bwana Isa kwamba, msiishi tena
kama watu wa Mataifa wanavyoishi, katika ubatili
wa mawazo yao. 18 Watu hao akili zao zimetiwa
giza na wametengwa mbali na uzima wa Mungu
kwa sababu ya ujinga wao kutokana na ugumu wa
mioyo yao. 19 Wakiisha kufa ganzi, wamejitia katika
mambo ya ufisadi na kujiingiza katika kila aina ya
uchafu, wakiendelea kutamani zaidi. 20 Lakini ninyi,
hivyo sivyo mlivyojifunza Al-Masihi. 21 Kama hivyo
ndivyo ilivyo, ninyi mmemsikia, tena mmefundishwa
naye, vile kweli ilivyo katika Isa. 22 Mlifundishwa
kuuvua mwenendo wenu wa zamani, utu wenu wa
kale, ulioharibiwa na tamaa zake za udanganyifu,
23 ili mfanywe upya katika roho ya nia zenu, 24 na
mkajivike utu mpya, ulioumbwa sawasawa na mfano
wa Mungu katika haki ya kweli na utakatifu. 25 Kwa
hiyo kila mmoja wenu avue uongo na kuambiana kweli
mtu na jirani yake, kwa maana sisi sote tu viungo
vya mwili mmoja. 26 Mkikasirika, msitende dhambi,
wala jua lisichwe mkiwa bado mmekasirika, 27 wala
msimpe ibilisi nafasi. 28 Yeye ambaye amekuwa
akiiba, asiibe tena, lakini lazima ajishughulishe, afanye
kitu kinachofaa kwa mikono yake mwenyewe, ili awe
na kitu cha kuwagawia wahitaji. 29 Maneno mabaya
yasitoke vinywani mwenu, bali yale yanayofaa kwa
ajili ya kuwajenga wengine kulingana na mahitaji yao,
ili yawafae wale wasikiao. 30 Wala msimhuzunishe
Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwake mlitiwa
muhuri kwa ajili ya siku ya ukombozi. 31 Ondoeni
kabisa uchungu, ghadhabu na hasira, makelele na
masingizio, pamoja na kila aina ya uovu. 32 Kuweni
wafadhili na wenye kuhurumiana ninyi kwa ninyi,
mkisameheana, kama vile naye Mungu katika Al-
Masihi alivyowasamehe ninyi.

**5** Kwa hiyo, mfuateni Mungu kama watoto
wanaopendwa, 2 mkiishi maisha ya upendo, kama
vile Al-Masihi alivyotupenda sisi akajitoa kwa ajili yetu
kuwa sadaka yenye harufu nzuri na dhabihu kwa
Mungu. 3 Lakini uasherati usitajwe miongoni mwenu
kamwe, wala uchafu wa aina yoyote, wala tamaa,
kwa sababu mambo haya hayastahili miongoni mwa
watakatifu wa Mungu. 4 Wala pasiwepo mazungumzo
machafu ya aibu, au maneno ya upuzi au mzaha,
ambayo hayafai, badala yake mshukuruni Mungu. 5
Kwa habari ya mambo haya mjue hakika kwamba:
Mwasherati, wala mtu mwovu, wala mwenye tamaa
mbaya (mtu kama huyo ni mwabudu sanamu) kamwe
hataurithi ufalme wa Al-Masihi na wa Mungu. 6 Mtu
yeyote na asiwadanganye kwa maneno matupu,
kwa kuwa hasira ya Mungu huwaka kwa sababu ya
mambo kama hayo juu ya wale wasiomtii. 7 Kwa
hiyo, msishirikiane nao. 8 Kwa maana zamani ninyi
mlikuwa giza, lakini sasa ninyi ni nuru katika Bwana
Isa. Nendeni kama watoto wa nuru 9 (kwa kuwa
tunda la nuru hupatikana katika wema wote, haki na
kweli), 10 nanyi tafuteni yale yanayompendeza Bwana
Isa. 11 Msishiriki matendo ya giza yasiyofaa, bali
yafichueni. 12 Kwa maana ni aibu hata kutaja mambo
yale ambayo wasiotii wanayafanya sirini. 13 Lakini
kila kitu kilichowekwa nuruni, huonekana, 14 kwa
kuwa nuru ndiyo hufanya kila kitu kionekane. Hii ndiyo
sababu imesemekana: "Amka, wewe uliyelala, ufufuke
kutoka kwa wafu, naye Al-Masihi atakuangazia." 15
Kwa hiyo angalieni sana jinsi mnavyoenenda, si kama
watu wasio na hekima, bali kama wenye hekima,
16 mkiukomboa wakati, kwa sababu nyakati hizi ni
za uovu. 17 Kwa hiyo msiwe wajinga, bali mpate
kujua nini mapenzi ya Bwana Isa. 18 Pia msilewe kwa
mvinyo, ambamo mna upotovu, bali mjazwe Roho wa
Mungu. 19 Msemezane ninyi kwa ninyi kwa zaburi,
nyimbo na tenzi za rohoni, mkimwimbia na kumsifu
Bwana Isa mioyoni mwenu, 20 siku zote mkimshukuru
Mungu Baba Mwenyezi kwa kila jambo katika Jina la
Bwana wetu Isa Al-Masihi. 21 Nyenyekeaneni ninyi
kwa ninyi kutokana na kumcha Al-Masihi. 22 Ninyi

wake, watiini waume zenu kama vile mnavyomtii
Bwana Isa. 23 Kwa maana mume ni kichwa cha
mkewe kama vile Al-Masihi alivyo kichwa cha jumuiya
ya waumini, ambayo ni mwili wake, naye Al-Masihi
ni Mwokozi wake. 24 Basi, kama vile jumuiya ya
waumini wanavyomtii Al-Masihi, vivyo hivyo na wake
nao imewapasa kuwatii waume zao kwa kila jambo.
25 Ninyi waume, wapendeni wake zenu, kama vile Al-
Masihi alivyoipenda jumuiya ya waumini na akajitoa
kwa ajili yake, 26 kusudi aifanye takatifu, akiitakasa
kwa kuiosha kwa maji katika neno lake, 27 apate
kujiletea jumuiya tukufu isiyo na doa wala kunyanzi
au waa lolote, bali takatifu na isiyo na hatia. 28 Vivyo
hivyo imewapasa waume kuwapenda wake zao kama
miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda
mwenyewe. 29 Hakuna mtu anayeuchukia mwili wake
mwenyewe, bali huulisha na kuutunza vizuri, kama
Al-Masihi anavyoitunza jumuiya yake ya waumini.
30 Sisi tu viungo vya mwili wake. 31 “Kwa sababu
hii, mwanaume atamwacha baba yake na mama
yake, naye ataambatana na mkewe, na hao wawili
watakuwa mwili mmoja.” 32 Siri hii ni kubwa, bali mimi
nanena kuhusu Al-Masihi na jumuiya ya waumini
wake. 33 Hata hivyo, kila mmoja wenu ampende
mkewe kama anavyoipenda nafsi yake mwenyewe,
naye mke lazima amheshimu mumewe.

6 Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana Isa,
kwa kuwa hili ni jema. 2 “Waheshimu baba yako
na mama yako,” hii ndio amri ya kwanza yenye ahadi,
3 “upate baraka na uishi siku nyingi duniani.” 4 Ninyi
akina baba, msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni
kwa nidhamu na mafundisho ya Bwana Isa. 5 Ninyi
watumwa, watiini hao walio mabwana zenu hapa
duniani kwa heshima na kwa kutetemeka na kwa
unyofu wa moyo, kama vile mnavyomtii Al-Masihi. 6
Watiini, si tu wakati wakiwaona ili mpate upendeleo
wao, bali mtumike kama watumwa wa Al-Masihi,
mkifanya mapenzi ya Mungu kwa moyo. 7 Tumikeni
kwa moyo wote, kama vile mngemtumikia, wala si
wanadamu, 8 mkijua kwamba Bwana Isa atampa
kila mtu thawabu kwa lolote jema alilotenda, awe
mtumwa au mtu huru. 9 Nanyi mabwana, watendeeni
watumwa wenu kwa jinsi hiyo hiyo. Msiwatishe, kwa
kuwa mnajua kwamba yeye aliye Bwana wenu na
Bwana wao yuko mbinguni, naye hana upendeleo.
10 Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana Isa
na katika uweza wa nguvu zake. 11 Vaeni silaha
zote za Mungu ili mweze kuzipinga hila za ibilisi.
12 Kwa maana kushindana kwetu si dhidi ya mwili
na damu, bali dhidi ya falme na mamlaka, dhidi ya
wakuu wa ulimwengu huu wa giza na majeshi ya
pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. **(aiōn g165)**
13 Kwa hiyo vaeni silaha zote za Mungu ili mweze
kushindana siku ya uovu itakapokuja, nanyi mkiisha
kufanya yote, simameni imara. 14 Kwa hiyo simameni
imara mkiwa mmejifunga kweli kiunoni na kuvaa
dirii ya haki kifuani, 15 nayo miguu yenu ivalishwe
viatu vya utayari tunaopata katika Injili ya amani. 16
Zaidi ya haya yote, twaeni ngao ya imani, ambayo
kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto
ya yule mwovu. 17 Vaeni chapeo ya wokovu na
mchukue upanga wa Roho wa Mungu, ambao ni
neno la Mungu, 18 mkiomba kwa Roho siku zote
katika sala zote na maombi, mkikesha kila wakati
mkiwaombea watakatifu wote. 19 Niombeeni na mimi
pia, ili kila nifunguapo kinywa changu, nipewe maneno
ya kusema, niweze kutangaza siri ya Injili kwa ujasiri,
20 ambayo mimi ni balozi wake katika vifungo. Ombeni
ili nipate kuhubiri kwa ujasiri kama inipasavyo. 21
Tikiko, aliye ndugu mpendwa na mtumishi mwaminifu
katika Bwana Isa, atawaambia kila kitu, ili pia mpate
kujua hali yangu na kile ninachofanya. 22 Ninamtuma
kwenu kwa ajili ya kusudi hili hasa, ili mpate kujua
hali yetu, na awatie moyo. 23 Amani iwe kwa ndugu,
na pendo pamoja na imani kutoka kwa Mungu Baba
Mwenyezi na kwa Bwana Isa Al-Masihi. 24 Neema
iwe na wote wanaompenda Bwana wetu Isa Al-Masihi
kwa upendo wa dhati. Amen.

# Wafilipi

**1** Paulo na Timotheo, watumishi wa Al-Masihi Isa.
2 Neema na amani zinazotoka kwa Mungu, Baba
yetu, na kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi ziwe nanyi. 3
Ninamshukuru Mungu wangu kila niwakumbukapo
ninyi. 4 Katika maombi yangu yote daima nimekuwa
nikiwaombea ninyi nyote kwa furaha, 5 kwa sababu
ya kushiriki kwenu katika kueneza Injili, tangu siku
ya kwanza hadi leo. 6 Nina hakika kwamba yeye
aliyeianza kazi njema mioyoni mwenu, ataiendeleza
na kuikamilisha hata siku ya Al-Masihi Isa. 7 Ni haki
na ni wajibu wangu kufikiri hivi juu yenu nyote, kwa
sababu ninyi mko moyoni mwangu. Ikiwa nimefungwa
au nikiwa ninaitetea na kuithibitisha Injili, ninyi nyote
mnashiriki neema ya Mungu pamoja nami. 8 Mungu
ni shahidi wangu jinsi ninavyowaonea shauku ninyi
nyote kwa huruma ya Al-Masihi Isa. 9 Haya ndio
maombi yangu: kwamba upendo wenu uongezeke
zaidi na zaidi katika maarifa na ufahamu wote, 10
ili mpate kutambua yale yaliyo mema, mkawe safi,
wasio na hatia hadi siku ya Al-Masihi, 11 mkiwa
mmejawa na matunda ya haki yapatikanayo kupitia
kwa Isa Al-Masihi, kwa utukufu na sifa za Mungu. 12
Basi, ndugu zangu, nataka mjue kwamba mambo
yale yaliyonipata kwa kweli yamesaidia sana kueneza
Injili. 13 Matokeo yake ni kwamba imejulikana wazi
kwa walinzi wote wa jumba la kifalme na kwa
wengine wote kuwa nimefungwa kwa ajili ya Al-Masihi.
14 Kwa sababu ya vifungo vyangu, ndugu wengi
katika Bwana Isa wametiwa moyo kuhubiri neno la
Mungu kwa ujasiri zaidi na bila woga. 15 Ni kweli
kwamba wengine wanamhubiri Al-Masihi kutokana
na wivu na kwa kutaka kushindana, lakini wengine
wanamhubiri Al-Masihi kwa nia njema. 16 Hawa wa
mwisho wanamhubiri Al-Masihi kwa moyo wa upendo,
wakifahamu kwamba nimo humu gerezani kwa ajili
ya kuitetea Injili. 17 Hao wa kwanza wanamtangaza
Al-Masihi kutokana na tamaa zao wenyewe wala
si kwa moyo mweupe, bali wanakusudia kuongeza
mateso yangu katika huku kufungwa kwangu. 18
Lakini inadhuru nini? Jambo la muhimu ni kwamba
kwa kila njia, ikiwa ni kwa nia mbaya au njema, Al-
Masihi anahubiriwa. Nami kwa ajili ya jambo hilo
ninafurahi. Naam, nami nitaendelea kufurahi, 19 kwa
maana ninajua kwamba kwa maombi yenu na kwa
msaada unaotolewa na Roho wa Isa Al-Masihi, yale
yaliyonipata mimi yatageuka kuwa wokovu wangu. 20
Ninatarajia kwa shauku kubwa na kutumaini kwamba
sitaaibika kwa njia yoyote, bali nitakuwa na ujasiri
wa kutosha ili sasa kama wakati mwingine wowote,
Al-Masihi atukuzwe katika mwili wangu, ikiwa ni
kwa kuishi au kwa kufa. 21 Kwa maana kwangu
mimi, kuishi ni Al-Masihi, na kufa ni faida. 22 Kama
nitaendelea kuishi katika mwili, kwangu hili ni kwa
ajili ya matunda ya kazi. Lakini nichague lipi? Mimi
sijui! 23 Ninavutwa kati ya mambo mawili: Ninatamani
kuondoka nikakae pamoja na Al-Masihi, jambo hilo ni
bora zaidi. 24 Lakini kwa sababu yenu ni muhimu
zaidi mimi nikiendelea kuishi katika mwili. 25 Nikiwa
na hakika ya jambo hili, ninajua kwamba nitaendelea
kuwepo pamoja nanyi nyote, ili mpate kukua na
kuwa na furaha katika imani, 26 ili kwa kuja kwangu
kwenu tena, furaha yenu iwe nyingi katika Al-Masihi
Isa kwa ajili yangu. 27 Lakini lolote litakalotukia,
mwenende kama ipasavyo Injili ya Al-Masihi, ili nikija
na kuwaona au ikiwa sipo, nipate kusikia haya juu
yenu: Kuwa mnasimama imara katika roho moja,
mkiishindania imani ya Injili kwa umoja, 28 wala
msitishwe na wale wanaowapinga. Hii ni ishara kwao
kuwa wataangamia, lakini ninyi mtaokolewa, na hii ni
kazi ya Mungu. 29 Kwa maana mmepewa kwa ajili
ya Al-Masihi, si kumwamini tu, bali pia kuteswa kwa
ajili yake, 30 kwa kuwa mnashiriki mashindano yale
yale mliyoyaona nikiwa nayo na ambayo hata sasa
mnasikia kuwa bado ninayo.

**2** Kama kukiwa na jambo lolote la kutia moyo katika
kuunganishwa na Al-Masihi, kukiwa faraja yoyote
katika upendo wake, kukiwa na ushirika wowote
na Roho wa Mungu, kukiwa na wema wowote na
huruma, 2 basi ikamilisheni furaha yangu kwa kuwa
na nia moja, mkiwa na upendo huo moja, mkiwa wa
roho na kusudi moja. 3 Msitende jambo lolote kwa nia
ya kujitukuza wala kujivuna, bali kwa unyenyekevu
kila mtu amhesabu mwingine bora kuliko nafsi yake.
4 Kila mmoja wenu asiangalie faida yake mwenyewe
tu, bali pia ajishughulishe kwa faida ya wengine. 5
Kuweni na nia ile ile aliyokuwa nayo Al-Masihi Isa:
6 Yeye, ingawa alikuwa na asili ya Mungu hasa,
hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa kitu cha
kushikilia, 7 bali alijifanya si kitu, akachukua hali
hasa ya mtumwa, naye akazaliwa katika umbo la

mwanadamu. 8 Naye akiwa na umbo la mwanadamu,
alijinyenyekeza, akatii hata mauti: naam, mauti ya
msalaba! 9 Kwa hiyo, Mungu alimtukuza juu sana,
na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina, 10 ili kwa
Jina la Isa, kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni,
na vya duniani, na vya chini ya nchi, 11 na kila
ulimi ukiri kwamba Isa Al-Masihi ni Bwana, kwa
utukufu wa Mungu Baba Mwenyezi. 12 Kwa hiyo,
wapendwa wangu, kama vile mmekuwa mkitii siku
zote, si tu wakati nikiwa pamoja nanyi, bali sasa
zaidi sana nisipokuwepo, utimizeni wokovu wenu kwa
kuogopa na kutetemeka, 13 kwa maana Mungu ndiye
atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda
kwenu kwa kulitimiza kusudi lake jema. 14 Fanyeni
mambo yote bila kunung'unika wala kushindana,
15 ili msiwe na lawama wala hatia, bali mwe wana
wa Mungu wasio na kasoro katika kizazi chenye
ukaidi na kilichopotoka, ambacho ndani yake ninyi
mnang'aa kama mianga ulimwenguni. 16 Mkilishika
neno la uzima, ili nipate kuona fahari siku ya Al-
Masihi kwamba sikupiga mbio wala kujitaabisha
bure. 17 Lakini hata nikimiminwa kama sadaka ya
kinywaji kwenye dhabihu na huduma inayotoka katika
imani yenu, mimi ninafurahi na kushangilia pamoja
nanyi nyote. 18 Vivyo hivyo, ninyi nanyi imewapasa
kufurahi na kushangilia pamoja nami. 19 Natumaini
katika Bwana Isa kumtuma Timotheo hivi karibuni aje
kwenu, ili nipate kufarijika moyo nitakapopata habari
zenu. 20 Sina mtu mwingine kama yeye, ambaye
ataangalia hali yenu kwa halisi. 21 Kwa maana
kila mmoja anajishughulisha zaidi na mambo yake
mwenyewe wala si yale ya Isa Al-Masihi. 22 Lakini
ninyi wenyewe mnajua jinsi Timotheo alivyojithibitisha
mwenyewe, kwa maana ametumika pamoja nami
kwa kazi ya Injili, kama vile mwana kwa baba yake.
23 Kwa hiyo, ninatumaini kumtuma kwenu upesi
mara nitakapojua mambo yangu yatakavyokuwa.
24 Nami mwenyewe ninatumaini katika Bwana Isa
kwamba nitakuja kwenu hivi karibuni. 25 Lakini
nadhani ni muhimu kumtuma tena kwenu Epafrodito,
ndugu yangu na mtendakazi pamoja nami, aliye
askari mwenzangu, ambaye pia ni mjumbe wenu
mliyemtuma ili ashughulike na mahitaji yangu. 26 Kwa
maana amekuwa akiwaonea sana shauku ninyi nyote,
akiwa na wasiwasi kwa kuwa mlisikia kwamba alikuwa
mgonjwa. 27 Kweli alikuwa mgonjwa, tena karibu ya
kufa. Lakini Mungu alimhurumia, wala si yeye tu, bali
hata na mimi alinihurumia, nisipatwe na huzuni juu ya
huzuni. 28 Kwa hiyo mimi ninafanya bidii kumtuma
kwenu ili mtakapomwona kwa mara nyingine, mpate
kufurahi, nami wasiwasi wangu upungue. 29 Kwa
hiyo mpokeeni katika Bwana Isa kwa furaha kubwa,
nanyi wapeni heshima watu kama hawa, 30 kwa
sababu alikaribia kufa kwa ajili ya kazi ya Al-Masihi,
akihatarisha maisha yake ili aweze kunihudumia vile
ninyi hamkuweza.

**3** Hatimaye, ndugu zangu, furahini katika Bwana Isa!
Mimi kuwaandikia mambo yale yale hakuniudhi,
kwa maana ni kinga kwa ajili yenu. 2 Jihadharini
na mbwa, wale watenda maovu, jihadharini na wale
wajikatao miili yao. 3 Kwa maana sisi ndio tulio tohara,
sisi tumwabuduo Mungu katika Roho wake Mtakatifu,
tunaona fahari katika Al-Masihi Isa, ambao hatuweki
tumaini letu katika mwili, 4 ingawa mimi mwenyewe
ninazo sababu za kuutumainia mwili. Kama mtu
yeyote akidhani anazo sababu za kuutumainia mwili,
mimi zaidi. 5 Nilitahiriwa siku ya nane, mimi ni
Mwisraeli wa kabila la Benyamini, Mwebrania wa
Waebrania. Kwa habari ya Torati, ni Farisayo, 6
kwa habari ya juhudi, nilikuwa nikitesa jumuiya ya
waumini, kuhusu haki inayopatikana kwa Torati,
sikuwa na hatia. 7 Lakini mambo yale yaliyokuwa faida
kwangu, sasa nayahesabu kuwa hasara kwa ajili ya
Al-Masihi. 8 Zaidi ya hayo, nayahesabu mambo yote
kuwa hasara tupu nikiyalinganisha na faida kubwa
ipitayo kiasi cha kumjua Al-Masihi Isa Bwana wangu,
ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo
yote, nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nimpate Al-
Masihi. 9 Nami nionekane mbele zake bila kuwa na
haki yangu mwenyewe inayopatikana kwa sheria,
bali ile inayopatikana kwa imani katika Al-Masihi,
haki ile inayotoka kwa Mungu kupitia kwa imani.
10 Nataka nimjue Al-Masihi na uweza wa kufufuka
kwake na ushirika wa mateso yake, ili nifanane naye
katika mauti yake, 11 ili kwa njia yoyote niweze
kufikia ufufuo wa wafu. 12 Si kwamba nimekwisha
kufikia, au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu, la
hasha! Bali nakaza mwendo ili nipate kile ambacho
kwa ajili yake, nimeshikwa na Al-Masihi Isa. 13
Ndugu zangu, sijihesabu kuwa nimekwisha kushika.
Lakini ninafanya jambo moja: Ninasahau mambo
yale yaliyopita, nakaza mwendo kufikia yale yaliyo

mbele. 14 Nakaza mwendo nifikie ile alama ya ushindi
iliyowekwa ili nipate tuzo ya mwito mkuu wa Mungu
ambao nimeitiwa huko juu mbinguni katika Al-Masihi
Isa. 15 Hivyo sisi sote tuliokuwa kiroho tuwaze jambo
hili, hata mkiwaza mengine katika jambo lolote, Mungu
ataliweka wazi hilo nalo. 16 Lakini na tushike sana
lile ambalo tumekwisha kulifikia. 17 Ndugu zangu,
kwa pamoja fuateni mfano wangu na kuwatazama
wale wanaofuata kielelezo tulichowawekea. 18 Kwa
maana, kama nilivyokwisha kuwaambia mara nyingi
kabla, nami sasa nasema tena hata kwa machozi,
watu wengi wanaishi kama adui wa msalaba wa
Al-Masihi. 19 Mwisho wa watu hao ni maangamizi,
mungu wao ni tumbo, na utukufu wao ni aibu, na
mawazo yao yamo katika mambo ya dunia. 20 Lakini
uenyeji wetu uko mbinguni. Nasi tunamngoja kwa
shauku Mwokozi kutoka huko, yaani Bwana Isa Al-
Masihi, 21 atakayeubadili mwili wetu wa unyonge,
ili upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa
uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu
vyote chini yake.

4 Kwa hiyo, ndugu zangu, ninaowapenda na ambao
ninawaonea shauku, ninyi mlio furaha yangu
na taji langu, hivi ndivyo iwapasavyo kusimama
imara katika Bwana Isa, ninyi wapendwa wangu. 2
Nawasihi Euodia na Sintike wawe na nia moja katika
Bwana Isa. 3 Naam, nakusihi wewe pia, mwenzangu
mwaminifu, uwasaidie hawa wanawake, kwa sababu
walijitaabisha katika kazi ya Injili pamoja nami bega
kwa bega, wakiwa pamoja na Klementi na watendakazi
wenzangu ambao majina yao yameandikwa katika
kitabu cha uzima. 4 Furahini katika Bwana Isa
siku zote, tena nasema furahini! 5 Upole wenu
na ujulikane na watu wote. Bwana Isa yu karibu.
6 Msijisumbue kwa jambo lolote, bali katika kila
jambo kwa kuomba na kusihi pamoja na kushukuru,
haja zenu na zijulikane na Mungu. 7 Nayo amani
ya Mungu, inayopita fahamu zote, itailinda mioyo
yenu na nia zenu katika Al-Masihi Isa. 8 Hatimaye,
ndugu zangu, mambo yote yaliyo ya kweli, yoyote
yaliyo na sifa njema, yoyote yaliyo ya haki, yoyote
yaliyo safi, yoyote ya kupendeza, yoyote yenye
staha, ukiwepo uzuri wowote, pakiwepo chochote
kinachostahili kusifiwa, tafakarini mambo hayo. 9
Mambo yote mliyojifunza au kuyapokea au kuyasikia
kutoka kwangu, au kuyaona kwangu, yatendeni hayo.
Naye Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi. 10 Nina
furaha kubwa katika Bwana Isa kwamba hatimaye
mmeanza upya kushughulika tena na maisha yangu.
Kweli mmekuwa mkinifikiria lakini mlikuwa hamjapata
nafasi ya kufanya hivyo. 11 Sisemi hivyo kwa vile
nina mahitaji, la! Kwa maana nimejifunza kuridhika
katika hali yoyote. 12 Ninajua kupungukiwa, pia
ninajua kuwa na vingi. Nimejifunza siri ya kuridhika
katika kila hali, wakati wa kushiba na wakati wa
kuona njaa, wakati wa kuwa na vingi na wakati
wa kupungukiwa. 13 Naweza kuyafanya mambo
yote katika yeye anitiaye nguvu. 14 Lakini, mlifanya
vyema kushiriki nami katika taabu zangu. 15 Zaidi ya
hayo, ninyi Wafilipi mnajua kwamba siku za kwanza
nilipoanza kuhubiri Injili, nilipoondoka Makedonia,
hakuna kundi lingine la waumini lililoshiriki nami
katika masuala ya kutoa na kupokea isipokuwa ninyi.
16 Kwa maana hata nilipokuwa huko Thesalonike,
mliniletea msaada kwa ajili ya mahitaji yangu zaidi
ya mara moja. 17 Si kwamba natafuta sana yale
matoleo, bali natafuta sana ile faida itakayozidi
sana kwa upande wenu. 18 Nimelipwa kikamilifu
hata na zaidi; nimetoshelezwa kabisa sasa, kwa
kuwa nimepokea kutoka kwa Epafrodito vile vitu
mlivyonitumia, sadaka yenye harufu nzuri, dhabihu
inayokubalika na ya kumpendeza Mungu. 19 Naye
Mungu wangu atawajaza ninyi na kila mnachohitaji
kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani ya
Al-Masihi Isa. 20 Mungu wetu aliye Baba yetu
apewe utukufu milele na milele. Amen. **(aiōn g165)** 21
Msalimuni kila mtakatifu katika Al-Masihi Isa. Ndugu
walio pamoja nami wanawasalimu. 22 Watakatifu
wote wanawasalimu, hasa wale watu wa nyumbani
mwa Kaisari. 23 Neema ya Bwana wetu Isa Al-Masihi
iwe pamoja na roho zenu. Amen.

# Wakolosai

**1** Paulo, mtume wa Al-Masihi Isa, kwa mapenzi ya
Mungu, na Timotheo ndugu yetu. **2** Kwa ndugu
watakatifu na waaminifu katika Al-Masihi wanaoishi
Kolosai. **3** Siku zote tunamshukuru Mungu, Baba wa
Bwana wetu Isa Al-Masihi, tunapowaombea ninyi, **4**
kwa sababu tumesikia kuhusu imani yenu katika Al-
Masihi Isa, na upendo wenu mlio nao kwa watakatifu
wote: **5** imani na upendo ule unaotoka katika tumaini
mlilowekewa akiba mbinguni, na ambalo mmesikia
habari zake katika neno la kweli, yaani ile Injili
**6** iliyowafikia ninyi. Duniani kote Injili hii inazaa
matunda na kuenea kama ilivyokuwa kwenu tangu
siku ile mlipoisikia na kuielewa neema ya Mungu
katika kweli yote. **7** Mlijifunza habari zake kutoka
kwa Epafra, mtumishi mwenzetu mpendwa, aliye
mhudumu mwaminifu wa Al-Masihi kwa ajili yenu, **8**
ambaye pia ametuambia kuhusu upendo wenu katika
Roho wa Mungu. **9** Kwa sababu hii, tangu siku ile
tuliposikia habari zenu, hatujakoma kuomba kwa
ajili yenu na kumsihi Mungu awajaze ninyi maarifa
ya mapenzi yake katika hekima yote ya kiroho na
ufahamu. **10** Nasi tunaomba haya ili mpate kuishi
maisha yanayostahili mbele za Bwana Isa, na mpate
kumpendeza kwa kila namna: mkizaa matunda kwa
kila kazi njema, mkikua katika kumjua Mungu, **11**
mkiwa mmetiwa nguvu kwa uwezo wote kwa kadiri ya
nguvu yake yenye utukufu, ili mpate kuwa na wingi wa
saburi na uvumilivu. Nanyi kwa furaha **12** mkimshukuru
Baba, ambaye amewastahilisha kushiriki katika urithi
wa watakatifu katika ufalme wa nuru. **13** Kwa maana
ametuokoa kutoka ufalme wa giza na kutuingiza
katika ufalme wa Mwana wake Mpendwa, **14** ambaye
kwake tunao ukombozi, yaani msamaha wa dhambi.
**15** Yeye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa
wa kwanza wa viumbe vyote. **16** Kwake yeye vitu
vyote vilivyo mbinguni na juu ya nchi viliumbwa:
vitu vinavyoonekana na visivyoonekana, viwe ni
viti vya utawala au falme, au wenye mamlaka au
watawala; vitu vyote viliumbwa kupitia kwake na kwa
ajili yake. **17** Yeye alikuwako kabla ya vitu vyote,
na katika yeye vitu vyote vinashikamana pamoja.
**18** Yeye ndiye kichwa cha mwili, yaani jumuiya ya
waumini, naye ndiye mwanzo na mzaliwa wa kwanza
kutoka kwa wafu, ili yeye awe mkuu katika vitu vyote.
**19** Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba utimilifu
wake wote ukae ndani yake, **20** na kupitia kwake
aweze kuvipatanisha vitu vyote kwake mwenyewe,
viwe ni vitu vilivyo duniani au vilivyo mbinguni,
kwa kufanya amani kwa damu yake iliyomwagika
msalabani. **21** Hapo kwanza mlikuwa mmetengana
na Mungu, na mlikuwa adui zake katika nia zenu
kwa sababu ya mienendo yenu mibaya. **22** Lakini
sasa Mungu amewapatanisha ninyi kupitia kwa mwili
wa Al-Masihi kupitia mauti, ili awalete mbele zake
mkiwa watakatifu, bila dosari wala lawama, **23** ikiwa
mnaendelea katika imani yenu mkiwa imara na thabiti,
pasipo kuliacha tumaini lililoahidiwa katika Injili. Hii
ndiyo ile Injili mliyoisikia, ambayo imehubiriwa kwa
kila kiumbe chini ya mbingu, na ambayo mimi Paulo
nimekuwa mtumwa wake. **24** Sasa nafurahia kule
kuteseka kwangu kwa ajili yenu, na katika mwili
wangu ninatimiliza yale yaliyopungua katika mateso
ya Al-Masihi kwa ajili ya mwili wake, ambao ni jumuiya
ya waumini. **25** Mimi nimekuwa mtumishi wa jumuiya
ya waumini kwa wajibu alionipa Mungu ili kuwaletea
ninyi neno la Mungu kwa ukamilifu: **26** Hii ni siri
iliyokuwa imefichika tangu zamani na kwa vizazi
vingi, lakini sasa imefunuliwa kwa watakatifu. **(aiōn
g165)** **27** Kwao Mungu amechagua kujulisha miongoni
mwa watu wa Mataifa utukufu wa utajiri wa siri hii,
ambayo ni Al-Masihi ndani yenu, tumaini la utukufu.
**28** Yeye ndiye tunayemtangaza, tukimwonya kila mtu
na kumfundisha kila mtu kwa hekima yote ili tuweze
kumleta kila mmoja akiwa amekamilika katika Al-
Masihi. **29** Kwa ajili ya jambo hili, ninajitaabisha,
nikijitahidi kwa kadiri ya nguvu zake ambazo hutenda
kazi ndani yangu kwa uweza mwingi.

**2** Nataka mjue jinsi ninavyojitaabisha kwa ajili yenu
na kwa ajili ya wale walio Laodikia, na pia kwa
ajili ya wote ambao hawajapata kuniona mimi binafsi.
**2** Kusudi langu ni watiwe moyo na kuunganishwa
katika upendo, ili wapate ule utajiri wa ufahamu
mkamilifu, ili waijue siri ya Mungu, yaani Al-Masihi,
**3** ambaye ndani yake kumefichwa hazina zote za
hekima na maarifa. **4** Nawaambia mambo haya ili
mtu yeyote asiwadanganye kwa maneno matamu. **5**
Kwa kuwa ingawa mimi siko pamoja nanyi kimwili,
niko pamoja nanyi kiroho, nami nafurahi kuuona
utaratibu wenu na jinsi uthabiti wa imani yenu
katika Al-Masihi ulivyo. **6** Hivyo basi, kama vile

mlivyompokea Al-Masihi Isa kuwa Bwana, endeleeni
kukaa ndani yake, 7 mkijikita na kujengwa ndani yake,
mkiimarishwa katika imani kama mlivyofundishwa,
na kufurika kwa wingi wa shukrani. 8 Chungeni mtu
yeyote asiwafanye ninyi mateka kwa elimu batili na
madanganyo matupu, yanayotegemea mapokeo ya
wanadamu na mafundisho ya ulimwengu badala
ya Al-Masihi. 9 Maana utimilifu wote wa Mungu
unakaa ndani ya Al-Masihi katika umbile la mwili
wa kibinadamu, 10 nanyi mmepewa ukamilifu ndani
ya Al-Masihi, aliye mkuu juu ya kila nguvu na kila
mamlaka. 11 Katika Al-Masihi pia mlitahiriwa kwa
kutengwa mbali na asili ya dhambi, si kwa tohara
inayofanywa kwa mikono ya wanadamu, bali kwa ile
tohara iliyofanywa na Al-Masihi, 12 mkiwa mmezikwa
pamoja naye katika ubatizo, na kufufuliwa pamoja
naye kupitia kwa imani yenu katika uweza wa Mungu,
aliyemfufua kutoka kwa wafu. 13 Mlipokuwa wafu
katika dhambi zenu na kutokutahiriwa katika asili
yenu ya dhambi, Mungu aliwafanya mwe hai pamoja
na Al-Masihi. Alitusamehe dhambi zetu zote, 14
baada ya kuifuta ile hati yenye mashtaka yaliyokuwa
yanatukabili, pamoja na maagizo yake. Aliiondoa
isiwepo tena, akaigongelea kwenye msalaba wake.
15 Baada ya Mungu kuzivua enzi na mamlaka,
aliziaibisha hadharani, akishangilia katika ushindi wa
msalaba. 16 Basi, mtu asiwahukumu ninyi kuhusu
vyakula au vinywaji, au kuhusu kuadhimisha sikukuu
za dini, au Sikukuu za Mwezi Mwandamo au siku ya
Sabato. 17 Hizi zilikuwa kivuli cha mambo yajayo;
lakini uhalisi unapatikana kwa Al-Masihi. 18 Mtu
yeyote asiwaondolee thawabu yenu kwa kusisitiza
unyenyekevu wa uongo na kuabudu malaika. Mtu
kama huyo hudumu katika maono yake, akijivuna
bila sababu katika mawazo ya kibinadamu. 19 Yeye
amepoteza ushirikiano na Kichwa, ambaye kutoka
kwake mwili wote unalishwa na kushikamanishwa
pamoja kwa viungo na mishipa, nao hukua jinsi Mungu
anavyouwezesha. 20 Kwa kuwa mlikufa pamoja na
Al-Masihi, mkayaacha yale mafundisho ya msingi ya
ulimwengu huu, kwa nini bado mnaishi kana kwamba
ninyi ni wa ulimwengu? Kwa nini mnajitia chini ya amri
kama hizi: 21 "Msishike! Msionje! Msiguse!"? 22 Amri
hizi zote mwisho wake ni kuharibika zinapotumiwa,
kwa sababu msingi wake ni katika maagizo na
mafundisho ya wanadamu. 23 Kwa kweli amri kama
hizo huonekana kama zina hekima, katika namna za
ibada walizojitungia wenyewe, na unyenyekevu wa
uongo na kuutawala mwili kwa ukali, lakini hazifai kitu
katika kuzuia tamaa za mwili.

**3** Basi, kwa kuwa mmefufuliwa pamoja na Al-Masihi,
yatafuteni yaliyo juu, Al-Masihi alikoketi mkono
wa kuume wa Mungu. 2 Yafikirini mambo yaliyo
juu, wala si ya duniani. 3 Kwa maana ninyi mlikufa,
nao uhai wenu sasa umefichwa pamoja na Al-
Masihi katika Mungu. 4 Al-Masihi, aliye uzima wenu,
atakapofunuliwa, ndipo nanyi mtafunuliwa pamoja
naye katika utukufu. 5 Basi, ueni kabisa chochote
kilicho ndani yenu cha asili ya kidunia: yaani uasherati,
uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya na ulafi,
ambao ni ibada ya sanamu. 6 Kwa sababu ya mambo
haya, ghadhabu ya Mungu inakuja. 7 Ninyi pia zamani
mlienenda katika mambo haya mlipoishi maisha
hayo. 8 Lakini sasa yawekeni mbali nanyi mambo
kama haya yote: yaani hasira, ghadhabu, uovu,
masingizio na lugha chafu kutoka midomoni mwenu.
9 Msiambiane uongo, kwa maana mmevua kabisa utu
wenu wa kale pamoja na matendo yake, 10 nanyi
mmevaa utu mpya, unaofanywa upya katika ufahamu
sawasawa na mfano wa Muumba wake. 11 Hapa
hakuna Myunani wala Myahudi, aliyetahiriwa wala
asiyetahiriwa, asiyestaarabika wala aliyestaarabika,
mtumwa wala mtu huru, bali Al-Masihi ni yote, na ndani
ya yote. 12 Basi, kwa kuwa ninyi mmekuwa wateule
wa Mungu, watakatifu wanaopendwa sana, jivikeni
moyo wa huruma, utu wema, unyenyekevu, upole na
uvumilivu. 13 Vumilianeni na kusameheana mtu akiwa
na lalamiko lolote dhidi ya mwenzake. Sameheaneni
kama vile Bwana Isa alivyowasamehe ninyi. 14 Zaidi
ya maadili haya yote jivikeni upendo, ambao ndio
unaofunga kila kitu pamoja katika umoja mkamilifu. 15
Amani ya Al-Masihi na itawale mioyoni mwenu, kwa
kuwa ninyi kama viungo vya mwili mmoja mmeitiwa
amani. Tena kuweni watu wa shukrani. 16 Neno la Al-
Masihi na likae kwa wingi ndani yenu, mkifundishana
na kuonyana katika hekima yote, mkimwimbia Mungu
zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni, huku mkiwa na
shukrani mioyoni mwenu. 17 Lolote mfanyalo, ikiwa
ni kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina
la Bwana Isa, mkimshukuru Mungu Baba Mwenyezi
kupitia kwake. 18 Ninyi wake, watiini waume zenu,
kama inavyostahili katika Bwana Isa. 19 Ninyi waume,

wapendeni wake zenu, wala msiwe wakali kwao.
20 Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo
yote, kwa maana hii inampendeza Bwana Isa. 21
Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu, wasije
wakakata tamaa. 22 Ninyi watumwa, watiini mabwana
zenu wa hapa duniani katika mambo yote. Fanyeni
hivyo si wakiwepo tu, wala si kwa kujipendekeza tu
kwao, bali kwa moyo mnyofu na kumcha Bwana.
23 Lolote mfanyalo, fanyeni kwa moyo wote kama
watu wanaomtumikia Bwana Isa, na si wanadamu,
24 kwa kuwa mnajua kwamba mtapokea urithi wenu
kutoka kwa Bwana ukiwa thawabu yenu. Ni Bwana
Isa Al-Masihi mnayemtumikia. 25 Yeyote atendaye
mabaya atapewa adhabu ya mabaya yake, wala
hakuna upendeleo.

4 Ninyi mabwana, watendeeni watumwa wenu
yaliyo haki na yanayostahili, mkitambua kwamba
ninyi pia mnaye Bwana mbinguni. 2 Dumuni sana
katika maombi, mkikesha katika hayo pamoja na
kushukuru. 3 Pia tuombeeni na sisi ili Mungu
atufungulie mlango wa kunena neno lake, ili tupate
kuitangaza siri ya Al-Masihi, ambayo kwa ajili yake
nimefungwa. 4 Ombeni ili nipate kuitangaza hiyo
siri kwa udhahiri kama inipasavyo. 5 Nendeni kwa
hekima mbele yao walio nje, mkiukomboa wakati.
6 Maneno yenu yawe yamejaa neema siku zote,
yanayofaa, ili mjue jinsi iwapasavyo kumjibu kila
mtu. 7 Tikiko atawaambia habari zangu zote. Yeye ni
ndugu mpendwa, mtendakazi mwaminifu na mtumishi
mwenzangu katika Bwana Isa. 8 Nimemtuma kwenu
kwa lengo maalum la kuwafahamisha hali yetu, na pia
awatie moyo. 9 Anakuja pamoja na Onesimo, ndugu
yetu mpendwa na mwaminifu, ambaye ni mmoja
wenu. Watawaambia mambo yote yanayotendeka
hapa kwetu. 10 Aristarko aliye mfungwa pamoja
nami anawasalimu, vivyo hivyo Marko, binamu yake
Barnaba. (Mmeshapata maagizo yanayomhusu;
akija kwenu, mpokeeni.) 11 Isa aitwaye Yusto
pia anawasalimu. Hawa peke yao ndio Wayahudi
miongoni mwa watendakazi wenzangu kwa ajili ya
ufalme wa Mungu, nao wamekuwa faraja kwangu. 12
Epafra, ambaye ni mmoja wenu na mtumishi wa Al-
Masihi Isa, anawasalimu. Yeye siku zote anawaombea
kwa bidii kwamba msimame imara katika mapenzi
yote ya Mungu, mkiwa wakamilifu na thabiti. 13
Ninashuhudia kumhusu kwamba anafanya kazi kwa
bidii kwa ajili yenu, na kwa ajili ya ndugu wa Laodikia
na wale wa Hierapoli. 14 Rafiki yetu mpendwa, Luka
yule tabibu, pamoja na Dema, wanawasalimu. 15
Wasalimuni ndugu wote wa Laodikia, na pia Nimfa,
pamoja na kundi la waumini wanaokutana katika
nyumba yake. 16 Baada ya barua hii kusomwa
kwenu, hakikisheni kwamba inasomwa pia katika
kundi la waumini wa Walaodikia. Nanyi pia msome
barua inayotoka Laodikia. 17 Mwambieni Arkipo hivi:
“Hakikisha kuwa unakamilisha ile huduma uliyopokea
katika Bwana Isa.” 18 Mimi Paulo naandika salamu hizi
kwa mkono wangu mwenyewe. Kumbukeni minyororo
yangu. Neema iwe nanyi.

# 1 Wathesalonike

1 Paulo, Silvano na Timotheo. 2 Siku zote
tunamshukuru Mungu kwa ajili yenu ninyi
nyote, tukiwataja kwenye maombi yetu daima. 3
Tunaikumbuka daima kazi yenu ya imani mbele za
Mungu aliye Baba yetu, taabu yenu katika upendo na
saburi yenu ya tumaini katika Bwana wetu Isa Al-
Masihi. 4 Ndugu zetu mnaopendwa na Mungu, kwa
kuwa tunajua kwamba Mungu amewachagua, 5 kwa
sababu ujumbe wetu wa Injili haukuja kwenu kwa
maneno matupu bali pia ulidhihirishwa katika nguvu
na katika Roho wa Mungu, tena ukiwa na uthibitisho
kamili, kama vile ninyi wenyewe mnavyojua jinsi
tulivyoenenda kati yenu kwa ajili yenu. 6 Nanyi mkawa
wafuasi wetu na wa Bwana Isa, ingawa mlipata
mateso mengi, mlilipokea lile Neno kwa furaha katika
Roho wa Mungu. 7 Hivyo ninyi mkawa kielelezo kwa
waumini wote katika Makedonia na Akaya. 8 Kwa
maana kutoka kwenu neno la Bwana Isa limesikika,
si katika Makedonia na Akaya tu, bali pia imani yenu
katika Mungu imejulikana kila mahali, kiasi kwamba
hatuna haja ya kusema chochote juu yake. 9 Kwa
maana watu wa maeneo hayo wenyewe wanaeleza
jinsi mlivyotupokea na jinsi mlivyomgeukia Mungu
mkaacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai
na wa kweli, 10 na ili kumngojea Mwanawe kutoka
mbinguni, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa
wafu: yaani Isa, yeye aliyetuokoa kutoka ghadhabu
inayokuja.

2 Ndugu zangu, kwa kuwa ninyi wenyewe mnajua
kwamba kuja kwetu kwenu hakukuwa bure, 2
kama vile mjuavyo, tulikuwa tumeteswa na kutukanwa
huko Filipi, lakini hata hivyo, kwa msaada wa Mungu
wetu, tulikuwa na ujasiri wa kuwaambia Injili ya Mungu
ingawa kulikuwa na upinzani mkubwa. 3 Kwa maana
himizo letu halikutokana na hila wala nia mbaya
au udanganyifu. 4 Kinyume chake, tulinena kama
watu tuliokubaliwa na Mungu tukakabidhiwa Injili. Sisi
hatujaribu kuwapendeza wanadamu bali kumpendeza
Mungu, yeye ayachunguzaye mawazo ya ndani
sana ya mioyo yetu. 5 Kama mnavyojua, hatukuja
kwenu kwa maneno ya kujipendekeza au maneno
yasiyo ya kweli ili kuficha tamaa mbaya; Mungu
ndiye shahidi yetu. 6 Hatukuwa tukitafuta sifa kutoka
kwa wanadamu, wala kutoka kwenu au kwa mtu
mwingine yeyote, ingawa kama mitume wa Al-Masihi
tungeweza kuwa mzigo kwenu. 7 Lakini tulikuwa
wapole kati yenu, kama vile mama anawatunza watoto
wake wadogo. 8 Tuliwapenda sana, kiasi kwamba
tulifurahia kushirikiana nanyi, si Injili ya Mungu tu, bali
hata maisha yetu, kwa sababu mlikuwa wa thamani
mno kwetu. 9 Ndugu zetu, mnakumbuka juhudi yetu
na taabu yetu. Tulifanya kazi usiku na mchana, ili
tusiwe mzigo kwa mtu yeyote tulipokuwa tukiwahubiria
Injili ya Mungu. 10 Ninyi wenyewe ni mashahidi
na Mungu pia, jinsi tulivyokuwa watakatifu, wenye
haki na wasio na lawama miongoni mwenu ninyi
mlioamini. 11 Maana mnajua kwamba tuliwatendea
kila mmoja wenu kama vile baba anavyowatendea
watoto wake. 12 Tuliwatia moyo, tukiwafariji na
kuwahimiza kuishi maisha yanayompendeza Mungu,
anayewaita katika ufalme wake na utukufu wake.
13 Nasi pia tunamshukuru Mungu bila kukoma kwa
sababu mlipolipokea neno la Mungu mlilosikia kutoka
kwetu, hamkulipokea kama neno la wanadamu,
bali mlilipokea kama lilivyo hasa, neno la Mungu,
linalotenda kazi ndani yenu ninyi mnaoamini. 14
Kwa maana ninyi ndugu zetu, mlifanyika wafuasi wa
makundi ya waumini wa Mungu walio ndani ya Al-
Masihi Isa katika Yudea. Mlipata mateso yale yale
kutoka kwa watu wenu wenyewe kama vile waumini
hao walivyoteswa na Wayahudi, 15 wale waliomuua
Bwana Isa na manabii, nasi wakatufukuza pia. Watu
hao walimchukiza Mungu na tena ni adui wa watu
wote, 16 wakijitahidi kutuzuia tusizungumze na watu
wa Mataifa ili wapate kuokolewa. Kwa njia hii wanazidi
kujilundikia dhambi zao hadi kikomo. Lakini hatimaye
ghadhabu ya Mungu imewafikia. 17 Lakini ndugu zetu,
tulipotenganishwa nanyi kwa muda mfupi (ingawa
kutengana huko kulikuwa kwa mwili tu, si kwa moyo),
tulizidi kuwa na shauku kubwa kuwaona uso kwa
uso. 18 Maana tulitaka kuja kwenu, hasa mimi Paulo,
nilitaka kuja tena na tena, lakini Shetani akatuzuia. 19
Kwa maana tumaini letu ni nini, au furaha yetu, au taji
letu la kujisifia mbele za Bwana wetu Isa Al-Masihi
wakati wa kuja kwake? Je, si ni ninyi? 20 Naam, ninyi
ndio fahari yetu na furaha yetu.

3 Kwa hivyo tulipokuwa hatuwezi kuvumilia zaidi,
tuliamua tubaki Athene peke yetu. 2 Tukamtuma
Timotheo ambaye ni ndugu yetu na mtumishi
mwenzetu wa Mungu katika kuieneza Injili ya Al-

Masihi, aje kuwaimarisha na kuwatia moyo katika
imani yenu, 3 ili mtu yeyote asifadhaishwe na mateso
haya. Mnajua vyema kwamba tumewekewa hayo
mateso. 4 Kwa kweli, tulipokuwa pamoja nanyi
tuliwaambia mara kwa mara kwamba tutateswa na
imekuwa hivyo kama mnavyojua. 5 Kwa sababu
hii niliposhindwa kuvumilia zaidi, nilimtuma mtu ili
nipate habari za imani yenu. Niliogopa kwamba
kwa njia fulani yule mjaribu asiwe amewajaribu,
nasi tukawa tumejitaabisha bure. 6 Lakini Timotheo
amerejea kwetu hivi sasa kutoka kwenu, na ameleta
habari njema kuhusu imani yenu na upendo wenu.
Ametuambia kwamba siku zote mnatukumbuka kwa
wema, na kwamba mna shauku ya kutuona kama
vile sisi tulivyo na shauku ya kuwaona ninyi. 7 Kwa
hiyo, ndugu zetu, katika dhiki na mateso yetu yote
tumefarijika kwa sababu ya imani yenu. 8 Sasa kwa
kuwa hakika tunaishi, kwa kuwa ninyi mmesimama
imara katika Bwana Isa. 9 Je, tutawezaje kumshukuru
Mungu kiasi cha kutosha kwa ajili yenu, kutokana na
furaha tuliyo nayo mbele za Mungu wetu kwa sababu
yenu? 10 Usiku na mchana tunaomba kwa bidii ili
tupate kuwaona tena na kujaza kile kilichopungua
katika imani yenu. 11 Basi Mungu wetu na Baba
yetu mwenyewe na Bwana wetu Isa atengeneze
njia ya sisi kuja kwenu. 12 Bwana Isa na auongeze
upendo wenu na kuuzidisha kati yenu na kwa wengine
wote, kama vile tulivyo na upendo mwingi kwenu. 13
Tunamwomba Mungu aimarishe mioyo yenu ili msiwe
na lawama katika utakatifu mbele za Mungu wetu
aliye Baba yetu wakati wa kuja kwake Bwana wetu
Isa pamoja na watakatifu wote.

**4** Na kuhusu mambo mengine, ndugu, tuliwafundisha
jinsi ya kuishi ili kumpendeza Mungu, kama vile
mnavyoishi. Sasa tunawaomba na kuwasihi katika
Bwana Isa mfanye hivi zaidi na zaidi. 2 Kwa kuwa
mnajua maagizo tuliyowapa kwa mamlaka ya Bwana
Isa. 3 Mapenzi ya Mungu ni ninyi mtakaswe, ili
mjiepushe na uasherati, 4 na kila mmoja wenu ajifunze
kuutawala mwili wake mwenyewe katika utakatifu na
heshima, 5 bali si kwa tamaa mbaya kama watu wa
Mataifa wasiomjua Mungu. 6 Katika jambo hili mtu
asimkosee ndugu yake wala kumlaghai. Kwa kuwa
Mwenyezi Mungu ni mlipiza kisasi katika mambo haya
yote, kama vile tulivyokwisha kuwaambia mapema
na kuwaonya vikali. 7 Kwa maana Mungu hakutuitia
uchafu, bali utakatifu. 8 Kwa hiyo, mtu yeyote
anayekataa mafundisho haya hamkatai mwanadamu,
bali anamkataa Mungu anayewapa ninyi Roho wake
Mtakatifu. 9 Sasa kuhusu upendo wa ndugu hamna
haja mtu yeyote kuwaandikia, kwa maana ninyi
wenyewe mmefundishwa na Mungu kupendana. 10
Nanyi kwa kweli mnawapenda ndugu wote katika
Makedonia nzima. Lakini ndugu, tunawasihi mzidi
sana kuwapenda. 11 Jitahidini kuishi maisha ya
utulivu, kila mtu akijishughulisha na mambo yake
mwenyewe na kufanya kazi kwa mikono yake, kama
vile tulivyowaagiza, 12 ili maisha yenu ya kila siku
yajipatie heshima kutoka kwa watu walio nje, ili
msimtegemee mtu yeyote. 13 Lakini ndugu, hatutaki
mkose kujua kuhusu wale waliolala katika mauti,
ili msihuzunike kama watu wengine wasiokuwa na
tumaini. 14 Tunaamini kwamba Isa alikufa na kufufuka.
Na kwa hivyo, tunaamini kwamba Mungu atawaleta
pamoja naye wale waliolala katika Isa. 15 Kulingana
na neno la Bwana Isa mwenyewe, tunawaambia
kwamba sisi ambao bado tuko hai, tuliobaki hadi
kuja kwake Bwana Isa, hakika hatutawatangulia
waliolala katika mauti. 16 Kwa maana Bwana Isa
mwenyewe atashuka kutoka mbinguni, akitoa amri
kwa sauti kuu, pamoja na sauti ya malaika mkuu, na
sauti ya tarumbeta ya Mungu. Nao waliokufa wakiwa
katika Al-Masihi watafufuka kwanza. 17 Baada ya
hilo sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao
katika mawingu ili kumlaki Bwana Isa hewani, hivyo
tutakuwa pamoja na Bwana Isa milele. 18 Kwa hiyo
farijianeni kwa maneno haya.

**5** Basi ndugu, hatuna haja ya kuwaandikia kuhusu
nyakati na majira, 2 kwa kuwa mnajua vyema
kwamba siku ya Mwenyezi Mungu itakuja kama mwizi
anavyokuja usiku. 3 Watu wanaposema, “Kuna amani
na salama,” maangamizi huwajia ghafula, kama vile
uchungu unavyomjia mwanamke mwenye mimba;
nao hakika hawatatoroka. 4 Bali ninyi, ndugu, hampo
gizani hata siku ile iwakute ghafula kama mwizi. 5
Ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa mchana.
Sisi si wana wa giza wala wa usiku. 6 Kwa hiyo basi,
tusilale kama watu wengine wanavyolala, bali tukeshe
na kuwa na kiasi. 7 Kwa kuwa wote wanaolala, hulala
usiku, na wale wanaolewa, hulewa usiku. 8 Lakini
kwa kuwa sisi ni wana wa mchana, basi tuwe na kiasi,
tukijivika imani na upendo kama dirii kifuani na tumaini

letu la wokovu kama chapeo. 9 Kwa maana Mungu
hakutuita ili tupate ghadhabu bali tupate wokovu
kupitia kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi. 10 Yeye alikufa
kwa ajili yetu ili hata kama tuko macho au tumelala,
tupate kuishi pamoja naye. 11 Kwa hiyo farijianeni na
kujengana, kama vile mnavyofanya sasa. 12 Sasa
tunawaomba, ndugu, waheshimuni wale wanaofanya
kazi kwa bidii miongoni mwenu, wale ambao wana
mamlaka juu yenu katika Bwana Isa na ambao
wanawaonya. 13 Waheshimuni sana katika upendo
kwa ajili ya kazi zao. Ishini kwa amani ninyi kwa
ninyi. 14 Nasi twawasihi, ndugu, waonyeni walio
wavivu, watieni moyo waoga, wasaidieni wanyonge
na kuwavumilia watu wote. 15 Angalieni kuwa mtu
asimlipe mwenzake maovu kwa maovu, bali siku zote
tafuteni kutendeana mema ninyi kwa ninyi na kwa
watu wote. 16 Furahini siku zote; 17 ombeni bila
kukoma; 18 shukuruni kwa kila jambo, kwa maana
haya ndio mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Al-
Masihi Isa. 19 Msiuzime moto wa Roho wa Mungu.
20 Msiyadharau maneno ya unabii. 21 Jaribuni kila
kitu. Yashikeni yaliyo mema. 22 Jiepusheni na uovu
wa kila namna. 23 Mungu mwenyewe, Mungu wa
amani, awatakase ninyi kabisa. Nanyi mhifadhiwe
roho zenu, nafsi zenu na miili yenu, bila kuwa na
lawama katika Bwana wetu Isa Al-Masihi. 24 Yeye
aliyewaita ni mwaminifu naye atafanya hayo. 25
Ndugu, tuombeeni. 26 Wasalimuni ndugu wote kwa
busu takatifu. 27 Ninawaagiza mbele za Bwana Isa
mhakikishe kuwa ndugu wote wanasomewa barua hii.
28 Neema ya Bwana wetu Isa Al-Masihi iwe nanyi.
Amen.

# 2 Wathesalonike

1 Paulo, Silvano na Timotheo. 2 Neema na amani
zinazotoka kwa Mungu Baba Mwenyezi na kwa
Bwana Isa Al-Masihi ziwe nanyi. 3 Ndugu, inatupasa
kumshukuru Mungu kwa ajili yenu siku zote, na
inastahili hivyo kwa sababu imani yenu inazidi kukua
sana, nao upendo wa kila mmoja wenu kwa mwenzake
unazidi kuongezeka. 4 Ndiyo sababu miongoni mwa
makundi ya waumini ya Mungu, tunajivunia saburi
yenu na imani mliyo nayo katika mateso yote na
dhiki mnazostahimili. 5 Haya yote ni uthibitisho
kwamba hukumu ya Mungu ni ya haki, na kwa
sababu hiyo ninyi mtahesabiwa kwamba mnastahili
kuwa wa ufalme wa Mungu, mnaoteswa kwa ajili
yake. 6 Mungu ni mwenye haki: yeye atawalipa
mateso wale wanaowatesa ninyi, 7 na kuwapa ninyi
mnaoteseka amani pamoja na sisi, wakati Bwana
Isa atadhihirishwa kutoka mbinguni katika mwali
wa moto pamoja na malaika wake wenye nguvu.
8 Atawaadhibu wale wasiomjua Mungu na ambao
hawakuitii Injili ya Bwana wetu Isa. 9 Wataadhibiwa
kwa uangamivu wa milele na kutengwa na uso wa
Mwenyezi Mungu na utukufu wa uweza wake, **(aiōnios
g166)** 10 siku hiyo atakapokuja kutukuzwa katika
watakatifu wake na kustaajabiwa miongoni mwa wote
walioamini. Ninyi pia mtakuwa miongoni mwa hawa
kwa sababu mliamini ushuhuda wetu kwenu. 11 Kwa
sababu hii, tunawaombea ninyi bila kukoma, ili Mungu
wetu apate kuwahesabu kuwa mnastahili wito wake
na kwamba kwa uwezo wake apate kutimiza kila
kusudi lenu jema na kila tendo linaloongozwa na
imani yenu. 12 Tunaomba hivi ili Jina la Bwana wetu
Isa lipate kutukuzwa ndani yenu, nanyi ndani yake,
kulingana na neema ya Mungu wetu na Bwana Isa
Al-Masihi.

2 Ndugu, kuhusu kuja kwake Bwana wetu Isa
Al-Masihi na kukusanyika kwetu pamoja mbele
zake, tunawasihi, 2 msiyumbishwe kwa urahisi wala
msitiwe wasiwasi na roho, wala neno la unabii, au
barua inayosemekana kuwa imetoka kwetu, kusema
kwamba siku ya Mwenyezi Mungu imekwisha kuwepo.
3 Mtu yeyote asiwadanganye kwa namna yoyote
kwa maana siku ile haitakuja hadi uasi utokee
kwanza, na yule mtu wa kuasi adhihirishwe, yule
ambaye amehukumiwa kuangamizwa kabisa. 4 Yeye
atapingana na kujitukuza juu ya kila kitu kiitwacho
Mungu au kinachoabudiwa, ili kujiweka juu katika
Hekalu la Mungu, akijitangaza mwenyewe kuwa
ndiye Mungu. 5 Je, hamkumbuki kwamba nilipokuwa
pamoja nanyi niliwaambia mambo haya? 6 Nanyi
sasa mnajua kinachomzuia, ili apate kudhihirishwa
wakati wake utakapowadia. 7 Maana ile nguvu ya siri
ya uasi tayari inatenda kazi, lakini yule anayeizuia
ataendelea kufanya hivyo hadi atakapoondolewa. 8
Hapo ndipo yule mwasi atafunuliwa, ambaye Bwana
Isa atamteketeza kwa pumzi ya kinywa chake na
kumwangamiza kabisa kwa utukufu wa kuja kwake.
9 Kuja kwa yule mwasi kutalingana na vile Shetani
hufanya kazi. Atatumia nguvu za aina mbalimbali
katika miujiza, na ishara na ajabu za uongo, 10
na katika njia zote ambazo uovu hudanganya
wanaoangamia. Wanaangamia kwa sababu walikataa
kuipenda kweli ili wapate kuokolewa. 11 Kwa sababu
hii, Mungu anawatumia nguvu ya udanganyifu, ili
waamini uongo, 12 na hivyo wahukumiwe wote ambao
hawakuiamini ile kweli, bali wamefurahia uovu. 13
Lakini inatupasa kumshukuru Mungu daima kwa
ajili yenu, ndugu mpendwao na Bwana Isa, kwa
sababu Mungu aliwachagua ninyi tangu mwanzo ili
mwokolewe kwa kutakaswa na Roho wa Mungu kwa
kuiamini kweli. 14 Kwa kusudi hili Mungu aliwaita
ninyi kupitia Injili tuliyowahubiria, ili mpate kushiriki
katika utukufu wa Bwana wetu Isa Al-Masihi. 15
Hivyo basi, ndugu wapendwa, simameni imara na
myashike sana yale mafundisho tuliyowapa ikiwa ni
kwa maneno ya kinywa au kwa barua. 16 Bwana
wetu Isa Al-Masihi mwenyewe na Mungu, Baba yetu,
aliyetupenda na kwa neema yake akatupatia faraja
ya milele na tumaini jema, **(aiōnios g166)** 17 awafariji
mioyo yenu na kuwaimarisha katika kila neno na
tendo jema.

3 Hatimaye, ndugu, tuombeeni ili Neno la Bwana
Isa lipate kuenea kwa haraka na kuheshimiwa
kila mahali, kama vile ilivyokuwa kwenu. 2 Ombeni
pia ili tupate kuokolewa kutokana na watu waovu na
wabaya, kwa maana si wote wanaoamini. 3 Lakini
Bwana Isa ni mwaminifu, naye atawaimarisha ninyi
na kuwalinda kutokana na yule mwovu. 4 Nasi tuna
tumaini katika Bwana Isa ya kuwa mnafanya na
mtaendelea kufanya yale tuliyowaagiza. 5 Mwenyezi
Mungu aiongoze mioyo yenu katika upendo wa

Mungu na katika saburi ya Al-Masihi. 6 Ndugu,
tunawaagiza katika Jina la Bwana Isa Al-Masihi,
jitengeni na kila ndugu ambaye ni mvivu na ambaye
haishi kufuatana na maagizo tuliyowapa. 7 Maana
ninyi wenyewe mnajua jinsi iwapasavyo kufuata
mfano wetu. Sisi hatukuwa wavivu tulipokuwa pamoja
nanyi, 8 wala hatukula chakula cha mtu yeyote
pasipo kukilipia. Badala yake tulifanya kazi kwa bidii
usiku na mchana, ili tusimlemee mtu yeyote miongoni
mwenu. 9 Tulifanya hivi, si kwa sababu hatukuwa
na haki ya kupata msaada kama huo, bali ndio sisi
wenyewe tuwe mfano wenu wa kufuata. 10 Kwa
maana hata tulipokuwa pamoja nanyi, tuliwapa amri
kwamba: "Mtu yeyote asiyetaka kufanya kazi, hata
kula asile." 11 Kwa kuwa tunasikia kwamba baadhi ya
watu miongoni mwenu ni wavivu. Hawafanyi kazi,
bali hujishughulisha na mambo ya wengine. 12 Basi
watu kama hao tunawaagiza na kuwahimiza katika
Bwana Isa Al-Masihi, kwamba wafanye kazi kwa
utulivu kwa ajili ya chakula chao wenyewe. 13 Lakini
kwenu ninyi, ndugu, kamwe msichoke katika kutenda
mema. 14 Ikiwa mtu yeyote hayatii maagizo yetu
yaliyo katika barua hii, mwangalieni sana mtu huyo.
Msishirikiane naye, ili apate kuona aibu. 15 Lakini
msimhesabu kuwa adui, bali mwonyeni kama ndugu.
16 Basi, Bwana wa amani mwenyewe awapeni amani
nyakati zote na kwa kila njia. Mwenyezi Mungu awe
nanyi nyote. 17 Mimi, Paulo, ninaandika salamu hizi
kwa mkono wangu mwenyewe. Hii ndio alama ya
utambulisho katika barua zangu zote. Hivi ndivyo
niandikavyo. 18 Neema ya Bwana wetu Isa Al-Masihi
iwe nanyi nyote. Amen.

# 1 Timotheo

1 Paulo, mtume wa Al-Masihi Isa, kwa amri ya
Mungu Mwokozi wetu, na ya Al-Masihi Isa aliye
tumaini letu. 2 Kwa Timotheo, mwanangu halisi
katika imani. 3 Kama nilivyokusihi wakati nilipoenda
Makedonia, endelea kubaki Efeso, ili upate kuwaagiza
watu wasiendelee kufundisha mafundisho ya uongo
4 wala wasitoe muda wao kwa hadithi za kubuniwa
na orodha za majina ya vizazi visivyo na mwisho,
ambazo huchochea mabishano badala ya mpango
wa Mungu utokanao na imani. 5 Kusudi la maagizo
haya ni upendo unaotoka katika moyo safi, dhamiri
safi na imani ya kweli. 6 Watu wengine wamepotoka
kutoka haya na kugeukia majadiliano yasiyo na
maana kwa kuwa, 7 wanataka kuwa walimu wa Torati,
lakini hawajui mambo yale wanayosema wala hayo
wanayoyatumainia kwa uthabiti. 8 Tunajua kwamba
sheria ni njema ikiwa inatumika kwa halali kama
ilivyokusudiwa. 9 Lakini tunajua ya kuwa sheria si kwa
ajili ya wenye haki, bali kwa ajili ya wavunja sheria
na waasi, kwa ajili ya wasiomcha Mungu na wenye
dhambi, wasio watakatifu na wanaokufuru; kwa wale
wawauao baba zao au mama zao, kwa wauaji, 10
kwa wazinzi na wahanithi, kwa wale wauzao watu, na
kwa waongo na waapao kwa uongo, na kwa chochote
kingine kilicho kinyume na mafundisho ya kweli,
11 ambayo yanakubaliana na Injili ya utukufu wa
Mungu anayehimidiwa, ambayo mimi nimewekewa
amana. 12 Namshukuru Al-Masihi Isa Bwana wetu,
aliyenitia nguvu, kwa sababu aliniona mwaminifu,
akaniteua kwa kazi yake. 13 Ingawa wakati fulani
nilikuwa mwenye kukufuru, mtesaji na mwenye jeuri,
lakini nilipata rehema kwa sababu nilitenda hivyo kwa
kutojua na kutoamini kwangu. 14 Neema ya Bwana
wetu ilimiminwa juu yangu kwa wingi, ikiambatana
na imani na upendo ulio katika Al-Masihi Isa. 15
Msemo huu ni wa kweli na unaostahili kukubalika,
usemao kwamba: Al-Masihi Isa alikuja ulimwenguni
kuokoa wenye dhambi, ambao mimi ndiye niliye
mbaya kuliko wote. 16 Lakini kwa sababu hiyo nilipata
rehema, ili katika mimi, niliyekuwa mwenye dhambi
kuliko wote, Al-Masihi Isa apate kuonesha uvumilivu
wake usio na kikomo, ili niwe kielelezo kwa wale
watakaomwamini na wapate uzima wa milele. **(aiōnios
g166)** 17 Basi Mfalme wa milele, asiye na mwisho,
asiyeonekana, aliye Mungu pekee, apewe heshima
na utukufu milele na milele. Amen. **(aiōn g165)** 18
Mwanangu Timotheo, ninakupa agizo hili, kwa kadiri
ya maneno ya unabii yaliyosemwa kukuhusu, ili kwa
kuyafuata upate kupigana vita vizuri, 19 ukiishikilia
imani na dhamiri safi, ambazo wengine wamevikataa,
na hivyo wakaangamia kwa habari ya imani yao.
20 Miongoni mwao wako Himenayo na Iskanda,
ambao nimemkabidhi Shetani ili wafundishwe wasije
wakakufuru.

2 Awali ya yote, nasihi kwamba dua, sala, maombezi
na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote:
2 kwa ajili ya wafalme na wale wote walio katika
mamlaka, ili tupate kuishi kwa amani na utulivu,
katika uchaji wote wa Mungu na utakatifu. 3 Jambo
hili ni jema, tena linapendeza machoni pa Mungu
Mwokozi wetu, 4 anayetaka watu wote waokolewe
na wafikie kuijua kweli. 5 Kwa maana kuna Mungu
mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na
wanadamu, yaani mwanadamu Al-Masihi Isa, 6
aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wanadamu
wote: jambo hili lilishuhudiwa kwa wakati wake ufaao.
7 Nami kwa kusudi hili nimewekwa niwe mhubiri na
mtume (nasema kweli katika Al-Masihi wala sisemi
uongo), mwalimu wa watu wa Mataifa katika imani na
kweli. 8 Nataka kila mahali wanaume wasali wakiinua
mikono mitakatifu pasipo hasira wala kugombana. 9
Vivyo hivyo nataka wanawake wajipambe kwa adabu
na kwa heshima katika mavazi yanayostahili, si kwa
kusuka nywele, kuvalia dhahabu, lulu au mavazi ya
gharama kubwa, 10 bali kwa matendo mazuri kama
iwapasavyo wanawake wanaokiri kuwa wanamcha
Mungu. 11 Mwanamke na ajifunze katika utulivu na
utiifu wote. 12 Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha
au kuwa na mamlaka juu ya mwanaume. Mwanamke
inampasa kukaa kimya. 13 Kwa maana Adamu
aliumbwa kwanza, kisha Hawa. 14 Wala si Adamu
aliyedanganywa, bali ni mwanamke aliyedanganywa
akawa mkosaji. 15 Lakini mwanamke ataokolewa
kwa kuzaa kwake, wakiendelea kudumu katika imani,
upendo na utakatifu, pamoja na kuwa na kiasi.

3 Hili ni neno la kuaminiwa, kwamba mtu akitamani
kuwa mwangalizi wa kundi la waumini, atamani kazi
nzuri. 2 Basi, imempasa mwangalizi awe mtu asiye
na lawama, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi,
anayejitawala, anayeheshimika, mkarimu, ajuaye

kufundisha, 3 asiwe mlevi, wala mkali bali awe
mpole, asiwe mgomvi wala mpenda fedha. 4 Lazima
aweze kuisimamia nyumba yake mwenyewe vizuri na
kuhakikisha kwamba watoto wake wanamtii na kuwa
na heshima kwa kila njia. 5 (Kwa maana kama mtu
hajui jinsi ya kusimamia nyumba yake mwenyewe,
atawezaje kuliangalia kundi la waumini la Mungu?)
6 Asiwe mtu aliyeongoka karibuni asije akajivuna
na kuangukia kwenye hukumu ile ile ya ibilisi. 7
Inampasa pia awe na sifa njema kwa watu walio nje,
ili asije akalaumiwa na kuanguka kwenye mtego wa
ibilisi. 8 Vivyo hivyo, mashemasi nao wawe watu
wanaostahili heshima, wasiwe wenye kauli mbili au
wenye kujifurahisha kwa mvinyo, wala wanaotamani
faida isiyo halali. 9 Inawapasa kushikamana sana
na ile siri ya imani kwa dhamiri safi. 10 Ni lazima
wapimwe kwanza; kisha kama hakuna neno dhidi yao,
basi na waruhusiwe kuhudumu kama mashemasi. 11
Vivyo hivyo, wake zao wawe wanawake wanaostahili
heshima, wasio wasingiziaji, bali wawe na kiasi na
waaminifu katika kila jambo. 12 Shemasi awe mume
wa mke mmoja, na aweze kusimamia watoto wake na
watu wa nyumbani mwake vyema. 13 Wale ambao
wamehudumu vyema katika huduma ya ushemasi
hujipatia msimamo bora na ujasiri mkubwa katika
imani yao ndani ya Al-Masihi Isa. 14 Ingawa ninatarajia
kuja kwako hivi karibuni, ninakuandikia maagizo haya
sasa ili, 15 nikikawia, utajua jinsi iwapasavyo watu
kuenenda katika nyumba ya Mungu, ambayo ndiyo
jumuiya ya waumini ya Mungu aliye hai, iliyo nguzo na
msingi wa kweli. 16 Bila shaka yoyote, siri ya utauwa
ni kubwa: Alidhihirishwa katika mwili, akathibitishwa
kuwa na haki katika Roho wa Mungu, akaonekana
na malaika, akahubiriwa miongoni mwa mataifa,
akaaminiwa ulimwenguni, akachukuliwa juu katika
utukufu.

**4** Roho wa Mungu asema waziwazi kwamba katika
siku za mwisho baadhi ya watu wataiacha imani
na kufuata roho zidanganyazo na mafundisho ya
mashetani. 2 Mafundisho kama hayo huja kupitia kwa
waongo ambao ni wanafiki, hali dhamiri zao zikiungua
kwa kuchomwa moto. 3 Wao huwakataza watu
wasioe na kuwaagiza wajiepushe na vyakula fulani,
ambavyo Mungu aliviumba ili vipokewe kwa shukrani
na wale wanaoamini na kuijua kweli. 4 Kwa maana
kila kitu alichokiumba Mungu ni chema, wala hakuna
kitu chochote cha kukataliwa kama kikipokewa kwa
shukrani, 5 kwa sababu kimetakaswa kwa neno la
Mungu na kwa kuomba. 6 Ukiwakumbusha ndugu
mambo haya, utakuwa mtumishi mwema wa Al-
Masihi Isa, uliyelelewa katika kweli ya imani na yale
mafundisho mazuri uliyoyafuata. 7 Usijishughulishe
kamwe na hadithi za kipagani na masimulizi ya
uongo ya wanawake wazee; badala yake, jizoeze
kuwa mtauwa. 8 Kwa maana mazoezi ya mwili yana
faida kwa sehemu, lakini utauwa una faida katika
mambo yote, yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa
na ya ule ujao. 9 Hili ni neno la kuaminiwa tena
lastahili kukubaliwa kabisa. 10 Nasi kwa ajili ya
hili tunajitaabisha na kujitahidi, kwamba tumeweka
tumaini letu kwa Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi
wa watu wote, hasa wale waaminio. 11 Mambo haya
yaagize na kuyafundisha. 12 Mtu yeyote asikudharau
kwa kuwa wewe ni kijana, bali uwe kielelezo kizuri
kwa waumini katika usemi, mwenendo, upendo, imani
na usafi. 13 Fanya bidii kusoma Maandiko hadharani,
kuhubiri na kufundisha, hadi nitakapokuja. 14 Usiache
kutumia kipawa kilicho ndani yako, ambacho ulipewa
kwa neno la unabii wakati wazee walikuwekea mikono.
15 Uwe na bidii katika mambo haya; ujitolee kwa ajili
ya mambo haya kikamilifu, ili kila mtu aone kuendelea
kwako. 16 Jilinde sana nafsi yako na mafundisho
yako. Dumu katika hayo, kwa maana kwa kufanya
hivyo, utajiokoa wewe mwenyewe pamoja na wale
wanaokusikia.

**5** Usimkemee mzee kwa ukali bali umshawishi
kama vile angekuwa ni baba yako. Uwatendee
vijana kama vile ndugu zako; 2 nao wanawake
wazee uwatendee kama mama zako, na wanawake
vijana kama dada zako, katika usafi wote. 3
Waheshimu wanawake wajane ambao ni wajane
kweli kweli. 4 Kama mjane ana watoto ama wajukuu,
hawa inawapasa awali ya yote wajifunze kutimiza
wajibu wao wa kumcha Mungu katika matendo kwa
kuwatunza wale wa jamaa zao wenyewe, na hivyo
wawarudishie wema waliowatendea wazazi wao,
kwa kuwa hivi ndivyo inavyompendeza Mungu. 5
Mwanamke ambaye ni mjane kweli kweli, yaani
yeye aliyebaki peke yake huweka tumaini lake kwa
Mungu naye hudumu katika maombi usiku na mchana
akimwomba Mungu ili amsaidie. 6 Lakini mjane aishiye
kwa anasa amekufa, ingawa anaishi. 7 Wape watu

maagizo haya pia, ili asiwepo yeyote wa kulaumiwa.
8 Kama mtu hawatunzi wale wa jamaa yake, hasa
wale wa nyumbani mwake mwenyewe, ameikana
imani, tena ni mbaya kuliko yeye asiyeamini. 9 Mjane
yeyote asiwekwe kwenye orodha ya wajane isipokuwa
awe ametimiza umri wa miaka sitini, na amekuwa
mke wa mume mmoja; 10 awe ameshuhudiwa
kwa matendo yake mema, aliyewalea watoto wake
vizuri, aliye mkarimu, aliyewanawisha watakatifu
miguu, aliyewasaidia wenye shida na aliyejitolea kwa
ajili ya matendo mema ya kila namna. 11 Lakini
kwa habari za wajane vijana usiwaweke kwenye
orodha hiyo, maana tamaa zao za kimaumbile zikizidi
kule kujitoa kwao kwa Al-Masihi, watataka kuolewa
tena. 12 Nao kwa njia hiyo watajiletea hukumu kwa
kukiuka ahadi yao ya kwanza. 13 Zaidi ya hayo,
wajane kama hao huwa na tabia ya uvivu wakizurura
nyumba kwa nyumba, wala hawawi wavivu tu, bali
pia huwa wasengenyaji, wajiingizao katika mambo
yasiyowahusu na kusema mambo yasiyowapasa
kusema. 14 Hivyo nawashauri wajane vijana waolewe,
wazae watoto na wasimamie nyumba zao, wasije
wakampa adui nafasi ya kutushutumu. 15 Kwa
maana kwa kweli wajane wengine wamepotoka ili
kumfuata Shetani. 16 Lakini kama mwanamke yeyote
aaminiye ana wajane katika jamaa yake, inampasa
awasaidie wala si kuwaacha wakililemea kundi la
waumini, ili lile kundi liweze kuwasaidia wale ambao
ni wajane kweli kweli. 17 Wazee wa kundi la waumini
wanaoongoza shughuli za kundi hilo vizuri wanastahili
heshima mara mbili, hasa wale ambao kazi yao ni
kuhubiri na kufundisha. 18 Kwa maana Maandiko
husema, "Usimfunge maksai kinywa apurapo nafaka,"
tena, "Mfanyakazi anastahili mshahara wake." 19
Usiendekeze mashtaka dhidi ya mzee isipokuwa yawe
yameletwa na mashahidi wawili au watatu. 20 Wale
wanaodumu katika dhambi uwakemee hadharani,
ili wengine wapate kuogopa. 21 Ninakuagiza mbele
za Mungu na mbele za Al-Masihi Isa na mbele za
malaika wateule, shika maagizo haya pasipo ubaguzi
wala upendeleo. 22 Usiwe na haraka kumwekea
mtu mikono wala usishiriki dhambi za watu wengine.
Jilinde nafsi yako uwe safi. 23 Acha kunywa maji
peke yake, tumia divai kidogo kwa sababu ya tumbo
lako na maumivu yako ya mara kwa mara. 24 Dhambi
za watu wengine ni dhahiri nazo zinawatangulia
kwenda hukumuni; na dhambi za watu wengine
zinawafuata nyuma yao. 25 Vivyo hivyo, matendo
mema yako dhahiri, na hata yale yasiyo dhahiri
hayawezi kufichika.

6 Wale wote walio chini ya nira ya utumwa inawapasa
kuwahesabu mabwana zao kuwa wanastahili
heshima yote, ili jina la Mungu lisitukanwe wala
mafundisho yetu. 2 Wale watumwa ambao wana
mabwana waaminio, haiwapasi kupunguza heshima
yao kwa sababu wao ni ndugu. Badala yake,
wawatumikie hata vizuri zaidi, kwa sababu wale
wanaonufaika na huduma yao ni waumini, ambao ni
wapendwa wao. Fundisha mambo haya na uwahimize
kuyafuata. 3 Ikiwa mtu yeyote atafundisha mafundisho
mapotovu wala hakubaliani na mafundisho manyofu
ya Bwana wetu Isa Al-Masihi na yale ya utauwa,
4 huyo anajivuna wala hajui kitu chochote. Yeye
amejaa tamaa ya mabishano na ugomvi kuhusu
maneno ambavyo matokeo yake ni wivu na mapigano,
maneno ya ukorofi, shuku mbaya, 5 na kuzozana
kusikokoma kati ya watu waliharibika akili zao,
walioikosa kweli, na ambao hudhani kwamba utauwa
ni njia ya kupata faida. 6 Lakini utauwa na kuridhika
ni faida kubwa. 7 Kwa kuwa hatukuja humu duniani
na kitu chochote, wala hatuwezi kutoka humu na kitu.
8 Lakini kama tuna chakula na mavazi, tutaridhika
navyo. 9 Lakini wale watu wanaotamani kuwa na
mali kwa haraka huanguka kwenye majaribu, na
wamenaswa na tamaa nyingi za kipumbavu zenye
kudhuru, zinazowazamisha watu katika uharibifu na
maangamizi. 10 Kwa maana kupenda fedha ndiyo
shina moja la maovu ya kila namna. Baadhi ya watu
wakitamani fedha, wameiacha imani na kujichoma
wenyewe kwa maumivu mengi. 11 Lakini wewe,
mtu wa Mungu, yakimbie mambo haya yote. Fuata
haki, utauwa, imani, upendo, saburi na upole. 12
Pigana vile vita vizuri vya imani. Shika uzima wa
milele ambao ndio ulioitiwa ulipokiri ule ukiri mzuri
mbele ya mashahidi wengi. **(aiōnios g166)** 13 Nakuagiza
mbele za Mungu avipaye vitu vyote uhai, na mbele
za Al-Masihi Isa, ambaye alipokuwa anashuhudia
mbele ya Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri, 14 uishike
amri hii bila dosari wala lawama hadi kufunuliwa
kwake Bwana wetu Isa Al-Masihi; 15 ambako Mungu
atadhihirisha kwa wakati wake mwenyewe: Mungu
ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa

wafalme, na Bwana wa mabwana, 16 yeye pekee
aishiye milele, anayedumu katika nuru isiyoweza
kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona
wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una
yeye milele. Amen. **(aiōnios g166)** 17 Waagize wale
ambao ni matajiri wa ulimwengu huu waache kujivuna,
wala wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si
ya hakika, bali waweke tumaini lao katika Mungu
ambaye hutupatia vitu vyote kwa wingi ili tuvifurahie.
**(aiōn g165)** 18 Waagize watende mema, wawe matajiri
katika matendo mema, pia wawe wakarimu na walio
tayari kushiriki mali yao na wengine. 19 Kwa njia
hii watajiwekea hazina kama msingi kwa ajili ya
wakati ujao na hivyo watajipatia uzima, yaani ule
uzima ambao ni wa kweli. 20 Timotheo, linda kile
kilichowekwa amana kwako. Epuka majadiliano yasiyo
ya utauwa na mabishano ambayo kwa uongo huitwa
elimu, 21 ambayo wengine kwa kujidai kuwa nayo
wameiacha imani. Neema iwe nanyi. Amen.

# 2 Timotheo

1 Paulo mtume wa Al-Masihi Isa kwa mapenzi ya
Mungu, kulingana na ile ahadi ya uzima ulio
ndani ya Al-Masihi Isa. 2 Kwa Timotheo, mwanangu
mpendwa. 3 Ninamshukuru Mungu, ninayemtumikia
kwa dhamiri safi kama walivyofanya baba zangu,
ninapokukumbuka usiku na mchana katika maombi
yangu. 4 Nikiyakumbuka machozi yako, ninatamani
sana kukuona ili nipate kujawa na furaha. 5 Nimekuwa
nikiikumbuka imani yako ya kweli, waliokuwa nayo bibi
yako Loisi na mama yako Eunike, na ninasadiki sasa
wewe pia unayo. 6 Kwa sababu hii nakukumbusha
uchochee ile karama ya Mungu iliyowekwa ndani
yako nilipokuwekea mikono yangu. 7 Maana Mungu
hakutupatia roho ya woga, bali roho ya nguvu, ya
upendo na ya moyo wa kiasi. 8 Kwa hiyo usione haya
kushuhudia kuhusu Bwana wetu, wala usinionee
haya mimi niliye mfungwa kwa ajili yake. Bali uishiriki
pamoja nami taabu ya Injili, kwa kadiri ya nguvu ya
Mungu, 9 ambaye alituokoa na kutuita katika mwito
mtakatifu: si kwa kadiri ya matendo yetu mema, bali
kwa sababu ya kusudi lake mwenyewe na neema
yake. Neema hii tulipewa katika Al-Masihi Isa tangu
milele. **(aiōnios g166)** 10 Lakini sasa imefunuliwa kwa
kudhihirishwa kwake Mwokozi wetu, Al-Masihi Isa,
ambaye amebatilisha mauti na kuleta uzima na
kutokufa kupitia kwa Injili. 11 Nami nimewekwa kuwa
mhubiri, mtume na mwalimu wa Injili hii. 12 Hii ndiyo
sababu ninateseka namna hii, lakini sioni haya kwa
maana ninamjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya
kuwa anaweza kukilinda kile nilichokiweka amana
kwake hadi siku ile. 13 Shika kwa uthabiti kielelezo
cha mafundisho yenye uzima uliyoyasikia kwangu,
pamoja na imani na upendo katika Al-Masihi Isa.
14 Ilinde ile amana uliyokabidhiwa kwa Roho wa
Mungu akaaye ndani yetu. 15 Unajua ya kuwa watu
wote katika jimbo la Asia wameniacha, miongoni
mwao wamo Filego na Hermogene. 16 Bwana Isa
akawahurumie watu wa nyumbani mwa Onesiforo,
kwa sababu aliniburudisha mara kwa mara, wala
hakuionea aibu minyororo yangu. 17 Badala yake,
alipokuwa Rumi alinitafuta kwa bidii hadi akanipata.
18 Bwana Isa na amjalie kupata rehema zake siku ile!
Nawe unajua vyema jinsi alivyonisaidia huko Efeso.

2 Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema
iliyo ndani ya Al-Masihi Isa. 2 Nayo mambo
yale uliyonisikia nikiyasema mbele ya mashahidi
wengi, uwakabidhi watu waaminifu watakaoweza
kuwafundisha watu wengine vilevile. 3 Vumilia
taabu pamoja nasi kama askari mwema wa Al-
Masihi Isa. 4 Hakuna askari yeyote ambaye akiwa
vitani hujishughulisha na mambo ya kawaida ya
maisha haya kwa sababu nia yake ni kumpendeza
yule aliyemwandika awe askari. 5 Vivyo hivyo,
mwanariadha hawezi kupewa tuzo ya ushindi
asiposhindana kulingana na kanuni za mashindano.
6 Mkulima mwenye bidii ya kazi ndiye anayestahili
kuwa wa kwanza kupata fungu la mavuno. 7 Fikiri
sana kuhusu haya nisemayo, kwa maana Mwenyezi
Mungu atakupa ufahamu katika mambo haya yote.
8 Mkumbuke Isa Al-Masihi aliyefufuliwa kutoka kwa
wafu, yeye aliye wa uzao wa Daudi. Hii ndiyo Injili
yangu, 9 ambayo kwayo ninateseka hata kufikia
hatua ya kufungwa minyororo kama mhalifu. Lakini
neno la Mungu halifungwi. 10 Kwa hiyo ninavumilia
mambo yote kwa ajili ya wateule wa Mungu, kusudi
wao nao wapate wokovu ulio katika Al-Masihi Isa,
pamoja na utukufu wa milele. **(aiōnios g166)** 11 Hili ni
neno la kuaminiwa: Kama tumekufa pamoja naye,
tutaishi pia pamoja naye. 12 Kama tukistahimili,
pia tutatawala pamoja naye. Kama tukimkana, naye
atatukana. 13 Tusipoaminika, yeye hudumu akiwa
mwaminifu, kwa maana hawezi kujikana mwenyewe.
14 Endelea kuwakumbusha mambo haya, ukiwaonya
mbele za Mungu waache kushindana kwa maneno
ambayo hayana faida yoyote, bali huwaangamiza
tu wale wanaoyasikia. 15 Jitahidi kujionesha kwa
Mungu kuwa umekubaliwa naye, mtendakazi asiye
na sababu ya kuona aibu, ukilitumia kwa usahihi
neno la kweli. 16 Jiepushe na maneno machafu
yasiyo ya utauwa, kwa maana hayo huzidi kuwatosa
watu katika kutomcha Mungu. 17 Mafundisho yao
yataenea kama kidonda kisichopona. Miongoni mwao
wamo Himenayo na Fileto, 18 ambao wameiacha
kweli, wakisema kwamba ufufuo wa wafu umekwisha
kupita, nao hupindua imani ya baadhi ya watu. 19
Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama,
ukiwa na muhuri wenye maandishi haya: “Mwenyezi
Mungu anawajua walio wake”; tena, “Kila alitajaye
jina la Mwenyezi Mungu na auache uovu.” 20

Katika nyumba kubwa si kwamba kuna vyombo vya
dhahabu na fedha tu, bali pia vimo vyombo vya miti
na vya udongo; vingine kwa matumizi maalum, na
vingine kwa matumizi ya kawaida. 21 Basi ikiwa
mtu amejitakasa na kujitenga na hayo niliyoyataja,
atakuwa chombo maalum, kilichotengwa na ambacho
kinamfaa mwenye nyumba, kimeandaliwa tayari kwa
kila kazi njema. 22 Zikimbie tamaa mbaya za ujana,
ufuate haki, imani, upendo na amani pamoja na wale
wamwitao Bwana Isa kwa moyo safi. 23 Jiepushe na
mabishano ya kipumbavu na yasiyo na maana, kwa
kuwa unajua hayo huzaa magomvi. 24 Tena haimpasi
mtumishi wa Bwana Isa kuwa mgomvi, bali inampasa
awe mwema kwa kila mtu, awezaye kufundisha, tena
mvumilivu. 25 Inampasa kuwaonya kwa upole wale
wanaopingana naye, kwa matumaini kwamba Mungu
atawajalia kutubu na kuijua kweli, 26 ili fahamu zao
ziwarudie tena, nao waponyoke katika mtego wa ibilisi
ambaye amewateka wapate kufanya mapenzi yake.

3 Lakini yakupasa ufahamu jambo hili: kwamba siku
za mwisho kutakuwa na nyakati za hatari. 2 Kwa
maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe,
wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi,
wenye kumkufuru Mungu, wasiotii wazazi wao, wasio
na shukrani, wasio watakatifu, 3 wasio na upendo,
wasiopenda kupatanishwa, wasingiziaji, wasiozuia
tamaa zao, wakatili, wasiopenda mema, 4 wasaliti,
wakaidi, waliojaa majivuno, wanaopenda anasa kuliko
kumpenda Mungu: 5 wakiwa na mfano wa utauwa
kwa nje, lakini wakizikana nguvu za Mungu. Jiepushe
na watu kama hao. 6 Miongoni mwao wamo wale
wajiingizao katika nyumba za watu na kuwachukua
mateka wanawake wajinga, waliolemewa na dhambi
zao na kuyumbishwa na aina zote za tamaa mbaya.
7 Hawa hujifunza siku zote, lakini kamwe hawawezi
kuufikia ujuzi wa kweli. 8 Kama vile Yane na Yambre
walivyopingana na Musa, vivyo hivyo watu hawa
hupingana na kweli. Hawa ni watu wenye akili
zilizopotoka, ambao wamekataliwa kwa mambo ya
imani. 9 Lakini hawataendelea sana, kwa sababu
upumbavu wao utakuwa dhahiri kwa watu wote,
kama vile upumbavu wa hao watu wawili ulivyokuwa
dhahiri. 10 Lakini wewe umeyajua mafundisho yangu,
mwenendo, makusudi, imani, uvumilivu, upendo,
ustahimilivu, 11 mateso na taabu, yaani mambo yote
yaliyonipata huko Antiokia, Ikonio na Listra, mateso
yote niliyostahimili, lakini Bwana Isa aliniokoa katika
hayo yote. 12 Naam, yeyote anayetaka kuishi maisha
ya utauwa ndani ya Al-Masihi Isa atateswa. 13 Lakini
watu waovu na wadanganyaji watazidi kuwa waovu,
wakidanganya na kudanganyika. 14 Bali wewe,
udumu katika yale uliyojifunza na kuyaamini kwa
uthabiti, ukitambua ya kuwa ulijifunza hayo kutoka
kwa nani, 15 na jinsi tangu utoto umeyajua Maandiko
Matakatifu, ambayo yanaweza kukuhekimisha upate
wokovu kupitia kwa imani katika Al-Masihi Isa. 16
Maandiko yote yamevuviwa na Mungu, na yafaa kwa
mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa
kuwaongoza na kwa kuwafundisha katika haki, 17 ili
mtu wa Mungu awe amekamilishwa, apate kutenda
kila kazi njema.

4 Nakuagiza mbele za Mungu na mbele za Al-
Masihi Isa, atakayewahukumu watu walio hai na
waliokufa wakati wa kuja kwake na ufalme wake,
kwamba: 2 Hubiri Neno; kuwa tayari wakati ufaao
na wakati usiofaa; karipia, kemea na utie moyo
kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri. 3
Maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali
mafundisho yenye uzima. Badala yake, ili kutimiza
tamaa zao wenyewe, watajikusanyia idadi kubwa ya
walimu watakaowaambia yale masikio yao yanatamani
kusikia. 4 Watakataa kusikiliza kweli na kuzigeukia
hadithi za uongo. 5 Bali wewe, vumilia mateso,
fanya kazi ya mhubiri wa Injili, timiza wajibu wote
wa huduma yako. 6 Kwa maana mimi sasa ni tayari
kumiminwa kama sadaka ya kinywaji, nayo saa
yangu ya kuondoka imetimia. 7 Nimevipiga vita vizuri,
mashindano nimeyamaliza, imani nimeilinda. 8 Sasa
nimewekewa taji la haki ambalo Bwana, Mwamuzi wa
haki, atanitunukia siku ile: wala si mimi tu, bali pia
wote ambao wamengoja kwa shauku kudhihirishwa
kwake. 9 Jitahidi kuja kwangu upesi 10 kwa sababu
Dema, kwa kuupenda ulimwengu, ameniacha na
ameenda Thesalonike. Kreske ameenda Galatia,
na Tito ameenda Dalmatia. **(aiōn g165)** 11 Ni Luka
pekee aliye hapa nami. Mtafute Marko uje naye,
kwa sababu ananifaa sana katika huduma yangu.
12 Nimemtuma Tikiko huko Efeso. 13 Utakapokuja,
niletee lile joho nililoliacha kwa Karpo huko Troa, na
vile vitabu vyangu, hasa vile vya ngozi. 14 Iskanda
yule mfua chuma alinitendea ubaya mkubwa. Bwana
Isa atamlipa kwa ajili ya yale aliyotenda. 15 Wewe

pia ujihadhari naye kwa sababu aliyapinga maneno
yetu vikali. **16** Katika utetezi wangu wa mara ya
kwanza, hakuna hata mmoja aliyeniunga mkono,
bali kila mmoja aliniacha. Naomba wasihesabiwe
hatia kwa jambo hilo. **17** Lakini Bwana Isa alisimama
upande wangu akanitia nguvu, ili kupitia kwangu lile
Neno lihubiriwe kwa ukamilifu, watu wote Mataifa
wapate kulisikia. Mimi niliokolewa kutoka kinywa cha
simba. **18** Bwana Isa ataniokoa katika kila shambulio
baya na kunileta salama katika ufalme wake wa
mbinguni. Atukuzwe milele na milele. Amen. **(aiōn g165)**
**19** Wasalimu Prisila na Akila, na wote wa nyumbani
mwa Onesiforo. **20** Erasto alibaki Korintho, nami
nikamwacha Trofimo huko Mileto akiwa mgonjwa. **21**
Jitahidi ufike huku kabla ya majira ya baridi. Eubulo
anakusalimu, vivyo hivyo Pude, Lino, Klaudia na
ndugu wote. **22** Bwana Isa awe pamoja na roho yako.
Neema iwe pamoja nanyi.

# Tito

**1** Paulo, mtumishi wa Mungu na mtume wa Isa Al-
Masihi kwa ajili ya imani ya wateule wa Mungu
na kuijua kweli iletayo utauwa: **2** imani na ujuzi
katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu,
asiyesema uongo, aliahidi hata kabla ya kuwekwa
misingi ya ulimwengu, **(aiōnios g166)** **3** naye kwa wakati
wake aliouweka alilidhihirisha neno lake kupitia kwa
mahubiri ambayo mimi nimewekewa amana kwa amri
ya Mungu Mwokozi wetu. **4** Kwa Tito, mwanangu
hasa katika imani tunayoshiriki sote. **5** Sababu yangu
ya kukuacha huko Krete ni ili uweke utaratibu mambo
yale yaliyosalia na kuwateua wazee wa kundi la
waumini katika kila mji, kama nilivyokuagiza. **6**
Mzee wa kundi la waumini asiwe na lawama, awe
mume wa mke mmoja, mtu ambaye watoto wake
ni waumini, wala hawashtakiwi kwa ufisadi. **7** Kwa
kuwa mwangalizi wa kundi ni wakili wa Mungu,
imempasa kuwa mtu asiye na lawama, asiwe mwenye
majivuno au mwepesi wa hasira, wala mlevi, wala
asiwe mtu mwenye tamaa ya mapato yasiyo ya halali.
**8** Bali awe mkarimu, anayependa mema, mwenye
kiasi, mwenye haki, mwadilifu, mnyofu, mtakatifu
na mwenye kuitawala nafsi yake. **9** Lazima alishike
kwa uthabiti lile neno la imani kama lilivyofundishwa,
ili aweze kuwatia moyo wengine kwa mafundisho
yenye uzima na kuwakanusha wale wanaopingana
nayo. **10** Kwa maana wako wengi wasiotii, wenye
maneno yasiyo na maana, hasa wale wa kikundi cha
tohara. **11** Hao ni lazima wanyamazishwe, kwa sababu
wanaharibu watu wa nyumba nzima wakifundisha
mambo yasiyowapasa kufundisha. Wanafanya hivyo
kwa ajili ya kujipatia mapato ya udanganyifu. **12**
Hata mmoja wa manabii wao mwenyewe amesema,
“Wakrete ni waongo siku zote, wanyama wabaya,
walafi, wavivu.” **13** Ushuhuda huu ni kweli. Kwa hiyo,
uwakemee kwa ukali wapate kuwa wazima katika
imani, **14** ili wasiendelee kuangalia hadithi za Kiyahudi
au maagizo ya wale watu wanaoikataa kweli. **15** Kwa
wale walio safi, kila kitu ni safi kwao. Lakini kwa wale
waliopotoka na wasioamini, hakuna chochote kilicho
safi. Kwa kweli nia zao na dhamiri zao zimepotoka.
**16** Wanadai kumjua Mungu, lakini kwa matendo yao
wanamkana. Hao watu ni chukizo, wasiotii, wasiofaa
kwa jambo lolote jema.

**2** Bali wewe fundisha yale yaliyo sahihi kulingana
na mafundisho ya kweli. **2** Wafundishe wazee
kuwa na kiasi, wastahivu, wenye busara na wanyofu
katika imani, upendo na saburi. **3** Vivyo hivyo,
wafundishe wanawake wazee kuwa na mwenendo
wa utakatifu, wala wasiwe wasingiziaji au walevi,
bali wafundishe yale yaliyo mema, **4** ili waweze
kuwafundisha wanawake vijana kuwa na kiasi,
wawapende waume zao na kuwapenda watoto wao,
**5** wawe waaminifu, watakatifu, wakitunza vyema
nyumba zao, wema, watiifu kwa waume zao, ili mtu
yeyote asije akalikufuru neno la Mungu. **6** Vivyo
hivyo, himiza vijana wawe na kiasi. **7** Katika kila
jambo uwe kielelezo kwa kutenda mema. Katika
mafundisho yako uoneshe uadilifu, utaratibu, **8** na
usemi sahihi usio na lawama, ili wanaokupinga
watahayari, wakose neno lolote baya la kusema
kutuhusu. **9** Wafundishe watumwa kuwatii mabwana
zao katika kila jambo, wakijitahidi kuwapendeza wala
wasijibizane nao, **10** wala wasiwaibie, bali waoneshe
kuwa wanaweza kuaminika kabisa, ili kwa kila namna
wayafanye mafundisho ya Mungu Mwokozi wetu
yawe ya kuvutia. **11** Kwa maana neema ya Mungu
ambayo inawaokoa wanadamu wote imefunuliwa.
**12** Nayo inatufundisha kukataa ubaya na tamaa za
kidunia, ili tupate kuishi maisha ya kiasi, ya haki na
ya utaua katika ulimwengu huu wa sasa, **(aiōn g165)** **13**
huku tukilitazamia tumaini lenye baraka na ufunuo wa
utukufu wa Mungu wetu Mkuu, aliye Mwokozi wetu
Isa Al-Masihi. **14** Ndiye alijitoa nafsi yake kwa ajili
yetu, ili atukomboe kutoka uovu wote na kujisafishia
watu kuwa mali yake Mwenyewe, yaani wale walio na
juhudi katika kutenda mema. **15** Basi wewe fundisha
mambo haya. Himiza na kukaripia kwa mamlaka yote.
Usiruhusu mtu yeyote akudharau.

**3** Wakumbushe watu kunyenyekea kwa watawala
na kwa wenye mamlaka, na kutii, wakiwa tayari
kutenda kila lililo jema, **2** wasimnenee mtu yeyote
mabaya, wasiwe wagomvi bali wawe wema, wakiwa
wapole kwa watu wote. **3** Maana sisi wenyewe wakati
fulani tulikuwa wajinga, wasiotii, tukiwa watumwa
wa tamaa mbaya na anasa za kila aina. Tuliishi
katika uovu na wivu, tukichukiwa na kuchukiana
sisi kwa sisi. **4** Lakini wema na upendo wa Mungu
Mwokozi wetu ulipofunuliwa, **5** alituokoa, si kwa
sababu ya matendo ya haki tuliyotenda, bali kwa

sababu ya rehema zake. Alituokoa kwa kutuosha
kwa kuzaliwa mara ya pili na kwa kufanywa wapya
kupitia kwa Roho Mtakatifu wa Mungu, **6** ambaye
Mungu alitumiminia kwa wingi kupitia kwa Isa Al-
Masihi Mwokozi wetu, **7** ili, tukiisha kuhesabiwa haki
kwa neema yake, tupate kuwa warithi tukiwa na
tumaini la uzima wa milele. **(aiōnios g166)** **8** Hili ni
neno la kuaminiwa. Nami nataka uyasisitize mambo
haya, ili wale ambao wamemwamini Mungu wapate
kuwa waangalifu kujitoa kwa ajili ya kutenda mema
wakati wote. Mambo haya ni mazuri tena ya manufaa
kwa kila mtu. **9** Lakini jiepushe na maswali ya
kipuzi, mambo ya koo, mabishano na ugomvi kuhusu
sheria, kwa sababu hayana faida, tena ni ubatili. **10**
Mtu anayesababisha mafarakano, mwonye mara ya
kwanza, kisha mwonye mara ya pili. Baada ya hapo,
usihusike naye tena. **11** Kwa kuwa unajua kwamba
mtu kama huyo amepotoka na tena ni mwenye
dhambi. Yeye amejihukumu mwenyewe. **12** Mara
nitakapomtuma Artema au Tikiko kwako, jitahidi kuja
unione huko Nikopoli, kwa sababu nimeamua kukaa
huko wakati wa majira ya baridi. **13** Fanya kila uwezalo
uwasafirishe Zena yule mwanasheria na Apolo na
uhakikishe kwamba wana kila kitu wanachohitaji
katika safari yao. **14** Watu wetu hawana budi kujifunza
kutenda mema, ili waweze kuyakimu mahitaji ya kila
siku, wasije wakaishi maisha yasiyokuwa na matunda.
**15** Wote walio pamoja nami wanakusalimu. Wasalimu
wale wanaotupenda katika imani. Neema iwe nanyi
nyote. Amen.

# Filemoni

1 Paulo, mfungwa wa Al-Masihi Isa, pamoja na
Timotheo ndugu yetu. 2 kwa dada yetu mpendwa
Afia, kwa Arkipo askari mwenzetu na kwa kundi la
waumini wanaokutana nyumbani mwako. 3 Neema
na amani zitokazo kwa Mungu, Baba yetu, na kwa
Bwana wetu Isa Al-Masihi ziwe nanyi. 4 Siku zote
ninamshukuru Mungu wangu ninapokukumbuka katika
maombi yangu, 5 kwa sababu ninasikia kuhusu imani
yako katika Bwana Isa na upendo wako kwa watakatifu
wote. 6 Naomba utiwe nguvu katika kushiriki imani
yako na wengine, ili upate kuwa na ufahamu mkamilifu
wa kila kitu chema tunachoshiriki kwa ajili ya Al-Masihi.
7 Upendo wako umenifurahisha mno na kunitia moyo,
kwa sababu wewe ndugu, umeiburudisha mioyo ya
watakatifu. 8 Hata hivyo, ingawa katika Al-Masihi
ningekuwa na ujasiri wa kukuagiza yale yakupasayo
kutenda, 9 lakini ninakuomba kwa upendo. Mimi
Paulo, mzee na pia sasa nikiwa mfungwa wa Al-
Masihi Isa, 10 nakuomba kwa ajili ya mwanangu
Onesimo, aliyefanyika mwanangu nilipokuwa kwenye
minyororo. 11 Mwanzoni alikuwa hakufai, lakini sasa
anakufaa sana wewe na mimi pia. 12 Namtuma
kwako, yeye aliye moyo wangu hasa. 13 Ningependa
nikae naye ili ashike nafasi yako ya kunisaidia wakati
huu nikiwa kifungoni kwa ajili ya Injili. 14 Lakini
sikutaka kufanya lolote bila idhini yako, ili wema
wowote uufanyao usiwe wa lazima, bali wa hiari.
15 Huenda sababu ya Onesimo kutengwa nawe
kwa muda ni ili uwe naye daima, **(aiōnios g166)** 16
si kama mtumwa sasa, bali bora kuliko mtumwa,
kama ndugu mpendwa. Yeye ni mpendwa sana
kwangu na hata kwako zaidi, yeye kama mwanadamu
na kama ndugu katika Bwana Isa. 17 Hivyo kama
unanihesabu mimi kuwa mshirika nawe, mkaribishe
kama vile ungenikaribisha mimi mwenyewe. 18 Kama
amekukosea lolote au kama unamdai chochote,
nidai mimi. 19 Ni mimi Paulo, ninayeandika waraka
huu kwa mkono wangu mwenyewe. Nitakulipa hilo
deni. Kumbuka kwamba nakudai hata nafsi yako. 20
Ndugu yangu, natamani nipate faida kwako katika
Bwana Isa, yaani uniburudishe moyo wangu katika
Al-Masihi. 21 Huku nikiwa na hakika ya kutii kwako,
nakuandikia nikijua kwamba utafanya hata zaidi ya
yale ninayokuomba. 22 Jambo moja zaidi: Niandalie
chumba cha wageni, kwa kuwa nataraji kurudishwa
kwenu kama jibu la maombi yenu. 23 Epafra,
aliye mfungwa mwenzangu katika Al-Masihi Isa,
anakusalimu. 24 Vivyo hivyo Marko, Aristarko, Dema
na Luka, watendakazi wenzangu wanakusalimu. 25
Neema ya Bwana Isa Al-Masihi iwe pamoja na roho
zenu. Amen.

# Wahebrania

**1** Zamani, Mungu alisema na baba zetu kupitia kwa
manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, **2**
lakini katika siku hizi za mwisho anasema nasi kupitia
kwa Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi
wa vitu vyote, na ambaye kupitia kwake aliuumba
ulimwengu. **(aiōn g165)** **3** Mwana ni mng'ao wa utukufu
wa Mungu na mfano halisi wa nafsi yake, akivihifadhi
vitu vyote kwa neno lake lenye uweza. Baada ya
kufanya utakaso kwa ajili ya dhambi, aliketi mkono
wa kuume wa Aliye Mkuu huko mbinguni. **4** Kwa
hiyo alifanyika bora kuliko malaika, kama jina alilorithi
lilivyo bora kuliko lao. **5** Kwa maana ni kwa malaika
yupi Mungu aliwahi kusema, "Wewe ni Mwanangu;
leo mimi nimekuwa Baba yako"? Au tena, "Mimi
nitakuwa Baba yake, naye atakuwa Mwanangu"? **6**
Tena, Mungu amletapo mzaliwa wake wa kwanza
ulimwenguni, anasema, "Malaika wote wa Mungu na
wamsujudu." **7** Anaponena kuhusu malaika, anasema,
"Huwafanya malaika wake kuwa pepo, watumishi
wake kuwa miali ya moto." **8** Lakini kwa habari za
Mwana asema, "Kiti chako cha enzi, Ee Mungu,
kitadumu milele na milele, nayo haki itakuwa fimbo
ya utawala ya ufalme wako. **(aiōn g165)** **9** Umependa
haki na kuchukia uovu; kwa hiyo Mungu, Mungu
wako, amekuweka juu ya wenzako kwa kukupaka
mafuta ya furaha." **10** Pia asema, "Hapo mwanzo, Ee
Mwenyezi Mungu, uliweka misingi ya dunia, nazo
mbingu ni kazi ya mikono yako. **11** Hizo zitatoweka,
lakini wewe utadumu; zote zitachakaa kama vazi.
**12** Utazikunjakunja kama joho, nazo zitabadilishwa
kama vazi. Lakini wewe hubadiliki, nayo miaka yako
haikomi kamwe." **13** Je, ni kwa malaika yupi Mungu
aliwahi kusema, "Keti mkono wangu wa kuume, hadi
nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako"?
**14** Je, malaika wote si roho watumikao, waliotumwa
kuwahudumia wale watakaourithi wokovu?

**2** Kwa hiyo, imetupasa kuwa waangalifu sana kuhusu
kile tulichosikia, ili tusije tukakiacha. **2** Kwa kuwa
kama ujumbe ulionenwa na malaika ulikuwa imara,
na kila uasi na kutokutii kulipata adhabu ya haki, **3**
je, sisi tutapataje kupona kama tusipojali wokovu
mkuu namna hii? Wokovu huu, ambao mwanzo
ulitangazwa na Bwana Isa, ulithibitishwa kwetu na
wale waliomsikia. **4** Pia Mungu aliushuhudia kwa
ishara, maajabu, na kwa miujiza mbalimbali, na
karama za Roho wa Mungu alizozigawa kulingana na
mapenzi yake. **5** Mungu hakuuweka ulimwengu ujao
ambao tunanena habari zake chini ya malaika. **6** Lakini
kuna mahali mtu mmoja ameshuhudia, akisema:
"Mwanadamu ni kitu gani hata unamfikiria, binadamu
ni nani hata unamjali? **7** Umemfanya chini kidogo
kuliko malaika; ukamvika taji la utukufu na heshima, **8**
nawe umeweka vitu vyote chini ya miguu yake." Kwa
kuweka vitu vyote chini yake, Mungu hakuacha kitu
chochote ambacho hakukiweka chini ya mwanadamu.
Lakini kwa sasa, hatuoni kwamba kila kitu kiko chini
yake. **9** Lakini twamwona Isa, aliyefanywa chini
kidogo kuliko malaika, sasa akiwa amevikwa taji la
utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili
kwa neema ya Mungu apate kuonja mauti kwa ajili ya
kila mtu. **10** Ili kuwaleta wana wengi katika utukufu,
ilifaa kwamba Mungu, ambaye ni kwa ajili yake na
kupitia kwake kila kitu kimekuwepo, amkamilishe
mwanzilishi wa wokovu wao kupitia kwa mateso
yake. **11** Yeye awafanyaye watu kuwa watakatifu,
pamoja na hao ambao hufanywa watakatifu, wote
hutoka katika jamaa moja. Hivyo Isa haoni aibu
kuwaita ndugu zake. **12** Yeye anasema, "Nitalitangaza
jina lako kwa ndugu zangu; mbele ya kusanyiko
nitaimba sifa zako." **13** Tena, "Nitaweka tumaini
langu kwake." Tena anasema, "Niko hapa, pamoja
na watoto ambao Mungu amenipa." **14** Basi kwa
kuwa watoto wana mwili na damu, yeye pia alishiriki
katika ubinadamu wao, ili kwa kifo chake, apate
kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani
ibilisi, **15** na kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani
maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti. **16**
Kwa kuwa ni dhahiri kwamba hakuja kusaidia malaika,
bali uzao wa Ibrahimu. **17** Kwa sababu hii ilibidi
afanane na ndugu zake kwa kila hali, ili apate kuwa
Kuhani Mkuu mwenye huruma na mwaminifu katika
kumtumikia Mungu, ili pia apate kufanya upatanisho
kwa ajili ya dhambi za watu. **18** Kwa kuwa yeye
mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia
wale wanaojaribiwa.

**3** Kwa hiyo ndugu watakatifu, mnaoshiriki mwito
wa mbinguni, mtafakarini Isa, mtume na Kuhani
Mkuu wa ukiri wetu. **2** Alikuwa mwaminifu kwa
yeye aliyemteua, kama Musa alivyokuwa mwaminifu
katika nyumba yote ya Mungu. **3** Isa ameonekana

anastahili heshima kubwa kuliko Musa, kama vile
mjenzi wa nyumba alivyo wa heshima kubwa kuliko
nyumba yenyewe. 4 Kwa kuwa kila nyumba hujengwa
na mtu, lakini Mungu ni mjenzi wa kila kitu. 5
Musa, kama mtumishi, alikuwa mwaminifu katika
nyumba yote ya Mungu, akishuhudia kwa yale
Mungu angeyasema baadaye. 6 Lakini Al-Masihi ni
mwaminifu kama Mwana katika nyumba ya Mungu.
Sisi ndio nyumba yake, kama tutashikilia sana ujasiri
wetu na tumaini tunalojivunia. 7 Kwa hiyo, kama Roho
wa Mungu asemavyo: "Leo, mkiisikia sauti yake, 8
msiifanye mioyo yenu migumu, kama mlivyofanya
katika uasi, wakati ule wa kujaribiwa jangwani,
9 ambapo baba zenu walinijaribu na kunipima,
ingawa kwa miaka arobaini walikuwa wameyaona
matendo yangu. 10 Hiyo ndiyo sababu nilikasirikia
kizazi kile, nami nikasema, 'Siku zote mioyo yao
imepotoka, nao hawajazijua njia zangu.' 11 Hivyo
nikatangaza kwa kiapo katika hasira yangu, 'Kamwe
hawataingia rahani mwangu.'" 12 Ndugu zangu,
chungeni asiwepo miongoni mwenu mtu mwenye
moyo mwovu usioamini, unaojitenga na Mungu aliye
hai. 13 Lakini mtiane moyo mtu na mwenzake kila
siku, maadamu inaitwa "Leo", ili asiwepo hata mmoja
wenu mwenye kufanywa mgumu kwa udanganyifu
wa dhambi. 14 Kwa kuwa tumekuwa washiriki wa Al-
Masihi, tukishikamana tu kwa uthabiti na tumaini letu
la kwanza hadi mwisho. 15 Kama ilivyonenwa: "Leo,
mkiisikia sauti yake, msiifanye mioyo yenu migumu
kama mlivyofanya wakati wa kuasi." 16 Basi ni nani
waliosikia lakini bado wakaasi? Je, si wale wote
waliotoka Misri wakiongozwa na Musa? 17 Lakini
ni nani Mungu aliwakasirikia miaka arobaini? Je, si
wale waliofanya dhambi ambao miili yao ilianguka
jangwani? 18 Ni nani hao ambao Mungu aliapa
kuwa kamwe hawataingia rahani mwake isipokuwa
ni wale waliokataa kutii? 19 Hivyo tunaona kwamba
hawakuweza kuingia kwa sababu ya kutokuamini
kwao.

4 Kwa hiyo, kwa kuwa bado ahadi ya kuingia rahani
iko wazi, tujihadhari ili hata mmoja wenu asije
akaikosa. 2 Kwa maana sisi pia tumesikia Injili
iliyohubiriwa kwetu, kama nao walivyosikia; lakini
ujumbe ule waliousikia haukuwa na maana kwao,
kwa sababu wale waliousikia hawakuuchanganya na
imani. 3 Sasa sisi ambao tumeamini tunaingia katika
ile raha, kama vile Mungu alivyosema, "Kwa hiyo
nikaapa katika hasira yangu, 'Kamwe hawataingia
rahani mwangu.'" Lakini kazi yake ilikamilika tangu
kuumbwa kwa ulimwengu. 4 Kwa maana mahali
fulani amezungumza kuhusu siku ya saba, akisema:
"Katika siku ya saba Mungu alipumzika kutoka kazi
zake zote." 5 Tena hapo awali amesema, "Kamwe
hawataingia rahani mwangu." 6 Kwa hiyo inabaki
kuwa wazi kwa wengine kuingia, nao wale wa kwanza
waliopokea Injili walishindwa kuingia kwa sababu ya
kutokutii. 7 Kwa hiyo Mungu ameweka siku nyingine,
akaiita "Leo", akisema kwa kinywa cha Daudi baadaye
sana, kwa maneno yaliyotangulia kunenwa: "Leo,
mkiisikia sauti yake, msiifanye mioyo yenu migumu".
8 Kwa maana kama Yoshua angelikuwa amewapa
raha, Mungu hangesema tena baadaye kuhusu siku
nyingine. 9 Basi, imebaki raha ya Sabato kwa ajili ya
watu wa Mungu; 10 kwa kuwa kila mmoja aingiaye
katika raha ya Mungu pia hupumzika kutoka kazi
zake mwenyewe, kama vile Mungu alivyopumzika
kutoka kazi zake. 11 Basi, na tufanye bidii kuingia
katika raha hiyo, ili asiwepo yeyote atakayeanguka
kwa kufuata mfano wao wa kutokutii. 12 Kwa maana
neno la Mungu li hai tena lina nguvu. Lina makali
kuliko upanga wowote wenye makali kuwili, hivyo
linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na
mafuta yaliyo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua
mawazo na makusudi ya moyo. 13 Wala hakuna
kiumbe chochote kilichofichika machoni pa Mungu.
Kila kitu kimefunuliwa na kiko wazi machoni pake
yeye ambaye lazima tutawajibika kwake. 14 Kwa kuwa
tunaye Kuhani Mkuu kuliko wote ambaye ameingia
mbinguni, Isa Mwana wa Mungu, basi na tushikamane
sana kwa uthabiti na ule ukiri wa imani yetu. 15 Kwa
kuwa hatuna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuliana
na sisi katika udhaifu wetu, lakini tunaye mmoja
ambaye alijaribiwa kwa kila namna, kama vile sisi
tujaribiwavyo: lakini yeye hakutenda dhambi. 16 Basi
na tukikaribie kiti cha rehema kwa ujasiri, ili tupewe
rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa
mahitaji.

5 Kwa maana kila kuhani mkuu anayechaguliwa
miongoni mwa wanadamu anawekwa
kuwawakilisha kwa mambo yanayomhusu Mungu, ili
apate kutoa matoleo na dhabihu kwa ajili ya dhambi.
2 Kwa kuwa yeye mwenyewe ni dhaifu, aweza

kuwachukulia kwa upole wale wasiojua na kupotoka.
3 Hii ndiyo sababu inampasa kutoa dhabihu kwa ajili
ya dhambi zake mwenyewe na vivyo hivyo kwa ajili
ya dhambi za watu. 4 Hakuna anayejitwalia heshima
hii mwenyewe; ni lazima aitwe na Mungu, kama
vile Haruni alivyoitwa. 5 Pia Al-Masihi hakujitwalia
utukufu yeye mwenyewe wa kuwa Kuhani Mkuu,
bali Mungu alimwambia, “Wewe ni Mwanangu; leo
mimi nimekuwa Baba yako.” 6 Pia mahali pengine
asema, “Wewe ni kuhani milele, kwa mfano wa
Melkizedeki.” **(aiōn g165)** 7 Katika siku za maisha ya
Isa hapa duniani, alimtolea maombi na dua pamoja
na kulia sana na machozi, yeye awezaye kumwokoa
na mauti, naye Mungu akamsikia kwa sababu ya kutii
kwake kwa unyenyekevu. 8 Ingawa alikuwa Mwana,
alijifunza utiifu kutokana na mateso aliyoyapata,
9 naye akiisha kukamilishwa, akawa chanzo cha
wokovu wa milele kwa wote wanaomtii. **(aiōnios g166)**
10 Naye amewekwa na Mungu kuwa Kuhani Mkuu
kwa mfano wa Melkizedeki. 11 Tunayo mengi ya
kusema kuhusu habari ya ukuhani huu, lakini ni
vigumu kuyaeleza, kwa sababu ninyi ni wazito wa
kuelewa. 12 Kwa hakika, ingawa hadi wakati huu
ingewapasa kuwa walimu, bado mnahitaji mtu wa
kuwafundisha tena hatua za awali za kweli ya neno la
Mungu. Mnahitaji maziwa, wala si chakula kigumu! 13
Kwa maana yeyote aishiye kwa kunywa maziwa bado
yeye ni mtoto mchanga, hana ujuzi katika mafundisho
kuhusu neno la haki. 14 Lakini chakula kigumu ni
kwa ajili ya watu wazima, ambao kwa kujizoeza
wamejifunza kupambanua kati ya mema na mabaya.

**6** Kwa hiyo, tukiachana na mafundisho yale ya awali
kuhusu Al-Masihi na tukisonga mbele ili tufikie
utimilifu, tusiweke tena msingi wa mafundisho ya
kuzitubia kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu,
2 mafundisho kuhusu aina za ubatizo, kuwekea
watu mikono, ufufuo wa wafu, na hukumu ya milele.
**(aiōnios g166)** 3 Mungu akitujalia tutafanya hivyo. 4
Kwa kuwa ni vigumu kwa wale ambao wakati fulani
walishapata nuru, ambao walishaonja kipawa cha
mbinguni, ambao wamekwisha kushiriki katika Roho
wa Mungu, 5 ambao wameonja uzuri wa neno la
Mungu na nguvu za wakati ujao, **(aiōn g165)** 6 kisha
wakianguka, kuwarejesha tena katika toba. Kwa
kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu tena na
kumdhalilisha hadharani, nayo ikawa hasara kwao. 7
Ardhi inayopokea mvua inayonyesha mara kwa mara
juu yake na baadaye inatoa mazao ya kuwanufaisha
wale ambao inalimwa kwa ajili yao, hupokea baraka
za Mungu. 8 Lakini ardhi ikizaa miiba na mibaruti,
haina thamani na iko hatarini kulaaniwa. Mwisho wake
ni kuchomwa moto. 9 Ingawa tunasema hivi, ndugu
zangu wapendwa, kwa upande wenu tuna hakika
ya mambo mema zaidi, mambo kuhusu wokovu.
10 Mungu si mdhalimu: yeye hataisahau kazi yenu
na upendo ule mlioonesha kwa ajili yake katika
kuwahudumia watakatifu na hata sasa mnaendelea
kuwahudumia. 11 Nasi twataka kila mmoja wenu
aoneshe bidii hiyo hiyo ili mpate kujua uhakika kamili
wa lile tumaini hadi mwisho, 12 ili msije mkawa wavivu,
bali mpate kuwaiga wale ambao kwa imani na saburi
hurithi zile ahadi. 13 Mungu alipompa Ibrahimu ahadi
yake, kwa sababu hapakuwa mwingine mkuu kuliko
yeye ambaye angeapa naye, aliapa kwa nafsi yake,
14 akisema, “Hakika nitakubariki na kukupa wazao
wengi.” 15 Ibrahimu naye, baada ya kungoja kwa
saburi, alipokea kile kilichoahidiwa. 16 Wanadamu
huapa kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, nacho kiapo
hicho huthibitisha kile kilichosemwa na hivyo humaliza
mabishano yote. 17 Mungu alipotaka kuonesha
kwa udhahiri zaidi ile asili ya kutokubadilika kwa
ahadi yake kwa warithi wa ahadi, aliithitibisha kwa
kiapo. 18 Mungu alifanya hivyo ili kwa vitu viwili
visivyobadilika, yaani ahadi yake na kiapo chake,
ambavyo kwavyo Mungu hawezi kusema uongo,
sisi ambao tumemkimbilia ili tulishike lile tumaini
lililowekwa mbele yetu tuwe na faraja thabiti. 19
Tunalo tumaini hili kama nanga ya roho iliyo imara na
thabiti. Tumaini hili huingia katika mahali patakatifu
nyuma ya pazia, 20 ambapo Isa mtangulizi wetu
aliingia kwa niaba yetu. Yeye amekuwa Kuhani Mkuu
milele, kwa mfano wa Melkizedeki. **(aiōn g165)**

**7** Kwa kuwa huyu Melkizedeki alikuwa mfalme wa
Salemu na kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana.
Alipokutana na Ibrahimu akirudi kutoka kuwashinda
wafalme, Melkizedeki alimbariki, 2 naye Ibrahimu
alimpa sehemu ya kumi ya kila kitu. Kwanza, jina
hilo Melkizedeki maana yake ni “mfalme wa haki”.
Na pia “mfalme wa Salemu” maana yake ni “mfalme
wa amani”. 3 Hana baba wala mama, hana ukoo,
hana mwanzo wala mwisho wa siku zake, kama
Mwana wa Mungu. Yeye adumu akiwa kuhani milele.

4 Tazama jinsi alivyokuwa mkuu: Hata Ibrahimu, baba yetu wa zamani, alimpa sehemu ya kumi ya nyara zake. 5 Basi sheria inawaagiza wana wa Lawi ambao hufanyika makuhani kupokea sehemu ya kumi kutoka kwa watu ambao ni ndugu zao, ingawa ndugu zao ni wazao wa Ibrahimu. 6 Huyu Melkizedeki, ingawa hakufuatia ukoo wake kutoka kwa Lawi, lakini alipokea sehemu ya kumi kutoka kwa Ibrahimu na kumbariki yeye aliyekuwa na zile ahadi. 7 Wala hakuna shaka kwamba mdogo hubarikiwa na aliye mkuu kuliko yeye. 8 Kwa upande mmoja, sehemu ya kumi hupokelewa na watu ambao hufa; lakini kwa upande mwingine hupokelewa na yeye ambaye hushuhudiwa kuwa yu hai. 9 Mtu anaweza hata kusema kwamba Lawi, ambaye hupokea sehemu ya kumi, alitoa hiyo sehemu ya kumi kupitia kwa Ibrahimu, 10 kwa sababu Melkizedeki alipokutana na Ibrahimu, Lawi alikuwa bado katika viuno vya baba yake wa zamani. 11 Kama ukamilifu ungeweza kupatikana kupitia kwa ukuhani wa Walawi (kwa kuwa katika msingi huo, sheria ilitolewa kwa watu), kwa nini basi kulikuwa na haja ya kuja kuhani mwingine: kuhani kwa mfano wa Melkizedeki, wala si kwa mfano wa Haruni? 12 Kwa kuwa ukuhani ukibadilika, lazima sheria nayo ibadilike. 13 Yeye ambaye mambo haya yanasemwa alikuwa wa kabila lingine, na hakuna mtu wa kabila hilo aliyewahi kuhudumu katika madhabahu. 14 Kwa maana ni dhahiri kwamba Bwana wetu alitoka katika uzao wa Yuda, tena kuhusu kabila hilo Musa hakusema lolote kwa habari za makuhani. 15 Tena hayo tuliyosema yako wazi zaidi kama akitokea kuhani mwingine kama Melkizedeki, 16 yeye ambaye amefanyika kuhani si kwa misingi ya sheria kama ilivyokuwa kwa baba zake, bali kwa misingi ya uwezo wa uzima usioharibika. 17 Kwa maana imeshuhudiwa kwamba: "Wewe ni kuhani milele, kwa mfano wa Melkizedeki." **(aiōn g165)** 18 Kwa upande mmoja, ile amri ya mwanzo isiyofaa na dhaifu imebatilishwa 19 (kwa maana sheria haikufanya kitu chochote kuwa kikamilifu). Kwa upande mwingine, tumeletewa tumaini lililo bora zaidi ambalo linatuleta karibu na Mungu. 20 Nalo tumaini hilo halikutolewa pasipo kiapo! Wengine walikuwa makuhani pasipo kiapo chochote, 21 lakini Isa alifanywa kuhani kwa kiapo wakati Mungu alimwambia: "Mwenyezi Mungu ameapa, naye hatabadilisha mawazo yake: 'Wewe ni kuhani milele.'" **(aiōn g165)** 22 Kwa ajili ya kiapo hiki, Isa amekuwa mdhamini wa agano lililo bora zaidi. 23 Basi kumekuwa na makuhani wengi wa aina hiyo, kwa kuwa kifo kiliwazuia kuendelea na huduma yao ya ukuhani. 24 Lakini kwa sababu Isa anaishi milele, anao ukuhani wa kudumu. **(aiōn g165)** 25 Kwa hiyo anaweza kuwaokoa kabisa wale wanaomjia Mungu kupitia kwake, kwa sababu yeye adumu daima kuomba kwa ajili yao. 26 Kwa kuwa ilitupasa tuwe na Kuhani Mkuu wa namna hii, yaani aliye mtakatifu, asiye na lawama, asiye na dosari, aliyetengwa na wenye dhambi na kuinuliwa juu ya mbingu. 27 Yeye hahitaji kutoa dhabihu siku kwa siku kwa ajili ya dhambi, kwanza kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za watu kama wale makuhani wakuu wengine. Yeye alitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zao mara moja tu, alipojitoa mwenyewe. 28 Kwa kuwa sheria huwaweka makuhani wakuu watu ambao ni dhaifu; lakini lile neno la kiapo, lililokuja baada ya sheria, lilimweka Mwana, ambaye amefanywa kuwa mkamilifu milele. **(aiōn g165)**

**8** Basi jambo tunalotaka kulisema ni hili: Tunaye Kuhani Mkuu aliyeketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Aliye Mkuu mbinguni, 2 yeye anayehudumu katika patakatifu, hema la kweli lililowekwa na Mwenyezi Mungu, wala si na mwanadamu. 3 Kila kuhani mkuu huwekwa ili atoe sadaka na dhabihu. Vivyo hivyo, ilikuwa jambo muhimu kwa huyu Kuhani naye awe na kitu cha kutoa. 4 Kama angekuwa duniani, hangekuwa kuhani, kwa sababu tayari wapo watu watoao sadaka kama ilivyoelekezwa na sheria. 5 Wanahudumu katika patakatifu palipo mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni. Hii ndiyo sababu Musa alionywa alipokaribia kujenga Maskani, akaambiwa: "Hakikisha kuwa unavitengeneza vitu vyote kwa mfano uliooneshwa kule mlimani." 6 Lakini huduma aliyopewa Isa ni bora kuliko yao, kama vile agano ambalo yeye ni mpatanishi wake lilivyo bora zaidi ya lile la zamani, nalo limewekwa misingi ya ahadi zilizo bora zaidi. 7 Kwa maana kama hapakuwa na kasoro katika lile agano la kwanza, pasingekuwa na haja ya kutafuta nafasi kwa ajili ya jingine. 8 Lakini Mungu aliona kosa kwa watu, naye akasema: "Siku zinakuja, asema Mwenyezi Mungu, nitakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. 9 Agano langu halitakuwa kama

lile nililofanya na baba zao nilipowashika mkono
kuwaongoza watoke nchi ya Misri, kwa sababu
hawakuendelea kuwa waaminifu katika agano langu,
nami nikawaacha, asema Mwenyezi Mungu. **10** Hili
ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya Israeli baada
ya siku zile, asema Mwenyezi Mungu. Nitaziweka
sheria zangu katika nia zao na kuziandika mioyoni
mwao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu
wangu. **11** Mtu hatamfundisha tena jirani yake,
wala mtu kumfundisha ndugu yake akisema, 'Mjue
Mwenyezi Mungu,' kwa sababu wote watanijua mimi,
tangu aliye mdogo kabisa kwao, hadi aliye mkuu
sana. **12** Kwa sababu nitasamehe uovu wao, wala
sitazikumbuka dhambi zao tena!" **13** Kwa kuliita agano
hili "jipya", Mungu amefanya lile agano la kwanza
kuwa kuukuu; nacho kitu kinachoanza kuchakaa na
kuwa kikuukuu kiko karibu kutoweka.

**9** Basi agano lile la kwanza lilikuwa na kanuni
zake za kuabudu na pia patakatifu pake pa
kidunia. **2** Hema ilitengenezwa. Katika sehemu yake
ya kwanza kulikuwa na kinara cha taa, meza na
mikate iliyowekwa wakfu; hii sehemu iliitwa Mahali
Patakatifu. **3** Nyuma ya pazia la pili, palikuwa na
sehemu iliyoitwa Patakatifu pa Patakatifu, **4** ambapo
palikuwa na yale madhabahu ya dhahabu ya kufukizia
uvumba, na lile Sanduku la Agano lililofunikwa kwa
dhahabu. Sanduku hili lilikuwa na gudulia la dhahabu
lenye mana, ile fimbo ya Haruni iliyochipuka, na vile
vibao vya mawe vya Agano. **5** Juu ya lile Sanduku
kulikuwa na makerubi wa Utukufu, wakikitia kivuli kiti
cha rehema. Lakini hatuwezi kujadili vitu hivi kwa
undani sasa. **6** Basi vitu hivi vilipokuwa vimepangwa,
makuhani waliingia mara kwa mara katika sehemu ya
kwanza ya hema ili kufanya taratibu zao za ibada.
**7** Lakini ni kuhani mkuu peke yake aliyeingia ndani
ya sehemu ya pili ya hema. Tena hii ilikuwa mara
moja tu kwa mwaka, na hakuingia kamwe bila damu,
ambayo alitoa kwa ajili yake mwenyewe na kwa ajili
ya dhambi za watu walizotenda bila kukusudia. **8**
Kwa njia hii, Roho wa Mungu alikuwa anaonesha
kwamba, maadamu lile hema la kwanza lilikuwa bado
limesimama, njia ya kuingia Patakatifu pa Patakatifu
ilikuwa bado haijafunguliwa. **9** Huu ulikuwa mfano
kwa ajili ya wakati wa sasa, kuonesha kwamba
sadaka na dhabihu zilizokuwa zikitolewa hazikuweza
kusafisha dhamiri ya mtu anayeabudu. **10** Lakini
hizi zilishughulika tu na vyakula na vinywaji, pamoja
na taratibu mbalimbali za kunawa kwa nje, kanuni
kwa ajili ya mwili zilizowekwa hadi wakati utimie
wa matengenezo mapya. **11** Al-Masihi alipokuja
akiwa Kuhani Mkuu wa mambo mema ambayo tayari
yameshawasili, alipitia kwenye hema iliyo kuu zaidi
na bora zaidi, ambayo haikutengenezwa kwa mikono
ya binadamu, hii ni kusema, ambayo si sehemu ya
uumbaji huu. **12** Hakuingia kupitia kwa damu ya mbuzi
na ya ndama; lakini aliingia Patakatifu pa Patakatifu
mara moja tu kwa damu yake mwenyewe, akiisha
kupata ukombozi wa milele. **(aiōnios g166)** **13** Damu
ya mbuzi na ya mafahali, na majivu ya mitamba
walivyonyunyiziwa wale waliokuwa najisi viliwatakasa,
hata kuwaondolea uchafu wa nje. **14** Basi damu ya Al-
Masihi, ambaye kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake
kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na waa, si itazisafisha
dhamiri zetu zaidi kutokana na matendo yaletayo
mauti, ili tupate kumtumikia Mungu aliye hai! **(aiōnios
g166)** **15** Kwa sababu hii Al-Masihi ni mpatanishi wa
agano jipya, ili wale walioitwa waweze kupokea ile
ahadi ya urithi wa milele: kwa vile yeye alikufa awe
ukombozi wao kutoka kwa dhambi walizozitenda chini
ya agano la kwanza. **(aiōnios g166)** **16** Kwa habari ya
wosia, ni muhimu kuthibitisha kifo cha yule aliyeutoa,
**17** kwa sababu wosia huwa na nguvu tu wakati mtu
ameshakufa; kamwe hauwezi kutumika wakati yule
aliyeuandika bado yuko hai. **18** Hii ndiyo sababu hata
lile agano la kwanza halikuweza kutekelezwa pasipo
damu. **19** Musa alipotangaza kila amri kwa watu wote,
alichukua damu ya ndama na ya mbuzi, pamoja na
maji, sufu nyekundu na matawi ya mti wa hisopo,
akanyunyizia kile kitabu na watu wote. **20** Alisema, "Hii
ndiyo damu ya agano, ambalo Mungu amewaamuru
kulitii." **21** Vivyo hivyo alinyunyizia damu hiyo kwenye
ile hema pamoja na kila kifaa kilichotumika ndani
yake kwa taratibu za ibada. **22** Kwa kweli sheria
hudai kwamba, karibu kila kitu kitakaswe kwa damu,
wala pasipo kumwaga damu, hakuna msamaha wa
dhambi. **23** Kwa hiyo, ilikuwa muhimu kwa nakala
za vitu vile vya mbinguni vitakaswe kwa dhabihu
hizi, lakini vitu halisi vya mbinguni vilihitaji dhabihu
bora kuliko hizi. **24** Kwa maana Al-Masihi hakuingia
patakatifu palipofanywa kwa mikono ya mwanadamu,
ambao ni mfano wa kile kilicho halisi. Yeye aliingia
mbinguni penyewe, ili sasa aonekane mbele za

Mungu kwa ajili yetu. 25 Wala hakuingia mbinguni
ili apate kujitoa mwenyewe mara kwa mara, kama
vile kuhani mkuu aingiavyo Patakatifu pa Patakatifu
kila mwaka kwa damu ambayo si yake mwenyewe.
26 Ingekuwa hivyo, ingempasa Al-Masihi kuteswa
mara nyingi tangu kuumbwa kwa ulimwengu. Lakini
sasa ametokea mara moja tu katika mwisho wa
nyakati aiondoe dhambi kwa kujitoa mwenyewe
kuwa dhabihu. **(aiōn g165)** 27 Kama vile mwanadamu
alivyowekewa kufa mara moja tu na baada ya kufa
akabili hukumu, 28 vivyo hivyo Al-Masihi alitolewa
mara moja tu kuwa dhabihu ili azichukue dhambi za
watu wengi. Naye atakuja mara ya pili, sio kuchukua
dhambi, bali kuwaletea wokovu wale wanaomngoja
kwa shauku.

**10** Torati ni kivuli tu cha mambo mema yajayo, wala
si uhalisi wa mambo yenyewe. Kwa sababu hii,
haiwezekani kamwe kupitia kwa dhabihu zitolewazo
mwaka hadi mwaka kuwakamilisha wale wanaokaribia
ili kuabudu. 2 Kama dhabihu hizo zingeweza
kuwakamilisha, hazingeendelea kutolewa tena. Kwa
kuwa hao waabuduo wangekuwa wametakaswa mara
moja tu, wala wasingejiona tena kuwa na dhambi. 3
Lakini zile dhabihu zilikuwa ukumbusho wa dhambi
kila mwaka, 4 kwa sababu haiwezekani damu ya
mafahali na mbuzi kuondoa dhambi. 5 Kwa hiyo,
Al-Masihi alipokuja duniani, alisema: “Dhabihu na
sadaka hukuzitaka, bali mwili uliniandalia; 6 sadaka
za kuteketezwa na za dhambi hukupendezwa nazo. 7
Ndipo niliposema, ‘Mimi hapa, nimekuja, imeandikwa
kunihusu katika kitabu: Nimekuja kuyafanya mapenzi
yako, Ee Mungu.’” 8 Kwanza alisema, “Dhabihu
na sadaka, sadaka za kuteketezwa na za dhambi
hukuzitaka, wala hukupendezwa nazo” (ingawa sheria
iliagiza zitolewe). 9 Kisha akasema, “Mimi hapa,
nimekuja kuyafanya mapenzi yako.” Aondoa lile agano
la kwanza ili kuimarisha la pili. 10 Katika mapenzi
hayo sisi tumetakaswa na kufanywa watakatifu kupitia
kwa sadaka ya mwili wa Isa Al-Masihi alioutoa mara
moja tu. 11 Kila kuhani husimama siku kwa siku
akifanya huduma yake ya ibada, na kutoa tena na tena
dhabihu zile zile, ambazo haziwezi kamwe kuondoa
dhambi. 12 Lakini huyu kuhani baada ya kutoa
dhabihu moja kwa ajili ya dhambi kwa wakati wote,
aliketi mkono wa kuume wa Mungu. 13 Tangu wakati
huo anangoja hadi adui zake wawekwe chini ya miguu
yake, 14 kwa sababu kwa dhabihu moja amewafanya
wakamilifu milele wale wote wanaotakaswa. 15 Pia
Roho wa Mungu anatushuhudia kuhusu jambo hili.
Kwanza anasema: 16 “Hili ndilo agano nitakalofanya
nao baada ya siku hizo, asema Mwenyezi Mungu.
Nitaziweka sheria zangu mioyoni mwao, na kuziandika
katika nia zao.” 17 Kisha aongeza kusema: “Dhambi
zao na kutokutii kwao sitakumbuka tena.” 18 Basi
haya yaliposamehewa, hakuna tena dhabihu yoyote
inayohitajika kwa ajili ya dhambi. 19 Kwa hiyo,
ndugu zangu, kwa kuwa tunao ujasiri wa kupaingia
Patakatifu pa Patakatifu kwa damu ya Isa, 20 kwa njia
mpya iliyo hai tuliyofunguliwa kwa ajili yetu kupitia
kwenye lile pazia, yaani mwili wake, 21 basi kwa
kuwa tunaye Kuhani Mkuu juu ya nyumba ya Mungu,
22 sisi na tumkaribie Mungu kwa moyo mnyofu kwa
imani timilifu, mioyo yetu ikiwa imenyunyizwa damu
ya Al-Masihi na kuwa safi kutokana na dhamiri
mbaya nayo miili yetu ikiwa imeoshwa kwa maji
safi. 23 Tushike kwa uthabiti lile tumaini la ukiri wetu
bila kuyumbayumba, kwa maana yeye aliyeahidi ni
mwaminifu. 24 Tuangaliane na kuhimizana sisi kwa
sisi katika upendo na katika kutenda mema. 25 Wala
tusiache kukutana pamoja, kama wengine walivyo na
desturi, bali tuhimizane sisi kwa sisi kadiri tuonavyo
Siku ile inakaribia. 26 Tukiendelea kutenda dhambi
kwa makusudi baada ya kupokea ufahamu wa ile
kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi. 27
Lakini kinachobaki ni kungoja kwa hofu hukumu ya
moto uwakao, utakaowaangamiza adui za Mungu.
28 Yeyote aliyeikataa Torati ya Musa alikufa pasipo
huruma kwa ushahidi wa watu wawili au watatu. 29
Je, mnadhani ni adhabu kali kiasi gani anayostahili
kupewa mtu aliyemkanyaga Mwana wa Mungu chini
ya nyayo zake, yeye aliyeifanya damu ya agano
iliyomtakasa kuwa kitu najisi na kumtendea maovu
Roho wa neema? 30 Kwa kuwa tunamjua yeye
aliyesema, “Ni juu yangu kulipiza kisasi; nitalipiza.”
Tena asema, “Mwenyezi Mungu atawahukumu watu
wake.” 31 Ni jambo la kutisha kuanguka mikononi
mwa Mungu aliye hai. 32 Kumbukeni siku zile za
kwanza, ambazo baada ya kutiwa nuru mlistahimili
mashindano makali ya maumivu. 33 Wakati mwingine
mlitukanwa na kuteswa hadharani; wakati mwingine
mlikuwa radhi kuungana na wale waliotendwa hivyo.
34 Mliwahurumia wale waliokuwa kifungoni, mkikubali

kwa furaha kunyang'anywa mali yenu kwa maana
mlijua kwamba mnayo mali iliyo bora zaidi idumuyo.
35 Kwa hiyo msiutupe ujasiri wenu, kwa maana
una thawabu kubwa mno. 36 Inawapasa kuvumilia
ili mkiisha kufanya mapenzi ya Mungu mpate kile
alichoahidi. 37 Kwa kuwa, "Bado kitambo kidogo
tu, yeye ajaye atakuja wala hatakawia." 38 Na,
"Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani. Naye
akisitasita, sina furaha naye." 39 Lakini sisi hatumo
miongoni mwa hao wanaositasita na kuangamia,
bali tuko miongoni mwa hao wenye imani na hivyo
tunaokolewa.

11 Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo
yatarajiwayo, na udhahiri wa mambo
yasiyoonekana. 2 Maana baba zetu wa kale
walipongezwa kwa haya. 3 Kwa imani tunafahamu
kwamba ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu,
vitu vyote vinavyoonekana havikuumbwa kutoka kwa
vitu vinavyoonekana. **(aiōn g165)** 4 Kwa imani Habili
alimtolea Mungu dhabihu bora kuliko Kaini. Kwa imani
alishuhudiwa kuwa mwenye haki, Mungu mwenyewe
akazishuhudia sadaka zake. Kwa imani bado ananena
ingawa amekufa. 5 Kwa imani Idrisi alitwaliwa
kutoka maisha haya, kiasi kwamba hakuonja mauti.
Hakuonekana, "kwa sababu Mungu alimchukua". Kwa
kuwa kabla hajatwaliwa alikuwa ameshuhudiwa kuwa
ni mtu aliyempendeza Mungu. 6 Lakini pasipo imani
haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana yeyote
anayemjia Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko
na ya kuwa huwapa thawabu wale wanaomtafuta kwa
bidii. 7 Kwa imani, Nuhu alipoonywa na Mungu kuhusu
mambo ambayo hayajaonekana bado, kwa kumcha
Mungu alitengeneza safina ili kuokoa jamaa yake.
Kwa imani yake aliuhukumu ulimwengu na akawa
mrithi wa haki ipatikanayo kwa imani. 8 Kwa imani
Ibrahimu, alipoitwa aende mahali Mungu angempa
baadaye kuwa urithi, alitii na akaenda, ingawa hakujua
anakoenda. 9 Kwa imani alifanya maskani yake katika
nchi ya ahadi kama mgeni katika nchi ya kigeni; aliishi
katika mahema, kama Isaka na Yakobo walivyofanya,
waliokuwa pia warithi pamoja naye wa ahadi ile ile.
10 Kwa maana alikuwa akiutazamia mji wenye misingi
ya kudumu, ambao mwenye kuubuni na kuujenga
ni Mungu. 11 Kwa imani Ibrahimu, ingawa alikuwa
mzee wa umri, naye Sara mwenyewe aliyekuwa
tasa, alipokea uwezo wa kuwa baba kwa sababu
alimhesabu Mungu aliyemwahidi kuwa mwaminifu na
kwamba angetimiza ahadi yake. 12 Hivyo kutokana
na huyu mtu aliyekuwa sawa na mfu, wakazaliwa
wazao wengi kama nyota za mbinguni na kama
mchanga wa pwani usiohesabika. 13 Watu hawa
wote wakafa katika imani bila kuzipokea zile ahadi,
lakini waliziona kwa mbali na kuzishangilia. Nao
walikubali kwamba walikuwa wageni na wasiokuwa
na maskani hapa duniani. 14 Watu wasemao mambo
kama haya, wanaonesha wazi kwamba wanatafuta
nchi yao wenyewe. 15 Kwa kweli kama wangekuwa
wanafikiri kuhusu nchi waliyoiacha, wangepata nafasi
ya kurudi huko. 16 Lakini badala yake walitamani
nchi iliyo bora zaidi, yaani nchi ya mbinguni. Kwa
hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa kuwa
amekwisha kuandaa mji kwa ajili yao. 17 Kwa imani
Ibrahimu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaka kuwa
dhabihu. Yeye aliyekuwa amezipokea ahadi za Mungu
alikuwa tayari kumtoa mwanawe, aliyekuwa mwanawe
pekee awe dhabihu, 18 hata ingawa Mungu alikuwa
amemwambia Ibrahimu, "Uzao wako utahesabiwa
kupitia kwa Isaka." 19 Ibrahimu alihesabu kuwa
Mungu angeweza kumfufua Isaka kutoka kwa wafu.
Na kusema kwa mfano, alimpata tena Isaka kutoka
kwa wafu. 20 Kwa imani Isaka aliwabariki Yakobo na
Esau kuhusu maisha yao ya baadaye. 21 Kwa imani
Yakobo alipokuwa anakufa, alimbariki kila mmoja
wa mtoto wa Yusufu, akamwabudu Mungu akiwa
ameegemea juu ya kichwa cha fimbo yake. 22 Kwa
imani, Yusufu alipokaribia mwisho wa maisha yake,
alinena habari za kutoka kwa Waisraeli huko Misri na
akatoa maagizo kuhusu mifupa yake. 23 Kwa imani,
wazazi wa Musa walimficha kwa miezi mitatu baada
ya kuzaliwa, kwa sababu waliona kuwa si mtoto wa
kawaida, wala hawakuiogopa amri ya mfalme. 24 Kwa
imani, Musa alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa
mwana wa binti Farao. 25 Akachagua kupata mateso
pamoja na watu wa Mungu, kuliko kujifurahisha
kwa anasa za dhambi kwa muda mfupi. 26 Aliona
kushutumiwa kwa ajili ya Al-Masihi ni utajiri mkubwa
kuliko hazina za Misri, maana alikuwa anatazamia
kupata thawabu baadaye. 27 Kwa imani Musa
aliondoka Misri bila kuogopa ghadhabu ya mfalme.
Alivumilia kwa sababu alimwona yeye asiyeonekana
kwa macho. 28 Kwa imani akaadhimisha Pasaka na
kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza

wazaliwa wa kwanza asiwaguse wazaliwa wa Israeli.
29 Kwa imani, watu walivuka Bahari ya Shamu kama
vile juu ya nchi kavu; lakini Wamisri walipojaribu
kufanya hivyo, walitoswa ndani ya maji. 30 Kwa imani
kuta za Yeriko zilianguka, baada ya watu kuzizunguka
kwa siku saba. 31 Kwa imani, Rahabu, yule kahaba,
hakuangamizwa pamoja na wale waliomwasi Mungu,
kwa kuwa aliwakaribisha wale wapelelezi. 32 Basi
niseme nini zaidi? Sina wakati wa kusema habari za
Gideoni, Baraka, Samsoni, Yefta, Daudi, Samweli
na manabii, 33 ambao kwa imani walishinda milki za
wafalme, walitekeleza haki, na wakapokea ahadi za
Mungu; walifunga vinywa vya simba, 34 wakazima
makali ya miali ya moto, na wakaepuka kuuawa
kwa upanga; udhaifu wao uligeuka kuwa nguvu;
pia walikuwa hodari vitani na kuyafukuza majeshi
ya wageni. 35 Wanawake walipokea watu wao
waliokuwa wamekufa, wakafufuliwa. Lakini wengine
waliteswa, nao wakakataa kufunguliwa, ili wapate
ufufuo ulio bora zaidi. 36 Wengine walidhihakiwa
na kupigwa, hata walifungwa minyororo na kutiwa
gerezani. 37 Walipigwa kwa mawe; walipasuliwa
vipande viwili kwa msumeno; waliuawa kwa upanga.
Walizungukazunguka wakiwa wamevaa ngozi za
kondoo na mbuzi, wakiwa maskini, wakiteswa na
kutendwa mabaya, 38 watu ambao ulimwengu
haukustahili kuwa nao. Walizunguka majangwani
na milimani, katika mapango na katika mahandaki
ardhini. 39 Hawa wote walishuhudiwa vyema kwa
sababu ya imani yao, lakini hakuna hata mmoja wao
aliyepokea yale yaliyoahidiwa. 40 Kwa kuwa Mungu
alikuwa ametangulia kutuwekea kitu kilicho bora zaidi
ili wao wasikamilishwe pasipo sisi.

**12** Kwa sababu hii, kwa kuwa tumezungukwa na
wingu kubwa namna hii la mashahidi, basi na
tuweke kando kila kitu kinachotuzuia na ile dhambi
inayotuzinga kwa urahisi, nasi tupige mbio kwa
saburi katika yale mashindano yaliyowekwa kwa ajili
yetu. 2 Basi na tumtazame sana Isa mwanzilishi na
mkamilishaji wa imani yetu, yeye ambaye kwa ajili ya
furaha iliyowekwa mbele yake alistahimili msalaba,
bila kujali aibu ya huo msalaba, naye ameketi mkono
wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. 3 Mtafakarini
sana yeye aliyestahimili upinzani mkuu namna hii
kutoka kwa watu wenye dhambi, ili msije mkachoka
na kukata tamaa. 4 Katika kushindana kwenu dhidi
ya dhambi, bado hamjapigana kiasi cha kumwaga
damu yenu. 5 Nanyi mmesahau yale maneno ya
kuwaonya yanayowataja ninyi kuwa wana, yakisema:
“Mwanangu, usidharau adhabu ya Mwenyezi Mungu,
wala usikate tamaa akikukemea, 6 kwa sababu
Mwenyezi Mungu huwaadibisha wale anaowapenda,
na humwadhibu kila mmoja anayemkubali kuwa
mwana.” 7 Vumilieni taabu kwa ajili ya kufunzwa
adabu. Mungu anawatendea ninyi kama watoto
wake, kwa maana ni mtoto yupi asiyeadibishwa
na mzazi wake? 8 Kama hakuna kuadibishwa
(ambalo ni fungu la watoto wote), basi ninyi ni
watoto haramu, wala si watoto halali. 9 Tena, sisi
sote tunao baba wa kimwili, waliotuadibisha nasi
tukawaheshimu kwa ajili ya hilo. Je, si inatupasa
kujinyenyekeza zaidi kwa Baba wa roho zetu ili tuishi?
10 Baba zetu walituadibisha kwa kitambo kidogo
kama wao wenyewe walivyoona vyema, lakini Mungu
hutuadibisha kwa faida yetu ili tupate kushiriki utakatifu
wake. 11 Kuadibishwa wakati wowote hakuonekani
kuwa kitu cha kufurahisha bali chenye maumivu
kinapotekelezwa. Lakini baadaye huzaa matunda
ya haki na amani kwa wale waliofunzwa nayo. 12
Kwa hiyo, itieni nguvu mikono yenu iliyo dhaifu na
magoti yenu yaliyolegea. 13 Sawazisheni mapito ya
miguu yenu, ili kitu kilicho kiwete kisidhoofishwe bali
kiponywe. 14 Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu
wote na huo utakatifu, ambao bila kuwa nao hakuna
mtu atakayemwona Bwana. 15 Chungeni sana mtu
yeyote asiikose neema ya Mungu, na kwamba shina
la uchungu lisije likachipuka na kuwasumbua, na watu
wengi wakatiwa unajisi kwa hilo. 16 Chungeni miongoni
mwenu asiwepo mwasherati au mtu asiyemcha
Mungu kama Esau, ambaye kwa ajili ya mlo mmoja
aliuza haki ya uzaliwa wake wa kwanza. 17 Baadaye
kama mnavyofahamu, alipotaka kurithi ile baraka,
alikataliwa, maana hakupata nafasi ya kutubu, ingawa
aliitafuta kwa machozi. 18 Hamjaufikia mlima ule
uwezao kuguswa na ambao unawaka moto; wala
kwenye giza, utusitusi na dhoruba; 19 kwenye mlio
wa tarumbeta, au kwenye sauti isemayo maneno
ya kutisha kiasi ambacho wale walioisikia waliomba
wasiambiwe neno jingine zaidi, 20 kwa sababu
hawangeweza kustahimili neno lile lililoamriwa: “Hata
mnyama akigusa mlima huu, atapigwa mawe.” 21
Waliyoyaona yalikuwa ya kutisha kiasi kwamba Musa

alisema, “Ninatetemeka kwa hofu.” 22 Lakini ninyi
mmekuja Mlima Sayuni, Yerusalemu ya mbinguni,
mji wa Mungu aliye hai. Mmekuja penye kusanyiko
kubwa la malaika maelfu kwa maelfu wasiohesabika
wanaoshangilia, 23 kwenye jumuiya ya waumini
ya wazaliwa wa kwanza wa Mungu, ambao majina
yao yameandikwa mbinguni. Mmekuja kwa Mungu,
mhukumu wa watu wote, kwenye roho za wenye haki
waliokamilishwa, 24 kwa Isa mpatanishi wa agano
jipya, na kwa damu iliyonyunyizwa, ile inenayo mambo
mema kuliko damu ya Habili. 25 Angalieni msije
mkamkataa yeye anenaye. Ikiwa wao hawakuepuka
adhabu walipomkataa yeye aliyewaonya hapa duniani,
sisi je, tutaokokaje tusipomsikiliza yeye anayetuonya
kutoka mbinguni? 26 Wakati ule sauti yake ilitetemesha
dunia, lakini sasa ameahidi, “Kwa mara moja tena
nitatetemesha si nchi tu bali na mbingu pia.” 27 Maneno
haya “kwa mara moja tena” yanaonesha kuondoshwa
kwa vile vitu vinavyoweza kutetemeshwa, yaani vile
vitu vilivyoumbwa, kwa kusudi vile vitu visivyoweza
kutetemeshwa vibaki. 28 Kwa hiyo, kwa kuwa
tunapokea ufalme ambao hauwezi kutetemeshwa,
basi na tuwe na shukrani, na hivyo tumwabudu Mungu
kwa namna inayompendeza, kwa unyenyekevu na
uchaji, 29 kwa kuwa “Mungu wetu ni moto ulao.”

13 Endeleeni kupendana kama ndugu. 2 Msisahau
kuwakaribisha wageni, kwa kuwa kwa kufanya
hivyo, watu wengine waliwakaribisha malaika pasipo
kujua. 3 Wakumbukeni wale waliofungwa gerezani
kana kwamba ninyi mmefungwa pamoja nao. Pia
wakumbukeni wale wanaotendewa vibaya, kana
kwamba ni ninyi wenyewe mnateswa. 4 Ndoa na
iheshimiwe na watu wote, nayo malazi yawe safi, kwa
kuwa Mungu atawahukumu wazinzi na waasherati
wote. 5 Yalindeni maisha yenu msiwe na tabia ya
kupenda fedha, bali mridhike na vile mlivyo navyo,
kwa sababu Mungu amesema, “Kamwe sitakuacha,
wala sitakupungukia.” 6 Kwa hiyo tunaweza kusema
kwa ujasiri, “Mwenyezi Mungu ni msaada wangu;
sitaogopa. Mwanadamu anaweza kunitenda nini?” 7
Wakumbukeni viongozi wenu, wale waliowaambia
neno la Mungu. Angalieni matokeo ya mwenendo wa
maisha yao mkaiige imani yao. 8 Isa Al-Masihi ni yeye
yule jana, leo na hata milele. **(aiōn g165)** 9 Msichukuliwe
na kila aina ya mafundisho ya kigeni. Ni vyema mioyo
yenu iimarishwe kwa neema, wala si kwa sheria
kuhusu utaratibu wa vyakula, ambavyo havina faida
kwa wale wanaozishika hizo sheria. 10 Sisi tunayo
madhabahu ambayo wale wanaohudumu katika hema
hawana haki ya kula vile vitu vilivyowekwa juu yake.
11 Kuhani mkuu huchukua damu ya wanyama na
kuiingiza Patakatifu pa Patakatifu, kama sadaka ya
dhambi, lakini miili ya hao wanyama huteketezwa
nje ya kambi. 12 Vivyo hivyo, Isa naye aliteswa
nje ya lango la mji ili awatakase watu kwa damu
yake mwenyewe. 13 Kwa hiyo, basi na tumwendee
nje ya kambi, tukiichukua aibu aliyobeba. 14 Kwa
kuwa hapa hatuna mji udumuo, bali tunautafuta
ule ujao. 15 Basi kupitia kwa Isa, tuzidi kumtolea
Mungu dhabihu ya sifa, yaani matunda ya midomo
inayolikiri Jina lake. 16 Na msiache kutenda mema
na kushirikiana vile vitu mlivyo navyo, kwa kuwa
dhabihu kama hizo ndizo zinazompendeza Mungu.
17 Watiini viongozi wenu na kujinyenyekeza chini
ya mamlaka yao. Kwa maana wao wanakesha kwa
ajili yenu kama watu watakaopaswa kutoa maelezo.
Watiini ili wafanye kazi yao kwa furaha, wala si kama
mzigo, maana hiyo haitakuwa na faida kwenu. 18
Tuombeeni. Tuna hakika kuwa tunayo dhamiri safi
na shauku ya kuishi kwa uadilifu kwa kila njia. 19
Ninawasihi zaidi mniombee ili nipate kurudishwa
kwenu upesi. 20 Basi Mungu wa amani, ambaye
kwa damu ya agano la milele alimleta tena kutoka
kwa wafu Bwana wetu Isa, yule Mchungaji Mkuu wa
kondoo, **(aiōnios g166)** 21 awafanye ninyi wakamilifu
mkiwa mmekamilishwa katika kila jambo jema ili
mpate kutenda mapenzi yake, naye atende ndani
yetu kile kinachompendeza machoni pake, kupitia
kwa Isa Al-Masihi, ambaye utukufu una yeye milele
na milele. Amen. **(aiōn g165)** 22 Ndugu zangu, nawasihi
mchukuliane na maneno yangu ya maonyo, kwa
kuwa nimewaandikia waraka mfupi tu. 23 Nataka
mjue kwamba ndugu yetu Timotheo amefunguliwa
kutoka gerezani. Akifika mapema, nitakuja pamoja
naye kuwaona. 24 Wasalimuni viongozi wenu wote na
watakatifu wote. Wale wa kutoka Italia wanawasalimu.
25 Neema iwe nanyi nyote. Amen.

# Yakobo

1 Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Isa
Al-Masihi. 2 Ndugu zangu, hesabuni kuwa ni
furaha tupu mnapopatwa na majaribu mbalimbali,
3 kwa sababu mnajua ya kuwa kujaribiwa kwa
imani yenu huleta saburi. 4 Acheni saburi ikamilishe
kazi yake, ili mpate kuwa wakamilifu na watimilifu,
bila kupungukiwa chochote. 5 Kama mtu yeyote
miongoni mwenu amepungukiwa na hekima, basi
amwombe Mungu, yeye awapaye watu wote kwa
ukarimu wala hana kinyongo, naye atapewa. 6 Lakini
anapoomba, lazima aamini wala asiwe na shaka,
kwa sababu mtu aliye na shaka ni kama wimbi la
bahari, linalopeperushwa na upepo na kutupwa huku
na huko. 7 Mtu kama huyo asidhani ya kuwa atapata
kitu chochote kutoka kwa Bwana Isa. 8 Yeye ni
mtu mwenye nia mbili, mwenye kusitasita katika njia
zake zote. 9 Ndugu asiye na cheo kikubwa yampasa
ajivunie hali hiyo maana ametukuzwa. 10 Lakini yeye
aliye tajiri afurahi kwa kuwa ameshushwa, kwa sababu
atatoweka kama ua la shambani. 11 Kwa maana jua
kali huchomoza na kuyakausha majani ya mmea,
nalo ua lake linaanguka, na uzuri wake unaharibika.
Vivyo hivyo tajiri naye atanyauka akiwa anaendelea
na shughuli zake. 12 Heri mtu anayevumilia wakati
wa majaribu, kwa sababu akiisha kushinda hilo
jaribio atapewa taji lile la uzima Mungu alilowaahidia
wale wanaompenda. 13 Mtu anapojaribiwa asiseme,
"Ninajaribiwa na Mungu." Kwa maana Mungu hawezi
kujaribiwa na maovu wala yeye hamjaribu mtu yeyote.
14 Lakini kila mtu hujaribiwa wakati anapovutwa
na kudanganywa na tamaa zake mwenyewe zilizo
mbaya. 15 Basi ile tamaa mbaya ikishachukua mimba
huzaa dhambi, nayo ile dhambi ikikomaa huzaa
mauti. 16 Ndugu zangu wapendwa, msidanganyike.
17 Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili
hutoka juu, na hushuka kutoka kwa Baba wa mianga,
ambaye kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha
kugeukageuka. 18 Kwa mapenzi yake mwenyewe
alituzaa kwa neno la kweli, kusudi tuwe kama mazao
ya kwanza katika viumbe vyake vyote. 19 Ndugu
zangu wapendwa, fahamuni jambo hili: Kila mtu awe
mwepesi wa kusikiliza, lakini asiwe mwepesi wa
kusema wala wa kukasirika. 20 Kwa maana hasira
ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. 21 Kwa
hiyo, ondoleeni mbali uchafu wote na uovu ambao
umezidi kuwa mwingi, mkalipokee kwa unyenyekevu
lile Neno lililopandwa ndani yenu ambalo laweza
kuokoa nafsi zenu. 22 Basi kuweni watendaji wa
Neno, wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya
nafsi zenu. 23 Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa
Neno wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama
mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo 24 na baada
ya kujiona alivyo, huenda zake na husahau upesi
jinsi alivyo. 25 Lakini yeye anayeangalia kwa makini
katika sheria kamilifu iletayo uhuru, naye akaendelea
kufanya hivyo bila kusahau, bali akatenda alichosikia,
basi atabarikiwa katika kile anachofanya. 26 Kama
mtu akidhani ya kuwa anayo dini lakini hauzuii ulimi
wake kwa hatamu, hujidanganya moyoni mwake,
wala dini yake haifai kitu. 27 Dini iliyo safi, isiyo na
uchafu, inayokubalika mbele za Mungu, Baba yetu,
ndiyo hii: ni kuwasaidia yatima na wajane katika dhiki
zao na kujilinda usitiwe madoa na dunia.

2 Ndugu zangu, waumini katika imani ya Bwana wetu
wa utukufu, Isa Al-Masihi, hawapaswi kuwa na
upendeleo. 2 Je, ikiwa mtu anakuja katika kusanyiko
lenu akiwa amevaa pete ya dhahabu na mavazi
mazuri, na kisha akaingia mtu maskini aliyevaa
mavazi yaliyochakaa. 3 Mkimpa heshima yule aliyevaa
mavazi mazuri na kumwambia, "Keti hapa mahali
pazuri," lakini yule maskini mkamwambia, "Wewe
simama pale," au "Keti hapa sakafuni karibu na miguu
yangu," 4 je, hamjabagua kati yenu wenyewe na
kuwa mahakimu wenye mawazo maovu? 5 Ndugu
zangu, sikilizeni: Je, si Mungu huwachagua wale
walio maskini machoni pa ulimwengu kuwa matajiri
katika imani na kuurithi ufalme aliowaahidi wale
wanaompenda? 6 Lakini ninyi mmemdharau yule aliye
maskini. Je, hao matajiri si ndio wanaowadhulumu na
kuwaburuta mahakamani? 7 Je, si wao wanalikufuru
jina lile bora sana mliloitiwa? 8 Kama kweli mnaitimiza
ile sheria ya kifalme inayopatikana katika Maandiko,
isemayo, "Mpende jirani yako kama unavyoipenda
nafsi yako," mnafanya vyema. 9 Lakini mkiwapendelea
watu, mnatenda dhambi, na sheria inawahukumu
kuwa wakosaji. 10 Kwa maana mtu yeyote anayeishika
sheria yote lakini akajikwaa katika kipengele kimoja
tu, ana hatia ya kuivunja sheria yote. 11 Kwa sababu
yeye aliyesema, "Usizini," alisema pia, "Usiue." Basi
kama huzini lakini unaua, umekuwa mvunjaji wa

sheria. 12 Hivyo semeni na kutenda kama watu
watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru. 13
Kwa kuwa hukumu bila huruma itatolewa kwa mtu
yeyote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda
hukumu. 14 Ndugu zangu, yafaa nini ikiwa mtu
atadai kuwa anayo imani lakini hana matendo? Je,
imani kama hiyo yaweza kumwokoa? 15 Ikiwa ndugu
yako au dada hana mavazi wala chakula, 16 naye
mmoja wenu akamwambia, “Nenda zako kwa amani,
ukaote moto na kushiba,” pasipo kumpatia yale
mahitaji ya mwili aliyopungukiwa, yafaa nini? 17 Vivyo
hivyo, imani peke yake, kama haikuambatana na
matendo, imekufa. 18 Lakini mtu mwingine atasema,
“Wewe unayo imani; mimi ninayo matendo.” Nioneshe
imani yako pasipo matendo nami nitakuonesha imani
yangu kwa matendo. 19 Unaamini kwamba kuna
Mungu mmoja. Vyema! Hata mashetani wanaamini
hivyo na kutetemeka. 20 Ewe mpumbavu! Je,
wataka kujua kwamba imani bila matendo haifai
kitu? 21 Je, Ibrahimu baba yetu hakuhesabiwa
haki kwa kile alichotenda, alipomtoa mwanawe
Isaka madhabahuni? 22 Unaona jinsi imani yake na
matendo yake vilikuwa vinatenda kazi pamoja, nayo
imani yake ikakamilishwa na kile alichotenda. 23
Kwa njia hiyo likatimizwa andiko lisemalo, “Ibrahimu
alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kuwa
haki,” naye akaitwa rafiki wa Mungu. 24 Mnaona
kwamba mtu huhesabiwa haki kwa yale anayotenda
wala si kwa imani peke yake. 25 Vivyo hivyo, hata
Rahabu, yule kahaba: je, hakuhesabiwa haki kwa
yale aliyotenda alipowapokea wale wapelelezi na
kuwaambia waende njia nyingine? 26 Kama vile mwili
pasipo roho umekufa, kadhalika nayo imani pasipo
matendo imekufa.

3 Ndugu zangu, msiwe walimu wengi, kwa
maana mnafahamu kwamba sisi tufundishao
tutahukumiwa vikali zaidi. 2 Sisi sote tunajikwaa
katika mambo mengi. Ikiwa mtu yeyote hakosei
kamwe katika yale anayosema, yeye ni mkamilifu,
naye anaweza kuuzuia pia na mwili wake wote.
3 Tunapotia lijamu kwenye vinywa vya farasi ili
kuwafanya watutii, tunaweza kuigeuza miili yao yote.
4 Au chukua mfano wa meli: ingawa ni kubwa sana,
nazo hupelekwa na upepo mkali, zinaelekezwa kwa
usukani mdogo sana kokote wanakotaka nahodha.
5 Vivyo hivyo ulimi ni kiungo kidogo sana katika
mwili, lakini hujivuna majivuno makuu. Fikirini jinsi
moto mdogo unavyoweza kuteketeza msitu mkubwa!
6 Ulimi pia ni moto, ndio ulimwengu wa uovu kati
ya viungo vya mwili. Ulimi huutia mwili wote wa
mtu unajisi na kuuwasha moto mfumo mzima wa
maisha yake, nao wenyewe huchomwa moto wa
Jehanamu. (Geenna g1067) 7 Kwa maana kila aina ya
wanyama, ndege, wanyama watambaao na viumbe
vya baharini hufugika na hufugwa na binadamu, 8
lakini hakuna mtu awezaye kuufuga ulimi. Ni uovu
usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti. 9 Kwa ulimi
tunamhimidi Mwenyezi Mungu na Baba yetu, na kwa
huo twawalaani watu walioumbwa kwa mfano wa
Mungu. 10 Katika kinywa kile kile hutoka baraka na
laana. Ndugu zangu, haistahili kuwa hivyo. 11 Je,
chemchemi moja inaweza kutoa katika tundu moja
maji matamu na maji ya chumvi? 12 Je, ndugu zangu,
mtini unaweza kuzaa zeituni, au mzabibu kuzaa tini?
Wala chemchemi ya maji ya chumvi haiwezi kutoa
maji matamu. 13 Ni nani aliye na hekima na ufahamu
miongoni mwenu? Basi na aioneshe hiyo kwa maisha
yake mema na kwa matendo yake yaliyotendwa kwa
unyenyekevu utokanao na hekima. 14 Lakini ikiwa
mna wivu na ni wenye chuki na ugomvi mioyoni
mwenu, msijisifu kwa ajili ya hayo wala msiikatae
kweli. 15 Hekima kama hiyo haishuki kutoka mbinguni,
bali ni ya kidunia, isiyo ya kiroho, na ya kishetani.
16 Kwa maana panapokuwa na wivu na ubinafsi,
ndipo penye machafuko na uovu wa kila namna. 17
Lakini hekima inayotoka mbinguni kwanza ni safi,
kisha inapenda amani, tena ni ya upole, iliyo tayari
kusikiliza wengine kwa unyenyekevu, iliyojaa huruma
na matunda mema, isiyopendelea mtu, tena isiyokuwa
na unafiki. 18 Mavuno ya haki hupandwa katika amani
na wale wafanyao amani.

4 Ni kitu gani kinachosababisha mapigano na ugomvi
miongoni mwenu? Je, haya hayatokani na tamaa
zenu zinazoshindana ndani yenu? 2 Mnatamani
lakini hampati, kwa hiyo mwaua. Mwatamani kupata
lakini hampati vile mnavyotaka, kwa hiyo mnajitia
katika magomvi na mapigano. Mmepungukiwa kwa
sababu hammwombi Mungu. 3 Mnapoomba hampati
kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya, ili mpate
kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa zenu.
4 Ninyi wanaume na wanawake wazinzi, hamjui
kwamba urafiki na dunia ni uadui na Mungu? Kwa

hiyo mtu yeyote anayetaka kuwa rafiki wa dunia
hufanyika adui wa Mungu. 5 Au mwadhani kwamba
Maandiko yasema bure kuwa huyo Roho ambaye
Mungu amemweka ndani yetu hututamani kiasi cha
kuona wivu? 6 Lakini yeye hutupatia neema zaidi. Hii
ndiyo sababu Maandiko yasema: “Mungu huwapinga
wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.” 7
Basi mtiini Mungu. Mpingeni ibilisi, naye atawakimbia.
8 Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia. Itakaseni
mikono yenu ninyi wenye dhambi, na kuisafisha
mioyo yenu ninyi wenye nia mbili. 9 Huzunikeni, na
mwomboleze, na kulia. Kicheko chenu na kigeuzwe
kuwa kuomboleza, na furaha yenu kuwa huzuni. 10
Jinyenyekezeni mbele za Mwenyezi Mungu, naye
atawainua. 11 Ndugu, msineneane mabaya ninyi
kwa ninyi. Mtu yeyote anayesema mabaya dhidi
ya ndugu yake au kumhukumu, anasema dhidi ya
sheria na kuihukumu. Unapoihukumu sheria, basi
huishiki sheria, bali umekuwa hakimu wa kuihukumu
hiyo sheria. 12 Yuko Mtoa sheria mmoja tu na yeye
peke yake ndiye Hakimu; ndiye awezaye kuokoa au
kuangamiza. Lakini wewe ni nani hata umhukumu
jirani yako? 13 Basi sikilizeni ninyi msemao, “Leo au
kesho tutaenda katika mji huu ama ule tukae humo
mwaka mmoja, tufanye biashara na kupata faida.” 14
Lakini hamjui hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni
nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana kwa kitambo
kidogo kisha hutoweka. 15 Badala yake, inawapasa
kusema, “Kama Mwenyezi Mungu akipenda, tutaishi
na kufanya hili ama lile.” 16 Ilivyo sasa, mnajisifu na
kujigamba. Kujisifu kote kwa namna hii ni uovu. 17
Basi mtu yeyote anayejua jema limpasalo kutenda,
lakini asilitende, mtu huyo anatenda dhambi.

5 Basi sikilizeni, ninyi matajiri, lieni na kuomboleza
kwa ajili ya hali mbaya sana inayowajia. 2 Utajiri
wenu umeoza, na mavazi yenu yameliwa na nondo.
3 Dhahabu yenu na fedha yenu zimeliwa na kutu.
Kutu yake itashuhudia dhidi yenu, nayo itaila miili
yenu kama vile moto. Mmejiwekea hazina kwa ajili ya
siku za mwisho. 4 Angalieni! Ule ujira wa vibarua
waliolima mashamba yenu mliouzuia kwa hila unapiga
kelele dhidi yenu, na vilio vya wavunaji vimefika
masikioni mwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni. 5 Mmeishi duniani kwa anasa na
kwa starehe; mmejinenepesha tayari kwa siku ya
kuchinjwa. 6 Mmewahukumu na kuwaua watu wenye
haki, waliokuwa hawapingani nanyi. 7 Kwa hiyo,
ndugu zangu, vumilieni hadi kuja kwake Bwana Isa.
Tazameni jinsi mkulima angojavyo ardhi itoe mavuno
yake yaliyo ya thamani, na jinsi anavyovumilia kwa
ajili ya kupata mvua ya kwanza na ya mwisho. 8 Ninyi
nanyi vumilieni, tena simameni imara, kwa sababu
kuja kwa Bwana Isa kumekaribia. 9 Ndugu zangu,
msinung’unikiane, msije mkahukumiwa. Hakimu
amesimama mlangoni! 10 Ndugu zangu, waangalieni
manabii walionena kwa jina la Mwenyezi Mungu,
wakiwa mfano wa uvumilivu katika kukabiliana na
mateso. 11 Kama mnavyojua, tunawahesabu wale
waliovumilia kuwa wabarikiwa. Mmesikia habari za
uvumilivu wake Ayubu, na mmeona kile ambacho
hatimaye Mwenyezi Mungu alimtendea. Mwenyezi
Mungu ni mwingi wa huruma, na amejaa rehema.
12 Zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, iwe kwa
mbingu au kwa dunia, au kwa kitu kingine chochote.
“Ndiyo” yenu na iwe ndiyo, na “Hapana” yenu iwe
hapana, la sivyo mtahukumiwa. 13 Je, mtu yeyote
miongoni mwenu amepatwa na taabu? Basi inampasa
aombe. Je, kuna yeyote mwenye furaha? Basi
na aimbe nyimbo za kusifu. 14 Je, kuna yeyote
miongoni mwenu aliye mgonjwa? Basi inampasa
awaite wazee wa kundi la waumini wamwombee
na kumpaka mafuta kwa Jina la Bwana Isa. 15
Kule kuomba kwa imani kutamwokoa huyo mgonjwa,
naye Bwana Isa atamwinua, na kama ametenda
dhambi, atasamehewa. 16 Kwa hiyo, ungamianeni
dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana ili mpate
kuponywa. Maombi ya mwenye haki yana nguvu,
tena yanafaa sana. 17 Ilya alikuwa mwanadamu kama
sisi. Aliomba kwa bidii kwamba mvua isinyeshe, nayo
haikunyesha juu ya nchi kwa muda wa miaka mitatu
na miezi sita. 18 Kisha akaomba tena, nazo mbingu
zikatoa mvua, nayo ardhi ikatoa mazao yake. 19
Ndugu zangu, yeyote miongoni mwenu akipotoka na
kuicha kweli, naye akarejeshwa na mtu mwingine,
20 hamna budi kujua kwamba yeyote amrejeshaye
mwenye dhambi kutoka upotovu wake, ataiokoa roho
ya huyo mwenye dhambi kutoka mauti na kufunika
wingi wa dhambi.

# 1 Petro

1 Petro, mtume wa Isa Al-Masihi. 2 Ni ninyi ambao
mlichaguliwa tangu mwanzo na Mungu Baba
Mwenyezi kulingana na alivyotangulia kuwajua, kupitia
kwa kazi ya utakaso wa Roho wa Mungu, katika utiifu
kwa Isa Al-Masihi na kunyunyiziwa damu yake. 3
Ahimidiwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Isa Al-
Masihi! Kwa rehema zake kuu, ametuzaa sisi mara ya
pili katika tumaini lenye uzima, kupitia kwa kufufuka
kwa Isa Al-Masihi kutoka kwa wafu, 4 ili tuupate urithi
usioangamia, usioharibika, na usionyauka, uliotunzwa
mbinguni kwa ajili yenu. 5 Nanyi mnalindwa na nguvu
za Mungu kupitia kwa imani, hadi utakapokuja ule
wokovu ulio tayari kufunuliwa nyakati za mwisho.
6 Katika haya yote mnafurahi sana, ijapokuwa kwa
muda mfupi sasa mmehuzunishwa kwa majaribu ya
aina nyingi. 7 Haya yamewajia ili imani yenu, iliyo ya
thamani kuliko dhahabu ipoteayo ingawa inasafishwa
kwa moto, ionekane kuwa halisi, na imalizie kwa sifa,
utukufu na heshima Isa Al-Masihi atakapodhihirishwa.
8 Ijapokuwa hamjamwona, mnampenda; tena ingawa
sasa hammwoni, mnamwamini na kujawa na furaha
yenye utukufu na isiyoelezeka. 9 Maana mnaupokea
wokovu wa roho zenu, ambao ndio lengo la imani
yenu. 10 Kwa habari ya wokovu huu, wale manabii
waliosema kuhusu neema ambayo ingewafikia ninyi,
walitafuta kwa bidii na kwa uangalifu mkubwa.
11 Walijaribu kujua ni wakati upi na ni mazingira
yapi ambayo Roho wa Al-Masihi, aliyekuwa ndani
yao, alionesha alipotabiri mateso ya Al-Masihi na
utukufu ambao ungefuata. 12 Walifunuliwa kwamba
walikuwa wanawahudumia ninyi, bali si wao wenyewe,
waliponena kuhusu mambo hayo. Mmeambiwa
mambo haya sasa na wale waliowahubiria Injili kwa
Roho wa Mungu aliyetumwa kutoka mbinguni. Hata
malaika wanatamani kuyafahamu mambo haya. 13
Kwa hiyo, tayarisheni nia zenu kwa kazi; mwe na kiasi,
mkitumainia kikamilifu ile neema mtakayopewa Isa Al-
Masihi atakapodhihirishwa. 14 Kama watoto watiifu,
msifuate tamaa zenu mbaya wakati mlipoishi kwa
ujinga. 15 Bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu,
nanyi kuweni watakatifu katika mwenendo wenu wote.
16 Kwa maana imeandikwa: “Kuweni watakatifu, kwa
kuwa mimi ni mtakatifu.” 17 Kwa kuwa mnamlilia
Baba anayehukumu kila mtu kulingana na matendo
yake pasipo upendeleo, kaeni kama wageni wakati
wenu duniani, mkiogopa na kumcha Mungu. 18 Kwa
maana mnafahamu kwamba mlikombolewa kutoka
mwenendo wenu usiofaa, ambao mliurithi kutoka kwa
baba zenu. Hamkukombolewa kwa vitu viharibikavyo
kama fedha na dhahabu, 19 bali mlikombolewa kwa
damu ya thamani ya Al-Masihi, yule Mwana-Kondoo
asiye na dosari wala doa. 20 Yeye alichaguliwa
kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, lakini
akadhihirishwa katika nyakati hizi za mwisho kwa
ajili yenu. 21 Kupitia kwake mmemwamini Mungu,
aliyemfufua kutoka kwa wafu na akampa utukufu, ili
imani yenu na tumaini lenu ziwe kwa Mungu. 22 Basi
kwa kuwa mmejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli
hata mkawa na upendo wa ndugu usio na unafiki, basi
pendaneni kwa dhati kutoka moyoni. 23 Kwa maana
mmezaliwa upya, si kwa mbegu inayoharibika, bali
kwa mbegu isiyoharibika, kupitia kwa neno la Mungu
lililo hai na linalodumu milele. **(aiōn g165)** 24 Maana,
“Wanadamu wote ni kama majani, nao utukufu wao
wote ni kama maua ya kondeni; majani hunyauka na
maua huanguka, 25 lakini neno la Mwenyezi Mungu
ladumu milele.” Hili ndilo neno lililohubiriwa kwenu.
**(aiōn g165)**

2 Kwa hiyo, wekeni mbali nanyi uovu wote na
udanganyifu wote, unafiki, wivu na masingizio ya
kila namna. 2 Kama watoto wachanga, waliozaliwa
sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyochanganywa
na kitu kingine chochote, ili kwa hayo mpate kukua
katika wokovu, 3 ikiwa kweli mmeonja kwamba
Bwana Isa ni mwema. 4 Mnapokuja kwake, yeye
aliye Jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu bali
kwa Mungu ni teule na la thamani kwake, 5 ninyi
nanyi, kama mawe yaliyo hai, mnajengwa kuwa
nyumba ya kiroho, ili mpate kuwa ukuhani mtakatifu,
mkitoa dhabihu za kiroho zinazokubaliwa na Mungu
kupitia kwa Isa Al-Masihi. 6 Kwa maana imeandikwa
katika Maandiko: “Tazama, naweka katika Sayuni,
jiwe la pembeni teule lenye thamani, na yeyote
atakayemwamini hataaibishwa kamwe.” 7 Kwenu
ninyi mnaoamini, jiwe hili ni la thamani. Lakini kwao
wasioamini, “Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe
kuu la pembeni,” 8 tena, “Jiwe lenye kuwafanya
watu wajikwae, na mwamba wa kuwaangusha.”
Wanajikwaa kwa sababu hawakulitii lile neno, kama
walivyowekewa tangu zamani. 9 Lakini ninyi ni taifa

teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio
milki ya Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa zake yeye
aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru yake ya
ajabu. **10** Mwanzo ninyi mlikuwa si taifa, lakini sasa
ninyi ni taifa la Mungu. Mwanzo mlikuwa hamjapata
rehema, lakini sasa mmepata rehema. **11** Wapendwa,
ninawasihi, mkiwa kama wageni na wapitaji hapa
ulimwenguni, epukeni tamaa mbaya za mwili ambazo
hupigana vita na roho zenu. **12** Kuweni na mwenendo
mzuri mbele ya watu wasiomjua Mungu, ili kama
wanawasingizia kuwa watenda mabaya, wayaone
matendo yenu mema nao wamtukuze Mungu siku
atakapokuja kwetu. **13** Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,
tiini kila mamlaka iliyowekwa na wanadamu: Awe
ni mfalme kwani ndiye aliye na mamlaka ya juu
zaidi, **14** au wawe maafisa aliowaweka. Kwa kuwa
mfalme amewatuma ili kuwaadhibu wale wanaokosa,
na kuwapongeza wale wanaotenda mema. **15** Kwa
maana ni mapenzi ya Mungu kwamba kwa kutenda
mema myanyamazishe maneno ya kijinga ya watu
wapumbavu. **16** Ishini kama watu huru, lakini msitumie
uhuru wenu kama kisingizio cha kutenda uovu, bali
ishini kama watumishi wa Mungu. **17** Mheshimuni
kila mtu ipasavyo, wapendeni waumini wote, mcheni
Mungu, mpeni heshima mfalme. **18** Ninyi watumwa,
watiini mabwana zenu kwa heshima yote, si wale
mabwana walio wema na wapole peke yao, bali
pia wale walio wakali. **19** Kwa maana ni jambo la
sifa kama mtu akivumilia anapoteswa kwa uonevu
kwa ajili ya Mungu. **20** Kwani ni faida gani kwa
mtu kustahimili anapopigwa kwa sababu ya makosa
yake? Lakini mkiteswa kwa sababu ya kutenda
mema, nanyi mkastahimili, hili ni jambo la kusifiwa
mbele za Mungu. **21** Ninyi mliitwa kwa ajili ya haya,
kwa sababu Al-Masihi naye aliteswa kwa ajili yenu,
akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake. **22**
“Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana
kinywani mwake.” **23** Yeye alipotukanwa, hakurudisha
matukano; alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi
kwa yeye ahukumuye kwa haki. **24** Yeye mwenyewe
alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya
mti, ili tufe kwa mambo ya dhambi, na tupate kuishi
katika haki. Kwa majeraha yake, ninyi mmeponywa.
**25** Kwa maana mlikuwa mmepotea kama kondoo,
lakini sasa mmerudi kwa Mchungaji na Mwangalizi
wa roho zenu.

**3** Kadhalika enyi wake, watiini waume zenu, ili
kama kunao wasioamini lile neno, wapate kuvutwa
na mwenendo wa wake zao pasipo neno, **2** kwa
kuuona utakatifu na uchaji wa Mungu katika maisha
yenu. **3** Kujipamba kwenu kusiwe kwa nje tu, kama
vile kusuka nywele, kuvalia vitu vilivyofanyizwa kwa
dhahabu na kwa mavazi. **4** Badala yake, kujipamba
kwenu kuwe katika utu wenu wa moyoni, yaani uzuri
usioharibika wa roho ya upole na utulivu, ambayo
ni ya thamani sana machoni pa Mungu. **5** Kwa
kuwa hivi ndivyo walivyokuwa wakijipamba wanawake
watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu. Wao
walikuwa ni watiifu kwa waume zao, **6** kama Sara
alivyomtii mumewe Ibrahimu, hata akamwita bwana.
Ninyi ni watoto wa Sara mkitenda yaliyo mema, bila
kuogopa jambo lolote. **7** Vivyo hivyo ninyi waume,
kaeni na wake zenu kwa kuwajali, nanyi wapeni
heshima mkitambua ya kuwa wao ni wenzi walio
dhaifu, na kama warithi pamoja nanyi wa kipawa
cha neema cha uzima, ili kusiwepo na chochote
cha kuzuia maombi yenu. **8** Hatimaye, ninyi nyote
kuweni na nia moja, wenye kuhurumiana, mkipendana
kama ndugu, mkijaliana, na wanyenyekevu. **9** Msilipe
ovu kwa ovu, au jeuri kwa jeuri, bali barikini, kwa
maana hili ndilo mliloitiwa ili mpate kurithi baraka.
**10** Kwa maana, “Yeyote apendaye uzima na kuona
siku njema, basi auzuie ulimi wake usinene mabaya,
na midomo yake isiseme hila. **11** Mtu huyo lazima
aache uovu, akatende mema; lazima aitafute amani
na kuifuatilia sana. **12** Kwa maana macho ya Bwana
huwaelekea wenye haki, na masikio yake yako makini
kusikiliza maombi yao. Bali uso wa Mwenyezi Mungu
uko kinyume na watendao maovu.” **13** Basi, ni nani
atakayewadhuru mkiwa wenye juhudi katika kutenda
mema? **14** Lakini hata ikiwalazimu kuteseka kwa
ajili ya haki, mmebarikiwa. “Msiogope vitisho vyao,
wala msiwe na wasiwasi.” **15** Bali mtukuzeni Al-
Masihi kama Bwana mioyoni mwenu. Siku zote mwe
tayari kumjibu mtu yeyote atakayewauliza kuhusu
sababu ya tumaini lililo ndani yenu. Lakini fanyeni
hivyo kwa upole na kwa heshima, **16** mkizitunza
dhamiri zenu ziwe safi, ili wale wasemao mabaya
dhidi ya mwenendo wenu mzuri katika Al-Masihi
waaibike kwa ajili ya masingizio yao. **17** Kwa maana
ni afadhali kupata mateso kwa ajili ya kutenda mema,
ikiwa ni mapenzi ya Mungu, kuliko kuteseka kwa

kutenda maovu. 18 Kwa kuwa Al-Masihi naye aliteswa
mara moja tu kwa ajili ya dhambi, mwenye haki
kwa ajili ya wasio haki, ili awalete ninyi kwa Mungu.
Mwili wake ukauawa, lakini akafanywa hai katika
Roho wa Mungu. 19 Baada ya kufanywa hai, alienda
na kuzihubiria roho zilizokuwa kifungoni: 20 roho
ambazo zamani hazikutii, wakati ule uvumilivu wa
Mungu ulipokuwa ukingoja katika siku za Nuhu,
wakati wa kujenga safina, ambamo watu wachache
tu, yaani watu wanane, waliokolewa ili wasiangamie
kwa gharika. 21 Nayo maji hayo ni kielelezo cha
ubatizo ambao sasa unawaokoa ninyi pia: si kwa
kuondoa uchafu kwenye mwili, bali kama ahadi ya
dhamiri safi kwa Mungu. Inatuokoa kupitia kwa ufufuo
wa Isa Al-Masihi. 22 Yeye ameingia mbinguni na
amekaa mkono wa kuume wa Mungu; nao malaika,
mamlaka na nguvu zote zimetiishwa chini yake.

**4** Kwa hiyo, kwa kuwa Al-Masihi aliteswa katika mwili
wake, ninyi nanyi jivikeni nia hiyo hiyo kwa maana
mtu aliyekwisha kuteswa katika mwili ameachana na
dhambi. 2 Kwa hivyo, haishi maisha yake yaliyobaki
hapa duniani ili kutimiza tamaa mbaya za wanadamu,
bali anaishi ili kutimiza mapenzi ya Mungu. 3 Kwa
maana wakati uliopita, mmetumia muda mwingi
mkifanya yale wapagani hupenda kutenda: wakiishi
katika uasherati, tamaa mbaya, ulevi, karamu za ulafi,
vileo, ngoma mbaya, na ibada chukizo za sanamu. 4
Wao hushangaa kwamba ninyi hamjiingizi pamoja
nao katika maisha yao ya uovu uliopita kiasi, nao
huwatukana ninyi. 5 Lakini itawapasa wao kutoa
maelezo kwake yeye aliye tayari kuwahukumu walio
hai na waliokufa. 6 Kwa kuwa hii ndiyo sababu Injili
ilihubiriwa hata kwa wale waliokufa, ili wahukumiwe
sawasawa na wanadamu wengine katika mwili, lakini
katika roho waishi kulingana na Mungu aishivyo. 7
Mwisho wa mambo yote umekaribia. Kwa hiyo kuweni
na tahadhari, mkiwa na akili tulivu na kujidhibiti,
mkikesha katika kuomba. 8 Zaidi ya yote, dumuni
katika upendo kwa maana upendo husitiri wingi wa
dhambi. 9 Kuweni wakarimu kila mtu na mwenzake
pasipo manung'uniko. 10 Kila mmoja na atumie
kipawa chochote alichopewa kuwahudumia wengine,
kama mawakili waaminifu wa neema mbalimbali za
Mungu. 11 Yeyote asemaye hana budi kusema kama
mtu asemaye maneno ya Mungu mwenyewe. Yeyote
anayehudumu hana budi kuhudumu kwa nguvu zile
anazopewa na Mungu, ili Mungu apate kutukuzwa
katika mambo yote kupitia kwa Isa Al-Masihi. Utukufu
na uweza una yeye milele na milele. Amen. (aiōn
g165) 12 Wapendwa, msione ajabu kwa yale mateso
yanayotukia miongoni mwenu, kana kwamba ni kitu
kigeni kinachowapata. 13 Bali furahini kuwa mnashiriki
katika mateso ya Al-Masihi, ili mpate kufurahi zaidi
wakati utukufu wake utakapofunuliwa. 14 Mkitukanwa
kwa ajili ya jina la Al-Masihi, mmebarikiwa, kwa
sababu Roho wa utukufu na wa Mungu anakaa juu
yenu. 15 Lakini asiwepo mtu yeyote miongoni mwenu
anayeteswa kwa kuwa ni muuaji, au mwizi, au mhalifu
wa aina yoyote, au anayejishughulisha na mambo ya
watu wengine. 16 Lakini ukiteseka kwa kuwa mfuasi
wa Al-Masihi, usihesabu jambo hilo kuwa ni aibu, bali
mtukuze Mungu kwa sababu umeitwa kwa jina hilo.
17 Kwa maana wakati umewadia wa hukumu kuanzia
katika nyumba ya Mungu. Basi ikianzia kwetu sisi,
mwisho wa hao wasiotii Injili ya Mungu utakuwaje?
18 Basi, "Ikiwa ni vigumu kwa mwenye haki kuokoka,
itakuwaje kwa mtu asiyemcha Mungu na mwenye
dhambi?" 19 Kwa hiyo, wale wanaoteswa kulingana
na mapenzi ya Mungu, wajikabidhi kwa Muumba wao
aliye mwaminifu, huku wakizidi kutenda mema.

**5** Kwa wazee walio miongoni mwenu, nawasihi mimi
nikiwa mzee mwenzenu, shahidi wa mateso ya Al-
Masihi, na mshiriki katika utukufu utakaofunuliwa: 2
lichungeni kundi la Mungu mlilokabidhiwa, mkitumika
kama waangalizi, si kwa kulazimishwa bali kwa hiari,
kama Mungu anavyowataka mwe; si kwa tamaa ya
fedha, bali mlio na bidii katika kutumika. 3 Msijifanye
mabwana juu ya wale walio chini ya uangalizi wenu,
bali kuweni vielelezo kwa hilo kundi. 4 Naye Mchungaji
Mkuu atakapodhihirishwa, mtapokea taji la utukufu
lisiloharibika. 5 Vivyo hivyo, ninyi mlio vijana watiini
wazee. Nanyi nyote jivikeni unyenyekevu kila mtu kwa
mwenzake, kwa kuwa, "Mungu huwapinga wenye
kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema." 6 Basi,
nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari,
ili awakweze kwa wakati wake. 7 Mtwikeni yeye
fadhaa zenu zote, kwa maana yeye anajishughulisha
sana na mambo yenu. 8 Mwe na kiasi na kukesha,
maana adui yenu ibilisi huzungukazunguka kama
simba angurumaye akitafuta mtu ili apate kummeza. 9
Mpingeni, mkiwa thabiti katika imani, mkijua kwamba
mateso kama hayo yanawapata ndugu zenu pote

duniani. 10 Nanyi baada ya kuteswa kwa kitambo
kidogo, Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia
katika utukufu wake wa milele ndani ya Al-Masihi,
yeye mwenyewe atawarejesha na kuwatia nguvu,
akiwaimarisha na kuwathibitisha. **(aiōnios g166)** 11
Uweza una yeye milele na milele. Amen. **(aiōn g165)**
12 Kwa msaada wa Silvano, ninayemhesabu kuwa
ndugu mwaminifu, nimewaandikia waraka huu mfupi
ili kuwatia moyo, na kushuhudia kwamba hii ni neema
halisi ya Mungu. Simameni imara katika neema hiyo.
13 Kundi la waumini lililoko Babeli, lililochaguliwa
pamoja nanyi, wanawasalimu; vivyo hivyo mwanangu
Marko anawasalimu. 14 Salimianeni kwa busu la
upendo. Amani iwe nanyi nyote mlio katika Al-Masihi.

# 2 Petro

**1** Simoni Petro, mtumishi na mtume wa Isa Al-
Masihi. **2** Neema na amani ziwe kwenu kwa wingi
katika kumjua Mungu na Isa Bwana wetu. **3** Uweza
wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji
kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu, kwa kumjua
yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake
mwenyewe. **4** Kwa sababu hiyo, ametukirimia ahadi
zake kuu na za thamani kupitia mambo haya,
ili kupitia hayo mpate kuwa washiriki wa asili ya
uungu, na kuokoka kutoka upotovu ulioko duniani
unaosababishwa na tamaa mbaya. **5** Kwa sababu
hii hasa, jitahidini sana katika imani yenu kuongeza
wema; na katika wema, maarifa; **6** katika maarifa,
kiasi; katika kiasi, saburi; katika saburi, utauwa; **7**
katika utauwa, upendano wa kindugu; na katika
upendano wa kindugu, upendo. **8** Kwa maana haya
yakiwa ndani yenu kwa wingi na kuzidi kuongezeka,
yatawasaidia kutokosa bidii wala kutokuzaa matunda
katika kumjua Bwana wetu Isa Al-Masihi. **9** Lakini
mtu yeyote asipokuwa na mambo haya, haoni mbali
na ni kipofu, naye amesahau kwamba ametakaswa
kutoka dhambi zake za zamani. **10** Kwa hiyo,
ndugu zangu, fanyeni bidii zaidi kuuthibitisha wito
wenu na uteule wenu. Kwa maana mkifanya hivyo,
hamtajikwaa kamwe, **11** na mtajaliwa kwa ukarimu
mwingi kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana
na Mwokozi wetu Isa Al-Masihi. **(aiōnios g166)** **12**
Hivyo nitawakumbusha mambo haya siku zote, hata
ingawa mnayajua na mmethibitishwa katika kweli
mliyo nayo. **13** Naona ni vyema kuwakumbusha
mambo haya wakati wote niko katika hema hili
ambalo ni mwili wangu, **14** kwa sababu najua kwamba
hivi karibuni nitaliweka kando, kama vile Bwana
wetu Isa Al-Masihi alivyoliweka wazi kwangu. **15**
Nami nitafanya kila juhudi kuona kwamba baada ya
kuondoka kwangu mtaweza kuyakumbuka mambo
haya siku zote. **16** Tulipowafahamisha kuhusu uweza
na kuja kwa Bwana wetu Isa Al-Masihi, hatukufuata
hadithi zilizotungwa kwa werevu, bali tulishuhudia
kwa macho yetu ukuu wake. **17** Alipewa heshima na
utukufu kutoka kwa Mungu Baba Mwenyezi, sauti
ilipomjia katika Utukufu Mkuu, ikisema, “Huyu ni
Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa naye sana.”
**18** Sisi wenyewe tuliisikia sauti hii ambayo ilitoka
mbinguni, wakati tulipokuwa pamoja naye kwenye
ule mlima mtakatifu. **19** Nasi tunalo pia neno la
hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vyema
mkiliangalia kwa bidii, kama nuru inavyong’aa gizani,
hadi kupambazuke na nyota ya asubuhi izuke mioyoni
mwenu. **20** Zaidi ya yote, yawapasa mjue kwamba
hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa kama
alivyopenda nabii mwenyewe. **21** Kwa maana unabii
haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali
watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa
na Roho Mtakatifu wa Mungu.

**2** Lakini pia waliinuka manabii wa uongo miongoni
mwa watu, kama watakavyokuwako walimu wa
uongo miongoni mwenu. Wataingiza mafundisho
yasiyopatana na kweli kwa siri, hata kumkana Bwana
Mungu Mwenyezi wa pekee aliyewanunua, na hivyo
kujiletea wenyewe maangamizi ya haraka. **2** Nao
wengi watafuata njia zao potovu, na kwa ajili yao njia
ya kweli itatukanwa. **3** Nao katika tamaa zao mbaya,
walimu hawa watajipatia faida kwenu kwa hadithi
walizotunga wenyewe. Lakini hukumu imekwisha
kutangazwa dhidi yao tangu zamani, wala uangamivu
wao haujalala usingizi. **4** Kwa maana, kama Mungu
hakuwasamehe malaika walipotenda dhambi, bali
aliwatupa Kuzimu katika vifungo vya giza wakae humo
hadi ije hukumu; **(Tartaroō g5020)** **5** kama hakuusamehe
ulimwengu wa kale alipoleta gharika juu ya watu
wale wasiomcha Mungu, lakini akamhifadhi Nuhu,
mhubiri wa haki, pamoja na watu wengine saba; **6**
kama aliihukumu miji ya Sodoma na Gomora kwa
kuiteketeza kwa moto ikawa majivu, na kuifanya kuwa
kielelezo kwa yale yatakayowapata wale wasiomcha
Mungu; **7** na kama alimwokoa Lutu, mtu mwenye haki,
ambaye alihuzunishwa na maisha machafu ya watu
wapotovu **8** (kwa sababu yale matendo mapotovu
aliyoyaona na kuyasikia huyo mtu mwenye haki
alipoishi miongoni mwao yalimhuzunisha siku baada
ya siku): **9** ikiwa hivyo ndivyo, basi Mwenyezi Mungu
anajua jinsi ya kuwaokoa wamchao Mungu kutoka
majaribu, na kuwaweka waasi katika adhabu hadi siku
ya hukumu. **10** Hii ni hakika hasa kwa wale wanaofuata
tamaa mbaya za mwili na kudharau mamlaka. Kwa
ushupavu na kwa kiburi, watu hawa hawaogopi kunena
mabaya dhidi ya viumbe vya mbinguni. **11** Lakini
hata malaika, ijapokuwa wana nguvu na uwezo zaidi,
hawaleti mashtaka mabaya dhidi ya viumbe kama

hao mbele za Mwenyezi Mungu. **12** Lakini watu hawa
hukufuru katika mambo wasiyoyafahamu. Wao ni
kama wanyama wasio na akili, viumbe wanaotawaliwa
na hisia za mwili, waliozaliwa ili wakamatwe na
kuchinjwa. Hawa nao kama wanyama wataangamizwa
pia. **13** Watalipwa madhara kwa ajili ya madhara
waliyowatendea wengine. Huhesabu kuwa ni fahari
kufanya karamu za ulevi na ulafi mchana peupe. Wao
ni mawaa na dosari, wakijifurahisha katika anasa zao
wanaposhiriki karamu pamoja nanyi. **14** Wakiwa na
macho yaliyojaa uzinzi, kamwe hawaachi kutenda
dhambi. Huwashawishi wale wasio imara. Wao ni
hodari kwa kutamani; ni wana wa laana! **15** Wameiacha
njia iliyo nyoofu, wakapotoka na kuifuata njia ya
Balaamu mwana wa Beori aliyependa mshahara wa
uovu. **16** Lakini kwa ajili ya uovu wake, alikemewa na
punda, mnyama asiyejua kusema, alipoongea kwa
sauti ya mwanadamu na kuzuia wazimu wa huyo
nabii. **17** Watu hawa ni chemchemi zisizo na maji,
na ukungu unaopeperushwa na tufani. Giza nene
limewekwa tayari kwa ajili yao. **18** Kwa maana wao
hunena maneno matupu ya kiburi. Nao wanavutia
tamaa mbaya za asili ya mwili, ili kuwashawishi
watu ambao wanajiondoa kutoka kwa wale wanaoishi
katika hatia. **19** Wanawaahidi uhuru wakati wao
wenyewe ni watumwa wa upotovu; kwa maana "mtu
ni mtumwa wa chochote kinachomtawala." **20** Kama
wameukimbia upotovu wa dunia kwa kumjua Bwana
wetu na Mwokozi Isa Al-Masihi, kisha wakanaswa tena
humo na kushindwa, hali yao ya mwisho ni mbaya
kuliko ile ya kwanza. **21** Ingekuwa afadhali kwao
kama hawangeijua kamwe njia ya haki, kuliko kuijua
kisha wakaiacha ile amri takatifu waliyokabidhiwa. **22**
Kwao mithali zimetukia kuwa za kweli, zinaposema:
"Mbwa huyarudia matapiko yake mwenyewe," tena,
"Nguruwe aliyeoshwa hurudi kugaagaa matopeni."

**3** Wapendwa, huu ndio waraka wangu wa pili
ninaowaandikia. Katika nyaraka hizi mbili ninajaribu
kuziamsha nia zenu safi kwa mawazo makamilifu.
**2** Nataka ninyi mkumbuke maneno yaliyosemwa
zamani na manabii watakatifu na ile amri ya Bwana na
Mwokozi wetu mliyopewa kupitia kwa mitume wenu.
**3** Kwanza kabisa, ni lazima mfahamu kwamba siku za
mwisho watakuja watu wenye dhihaka, wakidhihaki na
kuzifuata tamaa zao mbovu. **4** Watasema, "Iko wapi
ile ahadi ya kuja kwake? Tangu baba zetu walipofariki,
kila kitu kinaendelea kama kilivyokuwa tangu mwanzo
wa kuumbwa." **5** Lakini wao kwa makusudi hupuuza
ukweli huu, kwamba kwa neno la Mungu mbingu
zilikuwa tangu zamani, nayo dunia ilifanyizwa kutoka
ndani ya maji na kwa maji. **6** Ulimwengu wa wakati ule
uligharikishwa kwa hayo maji na kuangamizwa. **7** Kwa
neno lilo hilo, mbingu za sasa na dunia zimewekwa
akiba kwa ajili ya moto, zikihifadhiwa hadi siku ile ya
hukumu na ya kuangamizwa kwa watu wasiomcha
Mungu. **8** Lakini wapendwa, msisahau neno hili:
kwamba kwa Mwenyezi Mungu, siku moja ni kama
miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. **9**
Mwenyezi Mungu hakawii kuitimiza ahadi yake, kama
watu wengine wanavyokudhani kukawia. Badala
yake, yeye anawavumilia ninyi, maana hataki mtu
yeyote aangamie, bali kila mtu afikilie toba. **10** Lakini
siku ya Mwenyezi Mungu itakuja kama mwizi. Ndipo
mbingu zitatoweka kwa kishindo kikuu; navyo vitu
vya asili vitateketezwa kwa moto, nayo dunia na kila
kitu kilicho ndani yake kitaunguzwa. **11** Kwa kuwa
vitu vyote vitaharibiwa namna hii, je, ninyi imewapasa
kuwa watu wa namna gani? Inawapasa kuishi maisha
matakatifu na ya kumcha Mungu, **12** mkingojea na
kuhimiza kuja kwa hiyo siku ya Mungu. Siku hiyo
italeta mbingu kuchomwa moto na kutoweka, na vitu
vya asili vitayeyuka kwa moto. **13** Lakini kufuatana
na ahadi yake, sisi tunatazamia mbingu mpya na
dunia mpya, ambayo haki hukaa ndani yake. **14**
Kwa sababu hii, wapendwa, kwa kuwa mnatazamia
mambo haya, fanyeni bidii ili awakute bila mawaa
wala dosari, na mkiwa na amani kwake. **15** Hesabuni
uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama
vile ndugu yetu mpendwa Paulo alivyowaandikia kwa
hekima ile aliyopewa na Mungu. **16** Huandika vivyo
hivyo katika nyaraka zake zote, akizungumzia ndani
yake mambo haya. Katika nyaraka zake kuna mambo
mengine ambayo ni vigumu kuyaelewa, ambayo
watu wajinga na wasio thabiti huyapotosha, kama
wanavyopotosha Maandiko mengine na kujiletea
maangamizi yao wenyewe. **17** Basi, ninyi wapendwa,
kwa kuwa mmekwisha kujua mambo haya, jilindeni
msije mkachukuliwa na kosa la watu hao waasi na
kuanguka kutoka kwa uthabiti wenu. **18** Bali kueni
katika neema na katika kumjua Bwana na Mwokozi
wetu Isa Al-Masihi. Utukufu una yeye sasa na milele!
Amen. **(aiōn g165)**

# 1 Yohana

**1** Tunawajulisha lile lililokuwako tangu mwanzo, lile
tulilosikia, ambalo tumeliona kwa macho yetu,
ambalo tumelitazama na kuligusa kwa mikono yetu,
kuhusu Neno la uzima. 2 Uzima huo ulidhihirishwa;
nasi tumeuona na kuushuhudia, nasi twawatangazia
uzima wa milele, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao
ukadhihirishwa kwetu. **(aiōnios g166)** 3 Twawatangazia
lile tulililoliona na kulisikia, ili nanyi mwe na ushirika
nasi. Na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba
na Mwanawe, Isa Al-Masihi. 4 Tunaandika mambo
haya ili furaha yetu ipate kuwa timilifu. 5 Huu ndio
ujumbe tuliosikia kutoka kwake na kuwatangazia ninyi:
kwamba Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza
lolote. 6 Tukisema kwamba twashirikiana naye huku
tukienenda gizani, twasema uongo, wala hatutendi lililo
kweli. 7 Lakini tukienenda nuruni, kama yeye alivyo
nuruni, twashirikiana sisi kwa sisi na damu yake Isa,
Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. 8 Tukisema
kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe
wala kweli haimo ndani yetu. 9 Tukiziungama dhambi
zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe
dhambi zetu na kutusafisha kutokana na udhalimu
wote. 10 Tukisema hatujatenda dhambi, twamfanya
yeye kuwa mwongo na neno lake halimo ndani yetu.

**2** Watoto wangu wapendwa, nawaandikia haya ili
msitende dhambi. Lakini mtu yeyote akitenda
dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba: ndiye Isa Al-
Masihi, Mwenye Haki. 2 Yeye ndiye dhabihu ya
upatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, wala si kwa
ajili ya dhambi zetu tu, bali pia kwa ajili ya dhambi
za ulimwengu wote. 3 Basi katika hili twajua ya
kuwa tumemjua, tukizishika amri zake. 4 Mtu yeyote
asemaye kuwa, “Ninamjua,” lakini hazishiki amri
zake, ni mwongo, wala ndani ya mtu huyo hamna
kweli. 5 Lakini mtu yeyote anayelitii neno lake,
upendo wa Mungu umekamilika ndani yake kweli
kweli. Katika hili twajua kuwa tumo ndani yake: 6
Yeyote anayesema anakaa ndani yake hana budi
kuenenda kama Isa alivyoenenda. 7 Wapendwa,
siwaandikii ninyi amri mpya bali ile ya zamani, ambayo
mmekuwa nayo tangu mwanzo. Amri hii ya zamani
ni lile neno mlilosikia. 8 Lakini nawaandikia amri
mpya, yaani lile neno lililo kweli ndani yake na
ndani yenu, kwa sababu giza linapita na ile nuru ya
kweli tayari inang’aa. 9 Yeyote anayesema yumo
nuruni lakini anamchukia ndugu yake bado yuko
gizani. 10 Yeye ampendaye ndugu yake anakaa
nuruni, wala hakuna kitu chochote ndani yake cha
kumkwaza. 11 Lakini yeyote amchukiaye ndugu
yake, yuko gizani na anaenenda gizani, wala hajui
anakoenda, kwa sababu giza limempofusha macho.
12 Nawaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa sababu
dhambi zenu zimesamehewa kwa ajili ya Jina lake. 13
Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua
yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi vijana
kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nawaandikia
ninyi watoto wadogo, kwa sababu mmemjua Baba.
14 Nawaandikia ninyi akina baba, kwa sababu
mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia
ninyi vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la
Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule
mwovu. 15 Msiupende ulimwengu wala mambo yaliyo
ulimwenguni. Mtu yeyote akiupenda ulimwengu,
upendo wa Baba haumo ndani yake. 16 Kwa maana
kila kitu kilichomo ulimwenguni, yaani tamaa ya mwili,
tamaa ya macho na kiburi cha uzima, havitokani
na Baba bali hutokana na ulimwengu. 17 Nao
ulimwengu unapita, pamoja na tamaa zake, bali
yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu milele.
**(aiōn g165)** 18 Watoto wadogo, huu ni wakati wa
mwisho! Kama mlivyosikia kwamba anayempinga Al-
Masihi anakuja, hivyo basi wanaompinga Al-Masihi
wengi wamekwisha kuja. Kutokana na hili twajua
kwamba huu ni wakati wa mwisho. 19 Walitoka kwetu,
lakini hawakuwa wa kwetu hasa. Kwa maana kama
wangekuwa wa kwetu, wangekaa pamoja nasi; lakini
kutoka kwao kulionesha kwamba hakuna hata mmoja
wao aliyekuwa wa kwetu. 20 Lakini ninyi mmepakwa
mafuta na yeye Aliye Mtakatifu, nanyi nyote mnaijua
kweli. 21 Siwaandikii kwa sababu hamuijui kweli,
bali kwa sababu mnaijua, nanyi mnajua hakuna
uongo unaotoka katika kweli. 22 Je, mwongo ni
nani? Mwongo ni mtu yule asemaye kwamba Isa si
Al-Masihi. Mtu kama huyo ndiye anayempinga Al-
Masihi, yaani yeye humkana Baba na Mwana. 23
Hakuna yeyote amkanaye Mwana aliye na Baba.
Yeyote anayemkubali Mwana anaye na Baba pia. 24
Bali ninyi, hakikisheni kwamba lile mlilosikia tangu
mwanzo linadumu ndani yenu. Kama lile mlilosikia
tangu mwanzo linakaa ndani yenu, ninyi nanyi mtakaa

ndani ya Mwana na ndani ya Baba. 25 Hii ndiyo
ahadi yake kwetu, yaani uzima wa milele. (aiōnios
g166) 26 Nawaandikia mambo haya kuhusu wale
watu ambao wanajaribu kuwapotosha. 27 Bali ninyi,
upako mlioupata kutoka kwake unadumu ndani yenu,
wala ninyi hamna haja ya mtu yeyote kuwafundisha.
Lakini kama vile upako wake unavyowafundisha
kuhusu mambo yote nayo ni kweli wala si uongo,
basi kama ulivyowafundisha kaeni ndani yake. 28
Sasa basi, watoto wapendwa, kaeni ndani yake,
ili atakapofunuliwa, tuwe na ujasiri, wala tusiaibike
mbele zake wakati wa kuja kwake. 29 Mkijua kuwa
yeye ni mwenye haki, mwajua kwamba kila atendaye
haki amezaliwa naye.

3 Tazameni ni pendo kuu namna gani alilotupatia
Baba, kwamba sisi tuitwe wana wa Mungu!
Na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu
haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye. 2
Wapendwa, sasa tu wana wa Mungu, lakini bado
haijadhihirika tutakavyokuwa, lakini twajua kwamba
yeye atakapodhihirishwa, tutafanana naye, kwa
maana tutamwona kama alivyo. 3 Kila mmoja mwenye
matumaini haya ndani yake hujitakasa, kama vile yeye
alivyo mtakatifu. 4 Kila mtu atendaye dhambi afanya
uasi, kwa kuwa dhambi ni uasi. 5 Lakini mwajua ya
kuwa yeye alidhihirishwa ili aziondoe dhambi, wala
ndani yake hamna dhambi. 6 Kila mtu akaaye ndani
yake hatendi dhambi. Kila mtu atendaye dhambi
hakumwona yeye wala hakumtambua. 7 Watoto
wapendwa, mtu yeyote asiwadanganye. Kila mtu
atendaye haki ana haki, kama yeye alivyo na haki.
8 Yeye atendaye dhambi ni wa ibilisi, kwa sababu
ibilisi amekuwa akitenda dhambi tangu mwanzo.
Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa,
ili aziangamize kazi za ibilisi. 9 Yeyote aliyezaliwa
na Mungu hatendi dhambi, kwa sababu uzao wa
Mungu wakaa ndani yake, wala hawezi kutenda
dhambi kwa sababu amezaliwa na Mungu. 10 Kwa
jinsi hii tunaweza kujua dhahiri watoto wa Mungu
na pia watoto wa ibilisi. Yeyote asiyetenda haki
hatokani na Mungu, wala yeye asiyempenda ndugu
yake. 11 Hili ndilo neno mlilolisikia tangu mwanzo:
Kwamba imetupasa tupendane sisi kwa sisi. 12 Msiwe
kama Kaini aliyekuwa wa yule mwovu akamuua
ndugu yake. Basi kwa nini alimuua? Ni kwa sababu
matendo yake Kaini yalikuwa mabaya na ya ndugu
yake yalikuwa ya haki. 13 Ndugu zangu, ninyi
msistaajabu kama ulimwengu ukiwachukia. 14 Sisi
tunajua kwamba tumepita mautini kuingia uzimani,
kwa sababu tunawapenda ndugu. Kila asiyempenda
ndugu yake akaa mautini. 15 Yeyote amchukiaye
ndugu yake ni muuaji, nanyi mwajua kwamba muuaji
hana uzima wa milele ndani yake. (aiōnios g166) 16
Kwa namna hii twaweza kulijua pendo la Mungu: Kwa
sababu Isa Al-Masihi aliutoa uhai wake kwa ajili yetu.
Nasi imetupasa kuutoa uhai kwa ajili ya hao ndugu.
17 Ikiwa mtu anavyo vitu vya ulimwengu huu na
akamwona ndugu yake ni mhitaji lakini asimhurumie,
upendo wa Mungu wakaaje ndani ya mtu huyo? 18
Watoto wapendwa, tusipende kwa maneno au kwa
ulimi bali kwa tendo na kweli. 19 Basi hivi ndivyo
tutakavyoweza kujua ya kuwa sisi tu wa kweli na
hivyo twaithibitisha mioyo yetu mbele za Mungu 20
kila mara mioyo yetu inapotuhukumu. Kwa maana
Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu, naye anajua kila
kitu. 21 Wapendwa, kama mioyo yetu haituhukumu,
tunao ujasiri mbele za Mungu, 22 lolote tuombalo,
twalipokea kutoka kwake, kwa sababu tumezitii amri
zake na kutenda yale yanayompendeza. 23 Hii ndiyo
amri yake: kwamba tuliamini Jina la Mwanawe, Isa
Al-Masihi, na kupendana sisi kwa sisi kama yeye
alivyotuamuru. 24 Wale wote wanaozishika amri zake
hukaa ndani yake na yeye ndani yao. Hivi ndivyo
tunavyojua kwamba anakaa ndani yetu. Nasi twajua
hili kupitia kwa Roho wa Mungu, yule aliyetupatia.

4 Wapendwa, msiamini kila roho, bali zijaribuni
hizo roho mwone kama zimetoka kwa Mungu,
kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea
ulimwenguni. 2 Hivi ndivyo mnavyoweza kutambua
Roho wa Mungu: Kila roho inayokubali kwamba Isa
Al-Masihi amekuja katika mwili yatoka kwa Mungu.
3 Lakini kila roho ambayo haimkubali Isa haitoki
kwa Mungu. Hii ndiyo roho ya anayempinga Al-
Masihi, ambayo mmesikia kwamba inakuja na sasa
tayari iko ulimwenguni. 4 Watoto wapendwa, ninyi
mmetokana na Mungu, nanyi mmewashinda kwa
sababu yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye
aliye katika ulimwengu. 5 Wao wanatokana na
ulimwengu na kwa hiyo hunena yaliyo ya ulimwengu,
hivyo ulimwengu huwasikiliza. 6 Sisi twatokana na
Mungu na yeyote anayemjua Mungu hutusikiliza,
lakini asiyetokana na Mungu hatusikilizi. Hivi ndivyo

tunavyoweza kutambua Roho wa Kweli na roho ya
upotovu. 7 Wapendwa, tupendane, kwa kuwa pendo
latoka kwa Mungu. Kila apendaye amezaliwa na
Mungu, naye anamjua Mungu. 8 Yeye asiyependa
hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni pendo. 9 Hivi
ndivyo Mungu alivyoonesha pendo lake kwetu: Mungu
alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ili tupate
uzima kupitia kwake. 10 Hili ndilo pendo: si kwamba
tulimpenda Mungu, bali yeye alitupenda, akamtuma
Mwanawe, ili yeye awe dhabihu ya upatanisho kwa
ajili ya dhambi zetu. 11 Wapendwa, kama Mungu
alivyotupenda sisi, imetupasa na sisi kupendana.
12 Hakuna mtu yeyote aliyemwona Mungu wakati
wowote. Lakini tukipendana, Mungu anakaa ndani
yetu, na pendo lake limekamilika ndani yetu. 13
Tunajua kwamba twakaa ndani yake na yeye ndani
yetu, kwa sababu ametupatia sisi sehemu ya Roho
wake Mtakatifu. 14 Nasi tumeona na kushuhudia
kwamba Baba amemtuma Mwanawe ili awe Mwokozi
wa ulimwengu. 15 Kila akiriye kwamba Isa ni Mwana
wa Mungu, basi Mungu hukaa ndani yake, naye
ndani ya Mungu. 16 Hivyo nasi twajua na kulitumainia
pendo la Mungu alilo nalo kwa ajili yetu. Mungu ni
Upendo. Kila akaaye katika upendo hukaa ndani ya
Mungu na Mungu hukaa ndani yake. 17 Kwa njia hii,
pendo hukamilishwa miongoni mwetu ili tupate kuwa
na ujasiri katika siku ya hukumu, kwa sababu kama
alivyo ndivyo tulivyo sisi katika ulimwengu huu. 18
Katika pendo hakuna hofu. Lakini pendo lililo kamili
huitupa nje hofu, kwa sababu hofu inahusika na
adhabu. Kila mwenye hofu hakukamilika katika pendo.
19 Twampenda yeye kwa sababu yeye alitupenda
kwanza. 20 Ikiwa mtu atasema, “Nampenda Mungu,”
lakini anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo. Kwa
maana kila mtu asiyempenda ndugu yake ambaye
anamwona, atampendaje Mungu asiyemwona? 21
Naye ametupatia amri hii: Yeyote anayempenda
Mungu lazima pia ampende ndugu yake.

**5** Kila mtu anayeamini kwamba Isa ndiye Al-Masihi
amezaliwa na Mungu, na yeyote ampendaye
Baba humpenda pia mtoto aliyezaliwa naye. 2 Hivi
ndivyo tunavyojua kwamba tunawapenda watoto wa
Mungu, kwa kumpenda Mungu na kuzitii amri zake.
3 Huku ndiko kumpenda Mungu, yaani kuzitii amri
zake. Nazo amri zake si nzito. 4 Kwa maana kila
aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku
ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, yaani hiyo
imani yetu. 5 Ni nani yule aushindaye ulimwengu?
Ni yule tu aaminiye kwamba Isa ni Mwana wa
Mungu. 6 Huyu ndiye alikuja kwa maji na damu,
yaani Isa Al-Masihi. Hakuja kwa maji peke yake, bali
kwa maji na damu. Naye Roho wa Mungu ndiye
ashuhudiaye, kwa sababu Roho ndiye kweli. 7 Kwa
maana wako watatu washuhudiao [mbinguni: hao
ni Baba, Neno na Roho wa Mungu. Hawa watatu ni
umoja. 8 Pia wako mashahidi watatu duniani]: hao ni
Roho, Maji na Damu; hawa watatu wanakubaliana
katika umoja. 9 Kama tunaukubali ushuhuda wa
wanadamu, basi ushuhuda wa Mungu ni mkuu zaidi,
kwa kuwa huu ndio ushuhuda wa Mungu kwamba
amemshuhudia Mwanawe. 10 Kila mtu amwaminiye
Mwana wa Mungu anao huu ushuhuda moyoni
mwake. Kila mtu asiyemwamini Mungu amemfanya
yeye kuwa mwongo, kwa sababu hakuamini ushuhuda
Mungu alioutoa kuhusu Mwanawe. 11 Huu ndio
ushuhuda: kwamba Mungu ametupatia uzima wa
milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. **(aiōnios
g166)** 12 Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima,
yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima. 13
Nawaandikia mambo haya ninyi mnaoliamini Jina la
Mwana wa Mungu ili mpate kujua ya kuwa mnao
uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 14 Huu ndio ujasiri tulio
nao tunapomkaribia Mungu, kwamba tukiomba kitu
sawasawa na mapenzi yake, atusikia. 15 Nasi kama
tunajua atusikia, lolote tuombalo, tunajua kwamba
tumekwisha kupata zile haja tulizomwomba. 16 Mtu
akimwona ndugu yake akitenda dhambi isiyo ya
mauti, inampasa aombe, naye Mungu atampa uzima
mtu huyo. Ninamaanisha wale ambao dhambi yao
si ya mauti. Iko dhambi ya mauti, sisemi kwamba
utaomba kwa ajili ya hiyo. 17 Jambo lolote lisilo la
haki ni dhambi, lakini iko dhambi isiyo ya mauti. 18
Tunajua ya kuwa yeye aliyezaliwa na Mungu hatendi
dhambi, bali aliyezaliwa na Mungu hujilinda, wala
yule mwovu hawezi kumdhuru. 19 Sisi twajua kuwa
tu watoto wa Mungu na kwamba ulimwengu wote
uko chini ya utawala wa yule mwovu. 20 Nasi pia
twajua kwamba Mwana wa Mungu amekuja, naye
ametupatia sisi ufahamu ili tupate kumjua yeye aliye
Kweli. Nasi tumo ndani yake yeye aliye Kweli, yaani
ndani ya Isa Al-Masihi Mwanawe. Yeye ndiye Mungu
wa kweli na uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 21 Watoto

wapendwa, jilindeni nafsi zenu kutokana na sanamu.
Amen.

# 2 Yohana

1 Mzee. 2 kwa sababu ya ile kweli inayokaa ndani
yetu, na ambayo itaendelea kukaa nasi milele.
**(aiōn g165)** 3 Neema, rehema na amani zinazotoka
kwa Mungu Baba Mwenyezi na kwa Isa Al-Masihi,
Mwanawe Baba, zitakuwa pamoja nasi katika kweli na
upendo. 4 Imenipa furaha kuu kuona baadhi ya watoto
wako wanaenenda katika kweli, kama vile Baba
alivyotuagiza. 5 Sasa, mama mteule mpendwa, si
kwamba ninakuandikia amri mpya, bali ile tuliyokuwa
nayo tangu mwanzo. Tupendane kila mmoja na
mwenzake. 6 Hili ndilo pendo: kwamba tuenende
kwa kuzitii amri zake. Hii ndiyo amri yake kama vile
mlivyosikia tangu mwanzo, kwamba mwenende katika
upendo. 7 Wadanganyifu wengi, wasiokubali kwamba
Isa Al-Masihi amekuja katika mwili, wametawanyika
ulimwenguni. Mtu kama huyo ni mdanganyifu na
anampinga Al-Masihi. 8 Jihadharini msije mkapoteza
kile mlichokitenda, bali mpate kupewa thawabu
kamilifu. 9 Mtu yeyote asiyedumu katika mafundisho ya
Al-Masihi bali ameyaacha, yeye hana Mungu. Yeyote
anayedumu katika mafundisho ana Baba na Mwana
pia. 10 Msimpokee mtu yeyote anayewajia ambaye
hawaletei mafundisho haya, wala msimkaribishe
nyumbani mwenu. 11 Yeyote amkaribishaye mtu
kama huyo anashiriki katika matendo yake maovu. 12
Ninayo mengi ya kuwaandikia, lakini sitaki kutumia
karatasi na wino. Badala yake, nataraji kuja kwenu
na kuongea nanyi ana kwa ana, ili furaha yetu
ipate kuwa timilifu. 13 Watoto wa dada yako mteule
wanakusalimu. Amen.

# 3 Yohana

1 Mzee. 2 Mpendwa, naomba ufanikiwe katika
mambo yote na kuwa na afya njema kama vile
roho yako ifanikiwavyo. 3 Ilinifurahisha sana baadhi
ya ndugu walipokuja na kutueleza kuhusu uaminifu
wako katika kweli na jinsi unavyoendelea kuenenda
katika hiyo kweli. 4 Sina furaha kubwa kuliko hii, ya
kusikia kwamba watoto wangu wanaenenda katika
kweli. 5 Rafiki mpendwa, wewe ni mwaminifu kwa yale
unayowatendea ndugu, ingawa wao ni wageni kwako.
6 Wameshuhudia kuhusu upendo wako mbele ya
jumuiya ya waumini. Utafanya vyema ukiwasafirisha
kama inavyostahili kwa Mungu. 7 Ilikuwa ni kwa
ajili ya hilo Jina waliondoka, bila kukubali kupokea
msaada wowote kutoka kwa watu wasiomwamini Al-
Masihi. 8 Kwa hiyo imetupasa sisi kuonesha ukarimu
kwa watu kama hao ili tuweze kutenda kazi pamoja
kwa ajili ya kweli. 9 Nililiandikia kundi la waumini,
lakini Deotrefe, yeye apendaye kujifanya wa kwanza,
hakubali mamlaka yetu. 10 Hivyo nikija, nitakumbuka
matendo yake atendayo, akitusingizia kwa maneno ya
hila. Wala hatosheki na hayo anayotusingizia, bali pia
hukataa kuwakaribisha ndugu, na hata huwazuia wale
walio tayari kufanya hivyo na kuwafukuza watoke
miongoni mwa waumini. 11 Rafiki mpendwa, usiige
lile lililo baya bali lile lililo jema. Yeyote atendaye
mema anatoka kwa Mungu, bali atendaye mabaya
hajamwona Mungu. 12 Kila mtu ameshuhudia mema
kuhusu Demetrio, vivyo hivyo hata na hiyo kweli
yenyewe. Sisi pia twashuhudia mema juu yake,
nanyi mwajua kwamba ushuhuda wetu ni kweli. 13
Ninayo mambo mengi ya kukuandikia, lakini sipendi
kuandika kwa kalamu na wino. 14 Badala yake,
nataraji kukuona upesi, nasi tutaongea pamoja ana
kwa ana. Amani iwe kwako. Rafiki zetu walio hapa
wanakusalimu. Wasalimu hao rafiki zetu walio huko,
kila mmoja kwa jina lake.

# Yuda

1 Yuda, mtumwa wa Isa Al-Masihi, na nduguye
Yakobo. 2 Rehema, amani na upendo ziwe
kwenu kwa wingi. 3 Wapendwa, ingawa nilikuwa
ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao
tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia
na kuwasihi kwamba mwitetee imani iliyokabidhiwa
watakatifu kwa nafasi moja itoshayo. 4 Kwa kuwa
kuna watu waliojipenyeza kwa siri kati yenu, watu
walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, waovu,
wanaopotosha neema ya Mungu, na kuifanya kuwa
ruhusa ya kutenda maovu, wakimkana Isa Al-
Masihi, ambaye pekee ni Mtawala wetu mkuu na
Bwana wetu. 5 Ingawa mmekwisha kujua haya
yote, nataka niwakumbushe kuwa Mwenyezi Mungu,
akiisha kuwaokoa watu wake kutoka nchi ya Misri,
baadaye aliwaangamiza wale ambao hawakuamini. 6
Nao malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini
wakayaacha makao yao, hawa amewaweka katika
giza, wakiwa wamefungwa kwa minyororo ya milele
kwa ajili ya hukumu Siku ile kuu. **(aïdios g126)** 7
Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora na pia ile miji
iliyokuwa kandokando, ambayo kwa jinsi moja na
hao, walijifurahisha kwa uasherati na kufuata tamaa
za mwili zisizo za asili, waliwekwa wawe mfano kwa
kuadhibiwa katika moto wa milele. **(aiōnios g166)** 8
Vivyo hivyo, hawa waotao ndoto huutia mwili unajisi,
hukataa kuwa chini ya mamlaka na kunena mabaya
juu ya wenye mamlaka. 9 Lakini hata malaika mkuu
Mikaeli alipokuwa anashindana na ibilisi kuhusu mwili
wa Musa, hakuthubutu kumlaumu, bali alimwambia,
“Mwenyezi Mungu na akukemee!” 10 Lakini watu hawa
hunena mabaya dhidi ya mambo wasiyoyafahamu.
Na katika mambo yale wanayoyafahamu kwa hisia
kama wanyama wasio na akili, hayo ndiyo hasa
yatakayowaangamiza. 11 Ole wao! Kwa kuwa
wanaifuata njia ya Kaini, wamekimbilia faida katika
kosa la Balaamu na kuangamia katika uasi wa Kora.
12 Watu hawa ni dosari katika karamu zenu za
upendo, wakila pamoja nanyi bila hofu, wakijilisha
wenyewe tu. Wao ni mawingu yasiyokuwa na maji,
yakichukuliwa na upepo, miti isiyo na matunda wakati
wa mapukutiko, ambayo hunyauka, iliyokufa mara
mbili na kung’olewa kabisa. 13 Wao ni mawimbi
makali ya bahari, yakitoa povu la aibu yao wenyewe,
ni nyota zipoteazo, ambao weusi wa giza ndio akiba
waliowekewa milele. **(aiōn g165)** 14 Idrisi, mtu wa
saba kuanzia Adamu, alitoa unabii kuhusu watu
hawa, akisema: “Tazama, Mwenyezi Mungu anakuja
pamoja na maelfu kwa maelfu ya watakatifu wake,
15 ili kumhukumu kila mmoja na kuwapatiliza wote
wasiomcha Mungu kwa matendo yao yote ya uasi
waliyoyatenda, pamoja na maneno yote ya kuchukiza
ambayo wenye dhambi wamesema dhidi yake.” 16
Watu hawa ni wenye kunung’unika na wenye kutafuta
makosa; wao hufuata tamaa zao mbovu; hujisifu
kwa maneno makuu, na kuwasifu mno watu wengine
kwa faida yao wenyewe. 17 Lakini ninyi wapendwa,
kumbukeni yale mitume wa Bwana wetu Isa Al-
Masihi waliyotabiri awali. 18 Kwa kuwa waliwaambia,
“Siku za mwisho kutakuwa na watu wenye kudhihaki,
watakaofuata tamaa zao wenyewe za upotovu.” 19
Hawa ndio watu wanaowagawanya ninyi, wanaofuata
tamaa zao za asili, wala hawana Roho wa Mungu. 20
Lakini ninyi wapendwa, jijengeni katika imani yenu iliyo
takatifu sana tena ombeni katika Roho wa Mungu. 21
Jilindeni katika upendo wa Mungu mkitazamia rehema
ya Bwana wetu Isa Al-Masihi, inayowapeleka katika
uzima wa milele. **(aiōnios g166)** 22 Wahurumieni walio
na mashaka; 23 okoeni wengine kwa kuwanyakua
kutoka motoni; nao wengine wahurumieni mkiwa na
hofu, mkichukia hata vazi lenye mawaa na kutiwa
unajisi na mwili. 24 Kwake yeye awezaye kuwalinda
ninyi msianguke na kuwaleta mbele za utukufu wake
mkuu bila dosari na kwa furaha ipitayo kiasi: 25 kwake
yeye Mungu pekee Mwokozi wetu, kwa Isa Al-Masihi
Bwana wetu, utukufu, ukuu, uweza na mamlaka ni
vyake tangu milele, sasa na hata milele! Amen. **(aiōn
g165)**

# Ufunuo

1 Ufunuo wa Isa Al-Masihi aliopewa na Mungu ili
awaoneshe watumishi wake mambo ambayo ni
lazima yatukie hivi karibuni. Alijulisha mambo haya
kwa kumtuma malaika wake kwa Yohana mtumishi
wake, 2 ambaye anashuhudia kuhusu kila kitu
alichokiona, yaani neno la Mungu na ushuhuda wa Isa
Al-Masihi. 3 Amebarikiwa yeye asomaye maneno ya
unabii huu, na wamebarikiwa wale wanaoyasikia na
kuyatia moyoni yale yaliyoandikwa humo, kwa sababu
wakati umekaribia. 4 Yohana. 5 na kutoka kwa Isa Al-
Masihi, aliye shahidi mwaminifu, mzaliwa wa kwanza
kutoka kwa wafu, mtawala wa wafalme wa dunia.
Kwake yeye anayetupenda na aliyetuweka huru
kutoka dhambi zetu kwa damu yake, 6 na akatufanya
sisi kuwa ufalme na makuhani, ili tumtumikie Mungu
wake ambaye ni Baba yake. Utukufu na uwezo ni
vyake milele na milele! Amen. **(aiōn g165)** 7 “Tazama!
Anakuja na mawingu,” na “kila jicho litamwona,
hata wale waliomchoma”; na makabila yote duniani
“yataomboleza kwa sababu yake.” 8 “Mimi ni Alfa na
Omega,” asema Bwana Mwenyezi Mungu, “aliyeko,
aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.” 9 Mimi,
Yohana, ndugu yenu ninayeshiriki pamoja nanyi
mateso katika Isa na katika ufalme na uvumilivu
katika saburi, nilikuwa katika kisiwa cha Patmo kwa
ajili ya neno la Mungu na ushuhuda wa Isa. 10
Katika Siku ya Bwana, nilikuwa katika Roho wa
Mungu na nikasikia sauti kubwa kama ya baragumu
nyuma yangu 11 ikisema, “Andika kwenye kitabu
haya yote unayoyaona, kisha uyapeleke kwa makundi
saba ya waumini: kwa Efeso, Smirna, Pergamo,
Thiatira, Sardi, Filadelfia na Laodikia.” 12 Ndipo
nikageuka ili nione ni sauti ya nani iliyokuwa ikisema
nami. Nami nilipogeuka, nikaona vinara saba vya
taa vya dhahabu, 13 na katikati ya vile vinara vya
taa, alikuwamo mtu kama Mwana wa Adamu, akiwa
amevaa joho refu, na mkanda wa dhahabu ukiwa
umefungwa kifuani mwake. 14 Kichwa chake na
nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu, nyeupe
kama theluji, nayo macho yake yalikuwa kama mwali
wa moto. 15 Nyayo zake zilikuwa kama shaba
inayong’aa katika tanuru la moto, nayo sauti yake
ilikuwa kama mngurumo wa maji mengi. 16 Katika
mkono wake wa kuume alishika nyota saba, na
kinywani mwake ulitoka upanga mkali wenye makali
kuwili. Uso wake ulikuwa kama jua liking’aa kwa
nguvu zake zote. 17 Nilipomwona, nilianguka miguuni
pake kama aliyekufa. Ndipo akauweka mkono wake
wa kuume juu yangu na kusema: “Usiogope, Mimi
ndiye wa Kwanza na wa Mwisho. 18 Mimi ni Yeye
Aliye Hai, niliyekuwa nimekufa, na tazama, ni hai
milele na milele! Nami ninazo funguo za mauti na
Kuzimu. **(aiōn g165, Hadēs g86)** 19 “Basi andika mambo
uliyoyaona, yaliyopo na yale yatakayotukia baada ya
haya. 20 Kuhusu siri ya zile nyota saba ulizoziona
katika mkono wangu wa kuume na vile vinara saba
vya taa vya dhahabu ni hii: Zile nyota saba ni malaika
wa yale makundi saba ya waumini, navyo vile vinara
saba ni hayo makundi saba.

2 “Kwa malaika wa kundi la waumini lililoko Efeso,
andika: Haya ndio maneno ya yule aliyezishika
zile nyota saba katika mkono wake wa kuume na
ambaye hutembea kati ya vile vinara saba vya taa
vya dhahabu. 2 Nayajua matendo yako, bidii yako na
saburi yako. Najua kuwa huwezi kuwavumilia watu
waovu, na kwamba umewajaribu wale wanaojifanya
mitume na kumbe sio, nawe umewatambua kuwa ni
waongo. 3 Umevumilia na kustahimili taabu kwa ajili
ya Jina langu, wala hukuchoka. 4 Lakini nina neno
dhidi yako: Umeuacha upendo wako wa kwanza. 5
Kumbuka basi ni wapi ulikoanguka! Tubu na ukafanye
matendo yale ya kwanza. Kama usipotubu, nitakuja
kwako na kukiondoa kinara chako cha taa kutoka
mahali pake. 6 Lakini una jambo hili kwa upande
wako: Unayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo
nami pia nayachukia. 7 Yeye aliye na sikio na asikie
yale ambayo Roho wa Mungu ayaambia makundi
ya waumini. Yeye ashindaye, nitampa haki ya kula
matunda ya uzima, ambao uko katika paradiso ya
Mungu. 8 “Kwa malaika wa kundi la waumini lililoko
Smirna, andika: Haya ndio maneno yake yeye aliye
wa Kwanza na wa Mwisho, aliyekufa kisha akafufuka.
9 Naijua dhiki yako na umaskini wako, lakini wewe ni
tajiri! Nayajua masingizio ya wale wasemao kuwa ni
Wayahudi lakini sio, bali wao ni sinagogi la Shetani.
10 Usiogope mateso yatakayokupata. Nakuambia
ibilisi atawatia baadhi yenu gerezani ili kuwajaribu,
nanyi mtapata dhiki kwa muda wa siku kumi. Uwe
mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji la uzima.
11 Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho

wa Mungu ayaambia makundi ya waumini. Yeye
ashindaye hatadhuriwa kamwe na mauti ya pili. 12
“Kwa malaika wa kundi la waumini lililoko Pergamo,
andika: Haya ndio maneno yake yeye aliye na upanga
mkali wenye makali kuwili. 13 Ninajua unakoishi: kule
Shetani ana kiti chake cha utawala. Lakini umelishika
Jina langu. Wala hukuikana imani yako kwangu,
hata katika siku za shahidi wangu mwaminifu Antipa,
ambaye aliuawa katika mji wenu mkuu, anakoishi
Shetani. 14 Hata hivyo, nina mambo machache
dhidi yako: Unao watu wafuatao mafundisho ya
Balaamu, yule aliyemfundisha Balaki kuwashawishi
Waisraeli watende dhambi kwa kula vitu vilivyotolewa
sadaka kwa sanamu na kufanya uasherati. 15 Vivyo
hivyo unao wale wanaoyashikilia mafundisho ya
Wanikolai. 16 Basi tubu! Ama sivyo, nitakuja kwako
upesi na kupigana na watu hao kwa upanga wa
kinywa changu. 17 Yeye aliye na sikio na asikie
yale ambayo Roho wa Mungu ayaambia makundi
ya waumini. Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile
mana iliyofichwa. Nitampa pia jiwe jeupe ambalo juu
yake limeandikwa jina jipya asilolijua mtu, isipokuwa
yule anayelipokea. 18 “Kwa malaika wa kundi la
waumini lililoko Thiatira, andika: Haya ndio maneno
ya Mwana wa Mungu, ambaye macho yake ni kama
mwali wa moto, na ambaye miguu yake ni kama
shaba iliyosuguliwa. 19 Nayajua matendo yako,
upendo wako na imani yako, huduma na saburi
yako, na kwamba matendo yako ya sasa yamezidi
yale ya kwanza. 20 Hata hivyo, nina neno dhidi
yako: Unamvumilia yule mwanamke Yezebeli ambaye
anajiita nabii, lakini anawafundisha na kuwapotosha
watumishi wangu ili wafanye uasherati na kula vyakula
vilivyotolewa sadaka kwa sanamu. 21 Nimempa muda
ili atubu kwa ajili ya uasherati wake, lakini hataki.
22 Kwa hiyo nitamtupa kwenye kitanda cha mateso,
na nitawafanya hao wanaozini naye kupata mateso
makali wasipotubia njia zake. 23 Nami nitawaua
watoto wake. Nayo makundi yote ya waumini yatajua
kwamba Mimi ndiye nichunguzaye mioyo na nia, na
kwamba nitamlipa kila mmoja wenu kwa kadiri ya
matendo yake. 24 Basi nawaambia ninyi wengine
mlioko Thiatira, ninyi ambao hamyafuati mafundisho
ya Yezebeli, wala hamkujifunza hayo yanayoitwa
mambo ya ndani sana ya Shetani (sitaweka mzigo
mwingine wowote juu yenu): 25 Lakini shikeni sana
mlicho nacho, hadi nitakapokuja. 26 Atakayeshinda
na kutenda mapenzi yangu hadi mwisho, nitampa
mamlaka juu ya mataifa: 27 ‘Atawatawala kwa fimbo
ya chuma, atawavunja vipande vipande kama chombo
cha udongo’: kama mimi nilivyopokea mamlaka kutoka
kwa Baba yangu. 28 Nami nitampa pia ile nyota ya
asubuhi. 29 Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo
Roho wa Mungu ayaambia makundi ya waumini.

3 “Kwa malaika wa kundi la waumini lililoko Sardi,
andika: Haya ndio maneno ya aliye na zile
Roho saba za Mungu na zile nyota saba. Nayajua
matendo yako, kwamba una sifa ya kuwa hai, lakini
umekufa. 2 Amka! Nawe uyaimarishe yale yaliyosalia
na yaliyo karibu kufa, kwa maana sikuona kwamba
kazi zako zimekamilika machoni pa Mungu wangu. 3
Kumbuka basi yale uliyoyapokea na kuyasikia; yatii na
ukatubu. Lakini usipoamka, nitakuja kama mwizi wala
hutajua saa nitakayokuja kwako. 4 Lakini bado una
watu wachache katika Sardi ambao hawajayachafua
mavazi yao. Wao wataenda pamoja nami, wakiwa
wamevaa mavazi meupe, kwa maana wanastahili.
5 Yeye ashindaye atavikwa vazi jeupe kama wao.
Sitafuta jina lake kutoka kitabu cha uzima, bali
nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu na mbele
za malaika wake. 6 Yeye aliye na sikio na asikie
yale ambayo Roho wa Mungu ayaambia makundi ya
waumini. 7 “Kwa malaika wa kundi la waumini lililoko
Filadelfia, andika: Haya ndio maneno yake yeye aliye
mtakatifu na wa kweli, yeye aliye na ufunguo wa
Daudi. Anachokifungua hakuna awezaye kukifunga,
wala anachokifunga hakuna awezaye kukifungua. 8
Nayajua matendo yako. Tazama, nimeweka mbele
yako mlango uliofunguliwa, wala hakuna awezaye
kuufunga. Ninajua kwamba una nguvu kidogo lakini
umelishika neno langu wala hukulikana Jina langu. 9
Nitawafanya wale wa sinagogi la Shetani, wale ambao
husema kuwa ni Wayahudi lakini sio, bali ni waongo,
nitawafanya waje wapige magoti miguuni pako, na
wakiri kwamba nimekupenda. 10 Kwa kuwa umeshika
amri yangu ya kuvumilia katika saburi, nitakulinda
katika saa ya kujaribiwa inayokuja ulimwenguni pote, ili
kuwajaribu wote wanaoishi duniani. 11 Ninakuja upesi.
Shika sana ulicho nacho, ili mtu asije akalichukua
taji lako. 12 Yeye ashindaye nitamfanya kuwa nguzo
katika Hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo
kamwe. Nitaandika juu yake Jina la Mungu wangu na

jina la mji mkubwa wa Mungu wangu, Yerusalemu
mpya, ambao unashuka kutoka mbinguni kwa Mungu
wangu. Nami pia nitaandika juu yake Jina langu jipya.
13 Yeye aliye na sikio na asikie yale ambayo Roho
wa Mungu ayaambia makundi ya waumini. 14 “Kwa
malaika wa kundi la waumini lililoko Laodikia, andika:
Haya ndio maneno yake yeye aliye Amen, shahidi
mwaminifu na wa kweli, mtawala wa uumbaji wote wa
Mungu. 15 Nayajua matendo yako, kwamba wewe
si baridi wala si moto. Afadhali ungekuwa moto au
baridi. 16 Hivyo kwa kuwa u vuguvugu, si baridi wala
moto, nitakutapika utoke kinywani mwangu. 17 Kwa
maana unasema: ‘Mimi ni tajiri, nimejilimbikizia mali,
wala sihitaji kitu chochote.’ Lakini hutambui kwamba
wewe ni mnyonge, wa kuhurumiwa, maskini, kipofu,
tena uliye uchi. 18 Nakushauri ununue kutoka kwangu
dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri,
na mavazi meupe ili uyavae upate kuficha aibu ya
uchi wako, na mafuta ya kupaka macho yako ili
upate kuona. 19 Wale ninaowapenda, ninawakemea
na kuwaadibisha. Hivyo uwe na bidii ukatubu. 20
Tazama! Nasimama mlangoni nabisha. Kama mtu
yeyote akisikia sauti yangu na kufungua mlango,
nitaingia ndani na kula pamoja naye, naye pamoja
nami. 21 Yeye ashindaye nitampa haki ya kuketi
pamoja nami kwenye kiti changu cha enzi, kama vile
mimi nilivyoshinda na nikaketi pamoja na Baba yangu
kwenye kiti chake cha enzi. 22 Yeye aliye na sikio
na asikie yale ambayo Roho wa Mungu ayaambia
makundi ya waumini.”

4 Baada ya mambo hayo nilitazama, nami nikaona
mbele yangu mlango uliokuwa wazi mbinguni. Nayo
ile sauti niliyokuwa nimeisikia hapo mwanzo ikisema
nami kama tarumbeta ikasema, “Njoo huku, nami
nitakuonesha yale ambayo hayana budi kutendeka
baada ya haya.” 2 Ghafula nilikuwa katika Roho wa
Mungu, na hapo mbele yangu palikuwa kiti cha enzi
mbinguni, kikiwa kimekaliwa na mtu. 3 Aliyekuwa
amekikalia alikuwa anaonekana kama yaspi na akiki.
Kukizunguka kile kiti cha enzi palikuwa na upinde
wa mvua uliong’aa kama zumaridi. 4 Kukizunguka
hicho kiti cha enzi palikuwa na viti vingine ishirini
na vinne vya utawala, na juu ya hivyo viti walikuwa
wameketi wazee ishirini na wanne. Walivaa mavazi
meupe, na walikuwa na taji za dhahabu vichwani
mwao. 5 Kwenye kile kiti cha enzi palikuwa panatoka
miali ya radi, ngurumo na sauti za radi. Mbele ya
kiti cha enzi, taa saba zilikuwa zinawaka. Hizi ndizo
roho saba za Mungu. 6 Pia mbele ya kiti cha enzi
palikuwa na kile kilichoonekana kama bahari ya kioo,
iliyokuwa angavu kama bilauri. Katikati, kukizunguka
kile kiti cha enzi, kulikuwa na viumbe wanne wenye
uhai, wamejaa macho mbele na nyuma. 7 Kiumbe
wa kwanza mwenye uhai alikuwa kama simba, wa pili
alikuwa kama ng’ombe dume, wa tatu alikuwa na uso
kama wa mwanadamu, na wa nne alikuwa kama tai
anayeruka. 8 Kila mmoja wa hawa viumbe wanne
wenye uhai alikuwa na mabawa sita, na kujawa na
macho pande zote hadi chini ya mabawa. Usiku na
mchana hawaachi kusema: 9 Kila mara viumbe hao
wanne wenye uhai wanapomtukuza, kumheshimu na
kumshukuru yeye aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi,
tena aishiye milele na milele, (aiōn g165) 10 wale wazee
ishirini na wanne huanguka mbele zake aliyeketi
kwenye kiti cha enzi, na kumwabudu yeye aliye hai
milele na milele. Huziweka taji zao mbele ya kiti cha
enzi, wakisema: (aiōn g165) 11 “Bwana wetu na Mungu
wetu, wewe unastahili kupokea utukufu na heshima
na uweza, kwa maana ndiwe uliyeviumba vitu vyote,
na kwa mapenzi yako viliumbwa na vimekuwako.”

5 Kisha nikaona katika mkono wake wa kuume wa
yule aliyeketi kwenye kile kiti cha enzi, kitabu
kilichoandikwa ndani na nje, kikiwa kimefungwa kwa
mihuri saba. 2 Nami nikamwona malaika mwenye
nguvu akitangaza kwa sauti kuu, “Ni nani anayestahili
kuivunja hiyo mihuri na kukifungua kitabu?” 3 Lakini
hapakuwa na yeyote mbinguni wala duniani au chini
ya dunia aliyeweza kukifungua hicho kitabu, wala hata
kutazama ndani yake. 4 Nikalia sana kwa sababu
hakuonekana yeyote anayestahili kukifungua hicho
kitabu wala kutazama ndani yake. 5 Kisha, mmoja wa
wale wazee akaniambia, “Usilie! Tazama, Simba wa
kabila la Yuda, wa Uzao wa Daudi, ameshinda. Yeye
ndiye anayeweza kukifungua hicho kitabu na kuvunja
mihuri yake saba.” 6 Ndipo nikaona katikati ya kile
kiti cha enzi na wale viumbe wenye uhai wanne, na
katikati ya wale wazee, Mwana-Kondoo amesimama,
akiwa kama amechinjwa. Alikuwa na pembe saba
na macho saba, ambazo ndizo zile Roho saba za
Mungu zilizotumwa duniani pote. 7 Huyo Mwana-
Kondoo akaja na kukitwaa kile kitabu kutoka mkono
wa kuume wa yule aliyeketi kwenye kile kiti cha

enzi. 8 Alipokwisha kukitwaa kile kitabu, wale viumbe
wenye uhai wanne pamoja na wale wazee ishirini na
wanne wakaanguka mbele ya yule Mwana-Kondoo.
Kila mmoja wao alikuwa na kinubi, nao walikuwa
wameshika mabakuli ya dhahabu yaliyojaa uvumba,
ambayo ni maombi ya watakatifu. 9 Nao wakaimba
wimbo mpya, wakisema: “Wewe unastahili kukitwaa
kitabu na kuivunja mihuri yake, kwa sababu ulichinjwa,
na kwa damu yako ukamnunulia Mungu watu kutoka
kila kabila, kila lugha, kila jamaa na kila taifa. 10
Wewe umewafanya hawa wawe ufalme na makuhani
wa kumtumikia Mungu wetu, nao watatawala duniani.”
11 Kisha nikatazama, nikasikia sauti za malaika wengi
wakiwa wamekizunguka kile kiti cha enzi, pamoja na
wale viumbe wenye uhai wanne na wale wazee ishirini
na wanne. Idadi yao ilikuwa kumi elfu mara kumi elfu
na maelfu ya maelfu. 12 Nao waliimba kwa sauti
kuu, wakisema: “Anastahili Mwana-Kondoo, yeye
aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima
na nguvu na heshima na utukufu na sifa!” 13 Kisha
nikasikia kila kiumbe mbinguni na duniani, chini ya
nchi, na baharini, na vyote vilivyomo, vikiimba: “Sifa
na heshima na utukufu na uweza ni vyake yeye
aliyeketi juu ya hicho kiti cha enzi, na kwa Mwana-
Kondoo, milele na milele!” **(aiōn g165)** 14 Wale viumbe
wenye uhai wanne wakasema, “Amen!” Nao wale
wazee wakaanguka kifudifudi wakaabudu.

**6** Nikaangalia Mwana-Kondoo alipofungua ule
muhuri wa kwanza miongoni mwa mihuri saba.
Ndipo nikasikia mmoja wa wale viumbe wanne wenye
uhai akisema kwa sauti kama ya radi: “Njoo!” 2
Nikatazama, na hapo mbele yangu palikuwa na
farasi mweupe! Yeye aliyempanda alikuwa na upinde,
naye akapewa taji, akampanda akatoka akiwa kama
mshindi aelekeaye katika kushinda. 3 Alipouvunja
ule muhuri wa pili, nikamsikia yule kiumbe wa pili
mwenye uhai akisema, “Njoo!” 4 Ndipo akatokea
farasi mwingine mwekundu sana. Yeye aliyempanda
akapewa uwezo wa kuondoa amani duniani na
kuwafanya watu wauane. Yeye akapewa upanga
mkubwa. 5 Mwana-kondoo alipouvunja ule muhuri
wa tatu, nikamsikia yule kiumbe wa tatu mwenye
uhai akisema, “Njoo!” Nikatazama, na mbele yangu
palikuwa na farasi mweusi! Yeye aliyempanda alikuwa
na mizani mkononi mwake. 6 Ndipo nikasikia kile
kilichokuwa kama sauti katikati ya wale viumbe wanne
wenye uhai ikisema, “Kipimo kimoja cha ngano kwa
mshahara wa kibarua wa siku moja, na vipimo vitatu
vya shayiri kwa mshahara wa kibarua cha siku moja.
Lakini usiharibu mafuta wala divai!” 7 Alipouvunja ule
muhuri wa nne, nikasikia sauti ya yule kiumbe wa
nne mwenye uhai ikisema, “Njoo!” 8 Nikatazama, na
hapo mbele yangu palikuwa na farasi mwenye rangi
ya kijivujivu! Yeye aliyempanda aliitwa Mauti, naye
Kuzimu alikuwa akimfuata nyuma yake kwa karibu.
Wakapewa mamlaka juu ya robo ya dunia, kuua kwa
upanga, njaa, tauni na kwa wanyama wakali wa dunia.
**(Hadēs g86)** 9 Mwana-kondoo alipouvunja ule muhuri
wa tano, nikaona chini ya madhabahu, roho za wale
waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu na kwa ajili
ya ushuhuda walioutunza. 10 Wakalia kwa sauti kuu,
wakasema, “Hata lini, Ee Bwana Mungu Mwenyezi,
uliye mtakatifu na mwaminifu, hutawahukumu na
kulipiza kisasi kwa watu wanaoishi duniani kwa ajili ya
damu yetu?” 11 Kisha kila mmoja wao akapewa joho
jeupe na wakaambiwa wangoje kwa muda kidogo
zaidi, hadi idadi ya ndugu zao na watumishi wenzao
watakaouawa kama wao walivyouawa, itakapotimia.
12 Nikatazama alipouvunja ule muhuri wa sita.
Pakatokea tetemeko kuu la ardhi, na jua likawa jeusi
kama gunia lililotengenezwa kwa singa za mbuzi, na
mwezi wote ukawa mwekundu kama damu. 13 Nyota
zilizo angani zikaanguka ardhini kama vile matunda
ya mtini yasiyokomaa yaangukavyo wakati mti wake
unapotikiswa na upepo mkali. 14 Anga ikatoweka
kama vile karatasi isokotwavyo, na kila mlima na kila
kisiwa kikaondolewa mahali pake. 15 Ndipo wafalme
wa dunia, wakuu wote, majemadari, matajiri, wenye
nguvu na kila mtu, mtumwa na mtu huru, wakajificha
katika mapango na kwenye miamba ya milima. 16
Wakaiita milima na miamba wakisema, “Tuangukieni,
mkatufiche na uso wake yeye aliyeketi kwenye kile kiti
cha enzi, na mkatuepushe na ghadhabu ya Mwana-
Kondoo! 17 Kwa maana siku ile kuu ya ghadhabu
yao imewadia. Je, ni nani awezaye kustahimili?”

**7** Baada ya hili nikaona malaika wanne wakiwa
wamesimama katika pembe nne za dunia, wakizuia
hizo pepo nne za dunia, ili pasiwe na upepo
utakaovuma juu ya nchi au juu ya bahari au juu ya
mti wowote. 2 Nikaona malaika mwingine akipanda
kutoka mawio ya jua akiwa na muhuri wa Mungu aliye
hai. Akawaita kwa sauti kubwa wale malaika wanne

waliokuwa wamepewa mamlaka ya kuidhuru nchi na
bahari, akisema, 3 “Msiidhuru nchi wala bahari, wala
miti, hadi tuwe tumetia muhuri kwenye paji za nyuso
za watumishi wa Mungu wetu.” 4 Ndipo nikasikia idadi
ya wale waliotiwa muhuri: elfu mia moja na arobaini
na nne kutoka makabila yote ya Israeli. 5 Kutoka
kabila la Yuda elfu kumi na mbili walitiwa muhuri,
kutoka kabila la Reubeni elfu kumi na mbili, kutoka
kabila la Gadi elfu kumi na mbili, 6 kutoka kabila
la Asheri elfu kumi na mbili, kutoka kabila la Naftali
elfu kumi na mbili, kutoka kabila la Manase elfu kumi
na mbili, 7 kutoka kabila la Simeoni elfu kumi na
mbili, kutoka kabila la Lawi elfu kumi na mbili, kutoka
kabila la Isakari elfu kumi na mbili, 8 kutoka kabila la
Zabuloni elfu kumi na mbili, kutoka kabila la Yusufu
elfu kumi na mbili, na kutoka kabila la Benyamini
elfu kumi na mbili. 9 Baada ya hili nikatazama na
hapo mbele yangu palikuwa na umati mkubwa wa
watu ambao hakuna yeyote awezaye kuwahesabu,
kutoka kila taifa, kila kabila, kila jamaa na kila lugha,
wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi na mbele ya
Mwana-Kondoo. Walikuwa wamevaa mavazi meupe
na wakiwa wameshika matawi ya mitende mikononi
mwao. 10 Nao walikuwa wakipaza sauti kwa nguvu,
wakisema: “Wokovu una Mungu wetu, yeye aliyeketi
kwenye kile kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo!” 11
Malaika wote walikuwa wamesimama kukizunguka
kile kiti cha enzi na wale wazee, na wale viumbe
wanne wenye uhai. Wakaanguka kifudifudi mbele
ya hicho kiti cha enzi na kumwabudu Mungu, 12
wakisema: “Amen! Sifa na utukufu na hekima na
shukrani na heshima na uweza na nguvu viwe kwa
Mungu wetu milele na milele. Amen!” **(aiōn g165)** 13
Kisha mmoja wa wale wazee akaniuliza, “Ni nani
hawa waliovaa mavazi meupe, nao wametoka wapi?”
14 Nikamjibu, “Bwana, wewe unajua.” Naye akasema,
“Hawa ni wale waliotoka katika ile dhiki kuu, nao
wamefua mavazi yao katika damu ya Mwana-Kondoo
na kuyafanya meupe kabisa. 15 Kwa hiyo, “Wako
mbele ya kiti cha enzi cha Mungu na kumtumikia
usiku na mchana katika Hekalu lake; naye aliyeketi
katika kile kiti cha enzi atatanda hema lake juu
yao. 16 Kamwe hawataona njaa wala kiu tena. Jua
halitawachoma wala joto lolote liunguzalo. 17 Kwa
maana Mwana-Kondoo aliyeko katikati ya kile kiti
cha enzi atakuwa Mchungaji wao; naye atawaongoza
kwenda kwenye chemchemi za maji yaliyo hai. Naye
Mungu atawafuta machozi kutoka machoni mwao.”

**8** Mwana-Kondoo alipouvunja ule muhuri wa saba,
pakawa kimya mbinguni kwa muda wa nusu saa.
2 Nami nikawaona wale malaika saba wanaosimama
mbele za Mungu, nao wakapewa tarumbeta saba.
3 Malaika mwingine, aliyekuwa na chetezo cha
dhahabu, akaja na kusimama mbele ya madhabahu.
Akapewa uvumba mwingi ili autoe pamoja na maombi
ya watakatifu wote, juu ya yale madhabahu ya
dhahabu yaliyo mbele ya kile kiti cha enzi. 4 Ule moshi
wa uvumba pamoja na yale maombi ya watakatifu,
vikapanda juu mbele za Mungu, kutoka mkononi mwa
huyo malaika. 5 Kisha yule malaika akakichukua kile
chetezo, akakijaza moto kutoka kwa yale madhabahu,
akautupa juu ya dunia. Pakatokea sauti za radi na
ngurumo, miali ya radi na tetemeko la ardhi. 6 Basi
wale malaika saba waliokuwa na zile tarumbeta saba
wakajiandaa kuzipiga. 7 Malaika wa kwanza akaipiga
tarumbeta yake, pakatokea mvua ya mawe na moto
uliochanganyika na damu, navyo vikatupwa kwa
nguvu juu ya nchi. Na theluthi ya dunia ikateketea,
theluthi ya miti ikateketea, na nyasi yote mbichi
ikateketea. 8 Malaika wa pili akaipiga tarumbeta
yake na kitu kama mlima mkubwa unaowaka moto
kikatupwa baharini. Theluthi ya bahari ikawa damu, 9
theluthi ya viumbe vyenye uhai vilivyoishi baharini
vikafa, na theluthi ya meli zikaharibiwa. 10 Malaika
wa tatu akaipiga tarumbeta yake, na nyota kubwa
iliyokuwa ikiwaka kama taa ikaanguka toka angani,
ikaangukia theluthi ya mito na chemchemi za maji.
11 Nyota hiyo inaitwa Pakanga. Theluthi ya maji
yakawa machungu na watu wengi wakafa kutokana
na maji hayo kwa maana yalikuwa machungu. 12
Kisha malaika wa nne akaipiga tarumbeta yake, na
theluthi ya jua, theluthi ya mwezi na theluthi ya nyota
zikapigwa. Kwa hiyo theluthi moja ya mwanga ikawa
giza. Theluthi ya mchana ikawa haina mwanga na
pia theluthi ya usiku. 13 Nilipokuwa tena nikitazama,
nikamsikia tai mmoja akipaza sauti kwa nguvu, huku
akiruka katikati ya anga, akasema, “Ole! Ole! Ole wa
watu wanaoishi duniani, kwa sababu ya tarumbeta
ambazo malaika hao wengine watatu wanakaribia
kuzipiga!”

9 Malaika wa tano akaipiga tarumbeta yake, nami
nikaona nyota iliyokuwa imeanguka toka angani
hadi ardhini. Nyota hiyo ilipewa ufunguo wa lile
Shimo. **(Abyssos g12)** **2** Alipolifungua hilo Shimo, moshi
ukapanda kutoka humo kama moshi wa tanuru kubwa
sana. Jua na anga vikatiwa giza na ule moshi uliotoka
katika hilo Shimo. **(Abyssos g12)** **3** Ndipo katika ule
moshi wakatoka nzige wakaenda juu ya nchi, nao
wakapewa nguvu kama zile za nge wa duniani. **4**
Wakaambiwa wasidhuru majani ya nchi, wala mmea
wala mti wowote, bali wawadhuru tu wale watu ambao
hawana muhuri wa Mungu kwenye paji za nyuso zao.
**5** Wakaruhusiwa kuwatesa kwa muda wa miezi mitano,
lakini wasiwaue. Uchungu wa kuuma kwao ulikuwa
kama ule wa mtu anapoumwa na nge. **6** Katika
siku hizo watu watatafuta kifo lakini hawatakiona,
watatamani kufa, lakini kifo kitawakimbia. **7** Wale nzige
walikuwa na umbo kama la farasi waliotayarishwa
kwa ajili ya vita. Kwenye vichwa vyao kulikuwa na kitu
kama taji za dhahabu, na nyuso zao zilikuwa kama za
binadamu. **8** Walikuwa na nywele kama za wanawake,
na meno yao yalikuwa kama ya simba. **9** Walikuwa
na dirii kama za chuma, na sauti za mabawa yao
zilikuwa kama ngurumo za farasi wengi na magari
ya vita mengi yakikimbia vitani. **10** Walikuwa na
mikia yenye miiba ya kuumia, kama nge. Nguvu
yao ya kutesa watu kwa huo muda wa miezi mitano
ilikuwa katika mikia yao. **11** Walikuwa na mfalme
wao, ambaye ni malaika wa lile Shimo, ambaye jina
lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani ni
Apolioni. **(Abyssos g12)** **12** Ole ya kwanza imepita, bado
nyingine mbili zinakuja. **13** Malaika wa sita akaipiga
tarumbeta yake, nami nikasikia sauti ikitoka katika
zile pembe za madhabahu ya dhahabu iliyo mbele
za Mungu. **14** Ile sauti ikamwambia yule malaika wa
sita mwenye tarumbeta, “Wafungulie wale malaika
wanne waliofungwa kwenye ule mto mkubwa Frati.”
**15** Basi wale malaika wanne, waliokuwa wamewekwa
tayari kwa ajili ya saa hiyo, na siku hiyo, na mwezi
huo, na mwaka huo ili wawaue theluthi ya wanadamu
wakafunguliwa. **16** Idadi ya majeshi wapanda farasi
ilikuwa milioni mia mbili. Nilisikia idadi yao. **17** Hivi
ndivyo nilivyowaona hao farasi na wapanda farasi
katika maono yangu: Wapanda farasi walivaa dirii
vifuani zenye rangi nyekundu sana kama ya moto,
na yakuti samawi, na kiberiti. Vichwa vya hao farasi
vilikuwa kama vichwa vya simba, na moto, moshi
na kiberiti vilitoka vinywani mwao. **18** Theluthi ya
wanadamu wakauawa kwa mapigo hayo matatu,
yaani huo moto, moshi na kiberiti, vilivyotoka kwenye
vinywa vya hao farasi. **19** Nguvu za hao farasi zilikuwa
katika vinywa vyao na kwenye mikia yao, kwa sababu
mikia yao ilikuwa kama nyoka, yenye vichwa ambayo
waliitumia kudhuru. **20** Wanadamu waliosalia, ambao
hawakuuawa katika mapigo hayo, bado walikataa
kutubia kazi za mikono yao na hawakuacha kuabudu
mashetani na sanamu za dhahabu, za fedha, za
shaba, za mawe na za miti, ambazo haziwezi kuona,
kusikia wala kutembea. **21** Wala hawakutubu na
kuacha matendo yao ya uuaji, uchawi, uasherati wala
wizi wao.

10 Kisha nikamwona malaika mwingine mwenye
nguvu akishuka kutoka mbinguni. Alikuwa
amevikwa wingu na upinde wa mvua juu ya kichwa
chake. Uso wake uling’aa kama jua na miguu yake
ilikuwa kama nguzo za moto. **2** Mkononi mwake
alikuwa ameshika kijitabu kilichokuwa kimefunguliwa.
Akauweka mguu wake wa kuume juu ya bahari
na mguu wake wa kushoto akauweka juu ya nchi
kavu. **3** Naye akapaza sauti kwa nguvu kama simba
anayenguruma. Aliponguruma, zile radi saba zikatoa
ngurumo zake. **4** Nazo zile radi saba zilipotoa
ngurumo, nilitaka kuanza kuandika, lakini nikasikia
sauti kutoka mbinguni ikisema, “Yatie muhuri hayo
yaliyosemwa na hizo radi saba na usiyaandike.” **5**
Kisha yule malaika niliyekuwa nimemwona akiwa
amesimama juu ya bahari na juu ya nchi akainua
mkono wake wa kuume kuelekea mbinguni. **6** Naye
akaapa kwa Yule aishiye milele na milele, aliyeumba
mbingu na vyote vilivyomo, dunia na vyote viijazavyo,
pamoja na bahari na vyote vilivyomo, akasema,
“Hakuna kungoja tena! **(aiōn g165)** **7** Lakini katika
siku zile huyo malaika wa saba atakaribia kuipiga
hiyo tarumbeta yake, siri ya Mungu itatimizwa, kama
vile alivyowatangazia watumishi wake manabii.” **8**
Ndipo ile sauti niliyokuwa nimeisikia kutoka mbinguni
ikasema nami tena, ikaniambia, “Nenda, chukua
kile kitabu kilichofunguliwa kilichoko mkononi mwa
yule malaika aliyesimama juu ya bahari na juu ya
nchi kavu.” **9** Basi nikamwendea nikamwomba yule
malaika anipe kile kijitabu. Akaniambia, “Chukua
na ukile. Kitakuwa kichungu tumboni mwako, lakini

kinywani mwako kitakuwa kitamu kama asali.” 10
Hivyo nikakichukua kile kijitabu kutoka mkononi mwa
yule malaika, nikakila. Kilikuwa kitamu kama asali
kinywani mwangu, lakini baada ya kukila, tumbo langu
likatiwa uchungu. 11 Kisha nikaambiwa, “Imekupasa
kutoa unabii tena kuhusu makabila mengi, mataifa,
lugha na wafalme.”

11 Ndipo nikapewa mwanzi uliokuwa kama ufito wa
kupimia, nikaambiwa, “Nenda ukapime Hekalu
la Mungu pamoja na madhabahu, nawe uwahesabu
wale waabuduo humo. 2 Lakini usiupime ua wa nje
wa Hekalu; uache, kwa sababu ua huo wamepewa
watu wa Mataifa. Hao wataukanyagakanyaga mji
mtakatifu kwa muda wa miezi arobaini na mbili. 3 Nami
nitawapa mashahidi wangu wawili uwezo, nao watoe
unabii kwa muda wa siku elfu moja mia mbili na sitini,
wakiwa wamevaa gunia.” 4 Hawa ndio ile mizeituni
miwili na vile vinara viwili vya taa visimamavyo mbele
za Mwenyezi Mungu, Mungu wa dunia yote. 5
Kama mtu yeyote akitaka kuwadhuru, moto hutoka
vinywani mwao na kuwateketeza adui zao. Hivi ndivyo
impasavyo kufa mtu yeyote atakayetaka kuwadhuru.
6 Watu hawa wanao uwezo wa kufunga anga ili
mvua isinyeshe wakati wote watakapokuwa wanatoa
unabii wao. Nao watakuwa na uwezo wa kuyabadili
maji kuwa damu na kuipiga dunia kwa kila aina ya
mapigo mara kwa mara kama watakavyo. 7 Basi
watakapokuwa wamemaliza ushuhuda wao, yule
mnyama atokaye katika lile Shimo atapigana nao
vita, atawashinda na kuwaua. **(Abyssos g12)** 8 Maiti
zao zitabaki katika barabara ya mji mkubwa, ambao
kwa fumbo unaitwa Sodoma na Misri, ambapo pia Isa
Bwana wao alisulubiwa. 9 Kwa muda wa siku tatu
na nusu, watu wa kila kabila, jamaa, lugha na taifa
wataziangalia hizo maiti zao na hawataruhusu zizikwe.
10 Watu wanaoishi duniani watazitazama maiti za
hao manabii wawili kwa furaha, na kushangilia kwa
kupeana zawadi, kwa sababu hao manabii waliwatesa
watu wanaoishi duniani. 11 Lakini baada ya zile siku
tatu na nusu, pumzi ya uhai kutoka kwa Mungu
ikawaingia, nao wakasimama kwa miguu yao na wote
waliowaona wakaingiwa na hofu kuu. 12 Kisha wale
manabii wawili wakasikia sauti kuu kutoka mbinguni
ikiwaambia, “Njooni huku juu!” Nao wakapaa mbinguni
katika wingu, wakati adui zao wakiwa wanawatazama.
13 Saa hiyo hiyo, kukawa na tetemeko kubwa la ardhi
na sehemu ya kumi ya mji ikaanguka. Watu elfu saba
wakauawa katika tetemeko hilo, nao walionusurika
wakaogopa sana, wakamtukuza Mungu wa mbinguni.
14 Ole ya pili imekwisha kupita, tazama ole ya tatu
inakuja upesi. 15 Yule malaika wa saba akaipiga
tarumbeta yake, pakawa na sauti kubwa mbinguni
iliyosema: “Ufalme wa ulimwengu umekuwa ufalme
wa Bwana wetu na wa Al-Masihi wake, naye atatawala
milele na milele.” **(aiōn g165)** 16 Nao wale wazee
ishirini na wanne, waliokuwa wameketi mbele za
Mungu, kwenye viti vyao vya utawala, wakaanguka
kifudifudi, wakamwabudu Mungu, 17 wakisema:
“Tunakushukuru, Bwana Mungu Mwenyezi, uliyeko
na uliyekuwako, kwa kuwa umetwaa uweza wako
mkuu na ukaanza kutawala. 18 Mataifa walikasirika;
nao wakati wa ghadhabu yako umewadia. Wakati
umewadia wa kuwahukumu waliokufa, na kuwapa
thawabu watumishi wako manabii, na watakatifu
wako pamoja na wale wote wanaoliheshimu Jina
lako, wakubwa kwa wadogo: na kuwaangamiza wale
wanaoiangamiza dunia.” 19 Ndipo Hekalu la Mungu
lililoko mbinguni likafunguliwa, na Sanduku la Agano
lake likaonekana humo. Kukatokea miali ya radi,
ngurumo, sauti za radi, tetemeko la ardhi na mvua
kubwa ya mawe.

12 Kukaonekana ishara kuu mbinguni: Palikuwa na
mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa
chini ya miguu yake, na taji lenye nyota kumi na mbili
lilikuwa kichwani mwake. 2 Alikuwa na mimba naye
akilia kwa uchungu kwa kuwa alikuwa anakaribia
kuzaa. 3 Kisha ishara nyingine ikaonekana mbinguni:
Likaonekana joka kubwa jekundu lenye vichwa
saba na pembe kumi, na taji saba katika vichwa
vyake. 4 Mkia wake ukakokota theluthi ya nyota
zote angani na kuziangusha katika nchi. Ndipo lile
joka likasimama mbele ya yule mwanamke aliyekuwa
karibu kuzaa ili lipate kumla huyo mtoto mara tu
atakapozaliwa. 5 Yule mwanamke akazaa mtoto wa
kiume, atakayeyatawala mataifa yote kwa fimbo ya
utawala ya chuma. Lakini huyo mtoto akanyakuliwa
na kupelekwa kwa Mungu kwenye kiti chake cha enzi.
6 Yule mwanamke akakimbilia jangwani, ambako
Mungu alikuwa amemtayarishia mahali ili apate
kutunzwa huko kwa muda wa siku elfu moja mia
mbili na sitini. 7 Basi palikuwa na vita mbinguni:
Mikaeli na malaika wake wakapigana na hilo joka,

nalo joka pamoja na malaika wake likapigana nao.
8 Lakini joka na malaika wake wakashindwa, na
hapakuwa tena na nafasi yao huko mbinguni. 9
Lile joka kuu likatupwa chini, yule nyoka wa zamani
aitwaye ibilisi au Shetani, aupotoshaye ulimwengu
wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na
malaika wake. 10 Kisha nikasikia sauti kuu mbinguni,
ikisema: "Sasa wokovu na uweza na ufalme wa
Mungu wetu Mwenyezi umekuja, na mamlaka ya Al-
Masihi wake. Kwa kuwa ametupwa chini mshtaki
wa ndugu zetu, anayewashtaki mbele za Mungu
usiku na mchana. 11 Nao wakamshinda kwa damu
ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao.
Wala wao hawakuyapenda maisha yao sana, hata
wakawa tayari kufa. 12 Kwa hiyo furahini, ninyi mbingu
na wote wanaoishi humo! Lakini ole wenu nchi na
bahari, kwa maana huyo ibilisi ameshuka kwenu,
akiwa amejaa ghadhabu, kwa sababu anajua ya kuwa
muda wake ni mfupi!" 13 Lile joka lilipoona kuwa
limetupwa chini duniani, lilimfuatilia yule mwanamke
aliyekuwa amezaa mtoto wa kiume. 14 Lakini huyo
mwanamke akapewa mabawa mawili ya tai mkubwa,
kusudi aweze kuruka hadi mahali palipotayarishwa
kwa ajili yake huko jangwani, ambako atatunzwa kwa
wakati na nyakati na nusu, ya wakati ambako lile joka
haliwezi kufika. 15 Ndipo lile joka likamwaga maji
kama mto kutoka kinywani mwake, ili kumfikia huyo
mwanamke, achukuliwe na mafuriko. 16 Lakini nchi
ikamsaidia huyo mwanamke kwa kufungua kinywa na
kuumeza huo mto ambao lile joka lilikuwa limeutoa
kinywani mwake. 17 Kisha lile joka likapatwa na
hasira kali kwa ajili ya huyo mwanamke na likaondoka
ili kupigana vita na wazawa waliosalia wa huyo
mwanamke, yaani wale wanaozitii amri za Mungu na
kuushika ushuhuda wa Isa Al-Masihi.

13 Lile joka likasimama kwenye mchanga wa
bahari. Nami nikamwona mnyama akitoka ndani
ya bahari. Mnyama huyo alikuwa na pembe kumi
na vichwa saba, akiwa na taji kumi kwenye hizo
pembe zake, na juu ya kila kichwa kulikuwa na jina
la kukufuru. 2 Mnyama yule niliyemwona alifanana
na chui, lakini miguu yake ilikuwa kama ya dubu na
kichwa chake kama cha simba. Lile joka likampa
huyo mnyama nguvu zake, kiti chake cha utawala na
mamlaka makubwa. 3 Mojawapo ya vichwa vya huyo
mnyama kilikuwa kama kilichokwisha kupata jeraha la
mauti, lakini jeraha hilo la mauti likapona. Ulimwengu
wote ukashangaa ukamfuata huyo mnyama. 4 Watu
wakaliabudu lile joka kwa sababu lilikuwa limempa
huyo mnyama mamlaka yake, pia wakamwabudu
huyo mnyama na kuuliza, "Ni nani aliye kama
huyu mnyama? Ni nani awezaye kupigana vita
naye?" 5 Huyo mnyama akapewa mdomo wa kusema
maneno ya kiburi na kukufuru, na uwezo wa kutumia
mamlaka yake kwa muda wa miezi arobaini na mbili.
6 Akafungua kinywa chake ili kumkufuru Mungu,
akilitukana Jina lake na mahali aishipo na wale
wanaokaa mbinguni. 7 Pia akaruhusiwa kufanya vita
na watakatifu na kuwashinda. Akapewa uwezo juu ya
watu wa kila kabila, jamaa, lugha na taifa. 8 Nao watu
wote wanaoishi duniani watamwabudu huyo mnyama:
wale wote ambao majina yao hayakuandikwa kwenye
kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo, aliyechinjwa
tangu kuumbwa kwa ulimwengu. 9 Yeye aliye na sikio
na asikie. 10 "Ikiwa mtu ni wa kuchukuliwa mateka,
atachukuliwa mateka. Ikiwa mtu ni wa kuuawa kwa
upanga, atauawa kwa upanga." Hapa ndipo penye
wito wa subira na imani ya watakatifu. 11 Kisha
nikamwona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka
ardhini. Alikuwa na pembe mbili kama mwana-
kondoo, lakini akanena kama joka. 12 Akatumia
mamlaka yote ya yule mnyama wa kwanza kwa niaba
yake, naye akaifanya dunia na wote walioishi duniani
kumwabudu yule mnyama wa kwanza, ambaye jeraha
lake la mauti lilipona. 13 Naye akafanya ishara
kuu na za ajabu, hata kusababisha moto kushuka
toka mbinguni kuja duniani watu wakiona waziwazi.
14 Kwa sababu ya zile ishara alizokuwa amepewa
uwezo wa kuzifanya kwa niaba ya yule mnyama
wa kwanza, akawadanganya watu walioishi duniani.
Akawaamuru wasimamishe sanamu kwa heshima ya
yule mnyama aliyekuwa amejeruhiwa kwa upanga
lakini akaishi. 15 Akapewa uwezo wa kuipa pumzi
ile sanamu ya yule mnyama wa kwanza, ili iweze
kusema na kuwasababisha wale wote waliokataa
kuiabudu hiyo sanamu kuuawa. 16 Pia alimlazimisha
kila mmoja, mdogo na mkubwa, tajiri na maskini,
mtu huru na mtumwa, atiwe chapa kwenye mkono
wake wa kuume au kwenye paji la uso wake, 17 ili
mtu yeyote asiweze kununua wala kuuza isipokuwa
amekuwa na hiyo chapa, ambayo ni jina la huyo
mnyama au tarakimu za jina lake. 18 Hapa ndipo

penye hekima. Yeye aliye na ufahamu na ahesabu
tarakimu za huyo mnyama, kwa maana ni tarakimu za
kibinadamu. Tarakimu zake ni mia sita sitini na sita.

**14** Kisha nikatazama, na hapo mbele yangu
Mwana-Kondoo alikuwa amesimama juu ya
Mlima Sayuni. Pamoja naye walikuwa wale elfu mia
moja na arobaini na nne wenye jina la Mwana-Kondoo
na jina la Baba yake limeandikwa kwenye paji za
nyuso zao. 2 Nami nikasikia sauti kutoka mbinguni
kama sauti ya maji mengi yaendayo kwa kasi na sauti
kama ngurumo ya radi. Sauti hiyo niliyoisikia ilikuwa
kama sauti ya wapiga vinubi wakipiga vinubi vyao.
3 Nao wakaimba wimbo mpya mbele ya hicho kiti
cha enzi, na mbele ya wale viumbe wanne wenye
uhai, na wale wazee. Hakuna mtu yeyote aliyeweza
kujifunza wimbo huo isipokuwa hao elfu mia moja
na arobaini na nne waliokuwa wamekombolewa
kutoka duniani. 4 Hawa ndio wale ambao hawakujitia
unajisi kwa wanawake, kwa kuwa wao ni bikira.
Wao humfuata Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa
wamekombolewa kutoka miongoni mwa wanadamu
wakawa malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-
Kondoo. 5 Vinywani mwao hapakuonekana uongo,
wala hawakuwa na hatia yoyote. 6 Kisha nikamwona
malaika mwingine akiruka juu angani, naye alikuwa
na Injili ya milele ya kuwatangazia wale wanaoishi
duniani: kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa. **(aiōnios
g166)** 7 Akasema kwa sauti kubwa, "Mcheni Mungu
na kumpa utukufu, kwa maana saa ya hukumu yake
imewadia. Mwabuduni yeye aliyeziumba mbingu,
dunia, bahari na chemchemi za maji." 8 Malaika
wa pili akafuata akisema, "Umeanguka! Umeanguka
Babeli Mkuu, mji ule ulioyafanya mataifa yote kulewa
kwa mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake." 9
Malaika wa tatu akawafuata hao wawili akisema
kwa sauti kubwa, "Kama mtu yeyote anamwabudu
huyo mnyama na sanamu yake na kutiwa chapa
yake kwenye paji la uso wake au kwenye mkono
wake, 10 yeye pia atakunywa mvinyo wa hasira
kali ya Mungu ambayo imemiminwa katika kikombe
cha ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji.
Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti mbele
ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo.
11 Nao moshi wa mateso yao hupanda juu milele
na milele. Hakuna mapumziko, mchana wala usiku,
kwa wale wamwabuduo huyo mnyama na sanamu
yake, au kwa yeyote anayepokea chapa ya jina lake."
**(aiōn g165)** 12 Hapa ndipo penye wito wa subira na
uvumilivu wa watakatifu; wale wanaozishika amri
za Mungu na kudumu katika uaminifu kwa Isa.
13 Kisha nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema,
"Andika: Wamebarikiwa wafu wafao katika Isa Bwana
tangu sasa." "Naam," asema Roho wa Mungu,
"watapumzika kutoka taabu zao, kwa kuwa matendo
yao yatawafuata." 14 Nikatazama, hapo mbele yangu
palikuwa na wingu jeupe, na aliyekuwa ameketi juu
ya hilo wingu alikuwa kama Mwana wa Adamu, akiwa
na taji la dhahabu kichwani mwake na mundu mkali
mkononi mwake. 15 Kisha malaika mwingine akaja
kutoka Hekaluni naye akamwita kwa sauti kubwa
yule aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu akasema,
"Chukua mundu wako ukavune kwa kuwa wakati wa
mavuno umewadia, kwa maana mavuno ya dunia
yamekomaa." 16 Hivyo yule aliyekuwa ameketi juu ya
lile wingu akauzungusha mundu wake duniani, nayo
dunia ikavunwa. 17 Malaika mwingine akatoka katika
Hekalu lililoko mbinguni, naye pia alikuwa na mundu
mkali. 18 Kisha malaika mwingine, aliyekuwa na
mamlaka juu ya moto, akatoka kwenye madhabahu,
naye akamwita yule malaika mwenye mundu mkali
kwa sauti kubwa, akisema, "Chukua mundu wako
mkali ukakusanye vichala vya mizabibu ya dunia,
maana zabibu zake zimeiva." 19 Hivyo yule malaika
akauzungusha mundu wake duniani na kukusanya
zabibu za dunia na kuzitupa kwenye shinikizo kubwa
la ghadhabu ya Mungu. 20 Lile shinikizo likakanyagwa
nje ya mji, nayo damu ikatiririka kama mafuriko kutoka
hilo shinikizo kufikia kimo cha hatamu za farasi, kwa
umbali wa maili mia moja na themanini.

**15** Ndipo nikaona ishara nyingine kubwa ya
ajabu mbinguni: malaika saba wenye yale
mapigo saba ya mwisho, kwa sababu kwa mapigo
hayo ghadhabu ya Mungu ilikuwa imekamilika. 2
Nikaona kile kilichoonekana kama bahari ya kioo
iliyochanganyikana na moto. Kando ya hiyo bahari,
walikuwa wamesimama wale watu waliomshinda
yule mnyama na sanamu yake pamoja na tarakimu
ya jina lake. Mikononi mwao walikuwa wameshika
vinubi walivyopewa na Mungu. 3 Nao wakaimba
wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu, na wimbo
wa Mwana-Kondoo, wakisema: "Bwana Mungu
Mwenyezi, matendo yako ni makuu na ya ajabu. Njia

zako wewe ni za haki na za kweli, Mfalme wa nyakati
zote! 4 Ni nani ambaye hatakuogopa wewe Mwenyezi
Mungu na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe
peke yako ndiwe mtakatifu. Mataifa yote yatakuja na
kuabudu mbele zako, kwa kuwa matendo yako ya haki
yamedhihirishwa.” 5 Baada ya haya nikatazama, nalo
Hekalu la Hema la Ushuhuda lilikuwa limefunguliwa
mbinguni. 6 Ndani ya lile Hekalu wakatoka malaika
saba wakiwa na mapigo saba. Walikuwa wamevaa
nguo safi za kitani iliyong’aa, na kufungwa mikanda
ya dhahabu vifuani mwao. 7 Ndipo mmoja wa wale
viumbe wanne wenye uhai akawapa wale malaika
saba mabakuli saba ya dhahabu yaliyojaa ghadhabu
ya Mungu, yeye aishiye milele na milele. **(aiōn g165)**
8 Nalo lile Hekalu lilijawa na moshi uliotokana na
utukufu wa Mungu na uweza wake, wala hakuna
yeyote aliyeweza kuingia mle Hekaluni hadi yale
mapigo saba ya wale malaika saba yalipomalizika.

**16** Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka mle Hekaluni
ikiwaambia wale malaika saba, “Nendeni,
mkayamwage duniani hayo mabakuli saba ya
ghadhabu ya Mungu.” 2 Malaika wa kwanza akaenda
akalimwaga hilo bakuli lake juu ya nchi. Majipu
mabaya yenye maumivu makali yakawapata wale
watu wote waliokuwa na chapa ya yule mnyama
na walioabudu sanamu yake. 3 Malaika wa pili
akalimwaga bakuli lake baharini, nayo ikabadilika
kuwa damu kama ya mtu aliyekufa na kila kiumbe hai
kilichokuwa ndani ya bahari kikafa. 4 Malaika wa tatu
akalimwaga bakuli lake katika mito na chemchemi za
maji, nazo zikawa damu. 5 Ndipo nikamsikia malaika
msimamizi wa maji akisema: “Wewe una haki katika
hukumu hizi ulizotoa, wewe uliyeko, uliyekuwako,
Uliye Mtakatifu, kwa sababu umehukumu hivyo; 6
kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu wako
na manabii wako, nawe umewapa damu wanywe
kama walivyostahili.” 7 Nikasikia madhabahu ikiitikia,
“Naam, Bwana Mungu Mwenyezi, hukumu zako
ni kweli na haki.” 8 Malaika wa nne akamimina
bakuli lake kwenye jua, nalo likapewa nguvu za
kuwaunguza watu kwa moto. 9 Watu wakaunguzwa
na hilo joto kali, wakalaani Jina la Mungu, aliyekuwa
na uwezo juu ya mapigo haya, tena wakakataa
kutubu na kumtukuza Mungu. 10 Malaika wa tano
akamimina bakuli lake kwenye kiti cha utawala cha
yule mnyama, nao ufalme wake ukagubikwa na giza.
Watu wakatafuna ndimi zao kwa ajili ya maumivu,
11 wakamlaani Mungu wa mbinguni kwa sababu ya
maumivu na majeraha yao, wala hawakutubu kwa
ajili ya matendo yao maovu. 12 Malaika wa sita
akamimina bakuli lake kwenye mto mkubwa Frati,
maji yake yakakauka ili kutayarisha njia kwa ajili
ya wafalme kutoka Mashariki. 13 Kisha nikaona
roho wachafu watatu waliofanana na vyura wakitoka
katika kinywa cha lile joka na katika kinywa cha yule
mnyama na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. 14
Hizo ndizo roho za pepo wachafu zitendazo miujiza.
Nazo huwaendea wafalme wa ulimwengu wote na
kuwakusanya tayari kwa ajili ya vita katika siku ile
kuu ya Mungu Mwenyezi. 15 “Tazama, naja kama
mwizi! Amebarikiwa yeye akeshaye na kuziweka
tayari nguo zake ili asiende uchi na kuonekana aibu
yake.” 16 Ndipo wakawakusanya wafalme pamoja
mahali paitwapo Har-Magedoni kwa Kiebrania. 17
Malaika wa saba akamimina bakuli lake angani na
sauti kubwa ikatoka mle Hekaluni katika kile kiti cha
enzi, ikisema, “Imekwisha kuwa!” 18 Kukawa na miali
ya radi, ngurumo, radi na tetemeko kubwa la ardhi.
Hapajawahi kuwa na tetemeko la ardhi kama hilo tangu
mwanadamu awepo duniani, kwani lilikuwa tetemeko
kubwa ajabu. 19 Ule mji mkubwa ukagawanyika
katika sehemu tatu, nayo miji ya mataifa ikaanguka.
Mungu akakumbuka Babeli Mkuu na kumpa kikombe
kilichojaa mvinyo wa ghadhabu ya hasira yake. 20
Kila kisiwa kikatoweka wala milima haikuonekana. 21
Mvua kubwa ya mawe yenye uzito wa talanta moja
ikashuka kutoka mbinguni, ikawaangukia wanadamu.
Nao wanadamu wakamlaani Mungu kwa ajili ya hayo
mapigo ya mvua ya mawe, kwa sababu pigo hilo
lilikuwa la kutisha.

**17** Mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na
yale mabakuli saba akaja akaniambia, “Njoo,
nitakuonesha adhabu ya yule kahaba mkuu, aliyeketi
juu ya maji mengi. 2 Yule ambaye wafalme wa dunia
walizini naye na watu walioishi duniani walilewa
kwa mvinyo wa uzinzi wake.” 3 Kisha yule malaika
akanichukua katika Roho wa Mungu, akanipeleka
jangwani. Huko nikamwona mwanamke mmoja
ameketi juu ya mnyama mwekundu aliyejaa majina ya
kumkufuru Mungu mwili mzima. Mnyama huyo alikuwa
na vichwa saba na pembe kumi. 4 Huyo mwanamke
alikuwa amevaa mavazi ya rangi ya zambarau

na nyekundu, akimetameta kwa dhahabu, vito vya
thamani na lulu. Mkononi mwake alikuwa ameshika
kikombe cha dhahabu kilichojaa mambo ya machukizo
na uchafu wa uzinzi wake. 5 Kwenye paji lake la uso
palikuwa pameandikwa jina la siri: Babeli Mkuu, Mama
wa makahaba na wa machukizo ya dunia. 6 Nikaona
kuwa huyo mwanamke alikuwa amelewa kwa damu
ya watakatifu, yaani damu ya wale watu waliouawa
kwa ushuhuda wa Isa. Nilipomwona huyo mwanamke,
nilistaajabu sana. 7 Ndipo yule malaika akaniambia,
“Kwa nini unastaajabu? Nitakufafanulia siri ya huyo
mwanamke na huyo mnyama aliyempanda, mwenye
vichwa saba na pembe kumi. 8 Huyo mnyama
ambaye ulimwona awali alikuwako, lakini sasa
hayuko, naye atapanda kutoka lile Shimo na kwenda
kwenye maangamizi yake. Watu wanaoishi duniani
ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha
uzima tangu kuumbwa kwa ulimwengu watastaajabu
kumwona huyo mnyama, kwa maana alikuwako hapo
awali, na sasa hayuko, lakini atakuwako baadaye.
**(Abyssos g12)** 9 “Hapa ndipo penye wito wa akili
pamoja na hekima. Vile vichwa saba ni vilima saba
ambavyo huyo mwanamke amevikalia. 10 Pia hivyo
vichwa saba ni wafalme saba. Watano wamekwisha
kuanguka, mmoja yupo, mwingine hajaja bado, lakini
atakapokuja atalazimika kukaa kwa muda mfupi.
11 Yule mnyama aliyekuwako hapo awali na sasa
hayuko, yeye ni mfalme wa nane. Ni miongoni mwa
wale saba, naye anaenda kwenye maangamizi yake.
12 “Zile pembe kumi ulizoziona ni wafalme kumi
ambao bado hawajapokea ufalme, lakini watapokea
mamlaka kuwa wafalme kwa saa moja pamoja
na yule mnyama. 13 Hawa wana nia moja, nao
watamwachia yule mnyama nguvu zao na mamlaka
yao. 14 Watafanya vita na Mwana-Kondoo, lakini
Mwana-Kondoo atawashinda kwa sababu yeye ni
Bwana wa mabwana na Mfalme wa wafalme. Yeye
atakuwa pamoja na watu wake walioitwa ambao ni
wateule wake na wafuasi wake waaminifu.” 15 Kisha
yule malaika akaniambia, “Yale maji uliyoyaona yule
kahaba akiwa ameketi juu yake ni jamaa, makundi ya
watu, mataifa na lugha. 16 Zile pembe kumi ulizoziona,
pamoja na huyo mnyama, watamchukia huyo kahaba,
watamfilisi na kumwacha uchi, watamla nyama yake
na kumteketeza kwa moto. 17 Kwa maana Mungu
ameweka mioyoni mwao kutimiza kusudi lake kwa
kukubali kumpa yule mnyama mamlaka yao ya
utawala hadi maneno ya Mungu yatakapotimia. 18
Yule mwanamke uliyemwona ni ule mji mkubwa
unaowatawala wafalme wa dunia.”

**18** Baada ya haya nikaona malaika mwingine
akishuka kutoka mbinguni, akiwa na mamlaka
kuu na dunia ikaangazwa kwa mng’ao wake. 2 Naye
akapaza sauti kwa nguvu, akisema: “‘Umeanguka!
Umeanguka Babeli Mkuu!’ Umekuwa makao ya
mashetani na makazi ya kila pepo mchafu, makazi
ya kila ndege na kila mnyama achukizaye. 3
Kwa maana mataifa yote yamekunywa mvinyo wa
ghadhabu ya uasherati wake. Nao wafalme wa dunia
wamefanya uzinzi naye, na wafanyabiashara wa
dunia wametajirika kutokana na wingi wa utajiri wake.”
4 Kisha nikasikia sauti nyingine kutoka mbinguni
ikisema: “‘Tokeni katikati yake, enyi watu wangu,’ ili
msije mkashiriki dhambi zake, ili msije mkapatwa
na pigo lake lolote; 5 kwa kuwa dhambi zake
zimefika hadi mbinguni, naye Mungu ameukumbuka
uhalifu wake. 6 Mtendee kama yeye alivyotenda;
umlipe mara mbili kwa ajili ya yale aliyotenda. Katika
kikombe chake mchanganyie mara mbili ya kile
alichochanganya. 7 Mpatie mateso na huzuni nyingi
sawa na utukufu na anasa alizojipatia. Kwa kuwa
moyoni mwake hujivuna, akisema, ‘Mimi ninatawala
kama malkia; mimi si mjane, wala sitaona huzuni
kamwe.’ 8 Kwa hiyo mapigo yatampata kwa siku moja:
mauti, maombolezo na njaa. Naye atateketezwa kwa
moto, kwa maana Mwenyezi Mungu amhukumuye
ana nguvu. 9 “Wafalme wa dunia waliozini naye
na kushiriki anasa zake watakapoona moshi wa
kuungua kwake, watamlilia na kumwombolezea. 10
Kwa hofu kubwa ya mateso yake, watasimama mbali
na kulia na wakisema: “‘Ole! Ole, ee mji mkubwa, ee
Babeli mji wenye nguvu! Hukumu yako imekuja katika
saa moja!’ 11 “Wafanyabiashara wa dunia watalia
na kumwomboleza kwa sababu hakuna anunuaye
bidhaa zao tena: 12 Bidhaa za dhahabu, za fedha,
za vito vya thamani na vya lulu, kitani safi, nguo
za rangi ya zambarau, hariri, nguo nyekundu, aina
zote za miti ya udi, na vifaa vyote vya pembe za
ndovu, vifaa vyote vya miti yenye thamani kuliko yote,
shaba, chuma na marumaru, 13 bidhaa za mdalasini
na vikolezo, za uvumba, manemane, na uvumba
wenye harufu nzuri, za divai, na mafuta ya zeituni,

za unga mzuri na ngano; ng'ombe na kondoo; farasi
na magari ya vita; na miili na roho za wanadamu.
**14** "Watasema, 'Yale matunda ambayo roho yako
iliyatamani yamekoma. Utajiri wako wote na fahari
yako vimetoweka, wala haviwezi kupatikana tena
kamwe!' **15** Wale wafanyabiashara waliotajirika kwa
bidhaa hizo kutoka kwake watasimama mbali naye
kwa hofu kubwa ya mateso yanayompata. Watalia na
kuomboleza, **16** wakisema: "'Ole! Ole, ee mji mkuu,
uliyekuwa umevikwa mavazi ya kitani safi, ya rangi ya
zambarau na nyekundu, ukimetameta kwa dhahabu,
vito vya thamani na lulu! **17** Katika muda wa saa
moja utajiri wote mkubwa kama huu umeangamia!'
"Kila nahodha, na wote wasafirio kwa meli, na wote
wapatao kipato chao kutokana na bahari, watasimama
mbali. **18** Watakapouona moshi wa kuungua kwake
watalia wakisema, 'Je, kulipata kuwako mji mkubwa
kama huu?' **19** Nao watajirushia mavumbi vichwani
mwao, huku wakilia na kuomboleza, wakisema: "'Ole!
Ole, ee mji mkubwa, mji ambao wote wenye meli
baharini walitajirika kupitia kwa mali yake! Katika saa
moja tu ameangamizwa!' **20** "Furahia kwa ajili yake,
ee mbingu! Furahini watakatifu, mitume na manabii!
Mungu amemhukumu kwa vile alivyowatendea ninyi."
**21** Kisha malaika mmoja mwenye nguvu akainua jiwe
kubwa kama la kusagia, akalitupa baharini akisema:
"Hivyo ndivyo mji mkubwa Babeli utakavyotupwa chini
kwa nguvu, wala hautaonekana tena. **22** Nyimbo za
wapiga vinubi na waimbaji, wapiga filimbi na wapiga
tarumbeta kamwe hazitasikika tena ndani yako. Ndani
yako kamwe hataonekana tena fundi mwenye ujuzi
wa aina yoyote. Wala sauti ya jiwe la kusagia kamwe
haitasikika tena. **23** Mwanga wa taa hautaangaza
ndani yako tena. Sauti ya bwana arusi na bibi arusi
kamwe haitasikika ndani yako tena. Wafanyabiashara
wako walikuwa watu maarufu wa dunia. Mataifa
yote yalipotoshwa kwa uchawi wako. **24** Ndani yake
ilionekana damu ya manabii na ya watakatifu, na
wote waliouawa duniani."

**19** Baada ya haya nikasikia sauti kama ya umati
mkubwa mbinguni wakipaza sauti na kusema:
"Haleluya! Wokovu na utukufu na uweza ni vya Mungu
wetu, **2** kwa maana hukumu zake ni za kweli na za
haki. Amemhukumu yule kahaba mkuu aliyeuharibu
ulimwengu kwa uzinzi wake. Mungu amemlipiza kisasi
kwa ajili ya damu ya watumishi wake." **3** Wakasema
tena kwa sauti kuu: "Haleluya! Moshi wake huyo
kahaba unapanda juu milele na milele." **(aiōn g165)**
**4** Wale wazee ishirini na wanne pamoja na wale
viumbe wanne wenye uhai wakaanguka kifudifudi,
wakamwabudu Mungu, aliyekuwa ameketi kwenye
kile kiti cha enzi. Wakasema kwa sauti kuu: "Amen,
Haleluya!" **5** Kisha sauti ikatoka katika kile kiti cha
enzi, ikisema: "Msifuni Mungu wetu, ninyi watumishi
wake wote, ninyi nyote mnaomcha, wadogo kwa
wakubwa!" **6** Kisha nikasikia sauti kama ya umati
mkubwa, kama sauti ya maji mengi yaendayo kasi
na kama ngurumo kubwa ya radi wakipaza sauti
na kusema: "Haleluya! Kwa maana Bwana Mungu
wetu Mwenyezi anatawala. **7** Tufurahi, tushangilie na
kumpa utukufu! Kwa maana arusi ya Mwana-Kondoo
imewadia na bibi arusi wake amejiweka tayari. **8**
Akapewa kitani safi, inayong'aa na nzuri, ili avae."
(Hiyo kitani safi inawakilisha matendo ya haki ya
watakatifu.) **9** Ndipo malaika akaniambia, "Andika:
'Wamebarikiwa wale walioalikwa kwenye karamu ya
arusi ya Mwana-Kondoo!'" Naye akaongeza kusema,
"Haya ndio maneno ya kweli ya Mungu." **10** Ndipo
nikaanguka kifudifudi miguuni pake ili kumwabudu,
lakini yeye akaniambia, "Usifanye hivyo! Mimi pia ni
mtumishi mwenzako pamoja na ndugu zako walio
na ushuhuda wa Isa. Mwabudu Mungu! Maana
ushuhuda wa Isa ndio roho ya unabii." **11** Kisha
nikaona mbingu imefunguka na hapo mbele yangu
akiwepo farasi mweupe, ambaye yeye aliyempanda
aliitwa Mwaminifu na Kweli. Yeye huhukumu kwa
haki na kufanya vita. **12** Macho yake ni kama miali
ya moto na juu ya kichwa chake kuna taji nyingi.
Ana jina lililoandikwa ambalo hakuna mtu yeyote
anayelijua isipokuwa yeye mwenyewe. **13** Amevaa
joho lililoloweshwa katika damu, na Jina lake ni
Neno la Mungu. **14** Majeshi ya mbinguni walikuwa
wakimfuata, wakiwa wamepanda farasi weupe, hali
wamevaa mavazi ya kitani safi, nyeupe na nzuri. **15**
Kinywani mwake hutoka upanga mkali ambao kwa
huo atayaangusha mataifa. "Atayatawala kwa fimbo
yake ya utawala ya chuma." Hulikanyaga shinikizo
la ghadhabu ya Mungu Mwenyezi. **16** Kwenye joho
lake na paja lake pameandikwa jina hili: Mfalme wa
wafalme na Bwana wa mabwana. **17** Nami nikamwona
malaika amesimama ndani kwenye jua, naye akaita
ndege wote warukao angani kwa sauti kuu, "Njooni,

kusanyikeni kwa ajili ya karamu kubwa ya Mungu, 18 ili mpate kula nyama ya wafalme na ya majemadari, ya mashujaa, ya farasi na ya wapanda farasi, nyama ya wanadamu, wote walio huru na watumwa, wadogo kwa wakubwa." 19 Kisha nikamwona yule mnyama na wafalme wa dunia pamoja na majeshi yao wakiwa wamekusanyika pamoja ili kufanya vita dhidi ya yule aliyempanda farasi pamoja na jeshi lake. 20 Lakini yule mnyama akakamatwa pamoja na huyo nabii wa uongo aliyekuwa amefanya ishara kwa niaba ya huyo mnyama, ambaye kwa ishara hizi aliwadanganya wale waliopokea chapa ya huyo mnyama na kuiabudu sanamu yake. Hawa wawili wakatupwa wakiwa hai ndani ya ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti. **(Limnē Pyr g3041 g4442)** 21 Wale waliosalia waliuawa kwa upanga uliotoka kinywani mwa yule aliyekuwa amempanda farasi nao ndege wote wakajishibisha kwa nyama yao.


**20** Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, akiwa ameshika ufunguo wa lile Shimo na mnyororo mkubwa mkononi mwake. **(Abyssos g12)** 2 Akalishika lile joka, yule nyoka wa zamani, ambaye ni ibilisi, au Shetani, naye akamfunga kwa muda wa miaka elfu. 3 Akamtupa katika lile Shimo, akamfunga humo na kulitia muhuri, ili kumzuia asiendelee kudanganya mataifa hadi hiyo miaka elfu itimie. Baada ya hayo lazima afunguliwe kwa muda mfupi. **(Abyssos g12)** 4 Kisha nikaona viti vya utawala vilivyokuwa vimekaliwa na wale waliopewa mamlaka ya kuhukumu. Tena nikaona roho za wale waliokatwa vichwa kwa sababu ya ushuhuda wa Isa na kwa sababu ya neno la Mungu. Hawakuwa wamemsujudu huyo mnyama wala sanamu yake wala hawakupokea ile chapa yake kwenye paji za nyuso zao au kwenye mikono yao. Wakawa hai na kutawala pamoja na Al-Masihi miaka elfu. 5 (Wafu waliosalia hawakufufuka hadi ilipotimia hiyo miaka elfu.) Huu ndio ufufuo wa kwanza. 6 Waliobarikiwa na walio watakatifu ni wale walio na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Hao mauti ya pili haina nguvu juu yao, bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Al-Masihi, nao watatawala pamoja naye kwa muda wa miaka elfu. 7 Hiyo miaka elfu itakapotimia, Shetani atafunguliwa atoke kifungoni mwake, 8 naye atatoka ili kuyadanganya mataifa yaliyopo katika pembe nne za dunia, yaani Gogu na Magogu apate kuwakusanya tayari kwa vita. Idadi yao ni kama mchanga ulioko pwani. 9 Nao walitembea katika eneo lote la dunia, wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule mji unaopendwa. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza. 10 Naye ibilisi aliyewadanganya akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti walikokuwa wametupwa yule mnyama na yule nabii wa uongo. Watateswa humo usiku na mchana, milele na milele. **(aiōn g165, Limnē Pyr g3041 g4442)** 11 Kisha nikaona kiti kikubwa cheupe cha enzi pamoja na yeye aliyeketi juu yake. Dunia na mbingu zikaukimbia uso wake wala mahali pao hapakuonekana. 12 Nami nikawaona wafu, wakubwa na wadogo, wakiwa wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi na vitabu vikafunguliwa. Pia kitabu kingine kikafunguliwa ambacho ni kitabu cha uzima. Hao wafu wakahukumiwa sawasawa na matendo yao kama yalivyoandikwa ndani ya hivyo vitabu. 13 Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo, nayo mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo. Kila mtu akahukumiwa kulingana na yale aliyoyatenda. **(Hadēs g86)** 14 Kisha mauti na Kuzimu zikatupwa katika ziwa la moto. Hii ndio mauti ya pili, yaani hilo ziwa la moto. **(Hadēs g86, Limnē Pyr g3041 g4442)** 15 Iwapo mtu yeyote jina lake halikuonekana katika kile kitabu cha uzima, alitupwa ndani ya lile ziwa la moto. **(Limnē Pyr g3041 g4442)**

**21** Kisha nikaona "mbingu mpya na nchi mpya", kwa maana mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza vimekwisha kupita, wala hapakuwa na bahari tena. 2 Nikauona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. 3 Nami nikasikia sauti kubwa kutoka kile kiti cha enzi ikisema, "Sasa makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake, naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. 4 Atafuta kila chozi kutoka macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita." 5 Naye yule aliyeketi juu ya kile kiti cha enzi akasema, "Tazama, nayafanya mambo yote kuwa mapya!" Kisha akasema, "Andika haya, maana maneno haya ni ya kuaminika tena ni kweli." 6 Akaniambia, "Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Yeye aonaye kiu nitampa kunywa kutoka chemchemi ya maji ya uzima bila gharama yoyote. 7 Yeye

ashindaye atayarithi haya yote, nami nitakuwa Mungu
wake, naye atakuwa mwanangu. 8 Lakini waoga,
wasioamini, wachafu, wauaji, wazinzi, wachawi,
waabudu sanamu, pamoja na waongo wote, mahali
pao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii
ndiyo mauti ya pili.” **(Limnē Pyr g3041 g4442)** 9 Mmoja wa
wale malaika saba waliokuwa na yale mabakuli saba
ya hayo mapigo saba ya mwisho akaja akaniambia,
“Njoo, nami nitakuonesha bibi arusi, yaani mke wa
Mwana-Kondoo.” 10 Naye akanichukua katika Roho
wa Mungu hadi kwenye mlima mkubwa na mrefu,
akanionesha ule Mji Mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka
kutoka mbinguni kwa Mungu. 11 Ulikuwa uking’aa
kwa utukufu wa Mungu kama kito chenye thamani
sana, kama yaspi, safi kama kioo. 12 Ulikuwa na
ukuta mkubwa, mrefu wenye malango kumi na mawili,
pakiwa na malaika kumi na wawili kwenye hayo
malango. Kwenye malango hayo yaliandikwa majina
ya yale makabila kumi na mawili ya Israeli. 13
Kulikuwa na malango matatu upande wa mashariki,
matatu upande wa kaskazini, matatu upande wa
kusini na matatu upande wa magharibi. 14 Ukuta wa
huo mji ulikuwa na misingi kumi na mbili, na juu yake
yaliandikwa majina ya wale mitume kumi na wawili
wa Mwana-Kondoo. 15 Huyo malaika aliyesema nami
alikuwa na ufito wa dhahabu wa kupimia huo mji,
malango yake na kuta zake. 16 Mji huo ulikuwa mraba,
urefu wake ulikuwa sawa na upana wake. Akaupima
huo mji kwa huo ufito akakuta una kama stadioni
12,000; urefu wake na upana wake na kwenda juu
kwake vilikuwa sawa. 17 Akaupima ukuta wake,
ulikuwa na unene wa dhiraa mia moja na arobaini
na nne kwa kipimo cha kibinadamu ambacho huyo
malaika alikuwa akikitumia. 18 Ukuta huo ulijengwa
kwa yaspi hali mji wenyewe ulijengwa kwa dhahabu
safi, iking’aa kama kioo. 19 Misingi ya kuta za mji
huo zilipambwa kwa kila aina ya kito cha thamani.
Msingi wa kwanza ulikuwa wa yaspi, wa pili yakuti
samawi, wa tatu kalkedoni, wa nne zumaridi, 20 wa
tano sardoniki, wa sita akiki, wa saba krisolitho, wa
nane zabarajadi, wa tisa yakuti manjano, wa kumi
krisopraso, wa kumi na moja hiakintho, wa kumi
na mbili amethisto. 21 Yale malango kumi na mbili
yalikuwa ni lulu kumi na mbili, kila lango lilikuwa
limetengenezwa kwa lulu moja. Barabara kuu ya mji
huo ilikuwa ya dhahabu safi iliyong’aa kama kioo.
22 Sikuona Hekalu ndani ya huo mji kwa sababu
Bwana Mungu Mwenyezi na Mwana-Kondoo ndio
Hekalu lake. 23 Ule mji hauhitaji jua wala mwezi
kuuangazia, kwa sababu utukufu wa Mungu ndio
nuru yake na Mwana-Kondoo ndiye taa yake. 24
Mataifa yatatembea yakiangaziwa na nuru yake na
wafalme wa duniani wataleta fahari yao ndani yake.
25 Malango yake hayatafungwa kamwe, kwa maana
hakutakuwa na usiku humo. 26 Utukufu na heshima
za mataifa zitaletwa humo. 27 Lakini kitu kichafu
hakitaingia humo kamwe, wala mtu yeyote atendaye
mambo ya aibu au ya udanganyifu. Bali watakaoingia
humo ni wale tu ambao majina yao yameandikwa
katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo.

**22** Kisha yule malaika akanionesha mto wa maji
ya uzima, maangavu kama kioo yakitiririka
kutoka kwa kile kiti cha enzi cha Mungu na cha
Mwana-Kondoo, 2 kupitia katikati ya barabara kuu ya
huo mji. Kwenye kila upande wa huo mto kulikuwa
na mti wa uzima utoao matunda ya aina kumi na
mbili, ukizaa matunda yake kila mwezi. Nayo majani
ya mti huo ni kwa ajili ya uponyaji wa mataifa.
3 Katika mji huo hakutakuwa tena na laana, bali
kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo
kitakuwamo humo na watumishi wake watamtumikia,
4 nao watamwona uso wake na Jina lake litakuwa
kwenye paji za nyuso zao. 5 Usiku hautakuwako
tena, wala hawatahitaji mwanga wa taa au wa jua,
kwa maana Bwana Mwenyezi Mungu atakuwa nuru
yao, nao watatawala milele na milele. **(aiōn g165)** 6
Kisha yule malaika akaniambia, “Maneno haya ni ya
kuaminika na kweli. Mwenyezi Mungu, Mungu wa
roho za manabii, alimtuma malaika wake kuwaonesha
watumishi wake yale ambayo hayana budi kutukia
upesi.” 7 “Tazama, naja upesi! Amebarikiwa yeye
ayashikaye maneno ya unabii wa kitabu hiki.” 8
Mimi, Yohana, ndiye niliyesikia na kuyaona mambo
haya. Nilipokwisha kuyasikia na kuyaona, nilianguka
chini nikasujudu miguuni pa yule malaika aliyekuwa
akinionesha mambo hayo. 9 Lakini yeye akaniambia,
“Usifanye hivyo! Mimi ni mtumishi pamoja nawe na
ndugu zako manabii na wote wanaoyashika maneno
ya kitabu hiki. Msujudie Mungu!” 10 Kisha akaniambia,
“Usiyafunge maneno ya unabii yaliyomo katika kitabu
hiki, kwa sababu wakati umekaribia. 11 Atendaye
mabaya na aendelee kutenda mabaya, aliye mchafu

na aendelee kuwa mchafu, yeye atendaye haki na
aendelee kutenda haki, na yeye aliye mtakatifu na
aendelee kuwa mtakatifu.” **12** “Tazama, naja upesi!
Thawabu yangu i mkononi mwangu, nami nitampa
kila mtu sawasawa na alivyotenda. **13** Mimi ni Alfa
na Omega, wa Kwanza na wa Mwisho, Mwanzo na
Mwisho. **14** “Wamebarikiwa wale wafuao mavazi yao,
ili wapate haki ya kuuendea huo mti wa uzima na
kuuingia huo mji kupitia kwenye malango yake. **15**
Huko nje wako mbwa, wachawi, wazinzi, wauaji,
waabudu sanamu, na kila mtu apendaye udanganyifu
na kuufanya. **16** “Mimi, Isa, nimemtuma malaika
wangu kushuhudia mambo haya kwa ajili ya jumuiya
ya waumini. Mimi ndimi Shina na Mzao wa Daudi, ile
Nyota ya Asubuhi inayong’aa.” **17** Roho wa Mungu na
bibi arusi wanasema, “Njoo!” Naye asikiaye na aseme,
“Njoo!” Yeyote mwenye kiu na aje, na kila anayetaka
na anywe maji ya uzima bure. **18** Namwonya kila mtu
asikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki: Mtu yeyote
akiongeza humo chochote, Mungu atamwongezea
mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. **19** Kama mtu
yeyote akipunguza humo chochote katika maneno ya
unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu
yake katika ule mti wa uzima na katika ule Mji
Mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika
kitabu hiki. **20** Yeye anayeshuhudia mambo haya
asema, “Hakika, naja upesi!” Amen. Njoo, Bwana
Isa. **21** Neema ya Bwana Isa iwe na watakatifu wote.
Amen.




*Nikauona Mji Mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, ukiwa umeandaliwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. Nami nikasikia sauti kubwa kutoka kile kiti cha enzi ikisema, “Sasa makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake,*
*naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.”*
Ufunuo 21:2-3

# Mwongozo kwa Msomaji

Kiswahili at AionianBible.org/Readers-Guide

The Aionian Bible republishes public domain and Creative Common Bible texts that are 100% free to copy and print. The original translation is unaltered and notes are added to help your study. The notes show the location of eleven special Greek and Hebrew Aionian Glossary words to help us better understand God's love for individuals and for all mankind, and the nature of afterlife destinies.

Who has the authority to interpret the Bible and examine the underlying Hebrew and Greek words? That is a good question! We read in 1 John 2:27, *"As for you, the anointing which you received from him remains in you, and you do not need for anyone to teach you. But as his anointing teaches you concerning all things, and is true, and is no lie, and even as it taught you, you remain in him."* Every Christian is qualified to interpret the Bible! Now that does not mean we will all agree. Each of us is still growing in our understanding of the truth. However, it does mean that there is no infallible human or tradition to answer all our questions. Instead the Holy Spirit helps each of us to know the truth and grow closer to God and each other.

The Bible is a library with 66 books in the Protestant Canon. The best way to learn God's word is to read entire books. Read the book of Genesis. Read the book of John. Read the entire Bible library. Topical studies and cross-referencing can be good. However, the safest way to understand context and meaning is to read whole Bible books. Chapter and verse numbers were added for convenience in the 16th century, but unfortunately they can cause the Bible to seem like an encyclopedia. The Aionian Bible is formatted with simple verse numbering, minimal notes, and no cross-referencing in order to encourage the reading of Bible books.

Bible reading must also begin with prayer. Any Christian is qualified to interpret the Bible with God's help. However, this freedom is also a responsibility because without the Holy Spirit we cannot interpret accurately. We read in 1 Corinthians 2:13-14, *"And we speak of these things, not with words taught by human wisdom, but with those taught by the Spirit, comparing spiritual things with spiritual things. Now the natural person does not receive the things of the Spirit of God, for they are foolishness to him, and he cannot understand them, because they are spiritually discerned."* So we cannot understand in our natural self, but we can with God's help through prayer.

The Holy Spirit is the best writer and he uses literary devices such as introductions, conclusions, paragraphs, and metaphors. He also writes various genres including historical narrative, prose, and poetry. So Bible study must spiritually discern and understand literature. Pray, read, observe, interpret, and apply. Finally, *"Do your best to present yourself approved by God, a worker who does not need to be ashamed, properly handling the word of truth."* 2 Timothy 2:15. *"God has granted to us his precious and exceedingly great promises; that through these you may become partakers of the divine nature, having escaped from the corruption that is in the world by lust. Yes, and for this very cause adding on your part all diligence, in your faith supply moral excellence; and in moral excellence, knowledge; and in knowledge, self-control; and in self-control patience; and in patience godliness; and in godliness brotherly affection; and in brotherly affection, love. For if these things are yours and abound, they make you to be not idle nor unfruitful to the knowledge of our Lord Jesus Christ,"* 2 Peter 1:4-8.

# Kamusi

Kiswahili at AionianBible.org/Glossary

The Aionian Bible un-translates and instead transliterates eleven special words to help us better understand the extent of God's love for individuals and all mankind, and the nature of afterlife destinies. The original translation is unaltered and a note is added to 64 Old Testament and 200 New Testament verses. Compare the meanings below to the Strong's Concordance and Glossary definitions.

***Abyssos*** g12
*Greek:* proper noun, place
*Usage:* 9 times in 3 books, 6 chapters, and 9 verses
*Meaning:*
Temporary prison for special fallen angels such as Apollyon, the Beast, and Satan.

***aïdios*** g126
*Greek:* adjective
*Usage:* 2 times in Romans 1:20 and Jude 6
*Meaning:*
Lasting, enduring forever, eternal.

***aiōn*** g165
*Greek:* noun
*Usage:* 127 times in 22 books, 75 chapters, and 102 verses
*Meaning:*
A lifetime or time period with a beginning and end, an era, an age, the completion of which is beyond human perception, but known only to God the creator of the aiōns, Hebrews 1:2. Never meaning simple endless or infinite chronological time in Greek usage. Read Dr. Heleen Keizer and Ramelli and Konstan for proofs.

***aiōnios*** g166
*Greek:* adjective
*Usage:* 71 times in 19 books, 44 chapters, and 69 verses
*Meaning:*
From start to finish, pertaining to the age, lifetime, entirety, complete, or even consummate. Never meaning simple endless or infinite chronological time in Koine Greek usage. Read Dr. Heleen Keizer and Ramelli and Konstan for proofs.

***eleēsē*** g1653
*Greek:* verb, aorist tense, active voice, subjunctive mood, 3rd person singular
*Usage:* 1 time in this conjugation, Romans 11:32
*Meaning:*
To have pity on, to show mercy. Typically, the subjunctive mood indicates possiblity, not certainty. However, a subjunctive in a purpose clause is a resulting action as certain as the causal action. The subjunctive in a purpose clause functions as an indicative, not an optative. Thus, the grand conclusion of grace theology in Romans 11:32 must be clarified. God's mercy on all is not a possibility, but a certainty. See ntgreek.org.

***Geenna*** g1067
*Greek:* proper noun, place
*Usage:* 12 times in 4 books, 7 chapters, and 12 verses
*Meaning:*
Valley of Hinnom, Jerusalem's trash dump, a place of ruin, destruction, and judgment in this life, or the next, though not eternal to Jesus' audience.

***Hadēs*** g86
*Greek:* proper noun, place
*Usage:* 11 times in 5 books, 9 chapters, and 11 verses
*Meaning:*
Synonomous with Sheol, though in New Testament usage Hades is the temporal place of punishment for deceased unbelieving mankind, distinct from Paradise for deceased believers.

***Limnē Pyr*** g3041 g4442
*Greek:* proper noun, place
*Usage:* Phrase 5 times in the New Testament
*Meaning:*
Lake of Fire, final punishment for those not named in the Book of Life, prepared for the Devil and his angels, Matthew 25:41.

***Sheol*** h7585
*Hebrew:* proper noun, place
*Usage:* 66 times in 17 books, 50 chapters, and 64 verses
*Meaning:*
The grave or temporal afterlife world of both the righteous and unrighteous, believing and unbelieving, until the general resurrection.

***Tartaroō*** g5020
*Greek:* proper noun, place
*Usage:* 1 time in 2 Peter 2:4
*Meaning:*
Temporary prison for particular fallen angels awaiting final judgment.

# Kamusi +

AionianBible.org/Bibles/Swahili---Swahili-Open-Bible/Noted

Glossary references are below. Strong's Hebrew and Greek number notes are added to 64 Old Testament and 200 New Testament verses. Questioned verse translations do not contain Aionian Glossary words and may wrongly imply *eternal* or *Hell*. * The note placement is skipped or adjusted for verses with non-standard numbering.

## *Abyssos*

Luka 8:31
Warumi 10:7
Ufunuo 9:1
Ufunuo 9:2
Ufunuo 9:11
Ufunuo 11:7
Ufunuo 17:8
Ufunuo 20:1
Ufunuo 20:3

## *aïdios*

Warumi 1:20
Yuda 1:6

## *aiōn*

Mathayo 12:32
Mathayo 13:22
Mathayo 13:39
Mathayo 13:40
Mathayo 13:49
Mathayo 21:19
Mathayo 24:3
Mathayo 28:20
Marko 3:29
Marko 4:19
Marko 10:30
Marko 11:14
Luka 1:33
Luka 1:55
Luka 1:70
Luka 16:8
Luka 18:30
Luka 20:34
Luka 20:35
Yohana 4:14
Yohana 6:51
Yohana 6:58
Yohana 8:35
Yohana 8:51
Yohana 8:52
Yohana 9:32
Yohana 10:28
Yohana 11:26
Yohana 12:34
Yohana 13:8
Yohana 14:16
Matendo 3:21
Matendo 15:18
Warumi 1:25
Warumi 9:5
Warumi 11:36
Warumi 12:2
Warumi 16:27
1 Wakorintho 1:20
1 Wakorintho 2:6
1 Wakorintho 2:7
1 Wakorintho 2:8
1 Wakorintho 3:18
1 Wakorintho 8:13
1 Wakorintho 10:11
2 Wakorintho 4:4
2 Wakorintho 9:9
2 Wakorintho 11:31
Wagalatia 1:4
Wagalatia 1:5
Waefeso 1:21
Waefeso 2:2
Waefeso 2:7
Waefeso 3:9
Waefeso 3:11
Waefeso 3:21
Waefeso 6:12
Wafilipi 4:20
Wakolosai 1:26
1 Timotheo 1:17
1 Timotheo 6:17
2 Timotheo 4:10
2 Timotheo 4:18
Tito 2:12
Wahebrania 1:2
Wahebrania 1:8
Wahebrania 5:6
Wahebrania 6:5
Wahebrania 6:20
Wahebrania 7:17
Wahebrania 7:21
Wahebrania 7:24
Wahebrania 7:28
Wahebrania 9:26
Wahebrania 11:3
Wahebrania 13:8
Wahebrania 13:21
1 Petro 1:23
1 Petro 1:25
1 Petro 4:11
1 Petro 5:11
2 Petro 3:18
1 Yohana 2:17
2 Yohana 1:2
Yuda 1:13
Yuda 1:25
Ufunuo 1:6
Ufunuo 1:18
Ufunuo 4:9
Ufunuo 4:10
Ufunuo 5:13
Ufunuo 7:12
Ufunuo 10:6
Ufunuo 11:15
Ufunuo 14:11
Ufunuo 15:7
Ufunuo 19:3
Ufunuo 20:10
Ufunuo 22:5

## *aiōnios*

Mathayo 18:8
Mathayo 19:16
Mathayo 19:29
Mathayo 25:41
Mathayo 25:46
Marko 3:29
Marko 10:17
Marko 10:30
Luka 10:25
Luka 16:9
Luka 18:18
Luka 18:30
Yohana 3:15
Yohana 3:16
Yohana 3:36
Yohana 4:14
Yohana 4:36
Yohana 5:24
Yohana 5:39
Yohana 6:27
Yohana 6:40
Yohana 6:47
Yohana 6:54
Yohana 6:68

Yohana 10:28
Yohana 12:25
Yohana 12:50
Yohana 17:2
Yohana 17:3
Matendo 13:46
Matendo 13:48
Warumi 2:7
Warumi 5:21
Warumi 6:22
Warumi 6:23
Warumi 16:25
Warumi 16:26
2 Wakorintho 4:17
2 Wakorintho 4:18
2 Wakorintho 5:1
Wagalatia 6:8
2 Wathesalonike 1:9
2 Wathesalonike 2:16
1 Timotheo 1:16
1 Timotheo 6:12
1 Timotheo 6:16
2 Timotheo 1:9
2 Timotheo 2:10
Tito 1:2
Tito 3:7
Filemoni 1:15
Wahebrania 5:9
Wahebrania 6:2
Wahebrania 9:12
Wahebrania 9:14
Wahebrania 9:15
Wahebrania 13:20
1 Petro 5:10
2 Petro 1:11
1 Yohana 1:2
1 Yohana 2:25
1 Yohana 3:15
1 Yohana 5:11
1 Yohana 5:13
1 Yohana 5:20
Yuda 1:7
Yuda 1:21
Ufunuo 14:6

## *eleēsē*

Warumi 11:32

## *Geenna*

Mathayo 5:22
Mathayo 5:29
Mathayo 5:30
Mathayo 10:28
Mathayo 18:9
Mathayo 23:15
Mathayo 23:33
Marko 9:43
Marko 9:45
Marko 9:47
Luka 12:5
Yakobo 3:6

## *Hadēs*

Mathayo 11:23
Mathayo 16:18
Luka 10:15
Luka 16:23
Matendo 2:27
Matendo 2:31
1 Wakorintho 15:55
Ufunuo 1:18
Ufunuo 6:8
Ufunuo 20:13
Ufunuo 20:14

## *Limnē Pyr*

Ufunuo 19:20
Ufunuo 20:10
Ufunuo 20:14
Ufunuo 20:15
Ufunuo 21:8

## *Sheol*


Mwanzo 37:35
Mwanzo 42:38
Mwanzo 44:29
Mwanzo 44:31
Hesabu 16:30
Hesabu 16:33
Torati 32:22
1 Samweli 2:6
2 Samweli 22:6
1 Wafalme 2:6
1 Wafalme 2:9
Ayubu 7:9
Ayubu 11:8
Ayubu 14:13
Ayubu 17:13
Ayubu 17:16
Ayubu 21:13
Ayubu 24:19
Ayubu 26:6
Zaburi 6:5
Zaburi 9:17
Zaburi 16:10
Zaburi 18:5
Zaburi 30:3
Zaburi 31:17
Zaburi 49:14
Zaburi 49:15
Zaburi 55:15
Zaburi 86:13
Zaburi 88:3
Zaburi 89:48
Zaburi 116:3
Zaburi 139:8
Zaburi 141:7
Mithali 1:12
Mithali 5:5
Mithali 7:27
Mithali 9:18
Mithali 15:11
Mithali 15:24
Mithali 23:14
Mithali 27:20
Mithali 30:16
Mhubiri 9:10
Wimbo wa Sulemani 8:6
Isaya 5:14
Isaya 7:11
Isaya 14:9
Isaya 14:11
Isaya 14:15
Isaya 28:15
Isaya 28:18
Isaya 38:10
Isaya 38:18
Isaya 57:9
Ezekieli 31:15
Ezekieli 31:16
Ezekieli 31:17
Ezekieli 32:21
Ezekieli 32:27
Hosea 13:14
Amosi 9:2
Yona 2:2
Habakuki 2:5

## *Tartaroō*


2 Petro 2:4

## *Questioned*


Ezekieli 32:18
Ezekieli 32:24




*Kwa imani Ibrahimu, alipoitwa aende mahali Mungu angempa baadaye kuwa urithi, alitii na akaenda, ingawa hakujua anakoenda.* - Wahebrania 11:8




*Farao alipowaachia watu waende, Mungu hakuwaongoza kufuata njia ipitayo katika nchi ya Wafilisti, ingawa njia hiyo ilikuwa fupi zaidi. Kwa maana Mungu alisema, "Wakikabiliana na vita, wanaweza kubadili mawazo yao na kurudi Misri."* - Kutoka 13:17




*Kwa kuwa hata Mwana wa Adamu hakuja ili kutumikiwa, bali kutumika na kuutoa uhai wake uwe fidia kwa ajili ya wengi.* - Marko 10:45




*Paulo, mtumishi wa Al-Masihi Isa, aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa kwa ajili ya Injili ya Mungu,* - Warumi 1:1

# Creation 4004 B.C.

| | |
|---|---|
| Adam and Eve created | 4004 |
| Tubal-cain forges metal | 3300 |
| Enoch walks with God | 3017 |
| Methuselah dies at age 969 | 2349 |
| God floods the Earth | 2349 |
| Tower of Babel thwarted | 2247 |
| Abraham sojourns to Canaan | 1922 |
| Jacob moves to Egypt | 1706 |
| Moses leads Exodus from Egypt | 1491 |
| Gideon judges Israel | 1245 |
| Ruth embraces the God of Israel | 1168 |
| David installed as King | 1055 |
| King Solomon builds the Temple | 1018 |
| Elijah defeats Baal's prophets | 896 |
| Jonah preaches to Nineveh | 800 |
| Assyrians conquer Israelites | 721 |
| King Josiah reforms Judah | 630 |
| Babylonians capture Judah | 605 |
| Persians conquer Babylonians | 539 |
| Cyrus frees Jews, rebuilds Temple | 537 |
| Nehemiah rebuilds the wall | 454 |
| Malachi prophecies the Messiah | 416 |
| Greeks conquer Persians | 331 |
| Seleucids conquer Greeks | 312 |
| Hebrew Bible translated to Greek | 250 |
| Maccabees defeat Seleucids | 165 |
| Romans subject Judea | 63 |
| Herod the Great rules Judea | 37 |

(The Annals of the World, James Uusher)

# Jesus Christ born 4 B.C.

# New Heavens and Earth

| | |
|---|---|
| | Christ returns for his people |
| 1956 | Jim Elliot martyrd in Ecuador |
| 1830 | John Williams reaches Polynesia |
| 1731 | Zinzendorf leads Moravian mission |
| 1614 | Japanese kill 40,000 Christians |
| 1572 | Jesuits reach Mexico |
| 1517 | Martin Luther leads Reformation |
| 1455 | Gutenberg prints first Bible |
| 1323 | Franciscans reach Sumatra |
| 1276 | Ramon Llull trains missionaries |
| 1100 | Crusades tarnish the church |
| 1054 | The Great Schism |
| 997 | Adalbert marytyrd in Prussia |
| 864 | Bulgarian Prince Boris converts |
| 716 | Boniface reaches Germany |
| 635 | Alopen reaches China |
| 569 | Longinus reaches Alodia / Sudan |
| 432 | Saint Patrick reaches Ireland |
| 397 | Carthage ratifies Bible Canon |
| 341 | Ulfilas reaches Goth / Romania |
| 325 | Niceae proclaims God is Trinity |
| 250 | Denis reaches Paris, France |
| 197 | Tertullian writes Christian literature |
| 70 | Titus destroys the Jewish Temple |
| 61 | Paul imprisoned in Rome, Italy |
| 52 | Thomas reaches Malabar, India |
| 39 | Peter reaches Gentile Cornelius |
| 33 | Holy Spirit empowers the Church |

(Wikipedia, Timeline of Christian missions)

# Resurrected 33 A.D.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **What are we?** | | | Genesis 1:26 - 2:3 | |
| **How are we sinful?** | | | Romans 5:12-19 | |
| **Where are we?** | | | | |
| | | | Innocence | |
| | | | Eternity Past | Creation 4004 B.C. |
| **Who are we?** | God | Father | John 10:30<br><br>God's perfect fellowship | Genesis 1:31<br><br>God's perfect fellowship with Adam in The Garden of Eden |
| | | Son | | |
| | | Holy Spirit | | |
| | Mankind | Living | Genesis 1:1<br><br>No Creation<br>No people | |
| | | Deceased believing | | |
| | | Deceased unbelieving | | |
| | Angels | Holy | | |
| | | Imprisoned | | Genesis 1:31<br><br>No Fall<br>No unholy Angels |
| | | Fugitive | | |
| | | First Beast | | |
| | | False Prophet | | |
| | | Satan | | |
| **Why are we?** | | | Romans 11:25-36, Ephesian 2:7 | |

Mankind is created in God’s image, male and female He created us

Sin entered the world through Adam and then death through sin

## When are we? ▼

<table>
<tr><td colspan="4">Fallen</td><td>Glory</td></tr>
<tr><td>Fall to sin<br>No Law</td><td>Moses’ Law<br>1500 B.C.</td><td>Christ<br>33 A.D.</td><td>Church Age<br>Kingdom Age</td><td>New Heavens<br>and Earth</td></tr>
<tr><td colspan="4">1 Timothy 6:16<br>Living in unapproachable light</td><td rowspan="7">Acts 3:21<br>Philippians 2:11<br>Revelation 20:3<br><br>God’s<br>perfectly<br>restored<br>fellowship<br>with all<br>Mankind<br>praising<br>Christ<br>as Lord<br>in the<br>Holy<br>City</td></tr>
<tr><td colspan="2">John 8:58<br>Pre-incarnate</td><td>John 1:14<br>Incarnate</td><td>Luke 23:43<br>Paradise</td></tr>
<tr><td colspan="2">Psalm 139:7<br>Everywhere</td><td colspan="2">John 14:17<br>Living in believers</td></tr>
<tr><td colspan="4">Ephesians 2:1-5<br>Serving the Savior or Satan on Earth</td></tr>
<tr><td colspan="4">Luke 16:22<br>Blessed in Paradise</td></tr>
<tr><td colspan="4">Luke 16:23, Revelation 20:5,13<br>Punished in Hades until the final judgment</td></tr>
<tr><td colspan="4">Hebrews 1:14<br>Serving mankind at God’s command</td></tr>
<tr><td colspan="4">2 Peter 2:4, Jude 6<br>Imprisoned in Tartarus</td><td rowspan="4">Matthew 25:41<br>Revelation 20:10<br><br>Lake of Fire<br>prepared<br>for the<br>Devil<br>and his<br>Angels</td></tr>
<tr><td colspan="3" rowspan="3">1 Peter 5:8, Revelation 12:10<br><br>Rebelling against Christ<br>Accusing mankind</td><td>Revelation 20:13<br>Thalaasa</td></tr>
<tr><td>Revelation 19:20<br>Lake of Fire</td></tr>
<tr><td>Revelation 20:2<br>Abyss</td></tr>
</table>

For God has bound all over to disobedience in order to show mercy to all

# Hatima

Kiswahili at AionianBible.org/Destiny


The Aionian Bible shows the location of eleven special Greek and Hebrew Aionian Glossary words to help us better understand God's love for individuals and for all mankind, and the nature of after-life destinies. The underlying Hebrew and Greek words typically translated as *Hell* show us that there are not just two after-life destinies, Heaven or Hell. Instead, there are a number of different locations, each with different purposes, different durations, and different inhabitants. Locations include 1) Old Testament *Sheol* and New Testament *Hadēs*, 2) *Geenna*, 3) *Tartaroō*, 4) *Abyssos*, 5) *Limnē Pyr*, 6) *Paradise*, 7) *The New Heaven*, and 8) *The New Earth*. So there is reason to review our conclusions about the destinies of redeemed mankind and fallen angels.

The key observation is that fallen angels will be present at the final judgment, 2 Peter 2:4 and Jude 6. Traditionally, we understand the separation of the Sheep and the Goats at the final judgment to divide believing from unbelieving mankind, Matthew 25:31-46 and Revelation 20:11-15. However, the presence of fallen angels alternatively suggests that Jesus is separating redeemed mankind from the fallen angels. We do know that Jesus is the helper of mankind and not the helper of the Devil, Hebrews 2. We also know that Jesus has atoned for the sins of all mankind, both believer and unbeliever alike, 1 John 2:1-2. Deceased believers are rewarded in Paradise, Luke 23:43, while unbelievers are punished in Hades as the story of Lazarus makes plain, Luke 16:19-31. Yet less commonly known, the punishment of this selfish man and all unbelievers is before the final judgment, is temporal, and is punctuated when Hades is evacuated, Revelation 20:13. So is there hope beyond Hades for unbelieving mankind? Jesus promised, *"the gates of Hades will not prevail,"* Matthew 16:18. Paul asks, *"Hades where is your victory?"* 1 Corinthians 15:55. John wrote, *"Hades gives up,"* Revelation 20:13.

Jesus comforts us saying, *"Do not be afraid,"* because he holds the keys to *unlock* death and Hades, Revelation 1:18. Yet too often our *Good News* sounds like a warning to *"be afraid"* because Jesus holds the keys to *lock* Hades! Wow, we have it backwards! Hades will be evacuated! And to guarrantee hope, once emptied, Hades is thrown into the Lake of Fire, never needed again, Revelation 20:14.

Finally, we read that anyone whose name is not written in the Book of Life is thrown into the Lake of Fire, the second death, with no exit ever mentioned or promised, Revelation 21:1-8. So are those evacuated from Hades then, *"out of the frying pan, into the fire?"* Certainly, the Lake of Fire is the destiny of the Goats. But, do not be afraid. Instead, read the Bible's explicit mention of the purpose of the Lake of Fire and the identity of the Goats, *"Then he will say also to those on the left hand, 'Depart from me, you cursed, into the consummate fire which is prepared for... the devil and his angels,'"* Matthew 25:41. Bad news for the Devil. Good news for all mankind!

Faith is not a pen to write your own name in the Book of Life. Instead, faith is the glasses to see that the love of Christ for all mankind has already written our names in Heaven. *"If the first fruit is holy, so is the lump,"* Romans 11:16. Though unbelievers will suffer regrettable punishment in Hades, redeemed mankind will never enter the Lake of Fire, prepared for the devil and his angels. And as God promised, all mankind will worship Christ together forever, Philippians 2:9-11.




*Kwa sababu hii, nendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho wa Mungu,* - Mathayo 28:19